

~~Bible
African
Swahili~~

Bible
Swahili
1883

Bible. Swahili
...

KITABU CHA

AGANO JIPIYA

LA

BWANA NA MWOKOZI WETU

ISA MASIYA.

KIMEFASIRIKA KATIKA MANENO YA KWANZA YA KIYONANI.

LONDON :

KIMEPIGWA CHAPA KWA BRITISH AND FOREIGN
BIBLE SOCIETY.

—
1883.

ANJILI KWA MATTAYO.

KITABU cha kizazi chake Isa Masiya, mwana wa 1
Daúd, mwana wa Ibrahimu.

Ibrahimu alizaa Isaak, Isaak akazaa Yakób, Yakób 2
akazaa Yuda na ndugu zake. Yuda akazaa Farez na Zara 3
kwa Tamar, Farez akazaa Hesrón, Hesrón akazaa Arám,
Arám akazaa Aminadáb, Aminadáb akazaa Nahashón, 4
Nahashón akazaa Salmón, Salmón akazaa Boaz kwa 5
Raháb, Boaz akazaa Obéd kwa Ruth, Obéd akazaa Yese,
Yese akazaa Mfalme Daúd. 6

Mfalme Daúd akazaa Sulemán kwake wa Uriya,
Sulemán akazaa Rehabyám, Rehabyám akazaa Abiya, 7
Abiya akazaa Asa, Asa akazaa Yehoshafát, Yeho- 8
shafát akazaa Yorám, Yorám akazaa Uziya, Uziya 9
akazaa Yothám, Yothám akazaa Aház, Aház akazaa
Hezekiya, Hezekiya akazaa Manasse, Manasse akazaa 10
Amón, Amón akazaa Yosiya, Yosiya akazaa Yekoniya 11
na ndugu zake wakati walipohamishwa Babél.

Na baada ya kuhamishwa Babél, Yekoniya akazaa 12
Shealtiel, Shealtiel akazaa Zerubabél, Zerubabél aka- 13
zaa Abihúd, Abihúd akazaa Eliyakim, Eliyakim akazaa
Azór, Azór akazaa Sadók, Sadók akazaa Ahím, Ahím 14
akazaa Eliyúd, Eliyúd akazaa Eleazar, Eleazar akazaa 15
Mattán, Mattán akazaa Yakób. Yakób akazaa Yusuf, 16
aliye mume wake Maryamu, aliye mzaa ISA, aitwaye
Masiya.

Navyo vizazi vyote tangu Ibrahimu hatta Daúd, vizazi 17
kumi na vinne; navyo tangu Daúd hatta kuhamishwa
Babél, vizazi kumi na vinne; navyo tangu kuhamishwa
Babél hatta Masiya, vizazi kumi na vinne.

Na kizazi chake Isa Masiya chalikuwa hivi. Walipoa- 18
hadiana mama yake Maryamu na Yusuf, hawajakari-
biana pamoja, alionekana ana mimba kwa Roho Mtaka-
tifu. Naye Yusuf mumewe, akiwa mwenyi kaki, asitake 19
kumwaibisha, alithani kumwacha kwa siri. Alipokuwa 20

- akiwaza vile, malaika ya Bwana akamtokea katika ndoto, akamwambia, Yusuf, mwana wa Daúd, usiogope kumtwaa mkewo Maryamu, kwani atakachozaa ndicho cha Roho
- 21 Mtakatifu. Naye atazaa mtoto mume, na utamwita jina lake ISA, kwani ndiye atakayeokoa watu wake katika tha-
- 22 mbi zao. Hivi vyote vyalifanywa illi litimie lililonenwa
- 23 na Bwana kwa nabii, akisema, Angalia, mwana mwali atachukua mimba, naye atazaa mwana, na watamwita jina lake Emmanuél, lililofasirika, Muungu naswi.
- 24 Alipoa'mka Yusuf katika usingizi, akafanya kama alivyomwagiza malaika wa Bwana, akamtwaa mkewe:
- 25 wala hakumjua hatta amezaa mwanawe wa kwanza: akamwita jina lake ISA.
- 2** ALIPOZALIWA Isa katika Betlehemu ya Uyahudi, zamani za mfalme Herode, Mamajusi wa mashariki
- 2 wakafika Yerusalemi, wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwani tumeona nyota yake katika mashariki, naswi tumekuja kumsujudia.
- 3 Aliposikia haya mfalme Herode akafathaika, na Yeru-
- 4 salemi pia naye. Akakusanya wakobani wakuu wote na waandishi wa watu, akawauliza, Masiya angazaliwa
- 5 wapi? Nao wakamwambia, Katika Betlehemu ya Uya-
- 6 hudi; kwani ndivyo ilivyoandikwa na nabii, Nawe Betlehemu ya Uyahudi si mdogo katika majumbe ya Yuda, kwani katika wewe atatoka liwali atakayewatawala watu wangu Israeli.
- 7 Bassi Herode, alipowaita kwa siri Mamajusi, akawau-
- 8 liza sana wakati gani nyota ilipoonekana. Akawapeleka Betlehemu, akawaambia, Enendeni, mkatafute sana mambo ya mtoto; hatta mtakapomwona, mnilettee habari, illi nami nije nimsujudie.
- 9 Walipomsikia mfalme, wakashika njia; nayo nyota waliyoiona katika mashariki ikawatangulia, hatta ikaja
- 10 ikasimama juu ya mahali alipokuwako mtoto. Wali-poiona nyota wakafurahi furaha bora.
- 11 Wakiingia nyumbani, wakamwona mtoto na Maryamu mama yake, wakaanguka, wakamsujudia, na walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu, thahabu,
- 12 na uvumba, na manemane. Na walipoonywa kwa ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.
- 13 Na hao walipokwisha kweenda zao malaika ya Bwana

akamtokea Yusuf ndotoni, akamwambia, Ondoka, umtwae mtoto na mama yake, ukimbie hatta Misri, ukae huko hatta nitakapokwambia; kwani Herode atamtafuta mtoto, ampoteze.

Naye alipoa'mka akatwaa mtoto na mamaye usiku, 14 akaenda zake hatta Misri. Akawa kule hatta alipokufa 15 Herode; illi litimie alilonena Bwana kwa nabii, akisema, Katika Misri nimemwita mwana wangu.

Naye Herode akiona ya kwamba amedanganywa na 16 Mamajusi, akaghathabika sana, akapeleka akawaua watoto wote walio katika Betlehemu na mipaka yake yote, tangu miaka miwili na waliopunguka, kwa majira aliyo-hakiki kwa Mamajusi. Ndipo likatimia alilonena 17 nabii Yeremiya, akisema, Sauti imesikiwa katika 18 Rama, kilio, na maombolezo, na msiba mwingi, Rahél akiwalilia watoto wake, asikubali kufarajika, kwani hapana.

Alipofariki Herode, malaika ya Bwana akamtokea 19 Yusuf ndotoni katika Misri, akamwambia, Ondoka, 20 utwae mtoto na mamaye, uende inchi ya Israeli: wale wamekufa waliotafuta roho ya mtoto. Akaondoka, 21 akamtwaa mtoto na mamaye, akaja inchi ya Israeli. Lakini aliposikia ya kwamba Arkhelao amiliki katika 22 Uyahudi mahali pa Herode babaye, akaogopa kwenda huko. Na alipopata jawabu katika ndoto, akaenda zake hatta inchi ya Galilaya, akaja, akakaa kitako ka- 23 tika mji ulioitwa Nazareti; illi litimie lililonenwa nao nabii, Ataitwa Mnazarayo.

SIKU zile akaja Yohana 'mbatizaji akihubiri barani 3 mwa Uyahudi, akasema, Tubuni, kwani utalme wa 2 mbingu umekaribia. Huyo ndiye aliyenenwa na nabii 3 Isaya, akisema, Sauti yake aliaye barani, Fanyeni njia ya Bwana, nyosheni mapito yake. Naye Yohana aliku- 4 wa na mavazi ya nyele za ngamia, na mshipi wa ngozi kiunoni mwake, na chakula chake nzige na asali ya mvituni.

Wakamtokea Yerusalemi na Uyahudi wote na inchi 5 yote ya upande wa Yardani, wakabatizwa naye mtoni 6 Yardani, wakiungama thambi zao. Hatta alipowaona 7 Mafarisayo wengi na Masadukayo wengi wakijia ubatizo wake, akawaambia, Enyi, waana nyoka, nani aliyewaonya mkimbie hasira itakayokuja? Fanyeni matunda yalio- 8

- 9 ipasa toba. Msithani kusema moyoni, Tunaye baba, ndiye Ibrahimu; kwani nawaambia ya kwamba Muungu anaweza kwa mawe haya kumfanyia Ibrahimu watoto.
- 10 Hatta leo shoka linakaa shinani kwa miti; nayo killa mti usiozaa matunda mema hukatwa, hutupwa motoni.
- 11 Mimi nawabatiza na maji kwa toba: yeye anifuataye ni hodari kuliko mimi, sistahili hatta kuchukua viatu vyake; naye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa
- 12 moto. Pepeo lake li mkononi mwake, naye atatakasa sana sakafu yake, atakusanya ngano ghalani, lakini makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.
- 13 Ndipo Isa akitoka Galilaya akamfikia Yohana katika
- 14 Yardani, abatizwe naye. Lakini Yohana akamkataza, akasema, Mimi naihtajia kubatizwa na wewe, nawe
- 15 waja kwangu? Akamjibu Isa, akamwambia, Uache sasa, kwani hivi imetupasa kutimiza haki yote. Kiisha akamwacha.
- 16 Naye Isa alipokwisha kubatizwa akatoka marra maji-ni: mbingu zikamfunukia, akaona Roho ya Muungu
- 17 akishuka kama hua, aka'mwasilia: na sauti katika mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa anipendezaye.
- 4 ISA akaongozwa barani na Roho, ajaribiwe na Shetani. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, hafu akaona njaa. Mjaribu akamkaribia, akamwambia, Kama ndiwe Mwana wa Muungu, unene mawe haya
- 4 yawe mikate. Akamjibu, akasema, Imeandikwa, Mtu haishi kwa mkate tu, illa kwa neno lo lote litokalo kanwani kwa Muungu.
- 5 Kiisha, Shetani akamleta hatta mji mtakatifu, aka-
- 6 'mweka juu ya mnara wa hekalu, akamwambia, Kama ndiwe Mwana wa Muungu, ujitupe chini, kwani imeandikwa, Atakuagizia malaika zake, mikononi mwao
- 7 watakuchukua, usijikwae mguu wako katika jiwe. Isa akamwambia, Imeandikwa tena, Usimjaribu Bwana Muungu wako.
- 8 Shetani akampeleka tena katika mlima mkubwa 'mno, akamwonyesha mulki zote za ulimwengu, na
- 9 fahari zao, akamwambia, Hizi zote nitakupa, utakapoa-
- 10 nguka kunisujudia. Naye Isa akamwambia, Ondokea mbali, Shetani, kwani imeandikwa, Utamsujudia Bwana Muungu wako, naye pekeyake utamwabudu.

Kiisha Shetani akamwacha; wakaja malaika wakam- 11
ngojea.

Aliposikia Isa ya kwamba Yohana amefungwa, aka- 12
enda zake hatta Galilaya. Akaacha Nazareti, akaja, 13
akakaa Kapernaúm, ulioko pwani katika mipaka ya
Zabulón na Nafthalím: illi litimie neno la nabii Isaya, 14
likisema, Inchi ya Zabulón na inchi ya Nafthalím, njia 15
ya bahari, ng'ambo ya pili ya Yardani, Galilaya ya
mataifa; watu waliokaa gizani wameona mwanga 16
mwingi, na wale waliokaa mahali na uvulini mwa mauti,
mwanga umewazukia.

Tangu hapo akaanza Isa kuhubiri na kusema, Tubuni, 17
kwani ufalme wa mbingu umekaribia.

Alipokuwa Isa akitembea karibu na bahari ya Galilaya, 18
akaona ndugu wawili, Simán alioitwa Petro na Andrea
nduguye, wakitupa jarifa baharini, kwani walikuwa
wavuvi. Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya 19
wavuvi wa watu. Marra wakaziacha nyavu wakam- 20
fuata.

Akiendelea mbele, akaona ndugu wawili wangine, 21
Yakób wa Zebedayo na Yohana nduguye, chomboni
pamoja na Zebedayo baba yao, wakitengeneza nyavu
zao: akawaita. Marra wakaacha chombo na baba yao 22
wakamfuata.

Akatembea Isa Galilaya yote akifundisha katika 23
masunagogi yao, na kuhubiri anjili ya ufalme, na ku-
ponya ugonjwa wote na uthaifu wote katika watu.
Zikatoka habari zake katika Sham yote: wakamletea 24
wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na marathi
menginemengine na mateso, nao wenyi pepo, na wenyi
kichaa, na wenyi kupooza; akawapona. Makutano 25
mengi wakamfuata, wakitoka Galilaya, na Dekapoli,
na Yerusalemi, na Uyahudi, na ng'ambo ya pili ya
Yardani.

AKIYAONA mafuatano akapanda jabalini; akakaa 5
kitako, waanafunzi wake wakamjilia. Akafunua kanwa 2
lake, akawafundisha, akisema: Heri walio maskini 3
kwa roho; kwani wao ni ufalme wa mbingu. Heri 4
wenyi huzuni; kwani watafarajika. Heri wenyi upole; 5
kwani watairithi inchi. Heri wenyi njaa na kiu kwa 6
haki; kwani watashiba. Heri wenyi rehema; kwani 7
watapata rehema. Heri walio safi mioyo; kwani wata- 8

9 mwona Muungu. Heri wasuluhishi; kwani wataitwa
 10 waana wa Muungu. Heri wafukuzwao kwa sababu ya
 11 haki; kwani ufalme wa mbingu ni wao. Heri ninyi
 watakapowatukana, na watakapowafukuza, na wataka-
 posema juu yenu killa neno baya kwa uwongo, kwa
 12 sababu yangu. Furahini, mkapendezewe: ya kuwa tha-
 wabu zenu nyingi mbinguni: kwani kama haya waliwa-
 fukuza nabii waliokuwa kabla yenu.

13 Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini kama chumvi ime-
 oza itatiwaje chumvi? Haifai tena kabisa, illa kutu-
 14 pwa 'nje, ikanyagwe na watu. Ninyi ni mwanga wa
 ulimwengu. Mji hauwezi kustirika, ulio juu ya mlima;
 15 wala haiwashwi taa ikatiwa chini ya kapu, illa kuwe-
 kwa juu ya mwango, nayo yangazia wote waliomo nyu-
 16 mbani. Mwanga wenu wangaze hivi mbele za watu,
 hatta waone vitendo vyenu vizuri, wamtukuze Baba
 yenu aliye mbinguni.

17 Msinithanie nimekuja kuzitangua torati ao nabii.
 18 Sikuja kutangua, illa kutimiliza. Kwani amín na-
 waambia, Hatta mbingu na inchi zitakapokoma, wala
 yodi moja, wala nukta moja ya torati haitakoma, hatta
 19 zote zitakapotimia. Naye atakayevunja amri hiyo
 mojawapo hatta ndogo kuliko zote, akifundisha hivi
 watu, ataitwa mdogo katika ufalme wa mbingu; naye
 atakayezitenda na atakayezifundisha, ndiye ataitwa
 20 mkuu katika ufalme wa mbingu. Kwani nawaambia,
 Isipokuwa haki yenu imepita haki yao waandishi na
 Mafarisayo, hamtaingia katika ufalme wa mbingu.
 21 Mmesikia watu wa kale walivyosema, Usiue, naye aua-
 22 ye itampasa hukumu. Nami nawaambia, Killa aonaye
 hasira kwa nduguye burre, itampasa hukumu; naye
 amwambiaye ndugu yake, Raka, itampasa baraza;
 naye anenaye Mpumbafu, itampasa mcto wa jehannum.

23 Hatta ukiwa umeleta sadaka yako hatta mathbahu,
 na huko ukikumbuka ya kwamba nduguyo analo neno
 24 juu yako; yache sadaka yako huko mbele ya mathbahu,
 uende ukapatane kwanza na nduguyo, halafu urudi
 25 ukatoe sadaka yako. Upatane na mtesi wako kwa
 haraka uwapo naye njiani, illi mtesi asikulete kwa
 kathi, wala kathi asikutoe kwa asikari, wala usitiwe
 26 kifungoni. Amín nakwambia, Hutatoka kule hatta
 utakapokwisha lipa pesa la mwisho.

Mmesikia watu wa kale walivyosema, Usizini. 27
 Nami nawaambia, Killa mtu amtazamaye mwanamke 28
 hatta kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni
 mwake. Kama jicho lako la kuume limekuchukizisha, 29
 uling'oe, ulitupie mbali; u heri kiungo kimoja chako
 kiharibike, wala mwili wako mzima usitupwe katika
 jehannum. Na kama mkono wako wa kuume umeku- 30
 chukizisha, ukate, utupie mbali; u heri kiungo ki-
 moja chako kiharibike, wala mwili wako mzima usi-
 tupwe katika jehannum.

Ilinenwa, Mtu akiacha mkewe, ampe khati ya talaka. 31
 Nami nawaambia, Mtu amwachaye mkewe, illa kwa sa- 32
 babu ya zani, amfanya azini; naye amwoaye aliyeachwa
 azini.

Mmesikia tena ilinenwa nao wa kale, Usifanye zuli, 33
 lakini umtimizie Bwana nyapo zako. Nami nawaambia, 34
 Usiape kabisa, wala kwa mbingu, ndizo kiti cha Muu-
 ngu; wala kwa inchi, ndiyo mahali pa nyayo zake; 35
 wala kwa Yerusalemi, ndio mji wa Mfalme mkuu; wala 36
 usiape kwa kitwa chako, kwani huwezi kufanya unyele
 mmoja wala mweupe wala mweusi. Maneno yenu yawe, 37
 Ndio, ndio; Siyo, siyo: kwani yapitayo haya yatoka ma-
 vuni. Mmesikia ilinenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa 38
 jino. Nami nawaambia, Msishindane na maovu, lakini 39
 mtu akupigaye chafu la kuume, umgeuzie na la pili;
 na atakaye kukushtaki atwae kanzu yako, umwachie 40
 na joho; na atakayekuongoza milio moja, uende naye 41
 mbili. Akuombaye mpe; usigeuke kwake atakaye kua- 42
 zima.

Mmesikia ya kwamba ilinenwa, Mpende jirani yako, 43
 na mchukie adui yako. Nami nawaambia, Pendeni 44
 adui zenu, wabarikini wawalaanio, 'mwatendee mema
 wawachukiao, 'mwaombee wawatendea mabaya, nao
 wawafukuzao; illi mpate kuwa waana wa Baba yenu 45
 aliye mbinguni, afanyaye jua lake liwazukie waovu na
 wema, awapaye mvua wenyi haki na wasio haki. Nanyi 46
 mkiwapenda wawapendao, mnayo thawabu gani? Hatta
 mapublikano hawafanyi hivi? Nanyi mkiwasalimia 47
 ndugu zenu tu, mmewapitaje? Hatta mapublikano hawa-
 fanyi hivi? 'Mwe wakamilifu, kama Baba yenu aliye 48
 mbinguni ni mkamilifu.

ANGALIENI msifanye haki zenu mbele za watu, illi 6

kuonekana nao ; kwani ukifanya hivyo hupati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni.

2 Kwa sababu hii, uzifanyapo sadaka, usipige mzomari mbele yako kama wanafiki katika masunagogi na njiani, wapate heshima kwa watu. Amín nawaambia, wamepata

3 thawabu zao. Lakini wewe ufanyapo sadaka, hatta mkono wako wa kushoto usijue mkono wa kuume
4 ufanyalo: hatta sadaka zako zikiwapo kwa siri, naye Baba yako aonaye kwa siri atakupa thawabu kwa thahiri.

5 Nawe usalipo, usiwe kama wanafiki, wapendao kusali wakisimama katika masunagogi na pembeni mwa njia, illi waonekane na watu. Amín nawaambia, wamepata
6 thawabu zao. Lakini wewe usalipo, ingie chumbani kwako kwa ndani, hatta ukiisha kufunga mlango umwombe Baba yako aliye kwa siri, na Baba yako aonaye kwa siri atakupa thawabu kwa thahiri.

7 Nanyi msalipo, msiseme maneno matupu, kama watu wa mataifa, wathanio watakubalika kwa maneno yao
8 kwa kuwa mengi. Msifanane na hao ; kwani Baba yenu ajua mtakavyo kabla ya ninyi hamjamwomba.

9 Bassi msali kama hivi :

Baba yetu, ulioko mbinguni, Litakate jina lako.
10 Ufalme wako uje. Upendalo litendeke, kama mbinguni,
11 na katika inchi. Utupe leo chakula tunachoihtajia.
12 Utusamehe deni zetu, kama tuwasamehevyo wawiwao
13 na sisi. Usitulete katika nyonda, lakini utuokoe maovuni. Hakika yako wewe ni ufaume, na nguvu, na heshima, hatta milele. Amina.

14 Kwani mkiwasamehe watu makosa yao, naye Baba
15 yenu ya mbinguni atawasamehe ninyi ; lakini msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe makosa yenu.

16 Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki, wenyi uso wa huzuni ; kwani hubadilika nyuso zao, illi waonekane na watu wakifunga. Amín nawaambia, wamepata
17 thawabu zao. Lakini wewe mfungapo, ujitie mafuta
18 kitwani, ukanawe uso ; illi usionekane na watu uki-funga, illa na Baba yako aliye kwa siri ; na Baba yako
19 aonaye kwa siri atakupa thawabu kwa thahiri. Msiji-wekee mali duniani, ziharibikapo na noondo na kutu,
20 na waivi hutoboa na kwiba ; lakini jiwekeeni mali mbinguni, zisikoharibika na noondo wala na kutu, wala

waivi hawatoboi wala hawaibi. Kwani zikiwapo mali 21
zenu, tena na moyo wenu utakuwapo.

Taa ya mwili ni jicho : jicho lako likiwa kwa moja, 22
mwili wako wote utajaa mwanga; lakini jicho lako 23
likiwa ovu, mwili wako wote utajaa giza. Mwanga
uliomo ndani yako ukiwa giza, giza ipi kubwa ?

Hakuna mtu awezaye kuwatumikia bwana wawili : 24
kwani ao atamchukia mmoja akimpenda wa pili; ao
atamshika mmoja akimtweza wa pili. Ha'mwezi
kuwatumikia na Muungu na Mamona. Kwa sababu 25
hii nawaambia, Msishughulike kwa maisha yenu,
mtakulani, wala mtakunwani; wala kwa mwili wenu
mtavaani. Si maisha zayidi ya chakula, na mwili
zayidi ya mavazi? Angalieni ndege za anga: ha- 26
wapandi, wala hawavuni, wala hawaweki ghalani; la-
kini Baba yenu ya mbinguni awalisha wale. Ninyi
ha'mwapiti hao? Nani wenu akishughulika, awezaye 27
kujizidisha urefu wake kwa mkono mmoja? Na mbo- 28
na mwashughulika kwa mavazi? Kumbukeni maua
ya mashamba, yameavyo; hayatendi kazi, wala hayaso-
koti; lakini nawaambia wala Sulemán katika utukufu 29
wake wote, hakuvaa kama mojawapo wao. Kwani 30
Muungu akivika hivi majani ya mashamba yaliyo leo,
na kesho hutupwa motoni, hatazidi kuvika ninyi, enyi
wa imani haba? Kwa sababu hii, msishughulike mki- 31
sema, Tutakulani, ao tutakunwani, ao tutavaani?
Kwani haya yote mataifa huyataka. Kwani Baba 32
yenu ya mbinguni amejua ya kwamba mwaihtajia haya
yote. Takeni kwanza ufalme wa Muungu na haki ya- 33
ke, na haya yote mtaletewa. Msishughulike kwa ke- 34
sho: kwani kesho itataabika kwa mambo yake. Yatasha
kwa siku mabaya yake.

MSIAMUE, illi msiamuliwe. Kwani na maamzi 7
yale mwamuavyo, mtaamuliwa: na kipimo kile mpi- 2
mavyo, mtapimiwa tena ninyi.

Mbona waangalia kibanzi kilicho jichoni pa nduguyo, 3
wala hukumbuki mti ulio jichoni pako? Ao utamwa- 4
mbiaje nduguyo, Uniache niondoe kibanzi kilicho ji-
choni pako; na tazama, pana mti jichoni pako wewe?
Ewe mnafiki, ondoa kwanza mti katika jicho lako, 5
ndipo utaona sana uondoe kibanzi katika jicho la ndu-
guyo.

- 6 Usiwape mbwa vilivyo vitakatifu; wala msitupe lulu zenu mbele ya nguuwe, wasizikanyage kwa miguu yao, wala wakigeuka wasiwararue ninyi.
- 7 Ombeni na mtapewa; tafuteni na mtaona; bisheni
8 na mtafunguliwa; kwani killa aombaye hupewa, na
9 atafutaye huona, na abishaye hufunguliwa. Ao mtu yupi wenu mwanawe akimwomba mkate, ampa jiwe?
10 Ao akimwomba samaki, aampa nyoka? Kama ninyi
11 tena, mlio waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vema, Baba yenu aliye mbinguni atazidije kuwapa vema
12 wamwombao? Kwa sababu hii, lo lote mtakalo kufanyiwa na watu, nanyi mwafanyie vivyo; kwandi ndio torati na nabii.
- 13 Ingieni katika mlango mwembamba: kwani mpana mlango, na nafasi i katika njia iletayo uharibifu, nao
14 wengi waingiao: kwani mwembamba ni mlango, na yenyi shidda njia iletayo uzima, nao wachache waionao.
- 15 Angalieni kwa nabii za uwongo, wawajiapo katika mavazi ya kondoo, wallakini kwa ndani ni mbwa wa
16 mwitu walio wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Huchuma zabibu kwa miiba, ao tini kwa mbaruti?
17 Vivyo killa mti mwema huzaa matunda mema, na mti
18 mbaya huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mbaya kuzaa matunda mema.
19 Killa mti usiozaa matunda mema hukatawa ukatupwa motoni. Vivyo kwa matunda yao mtawatambua.
- 21 Siye killa aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbingu, illa alitendaye alipendalo
22 Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukutabiri kwa jina lako? hatukufukuza pepo kwa jina lako? hatukufanya miujiza
23 mingi kwa jina lako? Ndipo nitawaambia, Sikuwajua
24 kamwe: niondokeleeni nyote mtendao uovu. Bassi killa asikiaye maneno yangu haya, akiyatenda, nitamfafanisha na mtu mwenyi akili, aliyeijenga nyumba yake katika
25 mwamba; mvua ikanya, maji mengi yakaja, pepo zikavuma, zikapiga nyumba ile, isianguke; kwani misingi yake ilikuwa katika mwamba. Na killa asikiaye maneno haya yangu, asiyatende, atafafanishwa na mtu mpumbafu, aliyeijenga nyumba yake katika mchanga;
27 mvua ikanya, maji mengi yakaja, pepo zikavuma, zika-

piga nyumba ile, ikaanguka ; na maanguko yake makubwa.

Ikawa alipokwisha Isa maneno haya, makutano wakashangaa kwa mafundisho yake ; kwani aliwafundisha kama mwenyi mamlaka, wala si kama waandishi. 28 29

ALIPOSHUKA jabalini makutano mengi wakamfuata. Akaja mwenyi ukoma akamsujudia, akasema, Bwana, kama ukipenda, waweza kunitakasa. Isa akanyosha mkono wake, akamgusa, akasema, Napenda ; utakasike. Marra ukoma wake ukatakasika. Isa akanwambia, Angalia, usimwambie mtu : illa enenda zako, akuone mkohani, ukatoe sadaka Musa aliyoiamuru kwa ushahidi kwao. 8 2 3 4

Akiingia Isa katika Kapernaúm, amiri akaja, akamsihi, akasema, Bwana, mtumishi wangu amelazwa nyumbani mwenyi kupooza, aumwa sana. Isa akanwambia, Nitakuja nimponye. Amiri akanjibu, akasema, Bwana, sistahili ya wewe kuingia chini ya dari yangu : lakini useme neno tu, na mtumishi wangu atapona. Kwani mimi ni mtu chini ya nguvu, mwenyi asikari chini yangu ; nikimwambia huyu, Enenda, huenda ; na mwingine, Njoo, huja ; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya. Akisikia Isa, akataajabu, akawaambia wafuatao, Amín, nawaambia, sikuona imani kama hii wala katika Israeli. Nami nawaambia ya kwamba wengi watatoka mashariki na magharibi, waketi na Ibrahimu, na Isaak, na Yakób, katika ufalme wa mbingu, na waana wa ufalme watatupwa katika giza za 'nje, ndiko kilio na kutafuna meno. Isa akanwambia amiri, Enda zako, na kama ulivyoamini, upate. Mtumishi wake akapona saa ileile. 5 6 7 8 9 10 11 12 13

Alipoingia Isa nyumbani mwa Petro akaona mkwe wake amelazwa, hawezi homa. Akamgusa mkono, homa ikamwacha : akaondoka, akawangojea. Ilipokuwa jioni, wakamletea wengi wenyi pepo : akawafukuza pepo kwa neno, akawaponya wote waliokuwa hawawezi : illi liti mie lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Yee alitwaa uthaifu wetu, akachukua uveli. 14 15 16 17

Isa alipoona makutano mengi wakimzunguka, akaamuru kuvuka hatta ng'ambo ya pili. Mwandishi mmoja akaja akanwambia, Mwalimu, nitakufuata uendako kote. Isa akanwambia, mbweha zinalo paango, 20

na ndege za anga matundu ; illa Mwana wa adamu hana pa kulaza kitwa chake.

21 Mwanafunzi wake mwingine akamwambia, Bwana,
22 uniruhusu kwanza, niende nimzike baba yangu. Isa
akamwambia, Nifuate: uwaache wafu wazike wafu wao.

23 Akipanda chomboni, waanafunzi wake wakamfuata.
24 Na tháruba kuu ilikuwa katika bahari, hatta chombo
25 kikafunikizwa na mawimbi: naye alikuwa amelala. Waa-
nafunzi wake wakaja, wakamwa'msha, wakasema, Bwana,

26 utuponye: tumekufa. Akawaambia, Mbona mwaogopa,
wenyi imani haba? Kiisha, akaondoka, akazikemea
27 pepo na bahari; ikawa shwari kuu. Watu wakataajabu
wakasema, Mtu gani huyu, hatta pepo na bahari zamtii?

28 Naye akafika ng'ambo ya pili katika inchi ya Wager-
geseni. Wakamjia wawili wenyi pepo, wakitoka maka-
burini, wakali mno, hatta hawezi mtu kupita njia ile.

29 Wakalia, wakasema, Tunani nawe, Isa, Mwana wa
Muungu? Umekuja kutuuma mbele ya muhulla wetu?

30 Kulikuwako mbali kundi la nguuwe wengi wakila.

31 Bassi pepo wakamsihi, wakasema, Ukitufukuza, utuache
32 tuwaendee kundi la nguuwe. Akawaambia, Enendeni.

Wakatoka, wakaenda kundini mwa nguuwe. Na kundi
pia la nguuwe wakaenda kwa kassi wakatelemkia baha-

33 rini, wakafa majini. Wachunga wakakimbia, wakaen-
da zao mjini wakahubiri pia, na mambo ya wenyi

34 pepo. Na mji wote ukatoka wamkute Isa; hatta wali-
pomwona, wakamsihi aondoke mipakani mwao.

9 AKAPANDA chomboni, akavuka, akafika mjini mwake
2 yeye. Wakamletea mwenyi kupooza amelazwa kita-

ndani. Na Isa akiona imani yao, akamwambia mwenyi
kupooza, Moyo wako na uwe mkuu, mwanangu; umeo-

3 ndolewa thambi zako. Na baathi ya waandishi wakasema
4 moyoni, Mnajisi huyu. Naye Isa akiona mawazo yao,

akasema, Ginsi gani, mwawaza viovu moyoni mwenu?
5 Ipi nyepesi, kusema, Umeondolewa thambi zako, ao

6 kusema, Simama, utembe? Illa mmjue Mwana wa
adamu ndiye mwenyi nguvu duniani kuondoa thambi,

(akamwambia mwenyi kupooza), Simama, utweke kita-
7 nda chako, uende nyumbani kwako. Akaondoka akaenda

8 zake hatta nyumbani kwake. Wakimwona maku-
tano wakastaajabu, wakamtukuza Muungu aliyetoa

nguvu kama hizi kwa watu.

Alipotoka kule Isa, akaona mtu anakaa forthani, 9
aliyeitwa Mattayo. Akamwambia, Nifuate. Akaondo-
ka akamfuata.

Ikawa alipokaa kitako nyumbani, wakaja mapubli- 10
kano wengi, na wengi wenyi thambi, wakaketi pamoja
na Isa na waanafunzi wake. Mafarisayo walipoona 11
wakawaambia waanafunzi wake, Sababu gani mwalimu
wenu anakula na mapublikano na wenyi thambi? Aki- 12
sikia Isa akawaambia, Wazima hawamtaki tabibu, illa
wagonjwa. Endeni mkajifunze nini hii, Nataka rehema, 13
wala si sadaka: kwani sikuja kuwaita wenyi haki, illa
wenyi thambi watubu.

Wakamjia waanafunzi wa Yohana, wakamwambia, 14
Sababu gani sisi na Mafarisayo twafunga marra nyingi,
lakini waanafunzi wako hawafungi? Isa akawaambia, 15
Wenyi arusi waweza kulia, akiwa bwana arusi nao?
Wallakini siku zitakuja watakapondolewa bwana arusi;
siku zile watafunga. Hakuna mtu atiaye kipande cha 16
nguo mpya katika vazi kukuu, kwani iliyotiwa kuli-
fanya huliharibu vazi, na iliyopasuka huzidi kupasuka.
Wala watu hawatii mvinyo mpya katika kiriba kukuu: 17
illa kiriba hupasuka na mvinyo humwagika, kiriba zika-
haribika: lakini hutia mvinyo mpya katika kiriba mpya,
na zote mbili zahifathika.

Alipokuwa akiwaambia maneno haya, yuaja jumbe 18
mmoja akamsujudia, akamwambia, Binti yangu hatta
sasa amekufa: lakini ukija wewe u'mwekee mkono ata-
pona. Akaondoka Isa akamfuata na waanafunzi wake. 19

Na mwanamke aliyekuwa hawezi na kutoka damu 20
miaka thenashara, akaja nyuma yake, akamgusa upindo
wa mavazi yake: kwani alisema moyoni, Kama nikiu- 21
gusa tu upindo wa mavazi yake nitapona. Isa akageu- 22
ka, akamwona, akamwambia, Moyo wako na uwe mkuu,
binti; imani yako imekuponya. Na mwanamke akapona
tangu saa ile. Isa alipofika nyumbani kwa jumbe, 23
akaona wapiga filimbi na makutano wakifanya maombo-
lezo, akawaambia, Ondokeni: kwani kijana hakufa; 24
amelala tu. Wakamchekelea. Hatta makutano wali- 25
pokwisha toka, akaingia, akamtwaa mkono wake, kijana
akasimama. Zikaenea habari hizi katika inchi ile yote. 26

Naye Isa alipokuwa akitoka kule, vipofu wawili 27
wakamfuata wakalia, wakasema, Uturehemu, ee mwana

28 wa Daúd. Alipofika nyumbani, vipofu wakaja, Isa
 akawaambia, Mwasadiki naweza kufanya haya? Waka-
 29 mwambia, Yakini, bwana. Akagusa macho yao, akisema,
 30 Kwa kadri ya imani yenu na mpate. Macho yao yaka-
 funuka; Isa akawaagiza, akasema, Angalieni asijue mtu.

31 Lakini wakatoka wakamnena katika inchi ile yote.
 32 Nao wakitoka wakamletea mtu bubu mwenyi pepo.
 33 Akafukuza pepo, yule bubu akanena. Wakastaajabu
 makutano, wakasema, Hakuonekana kabisa hivi katika
 34 Israeli. Mafarisayo wakasema, Kwa mkuu wa pepo
 afukuza pepo.

35 Akazunguka Isa miji yote mikubwa na midogo, aka-
 fundisha katika masunagogi yao, akahubiri anjili ya
 ufalme, akaponya ugonjwa wote na uthaifu wote ulio
 36 katika watu. Alipowaona makutano, akawasikitikia,
 kwani walikuwa wamechoka mmoja na wametawanyika
 37 kama kondoo wasio na mchungu. Akawaambia waana-
 funzi wake, Mavuno ni makubwa, na watenda kazi wa-
 38 chache; nanyi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke
 watenda kazi katika mavuno yake.

10 AKAWAITA waanafunzi wake thenashara, akawapa
 nguvu juu ya pepo wabaya, wawafukuze, na waponye
 ugonjwa wote na uthaifu wote.

2 Bassi majina yao mitume thenashara ni haya; wa
 kwanza Simán aliyelitwa Petro, na Andrea nduguye;
 3 Yakób wa Zebedayo na Yohana nduguye; Filipo na
 Bartolomayo; Tomaso, na Mattayo publikano; Yakób wa
 4 Alfayo, na Lebayo aliyelitwa Thadayo; Simán Kananita,
 na Yuda Iskariota aliyemtoa.

5 Isa akawatuma hawa thenashara, akawaonya, akisema,
 Katika njia ya mataifa msiende, wala mjini mwa Wasa-
 6 maria msiingie; endeni kwanza kwa kondoo waliopotea
 7 wa nyumba ya Israeli. Mkienda hubirini, mkaseme,
 8 Ufalme wa mbingu umekaribia. Ponyeni wagonjwa,
 watakaseni wenye ukoma, wafufueni wafu, wafukuzeni
 9 pepo: mmepata burre, burre na mtoe. Msitwae thahabu,
 10 wala fetha, wala shaba mishipini mwenu, wala mkoba
 wa safari, wala kanzu mbili, wala viatu, wala gongo;
 11 kwani mtenda kazi astahili posho yake. Na killa
 mwingiamo mji, mkubwa au mdogo, mwuuzi nani humo
 12 astahiliye; mkae kwake hatta mtakapotoka. Mkiingia
 13 nyumbani toeni salaamu, na nyumba ikistahili salaamu

yenu iingie humu ; kama haistahili, salaamu yenu iwaru-
die. Naye asiyewakaribisha ninyi, wala asiyesikia ma- 14
neno yenu, mkitoka nyumbani kule ao mjini kule,
kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu. Amín na- 15
waambia, inchi ya Sodoma na Gomorra itasameheka siku
ya hukumu kuliko mji ule.

Angalieni, nawatuma kama kondoo katika mbwa wa 16
mwitu : 'mwe tena na busara kama nyoka, msiwe na hila
kama hua. Angalieni kwa watu : kwani watawatoa kwa 17
baraza, na katika masunagogi yao watawapiga ; mtape- 18
lekwa mbele za maliwali na wafaline kwa sababu yangu,
kwa ushahidi kwao na kwa mataifa. Nanyi watakapo- 19
watoa msishughulike ginsi gani ao maneno gani mta-
nena : mtapewa saa ile mtakayonena ; kwani si ninyi 20
mnenao, illa Roho ya Baba yenu inenaye mwenu.

Na ndugu atamtoa ndugu afe, na baba mwana ; na 21
watoto watawaondokea wazazi wao wawafishe. Mta- 22
chukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu : lakini
atakayedumu hatta mwisho ataokoka. Watakapowa- 23
fukuza katika mji huu kimbieni hatta wa pili. Amín
nawaambia, hamtatimia miji ya Israeli, hatta atakapo-
kuja Mwana wa adamu.

Mwanafunzi hampiti mwalimu, wala mtumwa hampiti 24
bwana wake. Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwa- 25
limu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake.
Kwamba wamemwita mwenyi nyumba Beelzebúl, si
zayidi wale walio nyumbani mwake ?

Msiwaogope, kwani hakuna jambo lililostirika lisilo- 26
funuka ; wala lililofichwa, lisilojuliwa. Niwaambialo 27
gizani, lisemeni mchana ; na msikialo sikioni lihubirini
juu ya nyumba. Wala msiwaogope wauao mwili wasi- 28
weze kuua roho : afathali mmwogope awezaye kupoteza
na mwili na robo motoni. Haviuzanyi videge viwili 29
kwa pesa moja ? Na hatta mmojawapo wao haanguki
chini isipokuwa na Baba yenu. Na hatta nyele za ki- 30
twani kwenu zimehesabika zote. Msiogope tena, mwafaa 31
ninyi kuliko videge vingi.

Naye yote aniungamaye mbele za watu, nami nitamwu- 32
ngama mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Naye 33
yote anikaniaye mbele za watu, nami nitamkania mbele
za Baba yangu aliye mbinguni.

Msinithanie nimekuja kuleta amani duniani : sikuja 34

35 kuleta amani, illa upanga. Nimekuja kuwafarikisha
 mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na
 36 mkwewe; na adui za mtu watakuwa wale wakaaao naye.
 37 Apendaye baba ao mama kuliko mimi hanistahili; na
 apendaye mwana ao binti kuliko mimi hanistahili.
 38 Naye asiyetwaa msalaba wake akafuata nyuma yangu
 39 hanistahili. Aipataye roho yake ataipoteza, na aipote-
 zaye roho yake kwa ajili yangu ataipata.

40 Awakubaliye ninyi amenikubali mimi, anikubaliye
 41 mimi amemkubali aliyenituma. Amkubaliye nabii kwa
 jina la nabii, atapata thawabu ya nabii; naye amku-
 baliye mwenyi haki kwa jina la mwenyi haki, atapata
 42 thawabu ya mwenyi haki. Naye amnyweshaye mmoja-
 wapo wa wadogo hawa kikombe cha *maji ya* baridi tu
 kwa jina la mwanafunzi, amín nawaambia, haitampotea
 thawabu yake.

11 ALIPOKWISHA Isa kuwaagiza waanafunzi wake
 thenashara, akatoka huko kwenda kufundisha na kuhu-
 biri katika miji yao.

2 Naye Yohana akasikia mle gerezani matendo yake Ma-
 3 siya, akapeleka waanafunzi wake wawili, akamwambia,
 Wewe ndiye atakayekuja, ao tumtazamie mwingine?
 4 Akajibu Isa, akawaambia, Rudini, mmweleze Yohana
 5 mwonavyo na msikiavyo: vipofu waona, wachechemeao
 watembea, wenyi ukoma wametakasika, viziwi wasikia,
 wafu wafufuka, na masikini wamehubiriwa anjili.
 6 Ndiye heri asiyechukiwa nami.

7 Hao walipokwenda zao Isa akaanza kusema na maku-
 tano kwa Yohana, Mwalikwenda barani kutazama nini?
 8 'Mwanzi uliotikisika na upepo? Lakini mwalikwenda
 kutazama nini? Mtu aliyevaa meroro? Wale wavaa
 9 meroro, wamo nyumbani mwa wafalme. Lakini mwali-
 kwenda kutazama nini? Nabii? Yakini, nawaambia,
 10 na apitaye nabii. Kwani huyo ndiye aliyeandikiwa,
 Angalieni, namtuma tume yangu mbele ya uso wako,
 11 afanye tayari njia mbele yako. Amín, nawaambia,
 hakuondoka katika wale waliozaliwa na waanawake mtu
 mkuu kuliko Yohana 'mbatizaji; naye aliye mdogo
 12 katika ufalme wa mbingu ni mkuu kuliko yeye. Tangu
 siku za Yohana 'mbatizaji hatta leo ufalme wa mbingu
 wapatika kwa nguvu, nao wenyi nguvu wautwaa.
 13 Kwani nabii zote na torati walikitangaza hatta Yo-

hala; na mkipenda kukubali, ndiye Eliya atakayekuja. 14
Mwenyi masikio ya kusikia, asikie. 15

Nitafafanisha na nini kizazi hiki? Kimefanana na 16
watoto wakikaa ugani wakiwaita wenzi wao, wakisema, 17
tumewapigia mzomari wala ninyi hamkucheza, tumewa-
lilia wala hamkulia. Kwani Yohana alikuja asile wala 18
asinywe, wakasema, Yuna pepo. Mwana wa adamu 19
amekuja akila na kunywa, wakasema, Tazama, mlafi
huyu na mwa mvinyo, rafiki ya mapublikano na wenyi
thambi. Lakini hekima itasifiwa kwa watoto wake.

Akaanza tena kuinenea miji, alimofanya miujiza yake 20
mingi, kwa sababu haikutubu.

Ole wako Khorazín! Ole wako Betsaida! Kwani 21
kama miujiza ingalifanywa katika Turo na Sidón, kama
imefanywa kwenu, wangelitubu zamani katika sako na
majifu. Lakini nawaambia, Turo na Sidón watasame- 22
heka siku ya hukumu kuliko ninyi.

Nawe Kapernaúm ulioinuka hatta mbinguni, utashuka 23
hatta ahera: kwani kama miujiza ingalifanywa katika
Sodoma iliyofanyika kwako, ingaliishi hatta leo. La- 24
kini nawaambia, inchi ya Sodoma itasameheka siku ya
hukumu kuliko wewe.

Siku zile Isa akajibu, akasema, Nakushukuru, Baba, 25
Bwana wa mbingu na inchi, kwani umewaficha haya
wenyi hekima na busara, ukawafunulia wadogo. Ya- 26
kini, Baba, kwamba hivi umeona vema.

Nimetolewa vyote na Baba yangu, wala hakuna mtu 27
amjuaye Mwana, illa Baba, wala hamjui mtu Baba,
illa Mwana naye aliye Mwana apenda kufunulia. Njoo- 28
ni kwangu, enyi nyote msumbukao, nanyi wenyi mi-
zigo, nami nitawapumzisha. Twaeni nira yangu, mji- 29
funze kwangu, kwani ndimi mwenyi upole, na moyo
wangu umenenyekela; nanyi mtapata raha kwa roho
zenu: kwani laini nira yangu, na mzigo wangu mwepesi. 30

WAKATI ule Isa alikuwa akipita siku ya sabato kati- 12
ka makoonde, waanafunzi wake wakaona njaa, wakaanza
kuchuma masuke, wakala. Mafarisayo wakiwaona, 2
wakamwambia, Tazama, waanafunzi wako wafanya iliyo
haramu katika sabato. Akawaambia, Hamkusoma ali- 3
vyofanya Daúd alipokuwa na njaa, yeye na wafuasi
wake? alivyoingia nyumbani mwa Muungu, akala 4
mikate ya wonyesho, iliyo haramu iliwe na yeye na

- 5 wenziwe, illa na wakohani peke yao? Ao hamkusoma
 katika torati wakohani hekaluni siku ya sabato wavu-
 6 njavyo sabato wasipate hatiya? Nawaambia ya kwamba
 7 yupo hapa aliye mkuu kuliko hekalu. Kama mngalijua
 maana yake, Nataka rehema, wala si sadaka, hamngali-
 8 wahukumia wasio na hatiya. Kwani Mwana wa adamu
 ni Bwana tena wa sabato.
- 9 Akaondoka kule akaja katika sunagogi lao; yumo na
 10 mtu mwenyi mkono yabis. Wakamwuliza, wakisema,
 kama halali kumponyesha mtu siku za sabato, illi wa-
 11 pate kumshtaki. Akawaambia, Mtu yupi wenu mwe-
 nyi kondoo mmoja, ikitumbukia shimoni siku ya sabato,
 12 asiyemkamata akamwondoa? Mtu hapiti kondoo?
 13 Kwani ni halali kutenda mema siku ya sabato. Akamwa-
 mbia mtu, Unyoshe mkono wako. Akaunyosha; uka-
 14 pona kama mkono wa pili. Mafarisayo wakatoka waka-
 15 fanya shauri juu yake, wapate kumpoteza. Isa akajua,
 akatoka huko; makutano mengi wakamfuata, akawa-
 16
 17 ponya wote, akawaagiza wasimjulishe; illi litimie
 18 lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Angalia mtumishi
 wangu, mteule wangu, pendo langu, anifurahishaye
 roho yangu. Nitamtia Roho yangu, naye atawahubiria
 19 mataifa hukumu. Hatateta, wala hatalia, wala mtu
 20 hatamsikia sauti yake njiani: 'mwanzi uliopondeka
 hatauvunja, wala kitani zikivivia hatazizima, hatta ata-
 21 kapoleta haki kwa shangwi; na kwa jina lake mataifa
 wataamini.
- 22 Akaletewa mwenyi pepo kipofu na bubu; akamponya,
 23 hatta kipofu na bubu akaona akanena. Makutano wa-
 kashangaa wote, wakasema, Si huyu mwana Daúd?
 24 Wakisikia Mafarisayo wakasema, Huyu hafukuza pepo
 25 illa kwa Beelzebúl, mkuu wa pepo. Akijua Isa mawazo
 yao, akawaambia, Killa ufalme ukishindana na nafsi
 yake, utapotea; na killa mji ao nyumba ikishindana na
 26 nafsi yake, haitaishi. Na kama Shetani amfukuza She-
 tani, ashindana na nafsi yake, na ufalme wake utaishije?
 27 Na mimi nikifukuza pepo kwa Beelzebúl, kwa nani
 wawafukuza waana wenu? Kwa sababu hii na hawa
 28 watawaamua. Lakini mimi nikifukuza pepo kwa Roho
 ya Muungu, ndipo ufalme wa Muungu umewajilia.
 29 Atawezaje tena mtu kuingia nyumbani mwake mwenyi
 nguvu ateke vyombo vyake, isipokuwa kwanza amemfu-

nga mwenyi nguvu? ndipo atakapoteka nyumba yake. Mtu asipokuwa nami, yu juu yangu, na mtu asipoku- 30 sanya nami, hutawanya.

Kwa sababu hii nawaambia, Killa thambi na killa 31 tukano litasameheka kwa watu, illa kumtukana Roho hakutasameheka kwa watu. Naye asemaye neno juu 32 ya Mwana wa adamu, atasamehewa; lakini anenaye juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa, wala katika ulimwengu wa sasa, wala katika ũle utakaokuwa. Ao fa- 33 nyeni mti mwema na mazao yake mema, ao fanyeni mti 'mbaya na mazao yake mabaya, kwani kwa mazao yake mti hujulikana. Enyi kizazi cha nyoka, mtawezaje ku- 34 sema vema, mkiwa wabaya? Kwani kwa wingi wa moyoni kinwa hunena. Mtu mwema katika hazina jema 35 hutoa vema, na 'mbaya katika hazina baya hutoa vibaya. Lakini nawaambia, Killa neno vivu watu wane- 36 nalo, watatoa hesabu yake siku ya hukumu. Kwa ma- 37 neno yako utapata sifa za haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.

Baathi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wa- 38 kasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako. Aka- 39 jibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zani chataka ishara; wala hakitapewa ishara, illa ishara ya nabii Yunus. Kwani kama Yunus alivyokuwa siku tatu tu- 40 mboni mwa nyamgumi, vivyo na Mwana wa adamu atakuwa siku tatu moyoni mwa inchi.

Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu na watu 41 wa kizazi hiki, na watawahukumia: kwani walitubu kwa kuhubiri kwake Yunus; na aliyempita Yunus yupo hapa. Malkiya ya kusini atasimama katika hukumu na kizazi 42 hiki, na atawahukumia: kwani yeye alitoka katika 'ncha za ulimwengu, asikie hekima ya Sulemán; na aliyempita Sulemán yupo hapa.

Alipotoka katika mtu pepo mchafu, hutembea pa- 43 hali pakavu akitafuta raha, asiipate. Halafu husema, 44 Nitarudi nyumbani mwangu nilikotoka; akirudi aiona tupu, imefagiwa na imepambwa. Bassi huenda kutwaa 45 pepo saba waovu kuliko yeye, waingia wakaa mle: na hali ya mtu yule ya mwisho mbaya kuliko ile ya kwanza. Hivyo kitapata na kizazi kibaya hiki.

Alipokuwa akisema na makutano, mamaye na ndu- 46 guze walikuwa wakisimama 'nje, wakamtaka kusema

47 naye. Mmoja akamwambia, Mama yako na ndugu za-
 48 ko wasimama 'nje, wataka kusema nawe. Akajibu,
 akamwambia amwambiaye, Ni nani mama yangu, na
 49 ndugu zangu? Akanyosha mkono wake kwa waana-
 funzi wake, akasema, Tazama, mama yangu na ndugu
 50 zangu. Kwani yee yote atakayefanya alipendalo Baba
 yangu aliye mbinguni, ndiye ndugu yangu, na umbu
 langu, na mama yangu.

- 13** SIKU ileile Isa akitoka nyumbani akakaa kando la
 2 bahari. Wakamkusanyikia mafuatano mengi, hatta
 akapanda chomboni akakaa kitako; na makutano yote
 3 wakasimama pwani. Akawaambia mambo mengi kwa
 4 mifano, akasema, Mpanzi alitoka kupanda mbegu. Ali-
 pokuwa akipanda, nyingine zikaanguka katika njia,
 5 ndege wakaja wakazila; nyingine zikaanguka katika
 mawe, usipokuwako udongo mwingi, marra zikachupuka
 6 kwa udongo hauna kwenda chini sana, na jua lilipo-
 choma zikaangua, na kwa sababu hazina shina zika-
 7 kauka; nyingine zikaanguka katika magugu, magugu
 8 yakamea yakazithiisha; nyingine zikaanguka katika
 inchi njema, zikazaa, moja mia, moja sitini, moja the-
 9 lathini. Mwenyi masikio ya kusikia, asikie. Wakaja
 10 waanafunzi wakamwambia, Ya nini kusema nao kwa
 11 mifano? Akawajibu akasema, Ninyi mmepewa kujua
 12 siri za ufalme wa mbingu, hawa hawakupewa. Yee yote
 anayo, atapewa, hatta atazidi; yee yote asiye nayo, atao-
 13 ndolewa nacho anacho. Kwa sababu hii nasema nao
 kwa mifano, illi waonapo wasione, na wasikiapo wasi-
 14 sikie, wala wasitambue. Nalo lawatimilia alilotabiri
 Isaya, akisema, Kwa kusikia mtasikia wala hamtata-
 mbua; kwa kutazama mtatazama wala hamtaona.
 15 Kwani moyo wa watu hawa umenona, na masikio yao
 yamekuwa mavivu, na macho yao wameyafumba; illi
 wasipate kuona kwa macho, na kusikia kwa masikio, na
 kutambua kwa moyo, hatta kuongoka, nami niwaponye.
 16 Lakini macho yenu ya heri, kwamba yaona; na ma-
 17 sikio yenu, kwamba yasikia. Kwani amín nawaambia,
 Nabii wengi na wenyi haki wengi walitamani kuvaona
 mwonayo, wala hawakuyaona; na kuyasikia msikiayo,
 wala hawakuyasikia.
- 18 Nanyi msikie mfano wa mpanzi.
 19 Killa asikiaye maneno ya ufalme asipotambua, huja

yule mwovu ayanyakua yaliyopandika moyoni mwake ;
ndiye aliyezipokea mbegu njiani.

Naye aliyezipokea katika mawe, ndiye yule asikiapo 20
maneno ayakubaliye marra furaha, lakini hana shina 21
ndani yake, hubadilibadili; ukiwa uthia ao ufukuzo kwa
sababu ya maneno, marra huhukiwa.

Naye aliyezipokea mbegu maguguni, ndiye asikiaye 22
maneno, na taabu za dunia na udanganifu wa mali
huthiisha maneno, wala hazai.

Naye aliyezipokea mbegu katika inchi njema, ndiye 23
asikiaye maneno, akayatambua; na kuzaa, mwingine
mia, mwingine sitini, na mwingine thelathini. Aka- 24
watolea mfano mwingine, akasema, Ufalme wa mbingu
umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika koo-
nde lake: na watu wakilala, akaja adui akapanda magugu 25
mwitu katikati ya ngano, akaenda zake. Baadaye yali- 26
pochupuka majani yakazaa masuke, yakaonekana na ma-
gugu mwitu. Wakaja watumwa wake wakamwambia 27
mwenyi nyumba, Bwana, hukupanda mbegu njema koo-
ndeni mwako? imepataje magugu mwitu? Akawaambia, 28
Mtu adui ndiye aliyeifanya. Watumwa wakamwambia,
Wapenda twende tuyakusanye? Akawaambia, La; la- 29
buda mkiwa mnakusanya magugu mwitu mtang'oa na
ngano pamoja nayo. Yaacheni yamee yote hatta ma- 30
vuno; na wakati wa kuvuna nitawaambia wavunao, Ku-
sanyeni kwanza magugu mwitu myafunge kwa matiti
yateketee, nazo ngano 'mweke ghalani mwangu.

Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa 31
mbingu umefanana na chembe ya kharadali, aliyoit-
waa mtu akaipanda katika shamba lake. Ndiyo ndogo 32
kuliko mbegu zote; lakini ilipomea ndiyo kubwa kuliko
magugu, ikiwa mti, hatta ndege za anga huja wakae
katika matawi yake.

Akawaambia mfano mwingine. Ufalme wa mbingu 33
umefanana na chachu aliyoitwaa mwanamke akaisetiri
katika vipimo vitatu vya unga, hatta wote ukachachwa.

Haya yote Isa akawaambia mafuatano kwa mifano, na 34
isipokuwa kwa mfano hakuwaambia neno; illi litimie 35
lililonenwa na nabii, akisema, Nitafunua kanwa langu
kwa mifano, nitatoa mambo yaliyostirika tangu mwanzo
wa ulimwengu.

Akiisha Isa akawaaga makutano, akaingia nyumbani. 36
Waanafunzi wake wakamjia wakisema, Utueleze mfano

37 wa magugu mwitu katika koonde. Akajibu akawaambia,
 38 Apandaye mbegu njema ndiye Mwana wa adamu, koonde
 ndio ulimwengu, mbegu njema waana wa ufalme, na ma-
 39 gugu mwitu waana wa yule mwovu; adui aliyeyapanda
 ndiye shetani; mavuno ndiyo mwisho wa dunia, na
 40 wavunao ndio malaika. Kama magugu mwitu yakusa-
 nyikavyo yatekete motoni, vivyo katika mwisho wa
 41 dunia hii. Mwana wa adamu atawatuma malaika zake,
 nao watakusanya katika ufalme wake zote zichukizazo
 42 nao watendao ubaya, wawatupe katika tanuu la moto,
 43 ndiko kilio na kutafuna meno. Nao wenyi haki wata-
 ng'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenyi
 masikio ya kusikia, asikie.

44 Tena ufalme wa mbingu umefanana na hazina iliyosti-
 rika katika shamba, nayo mtu alipoiona aificha, na kwa
 tamaa yake aenda akauza alivyo navyo vyote, apate
 kununulia shamba lile.

45 Tena ufalme wa mbingu umefanana na mfanya biashara,
 46 atafutaye lulu nzuri, na alipoiona lulu moja ya thamani
 kubwa akaenda akauza alivyo navyo vyote, akainunua.

47 Tena ufalme wa mbingu umefanana na juya liliotupwa
 48 baharini likakusanya za killa namna; hatta lilipojaa wa-
 kalivuta pwani, wakakaa wakachagua njema vyomboni,
 49 nazo mbaya wakazitupa. Vivyo katika timio la dunia,
 malaika watatoka watawapambanua waovu katika wenyi
 50 haki, na watawatupa tanuuni mwa moto; ndiko kilio
 51 na kutafuna meno. Isa akawaambia, Haya yamewae-
 52 lea? Wakamwambia, Yakini, Bwana. Akawaambia,
 Kwa sababu hii, killa mwandishi mwenyi elimu ya
 ufalme wa mbingu, amefanana na mtu mwenyi nyumba
 atoye katika hazina yake vitu vipya na vya kale.

53 Ikawa alipokwisha Isa mifano hii akatoka akaenda
 54 zake. Hatta alipofika inchi yake, akawafundisha katika
 masunagogi yao, hatta wakashangaa wakasema, Huyu
 55 amepata wapi hekima hii na miujiza hii? Siye mwana
 wake sermala? Mamaye haitwi Maryamu? Na ndu-
 56 guze Yakób, na Yose, na Simán, na Yuda, na maumbu
 yake, si wote kwetu? Amepata wapi huyu mambo
 57 haya yote? Wakachukiwa naye.

Isa akawaambia, Nabii hakosi heshima, asipokuwa
 58 katika inchi yake na nyumbani mwake. Wala haku-
 fanya kule miujiza mingi, kwa sababu ya kutoa kuamini
 kwao.

WAKATI ule Herode tetrarkha akasikia habari za Isa, 14
 akawaambia watumwa wake, Ndiye Yohana 'mbatizaji, 2
 ameondoka katika wafu, na kwa sababu hii nguvu zime-
 fanyika naye. Kwani Herode alimkamata Yohana 3
 akamfunga, akamtia gerezani, kwa ajili ya Herodiade
 mke wa nduguye Filipino; kwani Yohana alimwambia, 4
 Ni haramu; usimtwae. Na alipotaka ku'mua akawao- 5
 gopa watu, kwani wakamwona wote alikuwa nabii.
 Hatta siku ya kuzaliwa kwake Herode, binti Herodiade 6
 akacheza mbele zao, akampendeza Herode, hatta aka- 7
 mwapia, atampa atakalo lote. Naye akifundishwa na 8
 mamaye, akasema, Nipe hapa kitwa cha Yohana 'mba-
 tizaji katika kombe. Mfalme akasikitika, lakini kwa 9
 ajili ya uapo wake na kwa ajili zao wakaa wakila pa-
 moja naye, akaamrisha kutolewa; akatuma akamkata 10
 kitwa Yohana gerezani, kitwa chake kikaletwa katika 11
 kombe, kijana akapewa; akakichukua kwa mamaye.
 Waanafunzi wake wakaja wakauchukua mwili wake 12
 wakauzika, wakaenda wakamwambia Isa. Isa aliposikia 13
 akatoka huko kwa chombo akaenda kwa siri mahali
 pasipo watu. Na mafuatano waliposikia, wakamfuata
 kwa miguu wakitoka mijini.

Isa akishuka akaona makutano mengi, akawasikitikia 14
 akawaponya wagonjwa wao.

Hatta ikiwa jioni waanafunzi wake wakamjia, waka- 15
 sema, Hapa ni nyikani, na saa imepita: uwaage maku-
 tano, waende zao mijini wapate kununua vyakula. Isa 16
 akawaambia, Hawaiihtajii kwenda zao; 'mwape wale.
 Wakamwambia, Hatuna hapa illa mikate mitano na 17
 samaki mbili. Akawaambia, Nileteeni hiyo hapa. 18
 Akaamrisha makutano wakae kitako katika majani, 19
 akaitwaa mikate mitano na samaki mbili, akatazama
 mbinguni akabariki, akaivunja mikate, akawapa waana-
 funzi, na waanafunzi makutano. Wakala wote, waka- 20
 shiba, wakaokota makombo yaliyosalia vikapu thenashara
 vilivyojaa. Nao waliokula walikuwa waanaume kama 21
 elfu tano, na waanaake na watoto.

Marra Isa akawalazimisha waanafunzi wake kupanda 22
 chomboni watangulie kwenda ng'ambo ya pili, akiwa
 yeye anaagana na makutano. Alipokwisha agana na 23
 makutano akapanda mlimani kwa faragha akaabudu.
 Ilipokuwa magharibi alikuwako peke yake. Na chombo 24

kilikuwako katikati ya bahari, wakasumbuka na ma-
 25 wimbi, kwani upepo ulikuwa wa omo. Hatta kesho la
 'nne la usiku Isa akaja kwao akienda juu ya bahari.
 26 Waanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, waka-
 fathaika wakasema, Ni mvuli; wakapiga yowe kwa hofu.
 27 Marra Isa akasema nao akanena, Moyo wenu na uwe
 28 mkuu; mimi hapa; msiogope. Petro akamjibu, akasema,
 Kama ni wewe, Bwana, uniamuru nije kwako juu ya
 29 maji. Akamwambia Njoo. Petro akashuka chomboni
 30 akaenda juu ya maji, kuja kwa Isa. Lakini akiziona
 pepo nyingi, akaogopa; akaanza kuzama, akapiga yowe,
 31 akasema, Bwana, uniokoe. Marra Isa akamnyoshea
 mkono akamshika, akamwambia, Ewe mwenyi imani
 32 haba, mbona umekuwa na shaka? Wakapanda cho-
 33 mboni; zikakoma pepo. Nao waliomo chomboni wakaja
 wakamsujudia, wakasema, Hakika yako u Mwana wa
 Muungu.

34 Na walipokwisha vuka wakafika inchi ya Genesareti.
 35 Wakamtambua watu wa mahali pale, wakapeleka ka-
 tika ujirani wote, wakamletea wote waliokuwa hawa-
 36 wezi, wakamsihi waguse hatta upindo wa mavazi yake;
 na waliogusa wakapona wote.

15 NDIPO wakaja kwa Isa waandishi na Mafarisayo wa
 2 Yerusalemi, wakasema, Mbona waanafunzi wako huli-
 halifu tulilopokea kwa wazee? kwani hawanawi mikono
 walapo chakula.

3 Akajibu akawaambia, Mbona na ninyi imahalifu
 4 amri za Muungu kwa mlivyopokea? Kwani Muungu
 aliamuru akasema, Waheshimu baba yako na mama,
 5 na, Atukanaye baba ao mama, afe mauti: nanyi mwa-
 sema, Amwambiaye baba ao mama, Ni sadaka, yote iku-
 6 faayo kwangu, asiheshimu babaye wala mamaye.
 Mmetangua amri za Muungu kwa mlivyopokea ninyi.
 7 Enyi wanafiki, vema aliwatabiria Isaya, akisema,
 8 Watu hawa wamenikaribia kwa kanwa lao, wameniheshimu kwa midomo, lakini mioyo yao imenifarikia
 9 sana. Nao waniabudu bure wafundishapo elimu amri
 10 za waana adamu. Akawaita mafuatano akawaambia,
 11 Sikieni, katambueni: sicho kiingiacho kanwani kimtiacho
 mtu uchafu; lakini kitokacho kanwani, ndicho kimtiacho
 uchafu.

12 Wakaja waanafunzi wake wakamwambia, Wajua ya

kwamba Mafarisayo wamechukiwa wakiyasikia maneno hayo? Akawajibu, akasema, Killa pando asilolipanda 13
Baba yangu ya mbinguni litang'olewa. Waacheni hao: 14
ndio vipofu viongozi wa vipofu, na kipofu akimchukua
kipofu wote wawili watatumbukia shimoni.

Akajibu Petro, akamwambia, Utufasirie mfano huo. 15
Isa akasema, Hatta ninyi tena hamtambui? Hamku-¹⁶₁₇
mbuki ya kwamba killa kiingiacho kanwani chapita
tumboni, na chatoka chooni? Lakini vitokavyo kanwani 18
vyatoka moyoni; ndivyo vimtiavyo mtu uchafu. Kwani 19
moyoni hutoka mawazo maovu, mauaji, mazini, asherati,
maibaji, shahidi za uwongo, matukano; ndiyo yamtiayo 20
mtu uchafu. Lakini kula asiponawa mikono hamtii
mtu uchafu.

Isa akatoka huko, akaenda upande wa Turo na Sidón. 21
Na mwanamke Mkananaya wa mipaka ile aliondoka 22
akamlilia, akasema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa
Daúd: binti yangu anasumbuka sana na pepo. Naye 23
hakumjibu neno. Waanafunzi wake wakaja wakamsihi,
wakasema, Mwache acende zake, kwani apiga makelele
nyuma yetu. Naye akajibu, akasema, Sikupelekwa illa 24
kwa kondoo zilizopotea za nyumba ya Israeli. Naye 25
akaja akamsujudia, akasema, Bwana, unisayidie. Aka- 26
jibu akasema, Si vema kutwaa mkate wa watoto kuwa-
tupia mbwa. Akasema, Yakini, Bwana, lakini mbwa hula 27
vidogo viangukavyo mezani kwa bwana zao. Akajibu 28
Isa, akamwambia, Ee mwanamke, imani yako ni kubwa;
ulipate ulitakalo. Akapona binti yake tangu saa ile.

Isa akapita huko akaja kando la bahari ya Gali- 29
laya. Akakwea mlimani, akakaa kitako huko. Wa- 30
kaja makutano mengi wakawaleta wachechemeo, na
vipofu na walio bubu, na vilema, na wangine wengi,
wakawaweka miguuni pa Isa; akawaponya. Hatta ma- 31
kutano wakastaajabu, wakiwaona bubu wakisema,
vilema wakiwa wazima, wachechemeo wakitembea,
na vipofu wakiona, wakamtukuza Muungu wa Israeli.

Isa akawaita waanafunzi wake, akasema, Nawasiki- 32
tikia mafuatano, kwani sasa wamedumu nami siku tatu
wasipate kula; sipendi kuwaacha kwenda zao waki-
funga, wasizimie njiani. Waanafunzi wake waka- 33
mwambia, Tutapataje vyakula hapa katika nyika tuwa-
shibishe makutano haya? Isa akawaambia, Mnayo 34

mikate mingapi? Wakamwambia, Saba, na samaki
 35 ndogo chache. Akaamrisha makutano wakae kitako.
 36 Akaitwaa mikate saba na samaki, akashukuru, aka-
 vunja, akawapa waanafunzi wake, na waanafunzi maku-
 37 tano. Wakala wote wakashiba; wakaokota makombo
 38 yaliyosalia vikapu saba vilivyojaa. Nao waliokula wali-
 kuwa waanaume elfu 'nne, na waanaake na watoto.
 39 Akawaaga makutano, akapanda chomboni akaenda
 upande wa Magdala.

16 MAFARISAYO na Masadukayo wakaja kumjaribu,
 2 wakamtaka awaonyeshe ishara mbinguni. Akajibu,
 akawaambia, Ikiwa jioni, mwasema, Shwari: uwingu u
 3 mwekundu; na assubui, Uwingu u mwekundu na kume-
 tanda: leo tháruba. Enyi wanafiki, mwajua kubashiri
 kwa kutazama uwingu, lakini dalili za zamani hamzijui?
 4 Kizazi kibaya na cha zani chataka ishara; wala hakita-
 pewa ishara, illa ishara ya nabii Yunus. Akawaacha,
 akaenda zake.

5 Na waanafunzi wake walipofika ng'ambo ya pili wali-
 6 kuwa wamesahau kuleta mikate. Isa akawaambia,
 Angalieni, mjilinde kwa chachu la Mafarisayo na Masa-
 7 dukayo. Wakawaza moyoni, wakasema, Ni kwa sababu
 8 hatukuleta mikate. Akajua Isa, akawaambia, Mwawa-
 zani moyoni, enyi wa imani haba, kwa sababu hamku-
 9 leta mikate? Hamjapata kujua, wala hamkumbuki
 mikate mitano kwa elfu tano, na vikapu vingapi mli-
 10 vyookota? Wala mikate saba kwa elfu 'nne na vikapu
 11 vingapi mlivyookota? Ginsi gani hamkutambua mimi
 sikunena kwa mikate, Angalieni chachu la Mafarisayo
 12 na Masadukayo? Ndipo wakatambua hakusema yeye
 kuangalia chachu la mkate, lakini mafundisho ya Mafa-
 risayo na Masadukayo.

13 Akija Isa upande wa Kaisaraya ya Filipino, akawaauliza
 waanafunzi wake, Watu waninena nani mimi Mwana
 14 wa adamu? Wakamwambia, Wangine Yohana 'mba-
 tizaji, wangine Eliya, wangine Yeremiya ao nabii
 15 mmoja. Akawaambia, Ninyi mwaninena nani? Si-
 16 mán Petro akajibu, akasema, Wewe u Masiya, Mwana
 17 wake Muungu aliye hayi. Akajibu Isa, akamwambia,
 Heri wewe, Simán bar Yunus; kwamba nyama na damu
 hazikufunulia haya, illa Baba yangu aliye mbinguni.
 18 Nami nakwambia, ndiwe Petro; na katika mwamba huu

nitalijenga kanisa langu, wala milango ya ahera haitalishinda. Nitakupa tena funguo za ufalme wa mbingu; 19 na lo lote utakalolifunga duniani, litafungwa mbinguni, na lo lote utakalolifungua duniani, litafunguliwa mbinguni. Akawaonya waanafunzi wake wasimwambie 20 mtu ya kwamba ndiye Masiya.

Tangu hapo akaanza Isa kuwafunulia waanafunzi 21 wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemi, na kusumbuka sana na wazee, na wakohani wakuu, na waandishi; na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka. Petro 22 akamtwaa akaanza kumnenea, akasema, Sivyoy, Bwana, hutapata hivi. Akageuka, akamwambia Petro, Rudi 23 nyuma yangu, Shetani: u chukizo kwangu; ukiwa hu- pendi mambo ya Muungu, illa yale ya waana adamu.

Isa akawaambia waanafunzi wake, Killa atakaye kuja 24 nyuma yangu, ajikanie nafsi yake, atweke msalaba wake, anifuate. Kwani yule atakaye kuhifathi roho 25 yake ataipoteza; na yule apotezaye roho yake kwa ajili yangu ataipata. Itamfaa mtu nini, kupata dunia pia, 26 roho yake ikimpotea, ao nini atatoa mtu kuwa badala ya roho yake? Kwani Mwana wa adamu atakuja ka- 27 tika utukufu wa Baba yake na malaika zake; ndipo atamlipia killa mtu kwa amali zake.

Amín nawaambia, pana watu wasimamao hapa, wa- 28 siopata kufa, hatta watakapomwona Mwana wa adamu akija katika ufalme wake.

BAADA ya siku sita Isa akawatwaa Petro na Yakób 17 na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mkubwa peke yao. Akageuka mbele zao, uso wake ukang'ara 2 kama jua, na mavazi yake yamekuwa meupe kama nuru. Wakawatokea Musa na Eliya, wakisema naye. Petro 3 akajibu akamwambia Isa, Pema, Bwana, hapa tukae; kama ukipenda, tutafanya hapa vibanda vitatu, kimoja 4 chako, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipo- 5 kuwa akisema, wingu jeupe likawatia uvuli, sauti ika- toka winguni, ikasema, Huyu ni mwanangu, mpenzi wangu, anifurahishaye: msikilizeni. Na waanafunzi 6 wakiisikia wakaanguka fulifuli, wakaogopa sana. Isa 7 akawakaribia, akawagusa, akasema, Ondokeni, wala msioCOPE. Wakainua macho yao, wasimwone mtu, illa 8 Isa peke yake.

Na walipokuwa wakishuka mlimani, Isa akawaamuru, 9

akasema, Msimwambie mtu mlivyoona, hatta Mwana wa adamu atakapofufuka katika wafu.

10 Wakamwuliza waanafunzi, wakasema, Mbona tena waandishi wasema ya kwamba imempasa Eliya kuja
11 kwanza? Isa akajibu akawaambia, Hakika, Eliya yuja
12 kwanza, na azitengeneza zote; lakini nawaambia ya kwamba Eliya amekwisha kuja, nao wamentendea walivyopenda; vivyo na Mwana wa adamu atateswa nao.
13 Yakawaelea waanafunzi, ya kwamba alimnenea Yohana 'mbatizaji.

14 Walipowawasilia makutano akaja mtu mmoja akam-
15 mpigia magote akamwambia, Bwana, umrehemu mwana-
ngu, aliye na kifafa na kuteswa sana, kwani marra
16 nyingi huanguka motoni na marra nyingi majini. Ni-
kamleta kwa waanafunzi wako, wasiweze kumponya.
17 Isa akajibu, akasema, Enyi kizazi kisicho na imani na
kilichopotoka, hatta lini nitakaa nanyi? hatta lini nita-
18 chukuliana nanyi? Niteee huyo hapa. Isa akamkari-
pia pepo; akatoka; kijana akapona tangu saa ile.

19 Waanafunzi wakamjia Isa kwa faragha wakasema,
20 Mbona sisi hatukuweza kumfukuza? Isa akawaambia,
Kwa sababu ya kutoa kuamini kwenu. Amín nawa-
ambia, kama mngekuwa na imani kama mbegu ya kha-
radali, mkiwambia mlima huu, Pita tangu hapa hatta
21 kule, ungepita; wala hakuna neno msiloweza. Lakini
ginsi hii hafukuzwi illa kwa kuomba na kufunga.

22 Walipokikaa katika Galilaya, Isa akawaambia, Mwana
wa adamu anakwenda kutolewa mikononi kwa watu,
23 nao wata'mua, na siku ya tatu atafufuka. Wakasikitika
sana.

24 Wakiwa wamefika Kapernaúm wale watwao fitiri
wakamjia Petro wakasema, Mwalimu wenu halipi fitiri?
25 Akasema, Yakini. Na alipoingia nyumbani, Isa aka-
mtangulia, akasema, Waonaje, Simán? Katika watu
gani wafalme wa dunia hutwaa ushuru na kodi? Ka-
26 tika waana wao, ao katika wageni? Petro akamwambia,
Wageni. Isa akamwambia, Bassi tena waana hawalipi.
27 Lakini illi tusiwachukize, enende baharini, ukatumbu-
kize doana, utwae samaki azukaye kwanza; ukifunua
kinwa chake, utaona fetha: utwae ukawape kwa mimi
na wewe.

18 SAA ile waanafunzi wakamjia Isa, wakisema, Ni

nani aliye mkuu katika ufalme wa mbingu? Isa akaita 2
 mtoto aka'mweka katikati yao, akasema, Amín nawaa- 3
 mbia, msipoongoka kuwa kama watoto, hamtaingia ka-
 tika ufalme wa mbingu. Bassi anenyekeaye kama 4
 mtoto huyu, ndiye mkuu katika ufalme wa mbingu.
 Naye amkaribishaye mtoto mmoja kama huyu kwa 5
 jina langu, ndimi anikaribishaye. Naye amchukizi- 6
 shaye mtoto mmoja wao waniaminio, afathali angali-
 funguwa shingoni jiwe la kusagia, na angalitupwa
 kilindini mwa bahari.

Ole wa ulimwengu kwa sababu ya machukizo! 7
 Hakuna buddi kuwa machukizo, lakini ole wake mtu
 yule machukizo yakitoka kwake! Kama mkono wako 8
 ao mguu wako utakuchukizisha, ukate, uutupie mbali;
 u heri uingie katika uzima ukipunguka mguu ao mkono,
 zayidi ya mwenyi mikono miwili na miguu miwili
 utupwe motoni mwa milele. Na kama jicho lako lita- 9
 kuchukizisha, uling'oe, ulitupie mbali; u heri uingie
 katika uzima mwenyi chongo, wala mwenyi macho ma-
 wili usitupwe katika jehannum ya moto.

Angalieni msitharau huyu mmojawapo mdogo; kwani 10
 nawaambia ya kwamba mbinguni malaika zao huona
 sikuzote uso wa Baba yangu aliye mbinguni. Kwani 11
 Mwana wa adamu amekuja amwokoe aliyepotea. Mwao- 12
 naje? Mtu angekuwa na kondoo mia, kama mmoja-
 wapo angepotea, hangewaacha tissia na tissaini, akaenda
 milimani amtafute aliyepotea? Na akipata kumwona, 13
 amín nawaambia, atamfurahia zayidi, kuliko wale tissia
 na tissaini wasiopotea. Vivyo haipendeki mbele za 14
 Baba yenu aliye mbinguni mmojawapo wa wadogo hawa
 apotee.

Kama ndugu yako amekukosa, enende umnenee wewe 15
 na yeye peke yenu: kama atakusikiliza, umepata ndugu
 yako. Kama hatakusikia, chukua nawe tena mmoja ao 16
 wawili, illi kwa kanwa la mashahidi wawili ao watatu
 killa nenø litengezeke. Kama hatawakubali hawa, 17
 uwaambie kanisa: hatta asipokubali kanisa, umwone
 kama mtu wa mataifa na aliye publikano. Amín na- 18
 waambia, mtakayoyafunga duniani, yatafungwa mbi-
 nguni; na mtakayofungua duniani, yatafunguliwa mbi-
 nguni. Tena nawaambia kwamba wawili wenu wataka- 19
 popatana duniani kwa jambo mtakaloliomba, watafanyi-

20 kiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwani wawili
ao watatu wakusanyikako kwa jina langu, nami niko
huko katinakati.

21 Akaja Petro akamwambia, Bwana, marra ngapi ndugu
22 yangu akinikosa, nimsamehe? hatta marra saba? Isa
akamwambia, Sikwambii hatta marra saba, lakini hatta
marra sabwini fi saba.

23 Kwa sababu hii ufalme wa mbingu umefanana na
mfalme mmoja atakaye kufanya hesabu na watumwa
24 wake. Akiwa amekwanza kutwaa hesabu, aliletewa
25 mmoja awiwaye naye talanta elfu kumi; na asipokuwa
na kitu cha kumlipia, bwana wake akaamuru auzwe,
yeye na mkewe na watoto wake, na cho chote alichu
26 nacho, illi deni ilipwe. Mtumwa yule akaanguka, aka-
msujudia, akamwambia, Bwana, niwie kwa saburi, nami
27 nitakulipia pia. Bwana wa mtumwa yule akamsikitikia,
akamfungua, akamsamehe deni ile.

28 Mtumwa yule akatoka akamwona mjoli wake, awiwaye
naye dinari mia; akamkamata akamshika koo, akasema,
29 Nilipie uwiwayo. Mjoli wake akamwangukia miguuni
pake, akamsihi akamwambia, Niwie kwa saburi, nami
30 nitakulipia pia. Akakataa, akaenda akamtupa kifu-
31 ngoni hatta atakapolipa deni. Wajoli wake wakiyaona
mambo haya, wakasikitika sana; wakaenda wakamwe-
32 lezea bwana wao mambo yaliyotendeka yote. Bassi,
bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa
33 mwovu, sikukusamehe deni ile yote uliponisihi? nawe
haikukupasa kumsikitikia mjoli wako, kama mimi nili-
34 vyokusikitikia wewe? Bwana wake akakasirika, akam-
toa kwa asikari, hatta atakapolipa deni yake yote.

35 Vivyo na Baba yangu wa mbinguni atawatendea
ninyi, kama ha'mwasamehe kwa moyo killa mtu ndu-
guye makosa yao.

19 IKAWA alipokwisha Isa maneno haya, akatoka ka-
tika Galilaya akaja upande wa Uyahudi ng'ambo ya
2 pili ya Yardeni. Makutano mengi wakamfuata, akawa-
ponya huko.

3 Mafarisayo wakamkaribia wakimjaribu, wakamwuliza
kama halali mtu amwache mkewe kwa sababu zote.
4 Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye
5 aliyewaumba kwanza, aliwaumba mume na mke, aka-
sema, Kwa sababu hii, mtu aache baba na mama,

aambatane na mkewe, nao wawili watakuwa mwili mmoja? Kama hivyo si wawili tena, lakini mwili mmoja. Bassi Muungu aliowaunga, mwana Adamu asiwatenge.

Wakamwambia, Ginsi gani Musa akaamuru, ampe khati ya talaka, amwache? Akawaambia, Musa kwa mioyo yenu kwa kuwa migumu amewapa ruhusa kuwacha wake wenu; lakini tangu mwanzo sivyo. Nawaambia ninyi, Yee yote amwachaye mkewe, illa kwa zani, akioa mwingine azini; naye amwoaye aliyeachwa azini.

Waanafunzi wake wakamwambia, Mambo ya mtu na mkewe yakiwa kama haya, afathali asioe. Akawaambia, Hawapokei wote neno lile, illa waliopewa. Kuna matowashi wangine waliozaliwa hivi toka tumbo la mama; kuna matowashi wangine waliofanyika maksai na watu; kuna matowashi wangine waliojifanya matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbingu. Awezaye kupokea, apokee.

Bassi wakamletea watoto, awatie mikono yake, awaombe; waanafunzi wakawafanyia ukali; lakini Isa akawaambia, Acheni watoto, usiwakataze kuja kwangu, kwani walio kama hawa ufalme wa mbingu ni wao. Akawatia mikono, akatoka huko.

Akaja mmoja, akamwambia, Mwalimu mwema, neno gani jema nitakalofanya, nipate uzima wa milele? Akamwambia, Mbona waniita mwema? Hakuna mwema illa mmoja, ndiye Muungu. Ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. Akamwambia, Amri zipi? Isa akasema, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uwongo, Uwaheshimu baba yako na mama, na, Umpende jirani yako kama moyo wako. Kijana akamwambia, Hizi zote nimezishika tangu utoto wangu: nimepunguka nini tena? Isa akamwambia, Kama wataka kuwa mkamilifu, enende uziuze mali zako uwape masikini; na utapata mali mbinguni; ukaje, unifuatē. Kijana aliposikia maneno haya akaenda zake akasikitika; kwani mali yake mengi.

Isa akawaambia waanafunzi wake, Amín nawaambia ya kwamba shidda mwenyi mali kuingia katika ufalme wa mbingu. Nawaambia tena, ni wepesi ngamia apite katika tundu ya sindano, kuliko mwenyi mali aingie katika ufalme wa Muungu.

25 Waanafunzi wake waliposikia haya, wakastaajabu
26 sana, wakasema, Ni nani tena awezaye kuokoka? Aka-
waangalia Isa, akawaambia, Kwa watu haiwezekani;
kwa Muungu mambo yote yawezekana.

27 Akajibu Petro, akamwambia, Sisi tumeacha vyote,
28 tukakufuata: tutapata nini tena? Isa akawaambia,
Amín nawaambia ya kwamba ninyi mwalionifuata,
katika uzazi wa pili, atakapoketi Mwana wa adamu
kitini mwa enzi yake, nanyi mtaketi vitini thenashara,
29 mkiwahukumu kabila thenashara za Israeli. Na yeye
yote aliyeacha nyumba, ao ndugu, ao maumbu, ao baba,
ao mama, ao mke, ao watoto, ao mashamba, kwa ajili
ya jina langu, atapata tena marra mia, na atarithi
30 uzima wa milele. Lakini wengi walio wa kwanza
watakuwa wa mwisho, na wa mwisho watakuwa wa
kwanza.

20 KWANI ufalme wa mbingu umefanana na mtu
mwenyi nyumba, aliyetoka alfajiri kuajiri kulima katika
2 mizabibu yake. Na alipokwisha kupatana na wakulima
kwa dinari kwa siku, akawatuma katika mizabibu yake.
3 Akatoka kama saa ya tatu, akaona wangine wasimamao
4 sokoni, wasio na kazi; akawaambia, Enendeni nanyi
katika mizabibu yangu, na kinipasacho nitawapa. Wa-
5 kaenda. Akatoka tena kama saa ya sita na saa ya
6 kenda, akafanya vilevile. Akatoka kama saa ya eda-
shara akaona wangine wakisimama wasio na kazi. Aka-
wauliza, Mbona mmesimama hapa mchana kutwa burre?
7 Wakamwambia, Kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri.
Akawaambia, Enendeni na ninyi katika mizabibu, na
kilicho haki mtapewa.

8 Na jua likichwa, bwana wa mizabibu amwambia msi-
mamizi wake, Waita wakulima uwalipe ijara, ukianza
9 na wale wa mwisho hatta wale wa kwanza. Na wakija
wao wa saa ya edashara wakapokea killa mtu dinari.
10 Na wakija wale wa kwanza wakathani watapewa zayidi,
11 wakapokea nao killa mtu dinari. Walipoipokea waka-
12 mwamba mwenyi nyumba, wakasema, Hawa wa mwisho
wametenda saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi
13 tuliosumbuka na uzito na hari ya mchana. Akamjibu
mmoja wao akasema, Mwenzangu, sikukuthuru. Huku-
14 patana nami kwa dinari? Twaa iliyo yako kaenda zako.
15 Napenda kumpa huyu wa mwisho kama wewe. Si

halali nitumie zilizo zangu nipendavyo mimi? Ao jicho
lako ovu kwa sababu kuwa mwema mimi?

Vivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa 16
kwanza wa mwisho; kwani wengi waitwao, wateule
wachache.

Akapanda Isa kwenda Yerusalemi. Akawatwaa wa- 17
anafunzi thenashara kwa faragha njiani akawaambia,
Angalieni, twapanda hatta Yerusalemi; na Mwana wa 18
adamu atatolewa kwa wakohani wakuu na kwa waandi-
shi, nao watamhukumia kufa, na watamtoa kwa ma- 19
taifa wamfanyizie mzaha, na wampige, na wamsulibi;
hatta siku ya tatu atafufuka.

Mama wa waana wa Zebedayo akamkaribia na waana- 20
we, akimsujudia, akataka haja kwake. Akamwambia, 21
Wataka nini? Akamwambia, Useme waana wangu
wawili hawa wakae mmoja mkono wa kuume wako, na
inmoja mkono wa kushoto wako, katika ufalme wako.
Isa akajibu, akasema, Hamjui mlitakalo. Mwaweza 22
kunywa kikombe nitakachokunywa mimi, na kubatizwa
kwa ubatizo nibatizwavyo mimi? Wakamwambia,
Twaweza. Akawaambia, Mtakunywa kikombe changu, 23
na kwa ubatizo nibatizwavyo mimi mtabatizwa; lakini
kukaa mkono wa kuume wangu na mkono wa kushoto
wangu, si kwangu nitoe, illa kwao waliofanyiziwa na
Baba yangu.

Na wale kumi waliposikia wakakasirika na ndugu 24
wawili. Lakini Isa akawaita akawaambia, Mwajua ya 25
kwamba majumbe wa mataifa huwatawala, na wakuu
wao huwafanyia nguvu. Lakini kwenu sivyo; yeye 26
yote atakaye kuwa mkuu kwenu, awangojee; na yeye 27
yote atakaye kuwa wa kwanza kwenu, awe mtumwa
wenu: kama Mwana wa adamu hakuja kutumikiwa, 28
lakini kutumika, na kutoa roho yake kwa dia za
wengi.

Na walipokuwa wakitoka Yerikho makutano mengi 29
wakamfuata. Na vipofu wawili wakikaa kando la njia, 30
waliposikia ya kwamba Isa anapita, wakapiga kelele,
wakasema, Uturehemu, Bwana, mwana wa Daúd!
Makutano wakawakaripia wanyamaze. Lakini waka- 31
zidi kupiga makelele, wakisema, Uturehemu, Bwana,
Mwana wa Daúd! Isa akasimama akawaita, akasema, 32
Mwanitaka niwafanyie nini? Wakamwambia, Bwana, 33

34 macho yetu yafunuke. Isa akawasikitikia, akawagusa macho; marra macho yao yakaona, wakamfuata.

21 WALIPOKUWA wamekaribia Yerusalemi, wakafika katika Betfage kwa kilima cha Zeituni, Isa aliwatuma
2 waanafunzi wawili, akawaambia, Enendeni mji ulio-walekea; na marra mtaona punda amefungwa na mtoto
3 naye; fungueni, mniletee. Na kama mtu atawaambia neno, semeni, Bwana ndiye awatakaye; na marra moja atawapeleka.

4 Haya yote yakafanywa illi yatimie yaliyonenwa na
5 nabii, akisema, Mwambie binti Sayuni, Tazama, mfalme wako anakuja kwako, mwenyi upole, amepanda punda na mwana punda mtoto wa punda.

6 Waanafunzi wakaenda wakafanya kama alivyowaagiza
7 Isa. Wakaleta punda na mtoto, wakaweka juu yao
8 nguo zao, wakampandisha juu yao. Na wengi wa mafuatano wakatua nguo zao njiani; wangine waka-
9 kata matawi ya miti, wakayatua njiani. Na makutano waliotangulia na waliofuata wakapiga makelele, waka-
10 sema, Osana Mwana wa Daúd, ndiye mbarikiwa ajaye
11 kwa jina la Bwana; Osana juu yote. Na alipoingia katika Yerusalemi, mji wote ukataharaki, wakasema,
12 Nani huyu? Mafuatano wakasema, Huyu ndiye Isa, nabii atokaye Nazareti ya Galilaya.

12 Akaingia Isa katika hekalu la Muungu, akawafukuza wote wakuzao na wafanyao biashara ndani ya hekalu, akapindua meza zao wabadilio fetha, na makao yao
13 wakuzao njiwa. Akawaambia, Imeandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya kuomba; nanyi mmeifanya paango la waivi.

14 Na vipofu na wachechemeo wakamjilia katika hekalu, akawaponya.

15 Wakohani wakuu na waandishi walipoona miujiza aliyoifanya, na vijana wapigao kelele katika hekalu, waki-
16 sema, Osana, Mwana wa Daúd, wakakasirika sana, wakamwambia, Wasikia hawa wasemalo? Isa akawaambia, Yakini. Hamkusoma kabisa, Kwa kanwa la watoto na
17 wanyonyao umetimiliza sifa? Akawaacha, akatoka mjini hatta Betania, akashinda kule.

18 Hatta assubui akirudi mjini, akashikwa na njaa.
19 Akaona mtini mmoja katika njia, akaufikia, asione kitu illa majani matupu. Akauambia, Usizae matunda tena

hatta milele. Mtini ukanyauka upesi. Waanafunzi 20
wakaona wakashangaa, wakasema, Umenyaukaje mtini
upesi! Isa akajibu, akawaambia, Amín nawaambia, 21
kama mngalikuwa na imani, msipoingiwa na shaka,
mngekuwa mkifanya si hii tu katika mtini, lakini
mkiuambia mlima huu, Utolewe, utupwe baharini, ita-
fanyika; na lo lote mtakalo katika kuomba, mkiwa na 22
imani, mtalipokea.

Akaja katika hekalu; na alipokuwa akifundisha, wako- 23
hani wakuu na wazee wa watu wakaja, wakasema, Kwa
nguvu gani wafanya hivi? Na umepewa na nani nguvu
hii? Akajibu Isa, akawaambia, Nami nitawauliza neno 24
moja: mtakaponijibu, nitawaambia kwa nguvu gani na-
fanya hivi. Ubatizo wa Yohana umetoka wapi? Ka- 25
tika mbingu, ao katika watu? Wakafikiri wao kwa
wao, wakasema, Tukimwambia katika mbingu, atasema,
Mbona hamkumsadiki? Tugesema, katika watu, 26
twaogopa makutano, kwani wote wamwona Yohana
alikuwa nabii. Wakamjibu Isa, wakasema, Hatujui. 27
Naye akawaambia, Wala mimi siwaambii kwa nguvu
gani nimefanya hivi. Mwaonaje? Mtu mmoja aliku- 28
wa na waana wawili; akamjia wa kwanza, akasema,
Mwanangu, enende leo ufanye kazi katika mizabibu
yangu. Akajibu, akasema, Sitaki; halafu akatubu, 29
akaenda. Akamjia wa pili, akasema yaleyale. Naye 30
akajibu akasema, Naenda, bwana; asiende. Yupi wa 31
hawa wawili aliyefanya alilolitaka babaye? Waka-
wambia, Yule wa kwanza.

Isa akawaambia, Amín, nawaambia, mapublikano na
makahaba wawatangulia ninyi kuingia katika ufalme
wa Muungu. Kwani Yohana alikuja kwenu kwa njia 32
ya haki, wala hamkumwamini; lakini mapublikano na
makahaba wakamwamini; wala ninyi mlipowaona ham-
kugeuka tena kumwamini.

Sikilizeni mfano mwingine. Kulikuwa mtu mwenyi 33
nyumba, akapanda mizabibu, akazungusha kitalu, aka-
chimba shinikizo, akajenga mnara, akawapangisha wa-
kulima, akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa 34
karibu akawapelekea wakulima watumwa wake wapokee
matunda; wakulima wakawatwaa watumwa wake, waka- 35
mpiga huyu, wakamtupia yule mawe, na yule waka'mua.
Akapeleka tena watumwa wangine wengi kuliko hao wa 36

- 37 kwanza, wakawatendea vilevile. Halafu akawapelekea mwanawe, akisema, Watamheshimu mwana wangu.
- 38 Nao wakulima walipomwona mwana wakasema wao kwa wao, Huyu ndiye mrithi: njooni tu'mue, naswi tuta-
- 39 pata urithi wake. Wakamtwaa wakamtoa mizabibuni
- 40 waka'mua. Atakapokuja bwana wa mizabibu atawa-
- 41 tendea nini wakulima wale? Wakamwambia, Atawa-
- haribu kwa vibaya wabaya wale; na atawapangisha mizabibu wakulima wangine, watakaomlipia matunda kwa wakati wao.
- 42 Isa akawaambia, Hamkusoma kamwe katika maandiko, Jiwe walilolitupa waashi limekuwa kuu la pembeni.
- 43 Kazi yake Bwana hii, na ajabu machoni petu? Kwa sababu hii nawaambia, ya kwamba ufalme wa Muungu utatolewa kwenu, na watapewa taifa wazao matunda
- 44 yake. Naye aangukaye juu ya jiwe hili atavunjika; naye juu yake hili litaanguka, litamvunjavunja kabisa.
- 45 Waliposikia wakobani wakuu na Mafarisayo mifano
- 46 yake, wakatambua aliwanena wao. Na walipotaka kumkamata, wakawaogopa makutano, walio wakamwona kama nabii.
- 22** ISA akajibu, akawaambia tena kwa mifano, akisema,
- 2 Ufalme wa mbingu umefanana na mfalme mmoja aliye-
- 3 fanya arusi ya mwanawe. Akapeleka watumwa wake
- 4 wawaite walioitwa kwa arusi; wakakataa kuja. Akapeleka tena watumwa wangine, akisema, Waambieni walioitwa, Angalia, nimeandaa karamu yangu, nimechinja ng'ombe na vinono, na vyote viko tayari; njooni arusini.
- 5 Wangine wakaenda zao wasisikilize, mmoja katika
- 6 shamba lake, mmoja katika biashara yake; waliosalia wakawatwaa watumwa wake wakawafanyia jeuri, waka-
- 7 waua. Mfalme alipopata habari, akaona hasira, akatuma asikari zake akawaharibu wauaji wale akauteketeza mji
- 8 wao. Akawaambia watumwa wake, Arusi i tayari, wale
- 9 walioitwa hawakustahili. Bassi endeni hatta miisho ya
- 10 njia, na wote 'mwaonao waiteni arusini. Watumwa wale wakatoka njiani wakakusanya wote waliowaona na waovu
- 11 na wema, arusi ikajaa wageni. Alipoingia mfalme kuwatazama wageni, akaona huko mtu asiyevaa vao la arusi.
- 12 Akamwambia, Rafiki, umeingiaje hapa usipokuwa na vao
- 13 la arusi? Akanyamaa kimya. Mfalme akawaambia watumishi, Mfungeni mikono na miguu, mkamchukue,

mmtupe katika giza la 'nje; ndiko kilio na kutafuna meno. Kwani wengi waitwao, wateule wachache. 14

Mafarisayo wakaenda wakafanya shauri wamtege kwa maneno. Wakampelekea waanafunzi wao pamoja na Maherodiani, wakasema, Mwalimu, twakujua wasema kweli, na wafundisha njia ya Muungu katika kweli, wala hujitunzi kwa mtu, kwani huangalii cheo cha watu. Bassi, utwambie, waonaje? Ni halali kumlipia Kaisari kodi au sivyo? Akawajua Isa uovu wao, akasema, Mbona mwanijaribu, enyi wanafiki? Nionyesha fetha la kodi. Wakamletea dinari. Akawaambia, Ya nani sanamu hii, na andiko hili? Wakamwambia, Ya Kaisari. Akawaambia, Mlipia Kaisari vilivyo vya Kaisari, na Muungu vilivyo vya Muungu. Waliposikia, wakataajabu; wakamwacha, wakaenda zao. 15 16 17 18 19 20 21 22

Siku ile wakamkaribia na Masadukayo, wasema hakuna kiyama, wakamwuliza wakasema, Mwalimu, Musa alisema, Mtu akifa, asipokuwa na mtoto, ndugu yake amwoe mkewe, ampatie nduguye wazao. Kulikuwako kwetu ndugu saba; naye wa kwanza akaoa mke, akafa, hana mtoto, akamwachia nduguye mke wake. Vivyo na wa pili, na wa tatu, hatta yule wa saba. Kwa mwisho wa wote akafa na mwanamke. Katika kiyama atakuwa mke wa yupi wa saba? Kwani wote walikuwa naye? Akajibu Isa, akawaambia, Mmekosa, msipojua maandiko wala nguvu zake Muungu. Kwani katika kiyama hawaoi, wala hawaolewi, lakini wako mbinguni kama malaika za Muungu. Na kwa kiyama ya wafu, hamkusoma lililonenwa na Muungu, akisema, Mimi ni Muungu wa Ibrahimu, na Muungu wa Isaak, na Muungu wa Yakób? Muungu si Muungu wa wafu, lakini wao walio hayi. Makutano waliposikia, wakasha ngaa kwa elimu yake. 23 24 25 26 27 28 29 30 31 32 33

Na Mafarisayo, waliposikia ya kwamba amewanyamazisha Masadukayo, wakakusanyika pamoja. Na mmoja wao mfanyaji sheria akamwuliza, akimjaribu, akasema, Mwalimu, amri ipi iliyo kuu ya torati? Isa akamwambia, Umpende Bwana Muungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri ya kwanza na iliyo kuu. Na ya pili imefanana nayo, Umpende jirani yako kama moyo wako. Katika amri hizi mbili zinazo torati yote na nabii zote. 34 35 36 37 38 39 40

⁴¹₄₂ Mafarisayo walipokusanyika Isa akawauliza, akase-
 ma, Mwamwonaje Masiya? Yu Mwana wa nani? Wa-
 43 kamwambia, Wa Daúd. Akawaambia, Kwaje tena
 44 Daúd kwa Roho amwambia Bwana, akisema, Bwana ali-
 mwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuu-
 me, hatta nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako?
 45 Kama Daúd akamwita Bwana wake, kwaje ni mwana
 46 wake? Hakuweza mtu kumjibu neno; wala tangu siku
 ile hakuthubutu mtu kumwuliza tena.

23 ISA akawaambia makutano na waanafunzi wake, aka-
 2 sema, Waandishi na Mafarisayo waketi kitini mwa
 3 Musa; nanyi killa wawaambialo mshike lishikeni mlifa-
 nye; lakini wafanyavyo wao msifanye, kwani wasema
 4 wala hawafanyi. Kwani wafunga mizigo mizito na isi-
 yochukuliana wakaitia watu begani, nao hawataki kui-
 5 tikisa kwa kidole chao. Killa wafanyalo wafanya illi
 kuonekana na watu. Wapanua fulakteria zao, wafanya
 6 makubwa matamvua ya lebasi zao. Wapenda mahali pa
 kwanza katika karamu, na viti vya kwanza katika ma-
 7 sunagogi, na kusalimiwa sokoni, na kuitwa na watu
 8 Rabbi, Rabbi. Ninyi msiitwe Rabbi; kwani mmoja yu
 Mwalimu wenu, ndiye Masiya; nanyi nyote ndugu.
 9 Msimwite mtu duniani baba, kwani mmoja Baba yenu,
 10 aliye mbinguni. Msiitwe ²waalimu; kwani mmoja
 11 Mwalimu wenu, ndiye Masiya. Naye aliye mkuu wenu
 12 awe mtumishi wenu. Yee yote ajitukuzaye atathilika;
 na yote ajithiliye atatukuka.

13 Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! mme-
 shindika ufalme wa mbingu mbele za watu: hamwingii
 ninyi, wala waliokuwa wakiingia ha'mwaachi kuingia.

14 Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki!
 mwakula nyumba za wajani, na mwajifanya kama
 kusali sana: kwa sababu hiyo mtazidi kulaaniwa.

15 Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! mme-
 zunguka katika bahari na inchi kumfanya mtu mmoja
 mwongofu, na mlipompata, mwamfanya mwana wa
 jehannum marra mbili kuliko wenyewe.

16 Ole wenu, viongozi vipofu, msemao, Killa aapaye
 kwa hekalu, ni ubatili; naye aapaye kwa thahabu za
 17 hekalu, amejifunga! Enyi wajinga na vipofu: ipi ku-
 18 bwa, thahabu ao hekalu lililozisafisha thahabu? Tena,
 Killa aapaye kwa mathbahu, ni ubatili; lakini killa

aapaye kwa sadaka iliyo juu yake, amejifunga. Enyi 19
wajinga na vipofu: ipi kubwa, sadaka, ao mathbahu
iliyoisafisha sadaka? Hakika yake aapaye kwa math- 20
bahu, aapa kwa hiyo na kwa killa kilicho juu yake;
naye aapaye kwa hekalu, aapa kwa hilo na kwa Yeye 21
akaaye humo; naye aapaye kwa uwingu, aapa kwa 22
kikao cha Muungu na kwa Yeye akaaye juu yake.

Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! mwa- 23
lipa zaka za naana na bizari na kumini, na mmea-
cha mambo makuu ya sheria, hukumumu, na rehema, na
imani: haya yamewapasa kuyafanya, wala msiache yale.
Enyi viongozi vipofu, huchujia imbu mmezapo ngamia. 24

Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! mwa- 25
fanya safi iliyo 'nje ya kikombe na chungu, na kwa
ndani vimejaa uizi na washerati. Ewe Farisayo kipofu, 26
takasa kwanza iliyo ndani ya kikombe na chungu, illi
na vilivyo 'nje viwe safi.

Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! mme- 27
fanana na makaburi yaliyopakiwa nyeupe, kwa 'nje
yaonekana mazuri, lakini kwa ndani yamejaa mifupa
ya wafu na uchafu wote. Vivyo nanyi kwa 'nje mwa- 28
onekana na watu kama wenyi haki, lakini kwa ndani
mmejaa unafiki na unajisi.

Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! mwa- 29
jenga makaburi ya nabii, na mwapamba makumbusho
ya wenyi haki, na husema, Kama sisi tungalikuwa 30
zamani za baba zetu, hatungalisharikiana nao katika
damu za nabii. Hivi mwajishuhudia nafsi zenu, ya 31
kwamba ndinyi waana wao waliowaua nabii. Nanyi 32
jalizeni kipimo cha baba zenu.

Enyi nyoka, waana wa majoka, mtakimbiaje huku- 33
mu ya jehannum? Kwa sababu hii, angalieni, nawa- 34
pelekea nabii na wenyi hekima na waandishi; nanyi
mtawaua na mtawasulibisha wengine wao, na wengine
wao mtawapiga katika masunagogi yenu, na mtawa-
fukuza mji kwa mji: illi mpatilizwe damu ya haki 35
iliyomwagika katika inchi, tangu damu ya Habil aliye
mwenyi haki, hatta damu ya Zakariya wa Barakiya,
mliye'mua kati ya hekalu na mathbahu. Amín na- 36
waambia, mambo haya yote yatafikia kizazi hiki.

Yerusalemi, Yerusalemi, uwauaye nabii, uwatupia 37
mawe waliopelekwa kwako! marra ngapi nimetaka kuwa-

kusanya watoto wako, kama kuku hukusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa, wala hamkukubali!

³⁸₃₉ Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa tupu. Kwani nawaambia, Hamtaniona tangu leo, hatta mtakaposema, Ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina lake Bwana.

24 ISA akatoka akaliacha hekalu; wakaja waanafunzi
2 wake, wamwonyeshe majengo ya hekalu. Isa akawaambia, Hamyaoni haya yote? Amín nawaambia, hali-
3 tasalia hapa jiwe juu ya jiwe lisiloangushwa. Alipokuwa amekaa kitako juu ya kilima cha Zeituni, waanafunzi wakaja kwa faragha, wakamwambia, Utwambie, mambo haya yatakuwa lini? Na nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?

4 Isa akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwada-
5 nganye. Ndio wengi watakaokuja na jina langu, wa-
6 kisema, Mimi Masiya; na watadanganya wengi. Nanyi mtasikia vita na habari za vita. Angalieni, msitaabike; shuruti haya yote yatakuwa; lakini mwisho hau-
7 jaja bado. Kwani taifa litaondokea taifa, na ufalme juu ya ufalme; zitakuwako na njaa, na tauni, na
8 matetemeko pahali pahali. Hizi ndizo mwanzo wa mi-
9 siba. Kiisha watawatoa ninyi kuteswa, na watawaua; na mtachukiwa na mataifa yote kwa sababu ya jina langu.
10 Ndipo wengi watachukizwa, nao watatoana na watachukiana. Na nabii wengi wa uwongo wataondoka, na
12 watadanganya wengi. Na kwa sababu ya kujaa uovu,
13 mapenzi ya wengi yatapoa. Naye atakayedumu hatta
14 mwisho ataokoka. Na anjili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kwa ushahidi kwa mataifa yote; halafu mwisho utakuja.

15 Wakati mtakapoona chukizo la ukiwa, alilonena nabii Danieli, likisimama mahali patakatifu; (asomaye atambue;) wakati ule walioko katika Uyahudi wakimbie
17 hatta milimani; alioko darini asishuke akichukue kitu
18 kilichomo nyumbani mwake, wala alioko mashamba
19 asirudi nyuma achukue nguo zake. Ole wao wanao na
20 mimba na wanyonyeshao zamani zile. Ombeni makimbio yenu yasiwe wakati wa baridi, wala siku ya sabato.
21 Kwani yatakuwa mateso mazito, kama hayakuwa tangu mwanzo wa ulimwengu hatta leo, wala hayatakuwa
22 baadaye. Na siku zile zisipopunguzwa, hangaliokoka mtu; lakini kwa sababu ya wateule siku zile zitapu-

nguzwa. Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, yupo 23
 hapa Masiya, ao yuko kule, msisadiki. Kwani Masiya 24
 za uwongo wataondoka na nabii za uwongo, nao watatoa
 ishara kubwa na mataajabu, hatta kupoteza, kama ya-
 mkini, nao wateule. Angalieni, nimewatabiria. Kwa ²⁵/₂₆
 sababu hii wakiwaambia, Yuko katika jangwa, msitoke :
 Yumo chumbani mwa ndani, msisadiki. Kwani kama 27
 umeme watoka mashariki na wamulika hatta magharibi,
 vivyo na kuwako Mwana wa adamu. Killa uliko mzoga, 28
 huko na tai watakusanyika.

Na gháfala baada ya mateso ya siku zile, jua litatiwa 29
 giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaan-
 nguka mbinguni, na nguvu za mbingu zitatikisika.
 Ndipo itaonekana dalili yake Mwana wa adamu, akija 30
 katika mawingu ya mbingu na nguvu na utukufu mwi-
 ngi. Naye atatuma malaika zake na paanda lenyi sauti 31
 kuu, nao watawakusanya wateule wake katika pepo 'nne,
 tokea 'ncha ya mbingu hatta 'ncha yao.

Mjifunze mfano kwa mtini : tawi zake zikiwa nyororo 32
 zikachanua majani, mwajua ya kwamba wakati wa hari
 u karibu ; vivyo na ninyi mtakapona haya yote, jueni 33
 ipo karibu mlangoni. Amín nawaambia, hakitapita ki- 34
 zazi hiki hatta haya yote yatakuwa. Mbingu na inchi 35
 zitapita ; maneno yangu hayapiti.

Lakini siku ile na saa ile hazijui mtu, wala malaika 36
 za mbingu, illa Baba yangu pekeyake.

Lakini kama siku za Nuhu hivyo na kuwako Mwana 37
 wa adamu. Kwani kama siku zilizokuwa mbele ya 38
 gharika, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa
 hatta siku alipoingia Nuhu katika safina, wasijue, hatta 39
 gharika lilipokuja likawachukua wote, vivyo atakapoku-
 wako Mwana wa adamu.

Wawili watakuwako mashamba, mmoja atatwaliwa, 40
 mmoja ataachwa ; waanawake wawili watakuwa waki- 41
 saga, mmoja atatwaliwa, mmoja ataachwa.

Kesheni, kwani hamjui wakati ajapo Bwana wenu. 42
 Lakini jueni, kama mwenyi nyumba angalijua wakati 43
 mwivi atakapokuja, angalikesha, wala hakuiacha nyumba
 yake itobolewe. Kwa sababu hii na ninyi 'mwe tayari ; 44
 kwani wakati msipothani Mwana wa adamu yuaja.

Ni yupi tena mtumwa yule amini na mwenyi akili, 45
 bwana wake aliyemfanya msimamizi nyumbani mwake,

46 awape chakula wakati wake? Heri mtumwa yule,
47 bwana wake atakapokuja, akimwona akitenda hivi. Amín
nawaambia, atamfanya mkuu juu ya mali zake zote.

48 Lakini kama mtumwa yule mbaya atasema moyoni
49 mwake, Bwana wangu anakawia kuja; naye atianza
kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na
50 walevi; bwana wa mtumwa yule atakuja siku asipomta-
51 zamia na saa asipothani, naye atamkata, na atamwamu-
ru sehemu yake pamoja na wanafiki; ndiko kilio na ku-
tafuna meno.

25 NDIPO ufalme wa mbingu utafanana na vijana
waanawali kumi, waliotwaa taa zao wakatoka kumlaki
2 bwana arusi. Na watano wao wenyi akili na watano
3 wajinga. Nao walio wajinga wakatwaa taa zao, wasi-
4 twae na mafuta. Wale wenyi akili wakatwaa na ma-
5 futa katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Naye
6 bwana arusi akikawia, wote wakasinzia wakalala. Hatta
usiku wa manane, pana kelele, Bwana arusi anakuja;
7 ondokeni mmwende. Nao vijana vyote wakaondoka
8 wakatengeneza taa zao. Wajinga wakawaambia walio
wenyi akili, Tupeni mafuta yenu; taa zetu zinazimika.
9 Lakini walio wa akili wakawajibu, kwamba Hayatoshi
na sisi na ninyi; afathali mwende kwao wakuzao, mpate
10 kununulia. Walipokuwa wakienda wanunue, bwana
arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia naye kwa
11 arusi; mlango ukafungwa. Halafu wakaja wale vijana
12 wangine wakasema, Bwana, bwana, utufungulie. Naye
akajibu, akasema, Amín nawaambia, siwajui ninyi.

13 Nanyi kesheni, kwani hamjui wala siku wala saa ata-
kapokuja Mwana wa adamu.

14 Kwani kama mtu akisafiri kwenda inchi iliyo mbali,
15 akawaita watumwa wake, akawatolea mali zake. Aka-
mpa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na
mmoja talanta moja, killa mtu kwa kadri yake; marra
16 akasafiri. Naye aliyepewa talanta tano akaenda aka-
fanya biashara nazo akapata kwa fayida na talanta tano.
17 Vivyo naye na talanta mbili, akapata kwa fayida na
18 talanta mbili. Naye aliyepewa moja, akaenda akafukua
19 katika inchi, akazificha fetha za bwana wake. Siku
nyingi zilipopita, akaja bwana wa watumwa hawo, aka-
20 fanya hesabu nao. Akaja yule aliyepewa talanta tano,
akaleta talanta nyingine tano, akasema, Bwana, ulinipa

talanta tano ; tazama, talanta tano tena nilizopata nazo
 kwa fayida. Bwana wake akamwambia, Vema, mtu- 21
 mwa mwema na amini : ulikuwa amini kwa vitu haba,
 nitakufanya mkuu juu ya vitu vingi : ingia katika furaha
 ya bwana wako. Akaja naye na talanta mbili, aka- 22
 sema, Bwana, ulimipa talanta mbili ; tazama, talanta
 mbili tena nilizopata kwa fayida nazo. Bwana wake 23
 akamwambia, Vema, mtumwa mwema na amini : uliku-
 wa amini katika vitu haba, nitakufanya mkuu juu ya
 vitu vingi : ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja 24
 naye aliyepewa talanta moja, akasema, Bwana, nime-
 kujua wewe mtu mgumu, uvunaye usipopanda, ukusa-
 nyaye usipomwaga ; nikaogopa, nikaenda nikaificha ta- 25
 lanta yako katika inchi ; tazama, unayo iliyo yako.
 Akajibu bwana wake akamwambia, Mtumwa mbaya na 26
 mvivu : umenijua ya kwamba navuna nisipopanda, na-
 kusanya nisipomwaga ; imekupasa kuiweka fetha yangu 27
 nao wazibadilio ; nami nikija ningalipata yangu na
 fayida yake. Mwondoleeni talanta, mpeni alizo nazo 28
 talanta kumi. Kwani killa anayo atapewa, atakuwa na 29
 wingi ; naye asiye nayo ataondolewa na alichu nacho.
 Mtupeni mtumwa asiye faa katika giza za 'nje : ndiko kilio 30
 na kutafuna meno.

Vivyo atakapokuja Mwana wa adamu kwa utukufu 31
 wake, na malaika watakatifu wote naye, atakaa kitini
 mwa utukufu wake, na mataifa yote watakusanyika 32
 mbele yake, naye atawapambanua kama mchungu hupa-
 mbanua kondoo na mbuzi, na atawaweka kondoo mkono 33
 wake wa kuume na mbuzi mkono wa kushoto.

Baadaye Mfalme atawaambia waliopo mkono wake wa 34
 kuume, Njoni, mmebarikiwa na Baba yangu, rithini
 ufalme mliofanyiziwa tangu mwanzo wa dunia. Kwani 35
 nalikuwa na njaa, mkanipa chakula ; nalikuwa na kiu,
 mkaninyweshwa ; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha ; utu- 36
 pu, mkanivika ; nalikuwa mgonjwa, mkanitunza ; nali-
 kuwa kifungoni, mkanijia.

Nao wenyi haki watamjibu, wakisema, Bwana, lini 37
 tulipokuona na njaa, tukakulisha, ao na kiu tukaku-
 nyweshwa ? Lini tulipokuona mgeni, tukakukaribisha, ao 38
 utupu, tukakuvika ? Ao lini tulipokuona mgonjwa, ao 39
 kifungoni, tukakujia ?

Mfalme atajibu akiwaambia, Amín nawaambia, kama 40

mlivyomtendea mmojawapo mdogo wa ndugu zangu hawa, mmenitendea mimi.

41 Kiisha atawaambia walio mkono wa kushoto, Ondokeni mbele yangu, mmelaaniwa, katika moto wa milele, alio-
42 fanyiziwa shetani na malaika zake. Kwani nalikuwa na njaa, wala hamkunipa chakula; nalikuwa na kiu, wala
43 hamkuninyweshwa; nalikuwa mgeni, wala hamkunikaribisha; utupu, wala hamkunivika; mgonjwa, na kifungoni, wala hamkunijia.

44 Na hawa watamjibu, wakisema, Bwana, lini tulipokuona na njaa, ao na kiu, ao mgeni, ao utupu, ao mgonjwa, ao kifungoni, tusipokungojea?

45 Naye atawajibu, akisema, Amín nawaambia, kama msivyomtendea mmojawapo wa hawa wadogo, hamkunitendea mimi.

46 Na hawa watakwenda katika athabu za milele: nao wenyi haki katika uzima wa milele.

26 IKAWA alipokwisha maneno haya yote, Isa akawaambia waanafunzi wake, Mwajua ya kwamba baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, naye Mwana wa adamu atolewa asulibiwe.

3 Ndipo walikusanyika wakohani wakuu, na waandishi, na wazee wa watu, katika nyumba ya Mkohani mkuu
4 aliyelitwa Kayafa, wakafanya shauri wamkamate Isa kwa
5 werevu, wa'mue. Wakasema, Si katika siku kuu, isiwe fitina katika watu.

6 Naye Isa alipokuwako katika Betania nyumbani mwa
7 Simán mwenyi ukoma, akamkaribia mwanamke na kibweta cha alabastro chenye marhamu ya thamani nyingi,
8 akaimimina kitwani mwake akiwa amekaa kitako. Na waanafunzi wakiona, wakakasirika, wakasema, Kwa
9 nini upotevu huu? Kwani marhamu ile ingalikuzwa kwa
10 fetha nyingi na wangalipewa masikini. Isa akijua, akawaambia, Mbona mwamtaabisha mwanamke? Amenifanyia tendo jema. Kwani sikuzote mnao masikini,
12 mimi hamnami sikuzote. Akinimwagia mwili marhamu
13 hii, kwa kuzikwa kwangu ameifanya. Amín nawaambia, killa ihubiriwapo anjili hii katika ulimwengu wote, hili alilolifanya mwanamke huyu litanenwa kwa ukumbusho wake.

14 Bassi mmoja wa wathenashara, jina lake Yuda Iskario-
15 ta, alikwenda kwa wakohani wakuu, akawaambia, Mtaka-

yonipa nini, nami nitamtoa kwenu? Wakafikana naye kwa vipande thelathini vya fetha; na tangu siku hiyo 16 akatafuta nafasi amtoe.

Hatta ya kwanza ya mikate isiyochachwa, waanafunzi 17 walimjia Isa wakamwambia, Wataka tukuandalie kula pasaka wapi? Akasema, Enendeni mjini kwa fullani 18 mkamwambie, Mwalimu anasema, Majira yangu i karibu; nitafanya pasaka kwako na waanafunzi wangu. Waanafunzi wakafanya alivyowaagiza Isa, wakaandalia 19 pasaka.

Ilipokuwa jioni akakaa kitako na wathenashara. 20 Walipokuwa wakila, akasema, Amín nawaambia, ya 21 kwamba mmoja wenu ndiye atakayenitoa. Wakaingiwa 22 na huzuni nyingi, wakaanza killa mtu kumwambia, Bwana, ni mimi? Akajibu, akasema, Yeye aliyetia mko- 23 no pamoja nami katika sahani, ndiye atakayenitoa. Mwana wa adamu yuenda, kama alivyoandikiwa, lakini 24 ole wake mtu yule atakayemtoa Mwana wa adamu! angalikuwa heri mtu yule asipozaliwa. Yuda aliyemtoa 25 akajibu, akamwambia, Rabbi, ni mimi? Akamwambia, Umesema.

Na walipokuwa wakila, Isa akatwaa mkate akauba- 26 riki, akauvunja, akawapa waanafunzi, akasema, Twaeni, leni; ndio mwili wangu. Akatwaa kikombe akashukuru, 27 akawapa, akasema, Nyweni kwa hiki nyote; kwani hiki 28 ni damu yangu ya maagano mapya, iliyomwagika kwa wengi kwa ondoleo la thambi. Nawaambia ya kwa- 29 mba sitakunywa tena zao hili la mzabibu, illa siku ile nitakapolikunywa pamoja nanyi jipya katika ufalme wa Baba yangu.

Na walipokwisha kuimba zaburi wakatoka wakaenda 30 kilima cha Zeituni. Isa akawaambia, Mtachukizwa 31 nyote kwa ájili yangu usiku huu: kwani imeandikwa, Nitampiga mehunga, na kondoo za kundi zitatawanyika. Nami nitakapofufuka nitawatangulia hatta Galilaya. 32 Petro akajibu, akamwambia, Wajapochukizwa wote kwa 33 ájili yako, mimi sitachukizwa kabisa. Isa akamwambia, 34 Amín nakwambia, usiku huu mbele ya kuwika jogoo utanikania marra tatu. Petro akamwambia, Ijaponipasa 35 kufa nawe, sitakukania. Waanafunzi wote wakasema vilevile.

Isa akafika nao mahali paitwapo Gethsemane, aka- 36

waambia waanafunzi, Kaeni hapa, nikienda niabudu kule.
 37 Akatwaa Petro na waana wawili wa Zebedayo, aka-
 38 anza kuwa na huzuni na sikitiko jingi. Akawaambia,
 Roho yangu inayo huzuni nyingi hatta kufa; kaeni
 39 hapa mkakeshe nami. Akaendelea mbele kidogo aka-
 sujudu akaomba, akasema, Baba yangu, kama yamkini,
 kiniache kikombe hiki; lakini si kama nitakavyo mimi,
 40 illa kama wewe. Akawakaribia waanafunzi, akawaona
 wamelala. Akamwambia Petro, Kumbe! hamkuweza
 41 kukesha nami hatta saa moja? Kesheni kaombeni, msii-
 ngie majaribuni. Roho ndiyo mpesi, lakini mwili u thaifu.
 42 Akaenda tena marra ya pili akaomba, akasema, Baba
 yangu, kwamba si yamkini kiniache kikombe hiki nisi-
 43 pokunywa, upendalo wewe lifanyike. Akaja akawaona
 44 wamelala tena; kwani macho yao mazito. Akawaacha,
 akaenda akaomba tena marra ya tatu, akisema maneno
 45 yaleyale. Akaja tena kwa waanafunzi wake, akawaam-
 bambia, Laleni sasa hatta mwisho, mpumzike.

Saa imekaribia, na Mwana wa adamu atolewa miko-
 46 noni kwa wenyi thambi. Ondokeni, twende zetu. Ta-
 zameni, yeye amekuja anitoaye.

47 Hatta anenapo na Yuda mmoja wa wathenashara
 alikuja, na mafuatano mengi naye wenyi panga na ma-
 gongo, waliotoka kwa wakohani wakuu na wazee wa
 48 watu. Bassi yeye aliyemtoa aliwapa ishara, akisema,
 49 Nitakayembusu, ndiye huyo; mkamateni. Marra aka-
 50 mkaribia Isa akasema, Salaamu, Rabbi; akambusu. Isa
 akamwambia, Mwenzangu, umekuja kwa nini? Nao
 51 wakaja wakamtia Isa mikono wakamkamata. Na
 mmoja wao waliokuwako na Isa akanyosha mkono aka-
 futa upanga wake, akapiga mtumwa wa mkohani mkuu,
 52 akamkata sikio. Isa akamwambia, Rudisha upanga
 wako mahali pake: wo wote watwao upanga watakufa
 53 kwa upanga. Wathani mimi siwezi sasa kumwomba
 Baba yangu, naye ataniletea zayidi ya lejioni thenashara
 54 za malaika? Lakini yatatimiaje maandiko, ya kwamba
 imepasa kuwa hivyo.

55 Saa hiyo Isa akawaambia makutano, Mmetoka kama
 juu ya mnyang'anyi na panga na magongo mnitwae?
 Nalikaa kitako siku kwa siku nanyi katika hekalu niki-
 56 fundisha, wala hamkunikamata. Lakini mambo haya
 pia yalikuwa illi maandiko ya nabii yatimie.

Bassi waanafunzi wote wakamwacha wakakimbia.

Na wale waliomkamata Isa wakampeleka kwa Kayafa 57
mkohani mkuu, walikokutana waandishi na wazce.
Naye Petro akamfuata mbali, hatta ukumbini kwa 58
mkohani mkuu; akaingia ndani akakaa na watumishi,
auone mwisho.

Bassi wakohani wakuu, na wazee, na baraza wote, 59
wakatafuta ushahidi wa uwongo juu ya Isa, illi wa'mue,
wasiupate; kwamba mashahidi wa uwongo wengi wali- 60
kuja, hawakuupata. Kwa mwisho mashahidi wa uwo-
ngo wawili walikuja, wakasema, Huyu amesema, Nawe- 61
za kuliharibu hekalu la Muungu, na kulijenga kwa siku
tatu.

Akaondoka mkohani mkuu, akamwambia, Hujibu 62
neni? Mambo gani hawa wanayokushuhudia? Isa 63
akanyamaa kimya. Mkohani mkuu akajibu, akamwa-
mbia, Nakuapisha kwa Muungu aliye hayi, utwambie
kwamba ndiwe Masiya, Mwana wa Muungu. Isa aka- 64
mwambia, Umesema; lakini nawaambia, baadaye uta-
mwona Mwana wa adamu akikaa mkono wa kuume wa
uwezo, akija juu ya mawingu ya mbingu.

Naye mkohani mkuu akayararua mavazi yake, aka- 65
sema, Amenena unajisi: twatakaje tena mashahidi?
Angalieni, mmesikia sasa unajisi wake; mwaonaje? 66
Wakajibu wakasema, Astahili kufa. Nao wakatema ma- 67
te usoni mwake, wakampiga; wengine wakampiga kofi,
wakasema, Utufasirie, ewe Masiya, ni nani aliyekupiga? 68

Bassi Petro akakaa 'nje katika ukumbi; akaja kijakazi 69
kimoja akasema, Na wewe ulikuwa pamoja na Isa wa
Galilaya. Akakana mbele za wote, akisema, Silijui uli- 70
semalo. Alipotoka hatta mlangoni, kingine akamwona, 71
akawaambia watu walioko, Na huyu alikuwa pamoja na
Isa Mnazareti. Akakana tena kwa kiapo, Simjui mtu 72
yule. Baadaye kidogo, watu walioko wakisimama wa- 73
kamkaribia, wakamwambia Petro, Hakika yako wewe
mmoja wao; ulimi wako wakuonyesha. Akaanza ku- 74
laani na kuapa, Simjui huyo. Marra akawika jogoo. 75
Petro akakumbuka maneno ya Isa, alipomwambia,
Mbele ya kuwika jogoo utanikania marra tatu. Aka-
toka, akalia 'mno.

IKIWA assubui wakohani wakuu wote na wazee wa 27
watu wakafanya shauri juu ya Isa, wa'mue. Wakam- 2

funga, wakamechukua, wakamtoa kwa Pontio Pilato, aliye liwali.

- 3 Na Yuda aliyemtoa, akiona ya kwamba amehukumwiwa,
 4 akajuta, akawarudishia wakohani wakuu na wazee vipa-
 5 nde vile thelathini vya fetha, akisema, Nimekosa nilipotoa
 6 damu isiyo na hatiya. Wakasema, Imetupasaje?
 7 Angalia wewe. Akatupa fetha katika hekalu, akatoka,
 8 akaenda akajisonga.
- 9 Wakohani wakuu wakazitwaa fetha, wakasema, Ni
 10 haramu kuziweka katika hazina, kwa kuwa kima cha
 11 damu. Wakafanya shauri, wakanunua nazo uwanja
 12 wa mfinyanzi, kuzikia humo wageni. Kwa sababu hii,
 13 uwanja ule unakwitwa uwanja wa damu, hatta leo.
 14 Ndipo yalitimia yaliyonenwa na nabii Yeremiya, aki-
 15 sema, Wakatwaa vipande thelathini vya fetha, kima
 16 chake aliyetiwa kima, waliyemtia kima wale waana wa
 17 Israeli, wakavitoe kwa uwanja wa mfinyanzi, kama
 18 Bwana alivyoniagiza.
- 19 Isa akasimama mbele ya liwali. Liwali akamwuliza,
 20 akasema, Ndiwe mfalme wa Wayahudi? Isa akamwa-
 21 mbia, Umesema. Aliposhtakiwa na wakohani wakuu
 22 na wazee, hakujibu hatta neno. Pilato akamwambia,
 23 Husikii mambo mangapi wakushuhudia? Wala haku-
 24 mjibu hatta neno, hatta liwali akataajabu sana.
- 25 Bassi kwa siku kuu liwali huwafungulia watu mfungwa
 26 mmoja, wamtakaye. Siku zile palikuwa mfungwa ma-
 27 shuhuri, jina lake Barabba. Walipokuwa wamekutanika,
 28 Pilato akawaambia, Mwataka niwafungulie nani? Ba-
 29 rabba, ao Isa aitwaye Masiya? Kwani akajua ya kwamba
 30 wamemtoa kwa hasidi.
- 31 Alipokaa kitini mwa hukumu, mkewe akampelekea,
 32 akisema, Usimfanyie neno mtu yule wa haki; kwani
 33 nimeteswa leo na mambo mengi katika ndoto kwa sababu
 34 yake.
- 35 Na wakohani wakuu na wazee wakawashawishi watu
 36 wamtake Barabba, wakampoteze Isa. Liwali akajibu,
 37 akawaambia, Yupi mmtakaye niwafungulie? Wakasema
 38 Barabba. Pilato akawaambia, Nimfanyieje Isa aitwaye
 39 Masiya? Wote wakamwambia, Asulibiwe. Liwali
 40 akasema, Kwa nini? ubaya gani alioufanya? Wakapiga
 41 makelele mengi 'mno, wakasema, Asulibiwe.
- 42 Pilato alipoona hakufaa kabisa, lakini fitina yatiwa,

akatwaa maji, akanawa mikono mbele za makutano, akisema, Mimi sina hatiya kwa damu ya mtu huyu mwenyi haki; angalieni ninyi. Wakajibu watu wote 25 wakasema, Damu yake juu yetu, na juu ya watoto wetu.

Akawafungulia Barabba : akampiga Isa, akamtoa asu- 26 libiwe.

Na asikari wa liwali wakamleta Isa katika maku- 27 sanyiko ya asikari, wakamkusanyikia wote. Wakao- 28 ndoa nguo zake, wakamvika vazi jekundu; wakafanya 29 taji ya miiba, waka'mweka kitwani, na unyasi mkononi mwake mwa kuume, wakapiga magote mbele yake, wakamfanyizia mzaha, wakisema, Salaamu, Mfalme wa Wayahudi! Wakatema mate juu yake, wakautwaa 30 unyasi, wakampiga kitwa.

Walipokwisha kumfanyizia mzaha, wakaondoa vazi 31 lile, wakamvika nguo zake; wakamwongoza kumsulibisha.

Na wakitoka, wakakuta mtu wa Kurene, jina lake 32 Simán; wakamjuuru amchukulie msalaba wake.

Walipofika mahali paitwapo Golgotha, maana yake 33 mahali pa kitwa, wakampa kunywa siki iliyochanganyi- 34 ka na safura; naye alipoonja hakupenda kunywa.

Wakamsulibisha; wakagawanya nguo zake, wakapiga 35 kura, illi yatimie yaliyonenwa na nabii, Walizigawanya nguo zangu wakapiga kura juu ya vazi langu. Waka- 36 kaa kitako, wakamngojea. Wakaweka juu ya kitwa 37 chake mshtaka wake, ulioandikwa,

HUYU NI ISA, MFALME WA WAYAHUDI.

Na wanyang'anyi wawili wakasulibiwa pamoja naye, 38 mmoja mkono wa kulia, na mmoja mkono wa kushoto.

Wale waliopita wakamshutumu, wakisukasuka vitwa, 39 wakisema, Ewe uliharibuye hekalu, ulijengaye kwa siku 40 tatu, ujiponye mwenyewe; kama ndiwe Mwana wa Muungu, ushuke msalabani. Vivyo na wakohani wakuu 41 wakamfanyizia mzaha pamoja na waandishi na wazee, wakasema, Aliponya watu, hawezi kujiponya mwenyewe. 42 Kana ndiye mfalme wa Israeli, ashuke sasa msalabani, naswi tutamsadiki. Alimwamini Muungu; amponye sasa, 43 kama amkubali: kwani akasema, Mimi ni Mwana wa Muungu. Wanyang'anyi tena waliosulibiwa naye wa- 44 kamshutumu vilevile

45 Bassi tangu saa a sita ilikuwa giza juu ya inchi pia
 46 hatta saa a tissia. Na kama saa a tissia, Isa akalia kwa
 sauti kuu, akisema, Eli, Eli, lama sabakhthani? maana
 yake, Muungu wangu, Muungu wangu, mbona umenia-
 47 cha? Watu walioko wakisimama, wakisikia, wakasema,
 48 Huyu amwita Eliya. Na marra mtu mmoja akaenda
 mbio, akatwaa sifongo akaijaza na siki, akaitia mwanzia-
 49 ni, akamnyweshwa. Wangine wakasema, Wache; tua-
 ngalie kama Eliya atakuja amponye.

50 Isa alipolia tena kwa sauti kuu, akatoa roho.

51 Na pazia la hekalu likararuka toka juu hatta chini;
 52 inchi ikatetema, miamba ikapasuka; makaburi yakafu-
 nuka, miili mingi ya watakatifu waliolala wakaondoka,
 53 wakatoka makaburini, baada ya ufufuo wake, wakaingia
 mjini mtakatifu, wakaonekana na wengi.

54 Bassi amiri na wale walio naye wakimngojea Isa,
 walipoona tetemeko na mambo yaliyofanyika, wakao-
 gopa sana, wakasema, Hakika huyu Mwana wa Muungu.

55 Palikuwako na waanawake wengi wakiangalia mbali.
 Ndio waliomfuata Isa, toka Galilaya, wakamngojea.
 56 Katika wale palikuwa na Maryamu Magdalene, na Mar-
 yamu mama yao Yakób na Yose, na mama yao waana
 wa Zebedayo.

57 Ilipopata jioni, akaja mtu mkwasi wa Arimathaya,
 jina lake Yusuf, naye mwenyewe mwanafunzi wa Isa;
 58 akaenda kwa Pilato akataka mwili wa Isa. Pilato akaa-
 59 muru mwili utolewe. Yusuf alipoutwaa mwili akaukunja
 60 katika saanda nyeupe, akauweka katika kaburi lake yeye
 jipya, alilofukua katika mwamba; akafingirisha jiwe ku-
 61 bwa mlangoni kwa kaburi, akaenda zake. Walikuwako
 na Maryamu Magdalene, na Maryamu yule wa pili, wa-
 kika mbele ya kaburi.

62 Siku ya pili, iliyo baada ya Uandao, wakohani wakuu
 63 na Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato, wakasema,
 Bwana, twakumbuka yule ayari alisema akiwa hayi,
 64 Baada ya siku tatu nitafufuka. Bassi uamuru kulilinda
 kaburi hatta siku ya tatu; wasije waanafunzi wake usiku
 wamwibe, wakawaambie watu, Amefufuka katika wafu;
 65 na kosa la mwisho litapita lile la kwanza. Pilato aka-
 waambia, Mnao asikari: enendeni mlilinde 'mwezavyo.
 66 Wakaenda wakalilinda kaburi, wakalitia jiwe muhuri,
 wakaweka walinzi.

JUMA a mosi ilipokwisha, ikacha juma a pili, wali- **28**
kuja Maryamu Magdalene, na Maryamu wa pili, kulita-
zama kaburi.

Likawa tetemeko kubwa ; kwani malaika wa Bwana **2**
alishuka mbinguni, akaja akafingirisha jiwe katika mla- **3**
ngo, akakaa juu yake. Alikuwa akionekana kama **3**
umeme, na mavazi yake meupe 'mno kama thuluji.
Walinzi wakatetemeka kwa kumwogopa, wakawa kama **4**
wafu.

Malaika akajibu, akawaambia waanawake, Msiogope **5**
ninyi ; nawajua mwamtafuta Isa aliyesulibiwa. Hapo ; **6**
kwani amefufuka, alivyosema. Njoooni, tazameni maha-
li alipolazwa Bwana. Endeni upesi, 'mwaambie waana- **7**
funzi wake, amefufuka katika wafu ; naye awatangulia
kwenda Galilaya ; ndiko mtamwona : angalieni, nime-
waambia.

Wakatoka kwa haraka kaburini wenyi kicho na furaha **8**
kuu, wakaenda mbio wawahubirie waanafunzi wake.
Hatta walipokuwa wakienda wawahubirie waanafunzi **9**
wake, Isa akaja akawaambia, Salaamu ! Wakaja waka-
mshika miguu, wakamsujudia. Isa akawaambia, Msio- **10**
gope : enendeni mkawaambie ndugu zangu waende Ga-
lilaya ; ndiko watakakoniona.

Wale walipokuwa wakienda, walinzi wakaingia mjini **11**
wakawaarifu wakohani wakuu mambo yote yaliyotende-
ka. Wakakusanyika pamoja na wazee, wakafanya shauri, **12**
wakawapa asikari fetha zitoshazo, wakawaambia, Se- **13**
meni, Waanafunzi wake walikuja usiku wakamwiba
tulipokuwa sisi katika kulala ; na liwali angepata kuya- **14**
sikia haya, tutamshawishi yeye na tutawahifathi ninyi.
Wakatwaa fetha wakafanya kama walivyofundishwa ; **15**
yakaenea maneno haya katika Wayahudi hatta leo.

Nao waanafunzi edashara wakaenda Galilaya, hatta **16**
mlima aliowaagiza Isa. Wakamwona, wakamsujudia ; **17**
wangine wakaona shaka. Isa akaja akasema nao, aka- **18**
waambia, Nimepewa nguvu zote katika mbingu na inchi ;
bassi enendeni, wafundisheni mataifa yote, 'mwabatize **19**
kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu,
'mwafundishe washike yote niliyowaamuru : nami nipo **20**
pamoja nanyi sikuzote, hatta mwisho wa dunia. Amina.

ANJILI KWA MARKO.

- 1 MWANZO wa anjili ya Isa Masiya, Mwana wa
 2 Muungu; kama ilivyoandikwa katika nabii, Angalia,
 3 mimi natuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, ataka-
 4 yetengeneza njia yako mbele yako. Sauti yake aliaye
 katika jangwa, Tengenezeni njia ya Bwana, ukanyoshe
 mapito yake.
- 4 Akawa Yohana akibatiza katika jangwa, na akihu-
 5 biri ubatizo wa toba kwa ondoleo la thambi. Waka-
 mtokea inchi yote ya Uyahudi, na Wayerusalemi, waka-
 batizwa wote naye katika mto Yardeni, wakiungama
 thambi zao.
- 6 Naye Yohana amevaa singa za ngamia, na mshipi wa
 ngozi kiunoni mwake, akila nzige na asali ya mwituni.
- 7 Akahubiri, akinena, Yuaja aliye hodari kuliko mimi nyu-
 ma yangu, wala mimi sistahili niiname kufungua kanda
 8 za viatu vyake. Mimi nawabatiza kwa maji; huyu ata-
 wabatiza kwa Roho Mtakatifu.
- 9 Ikawa siku zile, akaja Isa katika Nazareti ya Galilaya,
 10 akabatizwa na Yohana katika Yardeni. Marra akipanda
 katika maji, akaona mbingu zimefunuka, na Roho
 11 kama hua akashuka juu yake; sauti ikawa katika mbi-
 nguni, Ndiwe Mwana wangu aliyependwa, niliyepende-
 zwa naye.
- ¹²
¹³ Marra Roho akamfukuza hatta jangwani. Akawa
 katika jangwa siku arobaini, akijaribiwa na Shetani;
 akawako pamoja na nyama; malaika wakamngojea.
- 14 Hatta baada ya kutiwa gerezani Yohana, akaja Isa ka-
 tika Galilaya, akihubiri anjili ya ufalme wa Muungu,
 51 na akinena, ya kwamba, Wakati umetimia, umekaribia
 ufalme wa Muungu: tubuni, mkaamini anjili.
- 61 Akitembea kando la bahari ya Galilaya, akaona Siman
 na Andrea nduguye, wakitupa jarifa baharini: kwani
 17 walikuwa wavuvi. Akawaambia Isa, Haya, nyuma
 18 yangu, nami nitawafanya wavuvi wa watu. Marra wa-
 kaacha nyavu zao, wakamfuata.

Akiendelea mbele huko kidogo, akaona Yakobo wa 19
Zebedayo na Yohana ndugu yake, nao hawa katika
chombo wakizitengeneza nyavu. Marra akawaita; wa- 20
kamwacha baba yao Zebedayo katika chombo pamoja nao
walio kwa mshahara, wakaenda zao nyuma yake.

Wakaingia katika Kapernaum; na marra siku ya saba- 21
to akaingia katika sunagogi, akafundisha. Wakashangaa 22
kwa elimu yake; kwani alikuwa akifundisha kama mwen-
nyi uwezo, wala si kama waandishi. Palikuwako katika 23
sunagogi yao mtu mwenyi pepo mchafu; akalia, akinena, 24
Ah! tuna nini nawe, Isa Mnazareti? umekuja utupo-
teze? Nimekujua nani, Mtakatifu wa Muungu. Aka- 25
mkemea Isa, akinena, Nyamaza, ukatoke kwake. Pepo 26
mchafu akamrarua, akalia kwa sauti kuu, akatoka kwa-
ke. Wakataajabu wote, hatta kuulizana, wakinena, 27
Nini hii? Elimu gani hii mpya? Ya kuwa kwa uwezo
awaagiza nao pepo wachafu, nao wamtii! Habari yake 28
ikatoka marra moja katika inchi yote iliyozunguka ya
Galilaya.

Nao wakitoka katika sunagogi wakaenda marra katika 29
nyumba ya Siman na Andrea, pamoja na Yakobo na
Yohana. Mkwewe Siman akalazwa akishikwa na ho- 30
ma; marra wakamwambia mambo yake. Akija kwake 31
akamwinua, akimshika mkono; homa ikamwacha marra,
akawangojea.

Ikiwa jioni, lilipokuchwa jua, wakamletea wote wa- 32
liokuwa hawawezi, nao wenyi pepo; mji wote ukakusa- 33
nyika mlangoni. Akawaponya wengi waliokuwa hawa- 34
wezi kwa ugonjwa mwingine mwingine, akafukuza
pepo wengi, wala hakuacha pepo wanene, ya kuwa
wamemjua.

Hatta mapema sana usiku akiondoka, akatoka akaenda 35
mahali pasipo watu, huko akaomba. Wakamfuata Siman 36
nao walio naye; hatta wakimwona wakamwambia, ya 37
kwamba Wote wakutafuta wewe. Akawaambia, Twende 38
kwa vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri na huko; kwani
kwa hiyo nimetoka. Akawa akihubiri katika masuna- 39
gogi yao katika Galilaya pia, na akizifukuza pepo.

Akaja kwake mwenyi ukoma, akimsihi na kumpigia 40
magote, na kumwambia ya kwamba Ukipenda waweza
kunisafisha. Isa akimhurumia, akanyosha mkono, aka- 41
mgusa, akamwambia, Napenda: usafike. Hatta akinena, 42

- 43 marra ukoma ukamwacha akasafika. Marra akimwogofya,
 44 akamfukuza, akamwambia, Angalie, usimwambie mtu
 neno; illa nenda zako, ujionyeshe kwa mkohani, ukatoe
 kwa kusafishwa kwako alivyoamuru Musa kwa ushahidi
 45 kwao. Naye akitoka akaanza kuhubiri mengi na kueneza
 neno, hatta hakuweza tena kuingia mjini kwa wazi, illa
 alikuwa 'nje mahali pasipo watu; wakamjia kutoka pote.
- 2** AKAINGIA tena katika Kapernaum baada ya siku,
 2 ikasikiwa ya kwamba alikuwamo nyumbani. Marra
 wakakusanyika wengi, hatta hapana tena nafasi wala
 3 mbele ya mlango: akawaambia neno. Wakaja kwake,
 waliomleta mwenyi kupooza, akichukuliwa na wanne,
 4 wala hawakuweza kumkaribia kwa makutano. Wakafunua
 dari alipokuwako, wakatoboa, wakashusha kitanda
 5 alichokilalia mwenyi kupooza. Isa akiona imani yao
 akamwambia mwenyi kupooza, Mwanangu, thambi zako
 6 zimeondolewa. Walikuwako huko waandishi wamekaa
 7 kitako, wakifikiri moyoni mwao, Mbona huyu anena
 hivi unajisi? Nani awezaye kuondoa thambi, illa mmoja,
 8 ndiye Muungu? Marra Isa akijua rohoni mwake ya
 kwamba hawa wanafikiri hivi ndani yao, akawaambia,
 9 Mbona mwafikiri haya moyoni mwenu? Ipi nyepesi,
 kumwambia mwenyi kupooza, Thambi zako zimeondolewa,
 ao kunena, Ondoke, tweke kitanda chako, ukaende?
 10 Mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anao uwezo
 juu ya inchi kuondoa thambi, (amwambia mwenyi ku-
 11 pooza), nakwambia, Ondoke, tweke kitanda chako,
 12 ukaende zako nyumbani kwako. Akaondoka marra,
 akatweka kitanda chake, akatoka mbele yao wote, hatta
 wakataajabu wote, wakamtukuza Muungu, wakinena,
 ya kwamba Hatukuona kama hivi kabisa.
- 13 Akatoka tena kando la bahari; makutano yote wakaja
 kwake, akawafundisha.
- 14 Hatta akapita akamwona Lawi wa Alfayo, amekaa
 kitako forthani, akamwambia, Nifuate. Akasimama
 15 akamfuata. Ikawa katika kukaa mezani nyumbani
 mwake, mapublikano wengi na wenyi thambi walikuwa
 wamekaa pamoja na Isa na waanafunzi wake: kwani
 16 walikuwa wengi, wakamfuata. Nao waandishi na Mafarisayo
 wakimwona akila pamoja nao mapublikano na wenyi thambi,
 wakawaambia waanafunzi wake, Nini hii? anakula na kunywa
 pamoja na mapublikano na wenyi

thambi. Hatta akisikia Isa, akawaambia, Wenyi nguvu 17
hawahitajii mtabibu, illa walio hawawezi: sikuja kuwaita
wenyi haki illa wenyi thambi kwa toba.

Wakawa waanafunzi wa Yohana na ya Mafarisayo 18
wakifunga: wakaja wakamwambia, Kwa nini waanafunzi
wa Yohana nao wa Mafarisayo wafunga, illa waanafunzi
wako hawafungi? Akawaambia Isa, Hawawezi waana 19
wa arusi, bwana arusi akiwapo nao, kufunga. Wakati
ule wakiwa naye bwana arusi kwao, hawawezi kufunga.
Siku zitakuja, bwana arusi atakapoondolewa kwao, ndipo 20
watakapofunga siku zile. Hakuna mtu ashonaye kira- 21
ka cha nguo mpya juu ya vazi kukuu, illa, kipya kili-
chojaliza chaondoa katika lile kukuu, nalo lazidi kuta-
tuka. Wala hakuna mtu atiyaye mvinyo mpya katika 22
kiriba kukuu, illa, mvinyo ulio mpya hupasua kiriba,
mvinyo humwagika na kiriba zimepotea. Lakini mvinyo
mpya kutiwa katika kiriba mpya.

Ikawa akipita siku ya sabato katika makoonde, wa- 23
kaanza waanafunzi wake wakienda kuyafikicha masuke.
Mafarisayo wakamwambia, Angalia, mbona wafanya 24
isiyo halali siku ya sabato? Akawaambia, Hamkusoma 25
alivyofanya Daud, alipohitaji, akaona njaa yeye nao wa-
lio pamoja naye? kama alivyoingia katika nyumba ya 26
Muungu, akiwa Abiathar mkohani mkuu, wakala mikate
ya wonyesho, isiyo halali kula, illa kwa wakohani,
akawapa waliokuwa pamoja naye? Akawaambia, Saba- 27
to imekuwa kwa ajili ya mtu, wala si mtu kwa ajili ya sa-
bato. Hatta Mwana wa Adamu ni Bwana hatta ya sabato. 28

AKAINGIA tena katika sunagogi; palikuwako huko **3**
mtu mkono wake umepooza: wakamwangalia, kama siku 2
ya sabato atamponya, wapate kumshtaki. Akamwambia 3
mtu mwenyi mkono uliopooza, Simama katikati. Aka- 4
wambia, Ni halali siku za sabato kutenda vema ao ku-
tenda vibaya? Kuponya maisha, ao kuua? Wakanya-
maza. Naye akiwatazama kwa hasira, akikasirika kwa 5
kuwa mgumu moyo wao, akamwambia mtu, Nyosha
mkono wako. Akanyosha: mkono wake ukaponyeka,
mzima kama wa pili. Wakitoka marra Mafarisayo wa- 6
kafanya shauri na Maherodiani juu yake, wampotezeje.

Isa akaenda zake pamoja na waanafunzi wake hatta 7
bahari. Watu wengi sana wa katika Galilaya waka-
mfuata: na katika Uyahudi, na katika Yerusalemi, na 8

katika Idumayo, na ng'ambo ya pili ya Yardeni, nao walio karibu na Turo na Sidon, wengi sana, wakisikia 9 alivyovifanya, wakamjia. Akawaambia waanafunzi wake chombo kidogo kikae karibu yake, kwa makutano wasi- 10 msumbue. Kwani akawaponya wengi, hatta wakamwa- 11 ngukia, wapate kumgusa waliokuwa na mapigo. Na pepo wachafu, walipomwona wakaanguka mbele yake, wakalia, wakinena, ya kwamba, Ndiwe uliye Mwana wa 12 Muungu. Akawakemea sana, wasimthihirishe.

13 Apanda katika mlima, awaita aliowapenda; wakaja 14 kwake. Akafanya thenashara, wapate kuwa pamoja 15 naye, naye apate kuwatuma kuhubiri, na kuwa na nguvu 16 za kuponya ugonjwa, na kufukuza pepo. Na Siman 17 akampa jina Petro; na Yakobo wa Zebedayo, na Yohana ndugu wa Yakobo, akawapa majina Boanerge, ndio waa- 18 na wa ngurumo; na Andrea, na Filipo, na Bartolomayo, na Mattayo, na Thoma, na Yakobo wa Alfayo, na Thadda- 19 yo, na Siman Mkananayo, na Yuda Iskariota aliyemtoa.

20 Wakaja nyumbani. Makutano yakakusanyika tena, 21 hatta hawawezi hatta kula chakula. Nao wa kwake wakisikia, wakaja kumshurutisha, kwani wakasema ya kwamba akili zake zimepotea.

22 Nao waandishi walioshuka katika Yerusalemi wakena, ya kwamba anaye Beelzebul, na ya kuwa kwa 23 mkuu wa pepo awafukuza pepo. Naye akiwaitia akawaambia kwa mifano, Awezaje Shetani kumfukuza Shetani? Na kama ufalme umetengwa juu yake wenyewe 24 hauwezi kusimama ufalme ule. Na kama nyumba imetengwa juu yake yenyewe haiwezi kusimama nyumba 25 hii. Na Shetani akiondoka juu ya mwenyewe, akate- 26 ngwa, hawezi kusimama, lakini mwisho anao. Hawezi mtu akiingia nyumbani mwa mtu hodari, kuteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza aliye hodari, ndipo atakapo- 27 teka nyumba yake. Amin nawaambia, ya kwamba, wataachiliwa waana Adamu mathambi yote, na ma- 28 najisi watakayoyanena, illa yeye atakayemnena unajisi Roho Mtakatifu, hana kuachiliwa hatta milele, lakini 29 imempasa hukumu ya milele: ya kuwa walinena, Pepo mchafu anayo.

31 Wakaja ndugu zake na mama wake, nao wakisimama 32 'nje wakatuma kwake wakimwita. Makutano wakakaa wakimzunguka, wakamwambia, Mama wako na ndugu

zako 'nje wakutafuta. Akawajibu, akinena, Nani aliye 33
 mama wangu ao ndugu zangu? Akiwatazama pande zote 34
 walipokaa waliomzunguka, akanena, Angalieni, mama
 wangu na ndugu zangu. Kwani mtu atakayefanya ali- 35
 pendalo Muungu, huyu ni ndugu yangu, na umbu langu,
 na mama wangu.

AKAANZA tena kufundisha kando la bahari; waka- 4
 kusanyika kwake makutano mengi, hatta mwenyewe
 akipanda chomboni akakaa katika bahari, na makutano
 yote wako kando la bahari, juu ya inchi.

Akawafundisha mengi kwa mifano, akawaambia ka- 2
 tika elimu yake, Sikieni: Mpanda mbegu alitoka apande: 3
 ikawa katika kupanda, hiyo ikaanguka juu ya njia, zikaja 4
 ndege za anga zikaila. Nginge ikaanguka panapo mawe, 5
 isipokuwa na udongo mwingi; marra ikachupuka, kwa
 sababu udongo wake hauendi chini; hatta jua likipanda 6
 ikaungua, na kwa sababu haina shina ikakauka. Nginge 7
 ikaanguka panapo miiba; miiba ikakua, ikaisonga, wala
 haikutoa matunda. Nginge ikaanguka juu ya udongo 8
 mwema, ikatoa matunda yakimea na yakikua, ikaleta
 moja thelathini, na moja sitini, na moja mia. Aka- 9
 nena, Aliye na masikio ya kusikia asikie.

Alipokuwa pasipo watu, waliomzunguka na wathena- 10
 shara wakamulizia mfano. Akawaambia, Mmepewa 11
 ninyi kujua siri ya ufalme wa Muungu; wale walio 'nje
 yote yamewawia kwa mifano: illi wakitazama wata- 12
 zame, wala wasione, na wakisikia wasikie, wala wasifahamu,
 wasigeuke po pote, wakaondolewe thambi. Aka- 13
 waambia, Hamkujua mfano huu? mtajuaje mifano yote?

Apandaye alipanda neno. Wale walio njiani, nenc 14
 lipandwapo; nao waliposikia, marra huja Shetani, hilitwaa 15
 neno lililopandwa katika mioyo yao. Na hawa ni kama 16
 wao waliopandwa juu ya mawe, ndio waliposikia neno
 marra walipokea kwa furaha, wala hawana shina kwao, 17
 lakini ni kwa wakati; hatta ikiwa shidda ao ufukuzo
 kwa ajili ya neno, marra wamechukizwa. Nao wangine 18
 ni wao waliopandwa katika miiba; ndio walisikia neno,
 na tunza za ulimwengu huu, na udanganifu wa mali, 19
 na tamaa kwazo zilizosalia, zikiingia zalisonga neno,
 nalo limekuwa halizai. Nao ndio waliopandwa katika 20
 udongo mwema; walisikia neno, nao walikubali, na wa-
 zaa, moja thelathini, na moja sitini, na moja mia.

21 Akawaambia, Taa haiji, itiwe chini ya kikapo, ao chini
22 ya kitanda? siyo itiwe katika mwango? Kwani hapa-
na iliyostirika, isiyoonekana, wala iliyokuwa imefichwa,
23 illa ipate kuwa wazi. Mtu akiwa na masikio ya kusikia,
asikie.

24 Akawaambia, Angalieni msikieni. Kwa kipimo mpi-
mavyo, mtapimiwa ninyi, na itazidishwa kwenu mnaosi-
25 kia. Kwani mtu aliye nayo, atapewa; naye asiye nayo,
hatta aliyo nayo atatwaliwa.

26 Akanena, Hivi ni ufalme wa Muungu, kama mtu aki-
27 tupa mbegu katika inchi, akilala na kuondoka usiku na
mchana, na mbegu ikichupuka ikakua, kama asivyojua
28 huyu: kwani inchi kwa yenyewe huzaa, kwanza jani, tena
29 suke, tena ngano pevu katika suke. Itoapo tunda marra
atuma mundu, ya kuwa mavuno yako.

30 Akanena, Nifananishe na nini ufalme wa Muungu?
31 ao kwa mfano gani niufanyie mfano? Kama chembe ya
kharadali, ikipandwa juu ya inchi, ndiyo ndogo kuliko
32 mbegu zote zilizoko juu ya inchi, nayo ilipopandwa,
hukua, hatta imekuwa kubwa kuliko majani yote, na
kufanya matawi makubwa, hatta waweza ndege za anga
kukaa chini ya kivuli chake.

33 Kwa mifano mingi kama hii akawaambia neno, kama
34 walivyoweza kusikia: pasipo mfano hakusema nao. Kwa
faragha akawafasiria waanafunzi wake yote.

35 Naye awaambia siku ile ikiwa jioni, Tuvuke hatta
36 ng'ambo ya pili. Nao wakiagana na makutano, waka-
mchukua kama alivyokuwa katika chombo; na vyombo
37 vingine vidogo viko naye. Ikawa tharuba kuu ya upepo,
mawimbi yakatupwa juu ya chombo, hatta kimekwanza
38 kujaa. Naye alikuwa katika shetri akilala juu ya mto.
Nao wama'msha, wakimwambia, Mwalimu, huangalii
39 wewe ya kwamba tumepotea? Naye akiondoka akau-
kemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaze; uzuliwe.
40 Upepo ukakoma, ikawa shwari kuu. Akawaambia,
41 Mbona mwaoga hivi? Kwaje hamnayo imani? Wakao-
gopa hofu nyingi, wakaambiana, Huyu ni nani bassi, ya
kwamba na upepo na bahari zamtii?

5 WAKAFIKA ng'ambo ya pili ya bahari, katika inchi
2 ya Wagadareni. Akishuka katika chomboni, marra
akamkuta mtu katika makaburi mwenyi pepo mchafu,
3 aliyekuwa na makao katika makaburi: wala hakuna mtu

awezaye kumfunga, hatta kwa minyororo. Kwani ame- 4
 fungwa marra nyingi kwa pingu na minyororo, na minyo-
 roro imekatwa naye, na pingu zimepasuliwa naye: wala
 hawezi mtu kumtuliza. Naye sikuzote usiku na mchana 5
 katika milima na katika makaburi, akilia na akijikata
 kwa mawe. Alipomwona Isa mbali akapiga mbio aka- 6
 msujudia, akalia kwa sauti kuu akinena, Ni nani nawe, 7
 Isa Mwana wa Muungu aliye juu? Nakuapiza kwa
 Muungu, usiniumize. Kwani amemwambia, Pepo mcha- 8
 fu, utoke katika mtu. Akamwuliza, Jina lako nani? 9
 Akajibu akamwambia, Lejioni jina langu, ya kuwa sisi
 wengi. Akamsihi sana, asiwapeleke mbali 'nje ya inchi. 10
 Palikuwako katika mlima kundi la nguruwe kubwa liki- 11
 lishwa: wakamsihi pepo wote wakinena, Utupeleke sisi 12
 kwa nguruwe, tupate kuwaingia wale. Marra Isa aka- 13
 wakubalia. Hatta pepo wachafu wakitoka wakaingia
 katika nguruwe; kundi likaenda kassi katika palipocho-
 ngoka hatta baharini, wakawa kama elfeen, wakatoswa
 baharini. Nao waliolisha nguruwe wakakimbia, wakae- 14
 neza habari katika mji na katika mashamba. Wakaja
 waone nini iliyokuwa. Wakifika kwa Isa, na kumwona 15
 aliye na pepo ameketi amevaa na mwenyi akili, aliye-
 kuwa nao Lejioni, wakaogopa. Nao walioona wakafa- 16
 siria ginsi ilivyo'mwia aliye na pepo, na mambo ya ngu-
 ruwe. Wakaanza kumsihi atoke katika mipaka yao. 17
 Naye akiingia chomboni, aliyekuwa na pepo akamsihi 18
 awe pamoja naye; wala Isa hakumwacha, lakini amwa- 19
 mbia, Enda zako nyumbani mwako kwa watu wako,
 ukawape habari Bwana alivyokufanyia, akakuhurumia.
 Akaenda zake akaanza kuhubiri katika Dekapoli, ali- 20
 vyomfanyia Isa: wote wakataajabu.

Akiisha kuvuka Isa tena katika chombo hatta ng'a- 21
 mbo, wakakusanyika makutano mengi hatta kwake; naye
 alikuwako kando la bahari.

Akaja kwake mmoja wa wakuu wa sunagogi, jina 22
 lake Yairo; hatta akimwona, akaanguka miguuni pake,
 akamsihi sana, akinena ya kwamba Binti yangu mdogo 23
 ni katika mwisho wake: illa uje ukamtie mikono apate
 kuokoka, naye ataishi. Akaenda naye; wakamfuata 24
 makutano mengi, wakamsongasonga.

Na mwanamke aliye na kutoka damu miaka thena- 25
 shara, aliyefanyika mengi na watabibu wengi, akagha- 26

rimia alizo nazo zote, wala hakufaliwa, illa afathali maba-
 27 ya yamezidi, amesikia mambo ya Isa, akija nyuma yake
 28 katika makutano akagusa vazi lake : kwani alinena, ya
 29 kuwa, Hatta mavazi yake nikiyagusa, nitaokoka. Marra
 likakauka chemko la damu yake, akajua mwilini ya kuwa
 30 amepona katika pigo. Marra Isa akijua ndani yake
 nguvu iliyotoka kwake, akigeuka katika makutano, aka-
 31 nena, Nani aliyegusa mavazi yangu? Wakamwambia
 waanafunzi wake, Waona makutano wakikusonga, nawe
 32 wasema, Nani aliyenigusa? Akatazama kumwona ali-
 33 yelifanya hili. Mwanamke akiingiwa na hofu, na aki-
 tetemeka, akijua lililokuwa ndani yake, akaja akamwa-
 34 ngukia, akamwambia yaliyo kweli yote. Akamwambia,
 Binti, imani yako imekuokoa ; enda zako katika amani,
 ukawe mzima katika pigo lako.

35 Hatta akiwa katika kunena, waja katika kwa mkuu
 wa sunagogi, wakinena, ya kwamba, Binti yako ame-
 36 kufa : mbona wamsumbua tena mwalimu? Marra Isa
 akisikia neno lililonenwa, amwambia mkuu wa suna-
 37 gogi, Usiogope ; amini tu. Wala hakuacha mtu afua-
 tane naye, illa Petro, na Yakobo, na Yohana ndugu yake
 38 Yakobo. Waja katika nyumba yake mkuu wa sunagogi ;
 akaangalia uthia, nao waliao na wafanyao maombolezo
 39 mengi. Akiingia awaambia, Mbona mwafanya uthia
 40 na kulia? Mtoto hakufa illa amelala. Wakamchekelea.
 Naye akiwatoa wote, atwaa naye baba wa mtoto na
 mama, nao walio pamoja naye, na aingia alipolazwa
 41 mtoto. Akishika mkono wa mtoto amwambia, Talitha
 kumi ; ndilo, likifasirika, Kijana, nakwambia, Ondoke.
 42 Marra akasimama kijana akatembea ; kwani alikuwa na
 43 miaka thenashara : wakashangaa shangao jingi. Aka-
 waagiza sana mtu asilijue hili ; akasema apewe kula.

6 AKATOKA huko, akaja katika inchi yake yeye ; wa-
 2 kamfuata waanafunzi wake. Hatta ikiwa sabato, akaa-
 nza kufundisha katika sunagogi : wengi wakisikia, wa-
 katoshewa, wakinena, Huyu amepata wapi haya?
 Hekima gani hii aliyopewa, na nguvu gani hizi zilizo
 3 kwa mikono yake? Si huyu aliye sermala, mwana wa
 Maryamu, na ndugu wa Yakobo, na Yose, na Yuda, na
 Siman? na maumbu yake sio hapa kwetu? Wakachu-
 4 kizwa naye. Akawaambia Isa, ya kwamba, Nabii ha-
 kosi heshima, illa katika inchi yake na kwa jamaa zake,

na katika nyumba yake. Wala hakuweza huko kufanya 5
nguvu, illa amewatia mikono wagonjwa wasio wengi,
akawaponya. Akataajabu kwa kutoa kuamini kwao. 6
Akazunguka katika vijiji pande zote akifundisha.

Akawaita wathenashara, akaanza kuwatuma wawili 7
wawili, akawapa uwezo juu ya pepo wachafu. Akawaa- 8
muru wasitweke kitu cha njiani, illa gongo tu; si mkoba,
si mkate, si pesa katika mshipi; lakini wajifungie 9
viatu: wasivae kanzu mbili. Akawaambia, Mtakapoi- 10
ngia katika nyumba, mkae humo hatta mtakapokwenda
zenu huko. Nao wasiowakubali wala wasiowasikia, 11
mkitoka huko, mtikisie mbali mavumbi yaliyopo miguu-
ni mwenu, kwa ushahidi kwao. Amin nawaambia, ita-
kuwa kuchukuliana kwa Sodoma na Gomorra, siku ya
hukumu, kuliko kwa mji ule.

Wakatoka wakahubiri watubu; wakafukuza pepo nyi- 12
ngi; wakapaka kwa mafuta wengi walio wagonjwa, waka- 13
ponya.

Akasikia mfalme Herode; kwani jina lake limekuwa 14
thahiri: akanena ya kwamba Yohana 'mbatizaji amefu-
fuka katika wafu, na kwa hiyo nguvu zatendeka kwake.
Wangine wakanena ya kwamba Ni Eliya. Wangine 15
wakanena ya kwamba Ni nabii, kama mmoja wa nabii.
Akisikia Herode akanena ya kwamba Niliyemkata kitwa, 16
Yohana, ndiye; yule amefufuka katika wafu.

Kwani Herode mwenyewe ametuma akamkamata 17
Yohana, akamfunga gerezani, kwa ajili ya Herodia
mkewe Filipo ndugu yake, ya kuwa amemwoa. Kwani 18
Yohana amemwambia Herode ya kwamba Si halali kwa-
ko kuwa na mke wa ndugu yako. Kwa sababu hii 19
Herodia akamchukia akataka kumua, asiweze; kwani 20
Herode alikuwa akimwogopa Yohana, akimjua mtu wa
haki na mtakatifu, akamwangalia. Akimsikia akafanya
vingi, akamsikia kwa furaha. Hatta ikiwa siku ya ku- 21
faa, Herode alipofanya karamu, siku ya kuzaliwa kwake,
kwa wakuu, na majemadari, na watu wa kwanza wa
Galilaya, akiingia binti Herodia, akacheza, akampendeza 22
Herode nao waliokaa naye; mfalme akamwambia kijana,
Utake kwangu ulipendalo, nami nitakupa. Akamwapia, 23
ya kwamba, Ulitakalo kwangu, nitakupa, hatta nusu ya
ufalme wangu. Yeye akitoka akamwambia mama wake, 24
Nitake nini? Akamwambia, Kitwa cha Yohana 'mbati-

- 25 zaji. Akiingia marra hima kwa mfalme akataka, akine-
na, Nataka unipe halafu katika kombe kitwa cha Yohana
- 26 'mbatizaji. Mfalme akiwa na huzuni nyingi, kwa ajili
ya kiapo na wao waliokaa naye hakutaka kumnyima.
- 27 Marra mfalme akamtuma asikari, akaamuru kitwa chake
28 kiletwe. Naye akaenda akamkata kitwa gerezani, aka-
leta kitwa chake katika kombe, akampa kijana; kijana
29 akampa mama wake. Waanafunzi wake wakasikia,
wakaja wakachukua mzoga wake, wakauweka kaburini.
- 30 Mitume wakakusanyika kwa Isa, wakampa habari za
31 mambo yote waliyoyafanya na waliyoyafundisha. Aka-
waambia, Njooi ninyi peke yenu kwa faragha, maha-
li pasipo watu, mkapumzike kidogo: kwani walikuwako
wajao na waendao wengi wala hakuna nafasi hatta ya kula.
- 32 Wakaenda zao mahali pasipo watu kwa faragha kwa
33 chombo. Makutano wakawaona wakienda zao, waka-
mtambua wengi; wakapiga mbio huko kwa miguu katika
34 miji yote, wakawatangulia wakaja pamoja kwake. Hatta
akishuka akaona makutano mengi; akawahurumia, ya
kwamba walikuwa kama kondoo wasio na mhunga.
Akaanza kuwafundisha mengi.
- 35 Hatta sasa saa zikizidi waanafunzi wake wakimjia
wakanena ya kwamba Mahali hapa pasipo watu, na
36 sasa saa zimezidi: uagane nao, wapate, wakienda masha-
mba kote kote na vijiji, kujinunulia chakula; kwani
37 hawanacho chakula. Akijibu akawaambia, Wapeni
ninyi kula. Wakamwambia, Tuende tununue chakula
38 cha dinari miteen, tukawape kula? Akawaambia, Mi-
kate mingapi mnayo? Nendeni katazameni. Wakijua
39 wakanena, Mitanu, na samaki mbili Akawaamuru wa-
kae kitako wote, kikao kwa kikao, juu ya majani ma-
40 bichi. Wakaketi safu kwa safu, kwa mia, na kwa
41 hamsini. Naye akiitwaa mikate mitanu na samaki mbili,
akatazama juu mbinguni, akabarikia, akaivunja mikate,
akawapa waanafunzi wake, wapate kuwaletea wale, nazo
42 samaki mbili akagawanya kwa wote. Wakala wote wa-
43 kashiba. Wakaokota makombo ya kujaliza vikapu the-
44 nashara, na katika samaki. Wakawa walioila mikate
elfu tanu waume.
- 45 Marra akawashurutisha waanafunzi wake waingie
chomboni, wakatangulie ng'ambo kwa Betsaida, hatta
yeye atakapoagana na makutano.

Hatta alipowaachia akaenda mlimani kuomba. Hatta ⁴⁶/₄₇ ikiwa jioni, chombo kiko kati ya bahari, naye peke yake katika inchi. Akawaona wakisumbuka kwa kuvuta, 48 kwani upepo ulikuwa juu yao. Hatta kama zamu la 'nne la usiku yuaja kwao, akitembea juu ya bahari; akataka kuwapita. Nao wakimwona anatembea juu ya 49 bahari, walithani kuwa kivuli, wakapiga makelele: kwani wote wakamwona, wakataabika. Marra akasema 50 nao, akawaambia, Tulieni: ndimi; msiwe na hofu. Akapanda kwao katika chombo; upepo ukakoma: waka- 51 shangaa ndani yao sana mno wakataajabika; kwani ha- 52 waikumbuki mikate, kwani moyo wao umekuwa hauoni. Wakivuka wakaja inchi ya Gennesareti, wakafika 53 pwani.

Hatta wakitoka katika chombo, marra wakimtambua, 54 wakapiga mbio katika inchi ile yote, wakaanza kuwa- 55 chukua katika vitanda walio hawawezi, wakisikia mahali ya kwamba alipo. Naye akiingia katika vijiji, ao 56 miji, ao mashamba, wakawaweka wagonjwa sokoni, wakamsihi wapate kugusa hatta upindi wa vazi lake; nao waliomgusa wakapona.

WAKAMKUSANYIKIA Mafarisayo na baathi ya **7**
 waandishi, watokao katika Yerusalemi, wakawaona **2**
 baathi ya waanafunzi wake wakila vyakula kwa mikono
 ya uchafu, ndiyo isiyooshwa. Kwani Mafarisayo na **3**
 Wayahudi wote wasiponawa mikono sana, hawali, waki-
 shika mapokeo ya wazee; wala kutoka katika sokoni, **4**
 wasipotia maji hawali; na manginge ni mengi waliyoyapokea kushika, kutiwa maji vikombe, na makopo, na
 vyombo vya shaba, na meza. Ndipo wakamwuliza Ma- **5**
 farisayo na waandishi, Mbona waanafunzi wako hawaendi kwa mapokeo ya wazee, lakini wala chakula kwa
 mikono ya uchafu? Akajibu akawaambia, ya kwamba, **6**
 Vizuri alitoa nabii Isaya wa ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa waniheshimia kwa midomo,
 moyo wao umekuwa mbali katika kwangu. Kwa uba- **7**
 tili waniabudu, wakifundisha mafundisho, amri za waana Adamu. Kwani mkiondoa amri ya Muungu, mwa- **8**
 shika mapokeo ya watu, kutiwa maji makopo na vikombe, na manginge kama haya mengi myafanyayo.
 Akawaambia, Vizuri mwawekea mbali amri ya Muungu, **9**
 mpate kulinda mapokeo yenu. Kwani Musa alinena, **10**

Uwaheshimie baba wako na mama wako, naye amnenaye
 11 vibaya baba ao mama kwa kufa apotee. Ninyi mwa-
 sema, Mtu akimwambia baba ao mama, Korban (ndio
 12 sadaka) uliyofayidiwa nami, wala hammwachi amfanyie
 13 neno baba ao mama, mkibatilisha neno la Muungu
 kwa mapokeo yenu mliyoyapokea: na kama haya mengi
 mwafanya.

14 Akiwaita makutano yote akawaambia, Nisikieni wote,
 15 mkafahamu. Hapana kitu kilicho 'nje ya mtu kikimwi-
 ngia, kiwezacho kumtia uchafu; lakini vitokavyo katika
 16 mwake ndivyo vimtiavyo uchafu. Mtu akiwa na masikio
 ya kusikia, asikie.

17 Hatta alipoingia nyumbani katika kwa makutano,
 18 waanafunzi wake wakamulizia mfano. Awaambia, Hivi
 na ninyi hamna akili? wala hamfikiri ya kwamba killa
 kilicho 'nje kikimwingia mtu hakiwezi kumtia uchafu,
 19 ya kwamba hakimwingii moyoni, illa matumboni, na
 20 katika choo chatoka, kisafishapo vyakula vyote? Aka-
 nena, Kimtokacho mtu, ndicho kintiacho mtu uchafu;
 21 kwani katika ndani, katika moyo wa mtu, hutoka ma-
 22 zungumzo mabaya, uzini, asherati, uuaji, uizi, kutamani,
 maovu, hila, jeuri, jicho la uovu, unajisi, kiburi, upum-
 23 bafu: haya yote maovu yatoka katika ndani, nayo yamtia
 mtu uchafu.

24 Akiondoka huko akaenda hatta mipaka ya Turo na
 Sidoni; na akiingia katika nyumba ametaka mtu asijue,
 25 wala hakuweza kustirika. Kwani mwanamke amesikia
 mambo yake, binti yake akiwa na pepo mchafu; akija
 26 akamwangukia miguuni. Naye mwanamke alikuwa
 Helleni, kwa asili Msurofenissa, akamtaka amfukuze pepo
 27 katika binti yake. Isa akamwambia, Wache watoto wa-
 shibe kwanza, kwani si vizuri kutwaa chakula cha wa-
 28 toto, na kutupa kwa mbwa. Akajibu, akamwambia,
 Yakini, Bwana, kwani hatta mbwa chini ya meza wala
 29 katika maanguko ya watoto. Akamwambia, Kwa neno
 30 hili nenda zako: pepo imetoka katika binti yako. Aki-
 fika nyumbani mwake akaona pepo imetoka, na binti
 yake amelazwa kitandani.

31 Akitoka tena katika mipaka ya Turo na Sidoni, akaja
 kwa bahari ya Galilaya, katika kati ya mipaka ya Dekapoli.
 32 Wakamchukulia kiziwi asiyesema vema, nao wa-
 33 msihi amtie mkono. Akimondosha katika kwa maku-

tano, kwa faragha, akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate akamgusa ulimi, akitazama juu 34 mbinguni, akaugua, akamwambia, Effatha, ndio Fumbuke. Marra masikio yake yamefumbuka, na mshipa wa 35 ulimi wake umelegea, akanena vizuri. Akawaagiza wa- 36 simwambie mtu: alivyowaagiza wakazidi sana kuhubiri, wakatoshewa kupita cheo, wakinena, Amefanya yote 37 vizuri; awafanya viziwi wasikie, na bubu waseme.

SIKU zile, makutano yakiwa mengi mno, wala hawana 8 kitu cha kula, akiwaita waanafunzi wake, awaambia, Nawahurumia makutano, ya kwamba sasa siku tatu 2 wakaa nami, wala hawana kitu cha kula, nami niki- 3 waacha waende zao wenyi njaa nyumbani kwao, watazimia njiani, kwani baathi yao wametoka mbali. Wa- 4 kamjibu waanafunzi wake, Mtu awezaje kuwashibisha na mikate hapa pasipo watu? Akawauliza, Mikate 5 mingapi mnayo? Wakanena, Saba. Akaamuru ma- 6 kutano wakae katika inchi; akiitwaa mikate saba akashukuru akavunja, akawapa waanafunzi wake, waweke mbele; wakaweka mbele ya makutano. Wakawa na 7 visamaki vichache; akabarikia akaamuru na hivi viwekwe. Wakala, wakashiba: wakaokota vipande vilivyo- 8 salia mapeto saba. Wakawa waliokula kama elfu nne: 9 akawaacha waende zao.

Marra akipanda chomboni, pamoja na waanafunzi wa- 10 ke, wakaja katika sehemu za Dalmanutha.

Wakatoka Mafarisayo wakaanza kuulizana naye; 11 wakitaka kwake ishara katika mbinguni, wakimjaribu. Akiugua rohoni akanena, Mbona kizazi hiki chataka 12 ishara? Amin nawaambia, hakitapewa kizazi hiki ishara. Akiondoka kwao, akapanda tena chomboni, aka- 13 ja ng'ambo.

Nao wamesahau kuleta mikate, wala hawakuwa nao 14 katika chombo illa mkate mmoja. Akawaagiza akinena, 15 Angalieni, mtazamie chachu la Mafarisayo na chachu la Herode. Wakasemana wao kwa wao, wakinena, Ya 16 kwamba mikate hatunayo. Akijua Isa awaambia, Mbo- 17 na mwasemana ya kwamba mikate hamnayo? Hamjafikiri? wala hamjafahamu? Mnao moyo hatta sasa hauoni? Mkiwa na macho hamwoni? mkiwa na masi- 18 kio hamsikii? wala hamkumbuki? Nilipovunja mi- 19 kate mitano kwa elfu tano, vikapo vingapi mlivyookota

- 20 vimejaa makombo? Wakamwambia, Thenashara. Na
saba ilipo kwa elfu nne, mapeto mangapi yaliyojazwa
- 21 na vipande mmeyaokota? Wakanena, Saba. Aka-
waambia, Kwaje hamfahamu?
- 22 Akija hatta Betsaida, wamletea kipofu, wamsihi
23 amguse. Akimtwaa kipofu mkono, akamleta hatta 'nje
ya mji, akatema mate juu ya macho yake, akamtia mi-
24 kono, akauliza kama aona kitu. Akatazama juu aka-
nena, Naona watu, ya kwamba kama miti naona waki-
25 tembea. Tena akamtia mikono juu ya macho yake,
akamfanya atazame juu: akaponyeka, akaona kwa wazi
26 yote. Akamtuma nyumbani kwake, akinena, Usiingie
katika mji, wala usimwambie mtu wa mjini.
- 27 Akatoka Isa na waanafunzi wake kwa vijiji vya Kai-
sariya Filipino; hatta njiani akawauliza waanafunzi wake
28 akiwaambia, Wasema watu mimi ni nani? Wakajibu,
Yohana 'mbatizaji; na wangine Eliya; wangine mmoja
29 wa nabii. Yeye akawaambia, Ninyi mwasema mimi ni
nani? Akijibu Siman Petro amwambia, Wewe u Ma-
30 siya. Akawatia sharti wasimwambie mtu mambo yake.
31 Akaanza kuwafundisha ya kwamba imempasa Mwana
wa Adamu kuteswa mengi na kukataliwa na wazee na
wakohani wakuu, na waandishi; na kuuawa, na baada ya
32 siku tatu kufufuka. Akasema neno hili pasipo hofu.
33 Akamtwaa Petro akaanza kumkemea. Akageuka aka-
watazama waanafunzi wake, akamkemea Petro, akinena,
Nenda zako nyuma yangu, Shetani, ya kwamba huwazi
yaliyo ya Muungu, illa yaliyo ya watu.
- 34 Akiwaita makutano pamoja na waanafunzi wake,
akawaambia, Apendaye kufuata nyuma yangu, ajika-
35 nie, atweke msalaba wake, anifuata. Kwani apendaye
kuokoa maisha yake, ataipoteza; atakayepoteza maisha
36 yake kwa ajili yangu, na ya anjili, ataiokoa. Itamfaa
nini mtu, akifayidi ulimwengu wote, akipata hasara ya
37 maisha yake? Ao mtu atoe nini kwa badala ya mai-
38 sha yake? Aonaye haya kwa mimi na maneno yangu,
katika kizazi hiki cha uzini na thambi, naye Mwana wa
Adamu ataona haya kwa yule, atakapokuja katika utu-
kufu wa Baba wake pamoja nao malaika watakatifu.
- 9 AKAWAAMBIA, Amin nawaambia, ya kwamba
wako wamesimama hapa, hawataona kufa, hatta wataka-
poona ufalme wa Muungu ukija kwa nguvu.

Hatta baada ya siku sita Isa atwaa Petro na Yakobo 2
na Yohana, awachukua katika mlima mrefu kwa faragha 3
peke yao, akageuka mbele yao. Na mavazi yake yame- 3
kuwa yaking'aa, meupe sana kama theluji, kama hapana 4
fundi katika inchi ajuaye kuyafanya meupe. Wakawa- 4
tokea Eliya na Musa, wakawa wakisema na Isa. Aka- 5
jibu Petro amwambia Isa, Rabbi, tu heri kuwa hapa sisi;
tukafanye vibanda vitatu; chako kimoja, cha Musa ki- 6
moja, na cha Eliya kimoja. Kwani hajui asemaje, kwa- 6
ni wameingiwa na hofu. Likawa wingu likiwatia kivuli: 7
ikaja sauti katika wingu, ikisema, Huyu ni Mwana 7
wangu nimpendaye: msikieni. Wakitazama ghafala 8
hawaoni mtu tena illa Isa peke yake pamoja nao.

Wakishuka katika mlima, akawaagiza wasimfasirie 9
mtu waliyoyaona, illa Mwana wa Adamu atakapofufuka 9
katika wafu. Wakalishika neno kwao, wakiulizana, 10
kufufuka katika wafu ni nini.

Wakamwuliza, wakinena, Mbona wasema waandishi 11
ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza? Akijibu, 12
akawaambia, Eliya yuaja kwanza, arudisha vyote, na
kama imeandikwa kwa Mwana wa Adamu, ateswe sana,
atharauliwe: lakini nawaambia ya kwamba Eliya ame- 13
kuja, nao wamemfanyia walivyopenda, kama alivyoa-
ndikiwa.

Akija kwa waanafunzi wake akaona makutano mengi, 14
wakiwazunguka, na waandishi wakiulizana nao. Marra 15
makutano wote wakimwona wakashtuka wakapiga mbio,
wakamsalimia. Akawauliza waandishi, Mwaulizia nini 16
nao? Akijibu mmoja wa makutano, akanena, Mwali- 17
mu, nimeleta kwako mwana wangu, aliye na pepo isiyon-
ena; na killa amtwaapo, amrarua, naye atoa pofu, asaga 18
meno yake, anyauka: nikasema na waanafunzi wako
wapate kuifukuza, wala hawakuweza. Akimjibu, anena, 19
Ee kizazi kisichoamini, hatta lini nitakuwako kwenu,
hatta lini nitachukuliana nanyi? Mleteni kwangu.
Wakamleta kwake. Akimwona marra pepo akamrarua, 20
akianguka chini akafingirika akitoa pofu. Akamwuliza 21
baba yake, Kwa muda gani imekuwa naye hivi? Aka-
nena, Tangu utoto. Na marra nyingi imemtupa katika 22
moto na katika maji, impoteze: lakini ukiweza neno,
utusayidie, uturehemu. Isa akamwambia, Ukiweza kua- 23
mini, yote yamkini kwake aaminiye. Marra akalia baba 24

- 25 wa mtoto na machozi, akanena, Bwana, naamini; unisaidie katika kutoa kuamini. Akiona Isa ya kwamba makutano wanakusanyika mbio, akamkemea pepo mchafu, akimwambia, Pepo usiyonena na kiziwi, nakuamuru,
- 26 toka kwake, wala usiingie tena kwake. Akalia akamraru sana, akatoka: akawa kama mfu, hatta wengi kune-
- 27 na ya kwamba amekufa. Isa akamshika mkono, akamwinua; akasimama.
- 28 Hatta akifika nyumbani waanafunzi wakamwuliza
- 29 kwa faragha, Mbona sisi hatukuweza kumfukuza? Akawaambia, Ginsi hiyo haiwezi kutoka illa kwa kuomba na kufunga.
- 30 Wakitoka huko wakaenda katika Galilaya; wala ha-
- 31 kupenda mtu ajue. Akawafundisha waanafunzi wake, akawaambia ya kwamba Mwana wa Adamu atolewa mikononi mwa watu, nao watamua; na akiisha kuuawa
- 32 atafufuka siku ya tatu. Hawa hawakufahamu anenalo, wakaogopa kumwuliza.
- 33 Akafika Kapernaum: hatta akiwa nyumbani, akawauliza, Nini mliyoadiliana ninyi kwa ninyi katika njia?
- 34 Wakanyamaza: kwani wamejadiliana njiani, ni nani
- 35 aliye mkuu. Akikaa kitako, akawaitia wathenashara, akawaambia, Mtu akitaka kuwa wa kwanza, atakuwa
- 36 wa mwisho wa wote na mngojea wote. Akitwaa mtoto, akamsimamisha kati yao, akamkumbatia, akawaambia,
- 37 Mtu atakayemkaribisha mmoja mtoto kama huyu kwa jina langu, anikaribisha mimi, na mtu anikaribishaye mimi, hanikaribishi mimi illa yeye aliyenituma.
- 38 Akamjibu Yohana akinena, Mwalimu, tumemwona mtu akifukuza pepo kwa jina lako, asiyetufuata sisi;
- 39 tukamkataza, ya kuwa hatufuati sisi. Isa akanena, Msimkataze; kwani hakuna atendaye nguvu kwa jina
- 40 langu, atakayeweza upesi kuninena vibaya. Kwani
- 41 asiye juu yetu, ni kwa ajili yetu. Kwani atakayewanyweshwa ninyi kikombe cha maji kwa jina langu, ya kuwa ninyi wa Masiya, amin nawaambia, thawabu yake
- 42 haitampotea. Naye atakayechukizisha mmoja wao wadogo waniaminio, yu heri afathali, akitiwa jiwe la kusagia katika shingo lake, akatupwe baharini. Na mkono wako ukikuchukizisha, ukatie mbali: u heri uingie katika uzima, ukipunguka kiungo, kuliko kwenda zako katika jehannum mwenyi mikono miwili, katika moto

usiozimika, funza wao asipo na mwisho, wala moto hau- 44
zimiki. Na mguu wako ukikuchukizisha, uukatie 45
mbali : u heri uingie katika uzima ukipunguka mguu
kuliko mwenyi miguu miwili kutupwa katika jehannum,
katika moto usiozimika, funza wao asipo na mwisho, 46
wala moto hauzimiki. Na jicho lako likikuchukizisha, 47
ulitupie mbali : u heri mwenyi chongo uingie katika ufa-
lme wa Muungu kuliko mwenyi macho mawili kutupwa
katika jehannum ya moto, funza wao asipo na mwisho, 48
wala moto hauzimiki. Killa mtu atatiwa chumvi kwa 49
moto, na killa thabihu itatiwa chumvi kwa chumvi.
Chumvi ni kizuri, illa chumvi kikiwa hakina chumvi, 50
kitatiwaje luththa? 'Mwe na chumvi ndani yenu,
mkapatane ninyi kwa ninyi.

AKIONDOKA huko yuaja katika mipaka ya Uya- 10
hudi kwa ng'ambo ya Yardeni, na tena makutano mengi
waenda kwake, na kama alivyozoea akawafundisha tena.

Nao Mafarisayo wakimwendea wakamwuliza kama 2
halali mtu amwache mkewe, wakimjaribu. Naye aki- 3
jibu, akawaambia, Ni nini aliyowaamuru Musa? Wa- 4
kanena, Musa akakubali kumwandikia khati ya talaka,
na kumwacha. Akajibu Isa, akawaambia, Kwa moyo 5
wenu kwa kuwa mgumu amewaandikia amri hii. Tangu 6
mwanzo wa kuumba Muungu amewafanya mume na
mke. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na 7
mama, ataambatana na mkewe, nao wawili watakuwa 8
mwili mmoja : hatta sio tena wawili, illa mwili mmoja.
Bassi Muungu aliyouna, mwana Adamu asiyatenge. 9

Na tena katika nyumba waanafunzi wake wakamwu- 10
liza ya hiyo. Awaambia, Atakayemwacha mke wake, 11
akimwoa mwingine, azini juu yake ; na mke akimwacha 12
mume wake, akiolewa na mgine, azini.

Wakamletea watoto awaguse : waanafunzi wakawa- 13
kemea waliowaleta. Akiona Isa akakasirika akawaa- 14
mbia, Waacheni watoto waje kwangu, msiwazuie : kwani
wao kama hawa ni ufalme wa Muungu. Amin nawaa- 15
mbia, asiyekubali ufalme wa Muungu kama mtoto, ha-
taingia humo. Akawakumbatia, akaweka mikono juu 16
yao, akawabarikia.

Hatta akitoka njiani, mtu akija mbio akimpigia 17
magote akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanyeni ni-
pate kuurithi uzima wa milele? Isa akamwambia, 18

- 19 Mbona waniita mwema? hakuna mwema illa mmoja,
 ndiye Muungu. Umezijua amri, Usizini, usiue, usiibe,
 usishuhudie uwongo, usidanganye, heshimie baba wako
 20 na mama. Akijibu amwambia, Mwalimu, haya yote
 21 nimeyalinda tangu ujana wangu. Isa akimtazama,
 akampenda, akamwambia, Moja umelipunguka. Nenda
 zako, kauza uliyo nayo, kawape masikini, nawe uta-
 kuwa na hasina mbinguni; haya tena, nifuate mimi,
 22 ukitweka msalaba. Naye akanuna kwa neno hili,
 akaenda zake huzunini, kwani alikuwa na mali mengi.
 23 Isa akitazama kuzunguka awaambia waanafunzi wake,
 Kwa shidda gani wenyi mali wataingia katika ufalme
 24 wa Muungu! Waanafunzi wakataajabika na maneno
 yake. Isa tena akijibu awaambia, Watoto, kwa shidda
 gani waaminio kwa mali waingie katika ufalme wa
 25 Muungu! Ni nyepesi ngamia apenye katika tundu la
 sindano, kuliko mtajiri kuingia katika ufalme wa
 26 Muungu. Wakatoshewa mno, wakinena wao kwa wao,
 27 Ni nani awezaye kuokoka? Akiwatazama Isa anena,
 Kwa watu haiyamkini, illa siyo kwa Muungu, kwani
 yote yamkini kwa Muungu.
 28 Akaanza Petro kumwambia, Angalia sisi tumeacha
 29 yote, tumekufuata wewe. Akijibu Isa, amwambia,
 Amin nawaambia, Hapana aliyeacha nyumba, ao ndugu,
 ao maumbu, ao laba, ao mama, ao mke, ao watoto, ao
 mashamba, kwa ajili yangu na kwa ajili ya aujili,
 30 asiyepewa marra mia sasa wakati huu, nyumba, na
 ndugu, na maumbu, na mama, na watoto, na mashamba,
 pamoja na mafukuzo, na katika zamani zijazo uzima
 31 wa milele. Wengi wa kwanza watakuwa wa mwisho,
 na wa mwisho wa kwanza.
 32 Walikuwa katika njia wakienda Yerusalemi, naye Isa
 akiwatangulia; wakatoshewa, hatta wakifuata wakao-
 gopa. Akiwatwaa tena wathenashara, akaanza ku-
 33 wambia yatakayompata, ya kwamba Tunakwenda
 Yerusalemi; naye Mwana wa Adamu atatolewa kwa
 wakohani wakuu na waandishi, nao watamhukumia
 34 kufa, na watamtoa kwa mataifa, na watamthihaki, na
 watampiga, na watamtemea mate, na watamua, na
 siku ya tatu atafufuka.
 35 Wamjia Yakobo na Yohana waana wa Zebedayo, wa-
 kinena, Mwalimu, twataka utufanyie tutakalotaka.

Akawaambia, Mwapenda niwafanyie nini? Waka-³⁶₃₇mwambia, Utupe tupate kukaa mmoja mkono wako wa kuume na mmoja mkono wako wa kushoto katika utukufu wako. Isa akawaambia, Hamjui mtakalo: mwa- 38weza kunywa kikombe mimi ninywacho, na kubatizwa na ubatizo nibatizwavyo mimi? Wakamwambia, Twa- 39weza. Isa akawaambia, Kikombe ninywacho mimi, mtakunywa, na ubatizo nibatizwavyo mimi, mtabatizwa; illa kukaa mkono wangu wa kuume ao wa kushoto si 40yangu nitoe, illa kwao waliofanyiziwa. Wakisikia wa- 41kumi wakaanza kukasirika na Yakobo na Yohana. Illa Isa akiwaita awaambia, Mwajua kama wanaothaniwa 42kuwa wa kwanza wa mataifa ndio bwana zao, na wakuu wao wanao uwezo juu yao. Haitakuwa hivyo kwenu: 43lakini apendaye kuwa mkuu kwenu atakuwa mngoje, naye apendaye kuwa wa kwanza kwenu atakuwa mtu- 44mwa wa wote. Kwani naye Mwana wa Adamu hakuja 45angojewe illa angojee, akatoe maisha yake ukombozi wa wengi.

Wakafika Yeriko: naye akitoka katika Yeriko, na 46waanafunzi wake, na makutano kathawakatha, mwana wa Timayo, Bartimayo kipofu, amekaa kitako upande wa njia akiomba. Hatta akisikia ya kwamba ni Isa 47Mnazareti, akaanza kulia na kunena, Mwana wa Daudi, Isa, unirehemu. Wakamkaripia wengi, anyamaze: aka- 48zidi sana kulia, Ee Mwana wa Daudi, unirehemu. Akisimama Isa, asema aitwe. Nao wamwita kipofu, 49wakimwambia, Uwe na moyo, ondoka; akuita. Akitupa 50vazi lake, akaondoka akaja kwa Isa. Isa akijibu 51amwambia, Wataka nini, nikufanyieje? Kipofu amwambia, Rabboni, nipate kuona. Isa amwambia, Nenda 52zako; imani yako imekuokoa. Marra akaona, akamfuata Isa njiani.

HATTA walipokaribia Yerusalemi, kwa Betfage na 11Betania mlimani mwa zeituni, atuma wawili wa waanafunzi wake, awaambia, Mwende zenu mji unaowalekea. 2Marra mkiingia huko mtaona mwana punda amefungwa, asiyepandika na mtu: mfungueni kamleteni. Mtu 3akiwaambia, Mwafanyani? semeni ya kwamba Bwana amwihtaji: marra atampeleka hapa. Wakaenda waka- 4mwona mwana punda amefungwa mlangoni 'nje, njia ilipozunguka; wakamfungua. Watu waliosimama huko 5

- wakawaambia, Mwafanyani, mkimfungua mwana punda?
 6 Wakawaambia kama alivyowaamuru Isa; wakawaacha.
 7 Wakamleta mwana punda kwa Isa, wakatupa juu yake
 8 mavazi yao; akakaa juu yake. Wengi wakatandika
 9 miti wakayatanda njiani. Waliotangulia na waliofuata
 10 wakalia, wakinena, Osanna; Mbarikiwa ajaye kwa jina
 la Bwana: Mbarikiwa ufalme ujao katika jina la Bwana,
 wa baba wetu Daud: Osanna katika juu.
- 11 Akafika Yerusalemi, hatta hekaluni: alipotazama yote,
 ikiwa saa ya jioni, akatoka hatta Betania, pamoja nao
 wathenashara.
- 12 Hatta assubui wakitoka katika Betania akaona njaa:
 13 hatta akiona mbali mtini mwenyi majani akaja, illi
 labuda aone kitu katika yake. Hatta akija hakuona
 kitu juu yake illa majani; kwani wakati wa tini bado.
- 14 Akajibu Isa akauambia, Mtu asile matunda katika
 wewe hatta milele. Waanafunzi wake wakamsikia.
- 15 Hatta wakifika Yerusalemi, Isa akaingia katika
 hekalu, akaanza kuwafukuza waliokuza na walionunua
 16 katika hekalu, akapindua meza zao waliovunja fetha,
 17 na viti vyao waliokuza njiwa, wala hakuacha mtu
 achukue chombo katika hekalu. Akafundisha, aki-
 waambia, Haikuandikwa ya kwamba Nyumba yangu
 itaitwa nyumba ya kuombea kwa mataifa yote? Ninyi
 18 mmeifanya paango la wanyang'anyi. Wakasikia wa-
 andishi na wakohani wakuu, wakatafuta wapateje ku-
 mpoteza: kwani wakamwogopa, ya kuwa makutano yote
 19 wakataajabu kwa elimu yake. Hatta ikiwa jioni, aka-
 toka 'nje ya mji.
- 20 Hatta assubui wakipita, wakaona mtini umekauka
 21 katika mashina. Akikumbuka Petro amwambia, Rabbi,
 22 tazama, mtini ulioulaani, umekauka. Akijibu Isa,
 23 awaambia, 'Mwe na imani ya Muungu. Kwani
 amin nawaambia, ya kwamba atakayeambia mlima
 huu, Ung'oke, utupwe baharini, wala hana shaka
 moyoni mwake, illa aamini anenalo litakuwa, itakuwa
 24 kwake kama anenavyo. Kwa hizo nawaambia, Killa
 mtakalolitaka katika kuomba, mkiamini ya kwamba
 25 mwapokea, litakuwa kwenu. Nanyi msimamapo ku-
 mba, msamehe, mkiwa na neno juu ya mtu, illi Baba
 yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi makosa yenu.

Msiposamehe ninyi, wala Baba yenu aliye mbinguni 26
hatasamehe makosa yenu.

Wakafika tena Yerusalemi: hatta akitembea katika 27
hekalu, wamjia wakohani wakuu na waandishi na
wazee, wamwambia, Kwa uwezo gani wafanya haya? 28
na nani aliyekupa uwezo huu upate kufanya haya?
Isa akijibu akawaambia, Nitawauliza na ninyi neno 29
moja, mkanijibu, nami nitawaambia kwa uwezo gani
nafanya haya. Ubatizo wa Yohana ulikuwa wa mbi- 30
nguni ao wa waana Adamu? Mnijibu. Wakafanya 31
huja wao kwa wao, wakinena, Tukisema, wa mbinguni,
atasema, Mbona hamkumwamini? Tukisema wa waana 32
Adamu, wakawaogopa watu, kwani wote wakamshika
Yohana, ya kwamba yakini nabii. Wakijibu wamwa- 33
mbia Isa, Hatujui. Isa akijibu awaambia, Wala mimi
siwaambii kwa uwezo gani nayafanya haya.

AKAANZA kuwaambia kwa mifano. Mtu alipanda 12
mizabibu, akazungusha kitalu, akachimbulia kwa shi-
nikizo, akajenga mnara, akapangisha kwa wakulima,
akasafiri. Akatuma mtumwa kwa wakulima wakati 2
wake, apokee kwa wakulima ya mazao ya mizabibu.
Hawa wakimtwa wakampiga wakamfukuza hana kitu. 3
Akatuma tena kwao mtumwa mwingine. Huyu waka- 4
mtupia mawe, wakamjeruhi kitwa, wakamfukuza amea-
ibishwa. Tena akapeleka mwingine; wakamua. Na we- 5
ngi wangineo; wangine wakapigwa, wangine wakauawa.
Hatta akiwa na mwana mmoja mpenzi wake, aka- 6
mtuma huyu kwao mwisho, akisema, ya kwamba Wata-
mwangalia mwana wangu. Wale wakulima wakanena 7
wao kwa wao, ya kwamba, Huyu ni mrithi; haya, tu-
mwulie mbali, na urithi utakuwa wetu. Wakamtwaa, 8
wakamua, wakamtupa 'nje ya mizabibu. Bassi atafa- 9
nyani mwenyi mizabibu? Atakuja atawapoteza wa-
kulima, atatoa mizabibu kwa wangineo. Hamkusoma 10
kamwe andiko hili? Jiwe wasilolikubali waashi, hili
limekuwa kuu la pembeni: kwa Bwana imekuwa hii, 11
nayo ajabu machoni petu. Wakatafuta wamkamate, 12
wakaogopa makutano: kwani wakatambua ya kwamba
juu yao amesema mfano. Wakimwacha wakaenda zao.

Watuma kwake watu wa Mafarisayo na Maherodiani 13
wamnase kwa neno. Wakija wamwambia, Mwalimu, 14
tumekujua kama mwenyi kweli, wala hufikiri kwa mtu,

kwani huangalii cheo cha mtu, illa wafundisha kwa kweli njia ya Muungu. Halali kutoa kodi kwa Kaisari
 15 ao sivyo? Tutoe, ao tusitoe? Naye akijua unafiki wao akawaambia, Mbona mwanjaribu? nileteeni dinari
 16 niione. Wakaleta. Naye awaambia, Ya nani sura hii
 17 na andiko? Wakamwambia, Ya Kaisari. Akijibu Isa akawaambia, Rudisheni kwa Kaisari yaliyo ya Kaisari, nayo yaliyo ya Muungu kwa Muungu. Wakamtaajibia.

18 Na Masadukayo waja kwake, wasemao hapana kiyama,
 19 wakamwuliza, wakinena, Mwalimu, Musa alituandikia, ya kwamba, ndugu yake mtu akifa, akimwacha mke, wala watoto hawaachi, ndugu yake amtwa mke wake,
 20 asimamisha uzao kwa ndugu yake. Bassi palikuwapo ndugu saba: wa kwanza akatwaa mke, akifa hakuacha
 21 uzao. Wa pili akamtwaa, akafa, wala yeye hakuacha
 22 uzao: na wa tatu kathálíka. Wakamtwaa saba, wala ha-
 23 wakuacha uzao. Mwisho wa wote na mke akafa. Bassi katika kiyama, watakapofufuka, wa yupi wao atakuwa
 24 mke? kwani saba walikuwa naye mke. Akijibu Isa akawaambia, Si kwa hiyo mmepotea, msipoyajua maa-
 25 ndiko, wala nguvu za Muungu? Kwani, watakapo-
 26 fufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi, lakini wako kama malaika katika mbingu. Kwa wafu, ya kwamba wafufuka, hamkusoma katika kitabu cha Musa, juu ya kijiti, alivyomwambia Muungu, akinena, Mimi ni Muungu wa Ibrahimu, na Muungu wa Isaak, na
 27 Muungu wa Yakobo? Siye Muungu wa wafu, illa Muungu wa wahayi: bassi ninyi mmepotea sana.

28 Akija mmoja wa waandishi akiwasikia wakiulizana, akijua ya kwamba amewajibia vizuri, akamwuliza, Ipi
 29 iliyo amri ya kwanza ya yote? Isa akamjibu ya kwamba Ya kwanza ya amri zote, Sikie, Israeli; Bwana
 30 Muungu wetu ni Bwana mmoja: nawe umpende Bwana Muungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.
 31 Ndiyo amri ya kwanza. Na ya pili kwa mfano wake, Umpende jirani wako kama mwenyewe. Iliyo kuu
 32 kuliko hizi hapana amri. Akamwambia mwandishi, Vizuri, mwalimu, vya kweli umenena: ya kwamba ni
 33 mmoja Muungu, wala hapana mwingine illa yeye; na kumpenda kwa moyo wote, na kwa akili zote, na kwa

roho yote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani kama mwenyewe, kumepita makafara yote na thabibu. Isa akimwona amejibu kama mwenyi akili, akamwa- 34 mbia, Si mbali wewe katika ufalme wa Muungu. Wala mtu hakuthubutu tena kumwuliza.

Akajibu Isa akanena, akifundisha katika hekalu, 35 Wasemaje waandishi ya kwamba Masiya ni mwana wa Daudi? Kwani Daudi mwenyewe anena kwa Roho 36 Mtakatifu, Bwana akamwambia bwana wangu, Uketi mkono wa kuume wangu, hatta nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako. Bassi Daudi mwenyewe 37 amwita Bwana; amekuwaje mwana wake? Walio wengi wa makutano wakamsikia kwa furaha.

Akawaambia katika fundisho lake, Angalieni waa- 38 ndishi, wapendao kutembea wenyi mavazi marefu, na kusalimiwa sokoni, na viti vya kwanza katika masu- 39 nagogi, na kuwekato katika karamu : walao nyumba 40 za wajaani, na kwa wonyesho wadumu katika kusali : hawa watapewa hukumu izidiyo.

Akikaa Isa akilekea hasina atazama watupavyo ma- 41 kutano fetha katika hasina : na wengi wenyi mali wakatupa mengi. Akija mmoja mjaani maskini akatupa 42 nusu pesa mbili, ndiyo kodranto. Akiwaita waanafunzi 43 wake awaambia, Amin nawaambia, ya kwamba mjaani huyu maskini ametupa nyingi kuliko wote watupao katika hasina : kwani wote walitupa katika yaliyozidi 44 kwao ; huyu katika kupunguka kwake ametupa yote aliyo nayo, maisha yake yote.

HATTA akitoka katika hekalu, amwambia mmoja 13 wa waanafunzi wake, Mwalimu, angalia, mawe gani na majengo gani ! Akijibu Isa akamwambia, Waona haya 2 majengo makubwa ? halitaachwa jiwe juu ya jiwe, lisiloangushwa.

Hatta akikaa kitako katika mlima wa zeituni kuli- 3 lekea hekalu, wakamwuliza kwa faragha Petro na Yakobo na Yohana na Andrea, Twambie, haya ya- 4 takuwa lini ? Na nini dalili haya yote yatakapotimizwa ? Isa akiwajibu akaanza kunena, Angalieni mtu asiwa- 5 danganye : kwani wengi watakuja kwa jina langu wa- 6 kinena, Ndimi ; na watadanganya wengi. Mtaka- 7 posikia vita na habari za vita, msilalamike : kwani sharti ziwe ; illa mwisho bado. Taifa litaondoka juu ya taifa, 8

na ufalme juu ya ufalme; yatakuwa matetemeko mahali mahali; zitakuwa na njaa na fitina. Mianza ya machungu haya.

9 Angalieni ninyi wenyewe: kwani watawatoa kwa mabaraza, na katika masunagogi mtapigwa, na mtaletwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu,
10 kwa ushahidi kwao. Na katika mataifa yote imepasa
11 kwanza anjili ihubiriwe. Watakapowaleta wakitoa, msitaabike kwanza mtanenani, wala msifikiri: lakini mtakalopewa ninyi saa ile, hilo mlinene: kwani si ninyi
12 mnenao, illa Roho Mtakatifu. Ndugu atamtoa ndugu kwa kufa, na baba mtoto, na watoto watasimama juu
13 ya wazazi wao, nao watawafisha. Mtakuwa mmechukiwa na wote kwa ajili ya jina langu: naye aliyestahimili hatta mwisho, huyu ataokoka.

14 Mtakapoliona chukizo la uharibifu, lililonenwa na Danieli nabii, limesimama pasipolipasa (asomaye afa-hamu), ndipo walio katika Uyahudi wakimbie milimani:
15 aliye juu darini asishuke katika nyumba, wala asiingie
16 achukue kitu katika nyumba yake; naye aliye katika
17 mashamba asigeuke nyuma atwae vazi lake. Ole wao
18 wenyi mimba nao wanyonyeshao siku zile! Ombeni
19 msipate kukimbia wakati wa baridi. Kwani siku zile zitakuwa shidda kama zisizo tangu mwanzo wa kuumba
20 alipoumba Muungu hatta sasa, wala hazitakuwa. Wala Bwana asipopunguza siku zile, haungaliokoka mwili: lakini kwa ajili yao wateule, aliowachagua, amezipunguza siku.

21 Wakati huu mtu akiwaambia, Angalia, hapa Masiya;
22 ao, angalia, huko; msimwamini: kwani wataondoka masiya za uwongo na nabii za uwongo, watatoa ishara na ajabu, hatta kudanganya, kama yamkini, nao wateule.
23 Angalieni ninyi: nimewaambia ninyi mbele yote.

24 Lakini siku zile baada ya shidda ile, jua litatiwa giza,
25 na mwezi hautatoa nuru yake, na nyota za mbinguni zitakuwa zikianguka, na nguvu za mbinguni zitatiki-
26 sika. Ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija
27 katika mawingu na nguvu nyingi na utukufu. Ndipo atakapotuma malaika zake, nao watakusanya wateule wake katika pepo nne, katika mwisho wa inchi hatta
28 mwisho wa mbingu. Kwa mtini mjifunze mfano: tawi

lake likiwa sasa limelainika, na kuchanua majani, mwajua kama wakati wa hari ni karibu. Hivi na ninyi 29 mwonapo haya yanakuwa, jueni ya kwamba karibu sasa milangoni. Amin nawaambia, ya kwamba kizazi hiki 30 hakitapita hatta haya yote yamekuwa. Mbingu na 31 inchi zitapita; maneno yangu hayapiti.

Mambo ya siku ile na saa hakuna ajuaye, wala 32 malaika walio mbinguni, wala Mwana, asipokuwa Baba.

Angalieni, kesheni kaombeni, kwani hamjui lini ni 33 wakati. Kama mtu asafiriye akiacha nyumba yake, 34 akiwapa watumwa wake uwezo, na killa mtu kazi yake, na mngoje mlango amwamuru akeshe. Bassi kesheni: 35 hamjui wakati bwana wa nyumba ajapo, jioni, ao kati ya usiku, ao awikapo jogoo, ao assubui: asije ghafala 36 kuwaona ninyi mmelala. Niwaambiayo ninyi nawaa- 37 mbia wote, Kesheni.

ILIKUWA pasaka na isiyochachwa baada ya siku 14 mbili: wakatafuta wakohani wakuu na waandishi wapateteje kumkamata kwa hila na kumua. Wakanena, Si 2 katika karamu, isiwe fitina katika watu.

Akiwa yeye katika Betania nyumbani mwa Siman 3 mwenyi ukoma, akikaa mezani, akaja mwanamke mwenyi alabastro ya marhamu ya nardo hassa ya thamani nyingi; akiivunja alabastro akaimimina kitwani mwake. Walikuwa waliokasirika kwa ndani, wakanena, Kwa 4 nini umekuwa upotevu huu wa marhamu? Kwani 5 marhamu ingalikuzwa kwa zayidi ya dinari mia tatu, na kutolewa kwa maskini. Wakamnung'unia. Aka- 6 nena Isa, Mwacheni; mbona mwamtia taabu? Ametenda tendo zuri kwangu. Kwani sikuzote mnao mas- 7 kini pamoja nanyi, na mpendapo mwaweza kuwate- ndea vema: mimi hamnami sikuzote. Ametenda alivyo 8 navyo: ametangulia kunitia mwili marhamu kwa kuzi- kwa kwangu. Amin nawaambia, itakapohubiriwa 9 anjili hii katika ulimwengu wote, navyo alivyofanya huyu vitanenwa kwa ukumbusho wake.

Na Yuda Iskariota, mmoja wa wathenashara, akaenda 10 zake kwa wakohani wakuu amtoe kwao. Wakisikia 11 wakafurahi, wakaahidi kumpa fetha. Akatafuta apateje kumtoa wakati wa kuwafaa.

Hatta siku ya kwanza ya isiyochachwa, walipochinja 12

pasaka, wamwambia waanafunzi wake, Pa wapi upe-
 13 ndapo tuende tufanye tayari, uile pasaka? Akatuma
 wawili wa waanafunzi wake, akiwambia, Mwende zenu
 katika mji; atawakuta mtu achukuaye mtungi wa maji;
 14 mfuateni: hatta atakapoingia, mwambieni mwenyi nyu-
 mba ya kwamba Mwalimu asema, Pa wapi pa kupu-
 15 mzika nile huko pasaka na waanafunzi wangu? naye
 atawaonyesha dari kubwa iliyotandikwa tayari: huko
 16 mfanyeni tayari. Wakatoka waanafunzi wake, wakaja
 mjini, wakaona kama alivyowaambia, wakaifanya tayari
 pasaka.

¹⁷₁₈ Ikiwa jioni yujaja pamoja nao wathenashara. Nao
 wakikaa mezani na kula, anena Isa, Amin nawaambia,
 19 ya kwamba mmoja wenu atanitoa akila nami. Wa-
 kaanza kuhuzunika na kumwambia mmoja mmoja, Ni
 20 mimi? Na mwingine, Ni nimi? Akijibu akawaambia,
 Mmoja wa wathenashara achovyaye pamoja nami katika
 21 kombe. Mwana wa Adamu aenda zake kama alivyo-
 andikiwa: ole wa mtu yule amtoaye Mwana wa Adamu!
 angalikuwa heri kama hangalizaliwa mtu yule.

22 Nao wakila, Isa akitwaa mkate, akibariki, akavunja,
 akawapa, akanena, Twaeni, leni: ndio mwili wangu.
 23 Akitwaa kikombe, akishukuru, akawapa; wakakinywea
 24 wote. Akawaambia, Ndicho damu yangu ya agano
 25 jipya iliyomwagika kwa wengi. Amin nawaambia, ya
 kwamba sitakunywa tena ya uzao wa mzabibu, hatta
 siku ile nitakapounywa mpya katika ufalme wa Muu-
 ngu.

26 Wakiisha kuimba uimbo wakatoka hatta mlimani mwa
 27 zeituni. Isa awaambia, ya kwamba Mtachukizwa wote
 katika mimi usiku huu: ya kuwa imeandikwa, Nitam-
 28 piga mchungu, na kondoo watatawanyika. Lakini nita-
 kapokwisha kufufuka, nitawatangulia kwenda Galilaya.
 29 Petro akamwambia, Na wote wakichukizwa, si mimi.
 30 Amwambia Isa, Amin nawaambia, ya kwamba wewe
 leo, usiku huu, mbele jogoo hajawika marra mbili, uta-
 31 nikania marra tatu. Naye akazidi sana kunena, Hatta
 ikinipasa kufa nawe, sitakukania. Hivi wakanena na
 wote.

32 Nao waja mahali jina lake Gethsemane: awaambia
 waanafunzi wake, Ketini hapa, hatta nitakapoomba.
 33 Atwaa Petro na Yakobo na Yohana pamoja naye, akaa-

nza kushangaa na kutaabika. Awaambia, Roho yangu 34
 inayo huzuni nyingi hatta kufa: kaeni hapa mkakeshe.
 Akienda mbele kidogo, akaanguka katika inchi, aka- 35
 mba kama yamkini saa impitie. Akanena, Abba, Baba, 36
 yote yamkini kwako; nichukulie kikombe hiki: illa silo
 nilipendalo mimi, illa wewe. Akija awaona wamelala; 37
 amwambia Petro, Siman, walala? Huna nguvu za
 kukesha saa moja? Kesheni kaombeni, msipate kuingia 38
 katika kujaribiwa. Roho nyepesi, mwili thaifu. Akie- 39
 nda zake tena akaomba, akinena neno lilihili. Hatta 40
 akirudi akawaona wamelala tena, kwani macho yao
 yamekuwa mazito, wala hawakujua kumjibu.

Akija ya tatu, awaambia, Laleni iliyosalia, mkapu- 41
 mzike: yatosha, saa imekuja; Mwana wa Adamu ame-
 tolewa mikononi mwao wenyi thambi. Ondokeni, 42
 twende; anitoaye amekaribia.

Marra hatta akiwa katika kunena, anafika Yuda, aliye 43
 mmoja wa wathenashara, na pamoja naye makutano
 mengi na panga na marungu, waliotoka kwa wakohani
 wakuu na waandishi na wazee. Atoaye amewapa 44
 ishara, akinena, Nitakayembusu, ndiye; mkamateni,
 mkamchukue salama. Akija marra akimwendea anena, 45
 Rabbi, Rabbi; akambusu sana.

Wale wakamtia mikono yao, wakamkamata. 46

Mmoja wao waliosimamia, akifuta upanga, akampiga 47
 mtumwa wa mkohani mkuu, akamkatia sikio. Akijibu 48
 Isa, akawaambia, Kama juu ya mnyang'anyi mmetoka
 na panga na marungu, mnitwae? Siku kwa siku nalikaa 49
 kwenu katika hekalu nikifundisha, wala hamkunika-
 mata: illa maandiko yapate kutimizwa. Wakimwacha 50
 wote wakakimbia.

Na kijana mmoja akamfuata, amevaa shuka juu ya 51
 utupu; wakamkamata vijana: naye akiiacha shuka aka- 52
 wakimbilia utupu.

Wakamchukua Isa kwa mkohani mkuu: wakakusa- 53
 nyika kwake wote wakohani wakuu na wazee na
 waandishi. Na Petro akamfuata mbali hatta ndani 54
 katika behewa ya mkohani mkuu; akawa amekaa kitako
 nao watumishi, akakota moto.

Wakohani wakuu na baraza yote wakataka juu ya 55
 Isa ushahidi wa kumfisha, wala hawakuona: kwani wengi 56
 wakamshuhudia uwongo, wala ushahidi wao si mmoja.

57 Hatta wangine wakisimama wakamshuhudia kwa uwo-
 58 ngo, wakinena ya kwamba Sisi tumemsikia akisema ya
 kwamba Mimi nitaliharibu hekalu hili, lililofanyika
 kwa mikono, na kwa siku tatu nitajenga linginelo lisilo-
 59 fanyika kwa mikono: wala hivi ushahidi wao si mmoja.
 60 Akisimama kati mkohani mkuu akamwuliza Isa aki-
 61 sema, Hujibu neno? Hawa wakushuhudiani? Aka-
 nyamaa, wala hakujibu neno.

Mkohani mkuu akamwuliza tena, akimwambia, Ndiwe
 62 Masiya Mwana wake aliyebarikiwa? Isa akanena,
 Ndimi: nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi
 mkono wa kuume wa nguvu, na akija na mawingu ya
 mbingu.

63 Mkohani mkuu akararua joho lake, akinena, Twa-
 64 takaje tena mashahidi? Mmesikia unajisi: Mwaonaje?
 65 Wote wakamhukumia imempasa kufa. Wakaanza wa-
 ngine kumtemea mate, na kumfunika uso, na kumpiga
 kwa konde, na kumwambia, Ufanye unabii. Watumishi
 wakampiga kofi.

66 Akiwa Petro katika behewa chini, yuaja mmoja wa
 67 vijakazi wa mkohani mkuu: akimwona Petro akikota
 moto akamtazama, akinena, Na wewe ulikuwa pamoja
 68 na Mnazreti Isa. Akakana, akinena, Sijui, wala sisikii
 unenayo. Akatoka 'nje ukumbini; jogoo akawika.
 69 Kijakazi akimwona tena akaanza kuwaambia waliosi-
 70 mama karibu, ya kwamba, Huyu ni wa kwao; akakana
 tena. Baadaye kidogo tena waliosimama karibu waka-
 mwambia Petro, U kweli wa kwao, kwani na Mgalilaya
 71 wee, na maneno yako ndiyo. Akaanza kulaani na
 kuapa, ya kwamba, Simjui mtu huyu 'mmnenaye.
 72 Marra ya pili jogoo akawika. Akakumbuka Petro neno
 alilomwambia Isa, ya kwamba Mbele ya kuwika jogoo
 marra mbili, utanikania marra tatu. Akafikiri, akalia.

15 MARRA assubui wakafanya shauri wakohani wakuu
 pamoja na wazee na waandishi na baraza yote, waka-
 mfunga Isa wakamchukua wakamleta kwa Pilato.

2 Akamwuliza Pilato, Ndiwe mfalme wa Wayahudi?
 3 Akijibu amwambia, Wasema. Wakamstaki sana wako-
 4 hani wakuu. Pilato tena akamwuliza akinena, Hujibu
 5 neno? Angalia, mangapi wakushuhudia. Wala Isa
 hakujibu neno kabisa, hatta kutaajabu Pilato.

6 Kwa karamu huwafungulia mmoja aliyefungwa,

wamtakaye. Palikuwa aliyelitwa Barabba, aliyefungwa 7
 pamoja nao waliofanya fitina naye, waliofanya uuaji
 katika fitina. Na makutano wakipiga kelele, wakaanza 8
 kutaka kama amefanya sikuzote kwao. Pilato aka- 9
 wajibu, akinena, Mwapenda niwafungulie mfalme wa
 Wayahudi? Kwani akajua ya kwamba kwa hasidi 10
 wakohani wakuu wamemtoa. Wakohani wakuu waka- 11
 washawishi makutano afathali awafungulie Barabba.
 Pilato akijibu tena awaambia, Mwapendani, nimfa- 12
 nyieje mmwitao mfalme wa Wayahudi? Wakalia tena, 13
 Msulibishe. Pilato akawaambia, Kwani uovu gani 14
 alioufanya? Wakazidi kulia, Msulibishe.

Pilato akitaka kuwafanyia rathi makutano, aka- 15
 wafungulia Barabba, akamtoa Isa, apigwe, illi asuli-
 bishwe.

Asikari wakamleta ndani ya behewa, ndiyo Praitorio, 16
 wakawaita pamoja kikosi chote. Wakamvika porfuro, 17
 wakamtia taji wakiisuka kwa miiba, wakaanza kumsa- 18
 limia, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! Wakampiga 19
 kitwa kwa unyasi, wakamtemea mate, wakapiga magote
 wakamsujudia. Hatta walipomthihaki, wakamvulia 20
 porfuro, wakamvalia nguo zake yeye, wakamleta wa-
 msulibishe. Wakamlazimisha mtu apitaye, Siman Mku- 21
 rene, akitoka mashamba, baba wa Iskander na Rufo,
 achukue msalaba wake.

Wakamleta juu ya mahali Golgotha, ndiyo ikifasirika 22
 mahali pa kitwa. Wakampa kunywa mvinyo uliotiwa 23
 manemane, illa yeye hakupokea. Hatta walipomsu- 24
 libisha wakagawanya nguo zake, wakipiga kura juu
 yao killa mtu atwae nini. Ilikuwa saa ya tatu, waka- 25
 msulibisha. Palikuwa na andiko la mstaki wake limea- 26
 ndikwa juu, MFALME WA WAYAHUDI.

Na pamoja naye wasulibisha wanyang'anyi wawili, 27
 mmoja upande wake wa kuume na mmoja upande wa
 kushoto. Limetimika andiko linenalo, Akahesabika 28
 pamoja nao wasio na sheria.

Nao waliopita wakamnenea unajisi, wakitikisa vitwa 29
 vyao, wakinena, Wa! Uharibuye hekalu, na kwa siku
 tatu ujengaye, ujiokoe mwenyewe, kashuka katika 30
 msalaba. Hivi na wakohani wakuu wakithihaki wao 31
 kwa wao pamoja na waandishi, wakanena, Aliwaokoa
 wangine; mwenyewe hawezi kujiokoa. Masiya mfalme 32

wa Israeli ashuke sasa katika msalaba, tupate kuona na kuamini. Waliosulibishwa pamoja naye wakamshu-
 33 tumu. Ikiwa saa ya sita, palikuwa giza juu ya inchi
 34 yote, hatta saa ya tissa. Na saa ya tissa Isa akapiga kelele kwa sauti kuu, akinena, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Ndiyo ikifasirika, Muungu wangu, Muungu
 35 wangu, kwa nini umeniacha? Watu waliosimama
 36 karibu wakisikia wakanena, Amwita Eliya. Mmoja akipiga mbio, akajaza sifongo na siki, akaitia 'mwanzini, akamnyweshwa, akinena, Mwache; tuone kama Eliya yuaja amshushe.

³⁷₃₈ Isa akitoa sauti kuu, akapuzia roho. Pazia la hekaluni likapasuka vipande viwili juu hatta chini.

39 Akiona akida aliyesimama kumlekea ya kwamba akilia hivi akapuzia roho, akanena, Kweli mtu huyu alikuwa Mwana wa Muungu.

40 Palikuwako na waanawake wakitazama mbali; katika hawa Maryamu Magdalene, na Maryamu mama wa
 41 Yakobo mdogo na Yose, na Salome, ndio alipokuwa katika Galilaya waliomfuata na waliomngojea; na wengine wengi waliopanda naye hatta Yerusalemi.

42 Hatta sasa ikiwa jioni, ilipokuwa paraskeue, ndiyo
 43 iliyo mbele ya sabato, akija Yusuf aliye wa Arimathaya, diwani mwenyi heshima, aliyekuwa na mwenyewe akiutazamia ufalme wa Muungu, amethubutu kuingia
 44 kwa Pilato, akataka mwili wa Isa. Pilato akataajabu kama sasa amekufa; hatta akimwita akida akamwuliza
 45 kama toka hapo amekufa: akijua kwa akida, akamtu-
 46 nikia Yusuf mwili. Naye akinunua kitani akamshusha akamkunja katika kitani, aka'mweka katika kaburi, lililochimbuka katika mwamba, akafingirisha jiwe juu
 47 ya mlango wa kaburi. Maryamu Magdalene na Maryamu wa Yose wakaona alipowekwa.

16 HATTA sabato ikipita Maryamu Magdalene na Maryamu wa Yakobo, na Salome, wakanunua manukato
 2 wapate kuja kumtia marhamu. Hatta asubui mapema ya kwanza ya sabato waja kwa kaburi jua likitoka.
 3 Wakasema wao kwa wao, Nani atatufingirishia jiwe
 4 katika mlango wa kaburi? Hatta wakitazama waona ya kwamba limefingirishiwa mbali jiwe: kwani lilikuwa kubwa mno.

5 Wakiingia kaburini wakaona kijana amekaa upande

wa kuume, amevaa vazi jeupe; wakastuka. Awaambia, 6
 Msistuke: mwamtafuta Isa Mnazareti aliyesulibishwa:
 amefufuka; hapo hapa. Angalia mahali walipo'mweka.
 Lakini mwende zenu, waambieni waanafunzi wake na 7
 Petro, ya kwamba awatangulia kufika Galilaya: huko
 mtamwona, kama alivyowaambia. Wakatoka upesi 8
 wakakimbia katika kaburini; wakawa na tetemeko
 na kupotewa akili: wala hawakumwambia mtu neno,
 kwani wakaogopa.

Akiondoka assubui ya kwanza ya sabato akamtokea 9
 kwanza Maryamu Magdalene, katika yake alifukuza
 pepo saba. Huyu akienda akawapa habari waliokuwa 10
 pamoja naye, wakihuzunika na wakilia. Nao wakisikia 11
 kama yu hayi, naye ameonekana naye, hawakusadiki.

Baada ya haya akawatokea wawili wao kwa namna 12
 ngingine wakitembea wakienda mashamba. Nao hawa 13
 wakienda zao wakawapa habari waliosalia: wala hawa
 hawakuwasadiki.

Hatima akawatokea edashara wakikaa mezani, aka- 14
 walaumu kwa kutoa kuamini na kuwa mgumu moyo
 wao, ya kwamba waliomwona alipofufuka hawakuwa-
 sadiki. Akawaambia, Mkienda katika ulimwengu wote 15
 pia hubirini anjili kwa kiumbe chote. Aaminiye na 16
 abatizwaye ataokoka; asiyeamini atahukumywa. Ishara 17
 hizi zitafuatana nao waaminio; kwa jina langu watafu-
 kuza pepo; watasema kwa ndimi mpya; watatwaa nyoka; 18
 hatta wakinywa kitu cha kufisha hakitawathuru; watatia
 mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.

Bassi Bwana alipokwisha kusema nao, akatwaliwa 19
 juu mbinguni, akaketi kwa kuume kwa Muungu.

Wale wakitoka wakahubiri po pote, Bwana akitenda 20
 nao, na akilifanya imara neno kwa ishara zilizofuatana.
 Amin.

ANJILI KWA LUKA.

- 1 NILIPOONA watu wangi walipotia mkono kuandika
 2 habari ya mambo yaliyokuwa sabidi kwetu, kama tuli-
 vyopokea kwa wale waliokuwa mashahidi na watumishi
 3 wa neno tangu mwanzo; mimi nami naliona heri, nili-
 pofuasa kwa bidii maneno yote tangu mwanzo, kukua-
 ndikia wewe, Teofilo, rafiki yangu, kama yafuatanavyo,
 4 kwamba nawe upate kujua hakika ya maneno uliyofu-
 nzwa.
- 5 Majira ya Herode mfalme wa Uyahudi, kulikuwa na
 mkohani, jina lakwe Zakariya, safu ya Abia, na mkewe
 alikuwa mwana wa benati Harun, na jina lakwe Elisabeti.
- 6 Nao wote wawili walikuwa na mioyo ya kunyoka mbele
 za Muungu, wakaendelea katika amuri na haki zote za
 7 Bwana, wasiwe na makosa. Nao walikuwa hawana
 mwana, kwani Elisabeti alikuwa tasa, nao wote wawili
 walikuwa wanakwenda mbele kwa siku zao.
- 8 Basi ikawa akifanya kazi yakwe ya ukohani mbele za
 9 Muungu kwa zamu ya safu yakwe, kura ikamwangukia
 kwa ada ya ukohani, kuvukiza uvumba, akaenda heka-
 10 luni mwa Bwana. Na ungi wote wa watu walikuwa
 11 wakisali 'nde kwa wakati wa kuvukiza. Basi akamtokea
 malaika wa Bwana, akisimama kwa mkono wa kulia wa
 12 mathbahu pavukizwapo. Akakutuka Zakariya alipo-
 mwona, na hofu ikamwangukia.
- 13 Laken malaika akamwambia, Usiogope, Zakariya,
 kwani kuomba kwako kunasikiwa, na mke wako Elisa-
 beti atakuvyalia mwana mume, na jina lakwe utamwita
 14 Yohana. Utakuwa na furaha na nderemo, na watu
 15 wangi watafurahiwa kwa kuvyawa kwakwe. Kwani
 atakuwa mkuu mbele ya Bwana, hatakunwa vinyu wala
 kileo kingine; naye atajazwa na Roho Takatifu tangu
 16 matumboni mwa mamaye. Na wangi katika waana wa
 Israeli atawarejeza kwa Bwana Muungu wao.
- 17 Naye atamtangulia kwa roho na nguvu za Eliya,
 kurejeza mioyo ya baba kwa waana wao, na wale wasio-

sikia kwa akili za watu wapendao haki; kuweka watu tayari kwa Bwana.

Zakariya akamwambia malaika, Talitambua kwa nini 18 jambo hili? kwani mimi ni mzee, na mke wangu naye amekwenda mbele kwa siku zakwe.

Malaika akamjibu, akimwambia, Mimi ni Gabrieli 19 asimamaye mbele za Muungu, nami nalitumwa kusema nawe, na kukuambia habari hii ngema. Basi angalia, 20 utakuwa bubu, usiweze kusema, hata siku yatakapotokea mambo haya; kwani wewe hukuamini maneno yangu, yatakayotimizwa kwa majira yao.

Na watu walikuwa wakimngoja Zakariya, wakataa- 21 jabu kwa kukawa kwakwe mle hekaluni.

Basi alipotoka hakuweza kusema nao: wakatambua 22 kwamba alitokewa ni neno mle hekaluni: naye mwenyewe aliwapungia mkono akikaa bubu. Ikawa siku za matu- 23 mishi yakwe zilipotimizwa, akaondoka kurudi nyumbani mwakwe. Basi akhiri ya siku hizo, mkewe Elisabeti 24 alipata mimba, akajifita miezi mitano, akinena, Ndivyo 25 Bwana alivyonyifanyia katika siku za kunitazama, kuni-ondolea aibu yangu katika watu.

Na mwezi wa sita malaika Gabrieli alitumwa ni Mu- 26 ungu, kwenda mji wa Galilaya, jina lakwe Nazareti, kwa 27 mwanamwali aliyekuwa akiozwa mume, jina lakwe Yusuf, wa nyumba ya Daudi; na jina la mwanamwali alii-
twa Maryamu. Na malaika alipoingia kwakwe aka- 28 nena, Salama i kwako uliyepata neema, Bwana yu pamoja nawe: umebarikiwa wewe katika watu wake.

Naye alipomwona, akakutuka kwa maneno yakwe, 29 akaaza ni salamu gani hiyo. Malaika akamwambia, 30 Usiogope Maryamu, kwani umepata neema kwa Muungu. Angalia, utapata mimba, utavyaa mwana mume, utaita 31 jina lakwe ISA. Huyu atakuwa mkuu, ataitwa mwana 32 wa aliye juu, na Bwana Muungu atampa kiti cha Daudi babaye; atamiliki nyumba ya Yakobo dayima, na ufa- 33 lme wakwe hautakuwa na mwisho.

Maryamu akamwambia malaika, Litakuwaje neno hili, 34 mbona simtambui mume? Malaika akamjibu, akimwa- 35 mbia, Roho Takatifu itakujia, na nguvu za aliye juu zita-
kukalia kama uvuli: ndipo napo kivyaliwacho kitakatifu kiitwe Mwana wa Muungu. Basi angalia Elisabeti 36 mbari yako, naye ana mimba ya mwana mume kwa

uzee wakwe, na mwezi huu ni wa sita kwakwe aliyea-
37 mbiwa ni tasa. Kwani kwa Muungu hapana neno asi-
loweza.

38 Maryamu akanena, Angalia, mimi ni mjakazi wa
Bwana, na liwe kwangu neno lako uliloniambia. Ma-
laika akatoka kwakwe.

39 Basi siku hizo Maryamu akaondoka, akaenenda mbio
40 milimani, katika mji wa Yuda, akaingia nyumbani
41 mwa Zakariya, akamwamkua Elisabeti. Ikawa, Elisa-
beti akisikia salamu ya Maryamu, mtoto akaruka matu-
mboni mwakwe, na Elisabeti akajazwa Roho Takatifu,
42 akaita kwa sauti kuu, akanena, Unabarikiwa wewe ka-
tika wake, linabarikiwa nalo tunda la matumbo yako.
43 Na jambo hili kwangu latokapi, mamaye Bwana wangu
44 kuja kwangu? Tazama, sauti ya salamu yako ilipoi-
ngia mashikioni mwangu, mtoto aliruka matumboni
45 mwangu kwa furaha. Na heri ina wewe uliyeamini,
kwani yatatimizwa maneno yale uliyoambiwa ni Bwana.

46 Maryamu akanena, Moyo wangu unamkuza Bwana,
47 na roho yangu inafurahiwa kwa Muungu Mwokozi
48 wangu. Kwani akajali udogo wa mjakazi wakwe; anga-
49 lia tangu sasa vivyazi vyote vitaniita mbarikiwa. Kwani
yeye mwinyi nguvu alinifanyia mambo makuu, na jina
50 lakwe li takatifu. Na rehema zakwe ziko, tangu
51 kivyazi hata kivyazi, kwa wale wamchao. Akafanya
nguvu kwa mkono wakwe, akatawanya watu walio na
52 kiburi kwa mawazo ya mioyo yao. Akashusha wenyi
53 nguvu vitini mwao, akawakweza wanyonge. Wenyi
ndaa akawajaza na vitu vyema, na wenyi mali akawa-
54 ondoa watupu. Akamsayidia Israeli mtu wakwe, aki-
55 kumbuka rehema zakwe, kama alivyonena na babu zetu,
kwa Ibrahimu na mbeyu yakwe siku zote.

56 Na Maryamu alikaa kwakwe kadiri ya miezi mitatu,
akarudi nyumbani mwakwe.

57 Basi Elisabeti akatimiziwa majira yakwe ya kuvyaa,
58 akavyaa mwana mume. Na jirani na mbari zakwe wa-
kasikia kwamba Bwana akamkuzia rehema zakwe, wa-
kafurahiwa pamoja naye.

59 Ikawa, siku ya nane, wakaja kumtahiri mwana, waka-
60 mwita jina la babaye, Zakariya. Basi mamaye akajibu
61 akanena, Sivyo, ataitwa Yohana. Wakamwambia, Ha-
62 pana mtu katika mbari zako aliyeitwa jina hilo. Wa-

kampungia babaye mikono, kwamba wajue yuataka aitwe jina gani. Akataka ubao wa kuandikia, aka- 63 andika, akinena, Jina lakwe ni Yohana. Wakataajabu wote.

Likafunguliwa kanwa lakwe, na ulimi wakwe tháruba 64 hiyo, akanena akimshukuru Muungu. Na hofu ikaingia 65 wote waliokaa kandokando yao; na maneno haya yote yakasemwa katika mlima wote wa Uyahudi; na wote 66 waliosikia wakayaweka mioyoni mwao, wakisema, Mwanahuyu atakuwa mwana gani? Na mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye.

Na Zakariya babaye akajazwa na Roho Takatifu, aka- 67 tabiri, akinena, Ahimidiwe Bwana Muungu wa Israeli; 68 kwani akatazama, akakomboa watu wakwe. Akatusi- 69 mikia pembe ya wokovu, katika nyumba ya Daudi mtu wakwe; kama alivyosema kwa kanwa la manabii 70 wakwe watakatifu tangu zamani. Wokovu wa kutoka 71 kwa adui zetu, na mkononi mwa watu wote watuzirao. Kutimiza rehema alizoagana na babuzetu, na kukumbuka 72 ahadi yakwe takatifu, kiapo alichomwapia Ibrahimu babu 73 yetu, kutujalia swiswi, kwamba tutolewe mkononi mwa 74 adui zetu, tukamtumikie yeye, tusipokuwa na hofu, kwa 75 utakatifu na haki mbele zakwe, siku zote za maisha yetu.

Na wewe, mwana, utaitwa nabii wa aliye juu; kwani 76 utatangulia mbele ya uso wa Bwana, kuweka tayari ndia zakwe; kuwapa watu wakwe maarifa ya wokovu katika 77 msamaha wa thambi zao, kwa rehema nyororo za Mu- 78 ungu wetu, kwazo kwamba alfajiri ikatoka, ikatutazama kwa juu, kuwapa mwanga wale wakaao kizani na uvulini 79 mwa mauti, na kulekeza maguu yetu katika ndia ya salama. Na huyo mwana akakua akafanya nguvu katika 80 roho, akakaa barani, hata siku ya kutokea kwakwe kwa watu Waisraeli.

IKAWA siku zile, amuri ikatoka kwa Kaisari Au- 2 gusto, kwamba ulimwengu wote uandikwe. Na andiko hili ndilo la kwanza lililokuwako Kirenio asipotasa kuwa wali wa Shami. Na watu wote wakaenenda 3 kuandikwa, kulla mmoja mjini mwakwe.

Na Yusuf naye akatoka Nazareti, mji wa Galilaya, aka- 4 kwea nti ya Uyahudi, kuenenda mji wa Daudi, uitwao Betlehem, kwani alikuwa mtu wa nyumba na kivyazi

- 5 cha Daudi, kwamba aandikwe pamoja na Maryamu aliye-
kuwa akiozwa kuwa mkewe, aliyekuwa na mimba.
- 6 Basi ikawa wakikaa kule, siku zakwe za kuvyaa zika-
7 timizwa; akavyaa mwana wakwe wa kwanza, akamtia
ndani ya vitambaa, aka'mweka horini, kwani hawakuwa
na pahali katika nyumba ya wageni.
- 8 Na watunga walikuwako nti ile, waliokaa barani, wa-
kilinda kundi lao kwa zamu, majira ya usiku.
- 9 Basi angalia, malaika ya Bwana akawajia, na enzi
ya Bwana ikawazungukia kwa nuru: wakacha kicho
10 kikubwa. Malaika akawaambia, Msifanye hofu: basi
angaliani, nawaletea nwinwi habari ngema ya furaha kuu,
11 itakayofika kwa watu wote; kwani mnavyaliwa Mwo-
kozi leo, ndiye Masiya Bwana, katika mji wa Daudi.
- 12 Na alama yenu ni hii; mtamwona mtoto aliyetiwa
13 ndani ya vitambaa, aliyelazwa horini. Na tháruba hiyo
unakuwapo pamoja na malaika yule ungi wa jeshi la
14 mbinguni, wakimhimidi Muungu, wakinena, Enzi ni
ya Muungu kwa juu, na salama kwa nti, na nderemo
15 kwa watu. Ikawa, malaika walipoepukana nao wakenda
mbinguni, watu wale watunga wakaambiana, Na tuende
hata Betlehem, tukaangalie neno hili lililokuwa, Bwana
alilotuhubiri.
- 16 Wakaja mbio, wakamwona Maryamu na Yusuf, na
17 mtoto aliyelazwa horini. Walipoona wakalieneza neno
18 lile waliloambiwa kwa mwana huyu. Na watu wote wa-
liosikia wakataajabu kwa hayo yaliyosemwa kwao ni wa-
19 tunga. Ela Maryamu akatunza maneno haya yote, aki-
20 yafikiri moyoni mwakwe. Na watunga wakarudi wa-
kimhimidi wakimsifu Muungu kwa mambo yote wali-
yosikia, waliyoona, kama walivyoambiwa.
- 21 Na siku nane zilipotimizwa za mwana kutahiriwa,
jina lakwe likaitwa ISA, lile lilioitwa ni malaika asitasa
kupatiwa mimba.
- 22 Na siku za tohara yao zilipotimizwa, kwa sheria ya
Musa, wakamleta Yerusalemini, ku'mweka kwa Bwana,
23 kama ilivyoandikwa katika sheria ya Bwana, Kulla kiume
kifunguacho matumbo ya mama kiitwe kitakatifu kwa
24 Bwana; na kwamba watoe sadaka, kama ilivyonenwa
katika sheria ya Bwana, ndiwa manga wawili, au ma-
kinda mawili ya ndiwa manga.
- 25 Basi angalia, kulikuwa na mtu Yerusalemini, jina

lakwe Simeon, na mtu huyo alikuwa salihi, akimecha Mwenyiezi Muungu, akilinda utulivu wa Israeli, na Roho Takatifu yalikuwa juu yakwe. Naye alikuwa 26 akihubiriwa ni Roho Takatifu, kwamba hataona mauti asipotasa kumwona kwanza Masiya wa Bwana.

Akaja hekaluni kwa Roho hiyo; basi mamaye na 27 babaye walipomleta mtoto Isa, kwamba wamfanyie kama ilivyokuwa ada ya sheria, yeye akampakata miko- 28 noni mwakwe, akamhimidi Muungu, akanena, Ewe 29 Bwana, sasa wamwaga mtumishi wako kwa salama, kama ulivyonena. Kwani mato yangu yanaona wokovu 30 wako, ulioweka tayari usoni mwa watu wote; mwanga wa ³¹/₃₂ kuwafunukia mataifa, na enzi ya watu wako Waisraeli.

Yusuf na mamaye wakataajabu kwa hayo yaliyo- 33 nenwa kwa ajili yakwe. Na Simeon akawabariki, 34 akamwambia Maryamu mamaye, Angalia, huyu ana-wekwa, watu wangi waanguke na wangi wasimame katika Waisraeli, awe alama ishindaniwayo. Nawe nafsi yako 35 upanga utakuvingia moyoni mwako, kwamba mawazo ya mioyo mingi yafunuliwe.

Kulikuwa na Hana nabii mke, mwana wa Fanueli, wa 36 kabila ya Asher, naye alikuwa na maisha mangi, na tangu alipokuwa mwana mwali alikuwa na mume miaka sabaa. Naye ni mjaani, wa kadiri ya miaka arba wa 37 thamanini, asiyeondoka hekaluni, akimwabudu Muungu kwa kufunga na kusali usiku na mtana. Akakurubia 38 naye saa ileile akamshukuru Bwana, akamsema kwa wote waliokuwa wakingojea ukombozi katika Yerusalem.

Basi walipotimiza mambo yote yaliyowapasa kwa 39 sheria ya Bwana, wakarudi Galilaya, mjini mwao Nazareti.

Na yule mtoto alikua alifanya nguvu katika roho, 40 akiwa akijazwa akili ngema, na neema ya Muungu ilikuwa juu yakwe.

Na kulla mwaka mamaye na babaye walikuwa wake- 41 nenda Yerusalemini, ikiwa siku kuu ya Pasaka. Basi 42 alipotimiza miaka kumi na miwili, akakwea nao Yerusalemini kama ilivyokuwa ada ya siku kuu, na siku zao 43 zilipokoma hatta wakirudi, yeye mwana Isa akakaa nyuma katika Yerusalem, babaye na mamaye wasipojua; wakihesabu kwamba yu pamoja na jamaa zao, wakenda 44 mwendo wa siku moja, wakamtafuta katika mbari zao na

- 45 wenzi wao, wasimwone: wakarudi Yerusalemini kumwenza.
- 46 Ikawa baada ya siku tatu, wakamwona hekaluni, aki-
47 keti katikati ya waalimu, akiwasikiza akiwauliza. Wakataajabu mno wote waliomsikia kwa akili zakwe na
48 kujibu kwakwe. Basi walipomwona wakakutuka, na mamaye akamwambia, Mwana, ukatufanyiani hivi? angalia, babayo na mimi tukakutafuta kwa uchungu.
- 49 Akawaambia, Kwani kunitafuta? hamkujua kwamba
50 yanipasa kuwa katika haya ya baba yangu? Nao hawakufahamu neno hili alilosema nao.
- 51 Akashuka nao, akaja Nazareti, akajiweka tini mwao. Na mamaye akaweka maneno haya yote moyoni mwakwe.
- 52 Na Isa aliongea kwa akili ngema na kwa maisha, na neema kwa Muungu na kwa watu.
- 3** KATIKA mwaka wa kumi na tano wa miliki ya Kaisari Tiberio, Pontio Pilato alipokuwa wali wa Uyahudi, na Herode alipokuwa mfalme wa Galilaya, na nduguye Filipo alipokuwa mfalme wa Iturea na wa nti ya Trakoniti, na Lisania alipokuwa mfalme wa Abilene,
2 na Hana na Kayafa walipokuwa wakohani wakuu, neno la Muungu likaja kwa Yohana mwana wa Zakariya, kule barani.
- 3 Akaja kandokando zote za Yardeni, akihubiri ubatizo
4 wa kujuta na kusamehewa thambi; kama ilivyoadnikwa chuoni mwa maneno ya Isaya nabii, akinena, Kuna sauti ya mtu ahubiriye barani, Fanyani tayari
5 ndia ya Bwana, nyoshani mikondo yakwe. Kulla bopo lijazwe, na kulla mlima na kilima vishushwe, na kitu kilicho kombo kinyoshwe, na ndia zenzi mashimo ziwe
6 sawasawa. Na viumbe vyote vione wokovu wa Muungu.
- 7 Akawaambia makundi waliotoka 'nde kwamba wabatizwe ni yeye, Enwi kivyazi cha nyoka, n'nani aliye-
8 waonyesha kukimbia ghatibu zitakazokuja? Kwa sababu hiyo leteni matunda yawapashayo kujuta, wala msiazimie kunena ndani mwenu, Kuliko baba wetu ni Ibrahimu: kwani mimi nawaambia, kwamba Muungu aweza kufufia haya mawe yawe waana wa Ibrahimu.
- 9 Na shoka linakwisha wekwa mashinani mwa miti, na kulla mti usiofanya tunda ngema ukakatwa ukatiwa motoni.
- 10 Makundi wakamuliza, wakinena, Tufanyeni sasa?

Akawajibu akiwaambia, Aliye na kanzu mbili atoe moja 11
 akampe mwenziwe asiye nayo; na aliye na vyakula,
 afanye vivyo. Watozi wa ushuru nao wakaja kubatizwa, 12
 wakamwambia, Mkufunzi, tufanyeni? Akawaambia, 13
 msitoze zayidi illa iliyowapasa baki yenu. Wakamuliza 14
 nao askari, wakinena, Naswi tufanyeni? Akawaambia,
 Msimfanyie mtu nguvu, wala msimthilimu mtu; 'mwe
 rathi kwa mshahara wenu.

Basi watu wote wakiwa wakitaraji, wakiaza mioyoni 15
 mwao kwa hali ya Yohana, kwamba ndiye hana budi
 kuwa Masiya; Yohana akajibu wote, akiwaambia, Mimi 16
 kwa kweli nawabatiza kwa maji, laken yuaja mwinyi
 nguvu zayidi ya mimi, ambaye kwamba simtoshi kum-
 fungulia ukanda wa viatu vyakwe: yeye atawabatiza
 nwinwi kwa Roho Takatifu na kwa moto. Mkononi 17
 mwakwe kuna mwiko wa kutupia nafaka, atafiagia
 kiwanda chakwe, atakusanya nganu boharini mwakwe,
 na mapepe atayateketeza kwa moto usiozimika. Na 18
 maneno mangi mangine akawaonya, akawaeleza watu.

Laken mfalme Herode akipatilizwa ni yeye kwa ajili 19
 ya Herodiade mke wa nduguye, na kwa maovu yote
 Herode aliyofanya, tena juu ya yote akaongeza na hili, 20
 kumfunga Yohana gerezani.

Ikawa, watu wote wakibatizwa, na Isa naye akibatizwa, 21
 na akisali, mbingu zikafunguka, na Roho Takatifu ika- 22
 shuka juu yakwe kwa sura ya mwili kama ndiwa manga,
 na sauti ikatoka mbinguni, ikinena, Ndiwe mwanangu,
 kipendo changu; kwako ninapendezewa.

Na mwenyewe Isa alikuwa anaingia mwaka wa tha- 23
 lathini, akiwa, kama alivyohesabiwa, mwana wa Yusuf
 aliyekuwa mwana wa Eli, aliyekuwa mwana wa Matati, 24
 aliyekuwa mwana wa Lawi, aliyekuwa mwana wa Melki,
 aliyekuwa mwana wa Jana, aliyekuwa mwana wa Yusuf,
 aliyekuwa mwana wa Matatia, aliyekuwa mwana wa 25
 Amos, aliyekuwa mwana wa Nahum, aliyekuwa mwana
 wa Esli, aliyekuwa mwana wa Nage, aliyekuwa mwana 26
 wa Maathi, aliyekuwa mwana wa Matatias, aliyekuwa
 mwana wa Simeji, aliyekuwa mwana wa Yusuf, aliye-
 kuwa mwana wa Yuda, aliyekuwa mwana wa Yohana, 27
 aliyekuwa mwana wa Resa, aliyekuwa mwana wa Zoro-
 babel, aliyekuwa mwana wa Salathiel, aliyekuwa mwana
 wa Neri, aliyekuwa mwana wa Melki, aliyekuwa mwana 28

wa Adi, aliyekuwa mwana wa Kosam, aliyekuwa mwana
 29 wa Elmodam, aliyekuwa mwana wa Eri, aliyekuwa
 mwana wa Yose, aliyekuwa mwana wa Eliezer, aliyekuwa
 mwana wa Jorim, aliyekuwa mwana wa Matati, aliye-
 30 kuwa mwana wa Lawi, aliyekuwa mwana wa Simeon,
 aliyekuwa mwana wa Yuda, aliyekuwa mwana wa Yusuf,
 aliyekuwa mwana wa Jonan, aliyekuwa mwana wa
 31 Eliakim, aliyekuwa mwana wa Melea, aliyekuwa mwana
 wa Mainan, aliyekuwa mwana wa Matatha, aliyekuwa
 32 mwana wa Nathan, aliyekuwa mwana wa Daudi, aliye-
 kuwa mwana wa Yese, aliyekuwa mwana wa Obedi,
 aliyekuwa mwana wa Boas, aliyekuwa mwana wa Salmon,
 33 aliyekuwa mwana wa Nahason, aliyekuwa mwana wa
 Aminadab, aliyekuwa mwana wa Aram, aliyekuwa
 mwana wa Esrom, aliyekuwa mwana wa Fares, aliye-
 34 kuwa mwana wa Yuda, aliyekuwa mwana wa Yakob,
 aliyekuwa mwana wa Isaak, aliyekuwa mwana wa Ibra-
 himu, aliyekuwa mwana wa Tara, aliyekuwa mwana wa
 35 Nahor, aliyekuwa mwana wa Saruhu, aliyekuwa mwana
 wa Ragau, aliyekuwa mwana wa Faleg, aliyekuwa
 36 mwana wa Eber, aliyekuwa mwana wa Sala, aliyekuwa
 mwana wa Kainan, aliyekuwa mwana wa Arfakhasad,
 aliyekuwa mwana wa Sem, aliyekuwa mwana wa Nuhu,
 37 aliyekuwa mwana wa Lamekh, aliyekuwa mwana wa
 Metusala, aliyekuwa mwana wa Enokh, aliyekuwa mwana
 wa Jaredi, aliyekuwa mwana wa Maleleel, aliyekuwa
 38 mwana wa Kainan, aliyekuwa mwana wa Enos, aliye-
 kuwa mwana wa Seti, aliyekuwa mwana wa Adam, aliye-
 kuwa wa Muungu.

4 BASI Isa alikuwa akijaa Roho Takatifu, akarudi
 2 kutoka Yardeni, akaongozwa barani kwa Roho hiyo siku
 arbaini, akajaribiwa ni Shetani; naye hakula kitu siku
 3 hizo, nazo zilipotimia, baada yakwe akaona ndaa. She-
 tani akamwambia, Ukiwa mwana wa Muungu, liambie
 4 jive hili, liwe mkate. Isa akamjibu, akinena, Yanaa-
 ndikwa, kwamba mtu haishi kwa mkate tu, illa kwa
 neno la Muungu liwalo lote.

5 Shetani akampeleka juu ya mlima mrefu, akamwo-
 nyeza miliki zote za ulimwengu, kwa ukope wa juu kuja
 6 tini. Shetani akamwambia, Mamlaka haya yote na enzi
 yakwe 'ntakupa, kwani 'nnapawa mimi, nami nampa
 7 nimitakaye; basi ukinisujudia mimi, yote itakuwa yako.

Isa akamjibu, akanena, Enenda nyuma yangu, Shetani: 8
yanaandikwa, Msujudie Bwana Muungu wako, mtumikie
yeye peke yakwe.

Akampeleka Yerusalemini, akamtia juu ya kileleta 9
cha hekalu, akamwambia, Ukiwa Mwana wa Muungu,
ujitupe tini kwa papahapa. Kwani yameandikwa, 10
Kwamba ataamuru malaika wakwe kwa ajili yako,
kwamba wakukinge, mwakutukue mikononi mwao, 11
kwamba usikungwae guu lako na jiwe. Isa akajibu, 12
akamwambia, Yanenwa, Usimjaribu Bwana Muungu
wako. Na shetani alipomaliza majaribu yote, akaondoka 13
kwakwe wakati huo.

Na Isa akarudi kwa nguvu zile za Roho, akaja Gali- 14
laya, na sifa yakwe ikatoka ikienea nti zote za kando-
kando. Akafunza katika makutano yao, akisifiwa ni 15
watu wote. Akaja Nazareti, alipolewa, na siku ya 16
sabato akaingia sunagoge kama ilivyokuwa ada yakwe,
akasimama kusoma. Akapawa chuo cha nabii Isaya; 17
basi alipokifunua chuo hicho, akaona pahali palipoandi-
kwa, Roho ya Bwana ni juu yangu, kwani akanipaka, 18
kuwahubiri masikini maneno ya anjili, akanituma kupoza
watu waliopondeka mioyo, na kuhubiri watu walio-
fungwa msamaha wao, na watofu wa mato kwamba
wafumbuke waone, kuwaata huru hao waliokuwa wana-
finyangwa; kuhubiri mwaka wa neema wa Bwana. 19
Akafinika chuo, akampa mtumishi, akaketi; na mato ya 20
watu wote waliokuwa katika sunagoge yakamlekea
yeye. Akaanza kuwaambia, Leo maandiko haya yana- 21
timizwa mashikioni mwenu. Na wote wakamshuhudia, 22
wakataajabu kwa maneno ya neema yaliyotoka kanwani
mwakwe, wakanena, Huyu si mwana wa Yusuf? Naye 23
akawaambia, Kwa kweli mtaniambia methali hii, Tabibu,
ujiague nafsi yako; yale tuliyosikia yanatendwa katika
Kapernaum, utende na hapa mjini mwako.

Akanena, Kwa kweli nawaambia nwinwi, hapana 24
nabii aliyetakabaliwa mjini mwakwe. Laken nawaa- 25
mbia kwa kweli, walikuwako wajaani wangi katika
Waisraeli kwa wakati wa Eliya, mbingu zilipokuwa
zikifungwa miaka mitatu na miezi sita, ilipokuwa ndaa
kuu katika nti yote; laken Eliya hakutumwa kwa 26
mmoja wao, ila kwa mtu mke mjaani wa Sarepta, mji
wa Sidoni. Na watu wangi wenyi ukoma walikuwako 27

katika Waisraeli kwa wakati wa Elisha nabii, asitakaswe
 28 mmoja wao, ila Naaman mtu wa Sham. Wakajawa ni
 hasira wote waliokuwa sunagogeni, wakisikia maneno
 29 haya. Wakasimama wakamsukuma kumtoa mjini
 mwao, wakampeleka hata gengeni mwa kilima palipoje-
 30 ngwa mji wao, kwamba wamtupe tini; laken yeye alipita
 katikati yao akenda zakwe.

31 Akatelemuka Kapernaum, mji wa Galilaya, akawa-
 32 funza kwa siku za sabato. Wakataajabu mno kwa
 kufunza kwakwe, kwani neno lakwe lilikuwa na nguvu.

33 Basi katika sunagoge kulikuwa na mtu, aliyekuwa
 na roho ya jinni mkoo, naye alipiga kelele kwa sauti
 34 kuu, akinena, Utuate; tunani nawe, Isa wa Nazareti?
 Unakuja kutuharibu? Nakujua kwamba ndiwe Mtaka-
 35 tifu wa Muungu. Isa akamkaripia, akinena, Nyamaa;
 toka ndani mwakwe. Jinni akamtupa katikati, akamto-
 36 ka asipomhasiri. Kiwewe kikawajia wote, wakaambiana
 wao kwa wao, wakinena, Nini neno hili? hakikaye kwa
 mamlaka na kwa nguvu aamuru roho zenyi taka, nazo
 37 zatoka. Na mshindo wakwe ukatoka ukaenea kulla
 pahali pa nti za kandokando.

38 Akaondoka sunagogeni, akaingia nyumba ya Siman.
 Basi mkwewe Siman alikuwa anashikwa ni homa kubwa,
 39 wakamwomba kwa ajili yakwe. Akamwinamia akakaripia
 ile homa, ikimwata; akaondoka tháruba'hiyo, akawatumi-
 40 kia. Na jua likiwa likitwa, watu wote waliokuwa na wago-
 njwa wa marathi mbalimbali wakawaleta kwakwe; naye
 kulla mmoja wao, aka'mwekea mikono juu yakwe aka-
 41 wapoza. Na majinni nayo yakawatoka watu wangi,
 yakilia na yakinena, Ndiwe Masiya, Mwana wa Mu-
 ungu; naye akawakaripia, asiwaliche kunena: kwani
 42 walimjua kwamba ndiye Masiya. Basi mtana ulipoku-
 wako, akatoka akaenenda pahali barani; makundi waka-
 mtafuta, wakaja hata kwakwe, wakamzuia kwamba asi-
 43 waondokee. Laken yeye akawaambia, Yanipasa kuhu-
 biri anjili ya ufalme wa Muungu miji mingine nayo,
 44 kwani ndilo neno nililotumwa. Basi akawa akihubiri
 katika masunagoge ya Galilaya.

5 IKAWA makundi wakimsonga kusikiza maneno
 ya Muungu, naye akisimama kandokando ya ziwa la
 2 Genesareti, akaona madau mawili yaliyokuwa kando-
 kando ya ziwa; laken wavuvi walikuwa wanatoka

kuosha nyavu zao. Akaingia dau moja, lililokuwa la 3
 Siman, akamtaka kuliepua kidogo na pwani, akaketi
 akafunza makundi ndani ya dau.

Basi alipokoma kunena, akamwambia Siman, Songea 4
 kinani mkatie nyavu zenu, mkavue. Siman akamjibu 5
 akamwambia, Bwana, tulisumbuka usiku kucha, tusipate
 kitu : laken kwa neno lako 'ntatia nyavu. Basi walipo- 6
 fanya hivi, wakashika ungi wa samaki wangi; nyavu
 zao zikiwa zikitaruka. Wakapungia mikono wenzi wao 7
 waliokuwa katika dau jingine, kuja kuwasayidia; nao
 wakaja, wakajaza madau yote mawili hata yakizama.
 Siman Petro alipoona, akaangukia magotini mwa Isa, 8
 akinena, Bwana, toka kwangu, kwani mimi ni mtu
 mkosa. Hakikaye kiwewe kilikuwa kinamshika yeye 9
 na wote waliokuwa pamoja naye, kwa hawa samaki
 waliopata. Na Yakobo vivyo, na Yohana, waana wa 10
 Zebedayo, waliokuwa washiriki pamoja na Siman. Isa
 akamwambia Siman, Usifanye hofu; tangu sasa utavua
 watu. Wakaleta madau pwani, wakaata pia, waka- 11
 mfuata yeye.

Ikawa alipokuwa katika mmoja wa miji ile, angalia, 12
 mtu aliyejaa ukoma : naye alipomwona Isa, akaanguka
 kwa uso wakwe, akamwomba, akinena, Bwana, ukitaka
 waweza kunitakasa. Akanyosha mkono akamgusa, 13
 akinena, Nataka; utakate. Na tháruba hiyo ukoma
 ukamtoka. Akamsisitiza kwamba asimwambie mtu; 14
 laken Uenende ukajionyeshe kwa mkohani, ukapeleke
 sadaka za kutakata kwako, kama Musa alivyoamuru,
 iwe ushuhuda kwao. Laken habari yakwe ikazidi 15
 kuenea, na makundi mengi wakakutana kumsikiza na
 kupozwa magonjwa yao. Laken mwenyewe alikuwa 16
 akijitenga barani, akisali.

Ikawa siku moja hizo, akiwa akifunza, na Mafarisayo 17
 na waalimu wa sheria walikuwako wanaketi, nao wali-
 kuwa wanatoka kulla mji wa Galilaya, na Uyahudi, na
 Yerusalem. Na nguvu za Bwana zilikuwako kupoza
 watu. Angalia, watu wamtukua mtu kitandani, aliye- 18
 kuwa ana katika viungo, wakitaka pahali pa kumpe-
 nyeza na kumweka mbele yakwe, wasipaone pakumpe- 19
 nyezea, kwa makundi kuwa mengi; wakakwea juu ya
 dari, wakafumua matufali, wakampuliza pamoja na
 kitanda katikati mbele ya Isa.

20 Naye alipoona imani yao, akamwambia, Mtu wewe
 21 usamehewe thambi zako. Basi wale waana vyuoni na
 Mafarisayo wakaanza kutafakari, wakinena, 'Nnani
 huyu asemaye kufuru? 'Nnani awezaye kusamehe
 22 thambi, isipokuwa Muungu pekeye? Isa akatambua
 mawazo yao, akajibu akawaambia, Mwawaza nini mio-
 23 yoni mwenu? Kilicho rahisi ni kunena, Usamehewe
 24 thambi zako, ima kunena, Simama uenende? Basi
 kwamba mjue, kwamba Mwana wa mtu yuna mamlaka
 katika ulimwengu kusamehe thambi, akamwambia
 yeye aliye katika viungo, Simama, ushike kitanda
 25 chako, enenda nyumbani mwako. Na tháruba hiyo aka-
 simama mbele zao, akashika kile alicholalia, akatoka
 26 kuenda nyumbani mwakwe, akimsifu Muungu. Wa-
 katokwa ni roho wote, wakamsifu Muungu, wakajawa
 ni hofu, wakinena, Tunaona miujiza leo.

27 Na akhiri ya haya akatoka, akaona mtozi wa ushuru,
 jina lakwe Lawi, akiketi forthani, akamwambia, Uni-
 28 fuate mimi. Akaata kulla kitu, akaondoka, akam-
 29 fuata. Na Lawi akamfanyia karamu kuu nyumbani
 mwakwe, na watozi wa ushuru wangi na watu wangine
 30 walikuwa wakiketi chakulani pamoja nao. Basi Ma-
 farisayo na waana vyuoni wao wakawaguna waanafunzi
 wakwe, wakinena, Kwani kula na kunwa pamoja na
 31 watozi wa ushuru na watu wenyi thambi? Isa akajibu
 akawaambia, Si watu wazima wamtakao tabibu, laken
 32 wagonjwa. Nami sikuja kuita watu wema, laken wale
 wabaya kujuta.

33 Nao wakamwambia, Waanafunzi wa Yohana wafunga
 mara nyingi, na wasali sala, na waanafunzi wa Mafari-
 34 sayo ni vivyo, laken wako wala wanwa. Akawaambia,
 Mwaweza kuwaambia watu walio na arusi, Fungani,
 35 yule mwinyi kuo a akiwa pamoja nao? Laken siku zita-
 kuja, mwinyi kuo a atakapoondolewa kwao, basi ndipo
 watakapofunga siku zile.

36 Akawaambia na fumbo, Kwamba hapana mtu atiaye
 kitambaa cha nguo mpya juu ya nguo kukuu; akitia,
 kile kipya nacho chararua, na kitambaa cha nguo mpya
 37 hakilingani na ile kukuu. Wala hapana mtu atiaye
 vinyu mpya katika viriba vikukuu; akitia, vinyu mpya
 itararua vile viriba, na vinyu itamwaika, na viriba vita-
 38 haribika. Laken vinyu mpya ni kutiwa katika viriba

vipya, basi vyote viili vitakaa vizima. Na mtu aliye- 39
kunwa vinyu ya kale, hana haraka ya kutaka mpya ;
kwani anena, Ya kale ni heri.

IKAWA, kwa siku ya sabato ya pili, akipita katika 6
mashamba ya nganu, waanafunzi wakwe wakaburura
mashuke wakala, wakifikicha kwa mikono. Basi Mafa- 2
risayo wangineo wakawaambia, Kwani kufanya jambo
lisilokuwa halali kwa siku za sabato? Isa akajibu, aka- 3
waambia, Hata neno hili hamkusoma, Daudi alilotenda,
alipokuwa na ndaa, yeye na wale waliokuwa pamoja
naye? Kwamba akaingia nyumbani mwa Muungu, 4
akitwaa mikate ya uso, akala akawapa na wale wenziwe,
nayo si halali kula ila kwa wakohani peke yao? Aka- 5
waambia, kwamba Mwana wa mtu ni Bwana hata wa
siku ya sabato.

Ikawa, kwa sabato nyingine nayo akiingia sunagoge 6
akifunza; alikuwako mtu, mkono wakwe wa kulia uli-
kuwa unapooza. Basi waanavyuoni na Mafarisayo wa- 7
kamtunduia kwamba ataagua mtu siku ya sabato, kusudi
wapate sababu kwakwe ya kumstaki. Laken yeye aka- 8
tambua mawazo yao, akamwambia yule mtu aliyekuwa
na mkono uliopooza, Ondoka, ukasimame katikati.
Akaondoka, akasimama. Isa akawaambia, Nawauliza 9
nwinwi, kipashacho kwa siku za sabato ni kufanya
vyema au kufanya vibaya? kuponya roho au kuianga-
miza? Akazunguka, akawaangalia watu wote, aka- 10
mwambia yule mtu, Nyosha mkono wako. Akaunyo-
sha; mkono wakwe ukarejezwa mzima kama ule wa
pili. Wakajawa ni wazimu, wakasemezana wao kwa 11
wao neno wawezalo kumtenda Isa.

Ikawa siku hizo, akatoka akenda juu ya mlima ku- 12
sali, akikeshwa usiku kucha kwa kumwomba Muungu.
Basi mtana ulipokuwako, akaita waanafunzi wakwe, 13
akatagua watu kumi na wawili, ambao kwamba aliwapa
na jina la wajumbe; Siman ambaye alimwita na Petro, 14
na Andrea nduguye, Yakobo na Yohana, Filipino na Bar-
tolomayo, Matayo na Tomasi, Yakobo mwana wa Alfayo, 15
na Siman aliyelitwa na Zelote, Yuda wa Yakobo na Yuda 16
Iskariota, aliyekuenda msema. Akashuka pamoja nao, 17
akasimama mahali kitelele, na kundi la waanafunzi
wakwe na ungi wa watu, waliotoka nti yote ya Uyahudi
na Yerusalem, na pwani ya Turo na Sidon, waliokuja

18 kumsikiza na kupozwa marathi yao ; na wao waliosu-
 19 mbuliwa ni roho zenzi ukoo ; nao wakapozwa. Na kundi
 lote walitaka kumgusa, kwani nguvu zilitoka kwakwe,
 20 nazo ziliwapoza wote. Akawainulia mato waanafunzi
 wakwe, akanena,

Mnabarikiwa nwinwi maskini, kwani ufalme wa Mu-
 ungu ni wenu.

21 Mnabarikiwa nwinwi mlio na ndaa sasa, kwani mta-
 shibishwa.

Mnabarikiwa nwinwi mliao sasa, kwani mtateka.

22 Mnabarikiwa, watu wakiwazira nwinwi, wakiwaepusha
 nwinwi, wakiwafiolea nwinwi, wakitupa jina lenu kama
 haya, kwa ajili ya Mwana wa mtu.

23 Furahiwani siku ile, rukani ; kwani angalia, ujira
 wenu ni ungi mbinguni ; hakika ya babu zao waliwafa-
 nyania manabii vivyo.

24 Laken ole wenu nwinwi wenzi mali ! kwani mna-
 kwisha twaa utulivu wenu.

25 Ole wenu nwinwi mliojaziwa ! kwani mtaona ndaa.

Ole wenu nwinwi mtekao sasa ! kwani mtasikitika,
 mtalia,

26 Ole wenu watu wote wakiwataja nwinwi kuwa wema !
 kwani babu zao waliwafanyia manabii wa uongo vivyo.

27 Laken nawaambia nwinwi msikizao, Pendani waovu

28 wenu, 'mwafanyie vyema wawazirao nwinwi, wabari-
 kini wawaapizao nwinwi, waombeeni wawasingizao nwi-

29 nwi. Akupigaye tafu moja, msongezee na la pili ; na
 akunyang'anyiaye nguo ya juu, na kanzu nayo usim-

30 zuilie. Kulla akuombaye, mpe ; na akupokaye vitu

31 vyako, usivitake tena kwakwe. Na kama mtakavyo

32 watu kuwafanyia nwinwi, nanwi 'mwafanyie vivyo.

33 Basi mkipenda wao wawapendao nwinwi, mna fathili
 gani ? kwani hata watu waovu wapenda wale wapendao

34 wao. Ima mkiwafanyia vyema wawafanyiao vyema
 nwinwi, mna fathili gani ? kwani hata watu waovu wa-

35 fanya vivyo. Ima mkiwaazima wao 'mwatumainio ku-
 pata tena kwao, mna fathili gani ? kwani hata watu

waovu waazima wenzi wao kwamba wapate kutwaa
 vilevile.

35 Laken pendani adui zenu, fanyani vyema, azimani
 msipotumaini kupata tena ; basi ujira wenu utakuwa
 ungi, mtakuwa waana wa aliye juu ; kwani yeye ni

mwema kwa watu wasioshukuru na kwa watu waovu. Ndipo 'mwe na huruma, kama baba yenu naye alivyo 36 na huruma. Msionee watu makosa, nanwi hamtaonewa 37 makosa; msipatilize, nanwi hamtapatilizwa; sameheni, mtasamehewa. Toani, nanwi mtatolewa; kipimo chema 38 kilichoshindiliwa, kilichosukwasukwa na kipukutikacho, watu watatia mapajani mwenu; kwani kipimo mpi-macho nwinwi, ndicho mtakachopimiwa nanwi.

Akawaambia fumbo, Mtofu wa mato aweza kumwo- 39 nyesha ndia mtofu wa mato mwenziwe? hawataanguka wote wawili shimoni? Mwanafundi hawi juu ya fundi 40 wakwe, laken kulla mmoja aliyetimilia kufunzwa atakuwa kama fundi wakwe.

Waangaliaje sasa kibanzi jitoni mwa ndugu yako, 41 na gogo jitoni mwako hulioni? Basi wawezapi ku- 42 mwambia ndugu yako, Ndugu yangu, niata nikutoe kibanzi kilicho jitoni mwako, usipoangalia gogo lililo jitoni mwako? Mwongo wee, kwanza toa gogo jitoni mwako, ndipo utakapopeleleza kutoa kibanzi jitoni mwa ndugu yako.

Kwani hapana mti mwema uvyaa matunda ma- 43 baya, wala hapana mti mbaya uvyaa matunda mema. Kulla mti watambulikana kwa matunda yakwe; kwani 44 watu hawavuni tini mibani, wala hawavuni zabibu katika mlimbolimbo. Mtu mwema atoa kitu chema 45 katika kandi ngema ya moyo wakwe, na mtu mwovu atoa kitu kiovu katika kandi mbovu ya moyo wakwe; kwani kitu kilicho cha moyoni, ndicho kistemwacho ni kanwa.

Basi mwaniitaje Bwana, Bwana, msipofanya haya 46 nisemayo? Kulla ajaye kwangu, asikiaye maneno 47 yangu, akiyafanya, tawaonyesha nwinwi yu kama nani: yu kama mtu ajengaye nyumba, akitimba tini sana, 48 na msingi ukiwa mwambani; basi maji ya mvo yakaja, yakipiga ile nyumba kwa nguvu, yasiweze kuitukutisha, kwani ilikuwa na msingi mwambani. La- 49 ken yeye aliyesikia asiyeafanya, yu kama mtu aliyejenga nyumba katika nti asipotimba msingi; basi mvo uliposhuka ukiipiga kwa nguvu ikaanguka mara moja; mavundiko ya nyumba ile yakiwa makuu.

BASI alipotimiza maneno yakwe yote watu waki- 7 msikiliza, akaingia Kapernaum. Basi mtumishi wa 2

- akida mmoja alikuwa hawezi, akitaka kufa, naye ali-
 3 kuwa katika huba yakwe sana. Basi huyo aliposikia
habari ya Isa, akatuma wazee wa Wayahudi kwakwe
 akimhitajia, kwamba aje amwokoze mtumishi wakwe.
- 4 Nao walipofika kwa Isa, wakamwomba kwa bidii, waki-
 5 nena, Yuastahili wewe kumtendea neno hilo : kwani
 apenda kabila letu ; hata sunagoge akatujengea yeye.
- 6 Isa akenda nao. Basi alipokuwa si mbali tena na
 nyumba, yeye akida akatuma rafikize kwakwe, akimwa-
 mbia, Ewe Bwana, usijisumbue : kwani mimi sistahili
 7 wewe kuingia tini ya dari yangu ; ndipo napo nisijista-
 hilishe nafsi yangu kuja kwako : laken sema kwa kauli
 8 tu, na mwanangu atapoa. Kwani nami ni mtu aliye-
 wekwa tini ya serikali ; nina askari tini mwangu ; na-
 mwambia mmoja, Enenda, akenda ; na mngine Ndo, o,
 9 akaja ; mtumishi wangu, Fanya neno hili, akafanya. Isa
 aliposikia maneno haya akataajabu kwakwe ; akazu-
 nguka kwa makundi waliomfuata, akanena, Nawaambia
 nwinwi, hata katika Waisraeli sikuona imani kuu kama
 10 hii. Basi watu waliotunwa, waliporudi nyumbani wa-
 kamwona mtumishi aliyekuwa hawezi anapoa.
- 11 Ikawa asubuhi yakwe, akenda mji uitwao Nain ;
 na waanafunzi wakwe wangi, na ungi wa watu, wali-
 12 kwenda pamoja naye. Basi akikaribia lango la mji,
 angalia mayiti inatukuliwa 'nde, mwana wa pekee wa
 mamaye, naye ni mjaani ; na kundi la mji wangi wali-
 13 kuwa pamoja naye. Na Bwana alipomwona, akamsi-
 14 kitikia, akamwambia, Usilie. Akajongea akagusa
 jenensa : wale watukuzi wakasimama. Akanena, Mfu-
 15 lana, nakuambia, Ondoka. Huyo mayiti akaondoka
 akiketi, akaanza kunena ; akamrudisha kwa mamaye.
- 16 Na hofu ikawashika wote : wakamhimidi Muungu, wa-
 kinena, Nabii mkuu anatokea kwetu ; na, Muungu aka-
 17 tazama watu wakwe. Na neno hili likatoka likaenea
 katika nti yote ya Uyahudi, na katika nti zote za ka-
 ndokando.
- 18 Basi waanafunzi wakwe Yohana wakamhubiri mambo
 19 haya yote. Yohana akiwaita waanafunzi wakwe wawili
 akawatuma kwa Isa, akinena, Ndiwe ambaye atakuja,
 20 au tungoje 'mngine ? Basi watu hao walipofika kwakwe,
 wakasema, Yohana mbatizaji akatutuma kwako, akinena,
 Ndiwe ambaye atakuja, au tungoje mngine ?

Basi kwa saa hiyo alikuwa akapoza watu wangi mwa 21
 marathi yao, na masumbuva yao, na roho mbaya; na
 watofu wa mato wangi akawapa mato wakiona. Isa 22
 akajibu akawaambia, Endani mkamhubiri Yohana haya
 mliyoona, mliyosikia; kwamba watofu wa mato waona,
 vivete waenenda, wenyi ukoma watakaswa, viziwi wa-
 sikia, mayiti wafufuka, maskini waelezwa anjili. Na 23
 mbarikiwa ni yeye ambaye hakungwai kwangu. Basi wa- 24
 jumbe wa Yohana wakiwa wakiondoka, akaanza kunena,
 kuambia makundi hali zakwe Yohana, Mlitoka kwenda
 barani kuangalia nini? 'Mwanzi utukutikao kwa pepo?
 Ama mlikwenda kuangalia nini? Mtu aliyevikwa nguo 25
 laini? Angaliani, wenyi nguo za kutukuka na vyakula
 marithawa wakaa nyumbani mwa wafalume. Ama 26
 mlikwenda kuangalia nini? Nabii? Kwa kweli, nawaam-
 bia nwinwi, yu zayidi bado ya nabii. Huyu ndiye 27
 aliyeandikiwa maneno haya, Angalia, namtuma malaika
 wangu mbele ya uso wako, atakayefanya tayari ndia yako
 mbele zako. Hakika yangu nawaambia nwinwi, katika 28
 watu waliovyawa ni wake, hapana nabii mkubwa kuliko
 Yohana mbatizaji: laken mtu ambaye ni mdogo katika
 ufalme wa Muungu ni mkubwa kuliko yeye.

Na watu wote waliomsikia, na watozi wa ushuru, wa- 29
 kampa Muungu haki, wakibatizwa kwa ubatizo wa Yo-
 hana. Laken Mafarisayo na waana vyuoni wakajiepushia 30
 shauri la Muungu, wakitoa batizwa ni yeye. Bwana 31
 akanena, Tawafananisha watu wa kivyazi hiki na nani
 basi? Wa kama nani? Wa kama vijana viketivyo sokoni 32
 viitanavyo, vikinena, Tuliwapigia nwinwi nzumari, ha-
 mkuteza; tuliwaanzia kilio, hamkulia. Kwani Yohana 33
 mbatizaji amekuja akitoa kula mkate, akitoa kunwa vi-
 nyu, mkanena, Yuna shetani. Mwana wa mtu amekuja 34
 akila akinwa, mkanena, Angalia, mtu mlafi, mnwaji wa vi-
 nyu, rafiki ya watozi wa ushuru na ya watu wenyi tha-
 mbi. Laken hekima ni kutakabaliwa kwa wote waanawe. 35

Basi mmoja wao Mafarisayo alimtaka kwamba ale 36
 naye: akaingia nyumbani mwa Farisayo akaketi. Basi 37
 angalia, mtu mke mmoja wa mji huo, aliyekuwa mwinyi
 thambi, alipojua kwamba anaketi kula chakula nyumbani
 mwa Farisayo, akaja na tupa la mafuta ya uudi, aka- 38
 simama kwa nyuma ya maguu yakwe akilia, akaanza
 kumtonea matozi maguuni mwakwe, akiyafuta kwa

nwele za kitwa chakwe, akabusu maguu yakwe, aka-
39 yapaka na mafuta ya uudi. Basi huyo Farisayo aliye-
mwita alipoona, akasema ndani mwakwe, akinena, Huyu
kwamba ni nabii, angalijua ni mtu mke gani aliyemgusa,
na hali zakwe ni hali gani: kwani ni mwinyi thambi.

40 Isa akajibu akamwambia, Siman, nina neno nataka
41 kukuambia. Akanena, Mkufunzi, sema. Kulikuwa na
mtu aliyepasha watu fetha, naye alikuwa na wadeni
wawili; mmoja alikuwa akiwiwa dinari hamsa mia, na
42 wa pili dinari hamsini. Basi wakiwa hawana kitu cha
kumlipia, akawasamehe wote wawili. Basi sema, mmoja
43 wao atakayempenda zayidi ni yupi? Siman akajibu,
akanena, Nathani yeye aliyesamehewa zayidi. Akamwa-
44 mbia, Unasema haki. Akazunguka kwa yule mtu mke,
akamwambia Siman, Wamwona mtu mke huyu? Nna-
ingia nyumbani mwako, hukunipa maji ya maguu: laken
huyu akatonea maguu yangu na matozi, akayafuta kwa
45 nwele za kitwa chakwe. Hukunibusu wewe: laken
huyu tangu alipoingia, hakuata kubusu maguu yangu.
46 Hukupaka kitwa changu na mafuta: laken huyu aka-
47 paka maguu yangu mafuta ya uudi. Ndipo nikuambie,
Anasamehewa thambi zakwe zilizo nyingi, kwani ku-
penda kwakwe ni kungi; laken aliyesamehewa kitu
48 kichache, kupenda kwakwe ni kuchache. Akamwambia
49 mtu mke, Unasamehewa thambi zako. Basi hao wa-
lioketi chakulani pamoja naye, wakaanza kunena ndani
50 mwao, 'Nnani huyu asameheye thambi nazo? Laken
yeye akamwambia mtu mke, Imani yako inakuokoza:
enenda kwa salama.

8 IKAWA, kwa akhiri yakwe, akapita katika miji
mikubwa na midogo, akihubiri, akieleza anjili ya ufalme
wa Muungu, na wale watu kumi na wawili pamoja
2 naye, na watu wake wachache, waliokuwa wanapozwa
roho mbaya na marathi, Maryamu aitwaye Magdalene,
3 aliyetokwa ni majinni sabaa, na Yoanna mke wa Kuza,
wakili wa Herode, na Susanna, na wangine wangi
waliomtumikia kwa mali zao.

4 Basi watu wangi wakiwa wanakutana, waliomwendea
5 mji kwa mji, akasema kwa fumbo, Mpanzi alitoka kusia
mbeyu yakwe: basi akiwa akisia, nyingine ikaanguka
6 ndiani, ikakanyagwa, na nyuni za angani zikala. Nyi-
ngine ikaanguka jiweni; ikamea, kisha ikanyauka kwa

kukosa kinamasi. Nyingine ikaanguka katika miiba; 7
 hiyo miiba ikamea pamoja nayo, ikaisonga. Na nyi- 8
 ngine ikaanguka katika mtanga mwema; ikamea,
 ikafanya nafaka mia mia. Aliposema maneno haya,
 akaita kwa sauti kuu, Aliye na mashikio ya kusikia
 asikie.

Basi waanafunzi wakwe wakamwuliza, wakinena, 9
 Maana yakwe nini fumbo hili? Akasema, Nwinwi 10
 mnapawa kujua siri za ufalme wa Muungu, laken wa-
 ngine kwa mafumbo, kwamba wakiona wasione, na
 wakisikia wasitambue. Ela fumbo ni hili: Mbeyu ni 11
 maneno ya Muungu. Wale wa ndiani ni watu wasi- 12
 kiao; kisha shetani yuaja akitwaa maneno moyoni 13
 mwao, kwamba wasiamini wasiokozwe. Na wale wa
 jiweni ni wao ambao kwamba wasikiapo, wakubali
 maneno kwa furaha: nao hawana mizi; waamini majira
 machache, laken kwa majira ya kujaribiwa wajitenga.
 Na ile iliyoanguka katika miiba ni wao ambao kwamba 14
 waliposikia, wakajiendea wakasongwa ni mawazo na mali
 na furaha za ulimwengu, wasitimize kufanya matunda.
 Laken ile iliyo katika mtanga mwema ni wao ambao 15
 kwamba waliposikia maneno, wakayatunza katika moyo
 ulionyoka, ulio mwema, wakifanya matunda kwa uvu-
 milivu.

Hapana awashaye taa akaifinika kwa chombo, ima 16
 akaiweka tini ya kitanda, laken aiweka juu ya mwango,
 kwamba watu waingiao waone mwanga. Kwani ha- 17
 pana kitu kilichofinikwa, ambacho hakitakuwa wazi;
 wala kilichofitwa ambacho hakitatambulikana kikawa
 wazi. Ndipo mwangalie gisi msikiavyo: kwani aliye 18
 nacho, atapawa; na yeye asiye nacho, hata kile athani-
 cho yunacho, kitatwawa kwakwe.

Basi mamaye na nduguze walikuwa wanakuja kwa- 19
 kwe, wasiweze kumfikia kwa watu kuwa wangi.
 Akahubiriwa *ni watu* wakinena, Mamayo na nduguzo 20
 wanasimama 'nde, wataka kukuona. Akajibu, aka- 21
 waambia, Mama yangu na ndugu zangu ni hawa,
 wasikiao maneno ya Muungu wakayafanya.

Ikawa, siku hizo katika moja yakwe, aliingia dauni 22
 yeye na waanafunzi wakwe: akawaambia, Tuvuke
 ng'ambo ya pili ya ziwa. Wakaepuka pwani. Basi 23
 wakiwa wakienda, akalala usingizi. Ikashuka tháruba

- ya pepo ziwani; wakapakiliwa *maji*, wakawa katika
 24 hatari. Wakamjia wakamwamsha, wakinena, Bwana,
 Bwana, twaangamia. Yeye basi akaondoka, akaka-
 ripia pepo na wimbi la maji: kukatulia, kukawa
 25 shwari. Akawaambia, Ni ipi imani yenu? Wakai-
 ngiwa ni oga, wakataajabu, wakisema wao kwa wao,
 'Nnani huyu, mbona hata pepo na maji aviamuru, navyo
 vikamsikia?
- 26 Wakenda wakafika nti ya Wagadareni, iliyolekea
 27 Galilaya. Basi aliposhuka akenda pwani, akaonana na
 mtu wa mjini mwao, aliyekuwa na majinni tangu siku
 nyingi, na nguo hakuva, na nyumbani hakukaa, laken
 28 alikaa makaburini. Naye alipomwona Isa, akapiga
 kelele, akamwangukia, akasema kwa sauti kuu, N'nani
 nawe, Isa, Mwana wa Muungu aliye juu? Nakuomba,
 usiniathibu.
- 29 Kwani alikuwa anamwamuru ile roho mkoo kutoka
 ndani ya mtu: hakikaye alikuwa akamshika tangu
 majira mangi; naye alikuwa akifungwa akilindwa kwa
 minyoo na pingu; kisha akakata vifungo, akasukumwa
 30 ni jinni kwenda barani. Isa akamwuliza, akinena,
 Waitwaje jina lako? Akanena, Lejioni; kwani ma-
 31 jinni mangi yalikuwa yakimwingia. Nayo yakamwo-
 mba, kwamba asiyaamuru kutoka kwenda shimoni.
- 32 Basi lilikuwako kundi kubwa la nguuwe, waliokuwa
 wakilishwa mlimani: yakamwomba kwamba awape
 33 ruhusa kuwaingia wao. Naye akawapa ruhusa. Basi
 majinni yakatoka ndani ya mtu, yakawaingia nguuwe:
 kundi likaforomoka kititini mwa mlima, wakaanguka zi-
 34 wani, wakisha pumzi. Basi watunga walipoona vilivyoku-
 wa, wakakimbia, wakenda sema mjini na mashambani.
- 35 Watu wakatoka kuangalia neno lililokuwa, wakaja kwa
 Isa, wakamwona yule mtu aliyetokwa ni majinni, anaketi
 maguuni mwa Isa, anavaa nguo, ana akili nzima;
 36 wakafanya oga. Na wale walioona, wakawaambia jisi
 alivyookozwa yule aliyekuwa anapagiwa ni majinni.
- 37 Wakamhitajia pia wote jamia, Wagadareni na watu
 wangi za kandokando, kwamba atoke kwao; kwani
 walikuwa wakishikwa ni hofu kuu. Basi akaingia
 38 dauni akarudi. Na huyo mtu aliyetokwa ni majinni
 alimwomba kukaa pamoja naye; ela Isa akamlikiza,
 39 akinena, Rejea nyumbani mwako, ukaseme hayo mambo

makuu Muungu aliyokufanyia. Akanenda, akahubiri mji wote mambo hayo makuu Isa aliyomfanyia.

Ikawa, Isa aliporudi, makundi wakamkubali kwa 40 furaha, kwani wote walikuwa wakimngojea.

Basi angalia, kulikuja mtu jina lakwe Yairo, aliyeku- 41 wa mzee wa sunagoge, akaanguka maguuni mwa Isa, akamwomba kuja nyumbani mwakwe: kwani alikuwa 42 na mwana mke aliyevyawa pekeye, na maisha yakwe kadiri ya miaka ethenashara, naye alikuwa akifa. Basi akiwa akenenda watu walimsonga.

Na mtu mke aliyekuwa akitokwa ni damu tangu 43 miaka kumi na miwili, aliyekuwa anatoa na mali yakwe yote akiwapa tabibu, asipate kupozwa ni mtu awaye yote, akamjia kwa nyuma akagusa upindo wa nguo 44 yakwe: kule kutoka kwa damu yakwe kukatulua mara moja.

Isa akanena, 'Nnani aliyenigusa? Basi wakiwa 45 wakikana wote, Petro na wenziwe wakanena, Bwana, watu wakusonga wakugandamiza, nawe wanena, 'Nnani aliyenigusa? Isa akanena, Mtu akanigusa; kwani 46 'nnasikia nguvu zikinitoka. Basi huyo mtu mke ali- 47 poona kwamba hakufitwa, akaja akitetema, akamwangukia, akasema mbele za watu wote, kwamba alimgusa kwa sababu gani, na jisi alivyopoa mara moja.

Akamwambia, Tulia, mwanangu: imani yako ina- 48 kuokoza; enenda kwa salama.

Basi akiwa yukali akisema, yuaja mtu wakwe mzee 49 wa sunagoge akimwambia, Mwana wako amekufa: usimsumbue mkufunzi. Isa aliposikia, akamjibu, aki- 50 nena, Usiogope: amini tu; ataokozwa. Basi alipokuja 51 nyumbani, hakuata mtu kuingia, ila Petro, na Yohana, na Yakobo, na babaye mwana na mamaye. Basi wali- 52 kuwa wakilia wote, wakimlilia mwana. Yeye akanena, Msilie: hakufa, alala usingizi. Wakamteka, wakijua 53 kwamba akafa. Yeye na kuwatoa wote, na kushika 54 mkono wakwe, na kuita akinena, Kijana, ondoka! Roho yakwe ikarudi, akiondoka papo mara moja. Isa 55 akaagiza kwamba apawe chakula. Babaye na mamaye 56 wakakutuka kwa ajabu; laken yeye aliwasisitiza kwamba wasimwambie mtu neno lililokuwa.

AKAWAITA hao waanafunzi wakwe kumi na wawili 9 pamoja, akawapa nguvu na mamlaka juu ya majinni

- 2 yote, na kupoza marathi, akawatuma kuhubiri watu
 3 ufalme wa Muungu, na kuonya wagonjwa. Akawaambia, Msitukue kitu ndiani, wala fimbo, wala mkoba, wala mkate, wala fetha, wala msiwe na kanzu mbili.
- 4 Na kadiri nyumba mwingiayo, kaani mumo, tokeani
 5 mumo. Na kadiri watu ambao kwamba hawawakubali nwinwi, mkiwa mkitoka mji wao, hata mtanga wa
 6 maguu yenu ukukuteni kuwa ushuhuda juu yao. Nao wakenenda, wakapita mji kwa mji wakieleza watu anjili, wakiponya mahali pote.
- 7 Basi mfalme Herode akasikia mambo yote yaliyotendwa ni yeye, akasangaa kwa watu wangine kunena,
 8 Yohana akafufuka nyufuni; wangine, Eliya akatokea; 9 na wangine, Manabii wa kale mmoja wao akaja. Na Herode akanena, Yohana 'nnamkata kitwa; laken 'nnani huyu ambaye kwamba sifa zakwe ni hizo nisi-kiazo? Akataka kumwona.
- 10 Na wajumbe walipokuwa wakarudi, wakamtolea habari ya mambo yote waliyofanya. Akawatwaa akajitenga nao faraghani pahali barani mwa mji uitwao Betsaida.
- 11 Basi watu walipojua, wakamwandamia; naye akawakubali, akasema nao maneno ya ufalme wa Muungu; na
 12 waliokuwa wahitaji wa kupozwa akawapoza. Basi jua lilianza kuinama; wakaja kwakwe hao kumi na wawili wakamwambia, Uwaage watu, waenende mijini na mashambani mwa kandokando, wapate malalo na vyakula:
 13 kwani hapa tulipo tu barani. Akawaambia, Wapeni nwinwi vyakula. Wakanena, Hatuna kitu zayidi ya mikate mitano na samaki wawili, bakasa tuende swiswi tukanunue vyakula viwatoshavyo watu hawa wote.
- 14 Kwani walikuwa watu waume kadiri ya elfu tano. Akawaambia waanafunzi wakwe, Waketisheni watu kwa
 15 safu, hamsini kwa hamsini. Wakafanya hivi, wakawa-
 16 ketisha wote. Akatwaa hiyo mikate mitano na hao samaki wawili, akainua mato mbinguni, akavibariki akavivunda, akawapa waanafunzi wakwe kuwaandikia
 17 watu. Wakala wakashiba wote; vikaondolewa vitu vilivyowasalia, vikapu kumi na viwili vya makombo.
- 18 Ikawa, akiwa akisali peke yakwe, walikuwa pamoja naye wale waanafunzi; akawauliza, akinena, Watu wanifanya
 19 mimi kuwa nani? Wakajibu wakanena, Wasema ndiwe Yohana mbatizaji, wangine wasema ndiwe Eliya, na

wangine wanena kwamba manabii wa kale mmoja wao akaja. Akawaambia, Laken nwinwi mwanifanya kuwa 20 nani? Petro akajibu akanena, Ndiwe Masiya wa Muungu. Akawasisitiza, akawaagiza kwamba wasimwambie 21 mtu neno hili; akinena, Yampasa Mwana wa mtu 22 kuumia maumivu mangi, na kukatawa ni wazee na wakohani na waana vyuoni, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka.

Akawaambia wote, Mtu akitaka kuniandamia, akane 23 nafsi yakwe, atukue msalaba wakwe siku zote, akani-fuate. Kwani atakaye kuokoza roho yakwe, ataipoteza, 24 laken apotezaye roho yakwe kwa ajili yangu, huyu ataiokoza. Kwani afayidi nini mtu aliyepata ulimwe- 25 ngu wote, laken aliyejipoteza nafsi yakwe, ima aliyeha-sirika? Kwani aonaye haya kwangu na kwa maneno 26 yangu, kwakwe Mwana wa mtu ataona haya, atakapo-kuja katika enzi yakwe, na ya baba, na ya malaika watakatifu. Ela nawaambia nwinwi kwa kweli, wako 27 wangineo wasimamao hapa, ambao hawataonda mauti, hata waone ufalme wa Muungu.

Ikawa kwa akhiri ya maneno haya, kadiri ya 28 siku nane, akamtwaa Petro na Yohana na Yakobo, akakwea mlima kusali. Basi akiwa akisali, sura ya 29 uso wakwe ikawa nyingine, na nguo yakwe ikawa nyeupe iking'aa. Basi angalia, watu wawili walisema 30 naye, nao walikuwa Musa na Eliya, waliotokea katika 31 enzi wakasema ukomo wakwe aliokuwa kuutimiza katika Yerusalem. Basi Petro na wenziwe walikuwa wakishi- 32 kwa ni usingizi: laken walipokuwa wanaamka wakiwa mato, wakaona enzi yakwe, na hao watu wawili walio-simama naye. Ikawa, wakiwa wakiepukana naye, 33 Petro akamwambia Isa, Bwana, ni kwema swiswi kuwa hapa: na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya: akitoa jua asemavyo. Basi akiwa akisema maneno haya, likaja wingu likawa- 34 fanyia uvuli: wakaogopa wakiwa wakiingia winguni. Na sauti ikatoka winguni ikinena, Huyu ni mwanangu 35 kipendo changu: msikieni yeye. Na sauti hiyo ilipo- 36 kuwapo, Isa akaonekana peke yakwe. Nao walinya-maa; hawakumbubiri mtu siku hizo neno waliloona.

Ikawa siku ya pili yakwe, waliposhuka mlimani, watu 37 wangi wakakutana naye. Basi angalia, mtu mmoja 38

- wao aliita, akinena, Mkufunzi, nakuomba, mtazame
 39 mwanangu mume; kwani ni mwanangu pekee. Basi
 angalia, roho yamshika, mara moja apiga kelele; yam-
 kutua akitokwa ni povu, nayo ikiwa ikimsumbua ni
 40 shida kumwondokea. Nami 'nnaomba wanafunzi wako
 41 kwamba waitoe, laken hawakuweza. Isa akajibu aka-
 nena, Ewe kivyazi kisicho amini, kilichopotoka, 'nta-
 kuwa nanwi, 'ntawavumilia, hata lini? Mlete mwana
 42 wako hapa. Basi akiwa akija, jinni likambwaga lika-
 msukasuka. Isa akaikaripia hiyo roho yenyi ukoo,
 43 akampoza mwana, akamrejeza kwa babaye. Wakaku-
 tuka wote kwa ukuu wa Muungu. Basi wote wakiwa
 wakitaajabu kwa mambo yote Isa aliyofanya, akawaambia
 44 waanafunzi wakwe, Wekani maneno haya mashikioni
 mwenu: hakikaye Mwana wa mtu hana budi atapele-
 45 kwa mikononi mwa watu. Laken wao hawakufahamu
 neno hili; lilikuwa likifitwa kwao, kwamba wasilitambue:
 tena walifanya hofu kumwuliza neno hili maana yakwe.
 46 Basi ukawaingilia muwazo wa kunena, mkubwa wao
 47 'nnani. Na Isa alipoona muwazo huo wa moyo wao,
 48 akashika mtoto aka'mweka mbavuni mwakwe, akawa-
 ambia, Amkubaliye huyu mtoto kwa jina langu, aniku-
 bali mimi: na akubaliye mimi, amkubali yeye aliyeni-
 tuma: kwani aliye mdogo katika nwinwi wote, ndiye
 atakayekuwa mkubwa.
- 49 Yohana akajibu akanena, Bwana, tuliona mtu akitoa
 majinni kwa jina lako, tukamkataza, kwani hafuatani
 50 naswi. Isa akamwambia, Si mkatazeni: kwani ambaye
 hana kondo naswi, ndiye hali yetu.
- 51 Ikawa siku za kukwezwa kwakwe zikiwa zikitimizwa,
 52 akakaza kulekeza uso wakwe kuenda Yerusalem. Aka-
 tuma wajumbe mbele ya uso wakwe: nao wakenda wa-
 kaingia mji wa Wasamaria, kwamba wamfanyie tayari.
 53 Nao hawakumkubali, kwa uso wakwe kulekezwa kuenda
 54 Yerusalem. Basi waanafunzi wakwe, Yakobo na Yo-
 hana, walipoona wakanena, Bwana, wapenda tuamuru
 moto ushuke mbinguni, ukawale hao, kama Eliya ali-
 vyofanya?
- 55 Laken yeye akazunguka, akawakaripia, akanena,
 56 Hamjui hali ya roho iwapasayo nwinwi? Kwani Mwana
 wa mtu hakuja kuangamiza roho za watu, laken kuzio-
 koza. Basi wakenenda mji mngine.

Ikawa, wakiwa wakenenda ndiani, mmoja akamwa- 57
mbia, Bwana, takufuata wendapo pote. Isa akamwa- 58
mbia, Maloma yana nyumba, na nyuni za angani zina
vitundu; laken Mwana wa mtu hana cha kuwekea kitwa
chakwe.

Akamwambia mngine, Unifuate. Laken huyu aka- 59
nena, Bwana, nipa ruhusa kwanza, n'ende nikamzike
baba yangu. Isa akamwambia, Uwaate wafu wazike 60
wafu wao: laken wewe enenda ukaeleze maneno ya
ufalme wa Muungu.

Na mngine naye akanena, Takufuata, Bwana; laken 61
kwanza unipe ruhusa niagane na watu wa nyumbani
mwangu. Isa akamwambia, Atiaye jembe mkononi, 62
akiangalia nyuma, hastawi katika ufalme wa Muungu.

KWA akhiri ya haya Bwana akatagua na watu 10
wengine sabaini, akawatuma wawili kwa wawili kwa-
mba waenende mbele yakwe kulla mji na kulla pa-
hali alipotaka kuja mwenyewe. Akawaambia, Ma- 2
vuno ni mangi kweli, laken watenda kazi ni wacha-
che: ndipo mwombeni Bwana wa mavuno, kwamba
atume watenda kazi mavunoni mwakwe. Enendani: 3
angaliani, nawatuma nwinwi kama kondoo katika
mbwa mwitu. Msitukue mfuko, wala mkoba, wala 4
viatu, wala msiamkue mtu ndiani. Na kadiri nyu- 5
mba mwingiayo, semani kwanza, Salama iwe na
nyumba hii. Na kwamba mwana wa salama yumo, 6
salama yenu itamtulilia; na kwamba hamna, ita-
rudi kwenu. Kaani nyumba moja, mkila mkinwa 7
vitu walivyo navyo; kwani mtenda kazi yuasta-
hili kupawa ujira wakwe. Msitoke nyumba moja
mkaingia nyingine. Na kadiri mji mwingiao, wakiwa- 8
kubali nwinwi, lani vitu viwekwavyo mbele zenu:
pozani wagonjwa waliomo, mkawaambie, Ufalme wa 9
Muungu unakuja karibu nanwi.

Na kadiri mji mwingiao, wasipokubali nwinwi, mki- 10
toka mkipita ndiani, waambieni, Hata mtanga ulioguiana 11
naswi wa mjini mwenu, twawafutia nwinwi: laken neno
hili mjue, kwamba unakuja karibu nanwi ufalme wa
Muungu. Nawaambia nwinwi, kwamba Sodoma ita- 12
kuwa na heri siku ile kuliko mji huo.

Ole wako, Khorazin! ole wako, Betsaida! kwani 13
vitendo hivi vya nguvu vilivyokuwa kwenu, kwamba

- vilikuwa katika Turo na Sidon, wangelijuta zamani hizo zao, wangeliketi jifuni wakivaa nguo za kujitusha.
- 14 Ela Turo na Sidon itaona heri katika maamzi, kuliko nwinwi.
- 15 Nawe Kapernaum, uliyekwezwa hata mbinguni; uta-
16 shushwa hata motoni. Awasikiaye nwinwi anisikia mimi; na awatharauye nwinwi anitharau mimi; laken anitharauye mimi amtharau yeye aliyenituma.
- 17 Basi hao sabaini wakarudi kwa furaha, wakinena, Bwana, hata majinni ya tini mwetu kwa jina lako.
- 18 Akawaambia, 'Nlimwona Shetani akianguka kutoka
19 mbinguni kama umeme. Angalia, nawapa nwinwi mamlaka kukanyaga nyoka na 'nge na nguvu zote za huyo adui: hapana kitu kitakachowahasiri nwinwi.
- 20 Laken kwa jambo hili msifurahiwe, zile roho kuwekwa tini mwenu; laken furahiwani kwa majina yenu kuandikwa mbinguni.
- 21 Kwa saa hiyo Isa alifurahiwa kwa roho, akanena, Nakushukuru, ewe Baba, Bwana wa mbingu na nti, kwa wewe kufinika mambo haya kwa watu wenyi elimu na werevu, ukiyafunua kwa watoto; ndivyo, ewe Baba,
22 kwani mapenzi yako ndivyo yalivyokuwa. Mambo yote yakawekwa kwangu ni Baba: hapana mtu ajuaye Mwana 'nnani, ila Baba; wala hapana ajuaye Baba 'nnani, ila Mwana, na huyo naye atajua ambaye kwamba Mwana atamfunulia.
- 23 Akazunguka kwa waanafunzi wakwe, akawaambia peke yao, Yanabarikiwa mato yaonayo mambo mwonayo
24 nwinwi. Kwani nawaambia nwinwi, Manabii wangi na wafalme walitaka kuona mwonayo nwinwi, wasione, na kusikia msikiayo nwinwi, wasisikie.
- 25 Basi angalia mwana chuoni mmoja akaja, akimjaribu, akinena, Mkufunzi, nifanye nini hata nipate uzima wa
26 ahera? Akamwambia, Katika taureti yaandikwaje? wa-
27 somaje? Akajibu, akanena, Mpende Bwana Muungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa nia yako yote; na mwenzio
28 kama nafsi yako. Akamwambia, Ukajibu sawasawa;
29 fanya hivi, basi utakuwa mzima. Laken yeye alitaka kujipa haki mwenyewe, akamwambia Isa, Na mwenzangu 'nnani?
- 30 Isa akajibu akanena, Mtu mmoja alitelemuka kwenda

Yerikho akitoka Yerusalem, akaguiwa ni watoro, nao wakamvua nguo, wakamtia tháruba, wakenda zao, wakimwata majuruhu. Basi kwa nasibu mkohani mmoja 31 akatelemuka kwa ndia ileile, akamwona, akamwepuka, akenda zakwe. Na Mlawi vivyo, alipofika pahali pale, 32 akaja, akamwona, akamwepuka, akenda zakwe. Laken 33 Msamaria mmoja aliyesafiri, akamjia, naye alipomwona akamsikitikia; akamjongelea, akamfunga jaraha zakwe, 34 akimtia mafuta na vinyu; akamkweza juu ya nyama wakwe, akamleta nyumbani mwa wageni, akamwuguza. Na asubuhi yakwe, akiondoka, akatoa dinari mbili, aka- 35 mpa mwinyi nyumba, akamwambia, Umwuguze: na kitu utakachotoa zayidi, n'takaporudi takulipa. Ni 36 yupi sasa katika hawa watatu umthaniaye alikuwa mwenziwe yeye aliyeguiwa ni watoro? Akanena, Yeye 37 aliyefanya huruma naye. Basi Isa akamwambia, Ene- nda nawe ukafanye vivyo.

Ikawa wakiwa wakenenda, akaingia mji mmoja: basi 38 mtu mke mmoja, jina lakwe Martha, akamkaribisha nyumbani mwakwe. Naye aliyekuwa na ndugu mke, 39 jina lakwe Maryamu, aliyeketi maguuni mwa Isa, akimsikiza maneno yakwe. Laken Martha alijiburu- 40 gusha kwa matumishi mangi, akaja akanena, Bwana, huoni ndugu yangu akaniata kutumika peke yangu? humwambii kwamba anisayidie? Isa akajibu, aka- 41 mwambia, Martha, Martha, wewe waaza, wajisumbua kwa mambo mangi: laken kitakwacho ni kitu kimoja: 42 na Maryamu akatagua fungu jema, ambalo kwamba halitaondolewa kwakwe.

IKAWA, akiwa katika pahali fulani akisali, basi 11 alipokoma, mmoja wao waanafunzi wakwe akamwambia, Bwana, utufunze kusali, kama Yohana naye alivyofunza waanafunzi wakwe.

Akawaambia, Mkisali, semani, Ewe Baba yetu uliye 2 mbinguni, Liwe takatifu jina lako. Uje ufalme wako. Yatimizwe mapenzi yako ulimwenguni, kama yati- 3 mizwavyo mbinguni. Riziki zetu za kututosha, utupe siku kwa siku. Utusamehe thambi zetu; kwani naswi 4 twamsamehe kulla mkosa wetu. Usitupeleke majari- buni; laken ututoe maovuni.

Akawaambia, Nani katika nwinwi aliye na rafiki, 5 akenda kwakwe katikati ya usiku, akimwambia, E rafiki

- 6 yangu, unipe karatha mikate mitatu; kwani rafiki
yangu amekuja, yuatoka safarini, nami sina kitu cha
7 kumpa? Na yule aliye ndani, amjibu anene, Usinikuze
mashaka: 'nnakwisha funga mlango, na watoto wangu
pamoja nami wamekwisha lala; siwezi kuondoka kukupa.
8 Nawaambia nwinwi, Na kwamba hataondoka akampa
kwa kuwa rafikiye, laken kwa ule utofu wa haya alio nao
ataondoka atampa vile atakavyo.
- 9 Nami nawaambia nwinwi, Ombani, mtapawa; tafu-
10 tani, mtaona; bishani, mtafunguliwa. Kwani kulla ao-
mbaye apokea; na atafutaye aona; na abishaye afungu-
liwa.
- 11 Yu wapi baba katika nwinwi, ambaye mwanawe aki-
mwomba mkate, akampa jiwe? au samaki, akampa
12
13 nyoka? ama akimwomba yayi, akampa 'nge? Basi
kwamba nwinwi mlio waovu mwajua kuwapa waana
wenu tunu ngema, kwa zayidi mara ngapi Baba aliye
mbinguni atawapa Roho Takatifu watu wamwombao?
- 14 Akawa akitoa jinni, nalo lilikuwa bubu: ikawa hilo
jinni lilipotoka, bubu akanena; makundi wakataajabu.
- 15 Laken wangineo wakasema, Atoa majinni kwa Beel-
16 zebul, mkubwa wao majinni. Na wangine walitaka
alama ya mbinguni kwakwe, wakimjaribu.
- 17 Basi mwenyewe, alipojua mawazo yao, akawaambia,
Kulla ufalme uliogawanikana kwa nafsi yakwe utahari-
bika, na nyumba itetayo na nafsi yakwe yaanguka.
- 18 Na Shetani vivyo, akigawanikana kwa nafsi yakwe,
ufalme wakwe utasimamaje? kwa nwinwi kusema, natoa
19 majinni kwa Beelzebul. Na kwamba mimi natoa ma-
jinni kwa Beelzebul, waana wenu wayatoa kwa nani?
20 kwa jambo hili wao watakuwa waamzi wenu. Laken
nikitoa majinni kwa chanda cha Muungu, hauna budi
ufalme wa Muungu unakuja kwenu.
- 21 Mtu mwinyi nguvu aliye na selaha zakwe akilinda
22 nyumba yakwe, mali yakwe yatakuwa salama; laken
mwinyi nguvu za kumpita yeye akija, akimshinda,
atamnyang'anyia selaha zakwe zote alizotegemea, ata-
23 gawanya nyara zakwe. Asiyekuwa hali moja nami,
yuna kondo nami; na ambaye hakusanyi pamoja nami,
24 atawanya. Roho mkoo akiwa akatoka ndani ya mtu
atembea akipita mahali pasipo maji, akitafuta raha: aki-
25 ikosa anena, Tarudi nyumbani mwangu nlimotoka. Akija

aiona imefiagiwa imepambwa. Basi yuenenda akatwaa 26
 roho sabaa ngine mbaya kuzidi nafsi yakwe, wakaingia
 wakakaa mumo; na mwisho wa mtu huyo u kuwa
 mbaya kuzidi mwanzo.

Ikawa aliposema maneno haya, mtu mke mmoja 27
 akainua sauti katika makundi, akamwambia, Yanabari-
 kiwa matumbo yaliyokutukua wewe, na matiti uliyoa-
 mwa. Mwenyewe akanena, Ndivyo; laken halisi walio- 28
 barikiwa ni watu wasikiao maneno ya Muungu, waki-
 yatunza.

Basi watu wakiwa wanakutana pamoja, akaanza ku- 29
 nena, Kivyazi ni kiovu hiki: watamani alama; na ala-
 ma hawatapawa, isipokuwa alama ya nabii Yunus.
 Kwani kama Yunus alivyokuwa alama kwa watu wa 30
 Ninawi, ndivyo Mwana wa mtu atakavyokuwa alama
 kwa kivyazi hiki. Mfalme mke wa suheli atasimama 31
 katika maamzi pamoja na watu wa kivyazi hiki, atawa-
 patiliza; kwani alikuja akatoka mwisho wa ulimwengu,
 kusikiza akili za Suleman: angalia na hapa ni zayidi ya
 Suleman. Watu wa Ninawi watasimama katika ma- 32
 amzi pamoja na kivyazi hiki, watakipatiliza; kwani
 walijuta kwa maneno ya Yunus: angalia na hapa ni
 zayidi ya Yunus.

Hapana awashaye taa aiweka mvunguni au tini ya 33
 pishi, laken aiweka juu ya mwango, kwamba watu wai-
 ngiao waone mwanga. Taa ya mwili ni jito: jito lako 34
 likiwa la kweli, na mwili wako wote utakuwa mwanga;
 laken likiwa bovu, mwili wako nao u kiza. Ndipo uji- 35
 tunze, mwanga ulio ndani mwako usiwe kiza. Basi 36
 mwili wako wote ukiwa mwanga, usipokuwa na fungu
 moja la kiza, utakuwa mwanga mtupu, kama kwamba
 taa ya kufanya nuru za umeme.

Basi akiwa akisema, Farisayo mmoja alimtaka kwamba 37
 ale chakula kwakwe. Akaingia akaketi kula. Huyo 38
 Farisayo alipoona, akataajabu kwamba hakunawa mi-
 kono kwanza asijala. Bwana akamwambia, Sasa nwi- 39
 nwi Mafarisayo 'nde ya mkebe na ya bakuli mwaiosha,
 laken ndani yenu inajaa uthalimu na uovu. 'M wapu- 40
 mbafu nwinwi: aliyefanya ile 'nde, na ile ndani nayo
 hakuifanya? Laken vitu vilivyo ndani vitoeni sadaka; 41
 angalia, na mambo yote yanakuwa tohara kwenu.
 Laken ole wenu, Mafarisayo! mwatoa zaka za fum- 42

- bani, na za ujaka, na za mboga zote, na kua-
 mua haki na kumpenda Muungu mwapita kando:
- 43 haya yapasa kufanywa, na yale nayo yasiatwe. Ole
 wenu, Mafarisayo! mwapenda kiti cha mbele katika
 masunagoge, na kupawa salamu katika ndia kuu.
- 44 Ole wenu, waana vyuoni na Mafarisayo, wanafiki!
 kwani 'm kama makaburi yaliyopotea, watu watembea
- 45 juu yao wasipojua. Basi mmoja wao waalimu wa
 sheria akajibu, akamwambia, Mkufunzi, ukisema hayo
- 46 watufolea naswi. Akanena, Nanwi waalimu wa
 sheria, ole wenu! kwani mwatukuza watu mizigo isi-
 yotukulika, nanwi nafsi zenu kwa kimoja cha vyanda
- 47 vyenu hamwigusi. Ole wenu! mwajengea makaburi
- 48 ya manabii, na babu zenu waliwaua. Kwa kweli mwa-
 shuhudia vitendo vya babu zenu mwapendezewa navyo:
 kwani hao waliwaua, na nwinwi mwajengea makaburi
- 49 yao. Ndipo napo hekima ya Muungu inene, Tatuma
 manabii na wajumbe kwenu, na wangineo watawaua,
- 50 watawaendea makusudi kuwasumbua: kwamba damu
 ya manabii wote, iliyomwaywa tangu mwanzo wa uli-
- 51 mwengu, itakwe kwa kivyazi hiki; tangu damu ya
 Habil hata damu ya Zakariya, aliyeuawa katikati ya
 mathbahu na hekalu: kwa kweli nawaambia nwi-
- 52 nwi, itatakwa kwa kivyazi hiki. Ole wenu, waalimu
 wa sheria! kwani mlitukua ufunguo wa maarifa: nwi-
 nwi nafsi zenu hamkuingia, na waliokuwa wakiingia
- 53 mliwazuilia. Basi alipowaambia maneno haya, waana
 vyuoni na Mafarisayo wakaanza kumwelemea sana, na
- 54 kumtoza maneno mangi kanwani mwakwe, wakimwotea
 wakitafuta kukamata neno kanwani mwakwe, kwamba
 wapate sababu ya kumstaki.
- 12** MAJIRA hayo jeshi za watu wakiwa wanakutana
 hata wakikanyagana, akaanza kunena kwa waanafunzi
 wakwe kwanza, Mjitunze matatu ya Mafarisayo ambayo
- 2 kwamba ni utawaa wa urongo. Ela hapana kitu kilicho-
 finikwa ambacho hakitafunuliwa, wala kilichofitwa amba-
- 3 cho hakitatambulikana. Ndipo na maneno yote mliyo-
 sema kizani yatasikiliwa mwangani; nayo mliyonong'o-
 nezana vyumbani yatahubiriwa juu ya sakafu.
- 4 Nawaambia nwinwi rafiki zangu, Msiche wao wauao
 mwili, wakisha wasiokuwa na neno zayidi la kutenda.
- 5 Laken tawaonyesha nwinwi kumcha nani: Mcheni yeye,

ambaye kwamba alipoua yuna nguvu za kumtupa mtu motoni : kwa kweli, nawaambia nwinwi, huyu mcheni.

Mashomoro matano hayauzwi kwa pesa mbili? na mmoja wao hakusahuliwa mbele za Muungu. Ela hata nwele za vitwa vyenu zote zinahesabiwa. Ndipo msio-
gope : kuhesabiwa kwenu kuwapita mashomoro mangi.

Nawaambia nwinwi, Kulla aniungamaye mbele za watu, Mwana wa mtu naye atamwungama mbele za malaika wa Muungu. Laken anikanaye mbele za watu, atakanwa mbele za malaika wa Muungu. Na kulla mmoja asemaye neno juu ya Mwana wa mtu, atasamehewa ; laken ambaye kwamba ashutumuru Roho Takatifu, hatasamehewa. Basi watakapoleta nwinwi ndani ya masunagoge na mbele za watu wakubwa na wenyi mamlaka, msiaze jisi mtakavyojibu au neno mtakalosema ; kwani Roho Takatifu itawafunza nwinwi kwa saa ileile yawapasanwi kusema.

Basi mtu mmoja katika makundi akamwambia, Mku- funzi, umwambie ndugu yangu, agawanye urithi pamoja nami. Akamwambia, Mtu wewe, nani aliyeniweka mwamzi au mgawanyi wenu? Akawaambia, Angaliani mjitunze tamaa : kwani katika vitu mtu alivyo navyo, si vile vingi viwekavyo roho.

Akawaambia fumbo, akinena, Mashamba ya mtu tajiri yalikuwa na vitu sana. Akaaza ndani mwakwe, aki- nena, Tafanyaje? kwani sina pahali pa kukusanya vitu vyangu. Akanena, Tafanya hivi : tavunda bokhari zangu, nikajenge ngine kubwa ; basi takusanya mumo nafaka zangu zote na mali yangu. Tamwambia roho yangu, Ewe roho yangu, una mali nyingi iliyowekwa akiba ya miaka mingi ; basi pumzika, ule, unwe, ufurahiwe. Ela Muungu akamwambia, Mpumbafu wee, usiku huu wa leo roho yako itatakwa kwako : basi vitu ulivyoweka tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo ajiwekeaye kandi, laken ambaye kwamba hana kitu kwa Muungu.

Akawaambia waanafunzi wakwe, Ndipo niwaambie nwinwi, Msiaze roho zenu, kitu mtakachokula ; wala mwili wenu, kitu mtakachovaa. Roho ni bora kuliko cha- kula, na mwili ni bora kuliko nguo. Tazamani kungulu : hawapandi wala hawavuni, hawana uchaga wala bokhari ; na Muungu awalisha vivyo : nanwi hampiti nyuni mara nyingi ?

- 25 Nani katika nwinwi awezaye kuongeza kimo chakwe
 26 thiraa moja kwa kuaza? Basi msipoweza jambo hili,
 nalo ni dogo kabisa, kwani kuaza yale yasaliayo mangine?
 27 Tazamani mayungi, gisi yameavyo: hayafanyi kazi wala
 hayavuti uzi; nami nawaambia nwinwi, hata Suleman
 28 kwa enzi yakwe yote hakuvikwa kama moja lao. Basi
 Muungu akipamba nyassi gisi hii, nazo leo zi barani
 na kesho zinateketezwa, hatawavika nwinwi kwa
 29 zayidi mara nyingi? Enwi, imani yenu ni ndogo! Na-
 nwi msitafute mtakachokula au mtakachokunwa, wala
 30 msiwe na roho za kubapa. Kwani mambo haya yote
 yatafutwa ni watu wa ulimwengu; na Baba yenu ajua
 31 kwamba mwahitajiwa mambo haya. Laken tafutani
 ufalmewa Muungu; na mambo haya yote nayo mtatiliwa.
 32 Usiogope wewe, kundi dogo; kwani baba yenu akape-
 33 ndezewa kuwapa nwinwi ufalme. Uzani mlivyo navyo,
 mkatoe sadaka za kuwapa maskini; mjifanyieni mifuko
 isiyokuwa mikukuu, kandi isiyopunguka mbinguni,
 34 mwivi asipofika na nondo wasipoharibu. Kwani kandi
 yenu ilipo, ndipo moyo wenu nao utakapokuwa.
 35 Vyuno vyenu viwe vikifungwa mahasamu, na taa zenu
 36 ziwe zikiwaka; na nafsi zenu sawasawa na watu wa-
 mngojoa Bwana wao, atakapoondoka arusini; kwamba
 37 akija akibisha wamfungulie mara moja. Wanabarikiwa
 watumishi hao, ambao kwamba Bwana ajapo awaona wa-
 mato: kwa kweli nawaambia nwinwi, atajifunga ata-
 38 waketisha chakulani, atakuja kuwatumikia. Na kwa-
 mba yuaja zamu ya pili, ama yuaja zamu ya tatu, akiwa-
 ona hivi, wabarikiwa watumishi wale.
 39 Ela neno hili juani, kwamba mwinyi nyumba alijua
 saa mwivi atakayokuja, angalikesha, hangaliata nyu-
 40 mba yakwe kutumbuliwa. Ndipo nanwi 'mwe tayari:
 41 kwani Mwana wa mtu yuaja kwa saa msiothania. Pe-
 tro akamwambia, Bwana, fumbo hili watuambia swiswi,
 42 au watu wote nao? Bwana akanena, Nani basi huyo
 wakili muaminivu na mwinyi akili, ambaye Bwana ata-
 mweka juu ya nyumba yakwe, kwamba awape watu cha-
 43 kula chao kwa wakati wao? Anabarikiwa mtumishi huyo,
 ambaye Bwana wakwe akija atamwona akifanya hivyo.
 44 Kwa kweli nawaambia nwinwi, atamweka juu ya mali
 yakwe yote.
 45 Laken huyo mtumishi akisema moyoni mwakwe,

Bwana wangu anakawilia kuja; akaanza kupiga watwana na wajakazi, na kula na kunwa na kulewa; basi bwana 46 wa mtumishi huyo atakuja kwa siku asiyomngoja, na kwa saa asiyojua, atampasua, atampa fungu lakwe pamoja na watu wasioamini.

Na mtumishi aliyejua mapenzi ya bwana wakwe, laken 47 hakufanya tayari, wala hakutimiza mapenzi yakwe, atapigwa tharba nyingi; na yeye aliyejua, laken aliyefanya 48 yampasayo kupigwa, atapigwa tharba chache. Na kulla mmoja aliyepawa kitu kingi, kwakwe kitatafutwa kingi; na aliyewekewa amana nyingi, kwakwe itatakwa bado zayidi. Moto nnakuja kuleta ulimwenguni; laiti kwa- 49 mba unakwisha waka! Laken nina ubatizo wa kuba- 50 tizwa nao, na thiki 'nliyo nayo hata utimizwe havineneki. Mwathani 'unakujakuleta salama ulimwenguni? Nawaa- 51 mbia nwinwi Sivo; ela magawanyo. Kwani tangu sasa, 52 watu watano katika nyumba moja watakuwa wanagawanikana, watatu watete na wawili, na wawili watete na watatu. Atagawanikana baba na mwanawe mume, na 53 mwanawe mume na babaye; mama na mwanawe mke, na mwanamke na mamaye; mamavyaa atagawanikana na mke wa mwanawe, na huyo mke wa mwanawe atagawanikana na mamavyaaye.

Akawaambia watu tena, Mkiona wingu litokalo maga- 54 ribi, mara moja mwanena, Mvua yaja; ikaja kweli. Mkiona kusi yavuma, mwanena, Jua litatoka; litatoka 55 kweli. Enwi wanafiki! sura ya nti na ya mbingu 56 mwaitambua; basi wakati huu nao msitambue kwani? Hata kwa nafsi zenu hamwamui haki kwani? 57

Ukenda na mdawa wako kwa mzee, ufanye bidii ndiani 58 kupatana naye, kwamba akusamehe, asikuvute kwa muamzi, na muamzi akakupeleka kwa bawabu, na bawabu akakutia chumbani. Nakuambia hutapata kutoka humo, 59 hata ulipe na pesa ile ya kwisha.

MAJIRA hayo walikuwako watu waliomtolea habari 13 ya Wagalilaya, ambao damu yao Pilato alikuwa akatanganya na sadaka zao.

Isa akajibu, akawaambia, Mwathani Wagalilaya hao 2 walikuwa wakosa zayidi ya Wagalilaya wote, kwa muamivu hayo yaliyowapata? Nawaambia nwinwi, Sivo; 3 laken msipojuta, nyote mtaangamia vivyo.

Ima wale watu kumi na wanane, ambao mnara wa 4 Siloa ukaanguka juu yao, ukawaua: mwathani hao

- walikuwa wakosa kuzidi watu wote wakaao katika
 5 Yerusalem? Nawaambia nwinwi, Sivo; laken msi-
 pojuta, nyote mtaangamia vivyo.
- 6 Akasema fumbo hili, Mtu mmoja alikuwa na mtini,
 uliokuwa unapandwa shambani mwakwe mwa zabibu;
 7 akaja akitafuta matunda juu yakwe, asiyaone. Aka-
 mwambia mkulima, Angalia, miaka mitatu 'nna-
 kuja nikitafuta matunda juu ya mtini huu, nisione:
 8 ukate, usiwe ukiharibu uwanda bure. Ela yee akijibu,
 amwambia, Bwana, uate mwaka huu nao, hata nika-
 9 utimbie kandokando, nikatie samadi. Kwenda ukafanya
 matunda; na kwamba haukufanya, huko mbeleni uta-
 ukata.
- 10 Na kwa siku ya sabato alikuwa akifunza watu katika
 11 moja lao masunagoge. Na angalia, kulikuwa na mtu
 mke aliyekuwa na roho ya ugonjwa miaka kumi na
 minane, naye alikuwa akikundana, asiweze kujiinua ka-
 12 bisa. Basi Isa alipomwona, akamwita aje kwakwe,
 akamwambia, Mtu mke wewe, umefunguliwa marathi
 13 yako. Akamwekea mikono: na mara moja akaongoka,
 14 akahimidi Muungu. Laken mzee wa sunagoge
 akajibu, akitukiwa kwa Isa kupoza mtu kwa siku ya
 sabato, akawaambia kundi, Kuna siku sita za makazi
 kupaswa kutendwa; katika hizo basi ndooni mkapozwe,
 15 laken kwa siku ya sabato msije. Huyu Bwana basi
 akamjibu, akanena, Mnafiki wewe, kulla mmoja wenu
 kwa siku ya sabato hamfungui ng'ombe wakwe au punda
 16 wakwe horini, akampeleka kumnweshwa? Na huyu,
 aliye mwana wa Ibrahimu, aliyefungwa ni Shetani,
 angalia, miaka kumi na minane, huyu asipaswe kufu-
 nguliwa katika kifungo hiki kwa siku ya sabato?
 17 Akiwa akisema maneno haya, wakatahayari wote wa-
 lioteta naye; na kundi lote wakafurahiwa kwa mambo
 yote ya utukufu aliyofanya.
- 18 Akasema, Ufalme wa Muungu u kama nini? niulinga-
 19 nische na nini? U kama tembe ya haridali, mtu akitwaa
 akaipanda shambani mwakwe; ikamea, ikawa mti mku-
 bwa; nyuni za angani zikakaa matanzini mwakwe.
- 20 Akasema tena, Nilinganishe ufalme wa Muungu na
 21 nini? U kama tatu, mtu mke akiitwaa akaitia katika
 pishi tatu za unga, hata wote ukiwa mkali.
- 22 Akapita katika miji mikubwa na midogo akifunza watu,
 23 akisafiri kwenda Yerusalem. Na mtu mmoja akamwa-

mbia, Bwana, ni watu wachache waokozwao? Yeye aka-
 waambia, Fanyani bidii kuingia mlango mwembamba; 24
 kwani nawaambia nwinwi, wangi watatafuta kuingia,
 laken hawataweza. Mwinyi nyumba akiwa akaenda 25
 fungu mlango, nanwi mkianza kusimama 'nde na ku-
 bisha mlango, mkinena, Bwana, Bwana, utufungulie!
 atajibu atawaambia nwinwi, Siwajui nwinwi, mtokapo.
 Ndipo mtakapoanza kunena, Tulikula, tulikunwa mbele 26
 zako, nawe ulikuwa ukifunza watu mijini mwetu. La- 27
 ken atasema, Nawaambia nwinwi, sijui mtokapo; ondo-
 kani nami, nyote watenda uthalimu. Kutakuwa na 28
 kilio na kuuma meno, mtakapoona Ibrahimu, na Isaak,
 na Yakob, na manabii wote, katika ufalme wa Muungu,
 laken nwinwi mkiwa mkitupwa 'nde. Watakuja wato- 29
 kao mashariki, na magarihi, na kibula, na suheli, wata-
 keti chakulani katika ufalme wa Muungu. Na anga- 30
 lia, wako wa kwisha watakaokuwa wa kwanza, na wako
 wa kwanza watakaokuwa wa kwisha.

Kwa siku hiyo Mafarisayo wangineo wakaja waki- 31
 mwambia, Ondoka huku, wende zako; kwani Herode
 ataka kukuua. Akawaambia, Endani mkamwambie 32
 mbwa mwitu huyo, Angalia, natoa majinni, napoza watu
 leo na kesho, na siku ya tatu 'ntamaliza. Laken yani- 33
 pasa kuenenda leo na kesho kutwa; kwani haistawi nabii
 kuuawa 'nde ya Yerusalem. Yerusalem, Yerusalem, 34
 uuaye manabii, upigaye mawe watumwao kwako! mara
 ngapi 'nlitaka kukusanya waana wako, kama kuku aku-
 sanyavyo waanawe tini ya mabawa yakwe, laken hamku-
 taka! Angalia, 'mnaatiwa nyumba yenu gofu; kwa 35
 kweli nawaambia nwinwi, hamtaniona hata mtakapokuja
 kunena, Akibarikiwa ajaye kwa jina la Bwana.

IKAWA kwa siku ya sabato, alipokuja nyumbani 14
 mwa Farisayo mmoja, mkubwa wao, kwamba ale mkate,
 wakamtunduia. Na angalia, kulikuwa na mtu mbele ya- 2
 kwe, aliyekuwa na safura. Isa akajibu akawaambia hao 3
 waalimu wa sheria na Mafarisayo, akinena, Je! Ni halali
 kupoza mtu kwa siku ya sabato? Wakanyamaa. Akamshi- 4
 ka, akampoza, akamlikiza. Akajibu akawaambia, 'Nna- 5
 ni katika nwinwi, ambaye ng'ombe wakwe au punda wa-
 kwe akianguka kisimani, asiyemtoa mara moja kwa siku
 ya sabato? Nao hawakuweza kumjibu kwa maneno haya. 6

Akawaambia fumbo hao walioitwa chakulani, akiona 7

8 jisi walivyotagua mahali pa mbele, akiwaambia, Ukiitwa ni mtu arusini, usiketi pahali pa mbele; kwamba
 9 mkubwa wako akiwa akiitwa, basi akija aliyekuita wewe na yeye asikuambie, Ondoka, mpishe huyu; wewe ukaa-
 10 nza kushika pahali pa nyuma kwa aibu. Laken ukiitwa, enenda ukaketi pahali pa nyuma; kwamba, akija aliyekuita akuambie, Rafiki yangu, jongea mbele huku; ndipo utakapokuwa na heshima kwa wale waketio cha-
 11 kulani pamoja nawe. Kwani kulla ajikwezaye nafsi yakwe atashushwa, na ashushaye nafsi yakwe atakwezwa.
 12 Akamwambia yeye aliyemwita naye, Ukifanya chakula cha mtana au cha jioni, usiite rafiki zako, wala ndugu zako, wala watu wa mlango wako, wala jirani zako wenyi mali, kwamba wasikuite nao, wakakulipa. Laken ukifanya karamu, uite maskini na wenyi
 13 vilema, na viwete, na watofu wa mato; basi utakuwa unabarikiwa; kwani hawanacho cha kukujazi: nawe utajaziwa kwa siku ya kiyama cha watu wema.
 15 Basi mmoja wao walioketi chakulani pamoja naye, aliposikia maneno haya akamwambia, Anabarikiwa atakayekula mkate katika ufalme wa Muungu. Yeye akamwambia, Kulikuwa na mtu aliyefanya kialio kiku-
 16 bwa, akiita watu wangi: akamtuma mtumishi wakwe kwa saa ya kialio kuwaambia wale walioitwa, Ndooni; kwani vinakwisha kuwa tayari vitu vyote. Laken wao wote kwa nia moja wakaanza kujishughulisha. Wa kwanza akamwambia, 'Nnanunua shamba, 'nnapaswa
 17 kutoka kwenda liangalia: nakuomba unisamehe. Na mngine akanena, Nimenunua ng'ombe kumi zifungwazo wawili zambamba, nenenda nikawatazame: nakuomba
 18 unisamehe. Na mngine akanena, 'Nnaoa mke, ndipo nisiweze kuja. Basi huyo mtumishi akaja, akamhubiri Bwana wakwe maneno hayo. Basi mwinyi nyumba akakasirika, akamwambia mtumishi wakwe, Enenda upesi ndia kuu na ndogo za mji, ukawatwae maskini, na wenyi vilema, na watofu wa mato, na viwete, uje
 19 nao hapa. Mtumishi akanena, Bwana, yanakuwa kama ulivyoamuru, laken ikalimo nafasi. Bwana akamwambia mtumishi, Enenda ndia kuu za 'nde na nyungoni, ukawalazimishe kuingia, kwamba ijazwe nyumba yangu.
 20 Kwani nawaambia nwinwi, katika wale waliokuwa wakiitwa, hapana atakayeonda kialio changu.

Basi watu wangi walikuwa wakifuatana naye: aka- 25
zunguka akawaambia, Mtu akija kwangu, asipomzira 26
babaye, na mamaye, na mkewe, na waana wakwe, na
nduguze waume na nduguze wake, na nafsi yakwe mwe-
nyewe, hataweza kuwa mwanafunzi wangu. Na ambaye 27
hatukui msalaba wakwe akanifuata, hawezi kuwa mwa-
nafunzi wangu. Hakikaye nani katika nwinwi atakaye 28
kujenga mnara, asiyeketi kwanza akahisabu gharama
zakwe, kwamba anayo mali ya kutimiza? Kwamba 29
alipomaliki, asipoweza kumaliza, wote watazamao wa-
sianze kumthihaki, wakinena, Mtu huyu akaanza kuje- 30
nga, laken hakuweza kumaliza. Ima mfalme gani 31
aendaye vitani kupigana na mfalme mngine, asiyeketi
kwanza akafanya shauri, kwamba aweza na elfu kumi
kumkimbilia yeye amjiaye na elfu asharini? Asipoweza, 32
yule akiwa yukali mbali, akapeleka wajumbe akitaka
amani. Na vivyo kulla mmoja wenu, asiyeaga mambo 33
yote aliyo nayo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. Mu- 34
nyu ni kitu chema, laken munyu ukipumbaa, utaungwa
kwa nini? Haufai kwa mtanga wala kwa samadi: wae- 35
nda watu wautupa. Aliye na mashikio ya kusikia asikie.

BASI watozi wa ushuru na watu wenyi thambi wali- 15
kuwa wakimkaribia wote, kumsikiza. Wakaguna hao 2
Mafarisayo na waana vyuoni, wakinena, Huyu akubali
watu wenyi thambi, yuala nao.

Akawaambia fumbo hili, akinena, Mtu gani katika 3
nwinwi aliye na kondoo mia, akipotewa ni mmoja wao, 4
asiyeata wale tisia wa tisaini barani, akimwendea yule
aliyepotea hata amwone? Na amwonapo a'mweka ma- 5
fuzini mwakwe, akifurahiwa: na ajapo nyumbani awaita 6
rafikize na jirani zakwe, akiwaambia, Furahiwani pamoja
nami, kwani 'nnaona kondoo wangu aliyepotea. Nawa- 7
ambia nwinwi, Kama hivi itakuwa furaha mbinguni kwa
mkosa mmoja ajutaye, zayidi ya kwa watu wema tisia
wa tisaini ambao si wahitajiwa kujuta.

Ima mtu mke gani aliye na robo kumi, akipotewa ni 8
moja, asiyewasha taa, akafiagia nyumba, akitafuta kwa
bidii hata aione? Aionapo awaita rafikize na jirani 9
zakwe akinena, Furahiwani pamoja nami, kwani 'nnaona
robo yangu iliyopotea. Kama hivi, nawaambia nwinwi, 10
itakuwa furaha mbele za malaika wa Muungu kwa
mkosa mmoja ajutaye.

¹¹₁₂ Akanena, Fulani alikuwa na waana wawili. Na mdogo
 wakwe akamwambia babaye, Baba, nipa fungu langu la
 13 mali liniangukialo. Basi akawagawanyia mali. Na
 halafu, hazikupita siku nyingi, yule mwana mdogo aka-
 kusanya vitu vyakwe pia, akatama akenda nti ya mbali,
 na huko akatapanya mali yakwe kwa maisha maovu.
 14 Basi akiwa anakula pia, ndaa kubwa ikaingia nti ile, naye
 15 akaanza kuwa muhitaji. Akenda akapatana na mwenyeji
 16 mmoja, aliyemtumafueni mwakwe, kulisha nguuwe: aka-
 fanya tamaaya kushibisha matumbonyakwe kwa maganda
 17 nguuwe waliyokula; laken hakupawa. Akaingia nafsini
 mwakwe, akanena, Watumishi wangapi baba alio nao,
 wana vyakula tele wakisaza, na mimi ndaa yaniua?
 18 Taondoka takwenda kwa baba, nikamwambie, Baba,
 19 'nnakosa mbinguni na mbele zako: sistahili tena kuitwa
 mwanao: unifanye kama mmoja wao watumishi wako.
 20 Akaondoka, akaja kwa babaye. Basi akiwa mbali,
 babaye akamwona, akamsikitikia, akapiga mbio aka-
 21 mwangukia shingoni mwakwe, akambusu. Huyo mwa-
 na akamwambia, Baba, 'nnakosa mbinguni na mbele
 22 zako: sistahili tena kuitwa mwanao. Laken huyo baba
 akawaambia watumishi wakwe, Enendani mkatwae nguo
 ile ngema ipitayo zote, mkamvike; mpeni pete mkononi
 23 mwakwe, na viatu maguuni mwakwe. Leteni na
 mwana ng'ombe aliyenona, 'mmtinde, tukale, tukafanye
 24 furaha; kwani huyu mwanangu alikuwa anakufa, ana-
 fufuka; alikuwa anapotea, anaonekana. Wakaanza
 25 kufanya furaha. Laken huyo mwanawe mkubwa ali-
 kuwa shambani: basi akija akikaribia nyumba, akasikia
 26 matezo na nyimbo. Akamwita 'mmoja wao watumishi,
 27 akamwuliza, Kuna nini? Akamwambia, Ndugu yako
 amekuja, na babayo akamtindia mwana ng'ombe aliye-
 28 nona, kwa kumpata mzima. Akatukiwa, asitake kuingia.
 29 Laken babaye akatoka, akamnasihii. Yeye akajibu
 akamwambia babaye, Angalia, miaka hiyo mingi naku-
 tumikia, na siku zote sikuhalifu amuri yako: na mimi
 siku zote hata mbuzi hukunipa, wa kufanya furaha na
 30 rafiki zangu. Laken mwana wako huyu, aliyemiza
 mali yako na makahaba, alipokuja, ukamtindia mwana
 31 ng'ombe wa kunona. Yeye akamwambia, Mwanangu,
 wewe siku zote u pamoja nami, na vitu vyote nilivyo
 32 navyo ni vyako. Basi kufanya furaha na kufurahiwa

kuna haki: kwani ndugu yako huyu alikuwa anakufa, anafufuka; alikuwa anapotea, anaonekana.

AKAWAAMBIA waanafunzi wakwe nao, Kulikuwa 16
na mtu tajiri, aliyekuwa na wakili, na huyu aliambwa
kwakwe kwamba atapanya mali yakwe. Akamwita, 2
akamwambia, Ni mambo gani nisikiayo kwako? Fanya
hisabu ya uwakili wako, kwani hutaweza kuwa wakili
tena.

Huyo wakili akanena moyoni mwakwe, Tafanyaje? 3
Bwana wangu auondoa uwakili kwangu; kutimba
siwezi, na kuomba naona haya.

'Nnatambua 'ntakalofanya, niondolewapo uwakili wa- 4
nitwae nyumbani kwao.

Akawaita kulla mmoja wadeni wa bwana wakwe, 5
akamwambia wa kwanza, Wawiwani wewe ni bwana
wangu? Akamwambia, Farasila mia za mafuta. 6
Akamwambia, Twaa hati yako, uketi upesi, ukaandike
hamsini. Akisha akamwambia mngine, Na wewe 7
unawiwani? Akasema, Jisila mia za nganu. Aka-
mwambia, Twaa hati yako ukaandike thamanini.

Basi bwana akamsifu huyo wakili wa uthalimu, 8
kwamba alifanya werevu; kwani waana wa ulimwengu
huu katika kivyazi chao ni werevu kupita waana wa
nuru.

Nami nawaambia nwinwi, Mjifanyie rafiki kwa ma- 9
mona ya uthalimu, kwamba, mkipunguka, wawakaribishe
nwinwi katika hema za ahera.

Ambaye ni mwaminifu kwa kitu kidogo, na kwa 10
kitu kikubwa atakuwa mwaminifu; na ambaye ni
muthalimu kwa kitu kidogo, na kwa kitu kikubwa
atakuwa muthalimu. Basi msipokuwa waaminifu ka- 11
tika mamona ya uthalimu, kile kitu cha kwele mtawe-
kewa amana ni nani? Na msipokuwa waaminifu kwa 12
kitu kisicho chenu, kile chenu mtapawa ni nani?

Hapana mtumishi awezaye kutumikia mabwana 13
wawili: kwani huyo mtumishi atamzira bwana mmoja,
na mmoja akampenda; au atapatana na bwana mmoja,
na mmoja akamtharau. Ha'mwezi kumtumikia Muungu
na mamona.

Na Mafarisayo, waliokuwa wanatunukwa ni fetha, 14
nao walisikia maneno haya yote, wakamthihaki. Aka- 15
wambia, Nwinwi ndinwi wajiwekao wemani mbele za

- watu, laken Muungu ajua mioyo yenu ; kwani kitu kilichokwezwa katika watu kinazirwa ni Muungu.
- 16 Taureti na manabii wenda hata Yohana : tangu majira hayo anjili ya ufalme wa Muungu inahubiriwa,
- 17 na kulla mtu apenya kuingia. Ni rahisi mbingu na nti kuondoka kuliko mstari mmoja wa taureti kuanzuka.
- 18 Kulla aatanaye na mkewe akaoa mngine, azinni : na kula amwoaye mtu mke aliyeatwa ni mumewe, azinni.
- 19 Kulikuwa na mtu tajiri, aliyevaa joho nyekundu na bafuta, akifanya furaha siku zote na uzuri.
- 20 Kulikuwa na maskini, jina lakwe Lazaro, aliyetupwa
- 21 mlangoni mwakwe, akiwa anatumbukatumbuka, akitaka kushiba kwa makombo yaliyoanguka mezani mwa mtu tajiri ; na mbwa nao walikuja wakamramba vionda
- 22 vyakwe. Ikawa, maskini akafa, akatukuliwa ni malaika akifichwa viweoni mwa Ibrahimu. Akafa na mtu tajiri
- 23 naye, akazikwa. Basi motoni akainua mato yakwe akiwa katika athabu, akamwona Ibrahimu kwa mbali,
- 24 na Lazaro viweoni mwakwe. Akaita akanena, Baba Ibrahimu, unihurumie, umtume Lazaro, kwamba atovye nta ya chanda chakwe majini akaburudishe ulimi wangu ; kwani naumia katika moto huu.
- 25 Ibrahimu akamwambia, Mwanangu, kumbuka kwamba wewe ukatwaa vyema vyako katika maisha yako, na Lazaro kathalika vile vibaya ; laken sasa yeye yunatulizwa, na wewe unaumizwa. Na juu ya haya, katikati ya swiswi na nwinwi kunakazwa ufa mkuu, kwamba watakao kuabiri, kutoka huku kwenda kwenu, wasiweze, na wale wa huko nao wasiabiri kuja kwetu.
- 27 Akasema, Basi nakuomba, baba, kwamba umtume nyu-
- 28 mbani kwa baba yangu, kwani 'nna ndugu watano, awashuhudie, kwamba wasije nao mahali hapa pa athabu.
- 29 Ibrahimu akamwambia, Wana Musa na manabii ; wa-
- 30 wasikize wao. Akasema, Siyo, baba Ibrahimu, laken kwamba mmoja wao waliokufa akenda kwao, watajuta.
- 31 Akamwambia, Kwamba hawasikii Musa na manabii, hata mmoja wao waliokufa akifufuka hawataamini.
- 17 **AKAWAAMBIA** waanafunzi wakwe, Havitendeki kwamba makwao yasije : laken ole wakwe yeye ayale-taye ! Ni heri kwakwe, jiwe la kusagia kufungwa

shingoni mwakwe na kutupwa baharini, kuliko kumkwaza mmoja wao wadogo hawa.

Mjitunze nafsi zenu. Ndugu yako akikukosa, mnee; akijuta, msamehe. Na kwamba akukosa mara sabaa siku moja, na mara sabaa arudi kwako, akinena, Najuta, yakupasa kumsamehe.

Na wajumbe walimwambia Bwana, Utuongezee imani. Bwana akanena, Kwamba mna imani kama tembe ya haridali, mngaliweza kuuambia msikamini huu, Ng'oka, ukajipande baharini, nao ungaliwasikia.

'Nnani katika nwinwi, aliye na mtumishi alimaye ima atungaye, arudipo nyumbani akitoka shamba, atakayemwambia, Enenda mara moja ukale chakula? Laken hatamwambia, Unifanyie tayari kialio changu, ujifunge ukanitumikie hata nikale nikanwe; nikisha basi nawe utakula utakunwa? Atamshukuru mtumishi huyo kwa kufanya yale aliyoamuriwa? Nathani sivyo. Kathalika nanwi, mlipofanya mambo yote mliyomuriwa, semani, Tu watumishi wasiofaa; yale yaliyotupasa kufanya, ndio tuliyoafanya.

Ikawa akenenda Yerusalem, akapita katikati ya Samaria na Galilaya. Basi akiwa akiingia mji mmoja, wakamjilia watu kumi wenyi ukoma, waliosimama kwa mbali: wakainua sauti zao, wakinena, Isa Bwana, utuhurumie. Naye alipowaona, akawaambia, Enendeni mkajionyeshe kwa wakohani. Ikawa, wakiwa wakenenda, wakatakaswa. Basi mmoja wao, alipoona ana-pozwa, akarudi, akimhimidi Muungu kwa sauti kuu; akaanguka usoni maguuni mwakwe, akimshukuru; naye alikuwa Msamaria. Isa akajibu, akanena, Si watu kumi waliotakaswa? Wale tissia wa wapi? Hawakuonekana waliorudi kumpa Muungu hemidi yakwe, illa mgeni huyu? Akamwambia, Ondoka, wende zako; imani yako inakuokoza.

Akaulizwa ni Mafarisayo, Ufalme wa Muungu waja lini? Akawajibu akanena, Ufalme wa Muungu hauji ukionekana. Wala hawatanena, Angalia, u hapa! au Angalia, u hapale! kwani, angalia, ufalme wa Muungu ni ndani mwenu. Akawaambia hao waanafunzi, Siku zitakuja, mtakapotamani kuona moja ya siku za Mwana wa mtu, wala hamtaiona. Watawaambia nwinwi, Angalia hapa! au Angalia hapale! msiende, wala msifuuate.

- 24 Kwani kama umeme umesao ukitoka upande mmoja wa mbingu, uking'aa hata upande mengine wa mbingu, ndivyo Mwana wa mtu naye atakavyokuwa katika siku
- 25 yakwe. Laken kwanza yampasa kuumia maumivu mangi na kukatawa ni kivyazi hiki.
- 26 Na kama yalivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo yatakavyokuwa katika siku za Mwana wa mtu nazo :
- 27 walikula, walikunwa, walioa, waliolewa, hata siku Nuhu aliyoingia safina, yakaja maji yakajaa, yakawaangamiza wote.
- 28 Na kathalika kama yalivyokuwa katika siku za Lut : walikula, walikunwa, walinunua, walipanda, walijenga ;
- 29 laken kwa siku Lut aliyotoka Sodoma, moto na kiberiti vikashuka, vikitoka mbinguni, vikawaangamiza wote.
- 30 Kama hivi itakuwa kwa siku Mwana wa mtu atakayo-thihirishwa.
- 31 Kwa siku ile, atakayekuwa juu ya sakafu, na vyombo vyakwe vi nyumbani, asishuke kuvitwaa ; na aliye shamba vivyo, asirudie vitu vya nyuma.
- 32 Mkumbukeni mke wa Lut.
- 33 Atafutaye kuokoza roho yakwe ataipoteza, na aipotezaye ataiponya.
- 34 Nawaambia nwinwi, katika usiku ule wawili watalala kitanda kimoja ; mmoja atakubaliwa na mmoja ataakwa.
- 35 Wawili watakuwa wakisaga pamoja ; mmoja atakubaliwa na mmoja ataakwa.
- 36 Wawili watakuwa shamba ;
- 37 mmoja atakubaliwa na mmoja ataakwa. Wakajibu wakamwambia, Wapi, Bwana ? Akawaambia, Ufu ulipo, ndipo tai watakapokutana.
- 18** AKAWAAMBIA na fumbo ya kwamba watu wapaswa kusali siku zote wasichoke ; akanena, Kulikuwa muamzi katika mji mmoja, asiyemhofu Muungu, wala asiyemjali mtu. Basi kulikuwa na mjaani mtumke katika mji huo, naye akaja kwakwe akinena, Niamua na mdawa wangu. Na wakati wa kwanza hakupenda ; laken punde akanena moyoni mwakwe, Na kwamba Muungu simchi, na mtu simjali, laken basi kwa uthia mtu mke huyu aniwekeao, tamwamua, kwamba mwishoni asije akanipige usoni.
- 6 Bwana akanena, Sikizani mwamzi wa uthalimu anenavyo. Na Muungu hata akiwa ana saburi nao hatawapatia haki watu wakwe aliowatagua, waliao kwakwe

usiku na mtana? Nawaambia nwinwi, atawapatia haki 8
kwa upesi. Laken Mwana wa mtu halisi ajapo, ataona
imani katika nti?

Na wangineo waliotumaini nafsi zao kwamba ni watu 9
wema, wakitharau wenzi wao, akawaambia fumbo hili,
Watu wawili walikwea hekaluni kusali, mmoja Farisayo 10
na mmoja mtozi wa ushuru. Farisayo akasimama aka- 11
sali kwa nafsi yakwe maneno haya, Ewe Muungu, naku-
shukuru kwa mimi kutoa kuwa kama watu wangine,
wanyang'anyi, wathalimu, wazinzi, au kama huyu mtozi
wa ushuru. Nafunga mara mbili katika juma moja, 12
natoa zaka katika vitu vyote nilivyo navyo. Na mtozi 13
wa ushuru alisimama kwa mbali, asitake hata kuinua
mato yakwe mbinguni, laken alijipiga kifua chakwe,
akinena, Ewe Muungu, uwe na rehema nami; mimi ni
mkosa. Nawaambia nwinwi, Huyu alishuka kurudi 14
nyumbani mwakwe akitakabaliwa kuliko huyule: kwa-
ni kulla ajikwezaye nafsi yakwe atashushwa, laken
ajishushaye nafsi yakwe atakwezwa.

Wakaleta na watoto kwakwe kwamba awaguse; basi 15
hao waanafunzi walipoona wakawakaripia. Laken Isa 16
akawaita, akanena, Waateni watoto waje kwangu,
msiwazuilie; kwani ufalme wa Muungu ni wa watu
kama wao. Kwa kweli nawaambia nwinwi, Ambaye 17
hakubali ufalme wa Muungu kama mtoto hataingia.

Na mtu mkuu mmoja akamwuliza, akinena, Ewe 18
mkufunzi mwema, nifanyeni nipate uzima wa ahera?
Isa akamwambia, Kwani kuniita mwema? Hakuna 19
aliye mwema, illa mmoja, naye ni Muungu. Hizo 20
amuri wazijua, Usizini; usiue; usiibe; usiseme ushu-
huda wa uwongo; mwekee heshima babayo na mamayo.
Akanena, Hayo yote 'nnatunza tangu utoto wangu. 21
Isa aliposikia maneno haya akamwambia, Bado jambo 22
moja linakupungukia: vitu vyote ulivyo navyo uviuze,
ukawape maskini, basi utakuwa na kandi mbinguni;
ukisha ndoo, ukanifuate mimi. Aliposikia maneno 23
haya, akafanya majonzi; kwani alikuwa tajiri mkuu.
Na Isa alipomwona akifanya majonzi, akanena, Laken 24
ni shida wenyi mali kuingia ufalme wa Muungu!

Kwani ni rahisi ngamia kupita tundu ya sindano, 25
kuliko mwinyi mali kuingia ufalme wa Muungu. Wa- 26
kanena hao waliomsikia, Nani basi ambaye ataokozwa?

- 27 Akanena, Yasiyowezekana kwa watu, yawezekana kwa Muungu.
- 28 Petro akanena, Angalia, swiswi tunaata mambo yote,
29 tukakufuata wewe. Akawaambia, Kwa kweli nawaa-
mbia nwinwi, Hapana aliyeata nyumba, au baba, au
mama, au ndugu, au mtumke, au waana, kwa ajili ya
30 ufalme wa Muungu, ambaye hapati tena kwa mara
nyingi katika majira haya, na majira ya keshoni atapata
uzima wa ahera.
- 31 Akawatwaa hao kumi na wawili akawaambia, Anga-
liani, twakwea Yerusalem; basi yatatimizwa mambo
32 yote Mwana wa mtu aliyoandikiwa ni manabii. Kwani
atapelekwa mikononi mwa wamataifa, atathihakiwa,
33 atashutumiwa, atatiwa mate; watampiga jalada, wata-
34 mua, na siku ya tatu atafufuka. Laken wao hawakue-
lewa ni neno hata moja, na maneno haya yalikuwa yaki-
fitwa kwao; hawakujua yaliyosemwa.
- 35 Ikawa, akikaribia Yerikho, mtofu wa mato alikuwa
36 anaketi ndiani akiomba. Basi aliposikia watu wangi
37 wakipita, akauliza, Kuna nini? Wakamhubiri kwamba
38 Isa wa Nazareti apita. Akapiga kelele, akinena, Isa,
39 mwana wa Daudi, unihurumie. Basi wale waliotangu-
lia wakamkataza kwamba anyamae; laken yeye aka-
ongeza kupiga kelele, akinena, Ewe Mwana wa Daudi,
40 unihurumie. Isa akasimama, akamtaka aletwe kwakwe:
41 basi akiwa anafika karibu, akamwuliza, akinena, Wani-
42 taka nikufanyeni? Akanena, Bwana, nataka nione. Isa
43 akamwambia, Ona; imani yako inakuokoza. Na mara
moja akaona, akamfuata, akimhimidi Muungu. Na
watu wote walipoona wakamsifu Muungu.
- 19** AKAINGIA Yerikho, akapita. Na angalia, mtu
2 aliyeitwa Zakayo jina lakwe, naye alikuwa mkubwa wao
3 watozi wa ushuru, tena alikuwa tajiri, naye alitaka ku-
mwona Isa, amjue ni mtu gani, asiweze kwa watu kuwa
4 wangi, na mwenyewe alikuwa mfupi. Akatangulia,
akakwea mti msikomori, kwamba apate mwona; kwani
5 alikuwa hana budi kupita ndia ile. Basi Isa alipofika
mahali pale, akaangalia juu, akamwona, akamwambia,
Zakayo, shuka upesi; kwani leo yanipasa kukaa nyu-
6 mbani mwako. Akashuka upesi, akamkaribisha akifura-
7 hiwa. Watu walipoona, wakaguna wote, wakinena,
8 Aenda kuwa mgeni wa mtu mwinyi thambi. Laken

Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, Angalia, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na kwamba 'unamdanganyia mtu kitu chakwe, namlipa mara 'nne. Isa akamwambia, Leo nyumba hii ikapata wokovu, 9 kwani naye ni mwana wa Ibrahimu. Kwani Mwana 10 wa mtu akaja kutafuta na kuokoza kile kilichopotea.

Basi watu wakiwa wakisikiza maneno haya, akaende- 11 leza, akasema fumbo, kwa hali ya kuwa karibu na Yerusalem, na kwa watu kuthani kwamba ufalme wa Muungu hauna budi utathahiri sasa hivi. Ndipo aka- 12 nena, Mtu moja mngwana alikuwa msafiri kuenda nti ya mbali, kujitwalia ufalme, na kurudi. Akaita watu- 13 mishi wakwe kumi, akawapa manni kumi za fetha, akiwaambia, Tumiani hata nikirudi. Laken raiya 14 zakwe walikuwa wakimzira, wakampelekea wajumbe kwa nyuma yakwe, wakinena, Hatumtaki huyu kutawala juu yetu. Ikawa, alipokuwa akatwaa ufalme aka- 15 rudi, akataka watumishi hao aliowapa hiyo fetha kuitwa kwakwe, kwamba ajue fayida kulla mmoja wao aliyojipatia.

Akaja wa kwanza akinena, Bwana, manni yako ika- 16 leta manni kumi. Akamwambia, Hasanta, mtumishi 17 mwema: ulikuwa mwaminifu kwa kitu kichache, basi uwe na mamlaka juu ya miji kumi.

Akaja wa pili akinena, Bwana, manni yako ikafanya 18 manni tano. Akamwambia huyu naye, Nawe uwe juu 19 ya miji mitano.

Na mngine akaja akinena, Bwana, angalia, manni 20 yako, 'nliyokuwa nayo ikiwekwa kando katika lesu. Kwani 'nlikuwa nikikucha, kwa wewe kuwa mtu 21 mgumu; watwaa usichoweka, wavuna usichopanda. Akamwambia, Kwa kanwa lako nakupatiliza, wewe 22 mtumishi mbaya. Ulikuwa ukijua kwamba mimi ni mtu mgumu, natwaa nisichoweka, navuna nisichopanda; na kwani usiweke fetha yangu mezani mwa watu watoao 23 riba, basi mimi 'nlipokuja ningaliitwaa na fayida yakwe?

Akawaambia hao waliosimama kando, Pokeani manni 24 yakwe, mkampe yeye aliye na manni kumi. Waka- 25 mwambia, Bwana, yunazo manni kumi. Hakika yangu 26 nawaambia nwinwi, kwamba kulla mmoja aliye nacho atapawa, laken asiye nacho, hata kile alichu nacho kita- 27 twawa kwakwe. Laken wale adui zangu, wasiotaka

mimi kutawala juu yao, waleteni huku mkawatinde mbele zangu.

28 Na aliposema maneno haya, akatangulia akikwea Yerusalemi.

29 Ikawa, alipofika karibu na Betfage na Betania, kando ya mlima ulioitwa mlima wa zeituni, akatuma waana-

30 funzi wakwe wawili, akinena, Enendani mji ulio mbele zenu; basi mkiingia mtaona mwana wa punda aliye-

31 mje naye. Na mtu akiwauliza nwinwi, Kwani kumfungua? mwambieni, Bwana ni muhitaji naye.

32 Wakenenda waliotumwa, wakaona kama alivyowa-

33 ambia. Basi wakiwa wakimfungua huyo mwana wa punda, wenyewe wakawaambia, Mwamfunguliani huyu

34 punda? Wakanena, Bwana ni muhitaji naye. Wa-

35 kamleta kwa Isa: wakatandika nguo zao juu ya punda, wakampandisha Isa.

36 Basi akiwa akenenda, wakamtandikia nguo zao ndiani.

37 Na alipokuwa karibu na telemuko ya mlima wa zeituni, jeshi yote ya hao waanafunzi wakafurahiwa, wakaanza

38 kumhimidi Muungu kwa sauti kuu, kwa vitendo vyote vya nguvu walivyoona, wakinena, Anabarikiwa mfalme

39 ajaye kwa jina la Bwana: salama mbinguni, na enzi katika juu. Na wangineo Mafarisayo katika kundi

40 wakamwambia, Mkufunzi, uwakataze waanafunzi wako. Akajibu, akawaambia, Nawaambia nwinwi,

41 kwamba hawa wanyamaa, mawe yatapiga kelele. Na alipokuja karibu, akiangalia mji, akalia kwa hali

42 yakwe, akinena, Kwamba ulijua nawe, katika siku yako hii ngawa, mambo yenyi salama yako! laken sasa

43 yanafitwa kwa mato yako. Kwani siku zitakuja juu yako, adui zako watakapojenga boma, watakungukia

44 watakuthiki kando zote, watakufanyia kitanga wewe na waana wako ndani mwako; hawataata ndani mwako

45 jiwe juu ya jiwe; kwa ajili hukutambua majira yako ya kutazamwa kwako.

46 Akaingia hekaluni, akaanza kuwatoa waliokuwa wa-

47 kiuza wakinunua ndani mwakwe, akiwaambia, Yaa-ndikwa, Nyumba yangu ni nyumba ya kusalia: laken nwinwi mliifanya paango la watoro.

48 Akawa akifunza watu hekaluni kulla siku. Laken wakohani na waana vyuoni na watu wakubwa walitafuta

kumwondoa : wasipate neno la kumtenda ; kwani watu 48
wote walikuwa wakipenda mno kumsikiza.

IKAWA, siku moja zile, akiwa akifunza watu heka-20
luni, akiwahubiri anjili, wakohani wakuu na waana
vyuoni pamoja na wazee wakamjia, wakamwambia wa- 2
kinena, Tuambie, unafanya mambo haya kwa mamlaka
gani, ima 'nnani aliyekupa mamlaka haya? Akajibu 3
akawaambia, Nawauliza neno moja nami ; mniambie :
Ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au ulitoka kwa 4
watu? Wakafanya shauri wao kwa wao, wakinena, 5
Tukisema, Ulitoka mbinguni, atanena, Kwani basi ha-
mkumwamini? Laken tukisema, Ulitoka kwa watu, 6
wote watatupiga mawe ; kwani wana hakika ya kua-
mini Yohana kuwa nabii. Wakajibu kwamba hawajui 7
ulipotoka. Isa akawaambia, Basi nami siwaambii nwi- 8
nwi mamlaka yakwe ya mambo haya nifanyayo.

Akaanza kuwaambia watu fumbo hili : Mtu mmoja 9
alilima shamba la zabibu, akalitoa akawapa wakulima,
akasafiri, akakawa sana. Na kwa wakati wakwe aka- 10
mtuma mtumishi kwa hao wakulima kwamba watoe,
wampe sehemu yakwe ya shamba : laken wakulima
wakampiga, wakamwata akenenda mikono mitupu.
Akaongeza akampeleka mtumishi mngine : wakampiga 11
naye, wakamfethehesha, wakamwata akenenda mikono
mitupu. Akaongeza kumpeleka wa tatu : na huyu 12
naye wakamtia jahara, wakamtupa 'nde. Huyo Bwana 13
wa shamba la zabibu akanena, Tafanyaje? Ntampeleka
mwanangu, kipendo changu ; labuda, wakimwona yeye,
watastahi. Basi hao wakulima walipomwona, waka- 14
fanya mashauri wao kwa wao, wakinena, Huyu ni
mrithi : ndooni, tukamue, kwamba urithi uwe wetu.
Wakamtupa 'nde ya shamba, wakamua. Atawatendani 15
sasa huyo Bwana wa shamba? Atakuja, ataharibu 16
wakulima hawa, na shamba lakwe atawapa watu wa-
ngine. Waliposikia maneno haya, wakanena, Yasiwe !
Ela yeye akawapeleleza, akanena, Nini basi neno hili lili- 17
loandikwa, kwamba Jiwe lililokatawa ni waashi ndilo lililo-
kuwa kitwa cha pembeni ? Kulla aangukaye juu ya jiwe 18
hili atavundika, na ambaye laanguka juu yakwe litampo-
nda unga. Basi wakohani na waana vyuoni wakataka 19
kumtia mikononi saa ileile ; wakahofu watu ; kwani wali-
kuwa wakitambua kwamba alisema fumbo hili juu yao.

- 20 Wakamtunduia, wakapeleka madoya waliojifanya kuwa watu wema, kwamba wamkamate kwa neno moja, wapate kumpeleka kwa serkali na kwa amuri ya wali.
- 21 Wakamwuliza, wakinena, Mkufunzi, twajua kwamba wewe wasema haki, na kufunza kwako ni swafi; huangalii wajihi wa mtu, laken wafunza watu ndia ya
- 22 Muungu kwa kweli. Yatupasha swiswi kumtolea
- 23 Kaisari ushuru, imaje? Yeye akatambua hila zao, aka-
- 24 waambia, Kwani kunijaribu? Nionyeshani denari. Ina sura na chapa cha nani? Wakajibu wakasema, Cha
- 25 Kaisari. Akawaambia, Basi cha Kaisari mpeni Kaisari,
- 26 na cha Muungu mpeni Muungu. Hawakuweza kumkamata kwa maneno mbele za watu: wakataajabu kwa jawabu yakwe, wakanyamaa.
- 27 Wakaja kwakwe wangineo Masadukayo wakaniao
- 28 kiyama, wakamuliza, wakinena, Mkufunzi, Musa akatuandikia kwamba mtu akifiwa ni nduguye aliye na mke, akifa asipokuwa na mwana, basi nduguye aoe yule
- 29 mke, amwekee nduguye mbeyu. Basi kulikuwa watu sabaa, ndugu mmoja. Wa kwanza alioa mke, akifa
- 30 hana mwana. Wa pili akamoa yule mke, na huyu naye
- 31 akafa hana mwana. Wa tatu akamoa, na kathalika
- 32 wote hao sabaa; hawakuata waana, wakafa. Kwa
- 33 nyuma ya wote akafa na mke. Basi katika kiyama atakuwa mke wa nani watu hao? kwani wote sabaa
- 34 walimoa. Isa akajibu akawaambia, Waana wa ulimwe-
- 35 ngu huu waoa waolewa. Laken watakaohesabiwa wastahili kupata ulimwengu wa ahera na kiyama,
- 36 hawaoi wala hawaolewi; kwani hawawezi kufa tena; hakika yao wa kama malaika; nao wakiwa waana wa
- 37 Muungu ni waana wa kiyama. Laken kwamba walio-
- kufa watafufuka, hata Musa akaonya katika pahali pa kijiti, amwitapo Bwana Muungu wa Ibrahimu, na Muungu wa Isaak, na Muungu wa Yakob. Ela yeye si Muungu wa watu wafu, laken wa watu walio hai.
- 38 Kwani wote wakali hai kwakwe. Wakajibu wangineo waana vyuoni, wakanena, Mkufunzi, ni maneno mazuri uliyosema.
- 40 Basi hawakuthubutu tena kumuliza neno.
- 41 Akawaambia, Watu wamsema Masiya kuwa mwana
- 42 wa Daudi kwaje? Na mwenyewe Daudi asema katika chuo cha Zaburi, Bwana akamwambia Bwana wangu,

Keti kwa mkono wangu wa kuume, hata nikiweka adui 43
zako tini ya maguu yako. Daudi amwita Masiya 44
Bwana wakwe; basi ni mwanawe kwaje? Basi watu 45
wote wakiwa wakimsikiza akawaambia waanafunzi
wakwe, Tahatharini na waanavyuoni, ambao kwamba 46
nia zao ni za kutembea wakivaa mifuria mirefu, wape-
ndao kupawa salamu sokoni, na vikao vya kwanza kati-
ka masunagoge, na mahali pa mbele karamuni. Ndio 47
wamezao nyumba za watu wake wajaani, wakijikingiza
kwa kusali sala ndefu; hawa wataona hukumu ya kuzidi
kupatilizwa.

AKAANGALIA, akaona watu wenyi mali wakitia **21**
sadaka zao katika hazina. Akaona na mtu mke mjaani 2
maskini akitia mumo pesa mbili. Akanena, Kwa kweli 3
nawaambia nwinwi, mjaani maskini huyu akatia zayidi
ya wote. Kwani hawa wote walitia katika sadaka za 4
Muungu kitu kiwasaliacho, laken huyu akatia kitu cha
upungufu wakwe, mali yakwe yote aliyokuwa nayo.

Na wangineo wakiwa wakisema kwa hekalu, jisi 5
ilivyopambwa na mawe mazuri na vitu vya tunu, aka-
nena, Katika mambo haya mtazamayo, siku zitakuja 6
ambazo kwamba halitaatwa jiwe juu ya jiwe, ambalo
halitavundwa. Wakamuliza, wakinena, Mkufunzi, lini 7
basi yatakapokuwa mambo haya? na alama yakwe nini,
mambo haya yatakapokuwako? Akanena, Tahatharini, 8
msidanganywe; kwani wangi watakuja kwa jina langu,
wakinena, kwamba Ni mimi, na kwamba Wakati una-
fika. Laken msiwaandame nyuma yao.

Na mtakaposikia mshindo wa vita na msukosuko, 9
msiingiwe ni kiwewe: kwani haya sharti yatangulie;
laken mwisho hautakuwako mara moja. Ndipo alipo- 10
waambia, Kabila itarukia kabila, na ufalme utarukia
ufalme. Itakuwako mitetemo mikuu ya nti katika 11
mahali mbalimbali, na ndaa na marathi ya tauni; na
vioja vitishavyo, na alama kuu za mbinguni zitakuwa-
ko. Laken mbele ya haya yote watawatia nwinwi 12
mikono, watawasumbua nwinwi, mkipelekwa masunago-
geni na gerezani, mkiongozwa kwa wafalme na mawali,
kwa ajili ya jina langu. Na hivi mtapata ndia ya ku- 13
sema ushuhuda wenu. Basi liwekeni mioyoni mwenu 14
neni hili, la kutoa tafakari mbele, jisi mtakavyojitetea;
kwani mimi ntawapa nwinwi kanwa, na akili, ambazo 15

- kwamba wakondo wenu wote wasiweze kukania wala
 16 kuzuilia. Laken hata baba na mama, na ndugu na
 mbari, na rafiki zenu, watawatoa nwinwi, mpelekwe
 kwa wakondo wenu; na wangine katika jamaa zenu
 17 watauawa. Mtakuwa mkizirwa ni watu wote kwa ajili
 18 ya jina langu. Na unwele wa vitwa vyenu hautapotea.
 19 Kwa kustahamili kwenu ponyani roho zenu.
- 20 Basi mtakapona Yerusalem imezungukwa ni jeshi za
 askari, juani kwamba uharibifu wakwe umekuwa karibu.
- 21 Majira yale watu wakaa nti ya Uyahudi wakimbie
 milimani, na walio ndani ya mji watoke, na walio 'nde
 22 wasiingie. Kwani hizo ndizo siku za kujaziwa, kwa-
 23 mba yatimizwe yote yaliyoandikwa. Ole wao wenyi
 mimba na waamwishao katika siku zile, kwani itakuwa
 thiki kuu katika nti, na ghathabu juu ya watu hawa.
- 24 Wataanguka kwa maso ya upanga, watatwawa nyara,
 watapanyike katika mataifa pia; na Yerusalemi itaka-
 nyagwa ni mataifa, hata majira ya mataifa yaki-
 25 timilia. Na alama zitakuwako katika jua, na mwezi,
 na nyota; na katika nti hamu ya watu kwa ushangazi;
 26 bahari ikivuma na mawimbi; roho za watu zikikauka
 kwa hofu, na mangojeo ya mambo yatakayoujia uli-
 mwengu; kwani nguvu za mbingu zitatukutishwa.
- 27 Ndipo watakapomwona Mwana wa mtu akija katika
 wingu kwa nguvu na enzi kuu.
- 28 Basi mambo haya yakianza kuwako, inukani, inuani
 vitwa vyenu, kwani ukombozi wenu unakaribia.
- 29 Akawaambia mfano, Angaliani mtini na miti yote;
 30 ikiwa itepuza, mkiangalia, mwajua kwa nafsi zenu kwa-
 31 mba sasa mwaka unakuwa karibu. Na kathalika nwinwi,
 mwonapo mambo haya yanakuwako, juani kwamba
 32 ufalme wa Muungu unakuwa karibu. Kwa kweli na-
 waambia nwinwi, Kivyazi hiki hakitaondoka hata yote
 33 yakiwa. Mbingu na nti zitaondoka, laken maneno yangu
 hayaondoki.
- 34 Mtunze nafsi zenu, kwamba mioyo yenu isiwe mizito
 kwa ulafi na ulevi, na mawazo ya dunia, siku ile ikawajia
 35 nwinwi kwa ghafula. Kwani kama tanzi, itawajia watu
 wote wakaa katika uso wa nti yote.
- 36 Ndipo keshani majira yote, ombani kwamba msta-
 hilizwe kukimbia mambo haya yote yatakayokuwa, na
 kusimama mbele za Mwana wa mtu.

Basi majira ya mtana alikuwa hekaluni akifunza watu, 37
na majira ya usiku akatoka, akakaa mlimani uitwao
mlima wa zeituni. Na kukicha, watu wote wakarauka 38
kumwendea hekaluni kumsikiza.

BASI siku kuu ya mikate isiyotiwa chachu, iitwayo **22**
Pasaka, ilikuwa karibu. Na wakohani wakuu na wa- 2
ana vyuoni wakatafuta ndia ya kumaulia; kwani wali-
kuwa wakicha watu. Na Shetani alimwingia Yuda, 3
aliyeitwa na Iskariota, aliyekuwa katika hisabu ya hao
wathenashara. Akenenda akasema na wakohani wakuu na 4
maakida, jisi atakavyompeleka mikononi mwao. Waka- 5
pendezewa, wakaagana kumpa fetha. Naye akakiri, aka- 6
tafuta nafasi kumpeleka mikononi mwao pasipo mshindo.

Basi siku ya mikate isiyotiwa chachu ikafika, ambayo 7
kwamba iliwapasha kutinda pasaka. Akawatuma Petro 8
na Yohana, akinena, Enendani, mkatufanyie tayari hiyo
pasaka, tukale. Wakamwambia, Ni wapi ututakapo 9
kufanya tayari? Akawaambia, Angalia, mkiwa mna- 10
ingia mjini, mtakutana na mtu atukuaye mtungi wa
maji: mfuateni aingiayo. Mkamwambie mwinyi nyu- 11
mba, Mkufunzi akuambia, Nyumbani ipi niwezapo kula
pasaka pamoja na waanafunzi wangu? Naye atawa- 12
onyesha nwinwi ghórofa kubwa iliyotandikwa; basi
hapo fanyani tayari. Wakenenda wakaona kama ali- 13
vyowaambia; wakafanya tayari hiyo pasaka.

Na saa ilipofika akaketi, na hao wajumbe thenashara 14
pamoja naye. Akawaambia, 'Nlikuwa nikitamani sana 15
kula pamoja nanwi pasaka hii, kabula 'nsitasa kuumia:
kwani nawaambia nwinwi, sitaila tena, hata itimizwapo 16
katika ufalme wa Muungu. Akashika mkebe, akashu- 17
kuru, akanena, Twaani mkebe huu, mgawanizane nwi-
nwi kwa nwinwi; kwani nawaambia nwinwi, sinwi 18
kitokacho katika matunda ya zabibu, hata utakapokuja
ufalme wa Muungu. Akatwaa mkate, akashukuru, 19
akauvunda, akawapa, akinena, Ndio mwili wangu, ulio-
tolewa kwa ajili yenu; fanyani haya kunikumbuka
mimi. Kathalika na mkebe baada ya kialio, akinena, 20
Mkebe huu ndio ahadi mpya kwa damu yangu, ili-
yomwaywa kwa ajili yenu. Laken angalia, mkono wa 21
mwinyi kunisema u pamoja nami katika meza. Ni 22
kweli, Mwana wa mtu yuenenda kama ilivyoandikwa:
laken ole wakwe mtu yule amsemaye!

- 23 Wakaanza kuulizana wao, kwamba 'nnani basi katika wao atakayetenda jambo hili.
- 24 Kulikuwa na mashindano baina yao, ya kunena nani
25 katika wao ahisabiwe mkubwa. Akawaambia, Hao wafalme wa mataifa watawala juu yao, na wenyi mamlaka
26 nao waitwa mahababi. Ela nwinwi sivyo : laken mkubwa wenu awe kama huyo mdogo, na sheke kama mtu-
27 mishi. 'Nnani basi mkubwa, aketiye chakulani ima atumikaye? Si yeye aketiye chakulani? Laken mimi
28 katika nwinwi ni kama atumikaye. Nwinwi ndinwi
29 mliostahamili nami katika mateso yangu. Nami nawa-
30 aga nwinwi ufalme, kama baba alivyoniaga mimi, kwamba mle na mnwe mezani mwangu katika ufalme wangu, mketi katika viti vya enzi mkiamua hizo kabila thenashara za Beni Israeli.
- 31 Bwana akanena, Siman, Siman, angalia Shetani aliwa-
32 taka nwinwi, kuwapepete kama nganu. Laken mimi 'nnakuombea, imani yako isikome ; nawe utakapokuwa
33 unazingadia, uwathubutishe ndugu zako. Akawaambia, Bwana, mimi ni tayari tuende sote hata gerezani
34 na mautini. Akanena, Nakuambia wewe, Petro, jimbi halitawika leo, usipotasa kukana mara tatu kwamba
35 wanijua. Akawaambia, 'Nlipowatuma nwinwi msipokuwa na mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlihitajiwa ni kitu? Wakanena, La : hatukuhitajiwa ni kitu kiwacho
36 chote. Basi akawaambia, Laken sasa, aliye na mfuko autwae, kathalika na mkoba ; na asiyekuwa nao, auze
37 nguo yakwe, akanunue upanga. Kwani nawaambia nwinwi, neno hili nalo lapasa kutimilizwa kwangu, lili-loandikwa, kwamba Alihasibiwa katika wahalifu : kwani
38 yale yanifikiliayo mimi, nayo yatimilia. Wakanena, Bwana, angalia, panga mbili zipo. Akawaambia, Zatosha.
- 39 Akatoka akenda mlimani mwa zeituni, kama ilivyokuwa desturi yakwe ; na waanafunzi wakwe nao wakawa
40 mwandama. Alipofika pahali pale, akawaambia, Salini
41 kwamba msiingie majaribuni. Naye akaepukana nao
42 kadiri ya mtupo wa jiwe, akapiga magoti akasali, akina-
43 nena, Baba, ukitaka nipitishia mkebe huu ; laken si mpenzi yangu, ela yako yawe. Akamtokea malaika wa
44 mbinguni, akimtia nguvu. Naye akiwa katika thiki kuu, akazidi kusali kwa nguvu : na hari zakwe zikawa

kama matone ya damu, yaliyokuwa yakianguka nti. Akaondoka katika sala, akaja kwa waanafunzi wakwe, 45 akawaona wanalala kwa huzuni. Akawaambia, Kwani 46 kulala? ondokani msali, kwamba msiingie majaribuni.

Akiwa akali akisema, angalia, kundi la watu, na yeye 47 aitwaye Yuda, mmoja wao katika wale thenashara, ali-watangulia, naye akamkurubia Isa, kumbusu. Isa aka- 48 mwambia, Yuda, wewe wamtabulisha Mwana wa mtu kwa kumbusu? Na hao waliokuwa pamoja naye, wali- 49 poona neno litakalokuwa, wakamwambia, Bwana, tupi-gane nao kwa upanga? Na mmoja wao akampiga mtu- 50 mishi wa mkohani mkuu, akamkata shikio la kuume. Isa akajibu, akanena, Waateni vivyo. Akagusa shikio 51 lakwe, akampoza. Isa akawaambia hao waliomjia wa- 52 kohani wakuu, na maakida ya hekalu, na wazee, Kama kumjia mtoro, mlitoka na panga na vigongo? Nami 53 kulla siku 'nlikuwa nanwi hekaluni, hata mkono hamku-ninyoshea; laken hii ndiyo saa yenu na nguvu za kiza.

Wakamshika, wakamwongoza, wakamleta nyumbani 54 mwa mkohani mkuu. Na Petro alimwandamia kwa mbali. Na walipokuwa wanawasha moto katikati ya 55 uwanda, wakiketi pamoja, Petro akaketi kati mwao. Basi mjakazi mmoja alipomwona akiketi mwangani, 56 akampeleleza, akanena, Na huyu alikuwa naye. Aka- 57 mkana, akinena, Mtumke wewe, simjui mimi. Na 58 punde kidogo mtu mngine alipomwona akanena, Nawe u mwenzi wao. Petro akanena, Mtu wewe, si mimi. Na halafu kadiri ya saa moja, mtu mngine akathubu- 59 tisha, akinena, Kwa kweli na huyu alikuwa pamoja naye; kwani ni Mgalilaya. Petro akanena, Mtu wewe, 60 sijui unenavyo. Na papo hapo akiwa yukali akisema, jimbi likawika. Huyo Bwana akazunguka, akamwa- 61 ngalia Petro: Petro akakumbuka neno la Bwana ali-lomwambia, kwamba Kabula ya jimbi asijawika, utani-kana mara tatu.

Akatoka 'nde Petro, akalia kwa uchungu. 62

Na watu waliokuwa wanamshika Isa, walimfanyia 63 mzaha, wakimpiga. Wakamfinika, wakampiga usoni, 64 wakamwuliza, wakinena, Mtambue, 'nnani aliyekupiga? Na makufuru mangi mngine wali wakimnenea. 65

Na mtana ulipokuwako, wazee wa watu na wakohani 66 wakuu na waana vyuoni wakakutana, wakamwongoza

- 67 mkutanoni mwao, wakinena, Ukiwa ndiwe Masiya, utuambie. Akawaambia, Nijapowaambia, hamtaamini ;
- 68 na kwamba nawauliza nwinwi, hamtanijibu, wala
- 69 hamtanifungua. Tangu sasa Mwana wa mtu atakuwa
- 70 akiketi kwa ya mini ya nguvu za Muungu. Wao wote wakanena, Wewe basi u Mwana wa Muungu ?
- 71 Akawaambia, Kama mnenavyo, ndimi. Wakanena, Twataka ushuhuda gani tena ? Kwani swiswi wenyewe tukasikia kwa kanwa lakwe.
- 23** WAKAONDOKA kundi lote la watu, wakamwo-
2 ngoza kwa Pilato. Wakaanza kumstaki, wakinena, Huyu twamwona abadili watu, awakataza kwamba wasimpe Kaisari ushuru, akijisema mwenyewe kuwa Masiya, mfalme. Pilato akamwuliza, akinena, Ndiwe mfalme wa Wayahudi ? Akamjibu akanena, Kama unenavyo ndivyo. Pilato akawaambia wakohani na hao makundi, Mimi sioni ukosa katika mtu huyu.
- 5 Laken wao walifanyia nguvu, wakinena, Asukasuka watu, akifunza katika nti yote ya Uyahudi, akianza tangu Galilaya hata hapa. Huyu Pilato aliposikia Galilaya, akauliza kwamba ni mtu wa Galilaya. Na alipopata kujua kwamba yu katika mamlaka ya Herode, akampeleka kwa Herode, aliyekuwamo naye nafsi yakwe katika Yerusalem kwa siku hizo.
- 8 Na Herode alipomwona Isa, akafurahi sana : kwani alikuwa akitaka kumwona tangu hapo, kwa ajili ya kusikia sifa zakwe nyingi ; akataraji kumwona akifanya muujiza mmoja. Akamsaili kwa maneno mangi ;
- 9 laken mwenyewe hakumjibu neno liwalo lote. Na wakohani wakuu na waana vyuoni wakasimama, wakikaza mno kumstaki. Na Herode pamoja na askari zakwe akamthili, akamthihaki, akamfinika nguo ya kung'ala ; kisha akamrudisha kwa Pilato.
- 12 Wakawa rafiki hao Pilato na Herode kwa siku hiyo :
13 kwani kwanza walikuwa wakiteta. Na Pilato alipokuwa analingana hao wakohani wakuu, na masheke na
14 watu wangineo, akawaambia, Nwinwi mmeniletea mtu huyu, kama ageuzaye watu : na angalia 'nnamsikiza mbele zenu, laken hilo neno 'mmstakialo, sikuliona kwa
15 mtu huyu : wala naye Herode, kwani 'nliwapeleka nwinwi kwakwe ; na angalia, hakutenda neno la kustahili
16 kuuawa. Basi tamwathibu, nimfungue.

Kwani alikuwa na lazima kuwafungulia mtu mmoja 17
kwa desturi ya siku kuu. Wakapiga kelele wote pa- 18
moja, wakinena, Mwondoe huyu : utufungulie Baraba.
Na huyu ndiye aliyekuwa anatiwa gerezani kwa sababu 19
ya ufitina uliokuwako mjini, na kwa sababu ya kumua
mtu. Basi Pilato akawaita tena, akisema nao akitaka 20
kumfungua Isa. Wao wakamwitikia, wakinena Msa- 21
libu, msalibu. Akawaambia mara ya tatu, Ni maovu 22
gani basi aliyotenda huyu? Sikuona uwaili wakwe wa
kuuawa : ndipo nimwathibishe, nimfungue.

Laken wao wakaelemea kwa kelele nyingi, wakimta- 23
ka asalibiwe : kelele zao na za wakohani wakuu zikishi-
nda nguvu. Pilato akakata maneno, kwamba yawe 24
kama watakavyo. Akamfungua yeye aliyetiwa gereza- 25
ni kwa ufitina na kwa kuua, waliomwomba ; laken Isa
akamtoa, akamtia mapenzini mwao.

Basi wamwongozapo, wakenda zao wakamshika 26
mmoja, Siman mtu wa Kurene, aliyekuwa akitoka
shamba, wakaweka msalaba juu yakwe, kuutukua kwa
nyuma ya Isa. Na kundi kubwa la watu waume, na 27
wake, wakamwandama, nao walikuwa wakimlilia, na
matozi yali yakiwatoka. Isa akazunguka kwao, aka- 28
nena, Enwi waanawake wa Yerusalem, msinililie mimi :
laken liliani nafsi zenu na waana wenu. Kwani angalia 29
siku zitakuja, ambazo kwamba watu watanena, Wana-
barikiwa walio tasa na matumbo yasiyovyaa, na matiti
yasioamwisha. Ndipo watakapoanza kuambia ile mili- 30
ma, Tuangukieni, na vile vilima, Tufinikeni. Kwani 31
wakifanya mambo haya kwa mti mbichi, kwa mti ulio
mkavu yatakuwaje? Wakaongozwa na watu wangine 32
wawili wahalifu, kwamba wauawe pamoja naye.

Na walipofika pahali paitwapo Pa kitwa, ndipo wali- 33
pomsalibu, na hao wahalifu, mmoja kwa mkono wa
kuume, na mmoja kwa mkono wa kushoto.

Isa akanena, Baba, uwasamehe, kwani hawajui wa- 34
fanyavyo. Wakagawanya nguo zakwe kwa kura. Na 35
watu walikuwa wakisimama wakitazama. Na hata
masheke pamoja nao wakamthilika, wakinena, Aliokoza
watu wangine ; basi aokoze nafsi yakwe, kwamba ndiye
Masiya aliyependwa ni Muungu.

Na hao askari nao wakamthihaki, wakija wakimjo- 36
ngezea siki, wakinena, Ukiwa ndiwe mfalme wa Waya- 37

38 hudi, okoza nafsi yako. Na hati ilikuwa ikiandikwa juu yakwe kwa harufu za Kiyonani, za Kirumi, na za Kiebrania, ya kunena, HUYU NDIYE MFALME WA WAYAHUDI.

39 Na mmoja wao hao wahalifu waliosalibiwa, alimkufurisha, akinena, Ukiwa ndiwe Masiya, okoza nafsi yako
40 na swiswi. Laken mwenziwe akajibu, akamkania, akinena, Hata wewe humchi Muungu, uliye katika
41 idili hii? Naswi halisi kwa haki, kwani twapokea ujira wa makazi tuliyotenda; laken huyu hakutenda neno
42 baya. Akamwambia Isa, Unikumbuke, Bwana, ukija
43 katika ufalme wako. Isa akamwambia, Kwa kweli nakuambia, hivi leo utakuwa pamoja nami peponi.

44 Basi ilikuwa kadiri ya saa sita: kikawa kiza katika
45 nti yote hata saa ya tisia; na jua likawa kiza: na pazia
46 ya hekalu ikapasuka katikati. Isa akaita kwa sauti kuu, akanena, Baba, naweka roho yangu mikononi mwako. Na aliposema maneno haya, akatoweka.

47 Na akida wao hao askari alipoona vilivyokuwa, akamhimidi Muungu, akinena, Kwa kweli mtu huyu
48 alikuwa salihi. Na makundi wote waliokuwako kuangalia, wakitazama vilivyokuwa, wakajipiga vifua vyao
49 wakarudi. Na jamaa zakwe wote, na watu wake waliofuatana naye tangu Galilaya, walikuwa wakisimama kwa mbali, wakitazama mambo haya.

50 Basi angalia, mtu mmoja, jina lakwe Yusuf, aliyeku-
51 wa sheke, mtu mwema, salihi, (huyu hakuwa rathi katika shauri lao na kitendo chao,) naye alikuwa mtu wa Arimataya, mji wa Wayahudi, na mwenyewe naye
52 alikuwa akingoja ufalme wa Muungu: ndiye aliyekwenda kwa Pilato, akitaka mwili wa Isa. Akamshusha, akamtia saandani, akamzika katika kaburi lililotimbwa
54 katika jabali, lisilotasa kuzikwa mtu. Basi ilikuwa siku ya kufanya tayari, na sabato ilikuwa karibu.

55 Na watu wake waliotoka Galilaya pamoja naye wakaja wakaangalia kaburi na jisi mwili wakwe ulivyowe-
56 kwa. Wakarudi, wakafanya tayari viungo na mafuta ya manukato: na siku ya sabato wakastarehe, kama ilivyokuwa amuri.

24 BASI siku ya kwanza katika hizo sabaa, majira ya alfajiri, wakaja kaburini, wakitukua vile viungo walivyokuwa wanatengeleza, na wangineo pamoja nao.

Wakaona jiwe linapinduliwa kaburini. Wakaingia, ³/₄
 watione mwili wa Bwana Isa. Ikawa, wakiwa waki-
 shangaa kwa mambo haya, na angalia, watu wawili
 wakasimama mbele zao kwa nguo za kumetameta.
 Basi wakiwa wanaingiwa ni hofu, wakiinika nyuso zao ⁵
 nti, wakawaambia, Kwani kumtafuta aliye mzima pa-
 moja na wafu? Hapo hapa, ameondoka: kumbukani, ⁶
 kama alivyowaambia nwinwi, alipokuwa bado katika nti
 ya Galilaya, akinena, Kwamba yampasa Mwana wa mtu ⁷
 kusalimishwa mikononi mwa watu waovu, na kusali-
 biwa, na siku ya tatu kufufuka.

Basi wakakumbuka maneno yakwe. Wakarudi ka- ⁸/₉
 burini, wakahubiri mambo haya yote kwa wale edashara
 na jamaa zao wote.

Walikuwa Maryamu Magdalene, na Yohana, na ¹⁰
 Maryamu mamaye Yakobo, na wangine pamoja nao,
 waliowaambia wajumbe mambo haya. Laken maneno ¹¹
 yao yaliwatokea kama hadithi; hawakuwasadiki.

Basi Petro akaondoka, akenenda haraka kaburini, ¹²
 akatungulia, akaona hizo tepe peke; akatoka akarudi
 kwakwe, akitaajabu vilivyokuwa.

Basi angalia, siku hiyohiyo, watu wawili jamaa zao ¹³
 walikuwa wakenenda mji, ambao kwamba kitambo
 chakwe, kutoka Yerusalem, cha baada saa mbili wa
 nusu, na jina lakwe Emmao. Nao walikuwa wakijizu- ¹⁴
 mgumza mambo haya yote yaliyopita kwao. Ikawa, ¹⁵
 wakiwa wakijizungumza, wakiulizana, Isa mwenyewe
 akawakaribia, akenenda pamoja nao.

Laken mato yao yalikuwa yanazuiwa, kwamba wasi- ¹⁶
 mtambue.

Akawaambia, Ni maneno gani haya mwelezanayo, ¹⁷
 mkitembea, kwa majonzi?

Na mmoja wao, jina lakwe Kleopa, akajibu akamwa- ¹⁸
 mbia, Wewe u peke yako katika wageni wa Yerusalem
 asiyejua mambo yaliyokuwako ndani mwakwe siku hizi?
 Akawanena, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ¹⁹
 ya Isa wa Nazareti, aliyekuwa nabii, mwinyi nguvu
 kwa kitendo na kwa neno, mbele za Muungu na mbele
 za watu wote; gisi wakohani wakuu na masheke yetu ²⁰
 walivyompeleka katika hukumu ya kuuawa, waki-
 msalibu. Naswi tulikuwa tukitumaini kwamba ndiye ²¹
 atakayekomboa Waisraeli. Na pamoja na haya yote,

- ni siku ya tatu leo tangu mambo haya yalipokuwa.
- 22 Na watu wake, jamaa zetu, wangineo, nao wanatuku-
- 23 tusha, waliokwenda kaburini majira ya alfajiri; wasione
mwili wakwe, wakaja, wakinena kwamba wametokewa ni
- 24 malaika, wanenao kwamba yu hai. Na wangine, jamaa
zetu, walikwenda kaburini, wakaona vivyo kama watu
wake walivyosema; laken mwenyewe hawakumwona.
- 25 Basi mwenyewe akawaambia, Enwi wapumbafu, na
wenyi mioyo mizito, katika kuamini maneno yote ma-
- 26 nabii waliyonena! Ela haikumpasha Masiya kumia
maumivu haya, ndipo aingie enzini mwakwe?
- 27 Akaanza kwa Musa na kwa manabii wote akawafu-
nulia katika vyo vyote, maneno yamfikiliayo yeye.
- 28 Wakafika karibu na mji walioendea; naye ali akiji-
29 fanya kama atakaye kwenda mbele. Wakamnasihi,
wakinena, Kaa pamoja naswi, kwani ni jioni tena, na
- 30 jua linakutwa. Akaingia kukaa nao. Ikawa, akiketi
chakulani pamoja nao, akatwaa mkate, akashukuru,
- 31 akauvunda, akawapa. Mato yao yakafunguliwa, wa-
kamtambua: akatokomea mbele zao.
- 32 Mmoja akamwambia mwenziwe, Laken mioyo yetu
haikuwa ikiwaka ndani mwetu, akiwa akisema naswi
- 33 ndiani, akitufunulia vyo? Wakaondoka saa hiyohiyo,
wakarudi Yerusalem, wakaona hao edashara na jamaa
- 34 zao wamekutana, wakinena, Bwana akafufuka halisi,
35 akamtokea Siman. Na wenyewe nao wakatoa habari
ile ya ndiani, na jinsi alivyotambulikana kwao akiwavu-
ndia mkate.
- 36 Basi wakiwa wakali wakisema, mwenyewe Isa aka-
simama katikati yao, awaambia, Salama iwe kwenu.
- 37 Wakikutuka, wakiingiwa ni hofu, wakathani wakaona
- 38 pepo. Akawaambia, Kwani kufathaika? na kwani ku-
39 fanya mawazo mioyoni mwenu? Angaliani mikono
yangu na maguu yangu, kwamba ni mimi mwenyewe:
nigusani, angaliani; kwani pepo hana nyama na mifupa,
- 40 kama mwonavyo mimi kuwa nayo. Na aliponena hivi,
akawaonyesha mikono na maguu.
- 41 Basi wakiwa hawatasa kuamini kwa furaha na kwa
- 42 ajabu, akawaambia, Mna kitu cha kula hapa? Waka-
mpa kipande cha samaki aliyeokwa, na kipande cha ka-
- 43 mba la asali. Akavitwaa, akala mbele zao. Aka-
- 44 waambia, Ndiyo maneno nliyowaambia 'nliyokuwa nikali

pamoja nanwi, kwamba yapasa kutimizwa maneno yote yalivoandikwa, yanifikiliayo mimi, katika taureti ya Musa, na katika manabii, na katika zaburi.

Akawazindua akili, kupata kufahamu vyuo. Akawaa-⁴⁵
mbia, Ndivyo ilivyoandikwa, na ndivyo ilivyompasa⁴⁶
Masiya kuumia, na kuondoka nyufuni siku ya tatu; na 47
kwamba kujuta na kusamehewa kwa thambi kuhubiriwe
katika watu wote, kwa jina lakwe, kuanzwe kwa Yeru-
salem. Na nwinwi m mashahidi wa mambo haya. 48

Basi angalia, napeleka maagano ya baba yangu juu 49
yenu: nanwi kaani katika mji wa Yerusalem, hata mki-
vikwa nguvu za juu.

Akawaleta 'nde hata Betania: akainua mikono yakwe 50
akawabariki. Ikawa, akiwa akiwabariki, akaepukana nao, 51
akapaazwa mbinguni. Nao wakimsujudia, wakarudi 52
Yerusalemini kwa furaha kuu. Wakawa hekaluni siku 53
zote, wakimsifu, wakimhimidi Muungu. Amina.

ANJILI KWA YOHANA.

MWANZO palikuwa na Neno, Neno akawa kwa Mu- 1
ungu, Neno akawa Muungu. Ndiye aliyekuwako mwa- 2
nzo kwa Muungu. Vyote vimepata kuwa kwa huyu, 3
wala pasipo yeye hakikuwa kitu kilichokuwa. Katika 4
huyu palikuwa na uzima; na uzima ndio nuru yao
watu. Uzima ukamulika gizani, wala giza haliku- 5
ushika.

Palikuwa mtu amepolekwa kwa Muungu, jina lake 6
Yohana. Huyu akaja kwa ushahidi aishuhudie nuru, 7
wote wapate kuamini kwa sababu yake. Huyu si nuru, 8
illa aishuhudie nuru.

Ndiye nuru ya kweli amtiaye nuru killa mtu ajaye 9
katika ulimwengu. Alikuwako ulimwenguni, ulimwengu 10
umepata kuwa kwa yeye, wala ulimwengu haukumjua.
Alikuwa kwa milki yake, wala walio katika milki yake 11
hawakumkubali. Wale wamkubalio amewapa nguvu 12
za kuwa watoto wake Muungu, wanaomini kwa jina

- 13 lake : wasiozaliwa kwa damu, wala kwa kutaka mwili, wala kwa kutaka mwana Adamu, illa kwa Muungu.
- 14 Neno akawa mwili, akaketi kwetu, tukauona utukufu wake, utukufu kama wake Mwana wa pekee wa Baba, aliyejaa neema na kweli.
- 15 Yohana akimshuhudia, amelia akisema, Ndiye niliyemnenea, Ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu, kwani alikuwa wa kwanza wangu.
- 16 Katika kujaa kwake sisi tumepokea sote, na neema
17 juu ya neema. Kwani torati imetolewa kwa Musa;
18 neema na kweli zimekuwa kwa Isa Masiya. Muungu hakuonekana na mtu po pote; Mwana wa pekee, aliye naye kifurangi mwa Baba, ndiye afasiriye.
- 19 Ushahidi wa Yohana ndio huu, Wayahudi wali-popeleka wakohani na Walawi, wamwulize, Wewe nani?
20 Akaungama, wala hakukana, akaungama, Mimi siye
21 Masiya. Wakamwuliza, Nini tena? Weye Eliya? Akanena, Siye. Wewe nabii yule? Akanena, La.
- 22 Wakamwambia, U nani? tuwape majibu waliotupeleka. Wajisemeaje?
- 23 Akasema, Mimi sauti yake aliaye nyikani, Fanyizeni njia yake Bwana, kama alivyonena nabii Isaya.
- ²⁴₂₅ Nao waliopelekwa walikuwa wa Mafarisayo. Wakamwuliza, wakamwambia, Mbona wabatiza, usipokuwa Masiya, wala Eliya, wala nabii yule?
- 26 Yohana akawajibu, akasema, Mimi nabatiza kwa
27 maji : kati mwenu amesimama msiyemjua ; ndiye ajaye nyuma yangu, aliyekuwa mbele yangu, wala mimi sista-hili nimlegezee ukanda wa kiatu.
- 28 Haya yalikuwa katika Betaniya ng'ambo ya pili ya Yardeni, alipokuwa Yohana akibatiza.
- 29 Siku ya pili akamtazama Isa akija kwake, akasema, Tazama Mwana kondoo wake Muungu, auchukuliaye
30 ulimwengu thambi! Ndiye niliyemnenea, Anakuja nyuma yangu mtu aliyekuwa mbele yangu : kwani
31 ndiye wa kwanza wangu. Wala mimi sikumjua ; lakini afunuliwe kwa Israeli, ndio sababu ya kuja kwangu, nikibatiza kwa maji.
- 32 Akashuhudu Yohana, akasema, Nimeona Roho iki-
33 shuka kama hua katika mbingu ikakaa juu yake. Wala mimi sikumjua : illa aliyenipeleka nibatize kwa maji, akaniambia, Utakayemwona Roho ikishuka ikikaa juu

yake, ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu. Mimi ni- 34
kaona, nikashuhudu kama ndiye Mwana wake Muungu.

Siku ya pili tena amesimama Yohana, na miongoni 35
mwa waanafunzi wake wawili.

Akamwangalia Isa akipita, akasema, Tazama Mwana 36
kondoo wake Muungu!

Waanafunzi wale wawili wakamsikia akinena, waka- 37
mfuata Isa. Isa akageuka akawaona wanafuata, aka- 38
waambia, Mwataka nini? Wakamwambia, Rabbi (ma-
ana yake Mwalimu), wakaa wapi? Akawaambia, Njo- 39
oni mwone. Wakaja wakaona alipokaa, wakakaa
kwake siku ile, ikiwa kama saa a kumi.

Andrea, nduguye Siman Petro, ndiye mmoja wao wa- 40
wili waliomsikia Yohana wakamfuata. Akamtafuta 41
kwanza ndugu yake yeye Siman, akamwambia, Tume-
mwona Masiya, iliyofasirika, Aliyetiwa mafuta (*Khristo*).
Akamleta kwa Isa. Isa akamwangalia akanena, Ndiwe 42
Siman wa Yunus: utaitwa Kefa, maana yake Jiwe
(*Petro*).

Siku ya pili akataka kutoka kwenda katika Gali- 43.
laya, akamkuta Filipino: Isa akamwambia, Nifuata.

Naye Filipino alikuwa wa Betsaida katika mji wa 44.
Andrea na Petro. Filipino akamkuta Natanael akamwa- 45
mbia, Musa katika torati na nabii waliomwandikia tu-
memwona, Isa mwanawe Yusuf aliye wa Nazareti.

Akamwambia Natanael, Katika Nazareti yamkini 46.
kuwa kitu kilicho chema?

Filipo akamwambia, Njoo uone.

Isa akamwona Natanael akija kwake, akamnenea, Ta- 47
zame Mwisraeli wa kweli, wala kwake hakuna hila.

Akamwambia Natanael, Umepataje kunijua? 48.

Akajibu Isa akamwambia, Kabla hujaambiwa na Fi-
lipo, ukiwa chini ya mtini, nimekuona.

Natanael akajibu, akamwambia, Rabbi, ndiwe Mwana 49
wa Muungu, ndiwe mfalme wa Israeli.

Akajibu Isa akamwambia, Kwa kukwambia, nime- 50
kuona chini ya mtini, unasadiki? utayaona makuu
kuliko haya. Akamwambia, Amin, amin, nawaambia, 51
halafu mtaona mbingu zikifunuka, na malaika za Mu-
ungu wanapanda na wanashuka juu yake Mwana wa
Adamu.

SIKU ya tatu palikuwa arusi katika Kana ya Ga- 2

- 2 lilaya; mama yake Isa alikuwako: Isa akaitwa na waanafunzi wake kwa arusi.
- 3 Hatta mvinyo ukipunguka, mama wake Isa akamwambia, Hawana mvinyo.
- 4 Isa akamwambia, Nina nini nawe, mwanamke? saa yangu haijafika.
- 5 Mama wake akawaambia wangoje, Atakavyowaambia mfanye.
- 6 Palikuwako makasiki sita ya mawe kwa kutakasa
- 7 kwao Wayahudi, ya vipimo viwili ao vitatu. Isa akawaambia, Jalizeni masiki ya maji; wakayajaliza
- 8 kabisa. Akawaambia, Tekeni mkachukue kwa mkuu wa meza. Wakachukua.
- 9 Mkuu wa meza alipouonja maji yalikuwa mvinyo, wala hakujua umetokako (lakini wangoje wakajua walioyateka maji), mkuu wa meza akamwita bwana
- 10 arusi, akamwambia, Killa mtu hutoa kwanza mvinyo ulio mwema, na watu walipokunywa, ule ulio thaifu: wewe umeuweka ulio mwema hatta sasa.
- 11 Mwanzo huu wa miujiza akafanya Isa katika Kana ya Galilaya, akauonyesha utukufu wake; waanafunzi wake wakamwamimi.
- 12 Baadaye akashuka hatta Kapernaum, yeye na mama wake, na ndugu, na waanafunzi wake, wakakaa huko siku zisizo nyingi.
- 13 Ikakaribu Pasaka ya Wayahudi, Isa akapanda
- 14 hatta Yerusalemi. Akaona katika hekalu waliokuza ng'ombe na kondoo na njiwa, nao wavunjao fetha waki-
15 kaa kitako. Akafanya mjeledi kwa kambaa akawafukuza katika hekalu, nazo kondoo na ng'ombe, akazimwaga pesa za wavunja fetha akazipindua meza zao.
- 16 Akawaambia wakuza njiwa, Chukueni hizi; msifanye nyumba ya Baba yangu nyumba ya biashara.
- 17 Waanafunzi wakakumbuka kama imeandikwa, Uwivu wa nyumba yako umenila.
- 18 Wayahudi wakajibu wakamwambia, Ishara gani utonyayo, ufanye haya?
- 19 Isa akajibu akawaambia, Haribuni hekalu hili, nami kwa siku tatu nitalifanyiza.
- 20 Wayahudi wakasema, Miaka arobaini na sita hekalu hili lilikuwa katika kujengwa, nawe utalifanyiza kwa siku tatu?

Naye amelinena hekalu la mwili wake. Hatta alipo-²¹₂₂
fufuka katika wafu waanafunzi wake wakakumbuka
kama amenena haya; wakayaamini maandiko, na neno
alilolinena Isa.

Alipokuwa katika Yerusalemi kwa Pasaka kwa siku 23
kuu, wengi wakaliamini jina lake wakiziona ishara ali-
zozifanya. Isa hakujiaminisha kwao, kwani akawajua 24
wote, wala hakuhitaji mtu amshuhudie mtu, kwani aka- 25
yajua yaliyomo katika watu.

PALIKUWA na mtu wa Mafarisayo, jina lake Niko- 3
demo, mkuu wa Wayahudi. Huyu akamjia Isa usiku, 2
akamwambia, Rabbi, twakujua mwalimu umetoka kwa
Muungu, kwani hawezi mtu kuzifanya ishara uzifa-
nyazo wewe, asipokuwa Muungu naye.

Isa akamwambia, Amin, amin, nakwambia, asipoza- 3
liwa katika juu hawezi mtu kuuona ufalme wa Mu-
ungu.

Akamwambia Nikodemo, Apateje kuzaliwa akiwa 4
mzee? hawezi kuingia mara ya pili tumboni mwa ma-
maye wala kuzaliwa.

Isa akamwambia, Amin, amin, nakwambia, asiyeza- 5
liwa kwa maji na Roho, hawezi kuingia katika ufalme
wa Muungu. Uliozaliwa kwa mwili ni mwili, na iliyo- 6
zaliwa kwa Roho ni roho. Usitaajabu nikikwambia, 7
hamna buddi mzaliwe katika juu. Upepo huvuma upe- 8
ndapo, unasikia sauti yake, illa hujui wala utokako wala
uendako: vivyo na killa aliyezaliwa kwa Roho..

Nikodemo akajibu, akamwambia, Yawezaje kuwa 9
haya?

Isa akajibu akamwambia, Ndiwe mwalimu wa Israeli, 10
wala huyajui haya? Amin, amin, nakwambia, twaya- 11
nena tuyajuayo, twashuhudu tuliyoyaona, wala hamku-
bali ushahidi wetu. Usiposadiki nikwambiapo mambo 12
ya ulimwengu, upateje kusadiki nikikwambia mambo
ya mbinguni? Hapana aliyepanda mbinguni illa aliye- 13
shuka mbinguni, ndiye Mwana wa Adamu aliye naye
mbinguni. Kama Musa alivyotweka nyoka katika 14
nyika, vivyo imempasa na Mwana wa Adamu atwekwe,
amwaminiye yote asipotee, illa apate uzima wa milele. 15
Muungu ameupenda ulimwengu, hatta akamtoa Mwana 16
wake wa pekee, amwaminiye yote asipotee, illa apate
uzima wa milele. Muungu hakumleta Mwana wake 17

katika ulimwengu auhukumie ulimwengu, lakini uli-
 18 mwengu upate kuokoka naye. Amwaminiye hahuku-
 miwi: asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sa-
 babu hakuamini kwa jina lake Mwana wa pekee wa
 19 Muungu. Ndio hukumu, nuru imekuja ulimwenguni,
 nao watu wamependa giza kuliko nuru, kwa sababu ya
 20 kuwa matendo yao mabaya. Killa ayatendaye yasiyo-
 faa huchukizwa na nuru, wala haji kwa nuru, matendo
 21 yake yasinenewe. Afanyaye kweli huja kwa nuru, ma-
 tendo yake yaonekane, kama yametendeka kwa Mu-
 ungu.

22 Baadaye alikuja Isa na waanafunzi wake katika
 inchi ya Uyahudi, akakaa huko pamoja nao, akibatiza.

23 Pakawa na Yohana akibatiza kwa Enon karibu na
 Salim, kwa sababu yako maji tele; wakaja, wakabatizwa.

24 Kwani Yohana hajatiwa gerezani.

25 Yakawa maulizo kati ya waanafunzi wake Yohana na

26 Wayahudi juu ya kutakasa. Wakaja kwa Yohana
 wakamwambia, Rabbi, yule aliyekuwa pamoja nawe
 ng'ambo ya Yardeni, uliyemshuhudia, abatiza, na wote
 wamjia.

27 Yohana akajibu akasema, Hawezi mtu kupokea neno

28 asipopewa mbinguni. Ndinyi mashahidi kama nime-
 sema, Mimi siye Masiya, illa nimepelekwa mbele yake.

29 Mwenyi mchumba ndiye bwana arusi: rafiki yake
 bwani arusi, asimamaye akimsikia, hufurahi furaha kwa
 sauti yake bwana arusi; ndiyo furaha yangu iliyoni-

³⁰
³¹ pata. Yeye atazidi, mimi nitapungua. Ajaye katika
 juu ni juu ya yote; aliye wa katika inchi ni wa inchi,
 ayasema yaliyo ya inchi: ajaye katika mbingu ni juu ya

32 yote. Ayashuhudia aliyoyaona na aliyoyasikia, wala

33 ushahidi wake mtu hakubali. Aukubaliye ushahidi
 wake ametia muhuri yake kama Muungu ndiye mwenyi

34 kweli. Aliyempeleka Muungu husema maneno yake
 Muungu: kwani Muungu hatoi Roho kwa kipimo.

35 Baba ampenda Mwana, amempa vyote mkononi mwake.

36 Amwaminiye Mwana anao uzima wa milele: asiyemwa-
 mini Mwana hatauona uzima, lakini hasira ya Muungu
 yakaa kwake.

4 BWANA akijua kama Mafarisayo wamesikia kama
 Isa anafanya waanafunzi wengi akibatiza kuliko Yo-
 2 hana (akiwa Isa hakubatiza, illa waanafunzi wake),

akatoka katika Uyahudi akaenda zake tena hatta Gali- 3
laya. Ikampasa kupita katika Samaria. 4

Akaja mji wa Samaria ulioitwa Sukar, karibu na sha- 5
mba alilompa Yakob mwanawe Yusuf; kiko kisima 6
chake Yakob. Isa akachoka na kusafiri, akakaa kitako
kwa kisima, kama saa ya sita.

Mwanamke wa Samaria akaja ateke maji. Isa aka- 7
mwambia, Unipe ninywe. Waanafunzi wake wame- 8
kwenda mjini wanunue chakula.

Mwanamke Msamaria akamwambia, Gissi gani wewe 9
Myahudi wataka kunywa kwangu niliye mwanamke
Msamaria? Kwani Wayahudi hawazumgumzi na Wa-
samaria.

Akajibu Isa, akamwambia, Kama ungalijua karama 10
yake Muungu, naye nani akuambiaye, Nipe ninywe,
wewe ungalimtaka, naye angalikupa maji mazima.

Akamwambia mwanamke, Bwana, huna cha kutekea, 11
na kisima kimekwenda chini sana : umepataje maji ya-
liyo mazima? Wewe mkuu kuliko baba wetu Yakobo, 12
aliyetupa kisima hiki, akanywa huko yeye na waanawe,
na makundi yake?

Akajibu Isa, akamwambia, Killa anywaye maji haya 13
ataona tena kiu : anywaye maji yale nitakayompa, ha- 14
taona kiu hatta milele ; lakini maji nitakayompa yata-
kuwa ndani yake jicho la maji likichemkachemka hatta
uzima wa milele.

Akamwambia mwanamke, Bwana, unipe maji haya, 15
nisione kiu wala nisije hapa niteke.

Akamwambia Isa, Enenda umwite mumeo, ukaje 16
hapa.

Akajibu mwanamke, akasema, Sina mume. 17

Akamwambia Isa, Umesema vema, Sina mume :
umekuwa na waume watanu ; naye uliye naye sasa si 18
mumeo : haya uliyoyasema kweli.

Akamwambia mwanamke, Bwana, nakuona u nabii. 19
Baba zetu waliabudu katika mlima huu ; na ninyi 20
mwasema kama katika Yerusalemi ndipo mahali pali-
popasa kuabudu.

Akamwambia Isa, Mwanamke, uniamini, wakati una- 21
kuja, wasipomwabudu Baba katika mlima huu wala ka-
tika Yerusalemi. Ninyi mwaabudu msiyemjua : sisi 22
twamwabudu tuliyemjua : kwani wokovu u katika Wa-

- 23 yahudi. Lakini wakati unakuja, nao leo, waabuduo kweli wamwabudupo Baba kwa roho na yaliyo kweli :
- 24 kwani Baba awatafuta hawa waabuduo hivyo. Muungu Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu kwa roho na yaliyo kweli.
- 25 Akamwambia mwanamke, Najua kama Masiya anakuja, ndiye Aliyetiwa mafuta (*Khristo*) : atakapokuja yeye atatwambia yote.
- 26 Akamwambia, Ndimi, nisemaye nawe.
- 27 Marra hiyo wakaja waanafunzi wake, wakastaajabu kwamba akasema naye mwanamke : illa hakunena mtu, Wataka nini ? ao Unasemani naye ?
- 28 Mwanamke akauacha mtungi wake akaenda zake
- 29 mjini, akawaambia waanaume, Njoooni, mmwone mtu aliyeniambia niliyoyafanya yote : si huyu ndiye Masiya ? Wakatoka katika mji, wakaja kwake.
- 30 Nao waanafunzi walikuwa wakimwambia, Mwalimu,
- 31 ule. Akawaambia, Ninacho chakula nikile msichokijua ninyi.
- 32 Waanafunzi wakanena wao kwa wao, Mtu hakumletea chakula ?
- 33 Isa akawaambia, Chakula changu ndicho niyafanye
- 34 ayapendayo aliyenipeleka, nikaitimize kazi yake. Hamsemi, kama bado miezi minne, na mavuno yatawadia ? Nami nawaambia, Inueni macho, katazameni inchi, kama
- 35 nyeupe kwa mavuno leo hivi. Avunaye hutwaa mshahara, hukusanya mazao kwa uzima wa milele, apandaye
- 36 afurahiwe kama avunaye. Hivi na mfano ule wa kweli,
- 37 Mmoja hupanda, mwingineo avunaye. Mimi nimewapeleka, myavune msiyoyatendea kazi : wangine wametenda kazi, ninyi mmeingia katika kazi zao.
- 38 Wengi wa mjini humo wakamwamini, Wasamaria, kwa neno lake mwanamke, akishuhudu kwamba, Ame-
- 39 niambia niliyoyafanya yote. Wakija kwake Wasamaria wakamwomba akae nao ; akakaa huko siku mbili.
- 40 Wengi tena sana wakaamini kwa neno lake ; wakamwambia mwanamke, Hatuamini sasa kwa neno lako : kwani naswi tumesikia, tumejua kama kweli huyu ndiye Mwokozi wa ulimwengu, aliye Masiya.
- 41 Baada ya siku hizi mbili akatoka huko akaja ka-
- 42 tika Galilaya. Naye Isa akashuhudu kwamba nabii ka-
- 43 tika inchi yake hana heshima. Alipokuja katika Gali-

laya, Wagalilaya wakamkubali wakiwa wameyaona yote aliyoyafanya katika Yerusalemi katika karamu: kwani huenda hawa katika karamu.

Akaja tena Isa hatta Kana ya Galilaya, alipoyafanya 46 maji mvinyo. Palikuwa na diwani, mwana wake akawa hawezi katika Kapernaum. Huyu akisikia kama Isa ame- 47 kuja katika Uyahudi kufika Galilaya, akamjia akamtaka ashuke amponye mwana wake, kwani amekaribia kufa.

Akamwambia Isa, Msipoona ishara na miujiza, ha- 48 mwamini.

Diwani akamwambia, Bwana, ushuke kabla mtoto 49 wangu hajafa.

Akamwambia Isa, Enenda zako; mwanako yu hayi. 50

Mtu yule akaliamini neno alilomwambia Isa, akaenda. Akiwa katika kushuka, watumwa wake wakamkuta, 51 wakampa habari wakinena, Kijana chako yu hayi. Akawauliza saa alipokuwa hajambo. Wakamwambia, 52 Jana saa ya saba homa ikamwacha. Akajua baba 53 kama saa hiyo ndiyo alipomwambia Isa, Mwana wako yu hayi. Akaamini yeye na nyumba yake yote.

Hii ndiyo ishara ya pili aliyofanya Isa akija katika 54 Uyahudi hatta Galilaya.

BAADA ya haya karamu ya Wayahudi, Isa aka- 5 panda hatta Yerusalemi.

Iko katika Yerusalemi penyi kondoo birika, iliyoi- 2 twa Kiebrania Bethesda, yenyi matao matano. Huko 3 wakakaa makutano mengi ya watu wagonjwa, vipofu, vijiguu, waliopooza, wakingoja maji yachemke. Kwani malaika hushuka wakati wake katika birika 4 akayachemsha maji. Naye aliyeshuka kwanza baada ya kuchemka maji akapata afya, katika ugonjwa wake wo wote.

Palikuwa na mtu huko aliyekuwa na ugonjwa mi- 5 aka thelathini na minane. Isa akimwona amelazwa, 6 akajua kama wakati umekuwa mwingi, akamwambia, Wataka kupona?

Akamjibu mgonjwa, Bwana, sina mtu, maji yaki- 7 chemka, anitupe birikani: wakati nikija mimi mgine hushuka mbele yangu.

Akamwambia Isa, Ondoka, tweka godoro lako, uka- 8 ende. Marra akapona mtu yule, akatweka godoro lake, 9 akaenda.

- 10 Ndiyo ya sabato siku ile. Wayahudi wakamwambia yule aliyeponyeka, Sabato leo : si halali ulitweke godoro.
- 11 Akawajibu, Yule aliyeniponya ndiye aliyenambia, Tweka godoro lako ukaende.
- 12 Wakamwuliza, Yu nani aliyekwambia, Tweka godoro lako, ukaende? Naye aliyeponyeka hamjui nani, kwani Isa amepita, watu walioko wakiwa wengi.
- 14 Baadaye Isa akamwona katika hekalu, akamwambia, Angalia, umepona : usikose tena, lililo baya lisikupate.
- 15 Mtu yule akatoka, akawaambia Wayahudi kama
- 16 Isa ndiye aliyemponya. Kwa hiyo Wayahudi wakamfuata Isa, wakataka kumua, kwa sababu ameyafanya haya siku ya sabato.
- 17 Isa akawajibu, Baba yangu hutenda kazi hatta leo, nami naitenda.
- 18 Kwa hiyo wakazidi Wayahudi kutaka kumua, kwa sababu hakuivunja sabato tu, lakini akamnena Muungu baba yake yeye, akijifanya sawa na Muungu.
- 19 Akajibu Isa akawaambia, Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya neno peke yake, illa amwonavyo Baba avifanya : kwani afanyavyo Yeye, hivi na Mwana
- 20 huvifanya vivyo. Kwani Baba humpenda Mwana, humpwonya killa afanyalo : naye atazidi kumpwonya mambo
- 21 makuu, mpate kutaajabu. Kwani kama Baba alivyowafufua wafu, awafanyavyo hayi, vivyo na Mwana huwafanya hayi awapendao. Wala Baba hamhukumii mtu,
- 23 lakini amempa Mwana hukumu yote, wote wamheshimie Mwana kama wamheshimavyo Baba. Asiyemheshimia
- 24 Mwana hamheshimii Baba aliyempeleka. Amin, amin, nawaambia, alisikiaye neno langu, akimwamini aliyenipeleka, anao uzima wa milele, wala hataingia katika kuhukumiwa, lakini amepita katika kufa kuwa hayi.
- 25 Amin, amin, nawaambia, saa inakuja, hatta sasa ipo, waliokufa waisikie sauti yake Mwana wa Muungu,
- 26 nao wasikiao wawe hayi. Kwani kama Baba alivyo na uzima mwake, vivyo amempa Mwana kuwa na uzima
- 27 mwake, akampa nguvu afanye na hukumu, kwani yu
- 28 Mwana wa Adamu. Si taajabuni haya : saa inakuja, wote waliomo makaburini watakapoisikia sauti yake,
- 29 wataondoka, wale waliofanya vema kwa kiyama ya uzima, nao waliotenda viovu kwa kiyama ya kuhukumiwa.

Mimi siwezi kufanya neno mimi peke yangu : nisi- 30
kiavyo nahukumu, na hukumu yangu ndiyo yenyi haki ;
kwani siyataki niyapendayo mimi, illa ayapendayo ali-
yenipeleka.

Nikijishuhudia mwenyewe, ushahidi wangu sio wa 31
kweli. Mgine yule anishuhudiaye ; najua kama usha- 32
hidi anishuhudiao ndio mwenyi kweli. Mmempelekea 33
Yohana, akayashuhudia yaliyo kweli. Illa mimi siuku- 34
bali ushahidi wake mwana Adamu : nayasema haya
mpate ninyi kuokoka. Yeye alikuwa taa iliyowaka, 35
ikamwangaza ; nanyi mmependa kufurahiwa saa hiyo na
nuru yake. Mimi ninao ushahidi mkubwa kuliko wa 36
Yohana : kwani matendo niliyopewa na Baba niyati-
mize, matendo niyafanyayo mimi, yanishuhudia ya kwa-
mba Baba amenipeleka ; naye Baba aliyenipeleka ndiye 37
anishuhudiaye. Hamkumsikia kabisa sauti, wala ha-
mkumwona namna : wala hamnalo neno lake likikaa 38
ndani yenu, ikiwa hamkumwamini yule aliyewapelekea.

Tafuteni katika maandiko ; kwani mmeona ninyi 39
kuwa humo uzima wa milele : nayo ndiyo yanishuhu-
diayo. Wala hampendi kunijia, mpate kuwa na uzima. 40

Sikubali kusifiwa na watu, lakini nimewajua ninyi ⁴¹
kwani kumpenda Muungu hamnako ndani yenu. Mimi ⁴²
nimekuja kwa jina la Baba wangu, wala hamnikubali :
mgine akija kwa jina lake mwenyewe, huyu mtamku-
bali. Mpateje ninyi kuamini, mkikubali kusifiana, msi- 44
pozitaka sifa zitokazo kwake Muungu aliye wa pekee ?
Msithani kama mimi nitawashtaki kwa Baba. Yuko 45
awashtakiye, Musa mliyemtumainia. Mkimwamini 46
Musa, mniamini na mimi : kwani ameniandikia mimi.
Msipoyaamini aliyoyaandika yeye, mpateje kuyaamini 47
niyanenayo mimi ?

BAADAYE akaenda Isa ng'ambo ya pili ya bahari **6**
ya Galilaya ya Tiberia, makutano mengi wakamfuata, 2
wakizona ishara alizowafanyia walio wagonjwa. Aka- 3
panda Isa katika mlima akakaa huko pamoja na waana-
funzi wake. Imekaribia Pasaka, karamu yao Waya- 4
hudi.

Isa akiinua macho, akawaona kama makutano mengi 5
yanamjia, akamwambia Filipo, Tununue wapi mikate,
hawa wapate kula ? Akanena haya akimjaribu, akijua 6
mwenyewe atakavyofanya.

- 7 Filipo akamjibu, Mikate ya dinari miteen haiwatoshi, killa mtu atwae kidogo.
- 8 Akamwambia mmoja wa waanafunzi wake, Andrea
- 9 nduguye Siman Petro, Yupo hapa kijana, anayo mikate mitano ya shayiri na samaki mbili, lakini hizi nini kwa hawa wengi?
- 10 Isa akanena, Wakalisheni watu.
Majani mengi yako huko. Watu wakakaa kitako
- 11 kwa hesabu kama elfu tano. Isa akaitwaa mikate, akashukuru, akawatolea waanafunzi, na waanafunzi wale waliokaa kitako, na samaki vivyo hatta walivyotaka.
- 12 Waliposhiba akawaambia waanafunzi wake, Kusa-
- 13 nyeni makombo yaliyosalia, kitu kisipotee. Wakaya-kusanya, wakajaza vikapu thenashara kwa vidogo vya mikate ya shayiri walivyovisaza waliokula.
- 14 Watu wale wakiiona ishara aliyoifanya Isa, wakanena, Huyu ndiye nabii aliyekuwa atakuja ulimwenguni.
- 15 Isa akijua kama watakuja wamkamate wamfanye mfalme, akatoka tena hatta mlimani peke yake.
- 16 Wakati ukipita waanafunzi wake wakashuka baha-
- 17 rini, wakaingia chomboni, wavuke katika bahari hatta
- 18 Kapernaum. Imekuwa giza wala hakuwafikia Isa. Bahari ikatutuma kwa kuwa pepo nyingi zilizovuma.
- 19 Walipokwisha kuvuta kama stadio hamsi u asharini ao thelathini, wakamwona Isa akitembea juu ya bahari amekikaribia chombo : wakaogopa.
- ²⁰₂₁ Akawaambia, Ndimi; msioCOPE. Wakataka kumtwaa katika chombo: marra chombo kimefika inchi ng'ambo ya pili.
- 22 Siku ya pili yake makutano yaliyokaa upande wa pili wa bahari, wakiona kama hapana mashua nyingine huko, illa ile moja waliyopandia waanafunzi wake, na kama Isa hakuingia katika mashua pamoja na waanafunzi wake, lakini waanafunzi wake wameingia
- 23 mashuani peke yao (illa mashua nyingine zimekuja katika Tiberia, karibu na mahali walipoila mikate,
- 24 Bwana akishukuru) ; makutano wakiona kama Isa hako, wala waanafunzi wake, wkapanda katika vyombo, wakaja hatta Kapernaum wakimtafuta Isa.
- 25 Hatta wakimwona upande wa pili wa bahari wakamwambia, Rabbi, umekujaje hapa?
- 26 Isa akawajibu, akanena, Amin, amin, nawaambia,

mwanitafuta si kwa sababu mmeziona ishara, lakini kwa sababu mmeila mikate mkashiba. Msishughulike 27 kwa chakula kipoteacho, lakini kwa chakula kikaacho hatta uzima wa milele, atakachowapa Mwana wa Adamu: kwani Baba aliye Muungu amemia muhuri.

Wakamwambia, Tufanyeje, tushughulike kwa shughuli yake Muungu? 28

Isa akajibu akawaambia, Ndiyo shughuli yake Muungu, mmwamini aliyempeleka. 29

Wakamwambia, Ishara gani uifanyayo, tuone tuka kuamini? Unatendaje? Baba zetu walikula mana katika jangwa, kama yalivyoandikwa, Akawatolea chakula cha mbinguni, wale. 31

Isa akawaambia, Amin, amin, nawaambia, Musa siye aliyewatolea chakula kile cha mbinguni, lakini Baba yangu ndiye aliyewapa chakula cha mbinguni kilicho cha kweli. Kwani chakula cha Muungu ndiye yule aliyeshuka mbinguni, atoaye uzima katika ulimwengu. 33

Wakamwambia, Bwani, utupe sikuzote chakula hicho. 34

Akawaambia Isa, Mimi ndimi chakula cha uzima: ajaye kwangu, hataona njaa, naye aniaminiye hataona kabisa kiu. Illa nawaambia, kama mmeniona wala ha- akua kuamini. Killa aliyenipa Baba, huja kwangu, naye ajaye kwangu, simfukuzi nje. Kwani nimeshuka mbinguni nisiyafanye niyapendayo, illa ayapendayo aliyenipeleka. Ndiyo ayapendayo aliyenipeleka, killa niye- yepewa naye asipotee kabisa, illa nimfufue siku ya mwisho. Ndiyo ayapendayo aliyenipeleka, killa amwan- ngaliaye Mwana, akimwamini, apate uzima wa milele: nitamfufua mimi siku ya mwisho. 40

Wakamnung'unikia Wayahudi kwa sababu amesema, Ndimi niliye chakula kilichoshuka mbinguni. Wakanena, Siye Isa mwanawe Yusuf? hatuwajui babaye na mamaye? asemaje kwamba Nimeshuka mbinguni? 42

Isa akajibu, akawaambia, Msinung'unikiane. Hawezi mtu kunifuata Baba aliyenipeleka asipomvuta: nami nitamfufua siku ya mwisho. Imeandikwa kwa nabii, Wote watafundishwa na Muungu. Killa aliyesikia akajifunza kwa Baba huja kwangu. Hakuna aliyemwona Baba, illa aishiye kwa Muungu, huyu amemwona Baba. Amin, amin, nawaambia, aniaminiye anao uzima wa milele. Mimi ni chakula cha uzima. 48

49 Baba zenu waliila mana katika jangwa wakafa.
 50 Ndicho chakula kilichoshuka mbinguni, akilaye asife.
 51 Mimi ni chakula chenye uzima kilichoshuka mbinguni,
 akilaye chakula hiki aishi hatta milele. Na chakula nitakachotoa ndicho mwili wangu, nitakaoutolea uzima wa ulimwengu.

52 Wakashindana Wayahudi wao kwa wao, wakinena, Awezaje huyu kutupa mwili wake tule?

53 Akawaambia Isa, Amin, amin, nawaambia, msipoula mwili wake Mwana wa Adamu, mkainywa damu yake,
 54 hamna uzima kwenu. Aulaye mwili wangu na ainywaye damu yangu anao uzima wa milele, nami nitamfu-
 55 fua siku ya mwisho; kwani mwili wangu ndicho kilicho
 56 chakula, na damu yangu ndicho kilicho kinywa. Aulaye mwili wangu na ainywaye damu yangu hukaa
 57 ndani yangu, nami ndani yake. Kama Baba aliye hayi alivyoniipeleka, nami naishi kwa Baba, vivyo anilaye
 58 mimi huyu ataishi kwa mimi. Ndicho chakula kilichoshuka mbinguni: si kama baba zenu walivyoila mana, wakafa: akilaye chakula hiki ataishi hatta milele.

59 Akanena haya katika sunagogi, akifundisha katika Kapernaum.

60 Wengi walioyasikia, waanafunzi wake, wakanena, Neno hili gumu, nani awezaye kulisikia?

61 Akijua Isa kwa ndani kama waanafunzi wake walikuwa wakiyanung'unikia haya, akawaambia, Hili lime-
 62 wachukiza? ginsi gani, mkimwona Mwana wa Adamu
 63 akipanda huko aliko kwanza? Roho ndiyo ifanyayo hayi; mwili haufai neno: maneno niliyowaambia, ndi-
 64 yo roho na uzima. Lakini wako kwenu wasioamini. Kwani amejua Isa tangu mwanzo nani wasioamini, naye
 65 nani atakayemtoa. Akanena, Kwa hiyo, nikawaambia, kwamba hawezi mtu kunifuata asiyepewa na Baba yangu.

66 Tangu hapo wengi waanafunzi wake wakatoka katika
 67 nyuma yake, wala hawakutembea tena kumfuata. Isa akawaambia wathenashara, Hatta ninyi mwapenda kwen-
 nda zenu?

68 Akamjibu Siman Petro, Bwana, tumwendee nani?
 69 unayo maneno ya uzima wa milele, naswi tumeamini tukajua kama ndiwe Masiya, Mwanawe Muungu aliye hayi.

Akawajibu Isa, Mimi sikuwachagua ninyi thena- 70
shara, hatta wenu mmoja ni shetani?

Akamnenea Yuda wa Siman Iskariota, ndiye atakaye- 71
mtoa, akiwa mmoja wa wathenashara.

BAADAYE Isa akatembea katika Galilaya, wala 7
hakupenda kutembea katika Uyahudi, kwani wakataka
Wayahudi kumua.

Ikawa karibu karamu ya Wayahudi, ndiyo ya vi- 2
banda.

Wakamwambia nduguze, Ondoka hapo, kaenda zako 3
Uyahudi, waanafunzi wako wayaone matendo uyafa-
nyayo. Hafanyi mtu neno kwa siri, akitaka kuone- 4
kana. Ukiyafanya haya, ujifanye uonekane na uli-
mwengu. Wala nduguze hawakumwamini. 5

Akawaambia Isa, Saa yangu haijaja : saa yenu siku- 6
zote iko tayari. Hauwezi ulimwengu kuwachukia ni- 7
nyi; hunichukia mimi, kwani nimeushuhudia kama
matendo yake maovu. Ninyi mwipandie karamu; mimi 8
siipandii karamu hii bado; kwani saa yangu haijatimia.

Akinena haya akakaa katika Galilaya. Walipokwe- 9
nda nduguze, naye akaiendea karamu, si kwa wazi, illa 10
kama kwa siri.

Wayahudi wakamtafuta katika karamu, wakanena, 11
Yuko wapi huyu? Na manung'uniko mengi kwa 12
mambo yake katika makutano. Wangine wakasema,
Ni mwema. Wangine wakasema, Siyo, lakini huwa-
danganya watu. Wala mtu hakumnena kwa wazi, kwa 13
kuwaogopa Wayahudi.

Hatta kati ya karamu akapanda Isa katika hekalu 14
akafundisha. Wayahudi wakaajibu wakanena, Ajuaje 15
huyu elimu, asipofundishwa?

Akawajibu Isa akanena, Elimu yangusiyangu, illa yake 16
aliyenipeleka. Apendaye kuyatenda ayapendayo, ataijua 17
elimu, kwamba ndiyo ya Muungu, ao mimi nanena kwa
akili zangu tu. Anenaye kwa akili zake tu hutaka 18
kusifiwa mwenyewe; atakaye asifiwe aliyempeleka, ndiye
wa kweli, wala haiko kwake illa haki. Siye Musa ali- 19
yewapa torati, wala hakuna kwenu aitendaye torati?
Mbona mwataka kuniua?

Makutano wakajibu wakanena, Una wazimo: nani 20
atakaye kukuua?

Akajibu Isa akawaambia, Nimefanya tendo moja, 21

- 22 mkastaajabu nyote. Musa amewapa tohara (wala si
kwa Musa illa kwa babu), na siku ya sabato humtahiri
- 23 mtu. Mtu akipata kutahiriwa siku ya sabato, torati ya
Musa isivunjike, umeghathabika kwa sababu nimem-
- 24 ponya mtu kuwa mzima siku ya sabato? Msihukumu
kwa macho; hukumuni hukumu ya haki.
- 25 Wakanena baathi ya Wayerusalemi, Siye huyu wa-
26 mtakaye wamue? Angalie ananena kwa wazi, wala ha-
wamsemei neno. Wamejua kweli wakuu kama ndiye
- 27 Masiya? Lakini twamjua huyu aliko. Masiya ataka-
pokuja hamjui mtu aliko.
- 28 Akatoa sauti katika hekalu akifundisha Isa, akanena,
Mmenijua na mimi na huko niliko: wala sikuja kwa
shauri langu mimi, lakini ndiye mwenyi kweli aliyeni-
- 29 peleka, msiyemjua ninyi. Mimi nimemjua, kwani ni-
metoka kwake, naye ndiye aliyenipeleka.
- 30 Wakataka kumkamata: wala mtu hakumtia mkono
31 kwa sababu saa yake haijawadia. Wengi wa katika
makutano wakamwamini, wakanena, Masiya akija, atatoa
ishara kuliko huyu alivyofanya?
- 32 Wakawasikia Mafarisayo makutano wakiyanung'unia-
haya. Wakampelekea wakohani wakuu na Mafarisayo
asikari wamkamate.
- 33 Akanena Isa, Bado kidogo kwenu mimi, nitakwenda
34 zangu kwake aliyenipeleka. Mtanitifuta wala hamta-
niona, wala mimi nilipo hamtaweza ninyi kuja.
- 35 Wakaambiana Wayahudi, Atakwenda wapi huyu, sisi
tusimwone? Atakwenda kwao waliotawanyika katika
- 36 mataifa, atawafundisha mataifa? Neno gani hili alilo-
lisema, Mtanitifuta wala hamtaniona, wala mimi nilipo
ha'mwezi ninyi kuja?
- 37 Siku ya mwisho iliyo kuu ya karamu, akasimama Isa
akatoa sauti, akanena, Mtu akiona kiu, anijilie anywe.
- 38 Aniaminiye mimi, kama yamenena maandiko, mito ya
39 maji ya uzima itatoka katika matumbo yake. Akaise-
mea haya Roho watakayopewa wamwaminio: kwani
Roho Mtakatifu haiko bado, kwamba Isa hajatukuzwa.
- 40 Wengi wa katika watu wakayasikia maneno waka-
nena, Ndiye nabii, kweli. Wangine wakanena, Ndiye
- 41 Masiya. Wangine wakanena, Hatoki Masiya katika
42 Galilaya. Hayaneni maandiko kwamba katika wazao
wa Daud na katika Betlehem mji Daud alipo, Masiya

atatoka? Makutano yakatengwa kwa sababu yake. 43
Walikuwa kwao waliotaka kumkamata, lakini mtu ha- 44
kumtia mkono.

Wakaja asikari kwa wakohani wakuu na Mafarisayo, 45
hawa wakawaambia, Mbona hamkumleta?

Wakajibu asikari, Hapana mtu kabisa anenaye kama 46
mtu huyu.

Wakawajibu Mafarisayo, Hatta ninyi mkadanganyi- 47
ka? Mtu gani aliyemwamini katika wakuu, ao katika 48
Mafarisayo? Illa makutano haya wasioijua torati wa- 49
melaaniwa.

Akawaambia Nikodemo aliyemjia usiku, akiwa 50
mmoja wao, Sheria yetu humhukumu mtu, asipokuwa 51
kwanza amesikiwa, afanyayo yamejulikana?

Wakajibu wakamwambia, Nawe umetoka katika 52
Galilaya? Tafute, kaangalie, kwani nabii haondoki ka-
tika Galilaya.

Wakaenda zao killa mtu nyumbani kwake. 53

ISA akaenda mlima wa zeituni. 8

Hatta assubui mapema akaja hekaluni, watu wote 2
wakamjia; akakaa kitako akawafundisha.

Wakamletea waandishi na Mafarisayo mwanamke 3
aliyetwaliwa akizini, wakamweka kati, wakamwambia, 4
Mwalimu, mwanamke huyu ametwaliwa akiwa katika
kuzini. Bassi katika torati Musa alituamuru tuwapigie 5
mawe walio kama huyu: wewe wasemaje? Wakanena 6
haya wamjaribu, wapate kumshtaki.

Isa akainama akaandika kwa kidole chini. Wakikaa 7
wakimuliza, akajiinua akawaambia, Yule wenu asiye-
kosa amtupie jiwe la kwanza. Akainama tena akaa- 8
ndika chini.

Wale wakisikia, wakihukumiwa na moyo, wakatoka 9
mmoja mmoja, kwanza walio wazee hatta wa mwisho,
wakamwacha Isa peke yake, na mwanamke akiwa kati.

Akajiinua Isa asione mtu illa mwanamke, akamwa- 10
mbia, Wako wapi waliokushtaki? hapana aliyekuhukumu?

Akanena, Hapana, Bwana. 11

Akamwambia Isa, Wala mimi sikuhukumu: uende,
usikose tena.

Isa akasema nao tena akinena, Mimi ni nuru ya uli- 12
mwengu: anifuataye hatembezi gizani, lakini atapata
nuru ya uzima.

- 13 Wakamwambia Mafarisayo, Unajishuhudia ; ushahidi wako sio wa kweli.
- 14 Akajibu Isa akawaambia, Mimi nikijishuhudia, ushahidi wangu wa kweli : kwani nimejua nilikotoka, na niendako ; ninyi hamjui wala nilikotoka wala niendako.
- 15 Ninyi huhukumu kwa mwili ; mimi simhukumu mtu.
- 16 Hatta nikihukumu mimi, hukumu yangu ina kweli : kwani mimi si peke yangu, lakini mimi na Baba aliye-
- 17 nipeleka. Katika torati yenu imeandikwa, kwamba
- 18 watu wawili wakishuhudu maneno yao ya kweli. Mimi najishuhudia mwenyewe, na Baba aliyenipeleka amenishuhudia.
- 19 Wakamwambia, Baba yako yuko wapi ?
Akajibu Isa, Hamkunijua mimi wala Baba yangu : kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba yangu.
- 20 Maneno haya akayasema katika hazina, akifundisha hekaluni: wala mtu hakumkamata, kwani saa yake haijaja bado.
- 21 Akawaambia tena, Naenda zangu, nanyi mtanitafuta, mtakufa katika thambi zenu : niendako mimi, ninyi ha'mwezi kuja.
- 22 Wakanena Wayahudi, Atajiua ? kwamba anasema, Niendako mimi, ninyi ha'mwezi kuja.
- 23 Akawaambia, Ninyi wa chini ; mimi wa juu : ninyi
- 24 wa ulimwengu huu ; mimi si wa ulimwengu huu. Na-waambia, kwamba mtakufa katika thambi zenu : msi-poamini kama ndimi niliye, mtakufa katika thambi zenu.
- 25 Wakamwambia, Nani weye ?
- 26 Akawaambia Isa, Mwanzo nilivyonena kwenu. Ndiye mengi ninayo niwanenee, nikahukumu : lakini aliye-nipeleka ndiye wa kweli ; nami niliyoyasikia kwake, haya nayanena ulimwenguni.
- 27 Hawakujua kama amewanenea Baba.
- 28 Akawaambia Isa, Mtakapomtweka Mwana wa Adamu, ndipo mtakaponijua ndimi niliye, wala kwa shauri langu mimi sifanyi neno, illa alivyonifundisha Baba yangu,
- 29 ndivyo nisemavyo. Naye aliyenipeleka yupo pamoja nami : Baba hakuniacha peke yangu, kwani mimi naya-fanya sikuzote yampendezayo.
- 30 Akiyanena haya wengi wakamwamini.
- 31 Akawaambia Isa Wayahudi wale waliomwamini,

Mkikaa katika neno langu, mmekuwa waanafunzi wangu wa kweli, mtayajua yaliyo kweli, na yaliyo kweli 32 yatawafanya huru.

Wakamjibu, Sisi wazao wake Ibrahimu, wala hatukuwa kabisa watumwa wa mtu: wasemaje, kwamba Mta- 33 kuwa huru?

Akawajibu Isa, Amin, amin, nawaambia, killa afa- 34 nyaye thambi ni mtumwa wa thambi. Mtumwa hakai 35 nyumbani milele: mwana hukaa milele. Mwana akiwa- 36 weka huru, mtakuwa huru halisi. Nawajua kama wazao 37 wa Ibrahimu; lakini mwataka kuniua, kwani neno langu balina nafasi kwenu. Mimi nayanena niliyoyaona kwa 38 Baba yangu, nanyi huyafanya mliyoyaona kwa baba yenu.

Wakajibu wakamwambia, Baba yetu ndiye Ibrahimu. 39

Akawaambia Isa, Kama mngekuwa watoto wake Ibrahimu, mngeyafanya matendo yake Ibrahimu. Sasa 40 mwataka kuniua, mtu niliyewaambia yaliyo kweli, niliyoyasikia kwa Muungu: hakufanya hivi Ibrahimu. Ninyi huyafanya matendo ya baba yenu. 41

Wakamwambia, Sisi si waana wa haramu: tunaye baba mmoja, ndiye Muungu.

Akawaambia Isa, Kama Muungu angekuwa baba yenu, 42 mngenipenda mimi: kwani nalitoka kwa Muungu nikaja; wala sikuja kwa shauri langu mimi, lakini yeye amenipeleka. Mbona hamjui niyanenayo? Kwa sababu 43 ha'mwezi kulisikia neno langu. Ninyi wa baba, She- 44 tani; mwapenda kuzifanya tamaa za baba yenu. Yule tangu mwanzo muaji, wala hakukaa katika kweli, kwani kweli haimo ndani yake. Asemapo uwongo, husema yaliyo yake, kwani ni mwongo na baba yake. Mimi 45 nikinena kweli, hamniamini. Nani wenu anionyaye 46 mwenyi thambi? Nikinena kweli, mbona ninyi hamniamini? Aliye wa Muungu huyasikia aliyoyasema Muu- 47 ngu: kwa sababu hiyo hamsikii, kwa sababu sinyi wa Muungu.

Wakajibu Wayahudi, wakamwambia, Hatusemi vema, 48 kwamba Msamaria wewe, na una wazimo?

Akajibu Isa, Mimi sina wazimo; lakini namheshimia 49 baba yangu, nanyi hamniheshimii. Mimi sitaki nisi- 50 fiwe: yuko atakaye na ahukumuye. Amin, amin, na- 51 waambia, mtu akilishika neno langu, hataona kufa hatta milele.

- 52 Wakamwambia Wayahudi, Sasa tumejua kama una wazimo. Ibrahimu amekufa, na nabii; nawe wanena, Mtu akilishika neno langu hataonja kufa hatta milele.
- 53 Wewe mkuu kuliko baba yetu Ibrahimu, aliyekufa? nao nabii wamekufa: wajifanya nani?
- 54 Akajibu Isa, Nikijisifu mwenyewe, sifa yangu si neno: Baba ndiye anisifuye, mmnenaye kwamba Muungu wenu.
- 55 Wala hamkunjua; mimi nimemjua: nikisema simjui, nitakuwa kama ninyi, mwongo. Lakini nimemjua, ni-
- 56 kalishika neno lake. Ibrahimu baba yenu alipendezewa aione siku yangu, akaiona akafurahi.
- 57 Wakamwambia Wayahudi, Hujapata miaka hamsini, ukamwona Ibrahimu?
- 58 Akawaambia Isa, Amin, amin, nawaambia, mbele ya kuwa Ibrahimu nipo mimi.
- 59 Wakatwaa mawe wantupie: lakini Isa akajisetiri, akatoka katika hekalu, akienda kati yao, vivi akapita.
- 9 AKIPITA** akamwona mtu kipofu tangu kuzaliwa.
- 2 Wakamwuliza waanafunzi wake, wakanena, Rabbi, nani aliyekosa, huyu ao wazazi wake, azaliwe kipofu?
- 3 Akajibu Isa, Wala huyu hakukosa, wala wazazi wake,
- 4 illa yaonekane matendo ya Muungu kwake. Imenipasa kutenda matendo yake aliyenipeleka, ukiwa mchana:
- 5 usiku unakuja asipoweza mtu kutenda *neno*. Nikiwa katika ulimwengu ni nuru ya ulimwengu.
- 6 Akinena haya akatema mate, akafanyiza udongo na
- 7 mate, akampaka macho kipofu kwa udongo, akamwambia, Enenda, unawe katika birika la Siloam, tafsiri yake, Amepelekwa. Akaenda akanawa, akarudi akiona.
- 8 Majirani nao waliomwona zamani akiwa mwombaji,
- 9 wakanena, Si huyu aliyekaa akaomba? Wangine wakanena, Ndiye. Wangine, Amefanana naye. Yeye akanena, Ndimi.
- 10 Wakamwambia, Macho yako yamepataje kufumbuka?
- 11 Akajibu akanena, Mtu aitwaye Isa akafanya udongo akanipaka macho, akaniambia, Enenda hatta birika la Siloam ukanawe; nikaenda nikanawa, nikaona.
- 12 Wakamwambia, Yuko wapi huyu? Akanena, Sijui.
- 13 Wakamleta kwa Mafarisayo aliye kwanza kipofu.
- 14 Ikawa siku ya sabato, alipoufanya udongo Isa, akamfumbua macho.

Wakamwuliza tena Mafarisayo, ginsi aonaje. Aka- 15
waambia, Alinitia udongo machoni, nikanawa, naona.

Wakanena baathi ya Mafarisayo, Mtu huyu si wa 16
Muungu, kwani haishiki sabato. Wangine wakanena,
Awezaje mtu mwenyi thambi kufanya ishara kama hizi?
Wakatengwa.

Wakamwambia tena kipofu, Wewe wamsemeaje, kama 17
amekufumbua macho? Akanena, Ndiye nabii.

Wayahudi hawakusadiki kama alikuwa kipofu akaona, 18
hatta wakawaita wazazi wake aliyepata kuona. Waka- 19
wauliza, wakanena, Huyu ndiye mwana wenu, mmnenaye
kama alizaliwa kipofu? amepataje sasa kuona?

Wakawajibu wazazi wake wakanena, Twamjua huyu 20
ndiye mwana wetu, na kama alizaliwa kipofu: amepa- 21
taje kuona, hatujui; ao nani aliyemfumbua macho, sisi
hatujui: mtu mzima huyu; mwulizeni: atoe mwenyewe
habari zake. Wakanena haya wazazi wake, kwa sababu 22
wakawaogopa Wayahudi. Kwani siku ile wameamuru
Wayahudi kama killa amwungamaye Masiya, atolewe
katika sunagogi. Kwa hiyo wazazi wake wakanena, 23
Mtu mzima huyu; mwulizeni.

Wakamwita marra ya pili mtu aliyekuwa kipofu, wa- 24
kamwambia, Msifu Muungu: twamjua mtu huyu mwe-
nyi thambi.

Akajibu yule, Kama mwenyi thambi sijui: neno moja 25
nalijua, kama nikiwa kipofu nikaona.

Wakamwambia tena, Amekufanyiaje? amekufumbuaje 26
macho?

Akawajibu, Nimewaambia sasa hivi, wala hamkusikia: 27
nini tena mtakayo kusikia? Nanyi mwataka kuwa
waanafunzi wake?

Wakamtukana wakanena, Wewe mwanafunzi wake; 28
sisi waanafunzi wa Musa. Twajua kama kwa Musa 29
amenena Muungu: huyu hatumjui aliko.

Akajibu mtu akawaambia, Hii ndiyo ajabu, kama 30
ninyi hamjui aliko, naye amenifumbua macho. Twajua 31
kama Muungu hawasikii wenyi thambi, lakini mtu aki-
wa mcha Muungu, akiyafanya ayapendayo, huyu humsi-
kia. Tangu zamani haikusikiwa kama mtu amemfumbua 32
macho aliyezaliwa kipofu. Kama hangalikuwa huyu wa 33
Muungu, hangaliweza kufanya neno.

Wakajibu wakamwambia, Katika thambi tupu umeza- 34
liwa, nawe utufundishe sisi? Wakamtoa 'nje.

- 35 Akasikia Isa kama wamemtoa 'nje; akamkuta akamwambia, Wamwamini Mwana wa Muungu?
- 36 Akajibu huyu, akanena, Ni nani, Bwana, nimwamini?
- 37 Akamwambia Isa, Umemwona, naye asemaye nawe ndiye.
- 38 Akasema, Naamini, Bwana; akamsujudia.
- 39 Akanena Isa, Kwa hukumu nimekuja katika ulimwengu huu, wasioona waone, na waonao wawe vipofu.
- 40 Wakayasikia haya Mafarisayo waliopo naye, wakamwambia, Nasi vipofu?
- 41 Akawaambia Isa, Kama mngalikuwa vipofu, hamngalikuwa na thambi: sasa mwanena, Twaona, na thambi zenu haziondolewi.
- 10** AMIN, amin, nawaambia, asiyeingia kwa mlango katika zizi la kondoo, illa amepanda panginepo, ndiye 2 mwivi na mnyang'anyi. Aingiaye kwa mlango ndiye 3 mchungwa wa kondoo. Humfunulia huyu mngoje mlango, 4 jina, huzileta 'nje. Akizitoa kondoo zake, huenda mbele 5 yao, na kondoo humfuata, kwani wamjua sauti. Mgeni hawamfuati, lakini humkimbilii, kwani hawamjui sauti mgeni.
- 6 Mfano huu akawaambia Isa, wala hawakuyajua mambo aliyowanena.
- 7 Akanena tena Isa, Amin, amin, nawaambia, kwani 8 ndimi niliye mlango wa kondoo. Wote waliokuja mbele yangu wevi na wanyang'anyi, lakini kondoo hawakuwasikia sauti.
- 9 Ndimi niliye mlango: aingiaye kwa mimi ataokoka, 10 ataingia, atatoka, ataona malisho. Mwivi haji illa aibe, achinje, aharibu: mimi nimekuja wapate uzima, waka- 11 zidi kuupata. Ndimi niliye mchungwa aliye mwema. Mchungwa aliye mwema huweka uzima wake kwa ajili 12 yao kondoo. Aliye kwa mshahara wala asiye mchungwa, wala asiye mwenyi kondoo, akimwona mbwa wa mwitu anakuja, huwaacha kondoo, hukimbia, mbwa wa mwitu 13 huwakamata, huwatawanya kondoo. Aliye kwa mshahara hukimbia, kwa sababu kuwa kwa mshahara tu, 14 wala hawatunzi kondoo. Ndimi niliye mchungwa aliye mwema; nawajua walio wangu, nikajulika nao walio 15 wangu. Kama alivyonijua Baba, nami namjua Baba: 16 na uzima wangu nauweka kwa ajili yao kondoo. Na kondoo wangine ninao, wasio wa zizi hili: nao imenipasa

kuwaleta, nao watanisikia sauti ; litakuwa kundi moja
na mchungwa mmoja. Kwa hiyo Baba amenipenda, 17
kwani mimi nauweka uzima wangu niutwae tena. Ha- 18
pana aondoaye, illa mimi nauweka mwenyewe : ninazo
nguvu za kuuweka, ninazo nguvu za kuutwaa tena : na
amri hii nimepewa na Baba yangu.

Wayahudi wakatengwa tena kwa ajili ya maneno haya. 19
Wakanena wengi wao, Ana wazimo, akili zake zimepo- 20
tea ; mbona mwamsikia ? Wangine wakanena, Mwenyi 21
wazimo hasemi hivi. Wazimo waweza kumfumbua
macho kipofu ?

Ilikuwa siku ya kuwekea wakf katika Yerusalemi, na 22
wakati wa baridi. Isa akatembea hekaluni katika uku- 23
mbi wa Sulemani.

Wakamzunguka Wayahudi wakamwambia, Hatta lini 24
uishike roho yetu ? Ukiwa Masiya, twambie kwa wazi.

Akawajibu Isa, Nimewaambia, wala hamkuamini : 25
matendo niyafanyayo kwa jina la Baba yangu, haya ya-
nishuhudia. Lakini ninyi hamwamini, kwani sinyi wa 26
kondoo zangu, kama nilivyowaambia. Kondoo zilizo 27
zangu hunisikia sauti, nami nazijua, nao hunifuata, nami 28
nawapa uzima wa milele, wala hawatapotea milele,
wala mtu hawezi kuwanyang'anya mkononi mwangu.
Baba yangu aliyenipa mkuu kuliko wote, wala hawezi 29
mtu kunyang'anya katika mkono wake Baba yangu.
Mimi na Baba mmoja. 30

Wayahudi wakatwaa mawe tena wamtupie. Akawa- 31
jibu Isa, Nimewaonya matendo mema mengi ya Baba 32
yangu : kwa tendo lipi mwanitupia mawe ?

Wakamjibu Wayahudi, Kwa tendo jema hatukutupii 33
mawe, lakini kwa unajisi, na kwamba wewe mwana
Adamu hujifanya Muungu.

Akawajibu Isa, Haikuandikwa katika torati yenu, 34
Mimi nalisema, ndinyi miungu. Akiwanena miungu 35
waliopewa neno la Muungu (wala maandiko hayawezi
kuvunjwa), mwamwambia yule aliyemtakasa Baba aka- 36
mpeleka ulimwenguni, Wasema unajisi, nikinena, Ni
Mwana wake Muungu ? Nisipoyafanya matendo ya Baba 37
yangu msiniamini : nikiyafanya, msiponiamini, yaamini- 38
ni matendo, mpate kujua na kuamini kama ndani yangu
yu Baba, nami ndani yake.

Wakataka tena kumkamata ; akatoka katika mikono 39

- 40 yao. Akaenda zake tena ng'ambo ya pili ya Yardeni, mahali alipokuwa kwanza Yohana akibatiza, akakaa
- 41 huko. Wengi wakaja kwake, wakanena, Yohana hakufanya ishara: yote aliyomsema huyu Yohana ya kweli.
- 42 Wakamwamini huko wengi.
- 11** PALIKUWA na mtu hawezi, Lazaro wa Betania, 2 wa mji wao Maryamu na Martha nduguye. Ndiye Maryamu aliyemtia marhamu Bwana, akamfuta miguu kwa nyele zake, nduguye Lazaro alikuwa hawezi.
- 3 Ndugu wakampelekea wakinena, Bwana, umpendaye hawezi.
- 4 Akisikia Isa akasema, Ugonjwa huu si kwa kufa, illa kwa sifa yake Muungu, asifiwe Mwana wa Muungu kwa ajili yake.
- 5 Akawapenda Isa Martha na nduguye, na Lazaro.
- 6 Akisikia kama hawezi akakaa mahali hapo siku mbili; 7 hatta baadaye akawaambia waanafunzi, Turudi katika Uyahudi.
- 8 Wakamwambia waanafunzi, Rabbi, siku hizi Wayahudi walitaka kukutupia mawe; utarudi tena huko?
- 9 Akajibu Isa, Hazipo saa thenashara za mchana? Mtu akitembea mchana hajikwai, kwani anaona nuru ya uli-
- 10 mwengu huu; mtu akitembea usiku hujikwaa, kwani nuru haipo kwake.
- 11 Akasema haya, baadaye akawaambia, Lazaro rafiki yetu amelala; lakini naenda nimamshe.
- 12 Waanafunzi wakamwambia, Bwana, akilala, ataokoka.
- 13 Amekunena Isa kufa kwake; wale wakathani amenena kulala kwa usingizi.
- ¹⁴₁₅ Akawaambia Isa kwa wazi, Lazaro amekufa: nawafurahia ninyi, mpate kuamini, kama mimi siko huko; 16 illa twende kwake. Akawaambia Tomaso (aliyeitwa Pacha) waanafunzi wenzake, Twende na sisi, tufe pamoja naye.
- 17 Akija Isa akaona amekuwa siku nne katika kaburi. 18 Betania iko karibu na Yerusalemi kama stadio hamstahara. 19 Wakaja Wayahudi wengi kwao Martha na Maryamu wawatulize kwa ajili ya ndugu yao. Naye Martha akisikia kama Isa anakuja, akamwendea: Maryamu akakaa nyumbani.
- 21 Martha akamwambia Isa, Bwana, kama ungaliku- 22 wapo hapa, ndugu yangu hangalikufa. Illa hatta

sasa najua killa utakayotaka kwa Muungu, Muungu atakupa.

Isa akamwambia, Nduguyo atafufuka. Akamwambia ²³₂₄ Martha, Najua kama atafufuka katika ufufuo wa siku ya mwisho.

Akamwambia Isa, Mimi ni ufufuo, na uzima : aniami- 25 niye, akifa, atakuwa hayi ; na killa aliye hayi akiniamini 26 hafi milele. Wayaamini haya ?

Akamwambia, Yakini, Bwana : nimeamini kama 27 ndiwe Masiya, Mwana wake Muungu, ajaye katika uli- mwengu.

Akisema haya akaenda akamwita Maryamu nduguye 28 kwa siri, akisema, Mwalimu yuko, anakwita. Naye 29 akisikia akaondoka upesi akamjia.

Hajafika Isa katika mji, lakini yuko mahali alipo- 30 mkuta Martha. Wayahudi waliokuwa naye katika 31 nyumba wakamtuliza, wakimwona Maryamu kama ameondoka upesi akatoka, wakamfuata wakinena, Ana- kwenda kaburini alie huko.

Maryamu akija mahali alipo Isa akamwona, akamwa- 32 ngukia miguu, akimwambia, Bwana, kama ungaliku- wapo hapa ndugu yangu hangalikufa.

Isa akimwona analia, nao Wayahudi waliofuatana 33 naye wakilia, akakasirika rohoni akataabika, akasema, 34 Wapi mlipo'mweka ? Wakamwambia, Bwana, uje uta- zame.

Isa akatoa machozi. 35

Wakasema Wayahudi, Tazama ginsi alivyompenda. 36 Baathi wao wakasema, Hawezi huyu amfumbuaye macho 37 kipofu kufanya kama na huyu asife ?

Isa akikasirika tena moyoni akafika kaburini. Ndilo 38 paango, na jiwe limewekwa juu yake. Akanena Isa, 39 Ondoeni jiwe.

Akamwambia nduguye aliyekufa, Martha, Bwana, sasa ameoza, kwani amepata siku nne.

Akamwambia Isa, Sikukwambia kama ukiamini, uta- 40 iona sifa ya Muungu ?

Wakaliondoa jiwe alipolazwa aliyekufa. Isa akainua 41 macho yake juu akasema, Baba, nakushukuru ya kwa- mba umenisikia. Nami najua kama wanisikia sikuzote, 42 lakini kwa ajili ya makutano wazungukao, nimenena, wapate kuamini kama ndiwe uliyenipeleka.

- 43 Akisema haya akatoa sauti kubwa, Lazaro, ondoka
 44 'nje! Akatoka aliyekufa, akifungwa miguu na mikono
 kwa saanda, na uso wake umefungwa na lesu. Akawa-
 ambia Isa, Mfungueni, mwacheni aende zake.
- 45 Wayahudi wengi waliokuja kwa Maryamu wakaya-
 46 angalia aliyoyafanya wakamwamini. Wangine wao
 wakaenda kwa Mafarisayo wakawaambia aliyoyafanya
 Isa.
- 47 Wakakusanya wakohani wakuu na Mafarisayo ba-
 raza, wakanena, Tunafanyani? kwani mtu huyu anafa-
 48 nya ishara nyingi. Tukimwacha hivi wote watamwa-
 mini, nao Warumi watakuja wataondoa sisi na mahali
 na taifa.
- 49 Mmoja wao Kayafa, aliye mkohani mkuu mwaka
 50 huo, akawaambia, Ninyi hamjui neno, wala hamfikiri,
 kama imetupasa mtu mmoja afe kwa watu, taifa wote
 wasipotee.
- 51 Haya hakuyasema kwa akili zake yeye, lakini akiwa
 mwaka huo mkohani mkuu, akatabiri, kama Isa atakufa
 52 kwa taifa, wala si kwa taifa lile tu, illa watoto wa Mu-
 ungu waliotawanyika awakusanye pamoja.
- ⁵³
⁵⁴ Tangu siku ile wakafanya shauri wamue. Isa haku-
 tembea tena kwa wazi katika Uyahudi, lakini akatoka
 huko hatta mahali karibu na jangwa, hatta mji ulioitwa
 Efraim, huko akakaa na waanafunzi wake.
- 55 Ikakaribia Pasaka ya Wayahudi, wakapanda wengi
 hatta Yerusalemi katika inchi mbele ya Pasaka, waji-
 takase.
- 56 Wakamtafuta Isa, wakanena wao kwa wao wakisi-
 57 mama hekaluni, Mwaonaje? haijii karamu? Wametoa
 wakohani wakuu na Mafarisayo amri, kama mtu aki-
 mjua alipo aonyeshe, wapate kumkamata.
- 12** HATTA siku sita mbele ya Pasaka, Isa akaja Betania,
 2 Lazaro alipo aliyekufa, aliyemfufua katika wafu. Wa-
 kamfanyia huko chakula cha jioni; Martha akangoja;
 3 Lazaro akawa mmoja wao waliojilaza naye. Naye
 Maryamu akitwaa ratli ya marhamu ya nardo safi yenyi
 thamani nyingi akampaka Isa miguu, akaifuta miguu
 yake kwa nyele zake; nyumba ikajaa manukato yake
 marhamu.
- 4 Akanena mmoja wa waanafunzi wake, Yuda wa Si-
 5 man Iskariota, atakayemtoa, Mbona marhamu hii hai-

kuzwa kwa dinari thelatha mia, wakapewa masikini? Akayasema haya, si kwa sababu anawatunza masikini, 6 lakini kwa kuwa mwivi, akawa na kifuko, akavichukua vilivyotiwa.

Akasema Isa, Mwache: ameiwekea siku ya kuzikwa 7 kwangu. Kwani masikini mnao sikuzote kwenu; mimi 8 sikuzote hamnami.

Makutano mengi wakamjua Isa yuko, wakaja, si kwa 9 ajili yake Isa tu, lakini wamwone na Lazaro, aliyefufuka katika wafu. Wakafanya shauri wakohani wakuu 10 wamue na Lazaro, kwani kwa ajili yake Wayahudi 11 wengi wakatoka wakamwamini Isa.

Siku ya pili yake makutano mengi wakija katika 12 karamu, wakisikia kama Isa anakuja Yerusalemi, wa- 13 kayatwaa majani ya mitende wakatoka wamwone, wakatoa sauti, Hosanna: amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana, ndiye Mfalme wa Israeli.

Isa akimwona mwana punda akampanda, kama yali- 14 vyoandikwa, Usiogope, binti Sayuni: tazama Mfalme 15 wako anakuja, amempanda mtoto wa punda.

Mambo haya hawakuyajua mwanzo waanafunzi wake; 16 illa alipotukuzwa Isa, ndipo walipokumbuka kama haya ndiyo aliyoandikiwa, nayo ndiyo waliyomfanyia.

Wakamshuhudia makutano walioko naye, kama ame- 17 mwita Lazaro katika kaburi, akamfufua katika wafu. Kwa sababu hiyo wakamjia makutano, kwani wame- 18 sikia kama ameifanya ishara hiyo.

Mafarisayo wakasema wao kwa wao, Angalieni ginsi 19 tusivyofaa neno: tazama, ulimwengu anamfuata.

Walikuwako na Wayonani katika wao waliokuja wa- 20 abudu wakati wa karamu. Wakamjia Filipino aliye wa 21 Betsaida ya Galilaya, wakamuliza wakimwambia, Bwana, twataka kumwona Isa. Akaja Filipino akamwa- 22 mbia Andrea, na Andrea na Filipino wakamwambia Isa.

Isa akawajibu akisema, Saa imefika atukuzwe Mwana 23 wa Adamu. Amin, amin, nawaambia, mbegu ya ngano 24 isipoanguka katika inchi ikafa, hukaa peke yake: ikifa hutoa mazao mengi. Aipendaye nafusi yake ata- 25 ipoteza, naye aichukiaye nafusi yake katika ulimwengu huu ataihifathi kwa maisha ya milele. Mtu akini- 26 ngoja, anifuate; nami nilipo, huko atakuwa na mngoje wangu: mtu akiningojea, Baba atamheshimu. Leo na- 27

fusi yangu imetaabika ; niseme nini? Baba, uniokoe katika saa hii : lakini kwa ajili hiyo nimekuja hatta saa 28 hii. Baba, ulitukuze jina lako.

Ikaja sauti katika mbinguni, Nimetukuza, na tena nitatukuza.

29 Makutano waliosimama wakasikia wakanena, Imekuwa ngurumu. Wangine wakanena, Malaika amesema naye.

30 Akajibu Isa akasema, Sauti hii haikuwa kwa ajili 31 yangu, illa yenu. Hukumu sasa iko ulimwenguni humu : mkuu wa ulimwengu huu sasa atatupwa 'nje.

32 Nami nikitwekwa katika inchi nitavuta kwangu 33 vyote. Akanena haya akiionya mauti atakayoifia.

34 Wakamjibu makutano, Sisi tumesikia katika torati kama Masiya hukaa milele : gissi gani wanena wewe, kama imempasa Mwana wa Adamu kutwekwa? nani huyu Mwana wa Adamu?

35 Akawaambia Isa, Bado wakati si mwingi nuru iko kwenu : tembeeni mkiwa na nuru, giza lisiwashike : 36 naye atembeaye katika giza hajui aendako. Mkiwa na nuru, iaminini nuru, mpate kuwa waana wa nuru.

Akasema haya Isa, akaenda zake akijificha wasi- 37 mwone. Akiwa amezifanya ishara nyingi hivi mbele 38 yao, hawakumwamini, neno la Isaya nabii litimike alilolisema, Bwana, yu nani aliyezisadiki habari zetu, na 39 mkono wake Bwana amefunuliwa nani? Kwa hiyo hawakuweza kuamini, kwani akasema tena Isaya, 40 Amewapofua macho, akawafanya moyo mgumu, wasione kwa macho, wasifikiri kwa moyo, wageuke, niwaponye. 41 Ndiyo aliyoyasema Isaya, alipouona utukufu wake, aka- mnena.

42 Hatta na miongoni mwa wakuu wengi wakamwa- mini, lakini kwa ajili ya Mafarisayo, hawakumwungama, 43 wasitolewe katika sunagogi. Wakazipenda sifa za watu kuliko sifa yake Muungu.

44 Isa akatoa sauti akasema, Aniaminiye, haniamini 45 mimi illa aliyenipeleka : aniangaliaye mimi humwa- 46 ngalia aliyenipeleka. Nimekuja nuru katika ulimwe- 47 ngu, killa aniaminiye asikae gizani. Naye ayasikiaye niyasemayo, asiyeyashika, mimi simhukumu, kwani sikuja niuhukumu ulimwengu, lakini niuokoe ulimwe- 48 ngu. Anikataaye, asiyeyakubali niyasemayo, anaye

ambukumuye : neno nililosema, ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho. Kwani mimi sikusema kwa shauri 49 langu tu ; lakini aliyenipeleka Baba, huyu akanipa amri ninenavyo na nisemavyo ; nami najua kama amri 50 yake ndiyo uzima wa milele. Niyasemayo mimi, alivyoniambia Baba, ndivyo nisemavyo.

KABLA ya karamu ya Pasaka, akijua Isa kama saa 13 yake imekuja apite katika ulimwengu huu kwenda kwa Baba, akiwa amewapenda walio wake katika ulimwengu, akawapenda hatta mwisho.

Chakula cha jioni kilipokuwa, shetani amemia moyoni Yuda wa Siman Iskariota amtoe ; akijua Isa 3 kama Baba amempa vyote mikononi mwake, na kama ametoka kwa Muungu, akawa akimrudia Muungu, akaondoka katika chakula, akaweka mavazi, akatwaa 4 kitambaa akajifungia, akatia maji katika bakuli, akaja 5 awaoshe miguu waanafunzi, kuifuta kwa kitambaa alichofungwa.

Akaja kwa Siman Petro, naye akamwambia, Bwana, 6 wewe waniosha miguu ?

Akajibu Isa akamwambia, Nifanyalo hujui wewe sasa ; 7 utajua baadaye.

Akamwambia Petro, Huniوشي miguu hatta milele. 8

Akamjibu Isa, Nisipokuosha, huna sehemu nami.

Akamwambia Siman Petro, Bwana, si miguu yangu 9 tu, illa na mikono na kitwa.

Akamwambia Isa, Aliyeoshwa haimpasi kuoshwa illa 10 miguu, lakini yu safi pia. Nanyi ni safi, illa si wote.

Kwani akamjua atakayemtoa ; kwa hiyo akasema, Ham 11 safi wote.

Alipowaosha miguu, akayatwaa mavazi akajilaza tena, 12 akawaambia, Mwayajua niliyowafanyia ? Ninyi mwa-

niita Mwalimu na Bwana, mkanena vema, kwani ndimi. 13

Nikiwa nimewaosha miguu mimi Bwana na Mwalimu, 14 nanyi imewapasa kuoshana miguu. Nimewapa namna, 15

illi kama nilivyowafanyia mimi, nanyi mfanye. Amin, 16 amin, nawaambia, mtumwa si mkuu kuliko bwana wake,

wala aliyepelekwa kuliko aliyempeleka. Mkiyajua haya, 17 mtabarikiwa mkiyafanya. Siwanenei wote : najua ni-

liowachagua : lakini yaliyoandikwa yatimike, Alaye 18 chakula pamoja nami ameniinulia mguu wake. Sasa 19

nawaambia kabla haijawa, illi itakapokuwa mwamini

- 20 kana mimi ndiye. Amin, amin, nawaambia, amkaribishaye nimpelekaye hunikaribisha mimi, naye anikaribishaye mimi humkaribisha aliyenipeleka.
- 21 Akinena haya Isa akataabika roho, akasema, Amin, amin, nawaambia, kama mmoja wenu atanitoa.
- 22 Waanafunzi wakatazamana wakitiwa shaka nayo aliyoyanena. Alikuwa mmoja wa waanafunzi wake aki-
23 lazwa kifuani mwa Isa, aliyempenda Isa. Akampungia
24 huyu Siman Petro aulize nani aliyemnena. Akilazwa
25 huyu kifuani mwa Isa akanwambia, Bwana, yu nani?
- 26 Akajibu Isa, Ndiye nitakayempa mego nitakalochovyo. Naye alipochovyo mego akampa Yuda wa Siman Iska-
27 riota. Baada ya mego akanwingia Shetani. Akanwa-
28 mbia Isa, Ufanyalo, ulifanye upesi. Wala hakuna mtu
29 aliyelazwa aliyejua kwa jambo gani amemwambia. Wangine wakathani, akiwa Yuda anacho kifuko, kwamba Isa amemwambia, Nunue tunayotaka kwa karamu, ao
30 atoe kitu kwa masikini. Akipokea mego marra akatoka : ukawa usiku.
- 31 Alipotoka akanena Isa, Sasa ametukuzwa Mwana wa
32 Adamu, na Muungu ametukuzwa kwake. Muungu akitukuzwa kwake, Muungu atamtukuza mwenyewe, na
33 marra atamtukuza. Watoto, kidogo tena nipo nanyi. Mtanitifuta, na kama nilivyowaambia Wayahudi, kama Niendako ninyi hamwezi kuja, sasa nawaambia na ninyi.
- 34 Amri mpya nawapa, Mpendane ; kama nilivyowapenda
35 ninyi, nanyi mkapendane. Kwa hiyo watajua wote ndinyi waanafunzi wangu, mkiwa na kupendana ninyi kwa ninyi.
- 36 Akanwambia Siman Petro, Bwana, uendako wapi ?
Akamjibu Isa, Niendako, huwezi sasa kunifuata ; utanifuata baadaye.
- 37 Akanwambia Petro, Bwana, mbona siwezi kukufuata sasa ? nitaweka maisha yangu kwa ajili yako.
- 38 Akajibu Isa, Utaweka maisha yako kwa ajili yangu ? Amin, amin, nakwambia, jogoo hatawika kabla hujanikania marra tatu.
- 14 MSITAABIKE moyo : mmemwamini Muungu, mnia-
2 mini na mimi. Katika nyumba yake Baba yangu yako makao mengi : kama sivyo ningaliwaambia. Naenda niwa-
3 fanyizie nafasi. Nikienda nikawafanyizia mahali, nita-

rudi niwakaribishe kwangu, illi nilipo mimi, nanyi 'mwe. 4
Nami niendako mwajua, na njia mwajua.

Akamwambia Tomaso, Bwana, hatujui uendako; tuwe- 5
zaje kujua njia?

Akamwambia Isa, Ndimi niliye njia, na kweli, na 6
uzima; hamjii mtu Baba, illa kwa mimi. Kama mnga- 7
linijua mimi mngalimjua Baba yangu; na tangu leo
mwamjua, na mmemwona.

Akamwambia Filipino, Bwana, utuonyeshe Baba, itatu- 8
tosh.

Akamwambia Isa, Siku hizi nyingi nipo kwenu, 9
wala hukunjua, Filipino? Aliyeniona mimi amemwona
Baba. Usemaje, Tuonyeshe Baba? Huamini kama 10
mimi katika Baba, naye Baba ni katika mimi? Maneno
niwaambiayo siyasemi kwa shauri langu tu: naye Baba
akaaye katika mimi huyafanya matendo. Niaminini, 11
kama mimi katika Baba, na Baba katika mimi: ao nia-
minini kwa matendo yenyewe. Amin, amin, nawaambia, 12
aniaminiye, matendo niyafanyayo, naye atafanya; na
makuu kuliko haya atafanya, kwani mimi naenda kwa
Baba yangu. Na killa mtakalolitaka kwa jina langu, 13
nitalifanya, Baba atukuzwe katika Mwana. Killa mta- 14
kalolitaka kwa jina langu nitalifanya.

Mkinipenda mimi, zishikeni amri zangu. Nami nita- 15
mwomba Baba, naye atawapa Mfariji mgine akae kwenu
milele, Roho ya kweli, asiyemweza kukubali ulimwengu, 17
kwani haumwoni, wala haumjui. Ninyi mmemjua, kwa-
ni atakaa kwenu, atakuwa ndani yenu. Siwaachi ninyi 18
yatima; nitawajia. Baadaye kidogo ulimwengu hau- 19
nioni tena; ninyi mtaniona: kwani naishi mimi mtaishi
nanyi. Siku ile mtajua kama mimi katika Baba ya- 20
ngu, nanyi katika mimi, nami katika ninyi. Aliye 21
nazo amri zangu, akizishika, ndiye anipendaye. Ani-
pendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda,
nitajionyesha kwake.

Akamwambia Yuda (siye Iskariota), Bwana, itakuwaje, 22
utajionyesha kwetu wala si kwa ulimwengu?

Akajibu Isa akamwambia, Mtu akinipenda atalishika 23
neni langu, na Baba wangu atampenda, tutakuja kwake,
tutafanya makao kwake. Asiyenipenda hayashiki ma- 24
neni yangu. Nalo neno mlisikialo si langu mimi, illa
lake aliyenipeleka, Baba.

- ²⁵₂₆ Nimesema haya nikikaa kwenu. Naye Mfariji, Roho Mtakatifu, Baba atakayempeleka kwa jina langu, yule atawafundisha yote, na atawakumbusha yote niliyowaaambia.
- 27 Amani nawaachia, amani yangu nawapa : si ginsi ulimwengu utoavyo, mimi nawatolea. Msitaabike moyoni,
- 28 wala msiingiwe na hofu. Mmesikia nilivyowaambia, Naenda na kurudi kwenu. Kama mngalinipenda, mngalifurahiwa, kwamba namwendea Baba; kwani Baba
- 29 mkuu kuliko mimi. Na sasa nimewaambia kwanza, ili itakapokuwa mpate kuamini.
- 30 Siwasemei tena sana, kwani mkuu wa ulimwengu
- 31 unakuja, wala hana neno kwangu. Lakini ulimwengu upate kujua kama nimempenda Baba, na kama Baba alivyoni amuru, ndivyo nifanyavyo. Ondokeni, tushike njia.
- 15** MIMI ni mzabibu wa kweli, na Baba yangu ni mkuu
- 2 lima : killa tawi kwangu lisilozaa hutoa, na killa lizaalo
- 3 hutakasa, azidi kuzaa. Sasa ninyi mmekuwa safi kwa
- 4 neno nililowaambia. Kaeni kwangu, nami kwenu. Kama tawi haliwezi kuzaa peke yake, lisipokaa katika
- 5 mzabibu, wala ninyi msipokaa kwangu. Mimi ndimi mzabibu, ninyi matawi : akaaye kwangu nami kwake, huyu huzaa sana : kwani pasipo mimi ha'mwezi kufanya neno.
- 6 Asipokaa kwangu, hutupwa 'nje kama tawi limekauka : 7 huyakusanya huyatupa motoni, yateketee. Mkikaa kwangu, nayo nisemayo yakikaa kwenu, takeni mpenda-
- 8 vyo, mtapewa. Hivyo Baba yangu hutukuzwa, mzae matunda mengi, mkawe waanafunzi wangu.
- 9 Kama alivyoni penda Baba, nami nimewapenda ninyi :
- 10 mkae katika kupenda kwangu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika kupenda kwangu, kama mimi nilivyozishika amri zake Baba wangu, nikakaa katika kupenda
- 11 kwake. Haya nimewaambia, furaha yangu ikae kwenu, 12 furaha yenu ikatimie. Ndiyo amri yangu, mpendane, 13 kama nilivyowapenda ninyi. Hapana azidiye kupenda kuliko aiachaye maisha yake kwa ajili ya rafiki zake.
- ¹⁴₁₅ Ninyi rafiki zangu, mkifanya nilivyowaamuru. Siwaiti tena watumwa, kwani mtumwa hajui afanyavyo bwana wake : nimewanena rafiki, kwani yote niliyoyasikia kwa
- 16 Baba wangu, nimewajulisha ninyi. Ninyi hamkunichagua mimi, lakini mimi nimewachagua ninyi, nikawaa-

mria, mwende mkazae na mazao yenu yaka, illi mmtakalo
Baba kwa jina langu, mpewe naye. Haya nimewaamuru, 17
mpendane.

Ulimwengu ukiwachukia, jueni kama umenichukia 18
mimi kabla yenu. Mkiwa wa ulimwengu, ulimwengu 19
ungewapenda wake. Kwani sinyi wa ulimwengu, laki-
ni mimi nimewachagua katika ulimwengu, kwa hiyo
ulimwengu huwachukia. Kumbukeni neno nililowaa- 20
mbia, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake. Kama wa-
menifukuza mimi watawafukuza ninyi; wakilishika neno
langu, watalishika na lenu. Lakini haya yote wa- 21
tawafanyia kwa ajili ya jina langu, kwa sababu ha-
wakumjua aliyenipeleka. Kama singalikuja nikasema 22
nao, hawangalikuwa na thambi; sasa hawana neno la
kuzisetiri thambi zao. Anichukiaye mimi amemchukia 23
na Baba yangu. Kama singalifanya kwao matendo, 24
asiyoyafanya mtu mwingineo, hawangalikuwa na thambi;
sasa wameona wakachukia na mimi na Baba yangu. La- 25
kini litimike neno lililoandikwa katika torati yao, Wa-
menichukia bure. Atakapokuja Mfariji, nitakayewa- 26
pelekea katika Baba, Roho ya kweli, atokaye katika
Baba, huyu atanishuhudia mimi: atawashuhudia na 27
ninyi, kwamba tangu mwanzo mmekuwa na mimi.

HAYA nimewaambia, msijikwae. Watawatoa katika 16
masunagogi: hatta saa inakuja, killa awauaye ataona
kama amemfanyia Muungu ibada. Haya watayafanya 3
kwani hawakumjua wala Baba wala mimi. Lakini haya 4
nimewaambia, illi saa ikija myakumbuke, kama mimi
nimewaambia. Sikuwaambia haya kwanza, kwa sababu
ya kuwa mimi kwenu. Sasa naenda zangu kwake ali- 5
yenipeleka, wala mtu wenu haniulizi, Uendako wapi?
Lakini kwa sababu nimewaambia haya, moyo wenu 6
umejaa huzuni. Lakini nawaambia kweli, imewafaa 7
mimi niende zangu: mimi nisipokwenda, Mfariji hata-
wajia; nikienda, nitampeleka kwenu. Naye akija atau- 8
hakiki ulimwengu kwa thambi, na kwa haki, na kwa
hukumu. Kwa thambi, kwamba hawakuniamini mimi. 9
Kwa haki, kwamba naenda kwa Baba, wala ninyi ham- 10
nioni tena. Kwa hukumu, kwani mkuu wa ulimwengu 11
huu amehukumiwa.

Ninayo mengi tena niwaambie, lakini ha'mwezi kuya- 12
pokea sasa. Hatta atakapokuja yule Roho wa kweli, 13

atawaonya njia yao yaliyo kweli yote : kwani hatanena kwa shauri lake yeye, lakini atakayosikia ndiyo ataka-
 14 yonena ; naye atawaonya yatakayokuja. Yeye atanitukuza, kwani atatwaa katika yaliyo yangu, atawaonya
 15 ninyi. Yote anayo Baba ndiyo yangu : kwa sababu hii nimesema, atatwaa katika yaliyo yangu, atawaonya
 16 ninyi. Kidogo tena hamtaniona, baadaye kidogo mtaniona, kwa sababu naenda kwa Baba.

17 Wakasema waanafunzi wake wao kwa wao, Nini hii atunenayo, Kidogo tena hamtaniona, baadaye kidogo
 18 mtaniona, na, kwa sababu naenda kwa Baba? Wakanena, Nini hii anenayo, Kidogo? wala hatujui anenayo.
 19 Akajua Isa kwamba walitaka kumwuliza, akawaambia, Kwa nini mwatafuta ninyi kwa ninyi, kwamba nalisema, Kidogo tena hamnioni, baadaye kidogo mtaniona?
 20 Amin, amin, nawaambia, mtaomboleza na mtalia ninyi, ulimwengu utafurahi : ninyi mtaona huzuni,
 21 lakini huzuni yenu itakuwa furaha. Mwanamke azaapo, huona huzuni, kwani saa yake amekuja : hatta mtoto ulipozaliwa, hakumbuki tena mateso, kwa sababu ya
 22 furaha ya kuzaliwa mtu katika ulimwengu. Nanyi sasa mnayo huzuni : nitawaona tena, moyo wenu utafurahiwa, wala furaha yenu mtu hawaondolei. Siku ile hamtanitaka neno.

Amin, amin, nawaambia kwamba mtakayoyataka kwa
 24 Baba kwa jina langu, atawapa. Hatta leo hamkutaka neno kwa jina langu : takeni, mtapewa, furaha yenu itimike.

25 Haya nimewaambia kwa mifano : saa inakuja nisipo-waambia tena kwa mifano, lakini nitawapa kwa wazi
 26 habari zake Baba. Siku ile mtataka kwa jina langu, wala siwaambii kama mimi nitawaombea kwa Baba,
 27 kwani Baba huwapenda mwenyewe, kwani mmenipenda mimi mkaamini kama nimetoka kwa Muungu. Nalitokea kwa Baba, nikaja ulimwenguni ; nauacha tena ulimwengu, nikienda kwa Baba.

29 Wakamwambia waanafunzi wake, Sasa unasema kwa
 30 wazi, wala huneni mfano. Sasa tumejua kama wayajua yote wala huhitaji mtu akuulize : hivyo tumejua kwa-
 mba umetoka kwa Muungu.

³¹₃₂ Akawajibu Isa, Leo mmeamini? Angalia, saa inakuja, hatta sasa imekuja, mtakapotawanyika killa mtu

kwake, mtaniacha mimi peke yangu : wala si peke yangu, kwani Baba yuko pamoja nami.

Nimewaambia haya mpate amani kwangu. Katika 33
ulimwengu mtateswa : lakini 'mwe na moyo mkuu ;
mimi nimeushinda ulimwengu.

HAYA akanena Isa, akainua macho mbinguni akase- 17
ma, Baba, saa imefika ; umtukuze Mwana wako, Mwana
wako akutukuze : kama ulivyompa nguvu juu ya wote 2
wenyi mwili, illi wote uliomba awape uzima wa milele.
Ndio uzima wa milele, wakujue wewe Muungu wa 3
kweli wa pekee, naye uliyempeleka, Isa Masiya. Nime- 4
kutukuza katika inchi, nimemaliza kazi uliyonipa nii-
fanye. Sasa ukanitukuze wewe, Baba, kwa utukufu 5
ule niliokuwa nao pamoja nawe mbele ya kuwa uli-
mwengu.

Nimewaonyesha jina lako watu ulionipa katika uli- 6
mwengu. Walikuwa wako, ukanipa mimi, nao wameli-
shika neno lako. Sasa wamejua kama vyote ulivyonipa 7
vyako. Kwani maneno uliyonipa nimewapa wao ; nao 8
wamekubali, wakajua kweli kama nimetoka kwako,
wakaamini kama ndiwe uliyenipeleka.

Mimi nawaombea : siuombei ulimwengu, lakini wale 9
ulionipa, kwani ni wako, na vyote vyangu vyako, na 10
vyako vyangu ; nami nimetukuzwa kwao. Wala sipo 11
tena katika ulimwengu, nao hawa katika ulimwengu,
nami nakuja kwako. Baba mtakatifu, uwalinde katika
jina lako ulionipa, wawe mmoja, kama sisi. Nikiwa 12
nao ulimwenguni, nimewalinda katika jina lako : ulio-
nipa nimewahifathi, wala mtu wao hakupotea, illa mwana
wa upotevu, maandiko yatimike. Sasa naja kwako, na 13
haya nayasema ulimwenguni, wapate kuwa na furaha
yangu timilifu kwao. Mimi nimewapa neno lako, na 14
ulimwengu umewachukia, kwani hawa si wa katika
ulimwengu, kama mimi si wa katika ulimwengu. Si- 15
ombi uwaondoe katika ulimwengu, illa uwalinde katika
maovu. Sio wa ulimwenguni, kama mimi si wa uli- 16
mwenguni. Uwatakase katika kweli yako : neno lako 17
ndilo kweli. Kama ulivyonipeleka ulimwenguni, nami 18
nimewapeleka ulimwenguni, na kwa ajili yao mimi na- 19
jitakasa, watakasike na hawa katika kweli.

Siwaombei hawa tu, lakini nao watakaoniamini kwa 20
neno lao, wote wapate kuwa mmoja, kama wewe, Baba, 21

ndani yangu, nami ndani yako, wapate kuwa na hawa mmoja katika sisi, ulimwengu uamini kama ndiwe
 22 uliyenipeleka. Nami nimewapa utukufu ulionipa, wa-
 23 pate kuwa mmoja, kama sisi mmoja, mimi katika wao, na wewe katika mimi, watimilike katika umoja, ulimwengu ukajue kama ndiwe uliyenipeleka, ukawapenda wale, kama ulivyonipenda mimi.

24 Baba, ulionipa nataka nilipo mimi, nao wawe huko pamoja nami, wauone utukufu wangu ulionipa : kwani ukanipenda mimi mbele ya kufanyika ulimwengu.

25 Baba wa haki, ulimwengu haukujua ; mimi nikaku-
 26 jua, na hawa wamejua kama ndiwe uliyenipeleka. Nimewajulisha jina lako, nami nitajulisha : mapenzi uliyonipenda mimi yawe kwao, na mimi kwao.

18 AKISEMA haya Isa akatoka na waanafunzi wake, akivuka kijito cha Kedron, ilipo bustani, akaingia humo na waanafunzi wake.

2 Akapajua Yuda aliyemtoa mahali, kwani Isa marra
 3 nyingi huenda huko na waanafunzi wake. Naye Yuda akiwatwaa asikari, na watu wao wakohani wakuu na Mafarisayo, akaja huko na kandila, na mienge, na selaha.

4 Isa akiyajua yote yatakayompata akatoka akawaa-
 5 mbia, Mwamtafuta nani? Wakamjibu, Isa Mnazareti. Akawaambia Isa, Ndimi. Akasimama Yuda aliyemtoa
 6 pamoja nao. Akiwaambia, Ndimi, wakarudi nyuma wakaanguka chini.

7 Akawauliza tena, Mwamtafuta nani? Wakasema, Isa
 8 Mnazareti. Akajibu Isa, Nimewaambia kama ndimi:
 9 mkinitafuta mimi, waacheni hawa waende zao : litimike neno alilolisema, Wale ulionipa, sikumpoteza mmoja wapo wao.

10 Siman Petro akiwa na upanga akauvuta akampiga mtumwa wake mkohani mkuu akamkata sikio la kuume;
 11 na jina lake mtumwa Malko. Isa akamwambia Petro, Rudishe upanga katika ala : kikombe alichonipa Baba nisinywe ?

12 Asikari, na akida, na watu wao Wayahudi, wakam-
 13 twaa Isa, wakamfunga, wakamleta kwanza kwa Anna, ndiye mkwewe Kayafa aliye mkohani mkuu mwaka ule,
 14 ndiye Kayafa aliyewapa shauri Wayahudi, kama imepasa mtu mmoja apotee kwa ajili ya watu.

Akamfuata Isa Siman Petro, na mwanafunzi mgine : 15
 mwanafunzi yule amejuliwa naye mkohani mkuu, akai-
 ngia pamoja na Isa katika sebule yake mkohani mkuu.
 Petro akasimama mlangoi 'nje. Akatoka mwanafunzi 16
 yule wa pili aliyejuliwa naye mkohani mkuu, akasema
 naye mngoje mlango, akamleta ndani Petro. Akamwa- 17
 mbia Petro kijana aliye mngoje mlango, Nawe tena wa
 waanafunzi wake mtu huyu. Akanena, Siyo. Waka- 18
 simama watumwa na watumishi, wamefanya moto wa
 makaa, ikiwa baridi, wakakota moto. Katika hawa na
 Petro amesimama akakota moto.

Mkohani mkuu akamwuliza Isa kwa mambo ya waa- 19
 nafunzi wake na elimu yake.

Akamjibu Isa, Mimi nimesema kwa wazi na ulimwe- 20
 ngu, nimefundisha po pote katika masunagogi na katika
 hekalu, Wayahudi wote wakutanapo, wala kwa siri siku-
 sema neno. Mbona waniuliza mimi? Waulize walio- 21
 sikia, nini nilivyowaambia ; wale wajua niliyoyasema.

Akisema haya mtumishi mmoja aliyesimama karibu 22
 akampiga kofi Isa, akinena, Wamjibu hivi mkohani mkuu?

Akamjibu Isa, Kama nimesema vibaya, unishuhudie 23
 vibaya : kama vema, mbona wanipiga ?

Anna amempeleka amefungwa kwa Kayafa mkohani 24
 mkuu.

Akawa Siman Petro akisimama akikota moto, waka- 25
 mwambia, Nawe wa waanafunzi wake. Akakana, aka-
 sema, Siyo. Akanena mmoja wa watumwa wake 26
 mkohani mkuu na jamaa yake aliyemkata sikio Petro,
 Sikukuona naye katika bustani? Akakana tena Petro : 27
 marra akawika jogoo.

Wakamleta Isa katika kwa Kayafa hatta Preto- 28
 rio : ikawa mapema ; wala hawakuingia katika Preto-
 rio, wasipate unajisi, lakini waile pasaka. Akatoka 29
 Pilato kwao akasema, Mshtaka gani mlioleta juu ya mtu
 huyu ?

Wakajibu wakamwambia, Kama hangalikuwa huyu 30
 mtenda vibaya, hatungalimleta kwako.

Akawaambia Pilato, Mtwani ninyi, mkamhukumu 31
 kwa sheria yenu.

Wakamwambia Wayahudi, Si halali sisi tumwue mtu :
 neno lake Isa litimike alilonena akionya mauti ipi ata- 32
 kayokufa.

- 33 Akaingia tena katika Pretorio Pilato, akamwita Isa, akamwambia, Ndiwe Mfalme wa Wayahudi?
- 34 Akajibu Isa, Wanena haya kwa akili yako, ao wangine wamekwambia mambo yangu?
- 35 Akajibu Pilato, Mimi Myahudi? Taifa lako na wakohani wakuu wamekuleta kwangu: umefanya nini?
- 36 Akajibu Isa, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu: kama ungalikuwa wa ulimwengu huu ufalme wangu, watu wangu wangalipigana, nisitolewe kwa Wayahudi: bassi sasa ufalme wangu sio wa huku.
- 37 Akamwambia Pilato, Ndiwe mfalme?
Akajibu Isa, Wasema ndimi mfalme. Mimi nimezaliwa kwa hiyo, na kwa hiyo nimekuja ulimwenguni, niishuhudie iliyo kweli. Killa aliye wa kweli husikia sauti yangu.
- 38 Akamwambia Pilato, Kweli ndiyo nini?
Akisema haya akatoka tena kwa Wayahudi akawaambia, Sioni hatiya kwake kabisa. Ndiyo desturi yenu niwafungulie mmoja katika Pasaka: mwataka niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?
- 40 Wakatoa sauti tena wote wakinena, Si huyu, illa Barabba. Naye Barabba mnyang'anyi.
- 19** PILATO akamtwaa Isa akampiga. (2) Asikari wakasokota taji ya miiba wakamtia kitwani, na vazi jekundu
3 wakamvika, wakanena Salaamu, ewe Mfalme wa Wayahudi! wakampiga kofi.
- 4 Akatoka tena Pilato akawaambia, Angalia, namleta
5 'nje, mjue kama sioni hatiya kwake. Akatoka Isa amei-vaa taji ya miiba na vazi jekundu. Akawaambia, Tazama, ndiye.
- 6 Walipomwona wakohani wakuu na watu wao, wakatoa sauti wakinena, Sulibishe, msulibishe.
Akawaambia Pilato, Mtwani ninyi mkamsulibishe: mimi sioni hatiya kwake.
- 7 Wakamjibu Wayahudi, Sisi tunayo sheria, na kwa sheria yetu imempasa kufa, kwani akajifanya Mwana wa Muungu.
- 8 Aliposikia Pilato neno hili akazidi kuogopa, akaingia tena katika Pretorio, akamwambia Isa, Umetoka wapi? Wala Isa hakumtolea majibu.
- 10 Akamwambia Pilato, Husemi nami? hujui kama ninazo nguvu za kukusulibisha na kukufungua?

AkajibuIsa, Hungalikuwa na nguvu juu yangu ka- 11
bisa, usipopewa katika juu : kwa hiyo, aliyenitoa kwako
amezidi kuwa na thambi.

Baada haya Pilato akataka kumfungua. Wayahudi 12
wakalia wakinena, Ukimfungua huyu, wewe si mpenda
Kaisari : killa ajifanyaye mfalme, humnenea Kaisari.

Pilato akiyasikia maneno haya, akaleta Isa tena 'nje, 13
akakaa barazani mahali palipoitwa Sakafu ya mawe, kwa
Kiebrania Gabbatha. Ilikuwa siku ya kuandalia Pasa- 14
ka, kama saa ya sita. Akawaambia Wayahudi, Tazama,
Mfalme wenu.

Wakalia, Tweke, tweke, msulibishe. 15

Akawaambia Pilato, Nimsulibishe Mfalme wenu ?

Wakajibu wakohani wakuu, Hatuna mfalme illa Kai-
sari.

Akamtoa kwao, asulibiwe. 16

Wakampokea Isa wakamwondosha. Naye akiuchu- 17
kua msalaba wake akatoka hatta mahali paliponenwa Pa
kitwa, paliponenwa kwa Kiebrania Golgotha : wakamsu- 18
libisha huko, na pamoja naye wangine wawili, huko na
huko, na Isa katikati.

Akaandika anwani Pilato, akaweka katika msalaba ; 19
ikaandikwa,

ISA MNAZARETI,
MFALME WA WAYAHUDI.

Wakaisoma anwani hii Wayahudi wengi : kwani ma- 20
hali pa karibu na mji aliposulibiwa Isa : ikaandikwa
kwa Kiebrania, Kiyonani, Kirumi.

Wakamwambia Pilato wakohani wakuu wa Wayahudi, 21
Usiandike, Mfalme wa Wayahudi, lakini kama Amesema,
Ni Mfalme wa Wayahudi.

Akajibu Pilato, Niliyoyaandika nimeandika. 22

Asikari, walipomsulibisha Isa, wakayatwaa mavazi 23
yake, wakafanya sehemu nne, kwa killa asikari sehemu,
na kanzu yake : na kanzu yake haikushonwa, tangu juu
imefumwa pia. Wakasemana, Tusiikate ; tupige kura 24
iwe ya nani ; litimike andiko linenalo, Wakagawanya
mavazi yangu, wakapiga kura juu ya vao langu. Waka-
fanya haya asikari.

Wakasimama msalabani mwa Isa, mama yake, na ndu- 25
gu ya mama yake, Maryamu wa Klopa, na Maryamu
Magdalene. Isa akimwona mama yake, naye mwana- 26

- funzi aliyempenda akisimama, akamwambia mamaye,
 27 Mke, tazama, mwana wako. Akamwambia mwanafunzi,
 Tazama, mama wako. Tangu saa ile akamtwaa mwana-
 funzi kwake.
- 28 Baadaye akijua Isa kama sasa yote yametimia,
 29 andiko litimike akanena, Nina kiu. Chombo kika-
 wako chenye siki: wakajaza sifongo kwa siki, wakatia
 katika husopo, wakamletea kanwani.
- 30 Alipoitwaa siki Isa, akasema, Imekwisha. Aka-
 inama kitwa, akatoa roho.
- 31 Nao Wayahudi, miili isikae msalabani siku ya sabato,
 ikiwa maandalio, nayo kuu siku ile ya sabato, waka-
 mwomba Pilato, miguu yao ivunjwe, wakaondolewe.
- 32 Wakaja asikari, wakamvunja miguu wa kwanza, na wa
 33 pili aliyesulibiwa pamoja naye. Hatta wakija kwa Isa,
 wakamwona kama amekwisha kufa, hawakumvunja
 34 miguu, lakini asikari mmoja kwa mkuki akamchoma
 mbavu, marra ikatoka damu na maji.
- 35 Naye aliyeona akashuhudu, na shuhudu lake la kweli,
 naye anajua kama aliyeyanena ya kweli, mpate kuamini.
- 36 Yakawa haya andiko litimike, Hatavunjika mfupa.
 37 Na tena andiko la pili lanena, Watamtazama waliye-
 mechoma.
- 38 Baada ya haya, akamwomba Pilato Yusuf wa Ari-
 mathaya, akiwa mwanafunzi wake Isa, illa kwa siri
 kwa hofu ya Wayahudi, auchukue mwili wake Isa;
 akakubali Pilato. Akaja akauondoa mwili wa Isa.
- 39 Akaja na Nikodemo, aliyemjia kwanza usiku, akileta
 machanganyiko ya manemane na uudi kama ratli mia.
- 40 Wakautwaa mwili wake Isa, wakaufunga kwa saanda
 pamoja na manukato, kama desturi yao Wayahudi wa-
 kizika.
- 41 Iko mahali aliposulibiwa bustani, na katika bustani
 42 kaburi jipya pasimotiwa mtu. Humo, kwa sababu ya
 maandalio ya Wayahudi, kwani kaburi karibu, waka-
 'mweka Isa.
- 20 SIKU ya pili yake sabato, Maryamu Magdalene
 akaja mapema, ikiwa giza, hatta kaburini. Akaona jiwe
 2 limeondolewa katika kaburi. Akapiga mbio akaja kwa
 Siman Petro, na mwanafunzi yule mgine aliyempenda
 Isa, akawaambia, Wamemwondoa Bwana katika kabu-
 rini, wala hatupajui walipo'mweka.

Akaondoka Petro, na mwanafunzi yule wa pili, wa- 3
 kaja katika kaburi. Wakapiga mbio wote wawili, 4
 naye mwanafunzi wa pili akaenda upesi kuliko Petro,
 akatangulia kufika kaburini. Akainama akazona chini 5
 saanda, wala hakuingia. Akaja Siman Petro aki- 6
 mfuata, akaingia katika kaburi, akaziangalia saanda
 ziko chini, na kitambaa kilichokuwa kitwani mwake, 7
 sipo pamoja na saanda, lakini kimekunjwa mbali ma-
 hali pake. Akaingia na yule mwanafunzi aliyetangulia 8
 kufika kaburini, akaona, akaamini. Kwani hatta siku 9
 ile hawakulijua lililoandikwa, kwamba imempasa kufu-
 fuka katika wafu.

Wakaenda zao tena waanafunzi kwao. 10

Maryamu akasimama mbele ya kaburi 'nje yake 11
 akilia. Akiwa akilia akainama kaburini akaona ma- 12
 laika wawili wamevaa nyeupe, wakikaa mmoja kitwani,
 mmoja miguuni, ulipolazwa mwili wake Isa. Waka- 13
 mwambia hawa, Mke, walilia nini?

Akawaambia, Wamemwondosha Bwana wangu, wala
 sijui walipo'mweka.

Akisema haya akageuka nyuma, akamwona Isa aki- 14
 simama; hakunjua kama ndiye Isa. Akamwambia 15
 Isa, Mke, walilia nini? Wataka nini?

Naye akimthania ndiye mtunza bustani, akamwa-
 mbia, Bwana, kama umemchukua, nambia ulipo'mweka,
 nami nitamwondoa.

Akamwambia Isa, Maryamu! 16

Akageuka akamwambia, Rabboni! maana yake Mwa-
 limu.

Akamwambia Isa, Usinishike, kwani sijapaa kwa 17
 Baba yangu: enenda kwa ndugu zangu, ukawaambie,
 naenda juu kwa Baba yangu na Baba yenu, kwa Mu-
 ungu wangu na Muungu wenu.

Akaja Maryamu Magdalene akawahubiria waanafu- 18
 nzi kwamba amemwona Bwana, akamwambia haya.

Ikiwa jioni siku ileile, juma a pili, milango iki- 19
 fungwa, walipokusanyika waanafunzi kwa hofu ya
 Wayahudi, akaja Isa akasimama katikati akawaambia,
 Amani kwenu. Akisema haya akawaonya mikono yake 20
 na mbavu zake. Wakafurahi waanafunzi wakimwona
 Bwana.

Akawaambia Isa tena, Amani kwenu. Kama Baba 21

22 alivyonituma mimi, nami nawatuma ninyi. Akisema
haya, akawapuzia, akawaambia, Pokeeni Roho Mtaka-
23 tifu: mtakaowaondolea thambi wataondolewa; mtakao-
wafungia, watafungiwa.

24 Tomaso, mmoja wa wathenashara, aliyeitwa Pacha,
25 hakuwako pamoja nao alipokuja Isa. Wakamwambia
waanafunzi wangine, Tumemwona Bwana.

Akawaambia, Nisipona mikononi mwake alama ya
mismari, nikatia kidole changu katika alama ya mismari,
nikatia mkono wangu katika mbavuni, sitaamini.

26 Baadaye siku nane walikuwamo tena waanafunzi, na
Tomaso pamoja nao. Akaja Isa, milango ikifungwa,
27 akasimama katikati, akasema, Amani kwenu. Aka-
mwambia Tomaso, Leta hapa kidole chako, katazame
mikono yangu, kalete mkono wako katika mbavuni mwa-
ngu, wala usiwe asiyeamini illa aaminiye.

28 Akajibu Tomaso akamwambia, Bwana wangu na
Muungu wangu.

29 Akamwambia Isa, Kwani umeniona, Tomaso, umea-
mini: ndio waliobarikiwa walioamini wasipona.

30 Na ishara nyingine zilizo nyingi akafanya Isa mbele
ya waanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki.

31 Haya yameandikwa, mpate kuamini kama Isa ndiye
aliye Masiya, Mwana wa Muungu, na mkiamini mpate
uzima kwa jina lake.

21 BAADAYE akajionyesha tena Isa kwa waanafunzi
2 katika bahari ya Tiberia; akajionyesha hivi. Walikuwa
pamoja Siman Petro, na Tomaso aliyeitwa Pacha, na
Nathanael wa katika Kana ya Galilaya, nao wa Zebe-
3 dayo, na wangine waanafunzi wake wawili. Akawaambia
Siman Petro, Naenda nivue samaki. Wakamwambia,
Naswi tutafuatana nawe. Wakaenda wakaingia marra
chomboni, wasitwae kitu usiku ule.

4 Hatta assubui mapema akasimama Isa pwani, wala
5 hawajui waanafunzi kama ndiye Isa. Akawaambia Isa,
6 Vijana, mnavyo vyakula? Wakamjibu, Hatuna. Aka-
waambia, Tupeni jarifa upande wa kuume wa chombo,
mtapata. Wakatupa, wala hawawezi kuvuta kwa sa-
maki kwa kuwa wengi.

7 Akamwambia Petro mwanafunzi yule aliyempenda
Isa, Ndiye Bwana.

Siman Petro akisikia kwamba ndiye Bwana, akaji-

fungia vazi, kwani utupu, akajitupa baharini. Wangine 8
 waanafunzi wakaja mashuani, kwani hawako mbali ya
 inchi, illa kama thiraa miteen, wakiivuta jarifa ya samaki.

Wakishuka katika inchi wakaona moto wa makaa uko, 9
 na kitoweo kimetiwa, na mkate. Akawaambia Isa, 10
 Leteni samaki mlizozitwaa sasa. Akapanda Siman 11
 Petro akaivuta jarifa katika inchi, imejaa samaki kubwa,
 mia, hamsini na tatu; nazo zikiwa nyingi ginsi hiyo
 jarifa haikukatika.

Akawaambia Isa, Njoooni, kaleni. Hakuthubutu mtu 12
 wa waanafunzi kumwuliza, Nani weye? wakijua kwamba
 ndiye Bwana. Akaja Isa akatwaa mkate akawapa, na 13
 samaki vivyo.

Hii ndiyo marra ya tatu Isa alipoonekana na waana- 14
 funzi wake akiwa amefufuka katika wafu.

Walipokwisha kula, Isa akamwambia Siman Petro, 15
 Siman wa Yunus, wanipenda kuliko hawa?

Akamwambia, Yakini, Bwana; wanijua nakupenda.

Akamwambia, Walishe waana kondoo wangu.

Akamwambia tena marra ya pili, Siman wa Yunus, 16
 wanipenda mimi?

Akamwambia, Yakini, Bwana; wanijua nakupenda.

Akamwambia, Wachunge kondoo zangu.

Akamwambia marra ya tatu, Siman wa Yunus, wani- 17
 penda mimi?

Akasikitika Petro kwa sababu amemwambia marra
 ya tatu, Wanipenda? Akamwambia, Bwana, ndiwe
 uyajuaye yote; wanijua kwamba nakupenda.

Akamwambia Isa, Walishe kondoo zangu. Amin, 18
 amin, nakwambia, ukiwa kijana umejifunga ukaenda
 upendako: ukiwa mzee, utanyosha mikono yako, mgine
 atakufunga, atakuchukua usikopenda.

Akasema haya kuonya kwa kufa gani atamtukuza 19
 Muungu. Akisema haya akamwambia, Nifuate.

Petro akigeuka akamwona mwanafunzi aliyempenda 20
 Isa anafuata, aliyelazwa katika chakula cha jioni kifuani
 mwake, akasema, Bwani nani akutoaye? Akimwona 21
 huyu, Petro akamwambia Isa, Bwana, na huyu nini?

Akamwambia Isa, Nikipenda huyu akae hatta nita- 22
 kapokuja, imekupasaje? Unifuate mimi wewe.

Likaenea na neno hili katika ndugu, kwamba mwana- 23
 funzi yule hatakufa. Wala hakumwambia Isa, hata-

24 kufa, lakini, Nikipenda akae hatta nitakapokuja, imeku-
pasaje? Ndiye mwanafunzi ashuhuduye kwa haya,
akayaandika: naswi tumejua kwamba ushahidi wake
una kweli.

25 Kuna tena mengine mengi aliyoyafanya Isa, nayo
yakiandikwa killa moja, nathani hatta ulimwengu wote
hautoshi kwa vitabu vitakavyoandikwa. Amina.

MATENDO YA MITUME.

1 KITABU cha kwanza nimekifanya, ee Teofilo, cha
2 yote aliyokwanza kufanya Isa na kufundisha, hatta
3 siku ile alipowaagiza kwa Roho Mtakatifu mitume alio-
wachagua, akachukuliwa juu. Akajionyesha kwao
4 hayi baada ya kuteswa kwake, kwa ishara nyingi, akio-
nekana nao muda wa siku arobaini, akiyanena yaliyo-
5 upasa ufalme wa Muungu. Hatta akikutanika nao aka-
waagiza wasitoke katika Yerusalemi, illa waingoje ahadi
6 ya Baba, "mliyoambiwa nami. Kama Yohana alivyo-
batiza kwa maji, ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtaka-
tifu baada ya siku hizi si nyingi."

6 Wakienda pamoja wakamwuliza, wakanena, Bwana,
wakati huu ndipo utakaporudisha ufalme kwa Israeli?
7 Akawaambia, Si kwenu kuzijua zamani wala wakati,
8 Baba alizoziweka katika uwezo wake yeye. Lakini
mtapewa nguvu, akija Roho Mtakatifu juu yenu, nanyi
mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemi, na ka-
tika Uyahudi wote, na Usamaria, na hatta mwisho wa
inchi.

9 Akisema haya, wakitazama wale, akainuliwa, wingu
likampokea katika machoni pao.

10 Nao wakiangalia mbinguni akienda zake, watu wawili
11 wakawasimamia wenyi nguo nyeupe, walionena, Watu
wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni?
Huyu Isa aliyechukuliwa kwenu kwenda mbinguni,
atakuja ginsi hiyo mlivyomwona akienda zake mbi-
nguni.

12 Wakarudi Yerusalemi katika mlima ulioitwa wa Zei-

tuni, uliopo karibu ya Yerusalemi, mwendo ukiwa wa sabato.

Hatta walipoingia wakapanda katika órofa, walipo- 13
keti Petro, na Yohana, na Yakobo, na Andrea, Filipo
na Tomaso, Bartolomayo na Mattayo, Yakobo wa Alfayo
na Siman Zelote, na Yuda wa Yakobo. Hawa wote 14
walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kuomba,
pamoja nao waanawake, Maryamu mama wake Isa, na
ndugu zake.

Siku hizi akasimama Petro kati mwa ndugu, akasema 15
(jamiu ya majina pamoja kama mia na asharini), Waa- 16
naume ndugu, imepasa maandiko yatimizwe, aliyoyane-
na mbele Roho Mtakatifu kwa kanwa la Daud, juu ya
Yuda, aliyekuwa rubani wao waliomtwa Isa, kama 17
amehesabika pamoja nasi, akapata sehemu ya ungoje huu.

(Huyu akanunua uanja kwa ijara ya uovu; akaangu- 18
ka usoni, akapasuka kati, matumbo yote yakatoka.
Ikajulika nao wote wakaao Yerusalemi, hatta uanja 19
ule umeitwa kwa lugha yao Akeldama, ndio Uanja wa
damu.) Kwani imeandikwa katika kitabu cha Zaburi, Ma- 20
kao yake yaachwe, wala asiwe mtu kukaa humo. Tena,
Usimamizi wake atwae mgine. Imepasa tena katika 21
watu waliofuatana nasi wakati wote alipoingia akatoka
kwetu Bwana Isa, kutoka katika ubatizo wa Yohana 22
hatta siku alipochukuliwa kwetu, mmoja wao awe sha-
hidi wa ufufuko wake pamoja nasi.

Wakatoa wawili, Yusuf aliyetitwa Barsaba, aliyepewa 23
jina Yusto, na Mattiya. Wakaomba, wakanena, We- 24
we, Bwana, ujuaye moyo wao wote, mwonyeshe mmoja
uliyemchagua katika hawa wawili, atwae sehemu ya 25
ungoje na utume, aliyoi kosa Yuda aende mahali pake.

Wakapiga kura zao, kura ikamwangukia Mattiya, 26
akahesabika pamoja nao mitume edashara.

HATTA katika kutimia siku ya Pentekote waliku- 2
wako wote kwa moyo mmoja mahali pamoja.

Marra ikawa katika mbinguni sauti kama upepo 2
uvumao kwa nguvu, ukajaza nyumba yote walipokuwa
wakikaa. Zikaonekana kwao kama ndimi za moto zili- 3
zogawanyika, ukakaa mmoja juu ya killa mmoja wao.
Wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa 4
maneno mangineyo, kama walivyopewa na Roho ku-
yatoa.

- 5 Walikuwako katika Yerusalemi Wayahudi wakikaa, watu wataowa, katika mataifa yote chini ya uwingu.
- 6 Habari hizo zikienea, makutano wakakusanyika, waka-fathaika, kwani wakawasikia killa mmoja wakisema
- 7 lugha yake yeye. Wakashangaa wote, wakaajabu, wakisema wao kwa wao, Tazama, si hawa wote wane-nao Wagalilaya? Ginsi gani sisi twasikia killa mtu
- 9 lugha yetu tuliyojaliwa, Waparthi na Wamedi, na Waelamiti, nao wakaa Mesopotamia, Uyahudi, Kappa-
- 10 dokia, Ponto na Asia, Frugia na Pamfulia, Misri na inchi za Libua kwa Kurene, Warumi wageni Waya-
- 11 hudi na waongofu, Wakrete na Waarabu, twawasikia hawa wakinena kwa maneno yetu makuu yake Muungu.
- 12 Wakafathaika wote wakaingiwa na shaka, wakiambia-
- 13 na, Maana yake nini hii? Wangine wakafanyizia mzaha wakasema, Wamelewa na mvinyo mpya.
- 14 Akisimama Petro na edashara wale, akapaliza sauti yake akanena, Waume Wayahudi na wote mkaao Ye-
- 15 rusalem, mjue haya, mkasikilize maneno yangu. Kwani hawa hawakulewa kama mlivyothani, kwani ni saa ya
- 16 tatu ya mchana. Lakini haya ndiyo yaliyonenwa kwa
- 17 nabii Yoel, Itakuwa siku za mwisho, ananena Muungu, nitamwaga ya Roho yangu juu ya watu wote; watatabiri waana wenu na binti zenu, na vijana wenu watao-
- 18 na njozi, na wazee wenu wataota ndoto. Na juu ya watumwa wangu waume na wake, siku zile nitamwaga ya
- 19 Roho yangu, nao watatabiri. Nitatoa ajabu mbinguni juu na ishara katika inchi chini, damu na moto na
- 20 mvuke wa moshi. Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, mbele ya kuja siku ya Bwana iliyo kuu na
- 21 kutetemesha. Itakuwa killa atakayeomba kwa jina la Bwana ataokoka. Waume Waisraeli, sikieni maneno
- 22 haya. Isa wa Nazareti, mtu aliyeonyeshwa kwetu na Muungu kwa uwezo na ajabu na ishara, alizozifanya Muungu kwa yeye kati mwetu, kama mkajua ninyi,
- 23 huyu aliyetolewa kwa shauri lililowekwa na kujua mbele kwake Muungu, mmetwaa mkamsulibisha kwa mikono
- 24 mibaya, mkamua. Naye Muungu amemfufua, akilegeza uchungu wa mauti: kwani haiyamkini ashikwe nao.
- 25 Daúd akamsema, Nalimwona Muungu siku zote mbele yangu, kwani yuko mkono wangu wa kuume nisitikisike.
- 26 Kwa hiyo ukapendezewa moyo wangu, ulimi wangu

ukafurahi, tena na mwili wangu utakaa katika kutu-
 maini: kwani hutaniacha roho yangu katika ahera, wala 27
 hutatoa mtakatifu wako aone uharibifu. Umenifundisha 28
 njia ya uzima; utanijaza kwa furaha kwa kuwa machoni
 pako. Waume ndugu, niwie rathi niseme pasipo hofu 29
 mbele yenu ya baba mkuu Daúd, kama alifariki, akazi-
 kwa, na kaburi lake liko kwetu hatta leo. Akiwa nabii, 30
 akijua kama Muungu amemwapia kwa kiapo kama ka-
 tika wazao wa kiunoni mwake kwa mwili atamleta Ma-
 siya, akae kitini mwake, akiona mbele akaunenea ufufuo 31
 wake Masiya, kama hakuacha roho yake katika ahera,
 wala mwili wake haukuona uharibifu. Huyu Isa, Muu- 32
 ngu amemfufua, na sisi wote mashahidi. Akipandishwa 33
 mkono wa kuume wa Muungu, akipokea ahadi ya Roho
 Mtakatifu kwa Baba, ametoa hili mliloliona sasa mka-
 sikia. Kwani Daúd hakupanda mbinguni: akisema, 34
 Bwana akamwambia bwana wangu, Kae mkono wa
 kuume wangu, hatta nitakapowatia adui zako chini ya 35
 pa nyayo zako. Nyumba yote ya Israeli wajue yakini 36
 kama Muungu amemfanya na Bwana na Masiya, huyu
 Isa mliyemsulibisha.

Wakiyasikia haya wakachomeka moyoni, wakamwa- 37
 mbia Petro na mitume waliosalia, Tufanyeni, waume
 ndugu? Petro akawaambia, Mtubu, mkabatizwe killa 38
 mmoja wenu kwa jina la Isa Masiya kwa ondoleo la tha-
 mbi, mtapewa ya Roho Mtakatifu. Kwani kwenu ni 39
 ahadi na kwa watoto wenu, nao wote walio mbali, wote
 watakaotwa na Bwana Muungu wetu. Akashuhudia 40
 kwa maneno mengine mengi akawaonya, akisema, Mji-
 ponye katika kizazi hiki kilichopotoka.

Nao waliolipokea neno lake kwa moyo wakabatizwa: 41
 wakazidishwa siku ile kwa watu kama elfu tatu.

Wakadumu katika fundisho la mitume, na usharika, 42
 na kuvunja mikate, na kusali. Killa mtu akaona hofu: 43
 ajabu nyingi na ishara zikafanyika na mitume. Wote 44
 walioamini walikuwako pamoja, wakawa wakisharikiana
 katika vitu vyote, na mali zao na vifaa vyao wakaviuza, 45
 wakagawanya kwa wote kama killa mtu alivyokuwa na
 kuhitaji. Nao wakadumu siku kwa siku kwa moyo 46
 mmoja katika hekalu, wakavunja mikate nyumba kwa
 nyumba, wakipata chakula kwa furaha pasipo hila moyo-
 ni, wakimsifu Muungu, wakiwapendeza watu wote. 47

Bwana akaleta waliokiokoka siku kwa siku katika kanisa.

- 3** PETRO na Yohana walikwenda pamoja katika hekalu saa ya kusali, saa a tissa.
- 2** Mtu aliyekuwa kiwete toka tumboni mwa mamaye alichukuliwa, aliyewekwa killa siku katika mlango wa hekalu ulioitwa mzuri, atake sadaka kwao walioingia hekaluni. Huyu akiwaona Petro na Yohana katika kuingia hekaluni akataka kupewa sadaka. Petro, akikaza macho juu yake pamoja na Yohana, akamwambia, Tutazama sisi. Akawasikiliza, akiwathania atapewa kitu nao. Akanena Petro, Fetha wala thababu hapana kwangu; ninalo ndilo nikupalo: kwa jina la Isa Masiya Mnazareti simama ukatembee. Akamshika mkono wa kuume akamwinua. Marra nyayo zake na vifundo vya miguu vikapata nguvu, akaruka, akasimama akatembea, akaingia pamoja nao katika hekalu, akienda akiruka, akimsifu Muungu. Watu wote wakamwona akienda akimsifu Muungu. Wakamtambua ndiye aliyekaa kwa sadaka katika mlango mzuri wa hekalu, wakajaa ushanga na ajabu kwa haya yaliyompata.
- 11** Akiwashika Petro na Yohana, watu wote wakawakusanyikia mbio katika ukumbi ulioitwa wa Sulemani, wakistaajabu.
- 12** Akiona Petro, akawajibu watu, Waume Waisraeli, mbona mnaajabu haya? mbona mwatukazia macho, kama kwa nguvu zetu sisi ao wema tumemfanya huyu atembee? Muungu wa Ibrahimu, na Isaak, na Yakobo, Muungu wa baba wetu, amemtukuza Kijana chake Isa, mliyemtoa mkamkania usoni pa Pilato, akihukumu kumwacha. Ninyi mkamkania Mtakatifu na Mwenyi haki, mkataka mpewe mtu muuaji. Mkamua Mkuu wa uzima, aliyefufuka na Muungu; na sisi mashahidi. Na kwa imani ya jina lake, huyu, mnayemwona mkamjua, amepewa nguvu na jina lake, na imani iliyo kwa huyo imempa uzima huu mbele yenu wote. Bassi sasa, ndugu, najua kama mmetenda msipojua, kama nao wakuu wenu. Lakini, mambo aliyoyahubiri mbele kwa kanwa la nabii zake wote, kama Masiya atateswa, Muungu ametimiza hivyo. Mtubu tena mkageuke, thambi zenu zifutwe, utakapokuja wakati wa kupumzika katika usoni pake Bwana; naye atampeleka

Isa Masiya aliyehubiriwa kwanza kwenu: aliyepaswa apo- 21
 kewe mbinguni hatta wakati wa kutengenezwa mambo
 yote, aliyonena Muungu kwa kanwa la nabii zake wata-
 katifu tangu zamani. Kwani Musa akawaambia baba 22
 kama, Bwana Muungu atawaletea nabii wa katika ndu-
 gu zenu kama mimi: msikieni killa atakavyowaambia.
 Itakuwa, killa hayi asiyemsikia nabii yule, atapotezwa 23
 katika taifa. Na nabii wote tangu Samwili nao walio- 24
 fuata, wote walionena wakahubiri siku hizi. Ninyi 25
 waana wa nabii, na wa maagano aliyoyafanya Muungu
 na baba zenu, akimwambia Ibrahimu, Katika uzao
 wako makabila yote ya ulimwengu yatabarikiwa. Kwe- 26
 nu kwanza Muungu, akimfufua Kijana chake Isa, aka-
 mpeleka awabarikie, kwa kumgeuza killa mtu katika
 maovu yake.

WAKISEMA na watu, wakaja juu yao wakohani, 4
 na jemadari ya hekalu, na Masadukayo, wakitaabika nao 2
 wakiwafundisha watu wakahubiri kwa Isa ufufuko ka-
 tika wafu. Wakawatia mikono, wakaweka katika lindo 3
 hatta assubui: kwani imekuwa jioni.

Wengi wao waliolisikia neno wakaamini; hesabu ya 4
 waume ikawa kama elfu tano.

Ikawa assubui walikusanyika wakuu, na wazee, na 5
 waandishi, katika Yerusalemi, na Anna mkohani mkuu, 6
 Kayafa, na Yohana, na Iskander, na wote waliokuwa
 jamaa za mkohani mkuu. Wakawaweka katikati, 7
 wakauliza, Kwa nguvu gani, ao kwa jina gani mmefa-
 nya haya ninyi? Ndipo Petro akijaa Roho Mtakatifu, 8
 akawaambia, Wakuu wa watu na wazee wa Israeli, tuki- 9
 ulizwa leo kwa mambo mema yake mtu thaifu, kwa
 nini ameokoka, jueni ninyi nyote na watu wote wa 10
 Israeli, kama kwa jina la Isa Masiya Mnazareti mliye-
 msulibisha, Muungu aliyemfufua katika wafu, kwa huyo
 huyu asimama mzima usoni penu. Ndiye huyo jiwe 11
 lililotupwa nanyi waashi, limekuwa kuu la pembeni.
 Wala hakuna katika mgineo wokovu, wala jina jingine 12
 hapana walilopewa watu katika mbinguni tupate kuo-
 koka nalo.

Wakiangalia uthabiti wa Petro na wa Yohana, waki- 13
 wajua watu wasio na elimu, wala wakuu, wakaajabu;
 wakawatambua walikuwa pamoja na Isa. Wakimwona 14
 mtu akisimama pamoja nao, yule aliyeponyeka, hawa-

- 15 kuwa na kujibu. Wakaamuru waondoshwe katika
 16 baraza, wakafanyana shauri, wakisema, Tuwafanyieni
 watu hawa? Kwani ishara mashuhuru imefanyika
 nao, ndiyo thahiri kwao wote wakao Yerusalemi,
 17 wala hatuwezi kuikana. Lakini isienee tena katika
 watu, tuwaogofishe kwa maogofya wasiseme tena kwa
 18 jina hili na mtu wo wote. Wakawaita wakawaamuru
 wasinene kabisa wala wasifundishe kwa jina lake Isa.
 19 Petro, na Yohana, akajibu akawaambia, Kama haki
 usoni pa Muungu tuwasikie ninyi kuliko Muungu msemi.
 20 Hatuwezi sisi tuliyoyajua tukayasikia tusiyanene. Nao
 21 walipowaogofya wakawaacha, wasione wapateje kuwa-
 thibu, kwa sababu ya watu : kwamba wote wakamsifu
 22 Muungu kwa haya yaliyokuwa. Kwani umri wake umepita
 miaka arobaini mtu aliyefanyiwa ishara hii ya kunya.
 23 Wakiachwa wakaenda kwa watu wao, wakahubiri yote
 24 waliyoambiwa na wakohani wakuu na wazee. Wakisikia
 wakapaliza sauti kwa moyo mmoja kwa Muungu, waka-
 nena, Mola, ndiwe Muungu, uliyefanya mbingu, na inchi,
 25 na bahari na vyote vilivyomo : uliyenena kwa kanwa la
 Daúd kijana chako, Mbona wamejitapa mataifa, na watu
 26 wamewaza matupu? Wafalme wa inchi walisimama,
 na wakuu walikusanyika pamoja, juu ya Bwana na juu
 27 ya Masiya wake. Kwani kweli walikusanyika juu ya
 Kijana chako mtakatifu Isa, uliyemtia mafuta, He-
 rode na Pontio Pilato, pamoja na wamataifa na watu wa
 28 Israeli, wafanye kama mkono wako na shauri lako uli-
 29 vyoshika mbele kuwa. Bassi sasa, Bwana, tazama ma-
 ogofya yao, ukawape watumwa wako pasipo hofu wanene
 30 neno lako, ukinyosha mkono wako uponye, ishara na ajabu
 zifanyike kwa jina la Kijana mtakatifu wako Isa.
 31 Nao wakiomba, mahali palitikisika walipokusanyika ;
 wakajaa wote Roho Mtakatifu, wakanena neno la Muu-
 ngu pasipo hofu.
 32 Na jamii yao walioamini walikuwa na moyo mmoja na
 uzima mmoja, wala hapana mmoja aliyesema kama kitu
 alichu nacho mali yake yeye, lakini yote yamesharikiwa.
 33 Kwa nguvu nyingi wakatoa mitume ushahidi wa kufu-
 fuka Bwana Isa. Neema nyingi ikawa juu yao wote.
 34 Wala hakuna aliyehitaji kwao, kwani wote waliokuwa na
 uwanja ao nyumba wakauza, wakaleta thamani yake
 35 iliyokuzwa, wakaiweka miguuni pa mitume, ikagawa-
 nyika kwa killa mmoja kwa ginsi alivyohitaji.

Na Yusuf aliyeitwa na mitume Barnaba (iliyofasirika, 36 Mwana wa faraja), Mlawi, kwa asili yake wa Kupro, akiwa na shamba, akauza, akaileta fetha akaweka migu- 37 uni pa mitume.

MTU aliyeitwa Anania, na Safira mkewe, akauza 5 uwanja, akajiwekea kwa siri katika thamani, mkewe 2 akijua, akaleta yaliyosalia akatia miguuuni pa mitume.

Akamwambia Petro, Anania, kwa nini Shetani ame- 3 kujaza moyo, umdanganye Roho Mtakatifu, ukajiwekea kwa siri katika thamani ya uwanja? Ukiwa kama kwa- 4 nza si wako? Ukiisha kuza si katika uwezo wako? Mbona umeweka moyoni kufanya hivi? Si mtu uliyemwambia uwongo, illa Muungu.

Akisikia Anania maneno haya, akaanguka, akafa. 5 Hofu nyingi ikawapata wote waliosikia haya. Wakao- 6 ndoka vijana, wakamfungia, wakachukua, wakazika.

Ikawa muda wa saa tatu baadaye, mkewe akaingia, 7 asipojua ilivyokuwa. Akamjibia Petro, Nambie, ume- 8 kuza uwanja kwa thamani hiyo? Akanena, Ndiyo hiyo. Petro akamwambia, Ginsi gani mmepatana kumjaribu 9 Roho ya Bwana? angalia, miguu yao waliomzika mumeo mlangoni, watakuchukua nawe. Marra akaa- 10 nguka miguuuni pake, akafa: wakiingia vijana waka- mwona amekufa, wakamchukua wakamzika pamoja na mumewe. Hofu nyingi ikawapata kanisa wote nao 11 wote walioyasikia haya.

Kwa mikono ya mitume zikafanyika ishara na ajabu 12 nyingi katika watu. (Wakawako wote kwa moyo mmoja katika ukumbi wa Sulemani, wala wang'ne 13 hatta mmoja hakuthubutu kujiunga nao, illa watu wakawatukuza. Waaminio wakamzidia Bwana, wengi 14 na waume na wake.) Hatta katika njia hutoa wago- 15 njwa huwaweka juu ya mikeka na vitanda, illi Petro akija hatta kivuli chake kiwafikie baathi yao. Wakaja 16 wengi katika miji iliyo karibu na Yerusalemi, waki- chukua wagonjwa, nao waliopagawa na pepo wabaya; wakaponyeshwa wote.

Akaondoka mkohani mkuu na wote walio pamoja 17 naye, ndio mathhebu ya Masadukayo, wakajaa uwivu, wakawatia mikono mitume, wakawaweka katika lindo 18 la watu. Malaika ya Bwana usiku akafungua mila- 19 ngo ya gereza, akawatoa, akanena, Enendeni, mkasi- 20

mame mkaseme katika hekalu maneno yote ya uzima
21 huu. Wakisikia wakaenda alfajiri katika hekalu, waka-
fundisha.

Wakiwako mkohani mkuu nao walio pamoja naye,
wakawaita baraza na diwani yote ya waana wa Israeli,
22 wakapeleka gerezani waletwe. Watumishi wakiwako
23 hawakuwaona gerezani, wakarudi wakatoa habari, waki-
sema, Pakufungwa tuliona pamefungwa salama salamini,
nao walinzi wamesimama mbele ya mlango : hatta tuki-
24 fungua hatukuona mtu ndani. Wakisikia maneno haya
mkohani mkuu, na jemadari wa hekalu, na wakohani
25 wakuu, wakaingiwa na shaka, yatakuwaje haya. Mmoja
aliyekuwako akawapa habari kama, Watu hawa mliowa-
weka gerezani, wako katika hekalu, wamesimama wana-
wafundisha watu.

26 Wakaenda jemadari pamoja na watumishi wakawaleta,
illa si kwa nguvu : kwani wakaogopa watu, wasiwatupie
27 mawe. Wakawaleta wakawaweka katika baraza. Mko-
28 hani mkuu akawauliza akisema, Hatukuwaamuru kwa
amri msifundishe kwa jina hili? kaangalieni, mmejaza
Yerusalemi na mafundisho yenu, mkataka kuleta juu
yetu damu ya mtu yule.

29 Akajibu Petro na mitume, wakanena, Imepasa kumtii
30 Muungu kuliko watu. Muungu wa baba zetu alimfufua
31 Isa mliyemua mkamtundika katika mti. Huyo Muungu
amemweka juu kwa mkono wake wa kuume, Mkuu na
Mwokozi, kutoa toba kwa Israeli na kuondolewa thambi.
32 Na sisi mashahidi wa maneno haya, naye Roho Mtaka-
tifu, aliyewapa Muungu waliomtii.

33 Wakisikia wakaumwa : wakafanya shauri kuwaua.
34 Akasimama mmoja katika baraza, Farisayo, jina lake
Gamaliel, mfunza sheria mwenyi heshima kwa watu
35 wote, akaamuru waweke mitume 'nje punde; aka-
waambia, Waume Waisraeli, mjiangalie mtakavyowa-
36 tendea watu hawa. Kwani mbele ya siku hizi akaondoka
Theuda, akisema ndiye mtu; wakamfuata watu kama
aroba mia : akauawa; wote waliomsikia wakatawanyika,
37 wasiwe neno. Baada yake akaondoka Yuda Mgalilaya
siku za kuandikwa, akachukua watu kathawakatha
nyuma yake; naye akapotea; wote waliomsikia wa-
38 katawanyika. Bassi sasa nawaambia, msiwakaribie
watu hawa, mkawaache : likiwa la waana Adamu shauri

hili na kazi hii, itaharibika : illa ikiwa ya Muungu 39
ha'mwezi kuiharibu ; msionekane kama wapiganao na
Muungu.

Wakamsikia : wakawaita mitume, wakawapiga, wa- 40
kaamuru wasiseme kwa jina lake Isa, wakawaacha.

Wakatoka katika mbele ya baraza, wakifurahi kama 41
kwa sababu ya jina wamestahiliwa kuaibika. Siku zote 42
katika hekalu na nyumbani hawakuacha kufundisha na
kuhubiri Isa aliye Masiya.

KATIKA siku hizi, waanafunzi wakizidi, palikuwa 6
kunong'onia kwa Wahelenisti juu ya Waebrania, kama
wajaani wao hawakupata haki katika ungoje wa killa
siku.

Wathenashara wakawaita jamii ya waanafunzi, waki- 2
nena, Haipendezi sisi tuache neno la Muungu tungoje
mezani. Bassi chagueni, ndugu, watu wa kwenu wenyi 3
sifa saba, waliojaa Roho Mtakatifu na hekima, tuwaweke
juu ya jambo hili ; nasi tutadumu katika kuomba na 4
ungoje wa neno.

Neno hilo likapendeza machoni pa makutano yote : 5
wakachagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mta-
katifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanor, na Timoni, na
Parmena, na Nikolao, mwongofu wa Antiokia ; wakawa- 6
weka mbele ya mitume ; wakaomba, wakawatia mikono.

Neno la Muungu likaenea ; hesabu ya waanafunzi ka- 7
tika Yerusalemi ikazidi sana ; jamaa kubwa ya wakohani
wakaifuata imani.

Stefano akijaa imani na nguvu akafanya ajabu na 8
ishara kuu katika watu.

Wakaondoka walio wa sunagogi iliyoitwa ya Mali- 9
bertino, na ya Wakurene na Waiskanderia, na yao wa
Kilikia na Asia, wakiulizana na Stefano : wala hawa- 10
kuweza kushindana na hekima na roho aliyonenea.
Hatta wakaingiza watu waliosema kama, Tumemsikia 11
huyu akinena maneno ya unajisi juu ya Musa na Muungu.
Wakaondokeshwa watu, na wazee, na waandishi. 12

Wakamjia wakamkamata, wakamleta katika baraza.
Wakasimamisha mashahidi wa uwongo waliosema, Mtu 13
huyu hakomi kunena maneno juu ya hapa patakatifu na
torati. Kwani tumemsikia akisema, kama Isa Mnaza- 14
reti huyu ataharibu mahali hapa, atabadili na desturi
tulizozipokea kwa Musa.

- 15 Wakikaza macho juu yake, wote waliokaa katika baramba, wakamwona uso wake uso wa malaika.
- 7 **AKANENA** mkohani mkuu, Ndivyo hivyo?
- 2 Akasema, Waume ndugu na baba, sikieni. Muungu wa utukufu alimtokea baba wetu Ibrahimu, akiwa katika Mesopotamia, mbele hajakaa Haran, akamwambia, Utoke katika inchi yako na katika jamaa zako, ukaende hatta inchi nitakayokuonya. Ndipo, akitoka katika inchi ya Wakaldayo, akakaa katika Haran, na huko baada ya kufa baba yake, akamhamisha hatta inchi hii, mkaapo ninyi sasa. Wala hakumpa urithi huku hatta kutia mguu: akaahidi atampa aimiliki, yeye na wazao wake baadaye, asipokuwa na mtoto. Akanena hivi Muungu, Kama wazao wake watakuwa wageni katika inchi ya watu, nao watakuwa watumwa, watatendewa vibaya huko miaka aroba mia. Na taifa watakaowafanya watumwa nitahukumu mimi, amesema Muungu, na baadaye watatoka wataniabudu mahali hapa. Akampa agano la tohara: vivyo akamzaa Isaak, akamtahiri siku ya nane; na Isaak Yakobo; na Yakobo baba wakuu thenashara. Baba wakuu wakiona uwivu wakamkuza Yusuf kwenda Misri. Muungu alikuwako naye, akamtoa katika misiba yake yote, akampa neema na hekima mbele ya Farao mfalme wa Misri, akamfanya msima-mizi wa Misri na nyumba yake yote. Ikaja njaa juu ya inchi yote ya Misri na Kanaan, na shidda nyingi, wala hawakuona chakula baba zetu. Aliposikia Yakobo, nafaka ziko katika Misri, alituma baba zetu kwanza. Hatta kwa pili Yusuf alitambuliwa na ndugu zake; jamaa ya Yusuf ikajulikana na Farao. Akapeleka Yusuf akamwita Yakobo baba yake na jamaa zake wote, watu sabwini na watano. Yakobo akashuka katika Misri, akafariki, yeye na baba zetu, wakachukuliwa hatta Sukem, wakazikwa katika kaburi alilolinunua Ibrahimu kwa thamani ya fetha kwa waana wa Emmor wa Sukem. Kama ulivyokaribia wakati wa abadi, Muungu aliymwambia Ibrahimu, watu wakazidi wakaongezeka katika Misri, hatta akaondoka mfalme mwingine, asiyemjua Yusuf. Huyu akiwafanyia hila jamaa zetu, akawatendea mabaya baba zetu, akiwatupisha watoto wadogo wao, wasihifathike hayi. Wakati huu akazaliwa Musa, akawa mzuri kwa Muungu, waliyemlisha miezi

mitatu katika nyumba ya babaye. Alipotupwa aka- 21
 mtwaa binti Farao, akamlea kwake kama mwana. Aka- 22
 fundishwa Musa katika hekima yote ya Misri, akawa
 hodari katika kunena na katika kufanya. Umri wake 23
 ukitimia miaka arobaini, ikaingia katika moyo wake ku-
 watazama ndugu zake waana wa Israeli. Akamwona 24
 mtu amethulumiwa, akamhami, akamfanyia kisasi, aka-
 mua Mmisri aliyemwonea. Akathani ndugu zake wata- 25
 mtambua kama Muungu kwa mkono wake anawapa
 wokovu: lakini hawakutambua. Siku ya pili yake, 26
 akawatokea wakipigana, akawapatanisha amani, akisema,
 Waume, ninyi ndugu; mbona hamfanyi haki? Yule 27
 aliyemthulumu jirani wake akamsukumia mbali, akise-
 ma, Nani aliyekufanya wewe mkuu na mwamuzi juu
 yetu? Wataka kuniua mimi, kama ulivyomua Mmisri 28
 jana? Akakimbia Musa kwa neno lile, akawa mgeni 29
 katika inchi ya Madiani, alipozaa waana wawili. Hatta 30
 miaka arobaini ikitimia, akamtokea katika jangwa la
 mlima Sinai malaika ya Bwana, kwa kuwa moto katika
 kijiti. Musa akiona akastaajabia iliyooneka; akikaribia 31
 atazame, sauti ya Bwana ikamjia, Mimi Muungu wa 32
 baba zako, Muungu wa Ibrahimu, na Muungu wa Isaak,
 na Muungu wa Yakobo. Akatetemeka Musa, asithu-
 butu kutazama. Akamwambia Bwana, Legeze viatu 33
 vya miguuni, kwani mahali hapa usimamapo ni inchi
 takatifu. Nikiona nimeona mabaya ya watu wangu 34
 walioko katika Misri, nikasikia kuugua kwao, nika-
 shuka niwatoe. Na sasa nitakutuma katika Misri.
 Huyu Musa, waliomkataa, wakisema, Nani aliyekuweka 35
 mkuu na mwamuzi? ndiye aliyemtuma Muungu kuwa
 mkuu na mkombozi, kwa mkono wa malaika aliyemtokea
 katika kijiti. Huyu akawaleta 'nje, akifanya ajabu na 36
 ishara katika inchi ya Misri, na katika bahari ya Sham,
 na katika bara miaka arobaini. Ndiye huyu Musa ase- 37
 maye kwa waana wa Israeli, Atawaletea nabii wa
 Bwana Muungu katika ndugu zenu, kama mimi:
 msikieni huyo. Ndiye huyu aliyekuwa katika kanisa 38
 barani, pamoja na malaika aliyesema naye katika mlima
 Sinai, na baba zetu, aliyepokea maneno ya uzima atupe
 sisi: wasiyemkubali baba zetu wamsikie, wakasukumia 39
 mbali, wakarudi moyoni Misri, wakimwambia Haruni, 40
 Utufanyie miungu watakaotutangulia: kwani huyu

Musa, aliyetuleta katika inchi ya Misri, hatujui ameku-
 41 waje. Wakafanya ng'ombe siku zile, wakaitetea sanamu
 42 thabihu, wakafurahiwa na kazi ya mikono yao. Muungu
 akageuka, akawatoa waabudu jeshi la mbinguni; kama
 ilivyoandikwa katika kitabu cha nabii, Mmenitolea mimi
 machinjo na thabihu miaka arobaini katika bara, nyumba
 43 ya Israeli? Mkainua hema ya Molok, na nyota ya
 muungu wenu Refan, sura mlizozifanya mziabudu: na-
 44 mi nitawahamisha hatta katika Babeli. Hema ya ushu-
 hudu ulikuwako kwa baba zetu katika bara, alivyoagiza
 45 aliyemwambia Musa, aifanye kwa sura aliyoiona. Wa-
 kaileta baba zetu walioipokea, pamoja na Isa katika
 milki ya mataifa, Muungu aliowafukuza katika usoni pa
 46 baba zetu, hatta siku za Daúd: aliyepata kupendeza
 mbele ya Muungu, akataka kuona pakukaa kwa Muungu
 47 wa Yakobo. Suleman akamjengea nyumba. Illakini
 48 aliye juu hakai katika nyumba zilizofanyika na mikono?
 49 kama nabii amesema, Mbingu kiti changu, na inchi
 pakutilia miguu yangu: nyumba gani mtakayonijengea;
 50 amesema Bwana: ao mahali gani nipapumzike? Sio
 51 mkono wangu ulioyafanya haya yote? Enyi wa shingo
 gumu, msiotahiriwa moyoni wala sikioni, mwamwasi siku
 52 zote Roho Mtakatifu: kama baba zenu, na ninyi. Nabii
 yupi asiyemfukuza baba zenu? Waliwaua waliotoa
 mbele habari za kuja kwake Mwenyi haki; mliyemtoa
 53 sasa mkamua: mlioipokea torati kwa amri ya malaika,
 wala hamkuishika.
 54 Wakisikia haya, wakaumwa moyoni, wakasaga meno
 juu yake.
 55 Akiwa amejaa Roho Mtakatifu, akakaza macho mbi-
 nguni, akaona utukufu wa Muungu, na Isa amesima-
 56 ma mkono wa kuume wa Muungu. Akasema, Tazama,
 naona mbingu zimefunuka, na Mwana wa Adamu ame-
 simama mkono wa kuume wa Muungu.
 57 Wakalia sauti kuu, wakaziba masikio yao, wakaji-
 58 tupa kwa moyo mmoja juu yake, wakamsukuma 'nje
 ya mji, wakamtupia mawe. Mashahidi wakaweka nguo
 59 zao miguuni pa kijana, jina lake Saul. Wakamtupia
 mawe Stefano, akiomba akisema, Bwana Isa, ukubali
 60 roho yangu. Akapiga magote, akalia sauti kuu, Bwa-
 na, usiweke juu yao thambi hii. Akisema haya akalala.
 8 SAUL alikuwa akiona vema auawe. Siku zile ufu-

kuzo mwingi ukawa juu ya kanisa katika Yerusalemi; wote wakatawanyika katika inchi za Uyahudi na Usamaria, illa mitume.

Watu wema wakamchukua Stefano, wakafanya maombolezo mengi juu yake. Saul akawafanyia kanisa jeuri nyingi, akiingia nyumba kwa nyumba, akakokota waume na wake akawaweka gerezani.

Waliotawanyika wakapita wakilibiri neno.

Akashuka Filipo hatta mjini Samaria, akawahubiria Masiya. Watu wale wakasikiliza kwa moyo mmoja mambo aliyoyanena Filipo, wakisikia wakaiona miujiza aliyofanya. Kwani pepo wachafu, wakilia kwa sauti kubwa, wakatoka katika wengi waliowapagaa, waka-pona wengi walioshikwa na upoozi, nao wajiguu. Furaha kuu ikawako mjini kule.

Palikuwapo mtu mmoja, jina lake Siman, aliyefanya zamani mjini kule uchawi, akawaloga watu wa Samaria, akijifanya aliye mkuu: wakamsikiliza wote, tangu mdogo hatta mkuu, wakisema, Mtu huyu ndiye nguvu iliyo kubwa ya Muungu. Wakamwangalia, kwa sababu siku nyingi amewaloga kwa uchawi. Hatta walipomwamini Filipo akiyahubiri mambo yaliyoipasa milki ya Muungu na jina lake Isa Masiya, wakabatizwa, na waume na wake. Akaamini na Siman mwenyewe, naye akibatizwa akakaa na Filipo, akataajabu akiiona miujiza na ishara kubwa zilizofanyika.

Nao mitume walioko katika Yerusalemi, waliposikia kama Samaria wamelikubali neno la Muungu, wakawapelekea Petro na Yohana. Nao walipofika, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu: kwani hajawashukia mmoja, wakabatizwa tu kwa jina lake Bwana Isa. Wakawatia mikono, wakapokea Roho Mtakatifu.

Alipoona Siman kama kwa kutia mikono ya mitume wamepeua Roho Mtakatifu, akawaletea fetha, akisema Nipe na mimi nguvu hii, killa nimtiaye mikono ampokee Roho Mtakatifu. Petro akamwambia, Fetha yako ipotee nawe, kwani umethani kama atoalo Muungu kununuliwa kwa fetha. Huna sehemu wala urithi katika neno hili, kwani moyo wako si vema mbele ya Muungu. Utubu katika uovu huu wako, ukamwombe Muungu, illi labuda usamehewe wazo lako la moyoni. Kwani nakuona katika safura ya uchungu, na fungoni

- 24 mwa uovu. Akajibu Siman akasema, Uniombe kwa Bwana, mambo haya uliyoyanena yasinifikie.
- 25 Nao walipokwisha kushuhudu na kulihubiri neno la Bwana, wakarudi Yerusalemi, wakaihubiri anjili katika miji mingi ya Wasamaria.
- 26 Malaika ya Bwana akamwambia Filipo akisema, Ondoka ukaende kwa kusini, hatta njia ishukayo katika Yerusalemi hatta Gaza, pasipo watu.
- 27 Akaondoka akaenda : hatta tazama, mtu wa Etiopia, towashi mwenyi nguvu nyingi chini ya Kandake malkiya yao Waetiopia, aliyetunza hazina yake yote,
- 28 amekuja Yerusalemi aabudu, akawa akirejea, akakaa garini mwake, akasoma nabii Isaya.
- 29 Roho akamwambia Filipo, Enenda karibu ukajiunge
- 30 na gari hili. Filipo akaenda upesi huko, akamsikia akisoma nabii Isaya, akanena, Yamekulea uyasomayo?
- 31 Akanena, Nipateje, mtu asiponionya? Akamtaka Filipo apande akae naye.
- 32 Mahali pa maandiko aliposoma ndipo, Alichukuliwa kama kondoo katika matindo, na kama mwana kondoo
- 33 akikatwa suffuf hakufunua kanwa lake. Katika kuthili kwake huhumu yake ikaondolewa : nani atakayeeleza kizazi chake? kwani maisha yake imetolewa katika ulimwengu.
- 34 Towashi akamjibu Filipo, akanena, Nakuomba, ya nani nabii amesema haya? ya mwenyewe au mtu
- 35 mwingine? Filipo akafunua kanwa lake akaanza kwa andiko hili akamhubiria Isa.
- 36 Nao wakienda njiani wakafika palipo maji : towashi akanena, Tazama, maji ; yanizuia nini nisibatizwe?
- 37 Filipo akanena, Ukiamini kwa moyo wote, ni halali. Akajibu akanena, Namwamini Isa ndiye Mwana wa
- 38 Muungu. Akaamuru gari lisimame : wakashuka wote wawili katika maji, na Filipo na towashi ; akambatiza.
- 39 Walipotoka katika maji, Roho ya Bwana ikamchukua Filipo, towashi asimwone tena : akaenda zake aki-furahi.
- 40 Filipo akaonekana katika Azoto : akipita akahubiri katika miji yote, hatta akafika Kaisariya.
- 9 SAUL akitoa kuogofya na kuua kwa waanafunzi wa Bwana, akamwendea mkohani mkuu, akataka kwake
- 2 nyaraka kwa Dameski, kwa masunagogi, akiona mtu

wa njia hii, akiwa mume akiwa mke, amlete Yerusalemi mfungwa.

Hatta katika kusafiri akakaribia Dameski: marra 3
 ikaangaza kwake nuru katika mbinguni: akaanguka 4
 chini, akasikia sauti ikimwambia, Saul, Saul, mbona 5
 wanifukuza? Akanena, Nani wewe, Bwana? Bwana aka- 6
 nena, Ndimi Isa, unifukuzaye. Ondoka ukaingie mjini; 7
 utaambiwa ufanyeje. Watu waliosafiri pamoja naye 8
 wakasimama wakinyamaza, wakasika sauti, wasione 9
 mtu. Saul akaondoka katika inchi; macho yake
 yalipofumbuka haoni mtu: wakamshika mkono waka-
 leta katika Dameski. Akawa siku tatu haoni, wala
 hali, wala hanywi.

Palikuwa na mwanafunzi kwa Dameski, jina lake 10
 Ananiya. Akamwambia Bwana katika njozi, Ana-
 niya! Akanena, Tazama, mimi, Bwana. Bwana 11
 kwake, Ondoka ukaende katika njia iliyoitwa Ime-
 nyoka, ukamtake nyumbani mwa Yuda aitwaye Saul
 wa Tarso: kwani yuko anaomba, naye amemwona 12
 katika njozi mtu jina lake Ananiya akiingia akimtia
 mikono, apewe kuona.

Ananiya akajibu, Bwana, nimemsikilia mtu huyu 13
 kwa wengi, mabaya aliyowafanyia watakatifu wako
 walioko Yerusalemi: hapa tena anazo nguvu kwa 14
 wakohani wakuu awafunge wote wakuombao jina lako.
 Bwana akamwambia, Enenda zako: kwani ndiye 15
 chombo kilichochaguliwa kwangu, alichukue jina langu
 kwa mataifa, na wafalme, na waana wa Israeli. Kwani 16
 nitamwonya mambo yapi makuu yatakayompata kwa
 ajili ya jina langu.

Ananiya akaenda zake, akaingia nyumbani, akatia 17
 mikono yake juu yake, akinena, Ndugu Saul, Bwana
 Isa, aliyekutokea njiani ujjayo, amenipeleka, upewe
 kuona, ukajae Roho Mtakatifu. Marra yakaanguka 18
 machoni kama mapao, akapewa marra kuona, aka-
 ondoka, akabatizwa. Alipopokea chakula akapata 19
 nguvu.

Saul akawako siku na waanafunzi walioko Dameski.
 Marra akamhubiri Masiya katika masunagogi, kama 20
 ndiye Mwana wa Muungu. Wote waliosikia waka- 21
 ajabu, wakanena, Siye huyu aliyewaharibu walioomba
 jina hili katika Yerusalemi, akaja hapa kusidi hili

- 22 awalete wafungwa kwa wakohani wakuu? Saul akazidi kupata nguvu, akawaaibisha Wayahudi waliokaa katika Dameski, akithubutisha kama huyu ndiye Masiya.
- 23 Hatta siku nyingi zilipopita, Wayahudi wakafanya
24 shauri wamue: lakini hila yao ikajulikana na Saul.
- 25 Wakavizia milangoni mchana na usiku wamue. Wanafunzi wakamtwaaw usiku wakashusha ukutani katika kapu.
- 26 Saul alipofika Yerusalemi, akataka kujiunga na wanafunzi: wakamwogopa wote, wala hawakusadiki kama
27 ndiye mwanafunzi. Barnabas akamtwaaw akaleta kwa mitume, akawaelezea kama amemwona Bwana njiani, naye akasema naye, na kama amehubiri pasipo hofu
28 katika Dameski kwa jina lake Isa. Akawa nao akiiingia akatoka katika Yerusalemi.
- 29 Akanena kwa jina lake Bwana Isa pasipo hofu, akashindana na Wahelenisti: nao wakataka kumua.
- 30 Ndugu wakijua wakamleta hatta Kaisariya, wakampe-
31 leka Tarso. Makanisa wakapumzika katika Uyahudi wote, na Galilaya, na Samaria, wakatengenezwa, wakazidi wakienda katika hofu ya Bwana na faraja ya Roho Mtakatifu.
- 32 Ikawa Petro akipita pote, akashuka kwa watakatifu
33 waliokaa Ludda. Huko akaona mtu jina lake Ainea, aliyekaa kitandani miaka minane, akaugua kupooza.
- 34 Petro akamwambia, Ainea, Isa Masiya akuponya:
35 ondoka ukafanyize matandiko. Marra akaondoka. Nao wote waliokaa katika Ludda na Saron wakamwona, wakamgeukia Bwana.
- 36 Palikuwa katika Yoppa mwanafunzi, jina lake Tabitha, maana yake Paa: mwanamke huyu akajaa matendo mema na sadaka alizozifanya. Ikawa siku zile
37 akaugua, akafa: walipomwosha wakaweka orofani. Na Ludda ikawa karibu na Yoppa, nao waanafunzi wamesikia kama Petro yuko, wakampelekea watu wawili, wakitaka asikawie kuja kwao.
- 39 Petro akaondoka akafuatana nao. Alipokuja wakamleta orofani: wajaani wote wakamsimamia wakilia, wakaonyesha kanzu na nguo alizozifanya Paa, alipoku-
40 wako nao. Petro akawatoa wote, akapiga magote, akaomba, akaugueukia mzoga akanena, Tabitha, ondoka!

Akafumbua macho, akamwona Petro, akakaa kitako. Akampa mkono akamwinua ; hatta akiisha kuwaita 41 watakatifu na wajaani akamtoa hayi. Ikajulikana 42 katika Yoppa pia ; wengi wakamwamini Bwana. Ikawa 43 akakaa siku nyingi katika Yoppa, nyumbani mwa Siman mfanyiza ngozi.

PALIKUWA na mtu katika Kaisariya, jina lake 10 Kornelio, amiri wa kikozi kilichoitwa Kiitaliano, mtawa, 2 na mcha Muungu pamoja na nyumba yake yote, aliyetoa sadaka nyingi kwa watu, akamwomba Muungu sikuzote. Akaona njozini kwa wazi, kama saa ya tissa ya mchana, 3 malaika wa Muungu akimwingilia, akamwambia, Kornelio ! Akimtazama akaogopa, akasema, Kuna nini, 4 Bwana ? Akamwambia, Kuomba na sadaka zako zimepanda kwa ukumbusho mbele ya Muungu. Bassi ukapeleke watu hatta Yoppa, ukamwite Siman, mwenyi jina la Petro : anakaa pamoja na Siman mfanyiza ngozi, 6 nyumba yake iko pwani : atakwambia yalivyokupasa kufanya. Malaika aliyesema na Kornelio alipotoka, 7 akaita watumishi wake wa nyumbani wawili, na asikari mtawa wao waliomngojea dayima ; alipokwisha kuwaelezea mambo yote akawapeleka Yoppa. 8

Hatta siku ya pili, wakienda katika kusafiri, wakaribia mji, Petro akapanda darini aombe kama saa a sita : akaingiwa na njaa nyingi, akataka kula : lakini 10 walipokuwa wakiandalia, ikazimia roho, akaona mbingu 11 zimefunuka, chombo kikamshukia kama tanga kubwa zimefungwa pembe 'ne, ikashushwa chini. Ndani 12 yake ginsi zote za nyama zenzi miguu minne, na nyama za mwituni, nazo zitambaazo, na ndege za anga. Aka- 13 jiwa na sauti, Ondoka, Petro, uchinje ukale. Petro 14 akanena, Sivyo, Bwana, kwani sikula kamwe kilicho kinyonge ao kinajisi. Sauti kwake tena marra ya pili, 15 Muungu alivyovitakasa, usivinene wewe najisi. Ika- 16 fanyika marra tatu : chombo kikapokewa tena mbinguni.

Hatta Petro akiona shaka moyoni, maana yao aliyo- 17 yaona nini, tazama, watu waliopelekwa na Kornelio wameiulizia nyumba ya Siman, wakasimama mbele ya mlango, wakaita, wakauliza kama Siman mwenyi jina 18 Petro amekaa humo. Petro akiifikiria njozi, Roho 19 ikamwambia, Tazama, watu watatu wanakutaka. Ondo- 20

ka kashuka, ukafuatane nao, usione shaka, kwani ndimi niliyewaleta.

21 Petro akawashukia watu aliompelekea Kornelio, aka-

22 mmekuja? Wakanena, Kornelio amiri, mtu wa haki,

na meha Muungu, mwenyi sifa njema kwa taifa lote la

23 akulete katika nyumba yake, akusikie maneno. Aka-

waingiza, akawakalisha. Hatta siku ya pili, Petro

akatoka pamoja nao, na ndugu wa katika Yoppa waka-

fuatana naye.

24 Hatta siku ya pili yake, wakaingia katika Kaisariya.

Kornelio akawangoja, amekusanya jamaa zake na rafiki

25 zake. Petro akaingia, Kornelio akamjia akamwangukia

26 miguuni, akasujudu. Petro akamwinua akisema, Si-

27 mama; nami ni mtu mwenyewe. Katika kusema naye

akaingia, akaona wengi waliokusanyika.

28 Akawaambia, Mwajua kama si halali mtu aliye Mya-

hudi azumgumze naye ao amjie aliye wa taifa jingine:

29 lakini Muungu amenionya nisimwite mtu wo wote

mnyonge ao mnajisi. Kwa sababu hiyo nalikuja nisi-

katae, nilipoitwa: nauliza tena kwa maana gani mme-

niita.

30 Kornelio akanena, Leo siku ya nne, nalikuwa niki-

funga hatta saa hii, saa ya tissa, nikaomba nyumbani

mwangu: hatta tazama, mtu akasimama mbele yangu

31 mwenyi nguo zing'azo, akanena, Kornelio, kuomba

kwako kumesikiwa, sadaka zako zikakumbukwa ma-

32 choni pa Muungu. Upeleke hatta Yoppa, ukamwite

hapa Siman, mwenyi jina Petro; anakaa nyumbani

mwa Siman mfanyiza ngozi, iliyoko pwani: naye akija

33 atasema nawe. Marra nikakupelekea; ukafanya vema

ukija. Bassi sisi tupo hapa sote mbele ya Muungu,

tuyasikie yote uliyoomriwa na Muungu.

34 Petro akafunua kanwa, akasema, Kweli naona kama

35 Muungu haangalii watu: lakini katika taifa lo lote,

36 amchaye, atendaye haki, amekubalika naye. Neno

alilolipeleka kwa waana wa Israeli, akihubiri amani kwa

37 Isa Masiya, ndiye Bwana wa yote, neno lile mmelijua,

lililotolewa katika Uyahudi wote, likaanza katika Gali-

38 laya baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana; kama

Muungu amemtia mafuta Isa wa Nazareti kwa Roho

Mtakatifu na nguvu : aliyetembea akifanya mema, aki-
waponya wote walioonewa na shetani; kwani Muungu
yuko naye. Naswi mashahidi ya mambo yote aliyoya- 39
ianya, na katika inchi ya Wayahudi, na katika Yeru-
salemi. Waliomua wakamtundika mtini ndiye Muungu 40
aliyemfufua siku ya tatu akamwonyesha kwa wazi, si 41
kwa watu wote, illa kwa mashahidi waliochaguliwa
mbele na Muungu, kwa sisi, tuliokula tukanywa naye
baada alipofufuka katika wafu. Akatuamuru tuwahu- 42
birie watu tukashuhudu kama ndiye aliyeamriwa na
Muungu, Mhukumu wahayi na wafu. Naye nabii wote 43
wamshuhudia, kama kwa jina lake amwaminiye yote
apewe ondoleo la thambi.

Petro akiwa katika kunena maneno haya, Roho Mta- 44
katifu akawaangukia wote waliolisikia neno. Wale 45
walio wa tohara walioamini wakaajabu, waliokuja pamoja
na Petro, kwa sababu na juu ya mataifa umetolewa
upaji wa Roho Mtakatifu. Kwani wakawasikia waki- 46
nena kwa lugha, wakamtukuza Muungu.

Akajibu Petro, Aweza mtu kukataza maji hawa wasi- 47
batizwe, waliopewa Roho Mtakatifu vivi kama sisi?
Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Bwana. Waka- 48
mwomba akae siku.

MITUME na ndugu walioko katika Uyahudi waka- 11
sikia kama mataifa tena wamepokea neno la Muungu.
Hatta Petro alipopanda Yerusalemi wale walio wa to- 2
hara wakashindana naye wakisema, Uliwaingilia watu 3
wasiotahiriwa, ukala nao. Petro akatoa tangu mwanzo 4
akaeleza kwao taratibu, akisema, Nalikuwa mjini mwa 5
Yoppa nikiomba, roho ikazimia, nikaona njozi. Chombo
kikashuka kama tanga kubwa, imeshushwa mbinguni
kwa pembe nne, ikanijia mimi : nilipokaza kuitazama 6
nikafikiri, nikaona nyama za inchi zenye miguu minne,
na nyama za mwituni, nazo zitambaazo, na ndege za
anga. Nikasikia sauti ikiniambia, Ondoka, Petro, 7
chinje ukale. Nikasema, Sivyoy, Bwana, kwani kitu 8
kilicho kinyonge ao kinajisi hakikuniingia kanwani
kamwe. Sauti ikanijibu tena katika mbinguni, Muungu 9
alivyovitakasa usiite vinyonge. Hivi vikafanyika marra 10
tatu, vyote vikapandishwa tena mbinguni. Na tazama 11
marra, walikuwako watu watatu wamekwisha kuja kwa
nyumba niliyomo, waliopelekwa kwangu katika Kai-

- 12 sariya. Roho akaniambia nifuatane nao, nisione shaka.
Hawa tena ndugu sita wakaenda pamoja nami, tukaingia
- 13 nyumbani mwake yule: akatuonya ginsi alivyoona
malaika nyumbani, aliyesimama akamwambia, Peleka
watu hatta Yoppa, ukamwite Siman mwenyi jina Petro,
- 14 atakayekwambia maneno, yatakayokuokoa wewe na
15 nyumba yako wote. Nami nikianza kunena, Roho
Mtakatifu akawaangukia, kama mwanzo juu yetu.
- 16 Nikakumbuka neno lake Bwana, akisema, Yohana
alibatiza kwa maji, lakini ninyi mtabatizwa na Roho
17 Mtakatifu. Bassi Muungu akiwapa karama ileile kama
kwetu, tuliomwamini Bwana Isa Masiya, mimi nani
nimpinge Muungu?
- 18 Walipoyasikia haya, wakanyamaza, wakamtukuza
Muungu, wakisema, Hatta kwa mataifa Muungu ame-
toa toba la uzima.
- 19 Nao waliotawanyika kwa fukuzo lililomwondokea Ste-
fano wakasafiri hatta Foiniki, na Kupro, na Antiokia,
20 wasihubiri neno illa kwa Wayahudi peke yao. Wangine
wao watu wa Kupro na Kurene, nao walipofika Antiokia
wakasema na Wahelenisti, wakimhubiri Bwana Isa.
- 21 Mkono wa Bwana ulikuwako nao: wengi wakaamini,
wakamgeukia Bwana.
- 22 Habari hizi zikafika masikioni pa kanisa lililo katika
Yerusalemi: wakampeleka Barnaba aende hatta Antio-
23 kia. Naye alipokwisha fika akaona neema ya Muungu,
akafurahi, akawaonya wote, kwa kusudi la moyoni wa-
24 mshike Bwana. Kwani mtu mwema, akajaa Roho
Mtakatifu na imani: makutano marithawa wakaletwa
kwa Bwana.
- 25 Akatoka Barnaba kwenda Tarso kumtafuta Saul:
26 akiisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa mwaka
mzima wakakusanyana na kanisa, wakawafundisha watu
wengi. Waanafunzi wakaitwa Wamasihya kwanza ka-
tika Antiokia.
- 27 Siku zile wakashuka nabii katika Yerusalemi hatta
28 Antiokia. Akasimama mmoja wao, jina lake Agabo,
akaonya kwa Roho itakuwa njaa nyingi katika ulimwe-
29 ngu wote: ikawa siku za Klaudio Kaisari. Waana-
funzi, killa mtu kwa kadri yake, wakashika wapeleke
30 riziki kwa ndugu waliokaa katika Uyahudi. Wakafanya,
wakapeleka kwa wazee, kwa mkono wa Barnaba na Saul.

WAKATI ule Herode mfalme akanyosha mikono 12
 athiishe walio wa kanisa. Akamua Yakobo ndugu wa 2
 Yohana kwa upanga. Na kwa sababu ameona imewa- 3
 pendeza Wayahudi, akaendelea tena akamtwa na Pe-
 tro. Ndizo siku za mikate isiyo na chachu. Alipo- 4
 kwisha kumkamata, akaweka gerezani, wakampokea
 manne manne wa asikari wamlinde, akikusudia baa-
 da ya Pasaka kumtoa kwa watu. Petro akalindwa 5
 gerezani: akaombewa pasipo kukoma na kanisa kwa
 Muungu.

Hatta wakati Herode angalimtoa, usiku uleule, Petro 6
 alikuwa amelala kati ya asikari wawili, amefungwa kwa
 minyororo miwili, walinzi mbele ya mlango wakailinda
 gereza. Malaika ya Bwana akasimama, nuru ikaangaza 7
 chumbani, akampiga Petro mbavuni akamwamsha, aki-
 sema, Ondoka upesi. Minyororo ikamwangukia mikono.
 Malaika akamwambia, Jifunge, ukavae viatu. Akafanya. 8
 Akamwambia, Jitupie vazi ukanifuata. Akatoka, aka- 9
 mfuata, wala hakujua ndiyo kweli aliyoyafanya malaika;
 akathani ameona njozi.

Walipopita lindo la kwanza na la pili, wakaja kwa 10
 mlango wa chuma ulioleta mjini. Ukawafunukia peke
 yake. Wakatoka, wakupita katika njia moja; marra
 malaika akamwacha. Hatta Petro alipojirudia, akanena, 11
 Sasa nimejua, yakini Bwana amepeleka malaika, ameni-
 toa katika mkono wa Herode, na kutazamia kwote kwa
 watu wa Wayahudi. Alipofikiri, akaja nyumbani pa 12
 Maryamu, mama wake Yohana mwenyi jina Marko,
 wengi walikokusanyika wakiomba.

Petro akigonga bau la mlangoni, kijakazi akaja asikie, 13
 jina lake Roda. Alipomjua sauti Petro, hafunui mlango 14
 kwa furaha, akaingia mbio, akanena kama Petro ana-
 simama mbele ya mlango. Wakamwambia, Una wazimo. 15
 Akasema kwa nguvu kama ndivyo. Wakanena, Ni ma-
 laika yake.

Petro akashinda kugonga: hatta walipofunua waka- 16
 mwona, wakaajabu. Naye akiwafanya ishara kwa mkono 17
 wanyamaze, akawahubiria Bwana alivyomtoa katika
 gereza. Akasema, Enendeni mkaonyeshe haya kwa
 Yakobo na ndugu. Akatoka, akaenda pahali pangine.

Bassi ukiwa mchana, asikari wakafathaika sana, ame- 18
 kuwaje Petro. Herode alipomtafuta, asimwone, akawau- 19

lizia walinzi, akaamuru waathibike. Akashuka katika Uyahudi hatta Kaisariya, akakaa.

- 20 Herode akakasirika sana nao wa Turo na Sidoni : waka-
kaja kwake kwa moyo mmoja, wamefanya urafiki na
21 Blasto aliye chumbani mwa mfalme, wakataka amani :
kwani inchi yao yalishwa nayo ya mfalme. Hatta siku
iliyochaguliwa, Herode amevaa mavazi ya kifaume,
22 akakaa kitini mwa enzi, akawafanyia maneno. Watu
wakapiga kelele, Sauti ya muungu, wala si ya mwana
23 Adamu. Marra malaika wa Bwana akampiga, kwa
sababu hakumpa heshima Muungu : akaliwa na funza,
akatoa roho.

²⁴₂₅ Neno la Muungu likakua, likazidi. Barnaba na Saul
wakarudi katika Yerusalemi walipotimiza kazi yao, wa-
kachukua nao Yohana mwenyi jina Marko.

- 13 PALIKUWAKO** katika Antiokia, katika kanisa
lilioko, nabii na waalimu, Barnaba, na Simeon aliyeitwa
Niger, na Lukio Mkurene, Manaen ndugu wa kunyonya
wake Herode tetrarko, na Saul.

2 Wakifanya dini yake Bwana, wakafunga, akanena
Roho Mtakatifu, Mniwekee Barnaba na Saul kwa kazi
3 waliyoitiwa nami. Wakafunga wakaomba, wakawatia
mikono, wakawaacha kwenda.

4 Nao wakipelekwa na Roho Mtakatifu, wakaenda
hatta Selukia; huko wakatweka wakaenda Kupro.

5 Wakiwa katika Salamini wakalihubiri neno la Muungu
katika masunagogi yao Wayahudi. Wakawa na Yoha-
na kuwasayidia.

6 Wakipita katika kisiwa chote hatta Pafu, wakaona
mtu mjuzi, nabii wa uwongo, Myahudi, jina lake Barisa,

7 aliyekuwako pamoja na prokonsuli Sergio Paolo, mtu
wa akili, aliyewaita Barnaba na Saul, akataka kulisikia

8 neno la Muungu. Akashindana nao Eluma, ndiye mju-
zi, kwani ndilo jina lake likifasirika, akitaka kumgeuza

9 prokonsuli katika imani. Illa Saul, aliye Paolo, akijaa

10 Roho Mtakatifu, akikaza macho juu yake, akanena, Ewe
uliyejaa hila na uharabu wote, mwana wa shetani, adui wa

11 ma? Bassi angalia, mkono wake Bwana juu yako, uta-
kuwa kipofu, usilione jua kitambo. Marra kikamwa-
ngukia kiwi na giza, akazunguka akitaka watu wa
kushika mkono.

Akiona prokonsuli yaliyokuwa, akaamini, akataajabu 12
kwa elimu ya Bwana.

Wakatoka katika Pafu wenzake Paolo, wakafika Perga 13
ya Pamfulia. Yohana akawaacha, akarudi Yerusalemi.

Nao wakipita katika Perga, wakafika Antiokia wa 14
Pisidia, wakaingia katika sunagogi siku ya sabato, wa-
kaka kitako. Baada ya kusomwa torati na nabii, wakuu 15
wa sunagogi wakawapelekea, wakisema, Waume ndugu,
mkiwa na neno la kuwafaa watu, mnene.

Akasimama Paolo, akapungia mkono akanena, Waume 16
Waisraeli, nanyi 'mmchao Muungu, sikieni. Muungu 17
wa watu hawa wa Israeli aliwachagua baba zetu, aka-
wainua watu wasipo kwao katika inchi ya Misri, na kwa
mkono ulioinuliwa akawatoshia. Kama muda wa miaka 18
arobaini akawalisha katika jangwa. Akaondoa mataifa 19
saba katika inchi ya Kanaan, akawagawanyia kwa kura
inchi yao. Baadaye kama miaka aroba mia na hamsini 20
akawapa waamuzi hatta nabii Samwil. Hatima wa- 21
kataka mfalme; Muungu akawapa Saul mwana wa Kish,
mtu wa kabila ya Benyamin, miaka arobaini. Akamwo- 22
ndoa huyu, akawaletea Daúd kuwa mfalme, aliyemnena
akishuhudia, Nimemwona Daúd wa Yesse, mtu kwa
moyo wangu, atakayefanya niyapendayo yote. Katika 23
wazao wake, Muungu kwa ahadi yake amewaletea Israeli
Mwokozi, Isa, akihubiri Yohana mbele ya kuja kwake 24
ubatizo wa kutubu kwa watu wote wa Israeli. Naye 25
Yohana akimaliza mwendo wake akanena, Mwanithani
ni nani? Si mimi, lakini angalia, anakuja nyuma yangu,
wala mimi sistahili kumlegezea ukanda wa miguuni
mwake. Waume ndugu, waana wa wazao wa Ibrahimu, 26
nanyi kwenu mmchao Muungu, kwenu neno la wokovu
huu limepelekwa. Kwani wakaa Yerusalemi na wakuu 27
wao, wasipomjua huyu, wala sauti za nabii wanaosomwa
killa sabato, wakihukumu wameyatimiza. Nao wasipo- 28
pata sababu ya kufa wakamtaka Pilato auawe. Hatta 29
yalipokwisha yote aliyoandikiwa, wakamshusha katika
mti waka'mweka kaburini. Muungu akamfufua katika 30
wafu: akaonekana siku nyingi nao waliopanda naye ka- 31
tika Galilaya hatta Yerusalemi, walio sasa mashahidi
wake kwa watu. Bassi sisi sasa twawapa habari njema, 32
kama ahadi iliyokuwa kwa baba, Muungu ameitimiza 33
kwa sisi waana wao, akimfufua Isa; kama ilivyoandikwa

katika Zaburi ya pili, Ndiwe Mwana wangu niliyekuzaa
 34 leo. Kama alifufuka katika wafu asigeuke tena kuhari-
 bika, akanena hivi, Nitakupa weve matakatifu amini ya
 35 Daudi. Kwa hiyo panginipo akasema, Hutamtoa mta-
 36 katifu wako aone uharibifu. Kwani Daúd akawafaa
 kizazi chake akalala kwa shauri lake Muungu, akawekwa
 37 kwa baba zake, akaona uharibifu. Yule, Muungu aliye-
 38 mfufua, hakuona uharibifu. Bassi ijulike kwenu, waume
 ndugu, kama kwa huyo ondoleo la tbambi limehubiriwa,
 39 na yote yasiyoweza kuondolewa kwa torati ya Musa,
 kwa huyo killa aaminiye huondolewa.

40 Angalieni yasije juu yenu yaliyonenwa na nabii,
 41 Tazameni, enyi mtharauo, taajabuni, mtoweke: kwani
 natenda jambo mimi siku zenu, jambo msilolisadiki,
 hatta mtu akiwaonyesha.

42 Wakitoka, wakawataka wawaambie maneno haya
 hatta sabato ya pili.

43 Sunagogi ikitawanyika, Wayahudi wengi na waongofu
 watawa wakawafuata Paolo na Barnaba; nao wakisema
 nao wakawathubutisha wakae katika neema ya Muungu.

44 Hatta sabato ya pili kama mji wote ukakusanyika
 wasikie neno la Muungu.

45 Wayahudi wakiwaona makutano, wakajaa uwivu,
 wakanena juu ya mambo yaliyonenwa na Paolo, waki-
 46 yanenea, wakiyafanyia unajisi. Paolo na Barnaba
 wakathubutika wakanena, Sharti tunene kwanza kwenu
 neno lake Muungu: mkilisukumia mbali, wala ha-
 mjioni kuustahilia uzima wa milele, angalia, twawageu-
 47 kia mataifa. Kwani hivi tumeamriwa na Bwana,
 Nimekuweka kuwa nuru ya mataifa, uwe kwa wokovu
 48 hatta mwisho wa ulimwengu. Mataifa wakisikia waka-
 furahi, wakalisifu neno lake Bwana, wakaamini walio-
 kuwa wamewekwa kwa uzima wa milele.

49 Likaenea neno la Bwana katika inchi ile yote.
 50 Illa Wayahudi wakawasukuma waanawake waongofu
 wenyi cheo, na wakuu wa mjini, wakafanya fukuzo
 juu ya Paolo na Barnaba, wakawatoa katika mipaka
 51 yao. Wakatikisia mbali mavumbi ya miguuni juu yao,
 52 wakaja hatta Ikonio. Waanafunzi wakajaa furaha na
 Roho Mtakatifu.

14 IKAWA katika Ikonio wakaingia wote katika
 sunagogi ya Wayahudi, wakanena hatta wengi wengi

wakaamini, na Wayahudi na Wayonani. Wayahudi 2
 wasioamini wakawasukuma wamataifa, wakawatia nia
 mbaya kwa ndugu. Wakati kathawakatha wakakaa, 3
 wakithubutika naye Bwana, aliyelishuhudia neno la
 neema yake, akitoa ishara na mataajabu kuwa kwa
 mikono yao. Jamii ya mjini ikatengwa: wangine 4
 wakawa kwa Wayahudi, wangine kwa mitume. Ilipo- 5
 kuwa fitina ya wamataifa na Wayahudi, pamoja na
 wakuu wao, wawafanyie jeuri, wawatupie mawe, waki- 6
 pata habari, wakakimbia hatta miji ya Lukaonia, Lustra
 na Derbe, na inchi karibu yao, wakakaa huko waki- 7
 hubiri anjili.

Mtu katika Lustra asiye na nguvu katika miguu 8
 akakaa, kiwete tangu tumboni mwa mamaye, asiye-
 kwenda kabisa. Huyu akasikia Paolo akinena: aka- 9
 mkazia macho, akaona amekuwa na imani aokoke,
 akanena kwa sauti kuu, Simama juu ya miguu yako 10
 ujinyoshe. Akaruka juu akatembea. Makutano wali- 11
 pouna Paolo alivyofanya, wakapaliza sauti yao, waki-
 sema kwa Kilukaonia, Miungu wamefanana na waana
 Adamu, wametushukia. Wakamwita Barnaba Zeu, na 12
 Paolo Herme, kwani ndiye aliyetangulia kunena.
 Mkohani wa Zeu, iliyoko mbele ya mji, akaleta ng'ombe 13
 na taji za maua hatta malangoni, akitaka kutoa tha-
 bihu pamoja na makutano. Waliposikia mitume, 14
 Barnaba na Paolo, wakararua nguo zao, wakawatokea
 makutano upesi, wakipiga kelele wakisema, Waume, 15
 mwafanyani haya? Sisi waana Adamu tunaopatwa
 kama ninyi, tunaowahubiria mgeuke katika matupu
 haya, kwa Muungu aliye hayi, aliyezifanya mbingu na
 inchi, na bahari, na yote yaliyomo. Zamani zilizopita 16
 amewaacha mataifa yote yaende katika njia zao.
 Illakini hakujiacha hana shahidi, akitenda vema, akitoa 17
 kwetu katika mbinguni mvua na wakati za kuzaliwa
 matunda, akijaliza mioyo yetu chakula na furaha.

Wakisema haya, kwa shidda wakawazuia makutano 18
 wasiwatolee thabihu.

Wakaja Wayahudi katika Antiokia na Ikonio, waka- 19
 washawishi makutano, wakamtupia mawe Paolo,
 wakamvuta 'nje ya mji, wakamthania amekufa. Hatta 20
 waanafunzi wakimzunguka akasimama, akaingia mjini:
 na siku ya pili yakeakaenda zake na Barnaba hatta Derbe.

- 21 Wakahubiri anjili katika mji ule, wakafundisha
marithawa, wakarudi katika Lustra, na Ikonio, na
- 22 Antiokia, wakifanya imara roho za waanafunzi, waka-
waonya wakae katika imani, na kama kwa shidda
nyingi imetupasa kuingia katika ufalme wa Muungu.
- 23 Wakawafanyia wazee kanisa kwa kanisa, wakiomba
na kufunga, wakawaweka kwa Bwana waliyemwa-
mini.
- 24 Wakapita katika Pisidia, wakaja hatta Pamfulia,
25 wakalitoa neno katika Perga, wakashuka Attalia,
26 huko wakatweka wakaenda hatta Antiokia, walikoto-
lewa katika neema ya Muungu kwa kazi waliyoiti-
miza.
- 27 Walipofika wakawakusanya kanisa, wakayatangaza
Muungu aliyoyafanya kwao, na kama amewafunulia
28 mataifa mlango wa imani. Wakaongea wakati si haba
pamoja nao waanafunzi.
- 15** HATTA watu waliotoka katika Uyahudi wakawa-
fundisha ndugu, Kama msipotahiriwa kwa desturi ya
Musa, ha'mwezi kuokoka.
- 2 Ikiwa fitina na maulizo mengi kwa Paolo na
Barnaba na hawo, wakashika waende Paolo na Barnaba
na wangine wao, kwa mitume na wazee walio katika
Yerusalemi, kwa swali hiyo.
- 3 Nao wakiletwa njiani na kanisa, wakapita katika
Foiniki na Samaria, wakionyesha kuongoka wama-
4 taifa: wakafanya furaha nyingi kwa ndugu. Waki-
fika Yerusalemi wakakaribishwa na kanisa, na mitume,
na wazee, wakatangaza mambo yapi Muungu aliyoya-
tenda kwao.
- 5 Wakaondoka watu walio wa mathehebu ya Mafarisayo
walioamini, wakisema kama sharti watahiriwe wakaa-
6 gizwe waishike torati ya Musa. Wakakusanyika
mitume na wazee waangalie kwa mambo haya.
- 7 Palipokuwa maulizo mengi, akasimama Petro, aka-
waambia, Waume ndugu, mwajua kama zamani
Muungu alichagua kwetu, wamataifa wasikie kwa
8 kanwa langu mimi neno la anjili, wakaamini. Naye
Muungu, ajuaye mioyo, akawashuhudia, akiwapa Roho
9 Mtakatifu kama sisi, wala hakuweka tofauti katika
10 sisi na wao, akisafisha mioyo yao kwa imani. Bassi
sasa mbona mwamjaribu Muungu, kuweka nira juu ya

shingo la waanafunzi, tusiyoweza kuichukua, wala sisi wala baba zetu? Illa kwa neema yake Bwana Isa 11 twaamini tuokoke, nao wale vivyo.

Jamii ya watu wakanyamaza, wakawasikia Barnaba 12 na Paolo, wakieleza ishara zipi na mataajabu Muungu aliyoyafanya kwao katika mataifa.

Baada ya kunyamaza hawa, Yakobo akajibu akanena, 13 Waume ndugu, nisikieni. Simeon ameeleza ginsi 14 Muungu alivyoangalia kutoa katika mataifa watu kwa jina lake. Maneno ya nabii yapatana na hayo; 15 kama imeandikwa, Baadaye nitageuka, nitajenga tena 16 masikani ya Daúd iliyoanguka, nitajenga tena yaliyo-pomoshwa yake, nitaitengeneza: illi wamtafute Bwana 17 waana Adamu waliosalia, na mataifa yote, walioitiwa kwa jina langu juu yao, amenena Bwana mfanya haya yote. Imejulika tangu milele na Muungu kazi yake 18 yote. Kwa hiyo naamua tusiwataabishe waliomgeukia 19 Muungu katika mataifa; illa tuwapelekee, waepuke ma- 20 chafu ya sanamu, na asherati, na zilizosongwa, na damu. Kwani Musa anao tangu zamani za kale mji kwa mji 21 wamhubirio; katika masunagogi killa sabato husomwa.

Ikawapendeza mitume, na wazee, na kanisa lote, wa- 22 peleke watu waliochaguliwa kwao hatta Antiokia pamoja na Paolo na Barnaba, Yuda aliyeitwa Barsaba, na Sila, watu wakuu katika ndugu. Wakaandika kwa mikono 23 yao hivi, Mitume, na wazee, na ndugu, kwa ndugu walioko katika Antiokia, na Shami, na Kilikia, walio wa mataifa, salaamu. Tukiwa tumesikia kama watu waliotoka 24 kwetu wamewatia shaka kwa maneno, wakiharibu roho zenu, wakitoa kutahiriwa na kushika torati, tusiowaagiza: tumeona vema, tukikusanyika kwa moyo mmoja, kuwa- 25 letea ninyi watu waliochaguliwa pamoja na wapenzi wetu Barnaba na Paolo, watu waliotoa maisha yao kwa 26 jina la Bwana wetu Isa Masiya. Tumepeleka Yuda na 27 Sila, watakaowapa wenyewe habari hizo. Kwani ime- 28 mpendeza Roho Mtakatifu, na sisi, tusizidi kuwatia mzungu illa haya yaliyo kanuni, kuepuka zilizotolewa kwa 29 sanamu, na damu, na zilizosongwa, na asherati. Mkiji-zuia katika haya mtatenda vema. Salaamu.

Nao wakipewa ruksa wakaja Antiokia, wakawakusa- 30 nya jamaa, wakawapa waraka. Wakasoma, wakafura- 31 hiwa na faraja ile. Yuda na Sila wakiwa nao nabii, 32

wakawaonya ndugu kwa maneno mengi, wakawatia
 33 moyo. Zamani zilipopita, wakaachwa na ndugu kwenda
 34 katika amani kwao waliowapeleka. Akapenda Sila ku-
 kaa huko.

35 Paolo na Barnaba wakakaa katika Antiokia wakifu-
 ndisha na kuhubiri, pamoja na wengine wengi, neno
 lake Bwana.

36 Baada ya siku, Paolo akamwambia Barnaba, Tuzu-
 nguke tena tuwaone ndugu katika killa mji, tulipohubiri

37 neno lake Bwana, wa hali gani. Barnaba akapenda ku-

38 chukua Yohana aliyeitwa Marko. Paolo hakuona vema
 kumchukua nao, aliyewaacha katika Pamfulia, wala ha-

39 kuenda nao katika kazi. Ukawa ukali, hatta wakajite-
 ngana: Barnaba akamchukua Marko akasafiri kwenda

40 Kupro; Paolo akamchagua Sila, akatoka, akitolewa kwa

41 neema ya Bwana na ndugu. Akapita katika Shami na
 Kilikia, akawatia moyo makanisa.

16 AKAFIKA Derbe na Lustra, palikuwako huko mwa-
 nafunzi, jina lake Timoteo, mwanawe mwanamke Mya-

2 hudi mwenyi imani, na babaye Myonani, aliyeshuhudiwa

3 na ndugu walioko katika Lustra na Ikonio. Huyu Paolo

akataka afuatane naye; akamtwa akamtahiri, kwa ajili
 ya Wayahudi walioko katika mahali pale: kwani wote

wakamjua babaye ni Myonani.

4 Wakipita katika miji, wakawapa mafundisho yaliyo-
 amriwa na mitume na wazee walio katika Yerusalemi,

5 wayalinde. Makanisa yakafanyika imara katika imani,
 yakazidi kuwa wengi siku kwa siku.

6 Wakapita katika Frugia na inchi ya Galatia, wakae-
 pushwa na Roho Mtakatifu, wasiliteo neno katika Asia.

7 Wakaja katika Musia, wakajaribu kwenda katika Bitu-

8 nia, lakini Roho yake Isa hakuwapa ruksa. Wakapita
 katika Musia wakafika Troa.

9 Njozi ikaonekana usiku na Paolo: mtu Mmakedoni
 alikuwako akimwita, akanena, Uvuke hatta Umakedoni

10 utusayidie. Akiiona njozi, marra tukataka kutoka kwe-
 nda Umakedoni, tukithubutika kama Bwana ametuita

tuwahubirie anjili.

11 Tuking'oa nanga katika Troa, tukafika kwa májira ya

12 kunyoka Samothraki, na siku ya pili yake Neapoli, na
 huko hatta Filippi, iliyo mji wa kwanza wa sehemu ile
 ya Umakedoni, na kolonia.

Tukawa katika mji ule tukikaa siku. Hatta siku ya 13
 sabato tukatoka mlangoni kwa mtoni, pamewekwa huko
 mahali pa kuomba, tukakaa kitako, tukasema na waa-
 naake waliokusanyika. Mwanamke mmoja, jina lake 14
 Ludia, mfanya biashara ya porfuro, mtu wa Tuatira,
 mecha Muungu, akasikia; Bwana akamfunua moyo, aya-
 shike yaliyonenwa na Paolo. Akabatizwa yeye na nyu- 15
 mba yake, akatusihi akanena, Kama mmenithani ni amini
 kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae. Aka-
 tufanyia nguvu.

Ikawa tukienda mahali pa kuomba, kijakazi aliye na 16
 pepo ya Puthoni akatukuta, aliyewapatia bwana zake
 fayida nyingi kwa kubashiri. Naye akifuata Paolo na 17
 sisi, akapiga kelele, akanena, Watu hawa watumwa wake
 Muungu aliye juu, watuhubiriao njia ya wokovu. Aka- 18
 fanya haya siku nyingi. Akitaabika Paolo, akageuka
 akamwambia pepo, Nakuamuru kwa jina lake Isa Masiya,
 utoke katika huyu. Akatoka saa ileile. Bwana zake 19
 walipoona kama tumaini la fayida yao limepotea, waka-
 washika Paolo na Sila, wakawavuta barazani kwa wakuu.
 Wakawaleta kwa maamiri, wakasema, Watu hawa wa- 20
 tuharikisha mji wetu, wakiwa Wayahudi, wakifundisha
 desturi zisizo halali tuzipokee, wala tusitende, tukiwa 21
 Warumi. Makutano wakawaondokea: maamiri waka- 22
 wararulia nguo, wakaamuru wapigwe. Wakawatia
 mapigo mengi, wakatupa gereza, wakamwamuru mli- 23
 nda gereza awalinde sana. Naye akipewa amri hiyo
 akawatupa katika kifungo cha ndani, akawakaza miguu 24
 katika mkatale.

Hatta kati ya usiku Paolo na Sila wakaomba waka- 25
 mwambia Muungu: waliofungwa wakawasikiliza. Gha- 26
 fula palikuwa tetemeko kuu, hatta misinji ya gereza
 ikatikisika: marra milango yote ikafunuka, na vifungo
 vyao wote vikalegezwa. Mlinda gereza akaamka, akaona 27
 milango ya gereza imekuwa miwazi: akafuta upanga
 wake, akawa katika kujiua, akithani wafungwa wame-
 kimbia. Paolo akanena kwa sauti kuu, akisema, Usiji- 28
 fanyie vibaya: sisi wote hapa. Akitaka nuru, akaruka
 ndani, akitetemeka, akawaangukia Paolo na Sila; aka- 30
 waleta 'nje, akasema, Bwana, nifanye nini, nipate kuo-
 koka? Wakanena, Mwamini Bwana Isa Masiya, utao- 31
 koka na nyumba yako. Wakamwambia neno la Bwana, 32

- 33 pamoja nao wote waliomo nyumbani mwake. Akawa-
karibisha saa ileile ya usiku, akawaosha katika mapigo ;
- 34 akabatizwa, yeye na walio wake wote marra moja. Aka-
waleta nyumbani mwake, akatandika meza, akafurahi
na nyumba yake, akanwamini Muungu.
- 35 Ukiwa mchana, maamiri wakapeleka asikari wao, wa-
36 kisema, Fungue watu wale. Mlinda gereza akamletea
Paolo maneno haya, Maamiri wamepeleka mfunguliwe :
37 bassi sasa mtoke mkaende kwa amani. Paolo akawaa-
mbia, Wametupiga machoni pa watu tusipohukumiwa,
tukiwa watu Warumi, wametutupa gerezani ; na sasa
wanatuondokeshwa kwa siri? Sivyo. Waje wenyewe
- 38 watulete 'nje. Asikari wakawaambia maamiri maneno
39 haya ; wakaogopa wakisikia kama hawa Warumi. Wa-
kaja wakawasihi, wakawaleta 'nje, wakawataka watoke
40 katika mjini. Wakatoka gerezani, wakaenda kwa
Ludia : hatta walipowaona ndugu, wakawatia moyo,
wakatoka.
- 17 WAKAPITA** katika Amfipoli na Apollonia, waka-
fika Thessalonika, palipokuwa sunagogi ya Wayahudi.
- 2 Kama alivyozoea Paolo akaingia kwao, na sabato
3 tatu akajadiliana nao kwa maandiko, akifunua na
akishuhudisha, kama imempasa Masiya kuteswa, na
kuondoka katika wafu ; na kama huyu ndiye Masiya,
- 4 Isa ninayewahubiria. Wangine wao wakaamini, waka-
jiweka pamoja na Paolo na Sila ; na Wayonani walio-
mcha Muungu wengi tele, na waanaake walio wa
kwanza si wachache.
- 5 Wayahudi wakaingiwa na uwivu, wakajitwalia watu
wabaya wa wanyonge walio mjini, wakafanya makutano
wakaufathaisha mji. Wakaizunguka nyumba ya Yason,
- 6 wakataka kuwaleta mbele ya watu. Wasipowaona,
wakamvuta Yason, na ndugu, mbele ya wakuu wa
mjini, wakipiga makelele kama, Hawa walioupindua
7 ulimwengu wamekuja na hapa, naye Yason amewaka-
ribisha. Nao wote waasi juu ya amri zake Kaisari,
- 8 wakisema kuna mfalme mwingine, Isa. Makutano
wakataharakishwa, na wakuu wa mjini, wakiyasikia
9 haya. Wakatwaa uthamini kwa Yason na wangine,
wakawaacha.
- 10 Ndugu wakapeleka marra usiku Paolo na Sila hatta
Beroya. Nao wakifika wakaingia katika sunagogi ya

Wayahudi. Hawa walikuwa wangwana kuliko wale 11
wa Thessalonika, wakalipokea neno kwa moyo mwepesi,
wakiangalia siku kwa siku katika maandiko kama hivi
ndivyo. Wengi wao wakaamini, na waanaake Wayo- 12
nani wenyi heshima, na waume si wachache.

Hatta Wayahudi wa Thessalonika wakajua kama 13
katika Beroya neno la Muungu linahubiriwa na Paolo,
wakaja huko wakawatikisa makutano. Ndugu waka- 14
mpeleka marra Paolo kwenda kama hatta bahari,
wakikaa huko Sila na Timoteo. Nao waliomchukua 15
Paolo wakamleta hatta Atene, wakapokea amri kwa
Sila na Timoteo waje kwake upesi, wakaenda zao.

Katika Atene alipowangoja Paolo, roho yake ikacho- 16
meka ndani akiona mji umejaa sanamu. Akajadiliana 17
katika sunagogi na Wayahudi na waliomcha Muungu,
na sokoni killa siku nao waliomkuta. Watu wa Wa- 18
epikurio na Wastoiko, mafilosofu, wakamjia. Wangine
wakasema, Anataka kusema nini huyu mpuuzi?
Wangine, Kama ahubiriye miungu migeni. Kwani
ametoa habari za Isa na kufufuka. Wakamtwaa 19
wakamleta hatta Areopago, wakisema, Ni halali tujue
nini elimu hii mpya iliyonenwa nawe? Kwani waleta 20
mambo mageni masikioni petu. Twataka kujua maana
ya mambo haya. Kwani Waatene na wageni waliopo 21
hawakuzumgumza kwa neno, illa kunena ao kusikia
habari zilizo mpya.

Akasimama Paolo kati ya Areopago, akasema, 22
Waume Waatene, nimewaona ninyi katika mambo
yote mwaogopa sana miungu. Kwani nikipita nika- 23
angalia maabudu yenu, nikaona na mathbahu iliyo-
andikwa, Kwa Muungu asiyejulika. Mliyemwabudu
pasipo kumjua ndiye niliyewahubiria. Muungu aliyeu- 24
fanya ulimwengu na vyote vilivyomo, huyu akiwa
Bwana wa mbingu na inchi, hakai katika nyumba
zilizofanyika na mikono, wala hatumikwi na mikono ya 25
watu kama amehitaji neno, ndiye aliyewapa wote uzima,
na pumuzi, na vyote; akafanya ya damu moja killa 26
taifa la watu kukaa juu ya inchi yote, akiandika
muhulla na mipaka ya kukaa kwao; wakimtafuta 27
Bwana, wakipapasa, wamwone, akiwa si mbali ya killa
mtu kwetu: kwani katika huyu tunaishi, tunakwenda, 28
tunakuwapo; kama wangine watungao mashairi kwenu

- 29 wamesema, Kwani sisi wazao wake. Tukiwa wazao wa Muungu, hatukupaswa kumthania Muungu, amefanana na thahabu, ao fetha, ao jiwe, lililofanyikizwa
- 30 na busara na akili za waana Adamu. Wakati huo wa ujinga Muungu hakuangalia; illa sasa amewaa-
- 31 muru watu wote po pote watubu: kwani ameweka siku, atakayouhukumu ulinwengu kwa haki, kwa mtu aliyemwandika, akiwapa imani wote, alipomfufua katika wafu.
- 32 Waliposikia kufufuka katika wafu, wangine waka-thibaki; wangine wakasema, Tutakusikia tena kwa ³³₃₄ hayo. Paolo akatoka hivi katika kati mwao. Baathi ya waume wakaambatana naye, wakaamini; katika hawa Dionusio Mwareopago, na mwanamke jina lake Damari, na wangine pamoja nao.
- 18 BAADAYE Paolo akitoka katika Atene, akaja 2 Korinto. Akaona Myahudi jina lake Akula, aliyezaliwa katika Ponto, amekuja karibu katika Italia, pamoja na Priskilla mkewe, kwa sababu Klaudio ameamuru Wayahudi wote watoke katika Rumi; 3 akawajia. Na kwa kuwa na kazi moja akakaa nao akatenda kazi: kwani walikuwa kwa kazi wafanyi hema.
- 4 Akajadiliana katika sunagogi killa sabato, akawaonya Wayahudi na Wayonani.
- 5 Walipokuja katika Umakedoni Sila na Timoteo, akashurutizwa Paolo rohani, akawashuhudia Wayahudi, Isa ndiye Masiya.
- 6 Walipojiweka juu yake wakanena unajisi, akakung'uta nguo zake, akawaambia, Damu yenu juu ya vitwa vyenu; mimi safi: tangu sasa nawageukia 7 mataifa. Akapita huko akaja nyumba ya mtu jina lake Yusto, mcha Muungu, nyumba yake mpaka mmoja na sunagogi.
- 8 Krispo, mkuu wa sunagogi, akamwamini Bwana, na nyumba yake yote. Wakorinto wengi wakisikia waka- 9 amini wakabatizwa. Bwana akamwambia Paolo usiku 10 kwa njozi, Si ogope, illa nene, usinyamaze: kwani mimi pamoja nawe, wala mtu hatakuja akuthuru: kwani ninao watu wengi katika mji huu.
- 11 Akakaa kitako mwaka na miezi sita, akifundisha kwao neno lake Muungu.

Hatta Gallio akiwa Prokonsuli wa Akaya, Wayahudi 12 wakamwondokelea Paolo, wakamleta kwa kiti cha hukumu, wakinena kama, Juu ya sheria yetu huyu 13 anawashawishi watu wamwabudu Muungu. Paolo 14 akiwa tayari afunue kanwa lake, Gallio akawaambia Wayahudi, Kama imekuwa thulumu ao unyonge mwovu, enyi Wayahudi, kwa huja ningalichukuliana nanyi; ikiwa swali ya neno, na majina, na sheria iliyo kwenu, 15 angalieni ninyi; mimi sitaki kuwa mwamuzi wa mambo haya. Akawafukuza katika kitini pa hukumu. Wale 16 17 wote wakamtwa Sostene, muku wa sunagogi, waka mpiga mbele ya kiti cha hukumu. Wala Gallio haku tunza neno la haya.

Paolo akakaa siku katháwakatha, akaagana na ndugu, 18 akatweka kwenda Shami, na pamoja naye Priskilla na Akula; akikata nyele za kitwani katika Kenkrea: kwani ameweka nathiri.

Akafika Efeso, akawaacha huko: akaingia mwenyewe 19 katika sunagogi, akajadiliana na Wayahudi.

Walipomtaka azidi kukaa nao, hakukubali; akaagana 20 21 nao, akisema, Imenipasa kabisa nifanye karamu hii inayokuja katika Yerusalemi. Nitarudi tena kwenu, Muungu akinijalia.

Akatoka katika Efeso, akafika Kaisariya, akaenda 22 juu akawasalimia kanisa, akashuka hatta Antiokia.

Hatta akiisha kukaa kitambo, akatoka akapita 23 taratibu katika inchi ya Galatia na Frugia, akiwatia moyo waanafunzi.

Myahudi jina lake Apollo, kwa asili Mwiskandera, 24 mtu mwenyi elimu, akafika Efeso, akiwa hodari katika maandiko. Huyu akafundishwa njia yake Bwana, 25 akawa mwepesi rohoni, akanena akafundisha sana mambo ya Isa, akijua ubatizo wa Yohana tu. Akaanza 26 kunena pasipo hofu katika sunagogi, hatta walipomsikia Akula na Priskilla wakamtwa wakamfasiria hasa njia ya Muungu. Alipotaka kupita hatta Akaya, ndugu 27 wakamtangulia, wakaandika kwa waanafunzi wamkaribishe; naye alipofika, akawasayidia sana walioamini kwa nema: kwani akawashinda Wayahudi kwa nguvu, 28 mbele ya watu wote, akionyesha kwa maandiko kama Isa ndiye Masiya.

IKAWA katika kuwako Apollo katika Korinto, 19

- Paolo akipita katika inchi za juu, akaja Efeso. Akaona
 2 waanafunzi, akawaambia, Mmepewa Roho Mtakatifu
 mkiamini? Wakamjibu, Illakini kama kuwa Roho
 3 Mtakatifu hatukusikia. Akanena, Kwa nini tena
 mmebatizwa? Wakanena, Kwa ubatizo wake Yohana.
 4 Akanena Paolo, Yohana alibatiza ubatizo wa kutubu,
 akiwaambia watu wamwamini atakayekuja baada yake,
 5 ndiye Masiya Isa. Wakisikia wakabatizwa kwa Jina
 6 lake Bwana Isa, Paolo akawatia mikono, akaja Roho
 Mtakatifu juu yao, wakanena kwa lugha, wakatabiri.
 7 Wakawa waume wote kama thenashara.
- 8 Akiingia katika sunagogi, akanena pasipo hofu,
 akitoa huja akionya miezi mitatu mambo ya ufalme wa
 9 Muungu. Hatta wangine wakiwa wamekuwa wagumu,
 wala hawakuamini, illa wakainenea vibaya njia mbele
 ya makutano, akatoka kwao, akawatenga waanafunzi,
 akitoa maneno killa siku katika darasa ya Turano.
- 10 Yakawa haya kwa miaka miwili, hatta wote waliokaa
 katika Asia wakalisikia neno la Bwana, na Wayahudi na
 Wayonani.
- 11 Muungu akatoa nguvu zisizo za killa siku kwa
 12 mikono yake Paolo, hatta wagonjwa wakaletewa nguo
 na mishipi ya katika mwili wake, marathi zikawaacha,
 pepo mbaya zikatoka.
- 13 Wakashika watu Wayahudi wasio kwao, waganga,
 kunena juu yao walio na pepo mbaya jina lake Bwana
 Isa, wakisema, Nawaapiza kwa Isa amhubiriye Paolo.
- 14 Wakawa waana saba wa Skewa Myahudi, mkohani
 15 mkuu, waliofanya hivi. Akajibu pepo mbaya akawa-
 ambia, Isa namjua, na Paolo namtambua: 'm nani
 16 ninyi? Akaruka juu yao mtu aliyepagawa na pepo
 mbaya, akawashinda akawaweza, hatta wakakimbia
 katika nyumba ile utupu na wenyi jeraha.
- 17 Haya yakajulika na Wayahudi wote na Wayonani
 waliokaa katika Efeso, hofu ikawaingia wote; jina lake
 18 Bwana Isa likakua. Na wengi wao walioamini wakaja
 19 wakaungama, wakaonyesha matendo yao. Na mari-
 thawa waliotenda mambo yasiyofaa wakaleta vitabu
 vyao, wakaviteketeza machoni pao wote: wakahasibu
 20 thamani yao, wakiona fetha hamsini elfu. Hivi kwa
 nguvu neno la Bwana likakua likaweza.
- 21 Haya yakaisha, Paolo akaona rohoni, kupita katika

Umakedoni na Akaya, aende Yerusalemi, akinena, Baada ya kuwako huko imenipasa kuona na Rumi.

Akapeleka katika Umakedoni waliomngojea wawili, 22
Timoteo na Erasto; akakaa mwenyewe kitambo katika
Asia. Ukawa wakati huu uthia si haba kwa njia hii. 23
Kwani mtu, jina lake Demetrio, mfua fetha, aliyefanya 24
vijumba vya fetha kwa Artemi, akawapatia mafundi
fayida zisizo chache. Akawakusanya hawa nao walio- 25
tenda kazi hizo, akanena, Waume, mwajua kama kwa
kazi hiyo tunayo mali yetu. Mmeona mkasikia kama si 26
katika Efeso tu, illa katika Asia kama yote, huyu Paolo
akiwashawishi amegeuza watu marithawa, akisema kama
siyo miungu iliyofanyika kwa mikono. Hatta si sisi tu 27
tulioingia hatarini urithi huu wetu ubatilike, illa hekalu
hili la muungu mke mkuu Artemi lisihesabike neno,
ukuu wake upate kuangamizwa, aliyeabudiwa na Asia
nao ulimwengu wote.

Wakisikia wakajaa hasira, wakapiga kelele wakinena, 28
Mkuu ni Artemi wa Waefesi. Mji wote ukajawa na 29
chafuo. Wakaenda kassi kwa moyo mmoja hatta teatro,
wakichukua nao Gayo na Aristarko, Wumakedoni walio-
safiri naye Paolo. Paolo akitaka kuwaingilia watu, 30
waanafunzi wakamzuia. Hatta baathi ya Waasiarko, 31
walio rafiki zake, wakampelekea, wamwonye asijitoe
katika teatro. Bassi wangineo wakalia mangineyo, 32
kwani makusanyiko yakachafuka, wala walio wengi
hawakujua kwa sababu gani wamekusanyika. Waka- 33
'mweka mbele Iskander katika makutano, Wayahudi
wakimsukuma. Iskander akawapungia mkono, akataka
kutoa huja kwa watu. Wakimjua kama Myahudi, ika- 34
pigwa kelele moja na wote kama saa mbili, wakilia,
Mkuu ni Artemi wa Waefesi.

Mwandishi alipowatuliza makutano akanena, Waume 35
Waefesi, mtu gani asiyejua kama mji wa Waefesi ni
mtunza hekalu la Artemi mkuu, nalo lililomwangukia
Zeu. Kama haya hayakanikani, imewapasa ninyi kuwa 36
watulivu, wala msifanye neno kwa haraka. Kwani 37
mmewaleta watu hawa, wasiokwiba kitu kilicho wakf,
wala wasiomtukana muungu mke wenu. Bassi kama 38
Demetrio nao mafundi walio naye wana neno na mtu,
baraza zinazo, kuna na Maprokonsuli: washtakiane.
Mkitaka neno kwa mambo mangineyo, litafanyika katika 39

- 40 kusanyiko lililo halali. Kwani tumeingia hatarini tushtakiwe fitina kwa hii ya leo, pasipo sababu tupate kutoa hesabu ya kukutanika huku.
- 41 Akinena haya akakomesha kusanyiko.
- 20 BAADA ya kutulia uthia, Paolo akawaita waanafunzi akawasalimia, akatoka asafiri kwenda Umakedoni.
- 2 Akipita katika inchi zile akawaonya sana, akafika
- 3 Uyonani, akakaa miezi mitatu. Wayahudi wakimfanyia hila akitaka kwenda Shami kwa bahari, akashika shauri la kurudi kwa Umakedoni.
- 4 Wakafuatana naye hatta Asia, Sopater Mberoya; Wathessalonika, Aristarko na Sekundo; na Gayo Mderbe, na Timoteo; Waasia, Tukiko na Trofimo. Hawa
- 6 wakitangulia wakatungoja kwa Troa. Sisi tukatweka baada ya siku za mikate isiyochachwa katika Filippi, tukawafikia katika Troa kwa siku tano; tukakaa huko siku saba.
- 7 Hatta siku ya juma a pili, tukakutanika tuvunje mikate, Paolo akasema nao, akitaka kusafiri assubui, akafuliza maneno yake hatta kati ya usiku. Zikawa taa
- 9 marithawa katika órofa tulipokutanika. Akakaa kitako kijana, jina lake Eutuko, katika dirisha, akalemewa na usingizi mzito. Hatta Paolo akisema maneno mengi, akilemewa na usingizi, akaanguka katika dari ya tatu,
- 10 akaokotwa amekufa. Paolo akashuka, akaanguka juu yake, akamkumbatia, akanena, Msitaabike; uzima wake
- 11 umo ndani yake. Akipanda tena, akavunja mkate, akaonja, akazumgumza katháwakatha hatta alfajiri,
- 12 hivi akatoka. Wakamleta kijana mzima, wakafarajika kupita kadiri.
- 13 Sisi tukatangulia kwa merikebu tukaenda hatta Asso, tukitaka huko kumpokea Paolo: kwani hivi alivyoa-
- 14 muru, akitaka kwenda mwenyewe kwa mguu. Alipotukuta katika Asso, tukampokea, tukaja Mitulene. Huko tukatweka, siku ya pili tukafika panapolekea Kio. Siku
- ngine tukaingia katika Samo, tukakaa Trogullio; siku
- 16 iliyofuata tukaja Mileto. Kwani Paolo ameona vema kupita Efeso merikebuni, asipate kuongea katika Asia: kwani alifanya hima, kama yamkini, awe siku ya Pentekote katika Yerusalemi.
- 17 Katika Mileto akatuma hatta Efeso, akawaita wazee
- 18 wa kanisa. Walipokuja kwake, akawaambia, Mmejua

ninyi, tangu siku za kwanza nilipofika katika Asia, ginsi
 nilivyokuwa kwenu wakati wote, nikimtumikia Bwana 19
 kwa unenyekevu wote, na machozi, na majaribu yaliyo-
 nipata kwa hila zao Wayahudi, nisivyonyima kitu ki- 20
 faacho, nisiwaonye, nisiwafundishe nyinyi mbele ya watu
 na nyumba kwa nyumba, nikiwashuhudia Wayahudi na 21
 Wayonani toba iliyo kwa Muungu, na imani iliyo kwa
 Bwana wetu Isa Masiya. Bassi sasa angalieni, niki- 22
 fungwa mimi kwa Roho nasafiri hatta Yerusalemi,
 nisipojua mambo yatakayonipata huko, illa kama Roho 23
 Mtakatifu mji kwa mji hunishuhudia kama mafungo na
 mateso yaningoja. Lakini silitanii neno, wala sioni 24
 maisha yangu ina thamani, nimalize mwendo wangu
 kwa furaha, na ungoje niliopewa na Bwana Isa, niishu-
 hudie anjili ya neema yake Muungu. Bassi sasa najua 25
 kama hamtaniona tena uso ninyi nyote, niliyepita kwenu
 nikihubiri ufalme. Kwa hiyo nawashuhudisha wote 26
 siku ya leo, kama mimi safi wa damu zao wote, kwani 27
 sikuepuka kuwahubiria shauri lote la Muungu. Anga- 28
 lieni kwenu, na kwa kundi lote Roho Mtakatifu alipo-
 waweka askafu, mlishe kanisa lake Muungu, alilojipatia
 kwa damu yake mwenyewe. Najua kama wataingia 29
 baada ya kutoka kwangu nyama wakali, watawaingilia
 wasiwaachilie kundi; na katika kwenu wenyewe watao- 30
 ndoka watu wanenao yasiyonyoka, wawavute waanafunzi
 nyuma yao. Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka kama 31
 miaka mitatu usiku na mchana, sikuacha kwa machozi
 kumwonya killa mtu. Bassi sasa, ndugu, nawaweka 32
 kwa Muungu na kwa neno la neema yake, awezaye kuwa-
 jenga na kuwapa ninyi urithi katika kwao wote waliota-
 kasika. Sikutamani fetha, wala thahabu, wala mavazi 33
 ya mtu. Ninyi mwajua, kama yaliohitajia kwangu ao 34
 kwao walio nami, mikono hii imeyatenda. Nimewao- 35
 nyesha yote, kama mkitenda kazi hivi, imepasa kuwasa-
 yidia wasio na nguvu, na kuyakumbuka maneno yake
 Bwana Isa, alivyosema, Ni heri kutoa kuliko kupokea.

Akinena haya, akapiga magote akaomba nao wote. 36
 Wakalia marithawa wote, wakamwangukia Paolo shi- 37
 ngoni wakambusu, wakihuzunika kuliko yote kwa neno 38
 alilosema, kama hawatamtazama tena uso. Wakamshi-
 ndikiza hatta merikebu.

IKAWA tulipowaacha, tukashua, tukaja kwa njia ya 21

kunyoka katta Koos, na ya pili yake hatta Rodo, na kuto-
 2 ka huko hatta Patara. Tukiona merikebu ikienda hatta
 3 Foiniki, tukapanda, tukatweka. Bassi Kupro ikionekana,
 tukaiacha upande wa kushoto, tukapita hatta Shami,
 tukashuka kwa Turo, kwani huko merikebu ishushapo
 4 shehena yake. Tukiona waanafunzi, tukakaa huko siku
 saba. Wakamwambia Paolo kwa Roho, asipande hatta
 5 Yerusalemi. Nasi tulipotimiza siku zile, tukatoka
 tukaenda zetu; nao wote wakatushindikiza na wake na
 watoto, hatta kutoka katika mjini: tukapiga magote
 6 pwani, tukaomba. Nasi tulipoagana, tukatwaa meri-
 7 kebu, wakarudi kwao. Hatta tulipokwisha njia yetu
 kutoka Turo, tukafika Ptolemai, tukawapa ndugu salaa-
 8 mu, tukakaa nao siku moja. Hatta ya pili yake sisi
 tuliofuatana naye Paolo tukatoka, tukafika Kaisariya,
 tukaingia nyumbani mwa Filipo mwanjilisti, aliye wao
 9 saba, tukakaa naye. Naye huyu alikuwa na binti wanne
 10 bikira, waliotabiri. Tukikaa siku nyingi, kukashuka
 11 katika Uyahudi nabii mmoja jina lake Agabo. Alipo-
 tufikia akatwaa mshipi wake Paolo akajifunga mikono
 na miguu, akanena, Ndivyo asemavyo Roho Mtakatifu,
 Ndivyo watakavyomfunga Wayahudi wa Yerusalemi mtu
 mwenyi mshipi huu, watamtoa katika mikono ya mataifa.
 12 Tulipoyasikia haya, na sisi na watu wa mahali pale, tuka-
 13 msihi asipande Yerusalemi. Akajibu Paolo, Maana gani
 kulia na kunivunja moyo? kwani ni tayari nisifungwe tu,
 illa nife tena kwa Yerusalemi kwa jina lake Bwana Isa.
 14 Hatta akikataa kushawishwa tukakoma, tukisema, Bwana
 15 apendalo liwe. Baada ya siku hizi tukatweka mizigo tu-
 16 kaenda Yerusalemi. Wakafuatana nasi na waanafunzi wa
 Kaisariya, wakaleta pamoja nao Mnason wa Kupro, mwa-
 nafunzi wa zamani, nyumba yake ndipo tutakapokaa.
 17 Tulipofika Yerusalemi, waanafunzi wakatukaribisha
 18 kwa furaha. Hatta ya pili yake Paolo akaingia pamoja
 19 nasi kwa Yakobo; walikuwako na wazee wote. Alipo-
 kwisha kuwasalimia, akafunua moja moja mambo
 Muungu aliyoyafanya katika mataifa kwa ungoje wake.
 20 Wale waliposikia wakamtukuza Muungu. Waka-
 mwambia, Waona, ndugu, elfu ngapi ziko za Wayahudi
 21 wanaoamini, nao wote wenyi uwivu kwa torati. Nao
 wameambiwa habari zako, kama unawafundisha Waya-
 hudi wote walioko katika mataifa, wamwache Musa,

ukisema imewapasa wasiwatahiri watoto, wala wasiende
kwa desturi. Bassi nini hii? Jamaa hawana buddi 22
kukusanyika, kwani watasikia kama umekuja. Bassi 23
tena ufanye tulivyokuambia. Tunao watu wanne wenyi
nathiri; uwatwae ujitakase pamoja nao, ukawatolee 24
fetha wajinyoe vitwa; wote wajue kama mambo wali-
yoambiwa juu yako, hayana maana, illa mwenyewe
unakwenda kwa taratibu, ukaishika torati. Nao wa 25
mataifa wanaoamini, tumeandika tukashika wasifanye
haya, illa wajilinde tu katika vitu vilivyotolewa kwa
sanamu, na katika damu, navyo vilivyosongwa, na ka-
tika usharati.

Paolo akawatwaa watu, siku ya pili akajitakasa 26
pamoja nao akaingia katika hekalu, kuonyesha kuti-
mizwa siku za kutakasa kwake, hatta sadaka itolewe
kwa killa mmoja wao. Hatta siku saba zilipo karibu 27
kwisha, Wayahudi walio wa Asia, walipomwona katika
hekalu, wakawataharikisha watu wote, wakamtia mi-
kono, wakiita, Watu wa Israeli, msayidie. Huyu ndiye 28
anayewafundisha wote pahali pote juu ya watu, na
torati, na mahali hapa. Naye tena amewaleta Wayo-
nani katika hekalu, akafanya unajisi kwa mahali hapa
patakatifu. Kwani wameona pamoja naye mjini Tro- 29
fimo Mwefesi, wakamthania Paolo amemleta hekaluni.
Mji wote ukafathaika, watu wakakusanyika hima. 30
Wakamtwaa Paolo, wakamvuta 'nje ya hekalu; marra
ikafungwa milango.

Wakitafuta wamue, habari zikamjia akida wa jeshi, 31
kama Yerusalemi yote imechafuka: akatwaa marra 32
asikari na amiri akapiga mbio kwao. Nao wakimwona
akida na asikari, wakaacha kumpiga Paolo. Akida 33
akakaribia akamtwaa, akaamuru afungwe na mikufu
miwili, akauliza, Yu nani, na alilolifanya nini? Wa- 34
ngine wa katika makutano wakanena mangineyo.
Asiweze kupata iliyo yakini kwa uthia, akaamuru
wamechukue gerezani. Walipofika juu ya daraja, ikawa 35
akachukuliwa na asikari kwa jeuri ya makutano: kwani 36
jamii ya watu wakafuata, wakilia, Mwondolee huyu.

Katika kuingizwa katika gereza Paolo akamwambia 37
akida, Ruksa nikwambie neno? Akasema, Wajua
Kiyonani? Si wewe Mmisri yule aliyefanya fitina ya 38
siku hizi, akachukua barani watu wale elfu 'nne wauaji?

39 Akanena Paolo, Mimi mtu Myahudi, Mtarso wa Kilikia, mwenyeji wa mji usio mnyonge. Nakuomba, uwe
40 rathi niseme nao watu. Akikubali, Paolo, akisimama juu ya madaraja, akawapungia watu mkono, hatta ikiwa kimya kabisa akawasemea kwa lugha ya Kiebrania, akanena,

22 WAUME ndugu na baba, mnisikie nikiwatolea huja.
2 Waliposikia kama anawasemea kwa lugha ya Kiebrania, wakazidi kunyamaza.

3 Akanena, Mimi ni mtu Myahudi, niliyezaliwa katika Tarso ya Kilikia, nikaelimishwa katika mji huu miguuni pa Gamaliel, nikafundishwa sheria ya baba zetu hasa, nikiwa 'mwivu kwa Muungu, kama ninyi nyote leo :
4 nikawafukuza wa njia hii hatta kufa, nikafunga nikatia
5 gerezani na waume na wake. Kama hatta mkohani mkuu ni shahidi wangu, na wazee : nikipewa nao barua kwa ndugu, nikaenda Dameski niwalete walioko wamefungwa hatta Yerusalemi waathibiwe.

6 Ikawa nikisafiri nikafika karibu na Dameski kama aththuuri, marra ikang'aa katika mbingu nuru kuu juu
7 yangu. Nikaanguka chini, nikasikia sauti ikinambia,
8 Saul, Saul, mbona wanifukuza ? Nikajibu, Nani weye, Bwana ? Akaniambia, Mimi ni Isa Mnazrani, unifu-
9 kuzaye. Wale walio nami wakaiona nuru wakaingiwa
10 na hofu, illa sauti iliyosema nami hawakuisikia. Nikanena, Nifanye nini, Bwana ? Bwana akaniambia, Ukiondoka uende Dameski, na huko utaambiwa yote
11 uliyoamriwa uyatende. Kama sikuona kwa anga la nuru ile, nikishikwa mkono nao walio nami, nalikuja
12 Dameski. Akaja kwangu Ananiya, mtu mtawa katika sheria, aliyeshuhudiwa na Wayahudi wote waliokaa
13 huko, akasimama, akaniambia, Ndugu Saul, uone. Nami saa ileile nikamwona. Akanena, Muungu wa baba zetu amekuchagua umjue apendavyo, ukamwone
15 Mwenyi haki, ukasikie sauti katika kanwa lake ; kama utakuwa shahidi kwake kwa watu wote ya haya uliyo-
16 yaona ukayasikia. Bassi sasa utakuwaje ? Ondoke ubatizwe uoshee mbali thambi zako, ukimwitia jina lake.

17 Ikawa nikirudi hatta Yerusalemi nikasali katika
18 hekalu, nikawa katika kuzimia roho, nikamwona aki-niambia, Hima, utoke upesi katika Yerusalemi, kwani

hawatakubali ushahidi wako juu yangu. Nikanena, 19
 Bwana, wajua hawa, kama mimi nalikuwa nikiwafunga,
 nikawapiga katika killa sunagogi, waliokuamini wewe.
 Napo ilipomwagwa damu ya shahidi wako Stefano, 20
 nalikuwa mimi nikisimamia nikakubali, nikalinda nguo
 zao waliompoteza. Akaniambia, Ondoka, nami nita- 21
 kupeleka mbali kwa mataifa—

Wakamsikia hatta neno hili, wakapaliza sauti za 22
 wakanena, Mtoe huyu katika inchi: haimpasi kuishi.
 Nao wakipiga makelele, wakitupia mbali nguo, waki- 23
 tupa juu mavumbi, akida akaamuru wamlete ndani ya 24
 gereza, akasema wamjaribu kwa mapigo, ajue kwa saba-
 bu gani wamemlilia hivyo.

Wakiwa wanamfunga kwa kanda, Paolo akamwambia 25
 amiri aliyesimamia, Ni halali kwenu kumpiga mtu aliye
 Mrumi, wala hajahukumiwa? Amiri akisikia haya, 26
 akaenda kwa akida akampa habari akisema, Wataka
 kutenda nini? Kwani mtu huyu ni Mrumi. Akaja 27
 akida akamwambia, Nambie, wewe u Mrumi? Akasema,
 Naam. Akajibu akida, Mimi nalipata wenyeji huu kwa 28
 ras il mali nyingi. Paolo akasema, Mimi kwa kuza-
 liwa. Marra wakamwacha waliokuwa wangalimjaribu: 29
 akida akaogopa akimjua ni Mrumi, ya kwamba ame-
 mfunga.

Siku ya pili akitaka kujua yaliyo yakini, kwa nini 30
 ameshtakiwa na Wayahudi, akamfungua, akaamuru
 wakusanyike wakohani wakuu na baraza yote, akamchu-
 kua chini Paolo aka'mweka kwao.

PAOLO akawatazana sana baraza, akanena, Waume 23
 ndugu, Mimi kwa moyo mwema wote nimekwenda
 mbele ya Muungu hatta siku hii.

Mkohani mkuu Ananiya akawaamuru waliosimama 2
 naye wampige kanwa. Paolo akamwambia, Muungu 3
 atakupiga wewe, ukuta uliokandikwa: umekaa kunia-
 mua kwa sheria, ukaikosa ukiniamria nipigwe. Walio- 4
 simama naye wakanena, Wamtukana mkohani mkuu
 wa Muungu? Akasema Paolo, Sikumjua, ndugu, 5
 kama ndiye mkohani mkuu: kwani imeandikwa, Mkuu
 wa watu wako, usimnenee vibaya.

Akijua Paolo, kama sehemu moja Masadukayo, nayo 6
 ya pili Mafarisayo, akapiga kelele katika baraza, Waume
 ndugu, mimi Farisayo, mwana wa Mafarisayo: kwa tu-

- 7 maini na kiyama ya wafu ninahukumiwa. Akinena
haya, ilikuwa fitina ya Mafarisayo na Masadukayo,
8 jamaa ikatengwa : kwani Masadukayo husema, hapana
kufufuka, wala malaika, wala pepo. Mafarisayo wa-
9 ungama wote. Kukawa makelele mengi. Wakasima-
ma waandishi wa sehemu ya Mafarisayo, wakashindana,
wakanena, Hatuoni baya katika mtu huyu : kama pepo
10 amesema naye, ao malaika— Fitina ikiwa nyingi, aki-
thani akida angaliraruliwa Paolo nao, akaamuru jeshi
washuke wamtwae kwa nguvu katika kati mwao, wa-
mlete gerezani.
- 11 Usiku uliofuata, Bwana akasimama naye akanena,
Uwe na moyo mkuu : kama ulivyonishuhudia katika
Yerusalemi, imekupasa kunishuhudia hivyo katika Rumi.
- 12 Ukiwa mchana, Wayahudi wakafanya agano wakaji-
laania, wakisema, hawatakula wala hawatakunywa, illa
13 walipomua Paolo. Wakapita arobaini walioapiana hivi.
14 Wakaja kwa wakohani wakuu na wazee, wakanena, Tume-
15 jiapia kiapo tusionje kitu, hatta tutakapomua Paolo. Sasa
ninyi pamoja na baraza mmwonye akida kama amlete
kwenu, kama mmetaka kuyajua yakini yaliyo yake, nasi
kabla asijakaribia, tu tayari tumue.
- 16 Akisikia mwana wa ndugu mke wake Paolo hila hii,
17 akaja akaingia katika gereza akamwambia Paolo. Akaita
Paolo amiri, akasema, Kijana huyu umlete kwa akida :
18 anazo habari za kumpa. Akamtwaa akamleta kwa akida,
akasema, Paolo aliyefungwa aliniita akanitaka nikuletee
19 kijana huyu, akiwa na neno la kukwambia. Akida
akimtwaa mkono akajitenga faraghani, akauliza, Habari
20 gani unazo unipe? Akanena, Wayahudi wameagana
wakutake umlete assubui Paolo katika baraza, kama
21 watakao kuzidi kumwulizia. Wewe usikubali : kwani
wanamwotea watu zayidi ya arobaini waliojilaania wa-
sile, wala wasinywe, hatta watakapomua ; nao sasa ta-
22 yari wakitazamia ahadi kwako. Akida akamwaga ki-
jana, akimwagiza, Usimwambie mtu kama umenionyesha
haya.
- 23 Akaita maamiri wawili, akinena, 'Mweke tayari asikari
miteen kwenda hatta Kaisariya, na wapanda frasi sabwini,
24 na wenyi mikuke miteen, kwa saa tatu ya usiku, kuwa-
patia nyama wampandishe Paolo, wamlete salama kwa
Felike ilwali.

Akaandika barua, akifuata namna hii : Klaudio Lus²⁵₂₆ kwa liwali en nasih Felike, salaamu. Mtu huyu ali-²⁷ kamatwa na Wayahudi, angaliuawa nao ; nikaja na jeshi nikamtoa, nikiambiwa kama ni Mrumi. Nikitaka kujua²⁸ sababu waliyomshtakia nikamleta barazani mwao : nikao-²⁹ na ameshtakiwa kwa maswali ya sheria yao, wala hakuna mshtaka wa kufa wala kufungwa. Nikipewa habari³⁰ kama hila zinafanyika na Wayahudi juu yake, marra nikampeleka kwako, nikawaonya waliomshtaki wanene mambo yake mbele yako. Salaamu.

Waasikari, walivyoagizwa, wakachukua Paolo waka-³¹ mleta usiku hatta Antipatri : hatta assubui wakawaacha³² wapandao frasi waenende naye, wakarudi gerezeni. Nao³³ wakifika Kaisariya wakampa liwali barua, wakamtolea Paolo. Akisoma akauliza ya eparkia gani. Akijua kama³⁴ ya Kilikia, akasema, Nitakusikia watakapokuwako na³⁵ washtaki wako. Akaamuru alindwe katika pretorio ya Herode.

BAADA ya siku tano akashuka mkohani mkuu²⁴ Ananiya nao wazee, na mnenaji mmoja Tertullo, walio-mpa liwali habari za Paolo. Alipoitwa, Tertullo akaa-² nza kumshtaki, akisema, Tukiwa tumepata amani nyingi kwa wewe, na mambo yamekuwa mema kwa taifa hili kwa tunza lako, siku zote na mahali pote tunakubali, ee³ Felike mwema, kwa shukrani yote. Illa nisizidi kuku-⁴ chosha, nakusihi utusikie kwa muhtasari kwa upole wako. Kwani tumemwona mtu huyu mkorofi, aliye-⁵ anza fitina katika Wayahudi wote walio ulimwenguni, mtangulia wa uzushi wao Nazarani, aliyejaribu kulitia⁶ unajisi hekalu : tuliyemkamata, na kwa sheria yetu tukataka kumhukumia. Akaja Lus⁷ akida na nguvu⁷ nyingi, akamtwaa katika mikononi mwetu, akiwaa-⁸ muru waliomshtaki waje kwako : kwa huyu waweza, kwa kumwuliza mwenyewe, kuyajua haya yote tunayo-⁹ mshtakia. Wayahudi wakakubali, wakasema ndivyo⁹ yalivyo.

Akajibu Paolo, liwali akifanya ishara anene, Nikijua¹⁰ kama umekuwa tangu miaka mingi mvamuzi wa taifa letu, nakutolea mambo yangu kwa moyo mwepesi, uki-¹¹ weza kuona kama siku hazipiti thenashara tangu nilipopanda kuabudu katika Yerusalemi. Wala hawaku-¹² niona katika hekalu nikijadiliana na mtu, wala kufanya

- fitina katika makutano, wala katika masunagogi, wala
 13 katika mji, wala hawawezi kuyathubutisha waliyoni-
 14 shtakia sasa. Illa naungama kwako kama kwa njia wa-
 itayo uzushi namwabudu Muungu wa baba zetu, nikiya-
 amini yote yaliyoandikwa katika torati na katika mana-
 15 bii, nikiwa na tumaini kwa Muungu, kama nao wenye-
 we hukubali, kama itakuwa kiyama ya wafu, nao wenyi
 16 haki, nao wasio na haki. Katika haya najizoeza kuwa
 na moyo pasipo kabisa hatiya, wala kwa Muungu, wala
 17 kwa watu. Hatta baada ya miaka mingi nalikuja niwa-
 18 letee fetha watu wa taifa langu, na sadaka. Kwa hiyo
 wakaniona katika hekalu nimesafika, pasipo makutano
 19 wala pasipo makelele, walio Wayahudi wa Asia: walio-
 paswa kuwapo mbele yako na kushtaki, kama wanalo
 20 neno nami. Ama hawa waseme wenyewe kosa gani
 21 waliloliona kwangu niliposimama mbele ya baraza, illa
 kwa sauti hii moja niliyopiga nikisimama kwao, kama
 kwa kufufuka wafu mimi nahukumywa leo kwenu.
- 22 Akawaakirisha Felike, akizidi kuyajua mambo ya
 njia hii, akisema, Atakapokuja Lusya akida, nitayajua
 23 yenu yote. Akaamuru amiri amlinde, asithiiki, wala
 asimzuie mtu aliye wake asimumikie.
- 24 Baada ya siku Felike akiwapo na Drusilla mkewe,
 aliye Myahudi, akamwita Paolo, akamsikia ya imani
 25 yake Masiya. Akiyanena ya haki, na kiasi, na hukumu
 itakayokuja, akatiwa hofu Felike, akajibu, Sasa uende
 26 zako: wakati ukiwadia nitakuitia tena. Akataraja
 kama atapewa mali na Paolo: kwa hiyo akazidi kumpe-
 lekea aseme naye.
- 27 Miaka miwili ikipita, Felike akapewa badala Portio
 Festo. Akitaka Felike kuwafanyia Wayahudi fathili,
 akamwacha Paolo amefungwa.
- 25** FESTO akifika katika eparkia, baada ya siku tatu
 2 akapanda hatta Yerusalemi katika Kaisariya. Waka-
 mwonyesha mkohani mkuu nao wa kwanza Wayahudi
 3 juu ya Paolo, wakamsihi, wakitaka fathili juu yake,
 ampelekee aje Yerusalemi, wakifanya maoteo wamue
 njiani.
- 4 Festo akajibu, Paolo atalindwa katika Kaisariya, naye
 5 mwenyewe karibu atakwenda zake. Naye akasema,
 Walio wenyi nguvu, mshuke pamoja nami, mmshtaki
 6 mtu huyu, likiwa neno kwake. Akiongea kwao siku

zisizopita kumi ao nane, akashuka Kaisariya ; assubui
 akakaa kitini mwa hukumu, akaamuru Paolo aletwe.
 Akiwako huko wakamsimamia Wayahudi walioshuka 7
 katika Yerusalemi, wakileta mashtaka mengi na mazito
 juu ya Paolo, wasiyoweza kuyathubutisha : akitoa huja 8
 yake, kama Si kwa sheria ya Wayahudi, wala si juu ya
 hekalu, wala si kwa Kaisari, sikukosa neno. Naye Festo 9
 akitaka kuwafanyia fathili Wayahudi, akamjibu Paolo,
 akisema, Wapenda kwenda Yerusalemi uhukumiwe
 huko mbele yangu? Akanena Paolo, Nipo nimesimama 10
 kitini pa Kaisari, nipaswapo nihukumiwe. Wayahudi
 sikuwakosa, kama nawe umejua sana. Kama nimekosa 11
 ao nimetenda neno la kustahili kufa, sikatai kufa ; kama
 silo neno wanalonishtakia hawa, hawezi mtu kunitoa
 kwao. Namwitia Kaisari. Festo akiisha kusema na 12
 baraza akajibu, Umemwitia Kaisari? Kwa Kaisari
 utakwenda.

Hatta siku zilipopita, Agrippa mfalme na Berenike wa- 13
 kafika Kaisariya, kumpa Festo salaamu. Nao wakiongea 14
 siku nyingi naye, Festo aka'mwekea mfalme mambo ya
 Paolo, akinena, Mtu yuko aliyeachwa na Felike amefu-
 ngwa : nami nikiwa katika Yerusalemi, wakohani wakuu 15
 na wazee wa Wayahudi wakamwonyeshea, wakitaka
 hukumu juu yake. Nikawajibu kama si desturi ya 16
 Warumi kumtoa mtu aliyeshtakiwa, asipokuwa nao
 wamshtakio uso kwa uso, akapewa nafasi atoe huja juu
 ya mashtaka. Wakifuatana hatta hapa, nisipokawia, 17
 siku ya pili nikakaa kitini mwa hukumu, nikaamuru
 mtu aletwe. Waliomshtaki wakimsimamia hawakuleta 18
 neno baya kama nilivyothani, illa walikuwa na maswali 19
 juu yake ya dini yao, na ya mtu Isa aliyekufa, aliyom-
 nenea Paolo yu hayi. Nikiona shaka mimi kwa maswali 20
 ya haya, nikanena kama amependa kwenda Yerusalemi
 ahukumiwe huko kwa haya. Paolo akiitia alindwe kwa 21
 kusikia kwa Augusto, nikaamuru alindwe hatta nitaka-
 popeleka kwa Kaisari. Agrippa akamwambia Festo, 22
 Ningalitaka na mimi kumsikia mtu huyu. Naye, Assu-
 bui, akasema, utamsikia.

Hatta assubui, akija Agrippa na Berenike na shangwi 23
 nyingi, wakaingia mahali pa kusikia, pamoja nao maa-
 kida, na watu walio bora wa mjini : akaamuru Festo,
 Paolo akaletwa.

- 24 Akanena Festo, Mfalme Agrippa, nanyi wote mnao pamoja nasi, mwamwona huyu, waliyemtakia sana kwangu jamii yote wa Wayahudi, na katika Yerusalemi na
- 25 hapa, wakipiga kelele haifai azidi kuwa hayi. Nikiona kama hakutenda neno la kustahili kufa, naye huyu
- 26 amemwitia Augusto, nikaamua kumpeleka. Wala sina neno lake lililo yakini nimwandikie bwana. Kwa hiyo nimemleta mbele yenu, na ya kwanza mbele yako, mfalme Agrippa, illi, maulizo yakifanyika, nipate neno
- 27 la kuandika. Kwani naona haina maana, kumpeleka aliyefungwa wala kutoa kuonyesha mashtaka yake.
- 26** AGRIPPA akamwambia Paolo, Unayo ruksa useme maneno yako. Paolo akanyosha mkono akatoa maneno,
- 2 Niliyoshtakiwa yote kwa Wayahudi, mfalme Agrippa,
- 3 najiona heri nकिनena mbele yako leo: kwani umeyajua yote yaliyo katika Wayahudi, na desturi, na maswali: kwa hivyo nakuomba unisikie kwa upole.
- 4 Maisha yangu tangu ujana, uliokuwa tangu mwanzo
- 5 katika taifa langu katika Yerusalemi, wajua Wayahudi wote; walionijua tangu zamani, kama wangependa kushuhudu, kama kwa mathehebu iliyo hasa ya dini yetu,
- 6 nikakaa Farisayo. Na sasa kwa tumaini la ahadi waliyopewa baba zetu na Muungu nasimama nihukumiwe.
- 7 Hiyo makabila yetu thenashara, wakiabudu kwa nguvu usiku na mchana, wataraja kuifikia. Kwa tumaini hilo
- 8 nimestakiwa, ee mfalme, na Wayahudi. Mbona imethaniwa nanyi isiyosadikiwa, Muungu akiwafufua wafu?
- 9 Mimi nalithani kwa ndani imenipasa nitende mambo
- 10 mengi juu ya jina lake Isa Mnazareti. Nikayafanya katika Yerusalemi: na watakatifu wengi mimi naliwafunga katika malindo, nikipewa nguvu na wa-
- 11 kohani wakuu: nao wakiuawa nikatia sauti. Katika masunagogi mengi marra nyingi nikawaathibu nikawashurutisba wanene unajisi; hatta nikichukuliwa na hasira nikawafukuza na katika miji ya ugenini. Katika hii nikiwa nikienda Dameski na nguvu na agizo la mko-
- 13 hani mkuu, aththuuri, ee mfalme, naliona njiani katika mbingu, juu yangu nao waliosafiri nami, iking'aa nuru
- 14 kuliko anga la jua. Tukaanguka katika inchi wote, nikasikia sauti ikisema nami, ikinena kwa maneno ya Kiebrania, Saul, Saul, mbona wanifukuza? ni gumu
- 15 uyapigie mateke yachomayo. Nikanena, U nani, Bwa-

na? Bwana akanena, Mimi ni Isa, unifikuzaye wewe. Illa ondoke, simama juu ya miguu yako: kwa hiyo 16 nimekutokea, nikufanye mtumishi na shahidi ya haya uliyoyaona nayo utakayoonyeshwa; nikikutoa katika 17 kwao watu na katika mataifa, kwao hawa sasa nakutuma, uwafumbushe macho, uwageuze kwa nuru katika 18 giza, na katika nguvu zake shetani kwa Muungu, wapewe masamehe ya thambi, na urithi kwao waliotakaswa, kwa imani iliyo kwa mimi. Nami, mfalme Agrippa, sikuasi 19 juu ya maonyesho ya mbinguni: lakini kwanza kwao 20 walio katika Dameski nao katika Yerusalemi, hatta inchi yote, kwa Wayahudi na kwa wamataifa, nalihubiri kutubu na kumgeukia Muungu, wakiyatenda yaliyoipasa toba. Kwa sababu ya haya Wayahudi wakanikamata 21 katika hekalu, wakajaribu kuniua. Nikijaliwa na Muu- 22 ngu, hatta siku hii nipo, nisipowashuhudia wadogo wala wakuu neno moja, illa nabii waliyosema yatakuwa, naye Musa: kama Masiya ni mteswa, kama akiwa wa kwanza 23 katika kufufuka wafu, atahubiri nuru kwao watu na kwa mataifa.

Akitoa hivi huja yake, Festo akasema kwa sauti kuu, 24 Akili zako zimepotea, Paolo; elimu nyingi zimepoteza akili zako.

Naye, Akili zangu hazikupotea, akanena, ee Festo 25 mwema; lakini nayatoa maneno yaliyo ya kweli na ya kiasi. Kwani mfalme amejua haya, mbele yake nanena 26 pasipo hofu. Kwani sithani neno moja la haya lime-mstirikia; kwani hilo halikufanyika pembeni. Waami- 27 ni, ee mfalme Agrippa, manabii? Najua kama waamini. Naye Agrippa kwa Paolo, Kwa machache mimi wani- 28 shawishi kuwa Mmasihiya.

Paolo akanena, Namwomba Muungu, kwa machache 29 na kwa mengi, si wewe tu, illa wanaonisikia leo wote, wawe kama mimi, pasipo mafungo haya. Akiisha 30 kunena haya, akaondoka mfalme, na liwali, na Berenike, nao waliokaa kitako pamoja nao. Wakienda mbali 31 wakanena wao kwa wao, wakasema, kama Hatendi neno mtu huyu la kustahili kufa wala kufungwa. Agrippa 32 akamwambia Festo, Mtu huyu angaliweza kufunguliwa kama hangalimwitia Kaisari.

IKIAMRIWA twende sisi kwa bahari hatta Italia, 27 wakamtoa Paolo na wangineo waliofungwa kwa amiri jina lake Yulio, wa kikozi cha Augusto.

- 2 Tukapanda katika merikebu ya Adramuttio, itaka-
yokwenda pahali katika Asia, tukatweka, akiwapo nasi
- 3 Aristarko Mmakedoni wa Thessalonika. Siku ya pili
tukatua katika Sidoni. Yulio akamtendea Paolo kwa
upole, akampa ruksa aende kwa rafiki zake apate kutu-
4 nzwa. Tukitweka huko tukapita chini ya Kupro, kwa
5 kuwa pepo za omo. Tukipita katika bahari iliyo kwa
6 Kilikia na Pamfulia, tukafika Mura ya Lukia. Huko
amiri akaona merikebu ya Iskanderia ikienda Italia,
akatupandisha.
- 7 Hatta siku katháwakatha tukaenda polepole, tukafika
kwa shidda hatta Knido, upepo ukituzuia, tukapita chini
8 ya Krete hatta Salmone. Tukaipita kwa shidda tukaja
mahali paitwapo Bandari nzuri, palipo karibu na mji
9 Lasaya. Wakati marithawa ukiisha, ikawa tena hatari
kwenda baharini, kwani siku ya kufunga sasa imepita,
10 Paolo akawaonya akinena, Waume, naona kama safari
hii itakuwa na mathara na hasara nyingi, si ya shehena
11 na merikebu tu, illa na maisha zetu. Amiri akawaa-
mini nakhotha na mwenyi merikebu kuliko yale aliyo-
12 yanena Paolo. Bandari isipowekwa vema wakae humu
wakati wa thóruba, walio wengi wakatoa shauri watweke
na huko, illi wapate kufika Foiniki, wakae huko wakati
wa thóruba, ndiyo bandari ya Krete iliyolekea matlaa
13 ayuk na matlaa akrab. Ikivuma kusi wakathani wame-
pata waliokusudia, wakang'oa nanga, wakapita karibu
14 sana na Krete. Baadaye kitambo ukawapiga upepo wa
15 tufanu ulioitwa Eurakulo. Merikebu ikikamatwa, wala
haikuweza kuulekea upepo, tukaiacha, tukichukuliwa.
16 Tukienda upesi chini ya kisiwa kilichoitwa Klauda,
17 tukapata kwa shidda kuiweza mashua. Tulipoitweka
tukatumia masayidio tukaifunga chini merikebu. Wa-
kiogopa wasiangukie Surti, wakashusha foramali, hivi
18 wakachukuliwa. Tukipigwa sana na thóruba, siku ya
19 pili wakatupa vizito, hatta ya tatu tukatupia mbali kwa
20 mikono yetu sisi pambo la merikebu. Wala jua wala
nyota siku nyingi hazionekani, thóruba si haba ikakaa
juu yetu, hatima tamaa yote ya kuokoka sisi ikakatika.
- 21 Njaa ikiwa nyingi, akasimama Paolo kati yao akawaa-
mbia, Iliwapasa, waume, kunisikilizia msing'oe katika
22 Krete, kupata mathara haya na hasara. Illa sasa na-
waonya mpate moyo: kwani haitapotea maisha moja
23 kwenu, illa merikebu. Kwani alisimama kwangu usiku

huu malaika yake Muungu, niliye wake nikimtumikia,
 akanena, Usiogope, Paolo; sharti usimame kwa Kaisari: 24
 kaangalia, amekupa Muungu wote wasafirio pamoja
 nawe. Kwa hiyo 'mwe na moyo, waume: kwani na- 25
 mwamini Muungu, kama itakuwa kwa ginsi nilivyoa-
 mbiwa. Illa sharti tupande katika kisiwa. Ukawa ²⁶₂₇
 usiku wa arobatashara, tukichukuliwa katika Adria,
 kati ya usiku wabaharia wakathani inchi inawakaribia.
 Wakitia bildi wakaona mapima asharini: wakiendelea 28
 kidogo wakatia bildi tena, wakaona mapima hamsta-
 shara. Wakaogopa tusipande panapo mawe; wakatupa 29
 nanga nne katika shetri, wakaomba mchana uwe. Ba- 30
 haria wakitaka kukimbia katika merikebuni, wakashusha
 mashua baharini, kama wangelitaka kunyosha nanga
 katika omo. Paolo akawaambia amiri na asikari, Wasi- 31
 pokaa hawa katika merikebu, ha'mwezi kuokoka ninyi.
 Asikari, wakazikata kamba za mashua, wakaiacha ia- 32
 nguke. Hatta ulipokuwa mchana unakuwa, Paolo 33
 akawasihi watwae wote vyakula, akinena, Leo siku ya
 arobatashara, mmengoja mkashinda pasipo chakula msi-
 twae kitu. Kwa hiyo nawasihi mtwae vyakula, kwani 34
 itakuwa kwa wokovu wenu: kwani hakuna unyele
 kitwani mwenu utakaopotea. Akinena haya akatwaa 35
 mkate, akamshukuru Muungu machoni pao wote, aka-
 vunja akaanza kula. Wakipata moyo wote, nao waka- 36
 twaa vyakula. Tukawa wote walio hayi katika meri- 37
 kebu, miteen, sabwini na sita. Wakishiba na chakula, 38
 wakaifanya merikebu nyepesi, wakaitupia nafaka ba-
 harini. Ukiwa mchana, hawakuitambua inchi: illa 39
 wakacna hori yenyi pwani; humo wakataka, kama
 yamkini, kuiingiza merikebu. Wakazitupia mbali nanga 40
 wakaacha katika bahari; wakizilegeza kamba za sukani,
 wakatweka tanga dogo kwa upepo, wakaendea pwani.
 Wakifikia pahali penyi mawimbi mawili, wakapandisha 41
 jahazi. Omo yake ikakazwa, ikakaa isitikisike, illa
 shetri ikafumuka kwa nguvu za mawimbi. Shauri la 42
 asikari likawa waliofungwa wauawe, mtu asiogelea
 mbali akimbie. Amiri akitaka kumponya Paolo aka- 43
 wazuilia makusudi, akaamuru wajuao kuogelea wajitupe
 kwanza, watoke hatta inchi; nao waliosalia, hawa juu 44
 ya mbao, hawa juu ya vitu vya merikebuni. Hivi
 wakapata wote kufika salama hatta inchi.

- 28 TUKIISHA kuokoka, tukajua Melita, ndilo jina lake
 2 kisiwa. Washenzi wakatufanyia wema usio wa killa
 siku. Wakakoka moto, wakatukaribisha killa mtu, kwa
 mvua iliyokunya na baridi.
- 3 Akikusanya Paolo mzigo wa vijiti, akatia motoni,
 4 nyoka akatoka kwa hari akamkamata mkono. Washe-
 nzi wakimwona nyama akimwangikia mkono, wakanena
 wao kwa wao, Yakini mtu huyu muuaji; akiokoka
 5 katika bahari, haki hamwachi aishi. Naye akamtikisia
 6 mbali nyama katika moto; hakuna mathara. Wale
 wakangoja angalivimba, ao angalianguka ghafala ame-
 kufa: hatta walipokwisha kungoja sana, wala haku-
 mwona neno limempata, wakageuka wakasema, Huyu
 ni muungu.
- 7 Katika karibu na mahali pale palikuwa mashamba
 yake mkuu wa kisiwa, jina lake Publio; aliyetukaribi-
 sha akatufanya wageni wake kwa moyo mwema siku
 8 tatu. Ikawa baba yake Publio amelazwa, akiwa na
 homa na kuhara damu: akamwingilia Paolo, akaomba,
 9 akamtia mikono, akamponya. Yakiwa haya, wangine
 walio na ugonjwa katika kisiwa wakaja, wakaponyeka:
 10 wakatuheshimia kwa heshima nyingi. Hatta tulipo-
 toka wakatupakilia vifaa.
- 11 Baada ya miezi mitatu tukatoka katika merikebu ya
 Iskanderia, iliyokaa wakati wa thóruba katika kisiwa,
 12 ishara yake Dioskuri. Tukashuka katika Surakusa, tuka-
 13 kaa siku tatu. Tukizunguka katika hapa tukafika Regio:
 baada ya siku moja ikavuma kusi, siku ya pili tukaja
 14 Puteoli. Huko tukaona ndugu, tukaitwa nao tukae siku
 15 saba: hivi tukaja Rumi. Na huko ndugu wakisikia
 mambo yetu, wakaja watukute hatta Appiiforo na Tres-
 taberne. Akiwaona Paolo akamshukuru Muungu, aka-
 thubutika.
- 16 Tukaja hatta Rumi; amiri akawatoa waliofungwa
 kwa jemadari: Paolo akapewa ruksa akae kwake mwe-
 nyewe pamoja na asikari aliyemlinda.
- 17 Ikawa baada ya siku tatu, akawaita Wayahudi walio
 wakuu: hatta walipokuja, akawaambia, Waume ndugu,
 mimi sikufanya neno juu ya watu, wala juu ya desturi
 za baba zetu, nikatolewa nimefungwa katika Yerusa-
 18 lemi mkononi mwa Warumi. Hawa wakiniuliza waka-
 taka kunifungua, kwani jambo la kufia hakuna kwangu.

Illa Wayahudi wakigombeza, nalishurutishwa nimwitie 19
Kaisari; si kama ninalo neno la kuwashtakia taifa langu.
Kwa sababu hiyo nimewaita, niwaone nikaseme nanyi: 20
kwani kwa ajili ya tumaini la Israeli nimezungukwa na
mkufu huu.

Wale wakamwambia, Sisi hatukupokea nyaraka juu 21
yako katika Uyahudi, wala ndugu aliyopo hakuleta
habari, wala hakunena neno baya juu yako. Illa sisi 22
twapenda kusikia kwako uonaje: kwani tumeijua ma-
thehebu hii po pote hugombeza.

Waka'mwekea siku, wakaja wengi kwake alikokaa, 23
akawaandikia akaushuhudia ufalme wa Muungu, aki-
waonya mambo yake Isa katika torati ya Musa nao
nabii, tangu assubui hatta jioni. Hawa wakayakubali 24
yaliyonenwa, hawa hawakuamini. Wasipopatana wao 25
kwa wao, wakaenda zao, akinena Paolo neno moja, Ali-
waambia baba zetu vema Roho Mtakatifu kwa nabii
Isaya, akinena, Enende kwa watu hawa, kanena, Kusi- 26
kia mtasikia, wala hamtafahamu; mkitazama mtata-
zama, wala hamtaona. Kwani moyo wa watu hawa 27
umenona, na masikio yao mazito wasikiapo, na macho
yao wameyafumba; wasione kwa macho, wasisikie kwa
masikio, wasifahamu moyoni, wageuke nikawaponye.
Mjue bassi, kama kwa mataifa umepelekwa wokovu wa 28
Muungu, nao watasikia. Akinena haya, wakaenda zao 29
Wayahudi, wakifanya maswali mengi wao kwa wao.

Akakaa muda mzima wa miaka miwili katika alipo- 30
panga, akawakaribisha wote waliomwingilia, akihubiri 31
ufalme wa Muungu, na kuyafundisha mambo yake Isa
Masiya pasipo hofu; hakuzuiliwa.

WARAKA WAKE PAOLO MTUME KWA WARUMI.

- 1 PAOLO, mtumwa wa Isa Masiya, aliyeitwa kuwa
 2 mtume, aliyewekwa kwa anjili ya Muungu, aliyoihidi
 3 kwa nabii zake katika maandiko matakatifu, ya Mwana
 4 wake, aliye kwa mwili wa wazao wa Daud, akapambanuka kuwa Mwana wa Muungu kwa uwezo, kwa roho ya utakatifu, katika ufufuo wa wafu ; Isa Masiya, Bwana
 5 wetu, naye yule tukapewa neema na utume, kwa kusi-
 6 kiwa imani katika mataifa yote kwa jina lake ; katika hawa mmekuwa na ninyi, mmeitwa na Isa Masiya :
 7 wote walioko katika Rumi, waliopendwa na Muungu, walioitwa watakatifu : Neema kwenu na amani kwa Muungu Baba wetu naye Bwana Isa Masiya.
- 8 Kwanza namshukuru Muungu wangu kwa Isa Masiya kwa ajili yenu nyote, kwamba imani yenu inahubiriwa
 9 ulimwenguni mwote. Muungu ni shahidi wangu, nimwabuduye rohoni katika anjili ya Mwana wake, kama pasipo kukoma nawanena sikuzote, dayima katika
 10 sala zangu naomba, kama hatta sasa nipate kusafiri
 11 vema kwa mapenzi ya Muungu kuja kwenu. Kwani natamani kuwaona, nipate kuwaletea ukarimu wa
 12 rohoni, mfanyike imara ; ndivyo nipate kufarijiana nanyi kwa imani yenu na yangu.
- 13 Sitaki msijue, ndugu, kama marra nyingi nimeshika kuja kwenu, nikazuiliwa hatta sasa, nipate matunda
 14 kwenu kama katika mataifa yaliyosalia. Wayonani na wangineo, wenyi hekima na wasio kufikiri, waniwia.
 15 Hivi nia yangu kuhubiri anjili na kwenu katika Rumi.
- 16 Kwani sitahayariki na anjili : ndiyo nguvu ya Muungu kwa wokovu wake killa aaminiye ; Myahudi kwanza, tena Myonani.
- 17 Kwani haki ya Muungu imethahirika nayo katika imani hatta imani : kama ilivyoandikwa, Mwenyi haki ataishi kwa imani.

Hasira ya Muungu katika mbinguni imefunuka juu 18
 ya unajisi wote na thulumu ya watu walio nayo kweli
 pasipo haki. Kwani iliyojulikana ya Muungu imekuwa 19
 wazi kwao; kwani Muungu amewaonyesha. Kwani 20
 yasiyoonekana yake tangu kuumbwa ulimwengu yame-
 onekana kwa akili katika viumbe, kama uwezo wake wa
 milele na umuungu usioonekana. Hatta hawana neno 21
 la kutoa: kwa sababu wakimjua Muungu hawakum-
 sifu kama Muungu wala hawakumshukuru; illa waka-
 batilika katika majadiliano yao, moyo wao wa bara-
 thuli ukaona giza; wakijinena wenyi hekima wame- 22
 pumbazika, wakabadili sifa zake Muungu asiyeharibika 23
 kuwa mfano wa sanamu ya mtu aharibikaye, nao
 wenyi mabawa, nao wenyi miguu minne, nao wata-
 mbao.

Kwa hiyo Muungu akawatoa kwa tamaa za mioyo 24
 yao katika uchafu, waharibiane heshima ya miili yao:
 waliobadili kweli ya Muungu kuwa uwongo, wakasu- 25
 judia wakaabudu kiumbe kuliko Muumba, aliyebarikiwa
 milele. Amina.

Kwa hiyo Muungu amewatoa wapatwe na aibu: 26
 hatta waanaake wao wakabadili tumio la asili kwa lile
 lisilo la asili: kama na waume, wakiacha tumio la mke 27
 la asili, wakawaka na tamaa wao kwa wao, waume
 wakifanya na waume yasiyosulihi, wakapokea wenyewe
 thawabu yaliyoistahilia makosa yao.

Na kama hawakukubali kumshika Muungu kwa 28
 akili, akawatoa Muungu kwa moyo usio na akili, waya-
 fanye yasiyofaa; wakajawa na thulumu yote, ubaya, 29
 kutamani, uovu; wakajaa hasidi, uaji, fitina, hila, ubaya;
 waambao, wasingiziao, wachukia Muungu, wenyi jeuri, 30
 wenyi kiburi, wajisifuo, watungao maovu, wawaasio
 wazee, wasio na akili, wavunjao ahadi, wasiopendana, 31
 wasiohurumia: waliojua hukumu ya Muungu kama 32
 wayafanyao haya wamestahili kufa, hawayafanyi tu, illa
 wamependezewa nao wayafanyao.

KWA hiyo huna neno la kutoa, ee killa mtu uhuku- 2
 muye; kwani ukimhukumu mwingineo umejihukumu
 mwenyewe; kwani uhukumuye wayafanya yaleyale.
 Twajua kama hukumu ya Muungu ni kwa kweli juu 2
 yao wayafanyao kama haya.

- 3 Wathani, ee mtu, uwahukumuye wayafanyayo, uka-
 4 yafanya wewe, kama utaokoka katika hukumu ya Muu-
 5 ngu? Ao wingi wa wema wake, na upole, na uvumilivu,
 6 umeutharau, usipojua kama wema wa Muungu wakuo-
 7 ngoa utubu? Illa katika ugumu wako na moyo usiotubu
 8 wajiwekea hasira kwa siku ya hasira na kufunuka huku-
 9 mu ya haki ya Muungu, atakayemlipa killa mtu kwa
 10 matendo yake: kwao watafutao katika kustahimili, wa-
 11 kitenda vema, sifa na heshima na kutoa kuharibika,
 12 uzima wa milele: kwao wasiotulia, wasioyafuata ya
 13 kweli, wayafuatao ya thulumu, hasira na ghathabu,
 14 mateso na shidda, kwa killa roho ya mtu mtenda uovu,
 15 Myahudi kwanza, tena Myonani; sifa na heshima na
 16 amani kwa killa atendaye mema, Myahudi kwanza, tena
 17 Myonani. Kwani hapana upendeleo wa mtu kwa Muu-
 18 ngu. Waliokosa pasipo torati watapotea pasipo torati;
 19 waliokosa wakiwa na torati watahukumiwa kwa torati.
 20 Kwani sio wasikiao torati walio na haki mbele ya Muu-
 21 ngu, illa watendao torati watakuwa na haki.
- 22 Kwani mataifa wasio na torati wakifanya kwa asili
 23 yaliyo katika torati, hawa wasio na torati wamekuwa
 24 torati yao wenyewe; waithahirisha kazi ya torati imea-
 25 ndikwa mioyoni mwao, thamiri ikiwashuhudia, mawazo
 26 yao yakishtakiana ao yakiachiliana; siku ile Muungu
 atakapohukumu siri za waana Adamu, kwa anjili yangu,
 kwa Isa Masiya.
- 27 Ukiwa umekwitwa Myahudi, ukategemea torati, uka-
 28 jisifu kwa Muungu, ukamjua apendalo, ukayapambanua
 29 yaliyo bora, ukielimishwa kwa torati, ukijithania mwe-
 30 nyewe kiongozi cha vipofu, mwanga wao walio gizani,
 31 mkufunzi wao wasio na akili, mwalimu wao watoto,
 32 ukiwa na namna ya hekima na kweli katika torati:
 33 umfundishaye mwingine, hujifundishi mwenyewe? Uhu-
 34 biriye wasiibe, umekwiba? Unenaye wasizini, umezini?
 35 Uchukiaye sanamu, umeyatwaa yaliyo wakf? Ujisifuye
 36 kwa torati, kwa kuikosa torati umemaibisha Muungu?
- 37 Kwani jina la Muungu limenenewa unajisi katika
 38 mataifa kwa ajili yenu, kama yalivyoandikwa. Tohara
 39 hufaa ukiishika torati: ukiwa mvunja torati, tohara yako
 40 umekuwa lisilo tohara. Pasipo tohara hukumu za torati
 41 zikishikwa, pasipo tohara isihesabiwe kuwa tohara?

Pasipo tohara, iliyo kwa asili, torati ikishikwa, itakuhu- 27
kumia wewe uliye na andiko na torati illa umeivunja
torati. Kwani siye Myahudi aliye kwa wazi, wala si 28
tohara iliyo kwa wazi katika mwili. Ndiye Myahudi 29
aliye kwa ndani; na tohara ya moyo, katika roho, wala
si katika andiko, yenyi sifa si kwa watu, illa kwa
Muungu.

BASSI Myahudi amezidije? na tohara yafaa nini? **3**
Sana kwa pande zote. Kwanza, kwani wameamriwa 2
ayanenayo Muungu. Nini tena, wangine wasipoamini? 3
Kutoa kuamini kwao kutabatili imani ya Muungu?
Hasha. Muungu awe na kweli, na killa mtu 'mwongo; 4
kama ilivyoandikwa, Illi uwe na haki katika maneno
yako, ukashinde uhukumiwapo.

Kama thulumu yetu imefanya imara haki ya Muungu, 5
tusemeje? Muungu hana haki atuletaye hasira? (Na-
nena kwa mwana Adamu.) Hasha. Ginsi gani Muungu 6
angehukumu ulimwengu? Kwani kweli ya Muungu 7
ikizidi kwa uwongo wangu, kwa kusifiwa Yeye, hatta
hivi kama akosaye nahukumiwa, wala si, kama tumene- 8
newa unajisi, na kama watu husema tumenena, Tuyafa-
nye mabaya, mema yakaje. Walukumiwao kwa haki.

Nini tena? Tumetangulia? Siyo kabisa. Kwani tu- 9
mewastaki na Wayahudi na Wayonani wote wako katika
thambi; kama yalivyoandikwa, Hapana mwenyi haki 10
hatta mmoja, hapana ajuaye, hapana amtakaye Muungu. 11
Wamekosa wote, wameoza pamoja. Hapana atendaye 12
mema hatta mmoja. Koo lao li kaburi wazi; kwa ulimi 13
wao hufanya hila. Sumu ya majoka chini ya midomo
yao. Kanwa lao limejaa laana na uchungu. Miguu ¹⁴/₁₅
yao mepesi kumwaga damu. Mathara na ubaya njiani 16
mwao, wala njia ya amani hawakuijua. Hapana hofu ya ¹⁷/₁₈
Muungu machoni pao.

Twajua kama inenayo torati yanena kwao walio chini 19
ya torati; killa kanwa lizibwe, ulimwengu wote usta-
kiwe mbele ya Muungu: kwa sababu katika matendo 20
ya sheria hapana kufanyiziwa haki mtu wo wote mbele
yake: kwani kwa sheria hujulikana makosa.

Sasa pasipo torati haki ya Muungu imeonekana, 21
iliyoshuhudiwa na torati na nabii; haki ya Muungu 22
kwa imani ya Isa Masiya katika wote na juu ya wote waa-

- 23 minio. Hapana tofauti; wote wamekosa, wamepunguka
 24 utukufu wa Muungu; wakafanyika kuwa na haki burre
 kwa neema yake kwa ukombozi ulio wa Masiya Isa:
 25 aliyemtoa Muungu upatanisho kwa imani katika damu
 yake, kuonyesha haki yake katika kuziachilia thambi
 26 zilizotangulia, akivumilia Muungu; kuonyesha haki
 yake wakati huu: akiwa mwenyi haki na mfanyiza
 haki kwake *aliye* wa imani ya Isa.
- 27 Wapi tena kujisifu? Kumeondolewa. Kwa sheria
 gani? Ya matendo? Siyo: illa kwa sheria ya imani.
- 28 Kwani twahasibu mtu kufanyiziwa haki kwa imani,
 pasipo matendo ya torati.
- 29 Ni Muungu wa Wayahudi tu? Siye tena wa mataifa?
 30 Na'am, wa mataifa tena; Muungu akiwa mmoja, afa-
 nyaye haki, kwao waliotahiriwa katika imani, na kwao
 31 wasiotahiriwa kwa imani. Sheria hatukuitangua kwa
 imani? Hasha; sheria tumeifanya imara.
- 4 TUSEMEJE** tena Ibrahimu baba wetu ameona nini
 2 katika mwili? Kwani Ibrahimu akipata kuwa na haki
 kwa matendo, anayo ajisifie, illa si kwa Muungu.
 3 Kwani maandiko yasema nini? Ibrahimu akamwamini
 4 Muungu, ikahesabika kwake kuwa haki. Atendaye,
 ijara yake haihesabiki kuwa neema, illa kuwa deni.
 5 Asiyetenda, aliyemwamini awafanyiaye haki wanajisi,
 6 imani yake imehesabika kuwa haki. Kama anenavyo
 na Daud heri yake mtu, Muungu aliyemhesabia haki
 7 pasipo matendo, Heri walioondolewa makosa, na thambi
 8 zao zimestirika. Heri ndiye mtu asiyemhesabia Bwana
 thambi.
- 9 Heri tena hii kwao waliotahiriwa, ao kwao tena
 wasiotahiriwa? Twasema kama imani imehesabika
 10 kwa Ibrahimu kuwa haki. Imehesabikaje? akiwa
 ametahiriwa, ao asipotahiriwa? Si alipokwisha kuta-
 11 hiriwa, illa asipotahiriwa: akapokea ishara ya tohara,
 muhuri ya haki ya imani iliyo asipotahiriwa: apate
 kuwa baba wao waaminio wasipotahiriwa, haki ikahesa-
 12 bike kwao; na baba wa tohara, wala si wao wenyi
 tohara tu, illa wafuatao nyayo za imani yake baba wetu
 13 Ibrahimu wakati asipotahiriwa. Kwani ahadi kwa
 Ibrahimu na kwa mzao wake, si kwa sheria, ataurithi
 14 ulimwengu, illa kwa haki ya imani. Kwani kama wale

walio katika sheria wangerithi, imani ingebatilika, ahadi ingetanguka, kwani ndiyo sheria ifanyayo hasira; 15 pasipokuwako sheria, hapana kukosa.

Kwa hiyo kwa imani, iwe kwa neema, ahadi iwe 16 imara kwa wazao wote; si kwa wale wa torati tu, illa tena wale wa imani ya Ibrahimu, aliye baba wetu wote (kama yalivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa 17 mataifa mengi) mbele ya Muungu aliyemwamini, awafanyaye hayi waliokufa, ayaitaye yasiyo kama yamekuwa. Aliyeamini kwa tumaini pasipo tumaini, apate 18 kuwa baba wa mataifa mengi, kama lililonenwa, Hivi litakuwa zao lako. Asiyethoofika katika imani, haku- 19 jikumbuka mwili wake kama umekwisha kufa, akiwa na miaka kama mia, wala ufu wa tumbo lake Sara: kwa ahadi ya Muungu hakuwa na shaka atoe kuamini, 20 illa kwa kuamini akapata nguvu, akimtukuza Muungu, akithubutika kama aliyoahidi akaweza kuyafanya. 21 Kwa hiyo ikahesabika kwake kuwa haki. 22

Hayakuandikwa kwa ajili yake tu, kama imehesabika; 23 illa kwa ajili yetu tena, tutakaohesabikiwa tukimwa- 24 mini aliyemfufua Isa Bwana wetu katika wafu, aliye- 25 tolewa kwa makosa yetu, akafufuka kwa kutufanyia haki.

BASSI tukipewa haki kwa imani, tunayo amani na 5 Muungu kwa Bwana wetu Isa Masiya; kwa huyo 2 tumepata katika imani kuifikia neema hii tunayoisi- mamia, tukifurahiwa na tumaini la utukufu wake Muungu. Wala si hiyo tu, illa twafurahi katika 3 shidda, tukijua kama shidda hufanya uvumilivu, na 4 uvumilivu kuthubutika, na kuthubutika tumaini, nalo 5 tumaini lisilotia haya; kwani upendo wa Muungu umemiminika mioyoni mwetu kwa Roho Mtakatifu tuliopewa.

Tena Masiya, tukiwa sisi thaifu, kwa wakati wake 6 akafa kwao waovu. Kwani kwa mtu wa haki mtu hafi 7 illa kwa shidda; kwa mtu mwema labuda na mtu atathubutu kufa. Muungu akaonyesha upendo wake 8 kwetu, kama, tukiwa sisi tumekosa, Masiya kwa sisi alikufa.

Sembuse sasa, tukipewa haki katika damu yake, 9 tutaokoka naye katika hasira. Kwani tulipokuwa 10

- maadui tukapatanishwa na Muungu kwa kufa Mwana wake, sembuse tukipatanishwa tutaokoka kwa uzima
- 11 wake. Illa si hiyo tu; tumefurahishwa tena katika Muungu kwa Bwana wetu Isa Masiya, kwa huyo
- 12 tuliyempokelea upatanisho. Hivi, kama kwa mtu mmoja thambi imeingia ulimwenguni, na kwa thambi kufa, kufa kukapita juu ya watu wote, kwa sababu
- 13 wote wamekosa: kwani hatta sheria kukosa kuli-kuwako katika ulimwengu, illa kukosa haina maana
- 14 pasipo sheria, kufa kukamiliki tangu Adamu hatta Musa juu yao wasiokosa kwa ginsi ya thambi yake Adamu, aliye namna yake atakayekuja.
- 15 Illa si kama anguko ni ukarimu. Ikiwa kwa kuanguka mtu mmoja walio wengi wamekufa, sembuse neema ya Muungu, nalo alilolitoa katika neema ya mtu mmoja, Isa Masiya, limezidi kwao walio wengi.
- 16 Wala si kama kwa mmoja aliyekosa, hili alitoalo: kwani hukumu ya mmoja kwa kuhukumia, ukarimu
- 17 ni wa matelezo mengi kwa kuwa na haki. Ikiwa katika kuteleza mmoja kufa kumemiliki kwa mmoja, sembuse wapokeao wingi wa neema, na kupewa haki, katika uzima watailiki kwa mmoja, Isa Masiya.
- 18 Kama tena kwa kuanguka mmoja kuhukumiwa kwa watu wote, hivi na kwa haki ya mmoja kwa watu wote
- 19 kupewa haki ya uzima. Kwani kama kwa kuasi mtu mmoja walio wengi wamekuwa na thambi, hivi na kwa kutii mtu mmoja walio wengi wamekuwa na haki.
- 20 Sheria ikaingilia anguko liwe kubwa; ukiwa kubwa
- 21 anguko, neema ikazidi kuwa nyingi: illi, kama kukosa kumemiliki katika kufa, hivi na neema imiliki kwa haki hatta uzima wa milele kwa Isa Masiya Bwana wetu.
- 6 TUSEMEJE** tena? Tufanye thambi illi neema izidi?
- 2 Hasha. Walioifia thambi wapateje kuishi katika thambi?
- 3 Hamjui kama waliobatizwa kwa Masiya Isa, kwa kufa
- 4 kwake wakabatizwa. Kwani tumezikwa pamoja naye kwa ubatizo kwa kufa, illi, kama Masiya alivyoondoka katika wafu kwa utukufu wa Baba, naswi tutembe
- 5 katika upya wa uzima. Tukiungwa pamoja naye katika mfano wa kufa kwake, tutakuwa tena katika ule wa
- 6 ufufuo wake: tukijua kama mtu wetu wa kwanza ame-sulibishwa pamoja naye, mwili wa thambi uharibike,

tusitumike tena sisi na thambi ; kwani aliyekufa ame- 7
kuwa huru katika thambi.

Tukifa pamoja naye Masiya twaamini kama tutaishi 8
pamoja naye ; tukijua kama Masiya akiondoka katika 9
wafu, hafi tena ; kufa haku'mwezi tena. Alivyokufa, 10
aliifia thambi marra moja ; alivyoishi, amwishia Muungu.
Hivi na ninyi jihesabuni wafu kwa thambi, wahayi kwa 11
Muungu katika Masiya Isa.

Bassi thambi isitawale katika mwili wenu ufao, kwa 12
kuzitii tamaa zake, wala msifanye viungo vyenu selaha 13
za thulumu katika thambi. Illakini mjifanyize kwa
Muungu kama wahayi katika kufa, na viungo vyenu
selaha za haki katika Muungu. Kwani thambi haiwa- 14
wezi : kwani hampo chini ya sheria, illa chini ya neema.

Nini tena? Tutende thambi, kwa sababu hatupo chini 15
ya sheria illa chini ya neema? Hasha. Hamjui kama 16
yule mtakayejifanyizia watumwa mmtii, mmekuwa wa-
tumwa wake mmtiye, ikiwa wa thambi kwa kufa, ikiwa
wa kutii kwa haki? Muungu ashukuriwe, kama mliku- 17
wa watumwa wa thambi, mkafuata kwa moyo namna ya
mafundisho mliyoipokea ; mkiwekwa huru katika thambi 18
mkatumika katika haki.

Nasema kwa mwana Adamu kwa sababu ya uthaifu 19
wa mwili wenu. Kama mlivyoweka viungo vyenu ku-
tumika na uchafu, na uovu kwa uovu, hivi sasa 'mweke
viungo vyenu kutumika na haki kwa kusafishwa. Kwani 20
mlipokuwa watumwa wa thambi, mlikuwa huru katika
haki.

Mazao gani mliyokuwa nayo ya mambo mliyoyata- 21
hayarikia sasa? Kwani mwisho wao ni kufa.

Illa sasa mmekuwa huru katika thambi, mkitumika 22
na Muungu, mnayo mazao yenu kwa kusafishwa, na
mwisho uzima wa milele. Kwani mshahara wa thambi 23
kufa ; ukarimu wa Muungu uzima wa milele katika Ma-
siya Isa Bwana wetu.

HAMJUI, ndugu (kwani nasema nao waijuao sheria), 7
kama sheria hu'mweza mtu, wakati ukiwapo hayi? 7
Kwani mwanamke aliyeolewa amefungwa na sheria kwa 2
mume akiwa hayi ; illa akifa mume, amefunguliwa katika
sheria yake mume. Mume akiwa hayi, huitwa mzini, 3
akiwa na mume mgine. Illa mume akifa, amekuwa
huru katika sheria, hatta si mzini, akiwa na mume mgine.

- 4 Hivi, ndugu zangu, mmekufa katika sheria, kwa mwili wake Masiya, mpate kuwa ninyi kwa mgine, aliyeondoka katika wafu, tupate kumzalia matunda Muungu.
- 5 Kwani tulipokuwa katika mwili, mapenzi ya thambi zilizo kwa sheria zikatenda katika viungo vyetu, tuzae matunda kwa kufa.
- 6 Illa sasa tumeondoka katika sheria, tumeifia iliyotuweza; utumwa wetu uwe katika upya wa rohoni, si kwa
- 7 ukale wa herufi. Tusemeje? Sheria ndiyo thambi? Hasha. Lakini singalijua thambi, illa kwa sheria: kwani singalijua kutamani, sheria isiponena, Usitamani.
- 8 Thambi ikipata asili kwa amri ikatenda kwangu killa kutamani: kwani pasipo sheria thambi kifu.
- 9 Mimi mzima kwanza pasipo sheria: ikija amri, thambi
- 10 imepata uzima, mimi nikafa. Nikaiona kwangu amri
- 11 iliyo kwa uzima, ndiyo kwa kufa. Kwani thambi ikipata chimbuko kwa amri ikanidanganya, nikafishwa nayo.
- 12 Hivi sheria takatifu, na amri takatifu, yenyi haki na
- 13 njema. Iliyo njema imekuwa mauti kwangu? Hasha. Illa thambi, ionekane kuwa thambi, ikinifanyia mauti kwalo lililo jema: thambi iwe kwa amri na thambi nyingi mno.
- 14 Twajua kama sheria inayo roho: nami ni wa mwilini,
- 15 niliyekuzwa chini ya thambi. Kwani sijui nifanyavyo:
- 16 nisiyoipenda naitenda; naichukia nitendayo. Kama
- 17 siipendi nitendayo, naikubali sheria kama nzuri. Bassi si mimi sasa niifanyaye, illa thambi ikaayo kwangu.
- 18 Najua kama halikai kwangu, ndiyo mwilini mwangu, neno lililo jema: kupenda ni karibu kwangu, kulifanya
- 19 lililo zuri sioni. Silo nilipendalo jema nilitendalo, lakini
- 20 nisilolipenda baya ndilo nilifanyalo. Kama nisilolipenda ndilo nilifanyalo, si mimi tena nilifanyaye, illa thambi ikaayo kwangu.
- 21 Bassi naona sheria, nipendapo kulitenda lililo zuri,
- 22 lililo baya karibu kwangu. Kwani napendezewa na she-
- 23 ria yake Muungu kwa mtu wa ndani: illa naona sheria ya pili katika viungo vyangu, ikipigana nayo sheria ya akili zangu, inifungayo katika sheria ya thambi iliyo katika viungo vyangu.
- 24 Mtu maskini mimi! ni nani atakayenitoa katika mwili wa mauti hii?
- 25 Namshukuru Muungu, kwa Isa Masiya Bwana wetu.

Bassi nami naitumikia sheria ya Muungu kwa akili, illa kwa mwili sheria ya thambi.

HAPANA tena kubukumiwa kwao walio katika Masiya Isa. Kwani sheria yake Roho ya uzima katika Masiya Isa imenitoa katika sheria ya thambi na kufa. 8 2

Isiyoyaweza sheria, kwa kuwa thaifu kwa sababu ya mwili, Muungu akimpeleka Mwana wake yeye, katika mfano wa mwili wa thambi, na kwa ajili ya thambi, amehukumu thambi katika mwili: haki yake sheria itimizwe kwetu, tusiokwenda kwa mwili, illa kwa Roho. 3 4

Walio kwa mwili huzifikiri za mwili; walio kwa Roho zile za Roho. Nia yake mwili ni mauti; nia ya Roho, uzima na amani. Kwa hiyo nia ya mwili ni wadui wa Muungu, kwani haitii sheria ya Muungu, wala haiwezi. Walio kwa mwili hawawezi kumpendeza Muungu. 5 6 7 8

Lakini ninyi si kwa mwili, illa kwa Roho, kama ana-kaa ndani yenu Roho ya Muungu. Mtu asiye na Roho ya Masiya, huyu si wake. Masiya akiwa kwenu, mwili umekufa kwa thambi; Roho ni uzima kwa haki. 9 10

Kama Roho iliyomfufua Isa katika wafu inakaa kwenu, aliyemfufua Isa katika wafu atafanya mizima na miili yenu ya kufa kwa Roho yake akaaye ndani yenu. Bassi ndugu, mwili hautuwii, tuufuate mwili. 11 12

Kwani mkifuata mwili, mtakufa: mkifisha matendo ya mwili kwa Roho, mtakuwa hayi. Kwani waifuatao Roho yake Muungu, ndio waanawe Muungu. Hamkupewa roho ya utumwa tena kwa hofu; illa mmepewa roho ya kuwa kama mwana, itulizayo, Abba, Baba. Roho mwenyewe hushuhudu pamoja na roho yetu kama sisi watoto wa Muungu: kama watoto, warithi tena; warithi wa Muungu, warithio pamoja naye Masiya; tukiwa tumeteswa naye tupate na kutukuzwa pamoja. 13 14 15 16 17

Kwani nahasibu, kama mateso ya wakati wa sasa halingani na utukufu utakaofunuliwa kwetu. Kwani kutazamia sana kwake kiumbe kunaungoja ufunuo wao waana wa Muungu. Kwani kimetiishwa na utupu kiumbe, si kwa moyo wake, illa kwa yule aliyekitiisha, katika tumaini, kama nacho kiumbe kitawekwa huru katika utumwa wa uharibifu, kupata ungwana wa utukufu wao waana wa Muungu. Kwani twajua kama kiumbe kinaugua, kinacho tena utungu hatta sasa. Wala si hivyo tu, illa na sisi, tulio nao mwanzo wa Roho, na sisi tunaugua ndani yetu, tusingoja kufanyika wa- 18 19 20 21 22 23

24 ana, ukombozi wa mwili wetu. Kwani tumeokoka kwa tumaini: tumaini lililoonekana silo tumaini. Aonaye
25 neno, mbona alitumainia? Tukilitumaini tusiloliona twalingoja kwa saburi.

26 Hivi na Roho huusayidia uthaifu wetu. Kwani hatujui kutaka neno kama ilivyotupasa; lakini Roho mwe-
27 nyewe hutombea kwa kuugua kusikonenekana. Ajaribuye mioyo anaijua nia yake Roho, kama anawaombea watakatifu kwa Muungu.

28 Twajua kama kwao wampendao Muungu yote huwa-
29 fanyia mema, kwao walioitwa kwa kusudi. Kama aliotangulia kuwajua, akawaweka kuwa mfano mmoja na namna ya Mwana wake, awe aliyezaliwa kwanza wa ndugu wengi. Aliowaweka, hawa akawaita. Aliowaita, hawa akawafanyizia haki. Aliowafanyizia haki, hawa akawatukuza.

31 Tuseme nini tena? Muungu akiwa kwetu, nani aliye
32 juu yetu? Asiyemwacha Mwana wake yeye, lakini amemtoa kwa ajili yetu, gissi gani asitukarimie naye mambo yote?

33 Nani atakayewastaki wateule wa Muungu? Muungu
34 ndiye afanyaye haki; nani atakayehukumu? Masiya ndiye aliyekufa, ao zayidi aliyefufuka, aliyoko mkono wa kuume wa Muungu, ndiye atumbeaye sisi.

35 Nani atakayetutenga katika mapenzi yake Masiya? Teso, ao shidda, ao fukuzo, ao njaa, ao utupu, ao hatari, ao upanga? kama ilivyoandikwa, Kwa sababu yako tuna-uawa mchana kutwa; tunahesabika kama kondoo za kuchinjwa. Lakini katika haya yote tumezidi kushinda
37 kwa yeye atupendaye. Kwani nimethubutika, kama wala mauti, wala maisha, wala malaika, wala mamlaka, wala yalipo, wala yatakayokuwa, wala nguvu, wala kwenda juu, wala kwenda chini, wala kiumbe cho chote chinginecho, hakiwezi kututenga katika mapenzi yake Muungu yaliyo katika Masiya Isa Bwana wetu.

9 NASEMA kweli katika Masiya, sisemi uwongo, moyo
2 wangu ukinishuhudia katika Roho Mtakatifu, kama huzuni nyingi kwangu, na kuuma kusikokwisha moyoni
3 mwangu. Kwani naomba mimi mwenyewe nitolewe katika Masiya kwa ajili ya ndugu zangu, jamaa zangu
4 kwa mwili, walio Waisraeli, wenyi kufanyika waana, na utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada, na
5 ahadi; walio nao baba, katika kwao Masiya kwa mwili,

aliye naye juu yote, Muungu mbarikiwa hatta milele.
Amin.

Isipokuwa kama neno la Muungu limeanguka. Kwa- 6
ni si wote walio wa Israeli, walio Israeli. Wala si kwa 7
kuwa wazao wa Ibrahimu watoto wote: illa, Katika
Isaak wazao wako wataitwa: ndio, sio watoto wa mwili 8
walio watoto wa Muungu; illa watoto wa ahadi wamehe-
sabika kuwa wazao. Kwani neno la ahadi ndilo hilo, 9
Kwa wakati huu nitakuja, na Sara atakuwa na mtoto.

Wala si hivyo tu; illa na Rebeka akiwa na mimba 10
kwa mmoja, baba wetu Isaak, wakiwa hawajazaliwa, 11
wala hawajafanya neno wala jema wala baya, kusudi
lake Muungu kuchagua likae, si kwa matendo, illa kwa
yule aliyeita, akaambiwa hivi, Mkubwa atamtumikia 12
mdogo. Kama ilivyoandikwa, Yakobo nimempenda, 13
Esau nimemchukia.

Tusemeje tena? Muungu hana haki? Hasha. Kwani 14
akamwambia Musa, Nitamrehemu nitakayemrehemu,
nitamhurumia nitakayemhurumia. Bassi tena si yake 16
apendaye, wala yake aendaye, illa yake Muungu arehe-
muye. Kwani maandiko yamsemea Farao, Kwa hiyo 17
nikakusimamisha, nionyeshe kwako uwezo wangu, jina
langu lihubiriwe katika inchi yote. Bassi appendaye 18
amrehemu, appendaye amfanya mgumu.

Utaniambia tena, Mbona analaumu? Nani aliyepiga- 19
na na shauri lake?

Illa afathali, nani wewe umjibuye Muungu? Kili- 20
chofanyika kimwambie mfanya, Mbona umenifanya hivi?
Hana mfinangi uwezo juu ya udongo, afanye katika 21
fungu moja, chombo hiki kwa heshima, na hiki kisiwe
na heshima?

Muungu akipenda kuonyesha hasira, uwezo wake 22
ujulike, amestahimilia kwa uvumilivu mwingi vyombo
vya hasira, vilivyotengenezwa viharibike; tena wingi 23
wa utukufu wake ujulike katika vyombo vya rehema,
alivyovifanya tayari vitukuzwe, ndivyo sisi aliyetuita, 24
si kwa Wayahudi tu, illa kwa mataifa; kama alivyose- 25
ma katika Hosea, Nitawaita watu wangu wasio watu
wangu, naye amependwa asiyependwa. Itakuwa mahali 26
walipoambiwa, Ninyi si watu wangu, huko wataitwa
waana wa Muungu aliye hayi. Isaya anawalilia Israeli, 27
Kama hesabu ya waana wa Israeli ingalikuwa kama

28 mchanga wa pwani, waliosalia wataokoka : kwani neno
 la kumaliza na neno la kukata katika haki, kama neno
 29 lililokatika, atalifanya Bwana katika inchi. Na kama
 alivyotangulia kunena Isaya, Kama Bwana wa Sabaoth
 hangalituachia uzao, kama Sodoma tungalikuwa, tunga-
 lifanana na Gomorra.

30 Tusemeje? Kama mataifa wasiofuata haki wamepewa
 31 haki, illa haki iliyo katika kuamini. Israeli walioifuata
 32 sheria ya haki hawakuifikia sheria. Kwa nini? Kwa
 sababu si kwa kuamini, illa kama kwa matendo : waka-
 33 jikwaa katika jiwe lile la kukwalia ; kama ilivyoandi-
 kwa, Angalia, naweka katika Sayuni jiwe la kukwalia
 na mwamba wa kuchukizisha : naye amwaminiye hataa-
 ibishwa.

10 NDUGU, mapenzi ya moyoni mwangu na kusihi kwa
 Muungu kwa ajili yao Waisraeli ndiyo hiyo, waokoke.
 2 Kwani nawashuhudia wanao uwivu kwa Muungu, illa
 3 si kwa hekima. Wasipoijua haki ya Muungu, wakitaka
 kuifanya imara yao wenyewe, hawakuifuata haki ya
 4 Muungu : kwani Masiya ndiye aliye mwisho wa sheria
 kwa haki kwao wote wanaoamini.

5 Kwani Musa aandika haki iliyo kwa sheria, kama,
 6 Mtu ayatendaye ataishi kwayo. Illa haki iliyo kwa
 imani yasema hivi, Usiseme moyoni mwako, Nani ata-
 kayepanda mbinguni? (ndio kumleta Masiya chini :)
 7 wala, Nani atakayeshuka shimoni? (ndio kumleta Ma-
 8 siya juu katika wafu.) Illa yasemaje? Neno liko
 karibu yako, katika kanwa lako, na katika moyo wako :
 9 ndilo neno la imani tulihubirilo. Kwani ukimwungama
 kwa kanwa lako Bwana Isa, ukaamini kwa moyo wako
 10 kama Muungu amemfufua katika wafu, utaokoka. Kwa-
 ni kwa moyo huamini kwa haki, kwa kanwa huungama
 kwa wokovu.

11 Kwani maandiko yasema, Killa amwaminiye haibiki.
 12 Wala hapana tofauti ya Myahudi na Myonani : kwani
 ndiye juu yote Bwana wa utajiri wote, kwao wote wamwi-
 13 tia : kwani, Killa atakayeliitia jina la Bwana ataokoka.
 14 Bassi wapateje kumwitia wasiyemwamini? Wapateje
 kumwamini wasiopata habari zake? Wapateje habari
 15 pasipo mhubiri? Wapateje kuhubiri wasiopelekwa?
 Kama ilivyoandikwa, Mizuri miguu yao wahubirio
 anjili ya amani, wahubirio anjili ya mema.

Illa wote hawakuikubali anjili. Kwani Isaya ana- 16
 sema, Bwana, nani aliyeamini habari zetu? Nayo 17
 imani kwa kusikia, na kusikia kwa neno la Muungu.
 Lakini nasema, Hawakusikia? Yakini, Hatta inchi 18
 yote imetoka sauti yao, na hatta mipaka ya ulimwengu
 maneno yao. Lakini nasema, Israeli hakujua? Kwanza 19
 Musa anasema, Nitawatia uwivu kwao wasio taifa, na
 kwa taifa wasio na akili nitawakasirisha. Isaya hakuo- 20
 gopa, akasema, Nimconwa nao wasionitafuta mimi, ni-
 meonekana nao wasioniulizia. Kwa Israeli anasema, 21
 Mchana kutwa nimewanyoshea mikono watu wasiotii na
 wasiokubali.

NASEMA tena, Muungu amewatupa watu wake? 11
 Hasha. Kwani na mimi ni Mwisraeli, katika wazao wa
 Ibrahimu, kabila la Benyamin. Hakutupa Muungu 2
 watu wake aliotangulia kuwajua. Hamjui ya Eliya
 yasemaje maandiko? kama alivyowanenea Israeli kwa
 Muungu, Bwana, nabii zako wamewaua, mathbahu zako 3
 wameyaangusha: nami nimesalia peke yangu, nao wa-
 nitafuta roho yangu. Lakini aambiwaje na jawabu? 4
 Nimejiwekea waume elfu saba, wasiokunja gote kwa
 Baal. Hivi na wakati huu yamekuwa masalia kwa 5
 kuchagua kwa neema. Ikiwa kwa neema, si tena kwa 6
 matendo, neema isiishe kuwa neema; kama kwa mate-
 ndo, si tena kwa neema, matendo yasiishe kuwa matendo.

Nini tena? Waitafutayo Israeli, hawakuiona; wa- 7
 liochaguliwa wameiona, waliosalia wakatiwa ugumu:
 kama ilivyoandikwa, Wakapewa na Muungu roho ya 8
 usingizi, macho yasiyoona na masikio yasiyosikia, hatta
 leo. Naye Daud anasema, Meza yao iwe shabuka, na 9
 mtego, na jiwe la kujikwaa, na thawabu kwao: macho 10
 yao yatiwe giza, wasione, ukawainamishe mgongo siku
 zote.

Nasema, Wamejikwaa illi waanguke? Hasha. La- 11
 kini kwa anguko lao wokovu wa mataifa, watiwe uwivu.
 Kosa lao likiwa fayida ya ulimwengu, na upungufu wao 12
 fayida ya mataifa, si zayidi sana utimilifu wao?

Kwani nasema nanyi wa mataifa. Nikiwa mimi 13
 mtume wa mataifa natukuza kazi yangu, nipate labuda 14
 kuwatia uwivu walio mwili wangu, niwaokoe baathi
 yao. Kwani kuwatupa wao kukiwa kupatanisha uli- 15
 mwengu, nini kuwakubali, illa uzima katika wafu?

- 16 Limbuko likiwa takatifu, nacho chungu; shina likiwa takatifu, nayo matawi.
- 17 Tawi zikikatika, wewe mzetuni wa mwituni utiliwe mahali pao, ukashariki shina na unono wa mzetuni,
- 18 usijisifu juu ya tawi: ukijisifu, si wewe ulichukuaye shina, illa shina wewe.
- 19 Bassi utasema, Tawi zimekatika nitiliwe mimi.
- 20 Vema; kwa kukosa kuamini zikakatika, nawe wasima-
- 21 ma kwa imani. Usione makuu, illa wogope: kwani Muungu asipoziachia tawi zilizo kwa asili, asikuachie wewe.
- 22 Angalia wema na uzito wa Muungu: kwao walio-
anguka uzito; kwako wema, ukikaa katika wema: illa
- 23 na wewe utakatika. Na hawa wasipokaa katika kutoa kuamini, watatiliwa: kwani Muungu aweza tena kuwatilia hawa.
- 24 Kama wewe uliyekatika katika mzetuni wa asili wa mwituni, juu ya asili ukatiliwa katika mzetuni mwema, si zayidi hawa walio wa asili watiliwe katika mzetuni wao wenyewe?
- 25 Kwani sipendi, ndugu, msijue siri hiyo, msijione ndinyi wa akili, kama ugumu kwa sehemu umewawia
- 26 Israeli, hatta utimilifu wa mataifa utakapoingia; na hivi Israeli wote wataokoka: kama ilivyoandikwa, Atatoka katika Sayuni aokoaye; atawageukia Yakobo unajisi: na hilo agano langu kwao, nitakapoondoa thambi
- 27 zao. Katika anjili, adui kwa ajili yenu: katika kuchaguliwa, wamependwa kwa ajili za baba. Kwani makarimu na mwito wa Muungu hauna kugeuka.
- 30 Kama ninyi kwanza hamkumwamini Muungu, mka-
- 31 pata rehema kwa kutoa kuamini kwao, hivi na hawa sasa hawakuamini, illi kwa rehema yenu na hawa wapate
- 32 rehema. Kwani Muungu amewafunga wote katika kutoa kuamini, awape wote rehema.
- 33 Ee malindi ya utajiri na hekima na kujua kwa Muungu! hukumu zake hazitafutikani, na njia zake hazia-
- 34 ndikani. Nani aliyemjua nia yake Bwana, ao nani aliyemshauri wake? Ao nani aliyemtolea, naye atarudishiwa? Kwani Yeye asili, na Yeye njia, na Yeye mwisho wa yote. Utukufu uwe kwake milele. Amin.
- 12 NAWASIHI, ndugu, kwa huruma za Muungu, mtoe miili yenu thabihu iliyo hayi, takatifu, kumpendeza

Muungu, ibada yenu ya akili; wala msifananishwe na 2
dunia hii: illa mgeuke kwa kufanya mpya nia zenu,
mpate kuthubutisha nini alipendalo Muungu lililo jema,
na kupendeza, na kamilifu.

Namwambia killa mtu wa kwenu, kwa neema niliyo- 3
pewa, asijithanie kuliko iliyompasa kuthani, illa afikiri
kwa kadiri, kama killa mtu aliyogawaniwa na Muungu
cheo cha imani. Kwani kama katika mwili mmoja kuna 4
viungo vingi, wala viungo vyote havinayo kazi moja;
hivi sisi wengi tumekuwa mwili mmoja katika Masiya, 5
na mmoja mmoja viungo sisi kwa sisi.

Tukiwa na makarimu kwa neema tuliopewa yasiyo 6
mamoja, kama unabii, kwa kadiri yake imani; kama
ungoje, katika kungojea; kama mkufunzi, katika ku- 7
fundisha; kama aonyaye, katika kuonya; atoaye, pasipo 8
hila; atawalaye, kwa bidii; arehemuye, katika ku-
furahiwa.

Kupenda pasipo unafiki: mkilichukia ovu, mkiamba- 9
tana nalo jema. Katika kupendana shauko mtu kwa 10
mtu. Katika heshima mkitanguliza wenzenu. Katika 11
makusudi si wavivu; wepesi rohoni; mkimtumikia Bwa-
na. Katika kutaraja mkifurahi; katika shidda mkivu- 12
milia; katika kuomba mkitia moyo; mkigawanya kwa 13
mahitaji yao watakatifu; mkifuata kuwakaribisha wa-
geni.

'Mwabariki wawafukuzao; barikini, msilaani. Ku- 14
furahi nao wafurahio; kulia nao waliao. Mkithania sa- 16
wa ninyi kwa ninyi. Msiyathanie yaliyo juu, illa mfua-
tane nao walio chini. Msiwe na akili kwenu wenyewe.
Msimlipie mtu ovu kwa ovu. Mkiandika vema machoni 17
pa watu wote. Kama yamkini, miongoni mwenu, mpa- 18
tane na watu wote, msipojilipiza haki, enyi niwapendao; 19
mkaiachie nafasi hasira: kwani imeandikwa, Kisasi ni
changu, mimi nitalipa, amenena Bwana. Naye adui 20
wako akiona njaa, mlishe; akiona kiu mnyweshe: kwa-
ni ukifanya hivi utamletea makaa ya moto mengi kitwani
mwake.

Msishindwe na uovu, illa mshinde uovu kwa wema. 21

KILLA mtu azitii nguvu zilizo juu: kwani nguvu 13
hapana, isipokuwa kwa Muungu; nguvu zilizo zimeam-
riwa na Muungu. Nao wanaoziasi nguvu waiasi amri 2
ya Muungu; nao waasio wajiletea hukumu. Watawa- 3

- lao si kuogofya katika tendo jema, illa katika baya. Uki-
penda usiogope nguvu, tenda vema, utakuwa na kusifiwa
4 naye. Kwani ni mtumishi wake Muungu kwako kwa
mema. Ukitenda vibaya, ogope; kwani hachukui upa-
nga burre: ni mtumishi wake Muungu amlipiaye ha-
5 sira atendaye vibaya. Hivi sharti mtii, si kwa hasira tu,
6 illa kwa moyo. Kwa hiyo tena mwatoa kodi; kwani
hawa wenyi amri kwa Muungu wakingoja hiyohiyo.
- 7 Mlipe killa mtu alivyopaswa: yule wa kodi, kodi;
yule wa ushuru, ushuru; yule wa kuogofya, kuogopa;
8 yule wa heshima, heshima. Msiwiwe na mtu cho chote,
illa kupendana: kwani ampendaye mtu ameitimiza torati.
- 9 Kwani ile, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani, na amringi-
neyo yote, katika neno hili imejumlishwa, katika hili,
10 Umpende jirani wako kama moyo wako. Ampendaye ji-
rani hamtendei vibaya: bassi kupenda ni timizo la sheria.
- 11 Na haya, mkiujua wakati, kama sasa saa sisi tuamke
katika usingizi: kwani wokovu wetu leo karibu kuliko
12 tulipoamini. Usiku unapita; mchana karibu: tuvue
13 matendo ya giza, tuvae selaha za weupe. Kama mcha-
na tutembea kwa taratibu; si katika kula na kulewa, si
katika asharati na jeuri, si katika ugomvi na uwivu.
- 14 Illa vaeni Bwana Isa Masiya, wala msifanye fikara za
mwili kwa tamaa.
- 14** ALIYE thaifu mkaribisheni katika imani, si kuya-
pambanua maswali.
- 2 Huyu athubutu kula vyote; huyu aliye thaifu hula
3 mboga. Alaye asimtharau asiyekula, wala asiyekula
asimhukumu alaye; kwani Muungu amkubaliye.
- 4 Nani weve umhukumuye mtumwa wa mwenyewe?
kwa bwana wake yeye husimama ao kuanguka. Atasi-
mamishwa; kwani Muungu awezaye kumsimamisha.
- 5 Huyu achagua katika siku na siku; huyu achagua
killa siku. Killa mtu athubutike katika nia yake.
- 6 Aifikiriye siku, kwa Bwana hufikiri; asiyefikiri siku,
kwa Bwana hafikiri. Alaye, hula kwa Bwana, akimshu-
kuru Muungu; asiyekula, kwa Bwana hali, naye am-
7 shukuru Muungu. Hakuna kwetu aishiye kwa nafsi
8 yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake. Tukiishi, kwa
Bwana twaishi; tukifa, kwa Bwana twafa. Bassi tu-
9 kiishi, tukifa, aliye naswi Bwana. Kwa hiyo Masiya
alikufa akafufuka, awamiliki na wafu na wahayi.

Mbona wewe wamhukumu ndugu yako? ama wewe 10
wamtharau ndugu wako? kwani wote tutasimama kitini
pa Muungu. Kwani imeandikwa, Mimi hayi, anena 11
Bwana, ya kwamba litanikunjia killa gote, na killa uli-
mi utamwungamia Muungu. Bassi tena sisi killa 12
mmoja wetu atatoa hesabu yake kwa Muungu.

Bassi tusihukumiane: illa afathali tuhukumu ndugu 13
asitiwe ukwazo wala chukizo.

Najua, nikimtumainia Bwana Isa, kama hakuna kitu 14
chenyi unajisi chenyewe: illa kwake akionaye cha una-
jisi, kinao unajisi. Ndugu wako akihuzunika kwa 15
chakula chako, huendi katika kupendana. Usimharibu
kwa chakula chako Masiya aliyekufa kwa ajili yake.

Jema lenu lisinenwe unajisi: kwani ufalme wa Muu- 16
ngu si kula na kunywa, illa haki, na amani, na furaha 17
katika Roho Mtakatifu; kwani amtumikiaye Masiya 18
hivi, hupendeza Muungu, husifiwa tena na watu.

Bassi tufuate mambo ya amani, nayo ya kujengeana. 19
Kwa ajili ya chakula usiharibu kazi yake Muungu. 20

Yote safi; illa mabaya kwake alaye kwa kujikwaa.
Ni heri kutoa kula nyama, na kunywa mvinyo, ama 21
yote yamkwazayo ndugu, ao yamechukizishayo, ao ya-
mthoofishayo.

Unayo imani? Uwe nayo mwenyewe machoni pa 22
Muungu. Yu heri asiyejihukumu katika alikubalilo.
Apambanuaye huhukumiwa akila, kwani silo la imani; 23
lisilo la imani lote ni thambi.

IMETUPASA sisi tulio hodari kuchukua uthaifu wao 15
wasio na nguvu, wala si kujipendeza. Killa wetu a- 2
mpendeze jirani wake kwa kujengea. Kwani Masiya 3
hakujipendeza mwenyewe; illa, kama ilivyoandikwa,
Mashutumumu yao waliokushutumumu yameniangukia mimi.

Yaliyoandikwa zamani yameandikwa kwa mafundisho 4
yetu, tupate kwa uvumilivu na faraja ya maandiko
kuwa na tumaini.

Muungu wa uvumilivu na faraja awajalie kuwaza 5
mamoja ninyi kwa ninyi katika Masiya Isa, mpate we- 6
nyi moyo mmoja kwa kanwa moja kumtukuza Muungu
na Baba wa Bwana wetu Isa Masiya. Kwa hiyo mku- 7
baliane, kama Masiya alivyotukubali, kwa utukufu
wake Muungu.

Kwani nasema Isa Masiya amekuwa mngoje wa tohara 8

- kwa ajili ya kweli yake Muungu, afanye imara ahadi
 9 zao baba, illi mataifa wamtukuze Muungu kwa ajili ya
 rehema; kama ilivyoandikwa, Kwa hiyo nitakuungama
 10 katika mataifa, na kwa jina lako nitaimba. Na tena
 anena, Mpendezewe, mataifa, pamoja na watu wake.
 11 Na tena, Msifuni Bwana, mataifa yote; mtukuzeni,
 12 enyi watu wote. Na tena Isaya anena, Litakuwa shina
 la Yesse, naye atakayesimama kuwatawala mataifa;
 ndiye mataifa watakayemtumainia.
- 13 Muungu wa tumaini awajaze na furaha yote na amani,
 katika kuamini, mzidi ninyi katika tumaini na nguvu
 za Roho Mtakatifu.
- 14 Nimethubutika mimi, ndugu zangu, juu yenu, kama
 ninyi mmejaa wema, mkijalizwa na elimu yote, mkiweza
 15 na kujifundishana. Nimewaandikia, ndugu, pasipo
 hofu, kwa sehemu, kama kuwakumbusha, kwa nema
 16 niliyopewa na Muungu, niwe mimi wakili wa Masiya
 Isa kwa mataifa, nikifanya kazi ya mkohani wa anjili
 ya Muungu, sadaka za mataifa zikubalike, zikitakaswa
 katika Roho Mtakatifu.
- ¹⁷₁₈ Nina kujisifu katika Masiya Isa kwa Muungu. Kwa-
 ni sitathubutu kutoa neno asilolitenda Masiya kwa mimi,
 19 mataifa watii, katika na neno na tendo, kwa nguvu ya
 ishara na ajabu, kwa nguvu yake Roho Mtakatifu;
 hatta mimi, kutoka Yerusalemi na kuzunguka hatta
 20 katika Illuriko, nimetimiliza anjili yake Masiya, nikio-
 na kazi ya heshima ndiyo kuhubiri pasiponenwa jina
 lake Masiya, nisijenge juu ya msinji wa mwenyewe;
 21 lakini, kama ilivyoandikwa, Wasiohubiriwa mambo
 22 yake wataona, nao wasiosikia watafahamu. Kwa hiyo
 nikazuiwa sana katika kuja kwenu.
- 23 Sasa nisipokuwa tena na nafasi katika inchi hizi, ni-
 24 kiwa tangu miaka mingi na shauko kuja kwenu, niki-
 safiri kwenda Spania, nataraja katika kupita kuwaona
 ninyi, na kupelekwa mbele nanyi, nikishibishwa kadiri
 kwanza nanyi.
- 25 Illa sasa nakwenda Yerusalemi, nikiwangojea wata-
 26 katifu. Kwani Umakedoni na Akaya wamependezwa
 kufanya usharika nao walio maskini wa watakatifu
 27 walioko Yerusalemi. Wamependezwa; nao imewapasa.
 Kwani mataifa wakishariki nao mambo ya roho, imewa-
 pasa kuwachukulia mizigo katika mambo ya mwili.

Nikitimiza haya, nikiwawekea kwa muhuri tunda hili, 28
 nitasafiri kwa ninyi kwenda Spania. Najua nikija 29
 kwenu, nitakuja katika kujaa mbaraka wake Masiya.

Nawasihi ninyi, ndugu, kwa Bwana wetu Isa Masiya, 30
 na kwa mapenzi yake Roho, mjitahidi pamoja nami, ka-
 tika kumwomba Muungu kwa ajili yangu, niokoke 31
 katika wale wasioamini wa Uyahudi, na ungoje wangu
 ulio katika Yerusalemi ukubalike nao watakatifu; ni- 32
 pate kuja kwenu furahani, kwa kupenda Muungu,
 nipumzike pamoja nanyi.

Muungu wa amani pamoja nanyi nyote. Amina. 33

NAWALETEA ninyi Foibe ndugu yetu, akiwa 16
 mngoje wa kanisa lilioko Kenkree: mmkubali katika 2
 Bwana, kama ilivyowapasa watakatifu, mkamsayidie
 katika neno lo lote atakalowahitajia: kwani na yeye
 amekuwa msayidia wengi, hatta na mimi.

Salimieni Priska na Akula, watendao kazi nami kati- 3
 ka Masiya Isa, waliolaza mashingo yao kwa ajili ya 4
 maisha yangu; nisiowashukuru mimi tu, illa makanisa
 yote ya mataifa: nalo kanisa katika nyumba yao. 5

Salimieni Epaineto, nimpendaye, aliye wa kwanza wa
 Asia kwa Masiya. Salimieni Maryamu, aliyetutendea 6
 kazi nyingi. Salimieni Androniko na Yunia, jamaa 7
 zangu, waliofungwa pamoja nami, walio wa heshima
 nao mitume, walionitangulia mimi kuwa katika Masiya.

Salimieni Amplia, nimpendaye katika Masiya. Sa- 8
 limieni Urbano, atendaye kazi pamoja nami katika Masi-
 ya; na Stakus, nimpendaye. Salimieni Apelle, aliye- 10
 kubalika katika Masiya. Salimieni wale kwa Aristobulo.

Salimieni Herodioni, jamaa yangu. Salimieni walio 11
 wa Narkisso walio katika Masiya. Salimieni Trufaina 12
 na Trufosa, watendao kazi katika Masiya. Salimieni
 Persi, aliyependwa, aliyetenda kazi nyingi katika
 Masiya. Salimieni Rufo, mteule katika Masiya; na 13
 mama yake na yangu. Salimieni Asunkrito, Flegoni, 14
 Herme, Patroba, Herma, nao ndugu walio pamoja nao.
 Salimieni Filologo na Yulia, Nereu na ndugu yake, na 15
 Olumpa, nao watakatifu wote walio pamoja nao.

Msalimiane kwa busu takatifu. Makanisa yote yake 16
 Masiya wawasalimia.

Nawasihi, ndugu, angalieni wale wafanyao fitina na 17
 machukizo juu ya mafundisho mliyojifunza, mkawageu-

- 18 kie. Kwani ndio wasiomtumikia Bwana wetu Masiya, illa matumbo yao wenyewe; na kwa maneno mazuri na mazungumzo mema wapoteza mioyo yao wajinga.
- 19 Kwani mutia wenu umewafikia wote. Juu yenu nafurahi: nataka 'mwe werevu katika mema, na wajinga
- 20 katika mabaya. Muungu wa amani atamvunja Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Isa Masiya kwenu.
- 21 Timoteo, atendaye kazi pamoja nami, awasalimia, na
- 22 Lukio, na Yason, na Sosipatro, jamaa zangu. Nawasalimia mimi Tertio, niandikaye waraka huu, katika Bwana.
- 23 Awasalimia Gayo, mwenyeji wangu na wa kanisa lote. Awasalimia Erasto wakili wa mji, na Kwarto
- 24 ndugu. Neema ya Bwana wetu Isa Masiya nanyi nyote. Amin.
- 25 Awezaye kutufanya imara kwa anjili yangu na kumhubiri Isa Masiya, kwa ufunuo wa siri isiyonenwa tangu
- 26 zamani za milele, imethihirishwa kwa maandiko ya nabii, kwa amri yake Muungu wa milele, ikajulikani-
- 27 shwa kwa mataifa yote, imani itiiwe; Muungu mwenyi peke yake hekima, kwa Isa Masiya awe na utukufu hatta milele. Amin.

WARAKA WA KWANZA WA PAOLO MTUME

KWA

WAKORINTI.

- 1 PAOLO, aitwaye mtume wa Masiya Isa kwa mapenzi
- 2 ya Muungu, na Sostene ndugu, kwa kanisa la Muungu lililoko katika Korinto, lililotakaswa katika Masiya Isa, waitwao watakatifu, pamoja nao wote waliitiao jina la Bwana wetu Isa Masiya mahali pote, na wao na wetu:
- 3 Neema kwenu na amani ya Muungu Baba wetu na Bwana Isa Masiya.
- 4 Namshukuru Muungu wangu dayima kwa ajili yenu, kwa neema yake Muungu mliyopewa katika Masiya Isa,
- 5 ya kwamba mmepewa mali katika huyu killa yaliyo,

katika akili na hekima yote, kama ushahidi wake Masiya 6
ya umekuwa imara kwenu, hatta msipunguke ukarimu, 7
mkiungoja ufunuo wa Bwana wetu Isa Masiya, atakaye- 8
wafanya ninyi imara hatta mwisho, msilaumiwe siku ya
Bwana wetu Isa Masiya. Amini Muungu, mlioitwa 9
naye kwa usharika wa Mwana wake Isa Masiya Bwana
wetu.

Nawasihi ninyi, ndugu, kwa jina la Bwana wetu Isa 10
Masiya, mnene wote mamoja, pasiwe kwenu kutengwa,
illa 'mwe mmeungana katika nia moja na wosia mmoja.

Imethihirishwa kwangu, ndugu, juu yenu, nao walio 11
wa Kloe, kama fitina ziko kwenu.

Nasema haya, ya kwamba killa kwenu husema, Mimi 12
wa Paolo; mimi wa Apollo; mimi wa Kefa; mimi wa
Masiya. Masiya amegawanyika? Paolo amesulibishwa 13
ajili yenu? Kwa jina la Paolo mmebatizwa? Na- 14
mshukuru Muungu ya kwamba sikubatiza mtu kwenu,
illa Krispo na Gayo, mtu asiseme nimebatiza kwa jina 15
langu mimi. Nikabatiza na nyumba yake Stefana; illa 16
hao sijui kama nimebatiza mtu mwingine.

Kwani Masiya hakunituma nibatize, illa nihubiri: 17
wala si kwa neno la hekima, msalaba wake Maziya usi-
batilike. Kwani neno la msalaba kwao wanaopotea 18
upuuzi; kwetu tunaokoka ni nguvu ya Muungu.
Kwani imeandikwa, Nitabaribu hekima zao wenyi he- 19
kima, na akili zao wenyi akili nitaziondoa. Yu wapi 20
mwenyi akili? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mtafu-
taji wa dunia hii? Siye Muungu aliyepumbazisha heki-
ma ya dunia? Kwani katika hekima ya Muungu dunia 21
isipomjua Muungu kwa hekima, akapenda Muungu, kwa
upumbafu wake iliyohubiriwa, kuwaokoa waaminio.
Kwani Wayahudi wataka ishara, na Wayonani wataka 22
hekima: nasi twahubiri Masiya amesulibishwa, kwa 23
Wayahudi ukwazo, kwa mataifa upumbafu, illa kwao 24
waitwao, na Wayahudi na Wayonani, Masiya nguvu
ya Muungu na hekima ya Muungu: upumbafu wa 25
Muungu ukiwa na hekima kuliko watu, na uthaifu
wa Muungu mwenyi nguvu kuliko watu.

Angalieni wito wenu, ndugu, kama si wengi wenyi 26
hekima ya mwilini, si wengi wenyi nguvu, si wengi
wakuu, lakini mapumbafu ya duniani Muungu ameya- 27
chagua, illi waaibike wenyi hekima; na thaifu za duni-

28 ani amezichagua, wenyi nguvu waaibike; na manyonge
ya duniani na yaliyotharauliwa ameyachagua Muungu,
29 hatta yasiyo nayo, yaliyo nayo yapotee: mwenyi mwili
30 asipate kujisifu mbele ya Muungu. Kwa huyo nanyi
katika Masiya Isa, aliyekuwa kwetu hekima, katika kwa
31 Muungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi: illi, ka-
ma ilivyoandikwa, Ajisifuye ajisifu katika Bwana.

2 NAMI nikija kwenu, ndugu, sikuja kuuhubiri usha-
hidi wa Muungu katika uzuri wa maneno, wala wa
2 hekima; kwani naliazimu nisijue neno kwenu, illa Isa
3 Masiya, naye amesulibishwa. Nami katika uthaifu, na
4 hofu, na matetemeko mengi, nalikuwako kwenu. Wala
neni langu wala habari zangu si katika maneno ya he-
kima ya kushawishi, illa katika wonyesho wa Roho na
5 wa nguvu: imani yenu isiwe katika hekima ya watu,
illa katika nguvu za Muungu.

6 Twanena hekima kwao walio wakamilifu: si hekima
ya dunia hii, wala wao wakuu wa duniani, wanaobati-
7 lika: illa twanena hekima ya Muungu katika siri, iliyo-
fichwa, aliyoiamuru Muungu mbele ya zamani, kwa
8 utukufu wetu: wasiyoijua wakuu wa dunia hii hatta
mmoja, kwani kama wanalijua, hawangalimsulibisha
9 Bwana wa utukufu: lakini, kama ilivyoandikwa, Jicho
lisiloliona, wala sikio lisilolisikia, wala halikumwingia
mtu moyoni, ndilo Muungu alilowafanyizia wampendao.
10 Muungu amelifunua kwetu kwa Roho yake: kwani
Roho hutafuta yote, hatta yaliyo chini ya Muungu.
11 Mtu gani ayajuaye ya mtu, illa roho ya mtu iliyo ndani
yake? Hivi yaliyo ya Muungu, hakuna ajuaye, illa
12 Roho yake Muungu. Wala sisi hatukupokea roho ya
dunia, illa Roho iliyo katika Muungu; tupate kuyajua
13 tuliyoneemeshwa na Muungu. Nayo twayanena, si
kwa maneno yaliyofundishwa kwa hekima ya waana
Adamu, illa yaliyofundishwa na Roho, tukiyalinganisha
ya rohani haya na haya.

14 Mtu wa ulimwengu hayapokei yaliyo ya Roho yake
Muungu, kwani kwake mapumbafu, wala havezi kuya-
15 jua, kwani yajaribika kwa roho. Mtu wa roho huyaja-
16 ribu yote, wala yeye hajaribiwi na mtu. Kwani, Nani
aliyejua nia yake Bwana, amwelimishe? Illa sisi tunayo
nia yake Masiya.

3 NAMI, ndugu, sikuweza kusema nanyi kama wa ro-

honi, illa kama wa mwilini, kama vitoto katika Masiya. Nimewanyweshwa maziwa, wala si nyama, kwani hamkuwa mmeweza: wala hatta leo hivi hamwezi; hatta leo wa mwili ninyi. Kwani ukiwa kwenu uwivu, na fitina, na kutengwa, si wa mwili ninyi, mkienda kwa watu? Mtu akisema, Mimi wa Paolo, na mwingine, Mimi wa Apollo, si ninyi wa watu tu?

Ni nani Paolo? nani Apollo? Wangoje, kwa hawa mmeamini; na killa mmoja alivyopewa na Bwana. Mimi nalipanda, Apollo akatia maji, Muungu ndiye anayesitawisha. Hivi apandaye si kitu, wala atiaye maji, illa Muungu asitawishaye.

Apandaye na atiaye maji mamoja: killa mtu atapewa ijara yake, kwa kazi yake yeye. Kwani twatenda pamoja na Muungu. Ninyi kilimo cha Muungu, wa Muungu ujengo. Kwa neema ya Muungu niliyopewa mimi, kama mwashi mkuu mwenyi akili, nimeweka misinji; mgine hujenga juu yao. Killa mtu aangalie ginsi ajengavyo. Msinji mwingine hawezi mtu kuweka illa uliowekwa, ndio Isa Masiya. Mtu akijenga juu ya msinji huu, thahabu, fetha, johari, miti, majani, manyassi, kazi yake killa mtu itakuwa thahiri: kwani siku ile itaweka thahiri, kwamba katika moto itafunuliwa; na kazi yake killa mtu ginsi yake moto ule utajaribu. Kazi ya mtu aliyojenga ikikaa, atapewa thawabu. Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara: mwenyewe ataokoka, illa ndivyo kama kwa moto.

Hamjui, kama hekalu la Muungu ninyi, na Roho yake Muungu akaaye ndani yenu? Mtu akiliharibu hekalu la Muungu, huyu ataharibika na Muungu. Kwani hekalu la Muungu ni takatifu, ndilo mlio ninyi. Mtu asijidanganye. Akijiona mwenyi hekima katika dunia hii, awe mpumbafu, apate kuwa na hekima. Kwani hekima ya ulimwengu huu ni upumbafu kwa Muungu. Kwani imeandikwa, Awanasaye wenyi hekima katika werevu wao; na tena, Bwana azijua fikara zao wenyi akili, ndizo ubatili tu.

Hivi asijisifu mtu kwa ajili ya watu. Kwani yote ni yenu: kama Paolo, kama Apollo, kama Kefa, kama dunia, kama uzima, kama kufa, kama yalipo, kama yatakayokuwa: yote yenu; nanyi wake Masiya; na Masiya wake Muungu.

- 4 MTU atuthanie kama watumishi wa Masiya na
 2 wasimamizi wa siri za Muungu. Illa tena, imewapasa
 3 wasimamizi mtu aonekane kuwa amini. Kwangu kido-
 go tu, nihukumie na ninyi, ama siku za watu, wala
 4 sijihukumu mwenyewe. Sijui neno kwangu; illa kwa
 5 hiyo sina haki: atakayenihukumu ni Muungu. Msi-
 hukumie neno mbele ya wakati wake, hatta ajapo
 Bwana, atakayemulika mafichoni mwa giza, atakaye-
 weka wazi mashauri ya moyoni; ndipo killa mtu
 atakapopata sifa zake kwa Muungu.
- 6 Haya, ndugu, nimetuandikia mimi na Apollo kwa
 ajili yenu; illi kwetu mjifunze msithanie kuliko yali-
 yoandikwa, msijivune mtu kwa ajili ya mmoja juu ya
 7 mgineo. Nani aliyekupambanukisha? Unayo nini
 usiyopewa? Kama umepewa, mbona wajisifu kama
 hukupewa?
- 8 Bassi sasa mmeshiba, sasa mmepata utajiri, pasipo
 sisi mmekuwa wafalme: laiti mngawa wafalme, sisi
 9 tupate kumiliki nanyi. Kwani, nathani, Muungu
 ametuonyesha sisi mitume mwishoni kama wafao, tu-
 10 tazamiwe na ulimwengu, na malaika, na watu. Sisi
 wapumbafu kwa sababu yake Masiya, ninyi wa akili
 katika Masiya; sisi thaifu, ninyi hodari; ninyi wa
 11 heshima, sisi wa aibu. Hatta saa hiyo twaona na njaa
 na kiu, tunao utupu na kupigwa, hatuna kwetu,
 12 tunalemewa tukitenda kazi kwa mikono yetu sisi. Tu-
 13 kishutumiwa twabarikia, tukifukuzwa twaombea, tuki-
 nenwa unajisi twaonya: tumekuwa kama taka za uli-
 mwengu, yaliyotupiwa ya yote, hatta sasa.
- 14 Siandiki haya kwa kutahayarisha, illa kama watoto
 15 wangu niwapendao nawakumbusha. Kwani kama
 mngekuwa na waalimu elfu katika Masiya, hamnao
 baba wengi; katika Masiya Isa kwa anjili ndimi nili-
¹⁶₁₇ yewazaa. Nawasihi ninyi mnifuate. Kwa hiyo na-
 limpeleka Timoteo kwenu, aliye mwana wangu nim-
 pendaye na amini katika Bwana, atakayewakumbusha
 njia zangu katika Masiya, kama po pote katika killa
 kanisa nifundishavyo.
- 18 Nisipokuja mwenyewe kwenu wangine wajivuna.
 19 Nitakuja upesi kwenu, Bwana akipenda, nitajua si neno
 20 lao waliojivuna, illa nguvu: kwani ufalme wa Muungu
 21 hauko katika neno illa katika nguvu. Mtakani,

nije kwenu na fimbo ao kwa kupenda, na rohoni mwa upole?

NASIKIA sana kwenu ni uzini, na uzini usionenwa hatta katika mataifa, mtu awe na mke wa babaye. Nanyi mmejivuna, wala hamkusikitika aondolewe katika kwenu aliyelitenda tendo hilo.

Kwani mimi nisipokuwako mwilini, nikiwapo rohoni, nimekwisha kuhukumu kama nikiwapo, atendaye hili, katika jina la Bwana wetu Isa Masiya, mkikusanyika ninyi na roho yangu, pamoja na nguvu ya Bwana wetu Isa Masiya, kumtoa huyu kwa Shetani, mwili upotee, illi roho ipate kuokoka siku ya Bwana Isa.

Kujisifu kwenu si kwema. Hamjui kama chachu iliyo ndogo huchacha machanganyiko yote? Takaseni chachu ya kwanza, mpate kuwa changanyiko jipya, kama msiochachwa. Kwani na Pasaka wetu ametolewa, ndiye Masiya: tufanye karamu, si kwa chachu ya kwanza, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, illa kwayo isiyochachwa ya kutakata na kweli.

Nimewaandikia katika waraka, msichanganyike na wazini: illa si hasa na wazini wa ulimwenguni, wala watamano, wala wevi, wala waabuduo sanamu: kama hivi, ingaliwapasa kutoka katika ulimwenguni. Sasa nimewaandikia msichanganyike, mtu aitwaye ndugu akiwa mzini, ama mtamani, ama mwabudu sanamu, ama mtukana, ama mlevi, ama mwivi; na mtu kama huyu hatta kwa kula naye. Nina amri gani niwahukumu walio 'nje? Ha'mwahukumu ninyi walio ndani? Walio 'nje Muungu awahukumu. Mtoeni aliye mbaya katika kwenu ninyi.

ATHUBUTU mtu wenu akiwa na neno juu ya mwenzake kuhukumiwa nao wasio na haki, wala si nao watakatifu? Ama hamjui kama watakatifu watahukumu ulimwengu? Ukiwa ulimwengu utahukumiwa nanyi, hamstahili hukumu zilizo ndogo? Hamjui kama tutahukumu malaika? sembuse mambo ya maisha hii? Mkiwa na hukumu za maisha hii, wasiokubalika katika kanisa, wekeni hawa. Nasema kwa aibu yenu. Hakuna kwenu mwenyi hekima hatta mmoja, awezaye kukata maneno ya ndugu zake? illa ndugu astakiane na ndugu, hatta kwao wasioamini?

Bassi sasa hatiya kabisa kwenu, mkiwa na mastaka ninyi kwa ninyi. Kwa nini afathali msithulumwiwe?

8 Kwa nini afathali msidanganyike? Lakini mwathulumu
 9 na mwadanganya, nao ndugu. Ama hamjui kama wathu-
 lumu hawatarithi ufalme wa Muungu? Msikose: wala
 wazini, wala makafiri, wala waasharati, wala wa kike,
 wala wafira, wala wanyang'anyi, wala watamano, wala
 10 walevi, wala watukanaji, wala wevi, ufalme wa Muungu
 11 hawataurithi. Na hao wenu walikuwa: illa mmeoshwa,
 illa mmetakasika, illa mmefanyiwa haki, katika jina la
 Bwana Isa, na katika Roho yake Muungu wetu.

12 Yote halali kwangu, illa yote si wájib. Yote halali
 13 kwangu, illa sitatumishwa na neno. Vyakula kwa
 tumbo, na tumbo kwa vyakula: naye Muungu atabati-
 lisha na hili na hivi. Mwili si kwa uzini, illa kwa
 14 Bwana; na Bwana kwa mwili. Muungu alimfufua
 15 Bwana, na sisi atatufufua kwa nguvu zake. Hamjui
 kama miili yenu ni viungo vyake Masiya? Bassi nitwae
 viungo vyake Masiya nivifanye viungo vya kahaba?
 16 Hasha! Hamjui kama aliyeungwa na kahaba ni mwili
 mmoja? Kwani asema, Wawili watakuwa mwili mmo-
 17 ja. Aliyeungwa na Bwana ni roho moja. Kimbieni
 18 uzini. Killa thambi afanyayo mtu 'nje ya mwili; azi-
 niye hufanya thambi juu ya mwili wake mwenyewe.
 19 Ama hamjui, kama mwili wenu hekalu yake Roho Mta-
 katifu aliyomo ndani yenu, mliyopewa na Muungu?
 20 Wala sinyi mali yenu; mmenunuliwa kwa thamani.
 Mtukuzeni Muungu kwa mwili wenu na roho yenu iliyo
 yake Muungu.

7 KWA mambo mliyoniandikia: Ni heri mtu asimguse
 2 mwanamke. Illa kwa sababu ya uzini, killa mume awe
 naye mke wake, na killa mke awe naye mume wake.
 3 Mume ampe mke yalivyompasa, na hivi mke ampe
 4 mume. Mke hauwezi mwili wake, illa mume; hivi na
 5 mume hauwezi mwili wake, illa mke. Msidanganyane,
 isipokuwa kwa kupatana kwa muhulla, mpate faragha
 kwa kuomba, mkajiane tena, Shetani asipate kuwajaribu
 6 kwa kukosa kujizuia kwenu. Haya nayanena kwa
 7 shauri, si kwa amri. Napenda watu wote wangekuwa
 kama mimi: illa killa mtu ana ukarimu wake kwa
 Muungu, huyu hivi na huyu hivi.

8 Nawaambia wasiooana na waliofiwa, wa heri wakae
 9 kama mimi. Illa wasipojiweza, waoane: afathali wao-
 ane kuliko kuwaka.

10 Nao waliokwisha oana nawaonya, si mimi, illa Bwana,

mke asifarakane na mumewe. Akifarakana, akae asio- 11
lewe, ao apatane na mumewe. Wala mume asimwache
mkewe.

Yaliyosalia nasema mimi, wala si Bwana. Ndugu 12
akiwa na mke asiyeamini, naye aona vema akae naye,
asimwache. Na mwanamke akiwa na mume asiyeamini, 13
naye aona vema akae naye, asimwache mumewe. Kwani 14
mume asiyeamini ametakaswa kwa mkewe, na mke asi-
yeamini kwa mumewe : illa watoto wenu tena hawanga-
litakata ; sasa watakatifu. Asiyeamini akifarakana, afa- 15
rakane : ndugu mume ao mke si mtumwa katika haya.
Mmeitwa ninyi na Muungu katika amani. Wajuaje, 16
mke, kama hutamwokoa mumeo ? Wajuaje, mume,
kama hutamwokoa mkeo ? Illa killa mtu alivyoga- 17
wanyikiwa na Bwana, killa mtu alivyomwita Muu-
ngu, hivi aendelee. Na hivi katika makanisa yote naa-
muru.

Mtu akiitwa ametahiriwa asijifanyie govi ; mtu ame- 18
itwa asipotahiriwa, asitahiriwe. Tohara si neno, wala 19
govi si neno, illa kuzishika amri za Muungu. Killa 20
mtu katika hali alivyoitwa, katika hiyo akae. Umeitwa 21
mtumwa ? usisikitike : hatta ukiweza kuwa huru, afa-
thali utwae. Kwani aliye katika Bwana akiitwa 22
mtumwa, ni huru wake Bwana. Hivi aliyeitwa huru
ni mtumwa wake Masiya. Mmenunuliwa kwa thamani ; 23
msiwe watumwa wa watu. Killa mtu, ndugu, alivyo- 24
itwa, hivi akae mbele ya Muungu.

Kwa mambo ya mabikira, sina amri ya Bwana : natoa 25
shauri kama niliyerehemewa na Bwana kuwa amini.
Naona iliyo heri kwa ajili ya shidda tuliyo nayo, kwa- 26
mba heri mtu awe hivi. Umefungwa kwa mke ? usi- 27
take kufunguliwa. Ukifunguliwa kwa mke, usitake
mke. Ukioa, huna thambi ; na bikira akioa hana 28
thambi. Hao watakuwa na mateso ya mwilini : mimi
nawaachilia.

Nisemalo, ndugu, ndilo, wakati unapunguka : yaliyo- 29
salia ndiyo, wanao wake wawe kama wasio nao ; waliao 30
kama wasiolia ; wafurahio kama wasiofurahi ; wanunua
kama wasiomiliki ; wautumiao ulimwengu huu kama 31
wasiotumia : kwani hupita namna ya ulimwengu huu.

Nataka msiwe na tunza. Asiyeoa huyatunza ya 32
Bwana, ampendezeje Bwana. Aliyeoa huyatunza ya 33

- 34 dunia, ampendezeje mkewe. Mke na bikira tena si mamoja. Asiyeolewa huyatunza ya Bwana, apate kuwa mtakatifu na mwili na roho. Aliyeolewa huyatunza ya
- 35 duniani, ampendezeje mume. Nasema haya kwa fayida yenu; nisiwategee kitanzi, lakini kwa kuwa heri na kumngojea Bwana pasipo kuchafuka.
- 36 Mtu akithani hamtendei vema bikira yake, majira yake ikipita, ikiwa kama ilivyopasa, afanye apendavyo;
- 37 hafanyi thambi: waoane. Aliye imara moyoni, pasipo shidda, akiweza tamaa zake, naye ameshika moyoni
- 38 kumlinda bikira yake, hutenda vema. Hivi aozaye hutenda vema; asiyeoza huzidi kutenda vema.
- 39 Mwanamke amefungwa kwa wakati akiwa mume wake hayi. Mumewe akilala, ni huru, aolewe naye
- 40 ampendaye, illa katika Bwana tu. Illakini yu heri akae alivyo, kwa shauri langu: nami nathani ninayo Roho yake Muungu.
- 8** KWA vitu vilivyotolewa kwa sanamu: Najua kama sisi wote tunayo elimu. Elimu huvuna, kupendana
- 2 hufaa. Mtu akithani amejua neno, hajajua kama ilivyo-
- 3 mpasa kujua; mtu akimpenda Muungu, huyu amejulika
- 4 naye. Kwa kuvila vilivyotolewa kwa sanamu, twajua kama sanamu si kitu cha ulimwenguni, na kama Muu-
- 5 ngu mwingine hapana illa mmoja. Kwani wakiwa walioitwa miungu, ama mbinguni ama katika inchi;
- 6 hatta wako miungu mingi na bwana wengi; kwetu Muungu mmoja, Baba, yote yametoka kwake, na sisi katika yake; na mmoja Bwana, Isa Masiya, kwa huyu yote, na sisi kwaye.
- 7 Illa wote hawana kujua: wangine, kwa kuikumbuka sanamu hatta sasa, wanakula vilivyotolewa kwa sanamu;
- 8 na ukumbuko wao ukiwa thaifu hutiwa unajisi. Chakula hakitupendezeshi kwa Muungu: wala tukila hatukuzidi, wala tusipokula hatukupunguka.
- 9 Angalieni uwezo wenu usiwe ukwazo kwao walio
- 10 thaifu. Kwani mtu akikuona wewe ujuaye umekaa kitako mahali pa sanamu, ukumbuko wake aliye thaifu hautathubutishwa avile vilivyotolewa kwa sanamu?
- 11 Naye aliye thaifu huharibika kwa kujua kwako, ndugu
- 12 aliyemfia Masiya. Hivi mkiwakosa ndugu, kuupiga ukumbuko wao ulio thaifu, Masiya ndiye 'mmkosaye.
- 13 Kwa hayo, chakula kikimchukizisha ndugu yangu,

sitakula nyama hatta milele, nisimchukizishe ndugu wangu.

MIMI si huru? Mimi si mtume? Sikumwona Isa 9
 Masiya Bwana wetu? Si ninyi kazi yangu katika 2
 Bwana? Kama si mtume kwa watu wangineo, illa 2
 kwenu ndimi: kwani muhuri ya utume wangu ndinyi 3
 katika Bwana. Jawabu yangu kwao waniuliziao ndilo 3
 hili.

Hatunao uwezo wa kula na kunywa? Hutunao 4
 uwezo kuchukua nasi ndugu mwanamke, kama mitume 5
 waliosalia, na nduguze Bwana, na Kefa? Ama mimi 6
 peke yangu na Barnaba hatunao uwezo tusitende kazi? 6

Nani aendaye kupigana kwa gharama yake yeye? 7

Nani apandaye mizabibu asiyekula matunda yao? 7

Nani achungaye kundi asiyekula ya maziwa ya kundi? 8

Nayanena haya kama mtu tu? illa na sheria haisemi 8

yaleyale? Kwani imeandikwa katika sheria ya Musa, 9

Usimfungue kanwa ng'ombe afikichaye. Ndio ng'ombe 9

tu awatunzao Muungu? illa kwa ajili yetu kabisa 10

amenena? Kwani kwa ajili yetu imeandikwa: kwamba 10

imempasa alimaye alime katika tumaini, naye afikichaye 11

katika tumaini la kushariki naye katika tumaini lake. 11

Kama sisi tumewapandia yaliyo ya rohoni, ni jambo 11

lililo kuu tukivuna sisi yenu ya mwilini? Wangine 12

wakisharikiana katika uwezo wenu, si sisi zayidi? 12

Illa hatukutumia uwezo huu; lakini twachukuliana 13

yote, tusiizuie anjili yake Masiya. Hamjui kama 13

wafanyao mambo ya dini wanakula ya hekalu? Wai- 14

ngojeao mathbahu washarikiana na mathbahu. Hivi 14

na Bwana ameamuru waihubirio anjili waruzukiwe kwa 14

anjili.

Mimi haya siyatumii. Sikuyaandika, iwe kwangu 15

hivi: ni heri nife, kuliko kutwaliwa na mtu kujisifu 15

kwangu. Nikihubiri anjili, hainipasi kujisifu: kwani 16

shidda juu yangu, ole wangu, nisipoihubiri. Nikii- 17

tenda kwa moyo nina thawabu; pasipo kwa moyo, 17

nimetiwa amri. Thawabu gani ninayo? Nikihubiri 18

nitoe anjili pasipo mshahara, nisiutumie uwezo wangu 18

ulio katika anjili.

Nikiwa huru katika watu wote nimejifanya mtumwa 19

wao wote, nipate kuwafayidia wengi. Nikawa kwa 20

Wayahudi kama Myahudi, niwafayidie Wayahudi; 20

kwao walio chini ya sheria kama chini ya sheria ; ni-
 21 wafayidie walio chini ya sheria ; kwao wasio na sheria
 kama sina sheria (nisipokuwa sina sheria ya Muungu,
 illa mwenyi sheria ya Masiya), niwafayidie wasio na
 22 sheria. Nalikuwa kwa thaifu, thaifu, niwafayidie
 thaifu. Kwa wote nimekuwa vyote, nipate kwa njia
 23 yote kuwaokoa. Nafanya yote kwa ajili ya anjili,
 nipate kusharikiana nayo.

24 Hamjui kama wapigao mbio katika washindanapo,
 wote wapiga mbio, mmoja hupewa brabio? Pigeni
 25 mbio ginsi hiyo, mpate kupokea. Killa ashindanaye
 hujizuia katika yote : nao hawa wapewe taji iozayo,
 26 illa ninyi isiyooza. Bassi mimi napiga mbio si kama
 27 asiyejua ; napigana si kama apigaye hewa : illa natiisha
 mwili, nautumikisha : isiwe niliyewahubiria wangine
 mwenyewe nipotee.

10 SITAKI, ndugu, mkose kujua kama baba zetu wote
 walikuwa chini yake wingu ; wote wakapita katika
 2 bahari ; wote wakabatizwa kwa Musa katika wingu na
 3 katika bahari ; wote wakala chakula kilekile cha roho ;
 4 wote wakanywa kinywa kilekile cha roho : kwani wa-
 kanywa katika mwamba ule wa rohoni uliowafuata :
 nao mwamba ndio Masiya.

5 Lakini nao wote hakupendezwa Muungu ; wakaa-
 ngamia katika jangwa.

6 Haya yalikuwa kwa dalili kwenu, illi tusiwe sisi
 7 watamani vibaya, kama wale walivyotamani. Wala
 msiwe waabudu sanamu kama wangine wao ; ilivyoa-
 ndikwa, Wakakaa kitako watu kula na kunywa, wakao-
 8 ndoka wacheze. Wala tusizini kama wangine wao
 walivyozini, wakaanguka siku moja asharini na tatu
 9 elfu. Wala tusimjaribu Masiya kama wangine wao
 walivyojaribu, wakaharibiwa nao majoka.

10 Wala msinung'unike kama wangine wao walivyo-
 11 nung'unika, wakaharibiwa na mharibu. Haya yote
 yakawapata kwa dalili ; yakaandikwa kwa kuelimishwa
 12 sisi tuliojiwa na utimilifu wa zamani. Hivi ajithaniye
 amesimama aangalie asianguke.

13 Jaribu halikuwapata illa la kadiri ya mwana Adamu.
 Muungu amini, asiyeacha mjaribiwe ninyi kuliko 'mwe-
 zavyo, lakini atafanya pamoja na jaribu pa kutokea,
 'mweze kustahimili.

Kwa ajili hiyo kimbilieni ibada ya sanamu. Nasema ¹⁴/₁₅ kama kwao wanao akili: mfikiri ninyi niyanenayo.

Kikombe cha mbaraka tukibarikicho sicho usharika 16 wa damu yake Masiya? Mkate tuuvunjao sio usharika wa mwili wake Masiya? Kwamba mkate mmoja, 17 mwili mmoja, sisi walio wengi: kwani wote twagawanyikia ya mkate ule mmoja. Angalieni Israeli wa 18 mwili: si wote walao thabihu washariki na mathbahu? Nisemeje tena? kwamba kilichotolewa kwa sanamu ni 19 kitu? ao kwamba sanamu ni kitu? Lakini wavitoavyo 20 mataifa, watoa kwa pepo, wala si kwa Muungu: sitaki ninyi msharikiane na pepo. Ha'mwezi kunywa ki- 21 kombe cha Bwana na kikombe cha pepo: ha'mwezi kugawanyikiwa meza ya Bwana na meza ya pepo. Ama 22 tumtie Bwana uwivu? sisi hodari kuliko yeye?

Yote halali, illa yote si wájib. Yote halali, illa yote 23 hayana fayida. Mtu asikumbuke yaliyo yake tu, illa 24 yaliyo ya wangineo.

Killa kilichouzwa sokoni mle, msipoulizia kwa ajili 25 ya thamiri; kwani, Inchi ni yake Bwana, nayo ijaayo. 26 Mtu wa makafiri akiwaita, nanyi mmependa kwenda, 27 killa kilichowekwa mbele yenu mle, msipoulizia kwa ajili ya thamiri. Illa mtu akiwaambia, Hiki kime- 28 tolewa kwa sanamu, msile, kwa ajili yake aliyewakumbusha, na kwa ajili ya thamiri (kwani, Inchi ni yake Bwana, nayo ijaayo): kwa thamiri, nasema, si yenu 29 ninyi, illa yake mgineo.

Kwa nini uhuru wangu uhukumiwe kwa thamiri yake mgineo? Nikitwaa sehemu katika neema, mbona 30 ninenwe unajisi kwa ajili yake nishukuriacho? Mkila, 31 mkinywa, mkitenda neno lo lote, mtende yote kwa utukufu wake Muungu. Msichukize, wala Wayahudi, 32 wala Wayonani, wala kanisa la Muungu: kama nami 33 nawapendeza wote kwa mambo yote, nisitake fayida yangu mimi illa yao wote, wapate kuokoka.

MNIFUATE mimi kama mimi namfuata Masiya. **11** Nawasifu ninyi kwamba nilivyowatolea mwayashika 2 yaliyotolewa. Nataka mjue kama kitwa cha killa 3 mume ni Masiya; kitwa cha mke ni mume; kitwa cha Masiya ni Muungu.

Killa mume akisali ao akitoa unabii kitwa kisipo 4 kiwazi, huaibisha kitwa chake. Killa mke akisali, 5

- akitoa unabii, kitwa kisipofunikwa huaibisha kitwa chake: kama ni mamoja naye yule aliyekatika nyele.
- 6 Mke asipofunikwa anyolewe tena. Illa ikiwa unyonge
7 mke akatike nyele ao anyolewe, afunikwe. Mume
haimpasi kufunikwa kitwa, akiwa mfano na sifa ya
8 Muungu. Mwanamke ni sifa ya mume. Kwani asili ya
9 mume si katika mke, illa mke katika mume. Kwani
mume hakuumbwa kwa ajili ya mke, illa mke kwa ajili
10 ya mume. Kwa hiyo imempasa mke awe na uwezo
11 kitwani, kwa ajili ya malaika. Illa tena si mke pasipo
12 mume, wala mume pasipo mke, katika Bwana. Kwani
kama asili ya mke katika mume, hivi mume kwa mwa-
13 namke; na yote asili yao kwa Muungu. Fikirini
kwenu ninyi: kuzuri mwanamke amsalie Muungu asi-
14 pofunikwa? Hatta asili tena siyo iwafundishayo, kwani
15 mume akiwa na nyele nyingi haina heshima, mwanamke
akiwa na nyele nyingi ni sifa yake? kwani amepewa
16 nyele kwa mavazi. Mtu akitaka kufanya fitina, sisi ha-
tunayo desturi kama hiyo, wala makanisa ya Muungu.
- 17 Nikitoa neno hili, si kwa kusifu, kwamba si kwa
18 vema illa kwa vibaya mwakusanyika. Kwani mkiku-
sanyika ninyi katika kanisa, nasikia kuna kutengwa
19 kwenu; nami sehemu nasadiki: kwani haina buddi kuwa
uzushi kwenu, waliokubalika kwenu wapate kuonekana.
- 20 Mkikusanyika kwa hiyo, siyo kula chakula cha
21 Bwana. Kwani killa mtu hutangulia kutwaa chakula
chake katika kula; mmoja ana njaa, mmoja amelewa.
- 22 Hamnazo nyumba za kulia na kunywea? ao mmetharau
kanisa la Muungu, mkawatia haya wasio nazo? Ni-
waambieje? niwasifu kwa haya? Siwasifu.
- 23 Kwani mimi nikapokea kwa Bwana, nilivyowatolea
ninyi, kwamba Bwana Isa, usiku ule alipotolewa, aka-
24 twaa mkate, akashukuru, akavunja, akanena, Twaeni,
leni: huo ndio mwili wangu, uvunjikao kwa ajili yenu:
25 fanyeni hayo kwa ukumbusho wangu. Vivihivi na
kikombe baada ya kula, akinena, Hiki ni kikombe cha
agano jipya katika damu yangu: fanyeni haya, killa
26 mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Kwani killa mlapo
mkate huu, na kikombe mnywapo, mwaonyesha kufa
kwake Bwana, hatta atakapokuja.
- 27 Hivi alaye mkate huo, ao anywaye kikombe hicho,
asipostahili, amehukumiwa ya mwili na damu ya

Bwana. Mtu ajiamue mwenyewe, hivi akaule mkate, 28
 akakinywe kikombe. Kwani alaye na anywaye asipo- 29
 stahili, hula na hunywa hukumu yake yeye, asipopa-
 mbanua mwili wa Bwana. Kwa sababu hiyo kwenu 30
 wengi walio thaifu na wagonjwa, na katháwakatha
 wamelala. Tukijihukumia, hatuhukumiwi. Tukihu- ³¹/₃₂
 kumiwa na Bwana, twaelimishwa, tusihukumiwe mbali
 pamoja na dunia.

Hivi, ndugu zangu, mkikusanyika kula, mkari- 33
 bishane. Mtu akiwa na njaa, ale nyumbani; msiingie 34
 pamoja katika kuhukumiwa. Nayo yaliyosalia nitaya-
 tengeneza nitakapokuja.

KWA mambo ya roho, ndugu, sitaki mkose kujua. 12
 Mwakumbuka kama mlikuwa wamataifa, mkachukuliwa 2
 kwa sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa. Kwa 3
 hiyo nawaarifu kama hapana mtu asemaye katika Roho
 ya Muungu amnenaye Isa anathema, wala hawezi mtu
 kumnena Bwana Isa isipokuwa katika Roho Mta-
 katifu.

Kuna tofauti ya makarimu, illa Roho ni moja; 4
 na tofauti ya kazi, na Bwana mmoja; na tofauti ⁵/₆
 ya kutenda, illa Muungu mmoja atendaye yote ka-
 tika watu wote. Killa mtu amepewa wonyesho wa 7
 Roho kwa fayida. Huyu kwa Roho amepewa neno la 8
 hekima; mwingine neno la elimu, kwa Roho ileile;
 mwingineo imani, kwa Roho ileile; mgine makarimu 9
 ya kuponya, kwa Roho ileile; mwingine uwezo wa 10
 nguvu; mwingine unabii; mwingine kuzipambanua
 roho; mwingineo ginsi za lugha; mwingine tafsiri
 ya lugha. Haya yote huyatenda Roho moja ileile, 11
 akiwagawanyia killa mtu peke yake kama apendavyo.

Kwani kama mwili ni mmoja, na viungo vyake vingi, 12
 na viungo vyote vya mwili, vikiwa vingi, ni mwili
 mmoja, hivi na Masiya. Kwani kwa Roho moja sisi 13
 wote tumebatizwa katika mwili mmoja, kama Waya-
 hudi, kama Wayonani, kama watumwa, kama huru;
 na wote tumenyweshwa katika Roho moja. Kwani na 14
 mwili si kiungo kimoja, illa vingi. Mguu ukisema, 15
 Kwamba mimi si mkono, si wa mwili, kwa hiyo sio wa
 mwili? Sikio likisema, Kwamba mimi si jicho, si wa 16
 mwili, kwa hiyo silo la mwili? Mwili wote ukiwa 17
 jicho, ku wapi kusikia? Kama wote kusikia, ku wapi
 kunusa? Sasa Muungu ameweka viungo, killa kimoja 18

- 19 chao, katika mwili, kama alivyopenda. Kama wote
 20 ungekuwa kiungo kimoja, mwili u wapi? Sasa viungo
 21 vingi na mwili mmoja. Haliwezi jicho kuuambia
 mkono, Hunifai: wala tena kitwa miguu, Hamnifai.
 22 Lakini zayidi sana viungo vya mwili vilivyothaniwa
 23 uthaifu vyahitajiwa; navyo vya mwili vilivyothaniwa
 havina heshima, hivi twazidi kuviheshimia, navyo
 24 visivyo vizuri vimezidi kuwa na uzuri. Vizuri vyetu
 havihitaji. Lakini Muungu ameutengeneza mwili,
 25 akizidi kukipa heshima kilichopunguka, pasiwe fitina
 26 katika mwili, lakini viungo vitunzane: hatta kiungo
 kimoja kikiumwa, viungo vyote viume nacho; kiungo
 kimoja kikitukuzwa, viungo vyote vifurahi nacho.
 27 Ninyi ni mwili wake Masiya, na viungo mmoja mmoja.
 28 Wangine Muungu amewaweka kanisani, kwanza
 mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, tena nguvu,
 na tena makarimu ya kuponya, kusayidia, kutawala,
 29 lugha hizi na hizi. Wote mitume? wote manabii?
 30 wote waalimu? wote wa nguvu? wote wanayo maka-
 rimu ya kuponya? wote wanena lugha? wote wafasiri?
 31 Takeni sana makarimu yaliyo mema. Hatta baadaye
 nawaonya njia iliyo bora.
- 13** NIKINENA lugha za watu na za malaika, nisipoku-
 wa na upendano, nimekuwa shaba iliayo, na upato uvu-
 2 mao. Nikiwa na unabii, nikijua na siri zote, na elimu
 yote, nikiwa tena na imani yote hatta kuhamisha milima,
 nisipokuwa na upendano, sikuwa kitu.
- 3 Hatta nikipokwani mali yangu yote, hatta nikijitoa
 mwili niliwe na moto, nisipokuwa na upendano, sifai neno.
 4 Upendano hustahimili, hufanikia; upendano hauna
 5 hasidi; upendano hauna makuu, haujivuni, haukosi
 adabu, hautaki yaliyo yake, haukasiriki, haufikiri
 6 maovu, haufurahishwi pasipo haki, hufurahiwa na kweli,
 7 huvumilia yote, huamini yote, hutaraja yote, huchukua
 8 yote. Upendano haupunguki po pote. Kama unabii
 utakwisha; kama lugha, zitakoma; kama elimu, ita-
 9 kwisha. Kwani twajua kwa sehemu tu, kwa sehemu
 10 twafanya unabii; iliyo kamilifu ikija, iliyo kwa sehemu
 11 itakwisha. Nilipokuwa mtoto, nalinena kwa kitoto,
 nalifikiri kwa kitoto, nikafahamu kwa kitoto; hatta
 12 nilipokuwa mzima, nikaziweka za kitoto. Kwani sasa
 twaona katika kioo kwa fumba; wakati ule uso kwa
 uso. Sasa twajua kwa sehemu; wakati ule tutajua sa-

na, kama tulivyojuliwa. Bassi zimesalia imani, tumaini, 13
upendano, hizi tatu; iliyo kuu yao ndiyo upendano.

FUATENI upendano; takeni sana amri za Roho, na 14
kwanza mfanye unabii.

Kwani anenaye lugha, hasemi na watu, illa na Muungu; 2
hakuna asikiaye; akiwa rohoni anasema siri. Afanyaye 3
unabii husema na watu, kuwajengea, kuwafariji, kuwatia
moyo. Anenaye lugha hujijengea mwenyewe; afanyaye 4
unabii hulijenga kanisa. Nataka ninyinyote msemelugha, 5
illa afathali mfanye unabii; kwani afanyaye unabii ni
mkuu kuliko asemaye lugha, asipokuwa afasiri, kanisa
wapate kujengewa.

Bassi, ndugu, nikija kwenu ninasema lugha, nitawafaa 6
nini nisipokuwa ninasema kwa ufunuo, ao kwa hekima,
ao kwa unabii, ao kwa fundisho?

Kama yasiyo hayi yatoayo sauti, kama filimbi, kama 7
kinubi, kisipotoa uvumi uliopambanuka, nani atakayejua
iliyopigwa kwa filimbi, ao kwa kinubi? Baragumu 8
ikitoa sauti isiyojulikana, nani atakayejifanya tayari
apigane? Hivi na ninyi, msipotoa kwa lugha neno lililo 9
wazi, lililonenwa lipateje kujulikana? Mtakuwa msemao
katika hewa tu.

Labuda sauti hizi nyingi ziko ulimwenguni, wala ha- 10
pana isiyo sauti. Bassi nisipojua nguvu yake sauti nita- 11
kuwa mshenzi kwake asemaye, naye asemaye atakuwa
mshenzi kwangu. Hivi na ninyi, mkitaka kuwa wa 12
rohoni, takeni kulijengea kanisa, mpate kuzidi. Kwa 13
hiyo asemaye lugha, aombe afasiri. Nikiomba kwa lugha, 14
roho yangu huomba, akili zangu hazitoi neno. Nini 15
tena? Nitaomba kwa roho, nitaomba tena kwa akili:
nitakwimba kwa roho, nitakwimba tena kwa akili. Uki- 16
barikia kwa roho, akaaye mahali pa mjinga asemeje
Amina kwa kushukuru kwako, akiwa hajui usemavyo?
Wewe washukuru vema, illakini mwingineo hajengewi. 17

Namshukuru Muungu, nasema lugha kuliko ninyi 18
nyote: lakini katika kanisa napenda kusema maneno 19
matano kwa akili zangu, wangine wasikie, kulikomaneno
elfu kwa lugha. Ndugu, msiwe watoto kwa akili: kwa 20
uovu 'mwe watoto, kwa akili 'mwe wazima.

Katika torati imeandikwa, Kwa lugha zinginezo na 21
kwa midomo ingineyo nitasema na watu hawa; wala
hivi hawataniisia, amenena Bwana.

22 Hatta hivi lugha ni ishara, si kwao waaminio, illa kwao wasioamini: unabii si kwao wasioamini, illa kwao waaminio.

23 Kama kanisa lote limekusanyika pamoja, wote wakisema lugha, wakiingia walio wajinga ao wasioamini, hawasemi kama mna wazimo? Illa wote wakitoe unabii, akiingia mmoja asiyeamini, ao mjinga, ashawishwa na wote, ahukumiwa na wote; siri za moyoni mwake zimekuwa wazi; hatta akianguka usoni amwambudu Muungu, akieneza kama kweli Muungu kwenu.

26 Nini tena, ndugu? Mkikutana, killa wenu ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Yote yawe kwa kujengea. Mtu akisema lugha, wawili kwa wawili, ao wakiwa wengi watatu, na kwa zamu; mmoja afasiri. Asipokuwako mfasiri, anyamaze kanisani, aseme na mwenyewe na Muungu. Manabii wanene wawili ama watatu, wangine wapambanue. Mgine akaaye kitako akifunuliwa, wa kwanza anyamaze. Mwaweza kutoa unabii wote mmoja mmoja, wote wapate kujifunza, wote wapewe moyo. Na roho za manabii zawatii manabii. Muungu siye wa kuasi, illa wa amani; kama katika makanisa yote ya watakatifu.

34 Waanaake wenu wanyamaze kanisani: hawana ruksa kunena; illa watii, kama inenavyo sheria. Wakitaka kujifunza neno, waulize nyumbani waume wao: ni aibu ya waanaake kunena kanisani.

36 Neno la Muungu limetoka kwenu? ao limewafikia ninyi peke yenu? Mtu akijiona nabii ao wa roho, ayatambue niaandikayo, kama ndiyo amri yake Bwana.

38 Asiyejua, asijue.

39 Hivi, ndugu, takeni kufanya unabii, na kusema lugha msikataze. Yote yawe yametengeneka na kwa taratibu.

15 NAWAKUMBUSHA, ndugu, anjili niliyowahu-
2 biria, mkaipokea, katika hiyo mwasimama, kwa hiyo mtaokoka, mkishika neno tulilowahubiria, isipokuwa mmeamini burre.

3 Kwani naliwatolea kwanza niliyoipokea, kama Masiya
4 alikufa kwa ajili ya thambi zetu kwa maandiko; akazi-
5 kwa; akaondoka siku ya tatu kwa maandiko; akaone-
6 kana na Kefa; tena nao wathenashara; baadaye akaonekana na zayidi ya ndugu hamsi mia pamoja, wengi wao

waliopo hatta leo, wangine wamelala; baadaye akaone- 7
kana na Yakobo; tena na mitume wote; baada yote, 8
kama naye asiyezaliwa wakati wake, akaonekana na
mimi. Kwani mimi ni mdogo wa mitume, nisiye na 9
haki kuitwa mtume, kwani nimelifukuza kanisa la
Muungu. Kwa neema ya Muungu nimekuwa nilivyo. 10
Wala neema yake iliyo kwangu siyo burre; illa nime-
zidi kutenda kazi kuliko wao wote: wala si mimi, illa
neema ya Muungu iliyo nami. Kama mimi, kama wale, 11
hivi tulivyohubiri, na hivi mkaamini.

Masiya akihubiriwa kama amefufuka katika wafu, 12
wasemaje wangine wa kwenu kama hapana kiyama ya
wafu? Kama hapana kiyama ya wafu, wala Masiya 13
hakufufuka: kama Masiya hakufufuka, habari zetu 14
hazifai, wala imani yenu haifai. Tumeonwa washu- 15
huduo uwongo wa Muungu: kwani tumeshuhudu ya
Muungu kama amemfufua Masiya, asiyemfufua kama
wafu hawafufuki. Kwani kama wafu hawafufuki wala 16
Masiya hakufufuka: kama Masiya hakufufuka imani 17
yenu haina maana; hatta sasa 'm katika thambi zenu.
Nao waliolala katika Masiya wamepotea. Kama katika 18
maisha hii tu tunalo tumaini katika Masiya, masikini 19
sisi kuliko watu wote.

Lakini sasa Masiya amefufuka katika wafu, wa kwa- 20
nza wao waliolala. Kwani kufa kukiwa kwa mtu, kwa 21
mtu tena kiyama ya wafu. Kwani kama katika Adamu 22
wote hufa, hivi na katika Masiya wote hupata uzima.
Killa mmoja mahali pake: wa kwanza Masiya; baadaye 23
walio wake Masiya, atakapokuwapo yeye. Tena 24
mwisho, atakapotoa ufalme kwa Muungu na Baba;
atakapokomesha mamlaka yote na uwezo wote na
nguvu. Kwani imempasa amiliki, hatta atakapokwisha 25
weka maadui wote chini ya miguu yake. Adui wa 26
mwisho atakayekoma ni kufa: kwani, Ametiisha vyote 27
chini ya miguu yake. Akisema vyote vitatiishwa
chini, ni thahiri kama sivyo yeye atiishaye vyote chini
yake. Hatta vyote vikitiishwa chini yake, ndipo naye 28
Mwana atatiishwa chini yake atiishaye vyote, illi
Muungu awe yote katika yote.

Ama watafanya nini waliobatizwa kwa ajili ya wafu, 29
kama wafu hawafufuki kabisa? Kwa nini wabatizwa 30
kwa ajili yao? Kwa nini nasi tunayo hatari saa zote?

- 31 Killa siku nafa; naitia kujisifu kwenu, niliko nako katika
 32 Masiya Isa Bwana wetu. Nikiwa kwa mwana Adamu
 nimepigana na nyama wakali katika Efeso, kunifaa
 nini, wafu wasipofufuka? Tule tukanywe, kwani kesho
 33 kufa. Si koseni: Desturi njema huharibika na mazu-
 34 mgunzo mabaya. Amkeni kwa haki, msitende thambi;
 kwani wangine hawamjui Muungu: nanena haya kwa
 maana yenu.
- 35 Lakini mtu atasema, Wafufukaje wafu? katika
 36 mwili gani waja? Huna akili, wewe: uzipandazo
 37 hazimezi zisipokufa: uipandayo sio mwili utakaokuwa,
 38 illa mbegu tupu, ikiwa ngano ao ingineyo yote; lakini
 Muungu huipa mwili kama apendavyo, na killa uzao
 39 mwili wake yeye. Nyama yote si nyama moja: lakini
 ngine ya watu, ngine nyama ya ng'ombe, ngine ya
 40 ndege, ngine ya samaki. Na miili ya mbinguni, na
 miili ya duniani: lakini sifa yao ya mbinguni mbali,
 41 na ya duniani mbali. Sifa ya jua mbali, na sifa ya
 mwezi mbali, na sifa ya nyota mbali; kwani nyota na
 42 nyota mbali kwa sifa zao. Hivi na kiyama ya wafu.
 43 Wapandwa katika kuharibika, wafufuka pasipo kuha-
 ribika; wapandwa katika unyonge, wafufuka katika utu-
 kufu; wapandwa katika uthaifu, wafufuka katika ngu-
 44 vu; wapandwa mwili wa kuwa hayi, wafufuka mwili wa
 45 roho. Mwili uko ulio hayi, uko nao wa roho. Hivi
 ikaandikwa, Mtu wa kwanza Adamu alikuwa mtu hayi;
 46 Adamu wa mwisho, roho ifanyayo hayi. Lakini si
 47 kwanza wa roho, illa hayi; baadaye wa roho. Mtu wa
 kwanza katika inchi, wa udongo; mtu wa pili Bwana
 48 katika mbinguni. Kama huyu wa udongo, hivi nao
 wa udongo; kama yule wa mbinguni, hivi nao wa
 49 mbinguni. Na kama tumechukua mfano wake wa
 udongo, tutachukua na mfano wake wa mbinguni.
- 50 Nisemayo ni hayo, ndugu, kama nyama na damu
 haziwezi kurithi ufalme wa Muungu, wala uharibifu
 51 haurithi yasiyoharibika. Angalia, nawaambia siri:
 52 Wote hatutalala; wote tutabadilika, marra moja, jicho
 likifumbuka, paanda la mwisho: kwani paanda litalia, na
 wafu watafufuka pasiwe uharibifu, na sisi tutabadilika.
- 53 Kwani imeupasa uharibifu huu uvae usioharibika, nao
 54 huu wa kufa uvae usiokufa. Uharibifu huu utakapovaa
 usioharibika, na wa kufa huu utakapovaa usiokufa, ndipo

litakapokuwa neuo lililoandikwa, Kufa kumemezwa
na kushinda. Ku wapi, ee kufa, kuuma kwako? Ku 55
wapi, ahera, kushinda kwako? Kuuma kwa kufa ni 56
thambi, na nguvu za thambi ni sheria. Muungu ashu- 57
kuriwe, atupaye kushinda kwa Bwana wetu Isa Masiya.

Hivi, ndugu niwapendao, 'mwe imara, msiotikisika, 58
mkizidi katika kazi ya Bwana siku zote, mkijua kama
taabu yenu si burre kwa Bwana.

KWA mambo ya sadaka za watakatifu, kama nili- 16
vyoamuru makanisa ya Galatia, hivi na ninyi mfanye.
Siku ya kwanza ya juma killa wenu aweke akiba kwake 2
mwenyewe, kama alivyofanikiwa, sadaka zisifanyike
mimi nijapo tu. Nitakapokuwako, mtakaowaagiza 3
kwa nyaraka nitawapeleka wachukue neema yenu hatta
Yerusalemi; nami ikistahili niende na mimi, watasafiri 4
pamoja nami.

Nitakuja kwenu nitakapopita katika Umakedoni: 5
kwani napita kwa Umakedoni. Kwenu labuda nitakaa, 6
hatta wakati wa tháruba upite, mpate kunipeleka tena
nisafiriko. Sipendi kuwaona ninyi kama katika kupita 7
tu; kwani nataraja kukaa wakati kwenu, Bwana akija-
lia. Nakaa katika Efeso hatta Pentekote; nimefunu- 8
liwa mlango mkubwa na wa nguvu, nao maadui wengi. 9

Akija Timoteo, angalieni awe kwenu pasipo hofu; 10
kwani aitenda kazi ya Bwana kama na mimi: mtu asi- 11
mtharau. Mpelekeni mbele katika amani, apate kuja
kwangu: kwani namtazamia pamoja nao ndugu.

Kwa mambo ya Apollo aliye ndugu, nalimsihi sana 12
aje kwenu pamoja nao ndugu: illa kabisa hakupenda
kuja sasa; atakuja atakapoona nafasi.

Kesheni, simameni katika imani, 'mwe waume, 'mwe 13
hodari. Mambo yenu yote yawe katika kupendana. 14

Nawasihi, ndugu (mwawajua nyumba ya Stefana, 15
kama ndiyo ya kwanza ya Akaya, nao wamejitia katika
kuwangojea watakatifu), 'mwatii walio kama hawa, 16
naye yote atendaye nao, naye afanyaye kazi. Nimefura- 17
hiwa na kuwako kwao Stefana na Fortunato na Akaiko:
hawa wametimiliza upungufu wenu. Wametupum- 18
zisha roho, mimi na ninyi. Waangalieni walio kama
hawa.

Makanisa ya Asia wawasalimia. Akula na Priskilla 19
wawasalimia sana katika Bwana, pamoja na kanisa

20 waliomo nyumbani mwao. Ndugu wote wawasalimia. Msalimiane kwa busu takatifu.

²¹ Salaamu kwa mkono wangu mimi Paolo. Asiyem-
²²penda Bwana Isa Masiya, awe anathema. Maran atha.

²³ Neema ya Bwana Isa Masiya pamoja nanyi. Upendo
²⁴wangu pamoja na ninyi nyote katika Masiya Isa. Amin.

WARAKA WA PILI WA PAOLO MTUME

KWA

WAKORINTI.

- 1 PAOLO, mtume wa Isa Masiya kwa mapenzi ya Muungu, na Timoteo aliye ndugu, kwa kanisa lake Muungu liliko Korinto, pamoja nao watakatifu wote
- 2 walioko katika Akaya yote : Neema kwenu na amani kwa Baba wetu na Bwana Isa Masiya.
- 3 Abarikiwe Muungu na Baba wa Bwana wetu Isa Masiya, Baba wa rehema, na Muungu wa faraja yote,
- 4 atufarijiye katika shidda zetu zote, tupate kuweza kuwafariji walio katika shidda yote, kwa faraja tuliyo-
- 5 farajika na Muungu. Kama mateso ya Masiya kwa sisi yalivyozidi, hivi kwa Masiya nazo faraja zetu zika-
- 6 zidi. Tukiwa katika shidda, ni kwa ajili ya faraja yenu na wokovu, ufanyao kazi yake katika kustahimili mateso yaleyale tulivyoteswa sisi ; ama tukifarajika,
- 7 ni kwa ajili ya faraja na wokovu wenu. Na tumaini letu imara juu yenu, tukijua kama mlivyoshariki katika mateso, hivi na katika faraja.
- 8 Kwani hatupendi, ndugu, msijue shidda zetu zilizo-tupata katika Asia, kama tumelemewa sana kuliko
- 9 nguvu, hatta tukakata tamaa ya kuishi. Lakini tume-hukumiwa sisi tufe, tusijiamini nafsi zetu, illa Muungu
- 10 awafufuaye wafu : aliyetuokoa sisi katika mauti ile,

aokoaye; ndiye tumwaminiye ataokoa tena; mkisayidia 11
ninyi pamoja nasi kwa kuombea; ukarimu wetu ulio
kwa watu wengi ushukuriwe na wengi kwa ajili yetu.

Kwani kujisifu kwetu ndiyo, ushahidi wa moyo 12
wetu, kama pasipo hila na kwa moyo mbele ya Muungu,
si kwa hekima ya mwilini, lakini kwa neema ya Muungu,
tunakwenda ulimwenguni, na juu yote kwenu. Kwani 13
hatuwaandikii illa mliyosoma mkatambua, nataraja
kama hatta mwisho mtatambua: kama mlivyotutambua 14
kwa sehemu, kama sisi kujisifu kwenu, kama na ninyi
kwetu, siku ile ya Bwana Isa.

Na katika tumaini hili nalitaka kwanza kuja kwenu, 15
mpate neema ya pili; na kwa ninyi kuupitia Umake- 16
doni, na tena katika Umakedoni kuja kwenu, na kupe-
lekwa nanyi hatta Uyahudi. Nikitaka haya nimekuwa 17
na hafifu? ao niliyoyataka nimetaka kwa mwili, niwe
mimi na ndiyo ndiyo, na sivyo sivyo?

Muungu amini, neno letu lililo kwenu si ndiyo ndiyo 18
na sivyo sivyo. Mwana wake Muungu, Isa Masiya, 19
aliyehubiriwa kwenu nasi, na mimi na Sulwano na
Timoteo, hakuwa ndiyo na sivyo, lakini katika yeye
imekuwa ndiyo. Ahadi za Muungu zote katika yeye 20
ndiyo: kwa yeye Amina, kwa Muungu kwa utukufu
kwa sisi. Atufanyaye imara na ninyi kwa Masiya, 21
naye atutiaye mafuta, ni Muungu, aliyetulia tena 22
muhuri, naye atoaye arabuni ya Roho katika mioyo
yetu.

Namwitia Muungu kuwa shahidi juu ya maisha 23
yangu, kama kuwaachilia sijaja Korinto bado: si kama 24
ningetawala imani yenu, lakini sisi watendao nanyi kwa
furaha yenu: kwani kwa imani mwasimama.

NALITHANI hivi moyoni, nisiwajie tena huzunini. 2
Kwani mimi nikiwatia huzuni, nani anifurahishaye, 2
asipokuwa aliyehuzunishwa nami? Nikaandika yale- 3
yale, nisitiwe huzuni nijapo nao waliopaswa kunifurahi-
sha; nikawatumainia ninyi nyote, kama furaha yangu
ni yenu wote. Kwani katika shidda nyingi na taabu 4
ya moyoni nikawaandikia kwa machozi mengi; si kwa
kusudi mhuzunike, illa mapenzi myajue niliyo nayo
sana kwenu.

Mtu akihuzunisha, hakunihuzunisha mimi, illa kwa 5
sehemu, nisiwalemeze ninyi nyote. Imemtosha huyu 6

- 7 athabu aliyotiwa na wengi : hatta sivyo sasa, afathali kusamehewa na kufarajika, asipotee huyo kwa wingi wa huzuni.
- 8 Kwa hiyo nawaonya ninyi mfanye imara mapenzi
9 kwake. Kwani nikaandika kwa ajili hii, nijue mkijari-
10 biwa kama watayi ninyi kabisa. Mtakayomsamehe mtu, na mimi : kwani nimesamehe niyasameheyo kwa
11 ninyi, kama ningalikuwa Masiya ; tusifayidiwe na She-
tani : kwani hila zake tumezijua.
- 12 Nikija Troa kwa anjili yake Masiya, mlango ukini-
13 funuliwa katika Bwana, sikuwa na raha rohoni mwangu, nisipomwona Tito ndugu yangu : lakini nikaagana nao, nikaja Umakedoni.
- 14 Muungu ashukuriwe, aliyetushangiliza sikuzote ka-
tika Masiya, aonyeshaye mahali pote kwa sisi manuka
15 ya elimu yake : ya kwamba manukato ya Masiya sisi,
16 katika kwao wanaookoka na kwao wanaopotea ; kwa hawa manuka ya kufa kwa kufa, kwa hawa manuka ya uzima kwa uzima.
- 17 Nani atoshaye haya ? Kwani sisi si kama wengi, waghoshio neno lake Muungu : illa kama kwa moyo safi, kama kwa Muungu, inbele yake Muungu, twanena katika Masiya.
- 3** TWAANZA tena kujisifu wenyewe, tusipotumia, kama wangine, barua za sifa kwa ninyi ao katika
2 kwenu ? Barua yetu ni ninyi, iliyoandikwa moyoni
3 mwetu ; imejulika ikasomwa na watu wote, mkithihirishwa kuwa barua ya Masiya iliyongojewa na sisi, isiyoandikwa kwa wino, illa kwa Roho yake Muungu aliye hayi ; si katika mabamba ya mawe, illa katika mabamba ya nyama ya moyoni.
- ⁴ Tumaini hili tunalo kwa Masiya kwa Muungu : si
5 kama twaweza kujithania neno wenyewe kama letu sisi,
6 lakini uwezo wetu ni wa Muungu, aliyetuwezesha kulingojea agano jipya ; si andiko, illa Roho : kwani andiko huua, Roho hutoa uzima.
- 7 Hatta ungoje wa kufa, katika maandiko, uliokatwa katika mawe, umekuwa na utukufu, hatta hawakuweza waana wa Israeli kumtazama uso Musa, kwa utukufu
8 wa uso wake ukomao, si zayidi tena ungoje wa Roho
9 usiwe na utukufu ? Kwani ungoje wa hukumu ukiwa utukufu, zayidi sana ungoje wa haki umezidi kuwa na

utukufu. Kwani uliotukuzwa haukutukuzwa kwa rejeo 10
hili, kwa sababu ya utukufu uzidio. Kwani ukomao 11
ukiwa kwa utukufu, zayidi sana ukaao unao utukufu.

Tukiwa na taraja hii, twatumia uthabiti mwingi, 12
wala si kama Musa, alivyojitia usoni pasia, kwa waana 13
wa Israeli hawakuweza kutazama mwisho wake ukomao :
lakini mawazo yao yametiwa giza ; hatta siku za leo 14
pasia lile limekaa katika kulisoma agano la kale haliku-
funuliwa ; kwamba katika Masiya limekoma. Lakini 15
hatta leo, Musa akisomwa, pasia limekaa juu ya mioyo
yao. Ila wamgeukapo Bwana, pasia linaondolewa. 16

Naye Bwana ni Roho : alipo Roho ya Bwana, kuwa 17
huru.

Sisi wote kwa uso usio na pasia, tukiuangalia utu- 18
kufu wake Bwana, twageuka kwa mfano ule katika utu-
kufu kwa utukufu, kama kwa Bwana Roho.

KWA hiyo, tukiwa nao ungoje huu, kama tulivyo- 4
pewa rehema, hatukuzimia : lakini tumezikataa siri za 2
aibu, tusiende katika hila, wala hatudanganyi kwa neno
lake Muungu, lakini kwa kuithiirisha kweli twajipatia
sifa kwa moyo wote wa watu machoni pa Muungu.

Hatta anjili yetu ikistirika, imestirika kwao wana- 3
opotea, aliowapofusha muungu wa dunia hii akili zao 4
wasioamini, usiwamulike mwanga wa anjili ya utukufu
wake Masiya, aliye mfano wa Muungu. Hatujihubiri 5
nafsi zetu, illa Masiya Isa Bwana, na sisi watumwa
wenu kwa Isa. Kwani Muungu aliyeiambia nuru 6
iangaze gizani, ndiye aliyeangaza mioyoni mwetu, kwa
mwanga wa elimu ya utukufu wake Muungu, katika
uso wa Isa Masiya.

Tunayo hazina hiyo katika vyombo vya udongo, wi- 7
ngi wa uwezo uwe wa Muungu, wala si wetu. Katika 8
yote wateswa, illa hatukuhuzunika ; tukitiwa shaka, illa
si shaka nyingi mno ; tukifukuzwa, illa hatukutupwa ; 9
tukipigwa illa hatukupotea ; tukichukua po pote katika 10
mwili mauti ya Isa, uzima wake Isa uonekane katika
mwili wetu. Siku zote sisi wenyi uzima twatolewa kufa 11
kwa Isa, uzima wake Isa uonekane katika nyama yetu
ya kufa. Hatta kufa kutenda mwetu, na uzima 12
mwenu.

Tukiwa na roho hiyo ya amani, kama ilivyoandikwa, 13
Nimeamini, kwa hiyo nikanena ; na sisi tumeamini, kwa

- 14 hiyo twanena; tukijua kama aliyemfufua Bwana Isa, atafufua na sisi pamoja na Isa, ataleta pamoja na ninyi.
- 15 Kwani yote kwa ajili yenu, neema ikizidi kwa kushukuru wengi, iongezeke kwa utukufu wa Muungu.
- 16 Kwa hiyo hatuzimii; lakini mtu wetu wa 'nje akihari-
17 bika, wa ndani siku kwa siku hutengenezwa. Kwani mateso yetu mepesi yapitayo yatufanyia uthani wa utu-
18 kufu wa milele kuzidi uzidio; tusipoyaangalia yaliyoonekana, illa yasiyoonekana: kwani yaliyoonekana yanayo muhulla; yasiyoonekana ndiyo ya milele.
- 5** KWANI twajua kama nyumba yetu ya duniani ya kihema ikikongolewa, tunalo jengo lake Muungu, nyumba isiyofanyika na mikono, iliyo ya milele, katika
2 mbinguni. Kwani nasi katika hiyo twaugua, tukita-
3 mani kuvikwa na makao yetu ya mbinguni, hatta tuki-
4 vikwa tusionekane utupu. Kwani tulio katika hema twaugua, tukilemewa; kwa hiyo hatutaki kuvua, illa
5 kuvaa, kufa kutoweke katika uzima. Naye aliyetufanyiza kwa hiyo ndiye Muungu, aliyetupa arabuni ya Roho.
- 6 Tukiwa na moyo sikuzote, tukijua kama tukiwapo
7 katika mwili hatukuwapo kwa Bwana (kwa imani tuna-
8 kwenda, wala si kwa kuona), tunao moyo, na twaona
9 vema kutoka katika mwili, tufike kwa Bwana. Kwa hiyo twajitahidi, tukikaa ama tukitoka, kumpendeza
10 huyo. Kwani imetupasa sisi wote kuonekana mbele ya kiti chake Masiya, killa mmoja ayapokelee yaliyo kwa mwili, kama alivyotenda, kama mema, kama mabaya.
- 11 Tukijua hofu yake Bwana, twawashawishi watu, kwa Muungu tumeonekana; nataraja na katika thamiri zenu tumeonekana.
- 12 Hatujisifu tena kwenu, illa tukiwapa ninyi ajili ya kujisifu kwa ajili yetu, 'mwe na neno kwao wajisifuo
13 kwa uso, wala si katika moyo. Akili zetu zikipotea, ni
14 kwa Muungu; tukiwa na akili, ni kwenu. Kwani mapenzi yake Masiya yatulazimisha; tukithani kama
15 mmoja akifa mahali pa wote, wote wamekufa; akafa mahali pa wote, walio hayi wasiwe hayi kwao wenyewe,
16 illa kwake aliyekufa mahali pao akafufuka. Hatta sisi tangu wakati huu hatujui kitu kwa mwili: hatta tulio-
mjua Masiya kwa mwili, wakati huu hatujui tena.
17 Hatta mtu akiwa katika Masiya, kiumbe kipya, ya

kwanza yamepita; angalia, yote yamekuwa mapya. Na yote asili yao kwa Muungu, aliyetupatanisha naye 18 mwenyewe kwa Masiya, atupaye ungoje wa kupatanisha, ya kwamba Muungu alivyoko katika Masiya 19 akiupatanisha ulimwengu naye mwenyewe, asiyewahe-sabia makosa yao, naye atutiaye neno la kupatanisha.

Bassi mahali pa Masiya tumepolekwa, kama Mu- 20 ungu ndiye awasihiye kwa sisi; twawaomba mahali pake Masiya, mpatanishwe na Muungu. Asiyejua 21 thambi, kwa ajili yetu amemfanya thambi, sisi tu-pate kuwa haki ya Muungu katika yeye.

TUKITENDA kazi naye, twasihi, neema ya Mu- 6 ungu msiipokee burre: kwani asema, Wakati ulioku- 2 balika nimekusikia, siku ya wokovu nimekusayidia. Angalia, sasa wakati wa kukubalika, leo siku ya wo- kovu. Tusiwatie mtu ukwazo wo wote, ungoje usi- 3 laumiwe; lakini tukijiona pote kama wangoje wake 4 Muungu, katika uvumilivu mwingi, katika mateso, katika shidda, katika taabu, katika mapigo, katika ma- 5 fungo, katika fitina, katika kazi, katika makesho, ka- tika kufunga; katika kuwa safi, katika hekima, katika 6 kustahimili, katika wema, katika Roho Mtakatifu, katika upendano pasipo unafiki, katika neno la kweli, 7 katika nguvu za Muungu; kwa selaha za haki mkono wa kuume na wa kushoto, kwa utukufu na aibu, kwa 8 kunenwa vema na kunenwa vibaya; kama wanaoko- sesha, na wenyi kweli; kama wasiojulika, na waliojulika 9 sana; kama wafao, naswi hayi; kama walioathibika, na wasiouawa; kama wenyi huzuni, na wenyi siku zote 10 furaha; kama masikini, na wawapatiao wengi mali; kama wasio na kitu, na wenyi vyote.

Kanwa letu limefumbuliwa kwenu, enyi Wakorinti; 11 moyo wetu umezidi. Hamkupunguka katika sisi; 12 mmepunguka katika yaliyo ndani yenu. Kama kulipa, 13 nawaambia kama watoto, mzidi na ninyi.

Msifungwe pasipo sawa nao wasioamini. Kugawanya 14 gani kati ya haki na thulumu? Usharika gani wa nuru na giza? Sauti gani moja ya Masiya na ya Beliali? 15 Sehemu gani yake aaminiye pamoja naye asiyeamini? Kuweka pamoja gani hekalu la Muungu na sanamu? 16 Ninyi hekalu la Muungu aliye hayi; kama anenavyo Muungu, Kwani nitakaa kati yao, kati nitatembea; ni-

- takuwa wao Muungu, nao watakuwa watu wangu.
- 17 Kwa hiyo, Tokeni katika kati yao, mkafarakane, amena Bwana, wala msinguse asiyetakasika; nami nita-
- 18 wakubali, nitakuwa kwenu Baba, na ninyi mtakuwa kwangu waana na binti, amesema Bwana Mwenyiezi.
- 7 TUKIWA na ahadi hizo, wapenzi, tujitakase katika unajisi wote wa mwili na wa roho, tukitimiza utakatifu katika hofu ya Muungu.
- 2 Tupeni nafasi: hatukumthulumu mtu, hatukumha-
- 3 ribu mtu, hatukumdanganya mtu. Sineni kwa hukumu: nimetangulia kusema kama ninyi mmo mioyoni
- 4 mwetu, kufa pamoja na kuishi pamoja. Sinao hofu kwenu, kujisifu kwangu kwingi kwa ajili yenu: nimejaa faraja, nimezidi kufurahi katika mateso yetu yote.
- 5 Kwani tukija Umakedoni, mwili wetu haukuona raha, lakini pote tumeteswa; kwa 'nje mapigano, kwa ndani
- 6 kuogopa. Lakini awafarijiye walio chini, Muungu,
- 7 akatufariji sisi katika kuwako Tito. Wala si kwa kuwako yee tu, illa kwa faraja alivyofarajika na ninyi, akitupa habari za tamani yenu, za uzito wenu, za uwivu
- 8 wenu kwa ajili yangu; hatta nikazidi kufurahi. Kwamba hatta nikiwahuzunisha kwa waraka sijuti, nikiwa nalijuta; kwani naona kama waraka ule uliwahuzunisha kitambo. Sasa nafurahi, si kwa ajili ya kuhuzunika ninyi, lakini kwa sababu mmehuzunika kwa kugeuka: kwani mmehuzunika kwa Muungu, msipate hasara kabisa kwa sisi.
- 10 Kwani huzuni ya kwa Muungu huleta kugeuka kusikojutiwa: lakini huzuni ya dunia huleta kufa tu.
- 11 Angalieni, kama mlivyohuzunika kwa Muungu, ilivyoleta kwenu bidii, hatta kujionyesha safi, hatta kukasirika, hatta hofu, hatta shauko, hatta uwivu, hatta kisasi. Kwani njia zote mmejifanya mmetakata katika tendo lile.
- 12 Illakini nilipoandika kwenu, si kwa sababu yake aliyefanya thulumu, wala si yake aliyethulumuwa, lakini upesi wenu wa ajili yetu uonekane kwa hesabu yenu
- 13 mbele yake Muungu. Kwa hiyo tumefarajika: baada ya faraja yetu tukafurahiwa sana na furaha yake Tito,
- 14 kama roho yake imeburudika nanyi nyote. Kama nimejisifu neno kwa ajili yenu, sikuaibika; lakini kama yote tuliyoaambia ninyi ya kweli, hivi na kujisifu

kwetu kwa Tito kumekuwa kweli. Naye kwa ndani 15
amezidi kuwa wenu, akikumbuka mliyotii nyote, mli-
vyomkubali yeye kwa hofu na tetemeko. Nafurahi 16
kama kwa yote nawatumainia.

TWAWAARIFU ninyi, ndugu, neema ya Muungu 8
iliyotolewa katika makanisa ya Umakedoni; ya kwa 2
mba katika kujaribiwa sana na mateso, wingi wa furaha
yao na fukara yao ya chini imezidi kufanya mwingi
ukarimu wao; ya kuwa kwa uwezo, nawashuhudia, na 3
kupita uwezo, kwa moyo wao wenyewe, wakituomba sisi 4
kwa kusihi sana tuipokee neema na usharika wa kuwa-
ngojea watakatifu: wala si kama tulivyothani, lakini 5
kwanza wakajitoa wenyewe kwa Bwana, na kwa sisi
kama apendavyo Muungu. Kwa hiyo tumemwonya 6
Tito, kama alivyoanza, hivi akatutumilie na neema hiyo.
Bassi kama mmezidi kwa yote, kwa imani, na kunena, na 7
elimu, na bidii yote, na kwa mapenzi yenu kwetu, mka-
zidi hivyo na katika neema hii. Sineni kwa amri, illa kwa 8
bidii zao wangineo, nikijaribu asili ya mapenzi yenu.

Kwani mmejua neema ya Bwana wetu Isa Masiya, ya 9
kwamba kwa ajili yenu amekuwa maskini akiwa tajiri,
mpate utajiri ninyi kwa umasikini wake. Natoa wosia 10
wangu katika haya. Kwani imewapasa ninyi, mliota-
ngulia, si kutenda tu, illa kutaka, tangu mwaka jana.
Sasa mkatimie kutenda, illi kama nia ya kutaka, hivi 11
na kutimia katika mliyoyo navyo. Ikiwa kwanza nia, 12
imekubalika kwa kadiri alivyo navyo, si kwa kadiri asi-
vyo navyo. Kwani sivyo, kwa wangine nafasi, kwa 13
ninyi shidda: illa kama kuwa sawa; wakati huu 14
wingi wenu kwa upungufu wao, na wingi wao upate
kuwa kwa upungufu wenu; hatta kuwa sawa: kama 15
ilivyoandikwa, Aliye nyingi hakuzidi, aliye chache ha-
kupunguka.

Muungu ashukuriwe, aliyempa moyoni Tito upesi uleule 16
juu yenu. Hatta akakubali kuonywa; illa akizidi ku- 17
wa mpesi, kwa moyo wake akasafiri kwenu. Tumepeleka 18
pamoja naye ndugu, sifa yake katika anjili makanisani
mwote. Illa si hivyo tu, lakini aliyechaguliwa kwa 19
makanisa asafiri pamoja naswi, katika neema hii tuli-
yoingojea sisi, kwa utukufu wa Muungu, na nia
yetu sisi: tukiepuka hiyo, mtu asitulaumu katika 20
uzidi uliongojewa nasi: tukitangulia kukumbuka yaliyo 21

22 mema mbele ya Bwana, hatta na mbele ya watu. Tu-
mepeleka pamoja nao ndugu wetu tuliyemjua katika
mambo mengi kuwa mwepesi, lakini sasa mwepesi sana
kwa tumaini lililo kwa ninyi.

23 Ikiwa ya Tito, ndiye asharikiye nami, atendaye kazi
kwenu nami; ao ndugu zetu, mitume ya makanisa,
24 utukufu wake Masiya. Bassi 'mwaonyeshe hawa, na
mbele ya makanisa, wonyesho wa mapenzi yenu na ku-
jisifu kwetu kwa ajili yenu.

9 KWA mambo ya ungoje wa watakatifu, haihitaji ni-
2 waandikie: kwani najua nia zenu, nilizojisifia kwa
Wamakedoni, kama Akaya imekuwa tayari mwaka jana;
3 na bidii zenu zimewatia moyo wengi. Nimewapeleka
ndugu, kujisifu kwetu kwa ajili yenu kusibatilike upande
4 huu; kama nilivyosema, 'mwe tayari: isiwe, Wamake-
doni wakija pamoja nami, wakiwaona ninyi hamjakuwa
tayari, sisi tusitahayarike (nisiseme ninyi), katika tu-
maini hili la kujisifu.

5 Nikaona sina buddi kuwaonya ndugu watangulie kwe-
nu, waweke pamoja ukarimu wenu, mliyohubiriwa, 'mwe
6 tayari, kama ukarimu, wala si kama kwa choyo. Ndilo,
Apandaye haba, haba atavuna; apandaye kwa ukarimu,
7 kwa ukarimu atavuna. Killa mtu kama alivyopenda
moyoni; si kwa huzuni ama kwa lazimu: kwani atoaye
8 kwa furaha ndiye ampendaye Muungu. Muungu ndi-
ye awezaye kuzidisha killa neema kwenu; illi, mkiwa po-
pote na riziki zote katika mambo yote, mpate kuzidi
9 katika killa tendo jema: kama ilivyoandikwa, Ameta-
wanya 'nje, amewapa maskini; haki yake yakaa milele.
10 Bassi aruzukuye mbegu kwa mpanda, aruzuku chakula
cha kuliwa, akazidishe mbegu zenu zilizopandwa, aka-
11 yaongeze mazao ya haki yenu: mkipewa utajiri wote kwa
killa ukarimu, ufanyao kwa sisi shukrani kwa Muu-
ngu.

12 Kwani ungoje wa uwakili huu, hautimizi tu upungufu
wao watakatifu, illa wazidi tena kwa shukrani ya watu
13 wengi kwa Muungu; kwa kuujua ungoje huu wakimtu-
kuza Muungu, kwa kuungama ninyi kutiishwa na anjili
yake Masiya, na ukarimu wa kushariki na hawa, nao
14 wote; na kwa kuwaomba ninyi, wanaowatamani kwa
15 ajili ya neema ya Muungu izidio kwenu. Shukrani kwa
Muungu kwa mambo atoayo yasiyofasirika.

NDIMI Paolo niwasihiye kwa utaratibu na upole **10**
 wake Masiya, niliye usoni kwenu mnenyekevu, nisipo-
 kuwako sina hofu kwenu; naomba, nikiwako nisitoe **2**
 kuwa na hofu katika tumaini, nililothania nitathubutu
 juu yao wanaotuthania twaenda kwa mwili. Kwani **3**
 tuendao katika mwili, hatupigani kwa mwili, wala sela- **4**
 ha za vita yetu sizo za mwili, illa ziwezazo katika Muu-
 ngu kuyaangusha maboma, ziangushazo majadiliano, **5**
 na killa kitu kilicho juu kijiinuacho juu ya elimu ya
 Muungu, zifungazo killa fikara katika kumtii Masiya, **6**
 zilizo tayari kulipa kisasi cha maasi yote, mkitimia
 ninyi kutii.

Mwaangalia yaliyo usoni? Mtu akitumaini ndiye wa **7**
 Masiya, afikiri tena kwa ndani, kama alivyo wa Masiya
 yeye, hivyo na sisi. Hatta nikizidi kitu kujisifu kwa **8**
 ajili ya uwezo wetu, tuliopewa sisi na Bwana kwa kuje-
 nga, wala si kuwaharibu, hatutatahayarika: nisione kane **9**
 kama kuwaogofya kwa nyaraka. Kwamba, Nyaraka **10**
 zake, husema, nzito na hodari, illa kuwako mwilini thaifu,
 na maneno manyonge. Huyu athani hivi, kama tulivyo **11**
 kwa maneno ya nyaraka tusipokuwako, hivyo na tuki-
 wapo kwa matendo.

Kwani hatuthubutu kujipambanua wala kujilinganisha **12**
 nao wanaojinenea: lakini hawa, wakijipima kwa wenyewe,
 wakijilinganisha wao kwa wao, hawana akili.

Sisi hatujisifu pasipo cheo, lakini kwa cheo cha ka- **13**
 nuni, aliyotugawanyia Muungu, cheo cha kuwafikia na
 ninyi. Kwani hatujitanui kama wasiowafikia ninyi; **14**
 kwani hatta kwenu tumewasili katika anjili yake Masiya,
 tusipojisifu pasipo cheo, katika kazi zao wangineo; tu- **15**
 kiwa na tumaini, imani yenu ikizidi, katika kwenu kuna-
 fisishwa nanyi sana kwa kanuni yetu, tuwahubirie walio **16**
 upande wa pili wenu, wala tusijisifu kwa mambo yaliyo-
 kwisha kutengenezwa, kwa kanuni yao wangineo.

Ajisifuye ajisifu katika Bwana. Kwani siye ajineneaye **17**
 aliye mwema, illa yeye Bwana amneneaye. **18**

AFATHALI mniachilie kidogo upumbafu: mkania- **11**
 chilie. Kwani nawaonea uwivu, uwivu wa Muungu: **2**
 kwani nimewaoza kwa mume mmoja, nimletee Masiya
 bikira safi. Naogopa illa, kama nyoka alivyomdanganya **3**
 Hawa katika werevu wake, akawapoteze ninyi fikara
 zenu katika ukarimu na utakatifu ulio kwa Masiya.

Kwani ajaye akihubiri Isa mwingine tusiyemhubiri, **4**

ama mmepokea Roho ingineyo msiyoipokea, ama anjili
5 ingineyo msiyoikubali, afathali mwachilie. Kwani na-
6 thani sikuwa nyuma yao mitume walio wakuu. Ukiwa
udogo katika neno, sio katika elimu; lakini katika yote
tumeonekana nanyi kabisa.

7 Nimetenda thambi nikijinenyekea niwatukuze ninyi,
kwamba anjili ya Muungu nalihubiri kwenu burre?
8 Naliwaibia makanisa mangine, nikitwaa posho niwango-
9 jee ninyi; hatta nikiwapo kwenu nikihitaji, sikumlemaa
mtu; mahitaji yangu wakatimia ndugu waliokuja ka-
tika Umakedoni. Nikajilinda nisiwalemee kabisa, nami
10 nitajilinda. Kweli yake Masiya ninayo ndani, ya
kwamba katika kujisifu huku sitapingwa katika mipaka
11 ya Akaya. Kwa nini? Kwamba siwapendi nyinyi?
12 Muungu ajuaye. Nifanyavyo nami nitafanya, niwakatie
ajili watafutao ajili, wapate kuonekana, wakijisifu kama
13 na sisi. Kwani hawa mitume wa uwongo, watendao
kwa hila, wakijigeuza kwa mfano wa mitume wa Masiya.
14 Wala hapana ajabu; kwani Shetani mwenyewe hugeuka
15 kwa mfano wa malaika ya nuru. Wala si kikubwa, wa-
ngoje wake wakigeuka kwa mfano wa wangoje wa haki.
Mwisho wao ndio kwa matendo yao.

16 Nasema tena, mtu asinione kuwa mpumbafu; illakini
hatta hivi, kama mpumbafu mnikubali, nami nikajisifu
17 kidogo. Ninenalo, sineni kwa Bwana, illa kama katika
18 upumbafu, katika hali hiyo ya kujisifu. Wengi wakiwa
19 wajisifu kwa mwili, nami nitajisifu. Mwawaachilia kwa
20 furaha wapumbafu, mkiwa na akili. Kwani mwaachilia
mtu akiwatia utumwani, mtu akiwapiga ninyi usoni.

21 Nasema kwa aibu, kama sisi tumekuwa thaifu. Mtu
akithubutu kwa neno (nasema katika upumbafu), na-
22 thubutu na mimi. Hawa Waebraia? na mimi. Hawa
Waisraeli? na mimi. Hawa wazao wa Ibrahimu? na
23 mimi. Hawa wangoje wa Masiya? (nanena kipumbafu)
mimi zayidi; katika taabu kuzidi, katika mapigo ku-
pita cheo, katika mafungo kuzidi, katika kufa marra
24 nyingi. Kwa Wayahudi marra tano nalipokea arobaini
25 illa moja, marra tatu nalipigwa na bakora, marra moja
nikatupiwa mawe, marra tatu merikebu imevunjwa,
26 mchana na usiku nimekaa katika vilindi; katika taabu
za safari nyingi, katika hatari za mtoni, hatari za wanya-
ng'anyi, hatari kwa jamaa, hatari kwa mataifa, hatari
za mjini, hatari za jangwani, hatari za baharini, hatari

kwa ndugu za uwongo ; katika taabu na shidda, katika 27
 makesha mengi, katika njaa na kiu, katika kufunga marra
 nyingi, katika baridi na utupu : baada yao yaliyo 'nje, 28
 injiayo killa siku, tunza la makanisa yote. Nani thaifu, 29
 nisipo thaifu mimi ? Nani ajikwaa, nisipowaka mimi ?
 Ikipasa kujisifu, nitajisifu kwa mambo ya uthaifu wangu. 30
 Muungu na Baba wa Bwana Isa Masiya ajuaye, aliye 31
 mbarikiwa milele, kama sisemi uwongo.

Katika Dameski mwenyi taifa wa Areta mfalme 32
 aliulinda mji wa Wadameski, anikamate : na katika 33
 dirisha kikaponi nikashushwa katika ukuta, nikaokoka
 katika mikono yao.

HAINIPASI kujisifu. Nitakuja kwa njozi na 12
 mafunuo ya Bwana.

Namjua mtu katika Masiya, tangu miaka arobata- 2
 shara (kama katika mwili sijui, kama pasipo mwili sijui ;
 Muungu ajuaye), amechukuliwa huyu hatta uwingu wa
 tatu.

Namjua tena mtu huyu (kama katika mwili sijui, 3
 kama pasipo mwili sijui ; Muungu ajuaye), kama ame- 4
 chukuliwa katika peponi, akasikia maneno yasiyoneneka,
 asiyoweza mtu kuyatamka.

Kwa mambo yake huyu nitajisifu : kwa mambo 5
 yangu mimi sijisifu, illa kwa thaifu zangu.

Kama ningalipenda kujisifu, singalipumbazika ; kwa- 6
 ni ninenayo kweli : illa najizuia, mtu asinithanie mimi
 kuliko anionavyo, ao neno langu alisikialo.

Na wingi wa mafunuo usipate kunivuna, nalipewa 7
 mwiba wa mwilini, tume wa Shetani, unipige, nisipate
 kujivuna. Kwa huo nalimsili Bwana marra tatu anio- 8
 ndolee. Akaniambia, Neema yangu yakutosha : kwani 9
 uwezo wangu hutimilika katika uthaifu. Bassi afathali
 sana nijisifu katika thaifu zangu, uwezo wake Masiya
 ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezewa katika utha- 10
 ifu, katika jeuri, katika taabu, katika mafukuzo, katika
 shidda, kwa ajili yake Masiya. Kwani niwapo thaifu,
 ndipo niwezapo.

Nimekuwa mpumbafu : mmenilazimisha ; kwani ime- 11
 pasa mimi ninenewe na ninyi : kwani sikuwapungukia
 mitume walio wakuu, mimi nisipokuwa kitu. Ishara za 12
 mtume zimetendeka kwenu katika uvumilivu wote, kwa
 ishara na ajabu na nguvu. Kwa nini hamkulingana nao 13

makanisa yaliyosalia, isipokuwa kama mimi sikuwalemea? Nisamehe thulumu hii.

- 14 Angalia, marra ya tatu mimi tayari nije kwenu; wala sitawalemea: kwani siyataki yaliyo yenu, illa ninyi: kwani haiwapasi watoto wawawekke wazee, illa wazee
 15 watoto. Nami ni heri nitawanye nikatawanyike kwa ajili ya maisha yenu, hatta nizidipo kuwapenda ninyi, nipunguke kupendwa.
- 16 Ikiwa, mimi sikuwalemea; illa, nikiwa mwerevu,
 17 naliwatwaa kwa hila. Mtu niliyempeleka kwenu, kwa huyu nimewafayidia? Nalimtaka Tito, nikampeleka na
 18 ndugu. Tito amewafayidia? Hakuenda katika roho ileile? si katika nyayo zilezile?
- 19 Mtuthanie tena kama twawatolea ninyi huja? Mbele ya Muungu katika Masiya twanena; na yote, wapenzi, kwa ajili ya kuwajengea.
- 20 Kwani naogopa, nikija, nisiwaone ninyi kama nilivyo-taka, nami nisionekane nanyi kama mlivyotaka ninyi; illa labuda fitina, uwivu, hasira, ugomvi, usingizio, ku-
 21 amba, kujivuna, kuchafuka; illa, nikija tena mimi, Muungu wangu asinithili kwenu, nikawahuzunie wengi waliokosa zamani, wasiotubu katika uchafu na uzini na washerati walioufanya.
- 13 HII ya tatu naja kwenu. Kwa kanwa la mashahidi
 2 wawili ama watatu killa neno lithubutike. Kutangulia nimenena, nami nasema, kama nikiwapo marra ya pili, hatta sasanisipokuwako, kwa waliokosa zamani, na kwao
 3 waliosalia wote, kama nitakapokuja tena sitaachilia; mkitaka kujua kama Masiya ndiye asemaye kwa mimi; asiye
 4 thaifu kwenu, illa awaweza ninyi. Kwani akiwa amesulibishwa katika uthaifu, yu hayi kwa nguvu ya Muungu. Kwani na sisi tunao uthaifu katika yeye, lakini
 5 tutakuwa hayi kwa nguvu za Muungu kwenu. Mjijari-ribu kama ninyi katika imani; jithubutisheni nafsi zenu. Ama hamjui wenyewe kama Isa Masiya yumo mwenu?
 6 msipokuwa mmetupwa. Natumaini mtajua kama sisi
 7 hatukutupwa. Namwomba Muungu msifanye baya lo lote; si kwa ajili tuonekane sisi tumekubalika, illa kwa ajili yenu, mlifanye lililo jema, hatta sisi tukiwa ka-
 8 ma tumetupwa. Kwani hatuwezi neno juu ya kweli, illa
 9 kwa ajili ya kweli. Twafurahiwa tukiwa sisi thaifu, ninyi mkiwa hodari: hili ndilo tuombalo, mtengezeke ninyi.

Kwa hiyo nimeyaandika haya nisipokuwako, illi niki- 10
wapo nisitumie ukali, kwa uwezo niliopewa na Bwana
kwa kujengea, wala si kwa kuharibu.

Imesalia, ndugu, mfurahi, mtengezeke, mfarajike, 11
mtake manoja, mkae katika amani: naye Muungu wa
upendano na amani awe kwenu.

Msalimiane kwa busu takatifu. Wawasalimia ninyi ¹³₁₃
watakatifu wote.

Neema ya Bwana Isa Masiya, na mapenzi ya Muu- 14
ngu, na usharika wa Roho Mtakatifu, nanyi nyote.

WARAKA WA PAOLO MTUME

KWA

WAGALATIA.

PAOLO, mtume (si wa watu, wala kwa mtu, illa kwa 1
Isa Masiya, na Muungu Baba, aliyemfufua katika wafu),
nao ndugu wote waliopo pamoja nami, kwa makanisa 2
ya Galatia: Neema kwenu na amani ya Muungu Baba, 3
na Bwana wetu Isa Masiya, ajitoaye kwa ajili ya tha- 4
mbi zetu, illi atuokoe katika dunia mbovu iliyopo, kama
alivyopenda Muungu na Baba wetu: awe na utukufu 5
milele hatta milele. Amina.

Naajabu kama upesi hivi mmemgeukia aliyewaita 6
katika neema ya Masiya kwa anjili ingineyo, isiyo 7
ngine, wasipokuwa watu wawataabishao, watakao kui-
geuza anjili yake Masiya. Lakini kama sisi, ao malaika 8
wa mbinguni, akiwahubiria ninyi anjili illa tulivyowa-
hubiria, atengewe mbali. Kama tulivyosema kwanza, 9
na sasa tena nasema, mtu akiwahubiria anjili illa mli-
vyopokea, atengewe mbali. Kwani sasa nashawishi watu, 10
ama Muungu? ao nataka kupendeza watu? Kama
ningependeza watu, singekuwa mtumwa wa Masiya.

Nawaarifu ninyi, ndugu, anjili iliyohubiriwa na mimi, 11
kama siyo kwa mtu. Wala mimi sikuipokea kwa mtu, 12
wala sikufundishwa, illa kwa ufunuo wa Isa Masiya.

- 13 Mmesikia mwenendo wangu zamani katika Uyahudi,
kama pasipo kiasi naliwafukuza kanisa la Muungu nika-
- 14 liaribu, nikafayidi katika Uyahudi kuliko wengi hiri-
mu zangu katika taifa langu, nikizidi kuwa na uwivu
kwa mapokeo ya baba zangu.
- 15 Hatta alipoona vema Muungu, aliyenitenga katika
16 tumbo la mamangu, akaniita kwa neema yake, akamfu-
nua Mwana wake katika mimi, nimhubiri kwa mataifa,
17 marra sikufanya shauri na mwili na damu, wala sikuenda
Yerusalemi kwao walio mitume mbele yangu; lakini
nalikwenda zangu Arabuni; nikarudi tena Dameski.
- 18 Halafu baada ya miaka mitatu nalikwenda Yerusa-
lemi nimzuru Kefa, nikakaa kwake siku hamstashara.
- 19 Mtume mgineo sikumwona, illa Yakobo ndugu wake
20 Bwana. Niyaandikayo, angalia, mbele ya Muungu, ya
kwamba sineni uwongo.
- 21 Halafu nalikwenda upande wa Shami na Kilikia.
22 Wala hawakunijua kwa uso makanisa ya Uyahudi walio
23 katika Masiya. Wamesikia tu kama aliyetufukuza za-
24 mani, sasa aihubiri imani aliyoiharibu; wakamtukuza
Muungu kwa ajili yangu.
- 2 HALAFU, miaka arobatashara ikipita, nalikwenda
Yerusalemi pamoja na Barnaba, nikiichukua nami
Tito.
- 2 Nalikwenda kwa ufunuo; nikaweka mbele yao anjili
nihubiriyo kwa mataifa, kwa faragha kwao walio wenyi
3 sifa, nisiwe naenda burre, ama nimekwenda. Wala Tito
aliye pamoja nami, akiwa Myonani, hakulazimishwa
4 atahiriwe: kwa sababu ya ndugu za uwongo walioingi-
zwa kwa siri, walioingia wapeleleze huru yetu tuliyo
5 nayo katika Masiya Isa, watutie utumwani. Hawa
hatta saa moja sikujitia chini yao; kweli ya anjili ipate
kuwakalia ninyi.
- 6 Nao walio na sifa ya kuwa neno (watu gani walioku-
wa, kwangu mamoja: Muungu hakubali cheo cha mtu),
7 kwangu wale wenyi sifa hawakunizidisha kitu: illakini
wakiona kama anjili yao wenyi ngovi nimeaminiwa na-
8 yo, kama na Petro ya tohara (afanyaye katika Petro
kwa utume wa tohara afanyaye kwangu kwa mataifa);
9 wakijua neema niliyopewa, Yakobo na Kefa na Yohana,
waliosifiwa kama nguzo, wakanipa mkono wa ushrika
mimi na Barnaba, sisi tuende kwa mataifa, nao wenye-

we kwao tohara ; illa tuwakumbuke masikini tu ; hiyo 10
nikataka sana kufanya.

Hatta, Kefa alipokuja Antiokia, nalimpinga usoni, 11
kwani amestahili kulaumiwa. Kwani mbele ya kuja 12
watu katika kwa Yakobo, alikula nao wamataifa : wa-
lipokuja akajitenga akafarakana nao, akiwaogopa walio
wa tohara. Wakajigeuza pamoja naye Wayahudi wa- 13
liosalia ; hatta na Barnaba akachukuliwa na kujigeuza
kwao.

Lakini nikiona njia yao hainyoki katika kweli yake 14
anjili, nalimwambia Kefa mbele yao wote, Kama wewe
ukiwa Myahudi unafuata desturi za kitaifa, wala si za
Kiyahudi, wafanyaje wamataifa wafuate desturi za Ki-
yahudi ? Sisi tulio Wayahudi kwa asili, wala si wenyi 15
thambi wa mataifa, tukijua kama mtu hafanyiziwi haki 16
kwa matendo ya sheria, illa kwa imani yake Isa Masiya,
na sisi tumemwamini Masiya Isa, tufanyiziwe haki kwa
imani ya Masiya, wala si kwa matendo ya sheria : kwani
kwa matendo ya sheria hapana hayi atakayefanyiziwa
haki. Lakini katika kutaka kufanyiziwa haki katika 17
Masiya, tukionwa kuwa na thambi, Masiya amekuwa
mngoje wa thambi ? Hasha ! Kwani nikiyajenga tena 18
niliyoyaangusha, najifanya mwenyewe mkosaji. Kwani 19
mimi kwa sheria naliifia sheria, nipate kuwa hayi kwa
Muungu. Nimesulibishwa katika Masiya ; ni hayi : si 20
mimi tena, Masiya yu hayi ndani yangu : uzima ninao
sasa katika mwili, uzima wa imani iliyo yake Mwana
wa Muungu, aliyenipenda, akajitoa kwa ajili yangu.
Siiondoi neema yake Muungu : kwani haki ikiwa kwa 21
sheria, Masiya amekufa burre.

ENYI Wagalatia wasio na akili, nani aliyewaloga, 3
Isa Masiya akiwa ameandikwa machoni penu amesuli-
bishwa ? Hili tu nitakalo kuarifiwa nanyi, Mmempokea 2
Roho kwa matendo ya sheria, ama kwa kusikia kwa
imani ?

Hamna akili hatta hiyo ? mkianza katika Roho, 3
mwataka kutimizwa katika mwili ? Mmeteswa hivi 4
burre ? ikiwa burre. Awaruzukiaye Roho, afanyaye 5
nguvu ndani yenu, kwa matendo ya sheria ao kwa ku-
sikia kwa imani ? Kama Ibrahimu alivyomwamini 6
Muungu, akahesabiwa kwa haki. Jueni kama walio wa 7
imani ndio walio waanawe Ibrahimu. Nalo andiko 8

likiona mbele kama Muungu atawafanyizia mataifa haki kwa imani, likahubiri mbele anjili kwa Ibrahimu, ya kwamba, Katika wewe mataifa yote watabarikiwa.

- 9 Hivi walio wa imani wabarikiwa pamoja naye Ibrahimu mwenyi imani.
- 10 Walio wa katika matendo ya sheria wako chini ya laana. Kwani imeandikwa, Amelaaniwa killa asiyeyatenda yote yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria, aya-
- 11 fanye. Kwamba katika sheria hakuna aliye na haki kwa Muungu ni wazi, kwamba, Mwenyi haki ataishi
- 12 kwa imani. Sheria siyo kwa imani, ila, Ayafanyaye ataishi katika hayo.
- 13 Masiya ametukomboza katika laana la sheria, akiwa laana kwa ajili yetu : kama imeandikwa, Amelaaniwa
- 14 killa aliyetundikwa juu ya mti : kwa maksudi mataifa wapate mbaraka wa Ibrahimu katika Masiya Isa ; tupe-
- 15 we ahadi ya Roho kwa imani.
- 15 Ndugu, nasema kwa mwana Adamu : hatta agano la mwana Adamu likithubutika, mtu haliondoi wala halibadili.
- 16 Kwa Ibrahimu ahadi zimenenwa, na mzao wake. Hasemi mazao, kama wengi ; illa kama mmoja, Mzao wako, ndiye Masiya.
- 17 Ndilo nisemalo, agano lililothubutika na Muungu kwa Masiya, sheria iliyokuwa miaka ároba mia na thelathini baadaye, haiwezi kuiondoa iibatilishe ahadi.
- 18 Kwani urithi ukiwa kwa sheria, siyo tena kwa ahadi. Naye Ibrahimu alipewa ahadi na Muungu.
- 19 Nini tena sheria ? Imetiwa kwa sababu ya makosa, hatta mzao atakapokuja aliyeahidiwa ; ikaamriwa kwa
- 20 malaika mkononi mwa mtu aliye kati. Aliye kati si wa moja ; naye Muungu ni mmoja.
- 21 Bassi sheria haipatani na ahadi zake Muungu ? Hasha : kwani sheria kama ingalitolewa iwezayo kufanya
- 22 uzima, yakini haki ingalikuwa kwa sheria. Lakini maandiko yamewafunga wote chini ya thambi, wapewe
- 23 ahadi ya imani ya Isa Masiya wanaoamini. Mbele ya kuja imani tumelindwa chini ya sheria, tukifungwa kwa
- 24 imani itakayofunuliwa. Hivi sheria mchukuzi wetu
- 25 kwa Masiya, tupewe haki ya imani. Imani ikija, hatu-
- 26 po tena chini ya mchukuzi. Kwani watoto wa Muungu
- 27 nyote kwa imani katika Masiya Isa. Kwani mliobati-

zwa kwa Masiya, mmemvaa Masiya. Hakuna Mya- 28
hudi wala Myonani, hakuna mtumwa wala mngwana,
hakuna mume na mke: kwani ninyi nyote mmekuwa
mmoja katika Masiya Isa. Ninyi mkiwa wa Masiya, 29
mmekuwa mzao wa Ibrahimu, na warithi kwa ahadi.

NASEMA, wakati mrithi ni mtoto, hapambanuki na 4
mtumwa, akiwa bwana wa yote, lakini yupo chini ya 2
mawakili na wasimamizi, hatta muhulla ulioandikwa na
baba. Hivi na sisi, tulipokuwa watoto, tumetumika chi- 3
ni ya mambo ya dunia. Hatta wakati ulipowadia kabisa, 4
Muungu akapeleka Mwana wake, amezaliwa na mwa-
namke, amezaliwa chini ya sheria, awakomboe walio 5
chini ya sheria, tupate kupewa kuwa waana. Kwamba 6
mmekuwa waana, Muungu amepeleka Roho ya Mwana
wake katika mioyo yetu, iliayo, Abba, ndiyo Baba.
Hatta wewe si mtumwa tena, illa mwana; kama mwa- 7
na, na mrithi wa Muungu kwa Masiya.

Lakini wakati msipomjua Muungu mmetumika nao 8
kwa asili isiyo miungu: sasa mkimjua Muungu, ama 9
afathali mkijuliwa na Muungu, mmegeukaje nyuma
kwa mambo thaifu na maskini, mliyotaka tena mtumi-
ke nayo? Mnashika siku, na miezi, na wakati, na 10
miaka. Nawaogopea, nisiwe nimeshughulika kwenu 11
burre. 'Mwe kama mimi, kwamba nami kama ninyi, 12
ndugu, nawasihi: hamkunithulumu. Mwajua ya kwa- 13
mba kwa uthaifu wa mwilini nimewahubiria kwanza
anjili: na jaribu lenu la mwilini hamkulitharau wala 14
hamkulikataa, lakini kama malaika wa Muungu mka-
nikubali, kama Masiya Isa.

Bassi wapi kuwa heri kwenu? Nawashuhudia ya 15
kwamba, kama yamkini, mngaling'oa macho yenu,
mngalinipa mimi. Hatta adui wenu nimekuwa, niki- 16
waambia kweli?

Wanao uwivu kwenu, illa si vema; lakini wataka 17
kuwafunga ninyi 'nje, 'mwe na uwivu kwao. Ndi- 18
vyo vema kuwa na uwivu sikuzote kwa mema, wala
sipo tu nikiwapo kwenu mimi. Vitoto vyangu, ninao 19
tena utungu wenu, hatta Masiya atakapoonekana kwe-
nu. Nataka kuwako kwenu sasa, na kuibadili sauti 20
yangu; kwani nawawia na shaka.

Nambieni, mpendao kuwa chini ya torati, hamwisi- 21
kii torati? Kwani imeandikwa, ya kwamba Ibrahimu 22

alikuwa na waana wawili, mmoja kwa suria, na mmoja
 23 kwa mngwana. Lakini aliye wa suria alizaliwa kwa
 24 mwili, aliye wa mngwana kwa ahadi. Haya yame-
 kuwa kwa mfano: kwani hawa maagano mawili;
 moja katika mlima Sinai, lizaalo kwa utumwa, ndilo
 25 Hajir. Kwani Hajir ni mlima Sinai ulioko Arabuni,
 umefanana na Yerusalemi wa sasa: kwani atumika,
 26 na watoto wake. Yerusalemi wa juu ni huru, ndio
 27 mama wetu wote. Kwani imeandikwa, Furahiwe,
 tassa usiyezaa; ondoke ukapige kelele, usiye na utu-
 ngu: kwani watoto wake aliyeachwa wengi kuliko
 28 wake aliye na mume. Sisi, ndugu, kama Isaak, wa-
 29 toto wa ahadi. Lakini kama wakati ule aliyezaliwa
 kwa mwili amemfukuza aliye kwa roho, hivi na sasa.
 30 Lakini yanenani maandiko? Mtupie mbali suria na
 mwana wake, kwani hatarithi mwana wa suria pamoja
 31 na mwana wake aliye huru. Bassi, ndugu, sisi si wa-
 toto wa suria, illa wake aliye huru.

5 BASSI, katika huru, Masiya alivyotuweka huru,
 simameni, wala msiingie tena katika mafungo ya utu-
 2 mwa. Angalia, mimi Paolo nawaambia, ya kwamba
 3 mkitahiriwa, Masiya hatawafaa neno. Namshuhudia te-
 na killa mtu aliyetahiriwa, imempasa aifanye sheria yote.
 4 Mmebatilika katika Masiya, mliofanyikwa haki katika
 5 sheria; mmeanguka katika neema. Kwani sisi kwa
 Roho katika imani twalitazamia tumaini la haki.
 6 Kwani katika Masiya Isa wala tohara haina nguvu,
 wala kutoa kutahiriwa; illa imani itendayo kwa upe-
 ndano.

7 Mlikwenda vizuri; nani aliyewazuia msiifuata kweli?
 8 Kushawishi huko si kwake aliyewaita. Chachu dogo
 10 huhacha machanganyiko yote. Mimi nawaaminia
 ninyi katika Bwana, ya kuwa hamtafikiri neno lingine-
 lo: awataabishaye aichukue hukumu, awaye yote.

11 Nami, ndugu, nikiihubiri tohara, mbona nifukuzwe?
 12 Ndipo chukizo la msalaba liondokapo. Wa heri waka-
 tiwe mbali wanaowaharibu.

13 Kwani ninyi, ndugu, mmekwitwa kuwa huru: illa
 huru yenu si chimbuko kwa mwili; kwa upendano
 14 mtumikane. Kwani sheria yote imetimika katika
 neno moja, ndilo, Umpende jirani yako kama moyo
 15 wako. Illakini mkiumana, mkilana, angalieni msilikane.

Nasema, mwende katika Roho, wala msitimize ngoa 16
za mwili. Kwani mwili hutamani juu ya Roho, na 17
Roho juu ya mwili; kwani haya hayapatani; hatta
hamvifanyi mvipendavyo. Mkiongozwa na Roho, ha- 18
'mnanyi chini ya sheria.

Kwani thahiri matendo ya mwili, ndiyo uzini, asha- 19
rati, uchafu, jeuri, kuabudu sanamu, kufanya sumu, 20
wadui, ugomvi, uwivu, hasira, fitina, kutengwa, uzu-
shi, hasidi, uuaji, ulevi, ulafi, nayo yaliyo kama haya: 21
nawaambia mbele, kama mbele nilivyowaambia, kama
wale watendao haya hawataurithi ufalme wa Muungu.

Nalo tunda la Roho, ndilo kupendana, kufurahi, 22
amani, kuvumilia, kusayidiana, wema, imani, upole, 23
kujizuia: juu ya haya hapana sheria. Nao walio wa 24
Masiya wameusulibisha mwili, pamoja na tamaa na
shauko. Tukiishi katika Roho, katika Roho tuenende. 25
Tusijisifu burre, tukikasirikiana, tukihacidiana. 26

NDUGU, mtu akipatwa na kosa, ninyi walio wa 6
Roho mwongoeni huyo katika roho ya upole; ukijia-
ngalia mwenyewe, usijaribiwe na wewe. Mchukuliane 2
mizigo, hivi mkatimize sheria yake Masiya. Kwani 3
mtu akijiona kuwa neno asipokuwa neno, amejida-
nganya. Killa mtu athubutishe kazi yake mwenye- 4
we, ndipo kujisifu kwake kwa nafsi yake, wala si
kwa mtu mwingineo. Kwani killa mtu atachukua 5
mzigo wake yeye.

Aliyefundishwa ashariki naye afundishaye katika 6
yote yaliyo mema. Msikose; Muungu hathihakiwi: 7
kwani apandayo mtu, ndiyo atakayoyavuna. Kama 8
apandaye kwa mwili wake, ya mwili atavuna uhari-
bifu; apandaye kwa roho, ya roho atavuna uzima wa
milele. Katika kutenda vema tusichoke: wakati 9
wake tutavuna, tusiozimia. Bassi tena, tukiona na- 10
fasi, tutende mema kwa wote, kwanza kwao walio wa
nyumba ya imani.

Mwaona kwa harufi gani kubwa nimewaandikia 11
kwa mkono wangu mimi.

Watakao kuonekana vema katika mwili, ndio wawa- 12
shurutishao ninyi mtahiriwe, wasifukuzwe tu kwa
ajili ya msalaba wake Masiya. Wala waliotahiriwa, 13
hawa sheria hawaishiki, illa wataka ninyi mtahiriwe,
wapate kujisifu kwa mwili wenu. Hasha, nisijisifu mi- 14

- mi, isipokuwa kwa ajili ya msalaba wa Bwana wetu Isa Masiya, kwa huo dunia imesulibishwa kwangu, na mimi
 15 kwa dunia. Kwani katika Masiya Isa tohara si kitu,
 16 wala ngovi, illa kiumbe kipya. Nao wafuatao kawaida hii, imani kwao na rehema, na kwa Israeli wake Muungu.
- 17 Baada ya haya mtu asinitie taabu: kwani mimi nachukua mwilini mwangu alama zake Masiya.
- 18 Neema ya Bwana wetu Isa Masiya pamoja na roho yenu, ndugu. Amina.

WARAKA WA PAOLO MTUME

KWA

WAEFESI.

- 1 PAOLO, mtume wa Isa Masiya kwa mapenzi yake Muungu, kwa watakatifu walioko katika Efesi, nao
 2 wanaomwamini Masiya Isa: Neema kwenu na amani kwa Muungu Baba wetu na Bwana Isa Masiya.
- 3 Abarikiwe Muungu na Baba wake Bwana wetu Isa Masiya, aliyetubariki kwa mibaraka yote ya roho katika
 4 mbinguni, katika Masiya: kama alivyotuchagua katika huyu mbele ya kuwekwa ulimwengu, tuwe watakatifu
 5 wasio hatiya mbele yake katika mapenzi: akiwa ametuweka tumfanyikie watoto kwa Isa Masiya kwa mapenzi
 6 ya kutaka kwake, usifiwe utukufu wa neema yake, kwayo ametukubalikisha sisi kwa Mpenzi. Kwa huyo tunao
 7 wokovu kwa damu yake, masamehe ya thambi, kwa
 8 wingi wa neema yake, aliyotuzidishia katika hekima yote
 9 na busara, akiwa ametujulisha siri ya kupenda kwake,
 10 kwa mapenzi aliyoyakusudia mwenyewe, kwamba katika kuamria wakati mkamilifu avikusanye vitu vyote pamoja
 katika Masiya, navyo vilivyoko mbinguni, navyo vilivyo
 11 ulimwenguni; katika huyu, kwa huyo nasi tumepata urithi, tukiwekwa kwa kusudi lake ayafanyaye yote kwa
 12 shauri la kupenda kwake; tuwe sisi kwa sifa za utukufu
 13 wake, tuliotangulia kumwamini Masiya. Katika huyo nanyi tena, mkiisha kulisikia neno la kweli, anjili ya wo-

kovu wenu. Katika huyo tena, mkiisha kumwamini, mkatiwa muhuri na Roho yule Mtakatifu wa ahadi, aliye arabuni ya urithi wetu, hatta ukombozi wa mali ili- 14
yonunuliwa, kwa sifa za utukufu wake.

Kwa sababu hiyo nami tena, nikipata habari za imani 15
yenu katika Bwana Isa, na kuwapenda watakatifu wote, siachi kuwashukuria, nikiwanena katika sala zangu; 16
Muungu wa Bwana wetu Isa Masiya, Baba wa utukufu, 17
awape roho ya hekima na ufunuo katika kumjua; macho 18
ya akili zenu yakipewa nuru, mjue nini tumaini la wito wake, na nini utajiri wa utukufu katika urithi wake kwao watakatifu, na nini ukuu bora wa uwezo wake kwetu 19
tutumainio, kwa kutenda kwa nguvu zake hodari, alizo- 20
tenda katika Masiya, alipomtoa katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika mbinguni, juu sana ku- 21
liko ufaume wote, na uwezo, na nguvu, na mamlaka, na killa jina litajwalo, si ulimwenguni humo tu, illa mle utakaokuja: akayaweka yote chini ya nyayo zake, aka- 22
mtoa kitwa cha juu yote kwa kanisa, ndilo mwili wake, 23
kujaa kwake ayajalizaye yote katika yote.

NANYI, mliokuwa wafu katika makosa na thambi, 2
mlioendea zamani kwa mwendo wa dunia hii, kwa 2
mfalme wa nguvu za anga, roho atendaye sasa katika watoto wa kuasi; pamoja nao nasi sote tukaenenda za- 3
mani, katika tamaa za mwili wetu, tukizitimia ngoa za mwili na za nia, tukawa kwa asili watoto wa ghathabu, kama nao wangine. Lakini Muungu aliye na rehema 4
nyingi, kwa mapenzi yake mengi alivyotupenda, hatta 5
tulipokuwa tumekufa katika thambi, ametufufua pamoja naye Masiya (kwa neema mmeokoka), akainua 6
pamoja akakalisha pamoja katika mbinguni katika Masiya Isa: illi kwa zamani zitakazokuja aonyeshe wingi wa 7
mali wa neema yake, kwa wema kwenu kwa Masiya Isa. Kwani kwa neema mmeokoka, kwa imani; wala si kwa 8
ninyi wenyewe; aliyetoa ndiye Muungu: wala si kwa 9
matendo, mtu asijisifu. Kwani sisi kazi yake, tumeu- 10
mbwa katika Masiya Isa kwa matendo mema, Muungu aliyotangulia kuyaamuru, tuyaendee.

Kumbukeni tena, kama ninyi zamani, mataifa kwa 11
mwili, mnaoitwa Wenyi ngovi kwao wanaoitwa Tohara, katika mwili, kwa mikono; kama zamani zile hamkuwa 12
naye Masiya, mkiwa wageni katika jamii ya Israeli,

msio katika maagano ya ahadi, msiotumaini, msio na
 13 Muungu duniani. Lakini sasa katika Masiya Isa ninyi
 mliokuwa mbali mmeletwa karibu kwa damu yake
 14 Masiya. Kwani ndiye amani yetu, aliyefanya wote moja,
 15 aliyevunja ukuta wa kati wa kupambanua, akiuondoa
 katika mwili wake wadui, sheria ya amri katika taratibu;
 afanye katika mwenyewe kwa wawili mtu mpya
 16 mmoja, akifanya amani; awapatanishe wote kwa Muungu
 katika mwili mmoja kwa msalaba, akiwa ameuua
 17 wadui kwao: akaja akawahubiria amani walio mbali, nao
 18 walio karibu. Kwani kwaye wote tumepata kumkaribia
 Baba kwa Roho mmoja.

19 Bassi sasa ninyi si wageni, wala waliotoka mbali, lakini
 watu wa kwao watakatifu, na katika nyumba yake Muungu,
 20 mmejengwa juu ya misinji yao mitume na nabii,
 21 Isa Masiya mwenyewe akiwa jiwe kuu la pembeni. Katika
 huyu jengo lote likiungwa vema hupata kuwa hekalu
 22 takatifu katika Bwana; katika huyu mmejengwa pamoja
 kuwa masikani ya Muungu kwa Roho.

3 KWA sababu hiyo mimi Paolo, mfungwa wake Isa
 2 Masiya kwa ninyi wa mataifa,—kama mmesikia uwakili
 3 wa neema yake Muungu niliopewa kwenu, kama kwa
 kufunua amenijulisha siri (kama nilivyoandika mbele
 4 kwa maneno machache, mkiyasoma mtajua maarifa yangu
 5 katika siri yake Masiya) isiyojulikana zamani na waana
 Adamu kama sasa wamefunuliwa mitume wake watakatifu
 6 na nabii kwa Roho; kama mataifa warithi pamoja katika
 mwili mmoja, wakashariki ahadi zilizo katika
 7 Masiya kwa anjili. Nami mngoje wake kwa kupewa
 neema ya Muungu, niliyoipokea kwa kutenda kwa nguvu
 kwa uwezo wake.

8 Mimi, niliye mdogo kuliko mdogo wa watakatifu wote,
 nimepewa neema hii, niwahubirie mataifa mali yake Masiya
 9 yasiyotafutikana; niwajulishe wote usharika wa siri
 iliyostirika tangu mwanzo wa ulimwengu katika Muungu,
 10 aliyeviumba vyote; kwa kusudi sasa ufaume na uwezo
 wa mbinguni ujue kwa kanisa hekima nyingi za
 11 Muungu, kwa nia ya milele, aliyoinuia katika Masiya
 12 Isa Bwana wetu; naswi kwa huyu tunao uthabiti na
 13 kumwendea kwa tumaini kwa imani yake. Kwa hiyo nataka
 msizimie kwa mateso yangu kwa ajili yenu, ndiyo utukufu wenu.

Kwa sababu hiyo nampigia magote Baba yake Bwana 14
 wetu Isa Masiya, kwa huyu jamii yote ya mbinguni na 15
 duniani imetajwa, awajalie kwa wingi wa utukufu wake, 16
 mtiwe nguvu na uwezo kwa Roho yake katika mtu wa
 ndani; Masiya akae mioyoni mwenu kwa imani; illi 17
 ninyi, mkiwa na mashina na misinji katika kupenda,
 mpate kushika pamoja na watakatifu wote upana na 18
 urefu na kwenda chini na kwenda juu, mkayajue ma- 19
 penzi yake Masiya yapitayo kujulikana, mpate kujaa ujao
 wake Muungu.

Bassi yeye awezaye kufanya sana, kuliko yote tutakayo 20
 ao tuwazayo, kwa nguvu zifanyazokwetu, yeye atukuzwe 21
 katika kanisa kwa Masiya Isa zamani zote maisha na
 milele. Amina.

NAMI, mfungwa wake Bwana, nawasihi, mwenende 4
 kama ilivyopasa wito mlivyoitiwa, kwa unyenyekevu wote 2
 na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika kupe-
 ndana, mkifanya bidii kuushika umoja wake Roho katika 3
 mafungo ya amani. Mwili mmoja, na Roho mmoja, 4
 kama mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.
 Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, mmoja 5
 Muungu na Baba wetu wote, aliye juu yote, na kwa 6
 yote, na katika ninyi nyote. Lakini killa mmoja 7
 tumepewa neema kwa kadiri ya kutoa kwake Ma-
 siya.

Kwa haya akanena, Alipopanda juu akafunga kufu- 8
 nga, akawatolea watu. Bassi akipanda, nini illa aka- 9
 shuka kwanza hatta sehemu za chini za ulimwengu?
 Aliyeshuka ndiye aliyepanda juu, juu sana kuliko mbi- 10
 ngu zote, vitu vyote vijae yeye. Akawatoa, wengine 11
 mitume, na wengine nabii, na wengine waanjilisti, na
 wengine wachunga na waalimu, wakamilike watakatifu, 12
 ungoje utendeke, mwili wake Masiya ufanyiziwe: hatta 13
 tutakapofika wote katika umoja wa imani, na katika
 kumjua Mwana wa Muungu, kuwa watu wakamilifu,
 kwa cheo cha ukubwa wa kujaa kwake Masiya; tusiwe 14
 tena watoto, tukitupwa huko na huko, tukichukuliwa na
 killa upepo wa elimu, kwa hila ya watu, mashauri ya
 werevu waoteavyo wadanganye; lakini mkiwa na kweli 15
 katika kupendana, mkue pia katika yeye, aliye kitwa,
 Masiya. Katika huyu mwili wote ukiungana vema, 16
 ukiwa imara kwa riziki za viungo vyote, kwa kutenda

sana katika kadri ya sehemu yote, mwili ukue, ujijenge katika kupenda.

17 Haya nayasema, nayashuhudu tena katika Bwana, msinde tena kama mataifa wangine waendavyo, katika
18 nia zao zisizofaa, akili zikitiwa giza, wakifarakana na uzima wake Muungu kwa ujinga ulio kwao kwa sababu
19 ya ufaganzi wa moyo wao; wakiwa wamepita kuona wamejitoa katika asharati, wayatende yaliyo machafu
20 kwa kutamani. Lakini ninyi hamkujifunza hivi Masiya; 21 mkiwa mmemsikia, mkafundishwa naye kama kweli
22 ilivyo katika Isa; mvue katika desturi za kwanza mtu
23 wa zamani, alieoza kwa tamaa zidanganyazo; mkafa-
24 nyike wapya katika roho ya nia zenu, mvae mtu mpya, aliyeumbwa kwa Muungu katika haki na utakatifu na kweli.

25 Acheni uwongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake:
26 kwani sisi viungo vya wenzetu. 'Mwe na hasira, wala
27 msifanye thambi: jua lisichwe juu ya ghatthabuyenu; wala
28 msimpe nafasi shetani. Aliyekwiba asiibe tena; illakini atende kazi, akiyafanya na mikono yake yaliyo mema,
29 apate kuwa na kitu cha kumpa ahitajiye. Mazumgumzo maovu yasitoke kanwani mwenu, illa yaliyo mema
30 kwa kujengea, yawalettee neema wasikiao. Wala msi-
mhuzunishe Roho yule Mtakatifu wa Muungu, aliyewatia muhuri kwa siku ya ukombozi.

31 Uchungu wote, na ghatthabu, na hasira, na makelele, na matukano, yawaondokelee mbali, na maovu yote:
32 mkawe wema ninyi kwa ninyi, wenyi moyo mwororo, mkisameheana, kama Muungu kwa ajili yake Masiya amewasamehe ninyi.

5 MFUATENI Muungu kama watoto wanaopendwa;
2 mkaende katika kupenda, kama Masiya alivyotupenda sisi, akajitoa kwa sisi sadaka na thabihu kwa Muungu
3 kuwa nukato lililo zuri. Lakini asharati, na uchafu wote, na kutamani, kusinenwe kabisa kwenu, kama ili-
4 vyowapasa watakatifu; wala aibu, wala mazumgumzo yasiyo na akili, wala ubishi usiofaa: illakini kushukuru.
5 Kwani mwajua kama hapana mwasharati, wala mtu mchafu, wala mtu wa tamaa, ndiye kafiri, aliye na
6 urithi katika ufalme wa Masiya na Muungu. Mtu asi-wadanganye kwa maneno yasiyofaa: kwani kwa sababu ya haya hasira yake Muungu huwafikia waana wa kuasi.

Msisharikiane nao. Kwani zamani mlikuwa giza, lakini 7
 sasa nuru katika Bwana : mwende kama watoto wa nu- 8
 ru (kwani zao la Roho katika wema wote na haki na 9
 kweli), mkiyakinisha yampendezayo Bwana. Wala 10
 msisharikiane nayo matendo yasiyozaa ya giza, illakini 11
 mkataze. Kwani aibu hatta kuyanena wayafanyayo 12
 kwa siri. Lakini mambo yote yaliyokatazwa huone- 13
 kana kwa nuru : kwani killa ionyayo ndiyo nuru. Hivi 14
 hunena, Amka, ulalaye, ufufuke katika wafu, Masiya 15
 atakupa nuru. Angalieni mwenende kwa kufikiri, si 16
 kama wapumbafu, illakini kama wenyi akili ; mkiuko- 16
 mboa wakati, kwa sababu siku zinao uovu. Msiwe 17
 wasiofikiri, illa wayakumbukao Bwana ayapendayo.

Msilewe na mvinyo, pasimo kiasi, lakini mjae Roho ; 18
 mkisema na nafusi zenu kwa zaburi, na utenzi, na 19
 nyimbo za rohoni, mkiimba mkamfanyia Bwana sauti
 nzuri moyoni mwenu ; mkiimshukuru siku zote kwa 20
 mambo yote Muungu na Baba, kwa jina lake Bwana
 wetu Isa Masiya ; mkitiiana ninyi kwa ninyi katika 21
 hofu ya Muungu.

Wake, 'mwatii waume wenu ninyi, kama kwa Bwana. 22
 Kwani mume ni kitwa chake mwanamke, kama Masiya 23
 ni kitwa chake kanisa, naye mwokozi wake mwili.
 Kama kanisa humtii Masiya, nao wake waume wao 24
 kwa mambo yote.

Waume, 'mwapende wake wenu, kama Masiya ali- 25
 vyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake, alitakase 26
 akalifishe kwa kuosha na maji kwa neno, ajiletee 27
 kanisa tukufu pasipo mawaa, wala kufinya, wala taka
 lo lote, illa liwe takatifu na pasipo ila. Imewapasa 28
 waume kuwapenda wakeo kama miili yao. Ampendaye
 mkewe, hujipenda mwenyewe. Kwani hapana mtu 29
 aliyeuchukia mwili wake ; lakini huulisha, huutunza,
 kama Bwana kanisa ; kwani sisi viungo vya mwili 30
 wake, vya nyama yake, vya mifupa yake. Kwa sa- 31
 babu hiyo mtu atamwacha babaye na mama, ataungana
 na mkewe, nao wawili watakuwa mwili mmoja. Hii 32
 ndiyo siri kuu : lakini namnena Masiya na kanisa.
 Illakini killa mmoja wenu ampende mkewe kama mwe- 33
 nyewe ; na mke amheshimie mume.

WATOTO, 'mwatii wazee wenu katika Bwana, kwani 6
 ndiyo haki. Mheshimie baba yako na mama (ndiyo 2

- 3 amri ya kwanza yenyi ahadi), mpate heri, mkakae sana katika ulimwengu.
- 4 Nanyi, baba, msiwatie watoto wenu hasira, lakini 'mwalee katika adabu na elimu yake Bwana.
- 5 Watumwa, 'mwatii walio bwana katika mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa moyo mmoja, kama kwa
- 6 Masiya; wala si kwa utumwa wa machoni kama wapendezao waana Adamu; lakini kama watumwa wake Masiya, mkitenda kwa moyo aliyoyapenda Muungu;
- 7 mkitumika kwa nia njema, kama na Bwana, wala si na
- 8 mwana Adamu: mkijua kama killa alitendalo mtu jema atapewa na Bwana, akiwa mtumwa ao akiwa huru.
- 9 Nanyi, bwana, 'mwatendee vivyo, msiogofye; mkijua kama yuko mbinguni aliye bwana na wao na wenu, wala kwake mwana Adamu hakubaliki kwa cheo chake.
- 10 Mwisho, ndugu zangu, 'mwe hodari katika Bwana,
- 11 na katika uwezo wa nguvu zake. Mvae selaha zote za Muungu, mpate kusimama katika hila zake shetani.
- 12 Kwani hatupigani na mwili na damu, illa na ufaume na nguvu, nao wakuu wa giza hili, nao roho za uovu
- 13 walio juu. Kwa hiyo mtwae selaha zote za Muungu, 'mweze kusimama katika siku ya uovu, na mkiyashinda yote kusimama.
- 14 Simameni tena, mmefunga viuno vyenu kwa kweli,
- 15 mkivaa kifuani haki, na katika miguu kuwa tayari
- 16 kwa anjili ya amani; juu yote mkitwaa ngao ya imani, kwa hiyo mtaweza kuizimia mishale yote ya moto yake
- 17 mwovu: mkapokee kofia ya wokovu, na upanga wa
- 18 Roho, ndio neno lake Muungu: mkiomba sikuzote na kuomba kwote na kusihi katika Roho, mkakeshe kwa hiyo na kudumu kwote, na kuwaombea watakatifu wote,
- 19 na mimi, nipewe kunena, nifunue kanwa langu kwa
- 20 uthabiti, niijulisha siri ya anjili, nikiwa mpelekwa wake katika mafungo; nipate kuthubutu kuinena, kama ilivyonipasa kunena.
- 21 Illakini mpate kuyajua mambo yangu ni hali gani, Tukiko, ndugu mpendwa na mngoje amini katika
- 22 Bwana, atawajulisha mambo yote: niliyempeleka kwenu makusudi mpate kuyajua mambo yetu, akawafariji ninyi moyo.
- 23 Amani kwa ndugu, na mapenzi pamoja na imani, ka-
- 24 tika Muungu Baba na Bwana Isa Masiya. Neema kwao wote wampendao Bwana wetu Isa pasipo hila. Amina.

WARAKA WAKE PAOLO MTUME

KWA

WAFILIFI.

PAOLO na Timoteo, watumwa wake Isa Masiya, kwa 1
 watakatifu wote katika Masiya Isa walioko katika Filifi,
 pamoja nao maaskafu na wangoje: Neema kwenu na 2
 amani katika kwa Muungu Baba wetu na Bwana Isa
 Masiya. Namshukuru Muungu wangu killa niwaku- 3
 mbukapo, sikuzote katika killa kuwaombea nataka kwa 4
 furaha, kwa sababu ya usharika wenu katika anjili tangu 5
 siku ya kwanza hatta leo. Niliaminilo ndilo hili, kama 6
 yeye aliyeanza jambo jema kwenu atalitimiza hatta siku
 yake Isa Masiya: kama ilivyonipasa kuwathania haya 7
 nyote, kwani ninanyi moyoni mwangu, kwa sababu
 katika kufungwa kwangu, na katika kuilinda na kui-
 fanya imara anjili, mmesharikiana nyote nami katika
 neema. Muungu ndiye ajuaye, ginsi niwatamanivyo 8
 nyote katika moyo wake Isa Masiya. Ndilo niliombalo, 9
 kupenda kwenu kuzidi na kuzidi katika maarifa na
 hukumu yote; mpate kuyakubali yaliyo bora; 'mwe 10
 safi na wasiochukiza hatta siku yake Masiya, mkijaa zao 11
 la haki iliyo kwa Isa Masiya, kwa utukufu na kwa sifu
 zake Muungu.

Lakini nataka mjue, enyi ndugu, ya kwamba ma- 12
 mbo ya kwangu yametoka kama kwa kuieneza anjili;
 hatta kufungwa kwangu katika Masiya kumeonekana 13
 katika nyumba yote ya mfalme, na panginepo pote.
 Nao wengi ndugu katika Bwana, wakitumaini kwa 14
 kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kulitoa
 neno pasipo hofu.

Wangine wamkena Masiya na kwa hasidi na ugomvi; 15
 nao wangine kwa moyo. Hawa humkena Masiya kwa 16
 ugomvi, wala si kwa moyo, wakithani kuniongezea ma-
 teso nikifungwa; wale kwa kupenda, wakinjua nimewe- 17
 kwa kuilinda anjili. Nini tena? Kwa njia zote, na 18
 katika kujifanya na katika kweli, Masiya anenwa; nami

- 19 nafurahi, wa inna nitafurahi. Kwani najua kama haya
 yatageuka kwa wokovu wangu, kwa kuomba kwenu,
 20 na kuleta Roho yake Isa Masiya, kama nilivyotazamia
 sana nikatumaini, nisiaibike kabisa, illa kwa uthabiti
 wote, kama sikuzote, sasa tena, Masiya atukuzwe
 kwa mwili wangu, ikiwa kwa maisha, ao kwa kufa.
 21 Kwani kwangu kuishi Masiya, na kufa fayida. Niki-
 22 shi mwili ndio zao la kazi yangu, illa kunathiri sijui.
- 23 Ni katika shidda, nikatamani niende zangu nikae naye
 24 Masiya; ndio bora sana: lakini kuishi mwili kuwafaa
 25 ninyi. Nami nikitumaini hivi, najua kama nitaishi,
 26 nitakaa nanyi, mzidi mkafurahi katika imani; furaha
 zenu zinongezekee katika Isa Masiya nikifika tena
 kwenu.
- 27 Illa mwendo wenu uwe kama ilivyopasa anjili yake
 Masiya: nikija niwaone, ao nisiwepo niyasikie mambo
 yenu, kama mmesimama imara katika roho moja, kwa
 28 nia moja mkishindana nyote kwa imani ya anjili, wala
 hamkuwaogopa adui zenu: waliyoiona dalili wazi ya
 kupotea, lakini kwenu ya wokovu, nao wake Muungu.
 29 Kwani mmepewa kwa ajili yake Masiya mwamini,
 30 mkateswe tena kwa ajili yake: mkiwa na pigano lilelile
 mliloliona kwangu, mkanisikilia.
- 2** IKIWA faraja katika Masiya, yakiwa matulizo ya
 mapenzi, ukiwa usharika wa Roho, ukiwa moyo na
 2 rehema, jalizeni furaha yangu, 'mwe na moyo mmoja,
 3 mkipenda mamoja, mkipatana, mkitaka mamoja. Li-
 siwe neno kwa ugomvi na kujisifu, illa kwa moyo usio-
 tukuka killa mtu awaone wangine wakuu kuliko yeye.
- 4 Msiyaangalie killa mtu mambo yake yeye, illa killa
 5 mtu na mambo yao wangineo. Mpate ninyi nia ileile
 6 aliyo nayo Masiya Isa: yeye, akiwa kwa mfano wa
 Muungu, hakuiona mateka kuwa sawa na Muungu,
 7 lakini amejifanya hana utukufu, akajitwalia mfano wa
 mtumwa, akafanyika kwa namna ya mwana Adamu;
 8 naye akionwa kwa namna ya mwana Adamu, akajithili,
 9 akatii hatta kufa, hatta kufa kwa msalaba. Kwa hiyo
 Muungu amemtukuza sana, akampa jina kuliko jina lo
 10 lote, kwa jina lake ISA killa gote liiname, la mbingu-
 11 ni, la duniani, la chini ya dunia, killa ulimi ukaungame
 kama Isa Masiya ndiye Bwana, kwa utukufu wake
 Muungu Baba.

Kwa sababu hiyo, wapenzi wangu, kama mlivyotii 12
sikuzote, si mimi nikiwapo tu, illa zayidi sasa mimi
siwepo, mtende wokovu wenu kwa kuogopa na kutete-
meka; kwani Muungu ndiye atendaye ndani yenu na 13
kutaka na kufanya, kwa mapenzi.

Myatende mambo yote pasipo kunong'oneza wala 14
kugombana; msiwe na laumu wala kuthuru, watoto 15
wake Muungu wasionenewa, kati ya taifa lililopotoka
na kaidi, mwangazamo ninyi kama nuru za ulimwengu,
mkilitoa neno la uzima; nifurahi siku ya Masiya, siku- 16
piga mbio burre, wala sikutenda kazi burre. Nami 17
nikitolewa juu ya thabihu na utumwa wa imani yenu,
nafurahi, nikapendezewa pamoja nanyi nyote. Kwa 18
sababu ileile furahini nanyi, mkapendezewe pamoja
nami.

Naamini kwa Bwana Isa nimpeleke kwenu karibu 19
Timoteo, nifarajike na mimi nikiwajua hali yenu. Sina 20
mtu wa nia moja, aangaliaye hali yenu mwenyewe.
Kwani wote wayataka yaliyo yao, wala siyo yaliyo yake 21
Masiya Isa. Lakini mmemjua huyu mathubutu, kama 22
ametumika nami katika anjili kama mwana na babaye.
Huyu nataraja nimpeleke marra, nikiisha kuyajua yata- 23
kayonipata. Illa naamini kwa Bwana nitakuja na 24
mwenyewe karibu.

Lakini nimeona wàjib niwapelekee Epafrodito, ndugu 25
yangu na mwenzangu katika kazi, na asikari pamoja
nami, lakini mtume wenu na wakili wa riziki zangu.
Kwani amewatamani ninyi nyote, akahuzunika kwa 26
sababu mmesikia kama amekuwa havezi. Kwani ndi- 27
vyo alikuwa havezi, karibu na kufa: illakini Muungu
akamhurumia; wala si yeye peke yake, illa mimi tena,
nisione huzuni juu ya huzuni. Nikazidi kumpeleka 28
kwa tunza, ili mkimwona tena mfurahi, nami huzuni
yangu ipunguke. Mpokeeni katika Bwana kwa furaha 29
yote, mkawaone kama huyu katika sifa: kwa sababu 30
kwa kazi yake Masiya akakaribia kufa, asipoangalia
maisha yake, atimize iliyohitajia kwenu.

HATIMA, ndugu zangu, furahini katika Bwana. 3
Kuwaandikia yaliyo mamoja, kwangu si taabu, kwenu
salama. Mwangalie mbwa, 'mwaangalie watendao ma- 2
baya, 'mwaangalie wakatao. Kwani ndisi waliotahiri- 3
wa, tumwabuduo Muungu kwa Roho, tukafurahi katika

- 4 Isa Masiya, wala hatuutumainia mwili. Lakini ninge-
weza kuutumainia mwili. Mtu wo wote akijiona analo
5 la kutumainia katika mwili, mimi zayidi : nimetahiriwa
siku ya nane, wa taifa la Israeli, wa kabila ya Benya-
min, Mwebrania wa Waebrania, kwa sheria Farisayo,
6 kwa uwivu mfukuza kanisa, kwa haki iliyo kwa sheria
7 nisiye hatiya. Lakini mambo yaliyokuwa kwangu fa-
8 yida, nayaona hasara kwa Masiya. Wa inna nayaona
mambo yote hasara kwa uzuri wa kumjua Isa Masiya
Bwana wangu : kwa sababu yake nimepata mambo yote
yapotee, nikayathania kama mavi, nimpate Masiya,
9 nikaonwe katika yeye, nisiwe na haki yangu iliyo kwa
sheria, illa ile iliyo kwa imani yake Masiya, haki iliyo
10 ya Muungu kwa imani : nimjue yeye, na uwezo wa
kufufuka kwake, na usharika wa mateso yake, nikifa-
11 nana na kufa kwake ; nipate kwa njia yo yote kuufika
12 ufufuo wa wafu. Si kama nimekwisha fika, ao nime-
kuwa mkamilifu : lakini nafuatafuata illi niyashike kwa
sababu yao nimeshikwa na Masiya Isa.
- 13 Ndugu, sijithanii nimekwisha shika : lakini moja tu,
nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo
14 mbele, nakaza mwendo kufika alama ya thawabu ya wito
mkuu wa Muungu katika Masiya Isa.
- 15 Nasi, tulio wakamilifu, tuyawaze haya : nanyi mkiya-
waza mangineyo yote, Muungu atawafunulia na hayo.
16 Illakini tulipofika twenende kwa kanuni moja, tuyanue
17 mamoja. Ndugu, mfuata pamoja nami, mkawaangalie
18 waendao kama mnasi sisi kwa mfano. Kwani waendao
wengi, niliowaambia marra nyingi, hatta sasa nawaa-
19 mbia kwa kulia, maadui ya msalaba wake Masiya : mwi-
sho wao uharibifu, muungu wao tumbo, utukufu wao
20 aibu, wawazao mambo ya duniani. Kwani sisi watu wa
mbinguni ; huko tunamtazamia Mwokozi, Bwana Isa
21 Masiya : atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate
kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uwezo awe-
zavyo kuvitiisha na vitu vyote chini yake.
- 4 BASSI, ndugu zangu, wapenzi wangu, niwatamano,
furaha yangu na taji, simameni imara katika Bwana,
wapenzi wangu.
- 2 Namsihi Euodia, namsihi Suntuke, wayawaze mamoja
3 katika Bwana. Nakutaka wewe tena, mjoli wangu wa
kweli, uwasayidie waanawake waliotenda kazi pamoja

nami katika anjili, na Klemente tena, nao wangine watenda kazi nami, majina yao katika kitabu cha uzima.

Furahini katika Bwana sikuzote: tena nasema, Fura- 4
hini. Kiasi chenu kijulikane na watu wote. Bwana 5
yupo. Msitaabike kwa neno; lakini kwa neno lo lote 6
kwa kuomba na kusihi, pamoja na kushukuru, haja zenu
zijulikane na Muungu. Na amani yake Muungu ipitayo 7
akili zote itawalinda mioyo na nia kwa Masiya Isa.
Hatima, ndugu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote 8
yawapasayo, yo yote ya haki, yo yote safi, yo yote ya
kupendeza, yo yote yenyi heshima; ukiwa wema, ikiwa
na sifa, myawaze haya. Mambo mliyojifunza, mkapo- 9
kea, mkasikia, mkaona kwangu, myatende: naye Mu-
ungu wa amani atakaa kwenu.

Nikafurahi sana katika Bwana kwamba sasa kwa 10
mwisho tunza lenu kwangu limesitawi; nanyi mka-
tunza, lakini mkataka nafasi. Sineni kama kwa kutaka: 11
kwamba nimejifunza, hali yangu ikiwa yote, kuwa rathi.
Najua na kuthilika, najua na kufanikiwa: po pote na 12
katika mambo yote nimefunzwa na kushiba na kuwa na
njaa, na kujaliwa na kupatwa na shidda. Nayaweza 13
yote kwa Masiya anitiaye nguvu. Illakini mmetenda 14
vema mkisharikiana na mateso yangu. Bassi, enyi 15
Wafilipi, jueni tena, kama mwanzo wa anjili, nilipotoka
katika Umakedoni, hapana kanisa waliosharikiana nami
kwa kutoa na kupewa, illa ninyi peke yenu. Hatta 16
katika Thessalonika mkapeleka marra na marra kwa
kuhitaji kwangu. Si kwa sababu nataka zawadi; lakini 17
nataka mazao yaongezeke kwa hesabu yenu.

Lakini ninayo yote, nikafanikiwa: nimeshiba, nime- 18
pokea kwa Epafrodito vitu vya kwenu, manukato ya
kunuka vema, sadaka ya kukubalika ya kumpendeza
Muungu. Naye Muungu wangu atawaruzukia killa 19
mnachohitajia kwa utajiri wake katika utukufu kwa
Masiya Isa. Sasa kwa Muungu na Baba wetu utukufu 20
milele na milele. Amina. Mmsalimie killa mtakatifu 21
katika Masiya Isa. Ndugu waliopo nami wawasalimia.
Watakatifu wote wawasalimia, wa kwanza walio nyu- 22
mbani mwa Kaisari. Neema ya Bwana wetu Isa Ma- 23
siya nanyi nyote. Amina.

WARAKA WA PAOLO MTUME

KWA

WAKOLOSSAI.

- 1 PAOLO, mtume wa Isa Masiya kwa mapenzi ya
 2 Muungu, na Timoteo ndugu, kwa watakatifu nao
 ndugu wenyi imani katika Masiya walioko Kolossai:
 Neema kwenu na amani ya Muungu Baba wetu.
- 3 Twamshukuru Muungu na Baba wake Bwana wetu
 4 Isa Masiya, sikuzote tukiwaombea ninyi, tukisikia
 imani yenu katika Masiya Isa, na upendano kwa wata-
 5 katifu wote, kwa tumaini lililowekwa mbele yenu katika
 mbingu, mlilosikia kwanza katika neno la kweli yake
 6 anjili, iliyoko kwenu, kama katika ulimwengu wote,
 ikizaa matunda, ikazidi, kama kwenu tangu siku mlipo-
 sikia mkatambua neema ya Muungu katika kweli;
 7 kama mmefundishwa na Epafra mjoli wetu mpendwa,
 8 aliye kwenu mngoje amini wake Masiya, aliyetuthihi-
 rishia sisi mapenzi yenu ya Rohoni.
- 9 Kwa hiyo na sisi, tangu siku tuliposikia, hatuachi
 kuwaombea, tukisihi mjae maarifa ya mapenzi yake,
 10 katika hekima yote na ukumbuko wa rohoni, mwenende
 ninyi nyote kama Bwana alivyostahili kwa kupendeza
 kwote, mkitoa matunda katika killa tendo jema, mka-
 11 zidi katika maarifa ya Muungu; mkiweza kwa uwezo
 wote kwa nguvu za utukufu wake, kwa uvumilivu wote
 12 na kustahimili furahani; mkimshukuru Baba, aliyetu-
 wezesha sehemu ya urithi wao watakatifu katika nuru;
 13 aliyetuokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha hatta
 14 ufalme wa Mwana wa mapenzi yake; katika huyo tu-
 15 nao ukombozi, ndio ondoleo la thambi: aliye mfano wa
 Muungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza kuliko viu-
 16 mbe vyote; kwamba katika huyo yote yameumbwa, ya-
 liyo mbinguni na yaliyo katika inchi, yaliyoonekana na
 yasiyoonekana, kama viti, kama kumiliki, kama ukuu,

kama nguvu ; yote yameumbwa naye na kwa yeye ;
naye aliye mbele yao yote, na yote yaishi kwa yeye. 17

Naye ni kitwa cha mwili, cha kanisa : aliye mwanzo, 18
wa kwanza katika wafu ; apate kuwa katika yote ata-
nguliaye : kama katika yeye imependeza kukaa killa 19
kujaa ; na kwa yeye kupatanisha yote katika yeye, aki- 20
fanya amani kwa damu ya msalaba wake ; kwa yeye,
yakiwa katika inchi, yakiwa mbinguni.

Na ninyi, mliokuwa mmefarakana na adui katika 21
akili, kwa matendo yaliyo mabaya, sasa amewapata-
nisha katika mwili wa nyama yake kwa kufa, awalete 22
ninyi watakatifu pasipo laumu, pasipo mshtaki, mbele
yake : mkikaa tu katika imani, mkiwa na misinji na 23
imara, wala msiotikisika katika tumaini la anjili mliyo-
isikia, iliyohubiriwa kwa killa kiumbe kilicho chini ya
uwingu ; na mimi Paolo mngoje wake.

Sasa nafurahiwa na kuumwa kwa ajili yenu, nikija- 24
liza yaliyosalia ya mateso yake Masiya katika mwili
wangu kwa ajili ya mwili wake, ndio kanisa ; nami 25
nimekuwa mngoje wake, kwa uwakili wa Muungu, nilio-
pewa kwenu, nilitimize neno la Muungu, siri iliyofichwa 26
tangu zamani, na tangu vizazi, illa sasa imethahirishwa
kwa watakatifu wake, akapenda Muungu kuwajulisha, 27
nini utajiri wa utukufu wa siri hii kwa mataifa, ndiye
Masiya kwenu, tumaini la utukufu : tumhubiriye, tuki- 28
mwonya killa mtu, tukimfundisha killa mtu katika he-
kima yote, tupate kumleta killa mtu mtimilifu katika
Masiya ; kwa hiyo nafanya bidii, nikijitahidi kwa 29
uwezo utendao katika kwangu kwa nguvu.

NINGEPENDA mjue bidii gani niifanyayo kwa 2
ajili yenu, nao wa Laodikiya, nao wasioniona uso wa
mwili ; mioyo yao wafarajike, wakiambatana katika 2
upendano, na kwa utajiri wote wa kuwa yakini kwa
akili, kwa maarifa ya siri yake Muungu, ya Baba, na
ya Masiya, katika huyo ziko hazina zote za hekima na 3
za elimu zimestirika.

Ndilo ninenalo, mtu asipate kuwadanganya kwa ma- 4
neno ya kushawishi. Kwani nikiwa kwa mwili sipo, 5
kwa roho nipo pamoja nanyi, nikifurahi nikiona utara-
tibu wenu, na imara ya imani yenu iliyo kwa Masiya.
Kama mliyompokea Masiya Isa Bwana, mwenende ka- 6
tika yeye, mkiwa na shina na misinji katika yeye, mki- 7

fanyika imara katika imani kama mlivyofundishwa, mkizidi katika shukrani.

- 8 Angalieni mtu asiwafanye mateka yake kwa filsofia na madanganya matupu, kwa mapokeo ya watu, kwa
 9 asili ya dunia, wala si kwa Masiya: kwamba katika yeye hukaa kujaa kwote kwa Muungu katika mwili.
- 10 Nanyi mwajaa katika yeye, aliye kitwa cha mamlaka
 11 yote na uwezo: katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyo kwa mkono, katika kuvua mwili wa thambi za
 12 nyama, katika tohara yake Masiya, mkizikwa pamoja naye katika ubatizo, mlipofufuka tena kwa imani ya
 13 nguvu za Muungu, aliyemfufua katika wafu. Nanyi, mkiwa mmekufa katika makosa na govi la mwili wenu, amewafanya ninyi wazima pamoja naye, akiwasamehe
 14 makosa yote; akifuta yaliyoandikwa katika mafundisho yaliyo juu yetu: akayaondoa katika kati, akayakaza
 15 msalabani; akiwa ameteka mamlaka na uwezo, akazio-nyesha kwa wazi, akizishangilia kwa huo.
- 16 Mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula, ao vinywa, ao hesabu ya siku kuu, ao mianzo ya mwezi, ao sabato:
 17 yaliyo kivuli chao yatakayokuwa; illa mwili ni wake
 18 Masiya. Mtu asiwachukulie atakavyo mliyostahili katika unenyekevu na kuabudu malaika, akiingia asipoona,
 19 akijivuna burre kwa akili ya mwili wake, wala hashiki Kitwa, chenyi mwili wote, umeruzukiwa kwa viungo na mafungo ukatiwa imara, unakua kukua kwa Muungu.
- 20 Kama pamoja na Masiya mmeifia asili ya dunia,
 21 mbona kama waishio duniani mnafundishwa, Usishike,
 22 usionje, usiguse (nayo yote kuharibika katika kutumiwa),
 23 kwa amri na elimu ya watu? yakiwa na sifa ya hekima katika kuabudu kwa mapenzi, na unenyekevu, pasipo kutunza mwili; pasipo heshima yote kwa ukinayi wa mwili.
- 3** MKIFUFUKA katika Masiya, tafuteni yaliyo juu, Masiya alipo akiketi mkono wa kuume wa Muungu;
²/₃ kumbukeni yaliyo juu, si yaliyo katika inchi. Kwani mmekufa, na uzima wenu umefichwa pamoja naye Masiya katika Muungu. Atakapoonekana Masiya uzima wetu, ndipo naswi pamoja naye tutaonekana katika utukufu.
- 5 Bassi fisheni viungo vilivyo katika inchi, washarati, uchafu, ngoa, nia mbovu, na kutamani, ndiyo ukafiri;

kwa ajili ya haya hasira ya Muungu juu yao waana wa 6
 kuasi; katika haya nanyi mlikwenda muda mlipoishi 7
 kwao. Sasa ninyi 'mwekee mbali yote, hasira, gha- 8
 thabu, uovu, unajisi, matukano katika kanwa lenu.

Msiambiane uwongo, mkiwa mmevua mtu wa kwanza 9
 pamoja na matendo yake, mkavaa mpya, aliyefanyika 10
 mpya katika kutambua kwa mfano wake aliyemumba:
 pasipo Myonani na Myahudi, tohara na govi, Mshenzi, 11
 Mskuthi, mtumwa, huru: illa yote katika yote Ma-
 siya.

Vaeni, kama wateule wa Muungu, watakatifu na wa- 12
 liopendwa, mioyo ya huruma, kusayidia, unenyekevu,
 upole, uvumilivu; mkichukuliana, mkiachiliana, mtu 13
 akiwa na laumu juu ya mtu; kama Masiya alivyowa-
 achilia ninyi, hivi nanyi; juu ya haya yote upendano, 14
 ndio ukazao ukamilifu.

Amani ya Masiya ikaamue katika mioyo yenu, mli- 15
 yoitiwa katika mwili mmoja; 'mwe na shukrani.

Neno lake Masiya likae kwenu kwa wingi katika he- 16
 kima yote, mkifundishana na mkionyana kwa zaburi,
 na nyimbo, na mashairi ya roho, mkimwambia Muungu
 katika neema mioyoni mwenu. Na killa mfanyalo kwa 17
 neno ao kwa tendo, yote katika jina lake Isa, mkimshu-
 kuru kwa yeye Muungu Baba.

Waanaake, tiini waume, kama wájib katika Bwana. 18

Waume, pendeni wake, msiwafanyie ukali. 19

Watoto, wasikieni wazee katika yote, kwani ndiyo 20
 ipendezayo vema katika Bwana.

Baba, msiwachukize watoto wenu, wasipunguke 21
 moyo.

Watumwa, wasikieni katika yote bwana kwa mwili; 22
 si kwa utumwa wa machoni, kama wapendezao watu,
 illa kwa moyo usio na hila, mkimwopoga Muungu.
 Mfanyalo lote, fanyeni kwa uwezo, kama kwa Bwana 23
 wala si kwa watu, mkijua kama mtalipiwa na Bwana 24
 ujira wa urithi. Mtumikieni Bwana Masiya. Kwani 25
 mthulumu atapewa alilothulumia: wala hakuna kuku-
 bali kwa cheo.

BWANA, 'mwawie watumwa kwa haki na sawa; 4
 mkijua kama nanyi mnaye Bwana mbinguni.

Mjitahidi katika kuomba, mkikesha katika hiyo ka- 2
 tika kushukuru; mkituombea na sisi, Muungu atufu- 3

- nulie mlango wa neno, kuinena siri yake Masiya nililo-
 4 funguwa ; nilithihirishe, kama ilivyonipasa kunena.
- 5 Mwenende katika hekima kwao walio 'nje, mkiko-
 6 mboa wakati. Neno lenu sikuzote katika neema, li-
 kiwa na chumvi, mjue ginsi ilivyowapasa kumjibu killa
 mtu.
- 7 Mambo yangu yote atawaarifu ninyi Tukiko, ndugu
 aliyependwa, na mngoje amini na mjoli katika Bwana :
 8 niliyempeleka kwenu kwa hiyo, ajue mambo yenu, aka-
 9 fariji mioyo yenu ; pamoja na Onesimo, ndugu amini na
 aliyependwa, aliye wa kwenu. Watawaarifu yote ya
 hapa.
- 10 Aristarko, aliyefungwa pamoja nami, awasalimia, na
 Marko, mjomba wake Barnaba (kwa huyu mmepokea
 11 amri; akija kwenu, mmkubali), naye Isa aliyeitwa Yusto,
 walio wa tohara. Hawa peke yao watendao kazi nami
 kwa ufalme wa Muungu, waliokuwa tulizo kwangu.
- 12 Awasalimia Epafra, aliye wa kwenu, mtumwa wake
 Masiya, akifanya bidii siku zote kwa ajili zenu katika
 kuomba, msimame wakamilifu na pasipo kupunguka
 13 katika killa alipendalo Muungu. Namshuhudia, ana
 uwivu mwingi kwa ajili ya ninyi, nao waliomo Laodi-
 kiya, nao wa Hierapoli.
- 14 Awasalimia Luka, mtabibu aliyependwa, na Dema.
- 15 Wasalimieni ndugu walioko katika Laodikiya, na
 Numfa, na kanisa lilioko nyumbani mwake.
- 16 Waraka huu ulipokwisha kusomwa kwenu, fanyeni
 usomwe katika kanisa lao Walaodikiya ; na ule wa ka-
 tika Laodikiya msome na ninyi.
- 17 Mwambieni Arkippo, Angalia ungoje uliopewa ka-
 tika Bwana, uutimize.
- 18 Salaamu kwa mkono wangu mimi Paolo. Kumbu-
 keni mafungo yangu. Neema nanyi.
-

WARAKA WA KWANZA WA PAOLO MTUME

KWA

WATHESALONIKI.

PAOLO, na Silwano, na Timoteo, kwa kanisa la **1**
Wathessaloniki katika Muungu Baba na Bwana Isa
Masiya: Neema kwenu na amani ya Muungu Baba wetu
na Bwana Isa Masiya.

Twamshukuru Muungu sikuzote kwa ajili yenu nyote, **2**
tukiwanena katika kuomba kwetu; tukikumbuga da- **3**
yima kazi yenu ya imani, na taabu ya mapenzi, na
uvumilivu wa tumaini la Bwana wetu Isa Masiya, mbele
ya Muungu na Baba wetu; tukijua, ndugu wapendwa **4**
na Muungu, uteule wenu, kama anjili yetu haikuwa **5**
kwenu katika neno tu, illa na katika nguvu, na katika
Roho Mtakatifu, na katika kwendelea sana, kama mli-
vyojua watu gani tumekuwa kwenu kwa ajili yenu.

Nanyi mkatufuata sisi na Bwana, mkipokea neno **6**
katika mateso mengi, kwa furaha ya Roho Mtakatifu:
hatta mmekuwa mfano kwao wote waaminio katika **7**
Umakedoni, na katika Akaya. Kwani katika kwenu **8**
imetolewa sauti ya neno lake Bwana, si katika Umake-
doni na Akaya tu, illa mahali pote imani yenu iliyo kwa
Muungu imeenea; hatta haihitaji sisi tuseme neno. **9**
Kwani wenyewe watuhubiria ginsi tulivyoingia kwenu,
nanyi mlivyomgeukia Muungu katika sanamu, mmtu-
mikie Muungu aliye hayi na wa kweli, na kumngoja **10**
Mwana wake katika mbinguni, aliyemfufua katika wafu,
Isa, atuokoaye katika hasira itakayokuja.

KWANI mwajua wenyewe, ndugu, ginsi tulivyoingia **2**
kwenu, kama si burre: lakini tukiteswa kwanza, tuka- **2**
tiwa jeuri, kama mjuavyo, katika Filippi, tukathubutu
katika Muungu wetu kunena kwenu anjili ya Muungu
katika bidii nyingi.

Kwani kuonya kwetu si kwa udanganifu, wala uchafu, **3**
wala hila: lakini kama tulivyostahilishwa na Muungu **4**

- kuaminiwa anjili, hivi twanena, kama wapendezao si
 5 watu, illa Muungu, aijaribuye mioyo yetu. Kwani
 hatukuwa na maneno ya kujipendekeza, kama mwajua,
 6 wala kuficha tamaa, Muungu shahidi; wala tukitaka
 kusifiwa na watu, wala na ninyi, wala nao wangineo,
 tukiweza kuwa wazito kwenu kama mitume yake Ma-
 7 siya: lakini tumekuwa wanana kwenu, kama yaya
 8 alivyotunza watoto wake; hivi tukiambatana nanyi,
 tukataka kutoa kwenu si anjili ya Muungu tu, illa na
 nafsi zetu, kwa ginsi mlivyokuwa wapenzi kwetu.
- 9 Kumbukeni, ndugu, taabu yetu na shughuli, tukitenda
 kazi mchana na usiku tusimleeme mtu kwenu, tukawa-
 10 hubiria ninyi anjili yake Muungu. Ninyi mashahidi,
 na Muungu, kama katika utakatifu na haki pasipo ku-
 11 laumiwa tulikuwa kwenu mwaminio: kama mwajua, sisi
 killa mmoja wenu, kama baba watoto wake, tukawaonya
 12 tukawatia moyo, tukashuhudia mwende kama ilivyosta-
 hili kwa Muungu, aliyetuita kwa ufalme wake na utu-
 kufu.
- 13 Kwa hiyo tena sisi twamshukuru Muungu dayima,
 kama mkipokea neno la kusikiwa kwa sisi la Muungu,
 mwaliipokea si kama neno la watu, illa kama ndivyo
 kweli, neno la Muungu, atendaye ndani yenu mwaminio.
- 14 Kwani ninyi, ndugu, mmefuata makanisa ya Muungu
 walioko katika Uyahudi, katika Masiya Isa: ya kwamba
 ninyi mmepata kwa watu wa taifa lenu yaleyale kama
 15 haya kwa Wayahudi; waliomua Bwana Isa na manabii,
 waliotufukuza sisi, wasiompandeza Muungu, wala hawa-
 16 patani na watu wo wote; wakituzuia sisi tuiseme na
 mataifa wapate kuokoka: kwa kujaliza sikuzote thambi
 zao: na hasira imewafikia hatta mwisho.
- 17 Naswi, ndugu, tukitwaliwa kwenu wakati wa kitambo,
 kwa uso, si kwa moyo, tumezidi kutamani kuwaona uso
 18 kwa shauko kuu. Kwa hiyo tukataka kuja kwenu, mi-
 mi Paolo, na marra ya kwanza na ya pili; Shetani aka-
 19 tupinga. Kwani tumaini gani kwetu, ao furaha, ao taji
 ya kujisifu, isipokuwa ninyi mbele ya Bwana wetu Isa
 20 Masiya akiwapo yeye? Kwani ninyi ni sifa yetu na
 furaha.
- 3** KWA hiyo, tusipojizuia tena, tumeona vema kua-
 2 chiwa katika Atene peke yetu; tukampeleka Timoteo,
 ndugu wetu na atendaye kazi wa Muungu katika anjili

yake Masiya, awafanye imara ninyi, awafariji kwa ajili
ya imani yenu ; mtu asitikisike na mateso haya ; kwani 3
mwajua wenyewe tumewekewa haya. Kwani na tuli- 4
pokuwako kwenu, tukawaambia mbele kama tutapata
kuteswa ; kama ilivyokuwa, nanyi mmejua.

Kwa hiyo nami, nisipojizua tena, nalipeleka nijue 5
imani yenu, ajaribuye asiwajaribu, wala taabu yetu isiwe
burre.

Sasa akija Timoteo kwetu katika kwenu, akituhubiria 6
sisi imani na upendano wenu, na kama mwatukumbuka
sikuzote vema, mkitaka kutuona sisi kama na sisi ninyi ;
kwa hiyo tumefarajika, ndugu, juu yenu katika shidda 7
na mateso yote yetu, kwa imani yenu : hatta sisi tunao 8
uzima, ninyi mkisimama katika Bwana.

Shukrani gani tuwezayo kumlipia Muungu kwa ajili 9
yenu, katika furaha yote tunayofurahia kwa ninyi mbele
yake Muungu wetu : mehana na usiku tukiomba kwa 10
nguvu tuwaone uso, tutimilize iliyosalia ya imani yenu ?
Muungu mwenyewe na Baba wetu, na Bwana wetu Isa 11
Masiya, ainyoshe njia yetu kwenu. Nanyi Bwana awa- 12
ongeze awazidishe katika upendano kwenu na kwa wote,
kama na sisi kwenu ; micyo yenu iwe imara pasipo ku- 13
laumiwa katika utakatifu, mbele ya Muungu na Baba
wetu, akiwapo Bwana wetu Isa pamoja na watakatifu
wake wote.

BAADAYE, ndugu, twawataka twawaonya katika 4
Bwana Isa, kama mlivyopokea kwetu imewapasa ninyi
kwenenda na kumpendeza Muungu, kama mkaenenda,
mpate afathali kuzidi. Kwani mwajua maagizo gani 2
mmepewa na sisi kwa Bwana Isa. Kwani ndilo alipe- 3
ndalo Muungu, utakatifu wenu, tuepukane na asha-
rati ; killa mtu wa kwetu ajue kukiweza chombo chake 4
katika utakatifu na heshima, si katika tamaa ya kutama- 5
ni, kama mataifa wasiomjua Muungu ; asimkose asi- 6
mdanganye ndugu katika jambo : kwani Bwana alipaye
kisasi cha haya yote, kama tulivyotangulia kuwaambia
na kushuhudia. Kwani Muungu hakuita kwa uchafu, 7
illa kwa utakatifu. Hivi naye atharauye hamtharau 8
mtu, illa Muungu, atoaye Roho yake Mtakatifu kwetu.

Kwa mapenzi ya ndugu, haihitaji niwaandikie : kwani 9
ninyi wenyewe mmefundishwa na Muungu mpendane ;
nanyi ndivyo mlivyowatendea ndugu wote katika Uma- 10

11 kedoni pia. Nawasihi, ndugu, afathali mzidi; mkaone
 makuu kutulia na kutenda yaliyo yenu, na kufanya kazi
 12 kwa mikono yenu, kama tulivyowaagiza; mwenende ka-
 tika heshima kwao walio 'nje, wala msipunguke neno.

13 Hatupendi, ndugu, msiwajulie waliolala; msihuzu-
 14 nike, kama wale wasio na tumaini. Kwani tukiamini
 kama Isa alikufa akafufuka, hivi na Muungu, waliolala
 15 kwa Isa, ataleta pamoja naye. Ndilo tuwaambialo kati-
 ka neno la Bwana, kama sisi tulio hayi, tuliosalia hatta
 akiwapo Bwana, hatutawatangulia waliolala; kama
 16 Bwana katika ukelele, katika sauti yake malaika mkuu,
 na katika kulia paanda la Muungu, atashuka mbinguni;
 17 na wafu wa katika Masiya wataondoka kwanza: tena
 sisi tulio hayi tuliosalia, pamoja nao tutachukuliwa ka-
 tika mawingu, tuonane naye Bwana katika hewa: na
 18 hivi sikuzote tutakuwa naye Bwana. Bassi mfarijiane
 kwa maneno haya.

5 KWA mambo ya muhulla na wakati, ndugu, haihi-
 2 taji kuwaandikia: kwani ninyi mwajua yakini kama
 3 siku ya Bwana kama mwivi usiku ndivyo ijavyo. Kwani
 wasemapo, Amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo
 kwa gháfula, kama utungu wake mwenyi mimba; wala
 hawataokoka.

4 Ninyi, ndugu, hammo katika giza, siku ile iwafikie
 5 ninyi kama mwivi: kwani ninyi nyote waana wa nuru,
 na waana wa mchana: sisi si wa usiku, wala si wa giza.

6 Bassi tena tusingizie kama wangine; tukeshe tukale-
 7 vuke. Kwani walalao walala usiku; na walewao wa-
 8 lewa usiku: sisi, tukiwa wa mchana, tulevuke, tukivaa
 kifuani imani na upendano, na kitwani tumaini la wo-
 9 kovu. Kwani Muungu hakutuwekea hasira, illa ku-
 10 pata wokovu kwa Bwana wetu Isa Masiya, aliyekufa
 kwa ajili yetu, illi, tukikesha tukilala, tupate kuwa
 11 hayi pamoja naye. Kwa hiyo mfarijiane, mkajengeane,
 kama na mfanyavyo.

12 Nawataka ninyi, ndugu, kuwajua wanaoshughulika
 kwenu, waliowekwa mbele yenu katika Bwana, wanao-
 13 warudi, mkawaone wakuu katika upendano kwa ajili ya
 kazi yao.

'Mwe na amani moyoni mwenu.

14 Nawaonya, ndugu, 'mwarudi wasio na taratibu, 'mwa-
 tie moyo walio tháifu, 'mwachukue wasio na nguvu,

mstahimili kwa wote. Angalieni mtu asimlipie mtu 15
ovu kwa ovu; lakini sikuzote fuateni mema, na kwenu
ninyi, na kwa wote.

Furahini sikuzote. Ombeni dayima. Katika yote ¹⁶
shukuruni; kwani ndilo apendalo Muungu katika Ma- 18
siya Isa kwenu. Msizimishe Roho. Msitweze unabii. ¹⁹
Jaribuni yote. Shikeni yaliyo mazuri. Epukeni namna ²⁰
yote ya ubaya. ²¹
²²

Muungu wa imani mwenyewe awatakase kabisa; na- 23
nyi pia yote, roho, na maisha, na mwili, mhifathike kwa
siku ya kuwapo Bwana wetu Isa Masiya. Ndiye amini 24
awaitaye, naye atafanya.

Ndugu, mtuombee sisi. Salimieni ndugu wote kwa ²⁵
busu takatifu. Nawaapiza kwa Bwana wasomewe 27
ndugu wakatakifu wote waraka huu.

Neema ya Bwana wetu Isa Masiya pamoja nanyi. 28

WARAKA WA PILI WA PAOLO MTUME

KWA

WATHESSALONIKI.

PAOLO, Silwano, na Timoteo, kwa kanisa la Wa- 1
thessaloniki katika Muungu Baba wetu na Bwana Isa
Masiya: Neema kwenu na imani ya Muungu Baba 2
wetu na Bwana Isa Masiya.

Imetupasa tumshukuru Muungu sikuzote kwa ajili 3
yenu, ndugu, kama ni wájib, kama imani yenu inazidi
sana, na mapenzi ya killa mtu wenu kwa wenzake
yamekuwa mengi. Hatta sisi wenyewe twajisifu ka- 4
tika makanisa ya Muungu kwa ajili ya uvumilivu wenu
na imani katika mafukuzo yenu yote, na mateso mliyo
nayo: ishara ya hukumu ya haki ya Muungu, kwa 5
kuwastabilisha ufalme wa Muungu, kwa ajili yake
mmeumiwa: ikiwa haki kwa Muungu kuwalipia mateso 6
wawatesao, na ninyi mlioteswa raha pamoja na sisi, 7
katika kufunuka Bwana Isa katika mbinguni na ma-

- 8 laika za uwezo wake, katika kuwaka moto, akiwalipia haki wasiomjua Muungu, nao wasiotii anjili yake Bwana
- 9 wetu Isa Masiya: watakaolipiwa haki, upotevu wa milele katika usoni pa Bwana na katika utukufu wa
- 10 nguvu yake, atakapokuja kutukuzwa katika watakatifu wake, na kuajabiwa katika wote waliomwamini (kwamba ushabidi wetu umeaminiwa kwenu), katika siku ile.
- 11 Kwa hiyo twawaombea ninyi sikuzote, mpate kuustahilia wito wa Muungu wetu, mkatimize killa ulitakalo
- 12 wema na kazi ya imani kwa nguvu; jina la Bwana wetu Isa litukuzwe kwenu, na ninyi kwake, kwa nema ya Muungu wetu na Bwana Isa Masiya.
- 2 TWAWATAKA, ndugu, kwa mambo ya kuja kwake Bwana wetu Isa Masiya, na kukusanyika sisi kwake,
- 2 msichukuliwe upesi katika fikara zenu, wala msitaabike wala na roho, wala na neno, wala na kama waraka wetu, ya kwamba siku ya Bwana imekuwa karibu.
- 3 Mtu asiwadanganye kwa njia yote: kwamba, usipokuja kwanza ufarakano ule, mtu wa thambi afunuke,
- 4 mwana wa upotevu, asimamaye na ajiinuaye juu ya killa kilichoitwa Muungu ama kuabudiwa, hatta mwenyewe kuketi katika hekalu la Muungu kama Muungu,
- 5 akijionyesha kama ndiye aliye Muungu. Hamkumbuki kama hatta nikiwapo kwenu naliwaambia haya?
- 6 Na sasa lizuialo mwajua, afunuke huyu wakati wake.
- 7 Kwani siri ya kuasi hatta sasa yatenda: asipokuwa
- 8 azuiaye, hatta asipo tena katikati. Ndipo atakapofunuka mwasi, Bwana Isa atakayempoteza kwa pumuzi ya kanwa lake, naye atamharibu kwa wonyesho wa
- 9 kuwako yeye. Ndiye aliyoko katika kutenda Shetani
- 10 katika uwezo wote, na ishara, na ajabu za uwongo, na katika killa kudanganyika kwa thulumu kwao walio-potea; kwa sababu hawakukubali mapenzi ya kweli,
- 11 wapate kuokoka. Kwa hiyo Muungu amewaletea
- 12 nguvu ikosao, wauamini uwongo; wahukumiwe wote wasioiamini kweli, lakini wamejipendeza katika thulumu.
- 13 Imetupasa sisi kumshukuru Muungu sikuzote kwa ajili yenu, ndugu wapendwa na Bwana, kama Muungu amewachagua tangu mwanzo kwa wokovu katika kuta-
- 14 kaswa kwa Roho na imani ya kweli, aliyowaitia ninyi kwa anjili yetu, kwa kuimiliki utukufu wa Bwana wetu Isa Masiya.

Bassi tena, ndugu, simameni, mkashike mapokeo 15
 mliyofundishwa, ao kwa neno, ao kwa waraka wetu.
 Naye Bwana wetu Isa Masiya, na Muungu Baba wetu, 16
 aliyetupenda akatupa faraja la milele na tumaini jema
 katika neema, awafariji mioyo, awafanye imara katika 17
 killa tendo na neno jema.

MWISHONI, ndugu, mtuombe, neno la Bwana
 liende, likatukuzwe kama na kwenu; tukaokoke katika 2
 watu wasio na akili na wabaya; kwani wote havana
 imani. Amini ndiye Bwana, atakayefanya ninyi imara, 3
 atakayeokoa katika ubaya. Tumemtumainia Bwana kwa 4
 mambo yenu, kama tuliyowaagiza ninyi na mwafanya
 na mtafanya. Bwana awatengeneze mioyo kwa ma- 5
 penzi ya Muungu na uvumilivu wa Masiya.

Nawaagiza ninyi, ndugu, katika jina la Bwana wetu 6
 Isa Masiya, jitengeni ninyi katika killa ndugu aendaye
 pasipo taratibu, wala si kwa mapokeo mliyoyapokea kwa
 sisi. Mwajua wenyewe ginsi ilivyowapasa kutufuata: 7
 kama hatukuchafuka kwenu; wala hatukula chakula 8
 bure kwa mtu yo yote, lakini katika taabu na shughuli
 mchana na usiku tukitenda kazi, tusimlemee mtu kwe-
 nu: si kama hatunao uwezo, lakini tuwape ninyi mfano, 9
 mtufuate. Kwani na tulipokuwako kwenu tumewaa- 10
 giza, asiyependa kutenda kazi, wala asile. Twasikia 11
 kama wako kwenu waendao pasipo taratibu, wasiotenda
 kazi, lakini watenda ufuthuli. Hawa twawaagiza twa- 12
 waonya kwa Bwana wetu Isa Masiya, wakitenda kazi
 katika utulivu, wale chakula chao wenyewe.

Ninyi, ndugu, msithoofike katika kutenda vema. 13
 Mtu asiposikia neno letu kwa waraka, mtie alama, wala 14
 msizumgumze naye, apate kutahayarika. Wala msi- 15
 mfanye adui, illa mmrudi kama ndugu. Bwana wa 16
 imani mwenyewe awape ninyi amani kwa yote kwa njia
 zote. Bwana nanyi nyote.

Salaamu kwa mkono wangu, Paolo, ndiyo ishara 17
 katika killa waraka: hivi naandika. Neema ya Bwana 18
 wetu Isa Masiya pamoja nanyi nyote. Amina.

WARAKA WA KWANZA WA PAOLO MTUME

KWA

TIMOTEO.

- 1 PAOLO, mtume wa Isa Masiya kwa amri ya Muungu Mwokozi wetu na ya Bwana Isa Masiya tumaini
 2 letu; kwa Timoteo, mwana wangu halisi katika imani: Neema, rehema, amani, ya Muungu Baba na Masiya Isa Bwana wetu.
- 3 Kama nilivyokuonya ukae katika Efeso, nikisafiri kwa Umakedoni, uwaagize wangine wasifundishe elimu ngineyo, wala wasiangalie hadithi na vitabu vya vizazi visivyokwisha, viletavyo maswali, zayidi ya kujengea kwa Muungu katika imani.
- 5 Mwisho wa maagizo ndio upendano katika moyo safi
 6 na thamiri njema, na imani pasipo unafiki: wangine wakikosa haya wamepotea katika maneno ya ubatili; wakipenda kuwa wafunza sheria, wasipofikiri wala wanao, wala mambo waliyofanyia wosia.
- 8 Twajua kama sheria ni njema, mtu akiitumia kwa
 9 sheria, akijua kama sheria hapana juu ya mtu wa haki, illa juu yao waasi, waasio taratibu, wanajisi na wenyi thambi, wasio watakatifu, wasio na dini, wapiga baba
 10 na wapiga mama, waua watu, washarati, wafira, wanyang'anya watu, wawongo, waapa uwongo, na yote ma-
 11 ngineyo yasiyopatana na elimu ya uzima; kwa anjili ya utukufu wake Muungu wa heri, ninayoaminiwa mimi.
- 12 Namshukuru Masiya Isa, Bwana wetu, aliyenitia nguvu, kwamba akiniona amini, akiniweka katika ungoje; niliyekuwa kwanza mnena unajisi, na mfukuza, na mwenyi jeuri. Lakini nalirehemewa, kwani nisipo-
 14 jua nimetenda pasipo kuamini. Neema ya Bwana wetu ikajaa 'mno pamoja na imani na mapenzi yaliyo katika Masiya Isa.
- 15 Neno amini, listahililo ukubali wote, kama Masiya Isa alikuja ulimwenguni, awaokoe wenyi thambi; ndimi

wa kwanza wao. Lakini kwa hiyo nalirehemewa, ka- 16
tika mimi kwanza Isa Masiya aonyeshe uvumilivu pia
kwa mfano kwao watakaomwamini kwa uzima wa milele.
Kwa mfalme wa milele, asiyeharibika, asiyeonekana, 17
Muungu wa hekima peke yake, heshima na utukufu
milele hatta milele. Amina.

Agizo hili nimekutia, mwanangu Timoteo, kwa una- 18
bii uliotangulia kuwa juu yako, ufanye katika haya vita
nzuri; ukiwa na imani, na thamiri njema; hizi wangine 19
wasiposhika wamevunja chombo cha imani: wa hawa 20
ni Humenayo na Iskander; niliowatoa kwa Shetani,
wajifunze wasinene unajisi.

NATAKA kwanza kabisa kufanyika kuomba, na **2**
sala, na kuombea, na kushukuru, kwa watu wote; kwa **2**
wafalme nao wote wenyi nguvu; tupite maisha tulivu
yenyi amani, katika utawa wote na utaratibu. Kwani **3**
ndilo zuri, lenyi ukubali mbele ya mwokozi wetu Muu-
ngungu; apendaye watu wote waokoke, wakaje katika **4**
maarifa ya kweli. Kwani mmoja ni Muungu, na **5**
mmoja aliye kati ya Muungu na watu, mtu Masiya
Isa, aliyejitoa kuwa ukombozi wao wote; ushahidi wa- **6**
kati wake; kwa huo naliwekwa mhubiri na mtume **7**
(nasema kweli katika Masiya, sisemi uwongo), mwalimu
wa mataifa katika imani na kweli.

Bassi nataka waume waombe mahali pote, wakiinua **8**
mikono mitakatifu, pasipo hasira na kujadiliana. Hivi **9**
na waanaake, katika mavazi yaliyotengenezwa, waji-
pambe kwa haya na moyo wa kiasi; si katika masuko,
ao thahahu, ao lulu, ao nguo za thamani; lakini, kama **10**
ilivyowapasa waanaake waliojifanya watawa, kwa ma-
tendo mema. Mwanamke ajifunze pasipo uthia katika **11**
kutii. Simpi mwanamke ruksa afundishe, wala ku- **12**
mtawala mume, lakini kuwa pasipo uthia. Kwani **13**
Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, halafu Hawa. Wala **14**
Adamu hakudanganyika, lakini mwanamke akidanga-
nyika alikuwako katika kosa. Ataokoka kwa kuza- **15**
liwa mtoto, wakikaa katika imani, na upendano, na
utakatifu, pamoja na moyo wa kiasi.

AMINI ni neno, mtu akitaka usimamizi atamani **3**
tendo jema. Imempasa askafu asiwe na laumu, mume **2**
wa mke mmoja, asiyelewa, mwenyi moyo wa kiasi, tara-
tibu, mkaribishaji, mfundishaji, si mnywa mvinyo, si **3**

- mpigaji, si apataye kwa aibu ; lakini mwema, mwanana,
 4 asiyetamani fetha, aliye juu ya nyumba yake vema,
 akiwa na watoto wake katika kumtii kwa heshima yote ;
 5 (mtu asipojua kusimamia nyumba yake yeye, atalitu-
 6 nzaje kanisa la Muungu?) si mwongofu mpya, asiji-
 7 vune akaanguke katika hukumu ya shetani. Imempasa
 tena kuwa na ushahidi mzuri kwao walio 'nje, asia-
 nguke katika shutumu na kitanzi cha shetani.
- 8 Hivi na wangoje, wenyi heshima, si wenyi maneno
 mawili, si watumiao mvinyo mwingi, si wapatao kwa
 9 aibu ; waishikao siri ya imani katika moyo safi. Hawa
 10 wakajaribiwe kwanza ; halafu wangojee, wasipostakiwa.
- 11 Waanaake hivyo, wenyi heshima, si wasingiziao ;
 wasiolewa, amini katika mambo yote.
- 12 Wangoje wawe waume wa mke mmoja, wakiwasi-
 mamia watoto wao vema, na nyumba zao wenyewe,
- 13 Kwani wanaongojea vema wajipatia daraja nzuri, na
 kuthubutu sana katika imani iliyo katika Masiya Isa.
- 14 Haya nakuandikia, nikitaraja kukujia karibu ; niki-
 15 kawia, upate kujua ilivyokupasa kuongea katika nyu-
 mba ya Muungu, ndiyo kanisa lake Muungu aliye hayi,
 16 nguzo na msinji wa kweli. Na pasipo shaka, kuu ni
 siri ya utawa ; Muungu aliyethihiriwa katika mwili,
 akafanyiwa haki katika roho, akaonekana na malaika,
 akahubiriwa kwa mataifa, akaaminiwa katika uli-
 mwengu, akapokewa katika utukufu.
- 4 ROHO yanena kwa wazi, kama siku za mwisho watu
 watafarakana na imani, wakijipatia roho za kukosa na
 2 elimu ya pepo, wakinena uwongo katika unafiki, waki-
 3 chomwa na moto thamiri zao ; wakizuia kuoana, kue-
 puka vyakula, Muungu aliyeviumba vipokewe kwa shu-
 4 krani nao walio na imani na maarifa ya kweli : ya kwa-
 mba killa kiumbe cha Muungu kizuri, wala hakuna
 5 cha kutupiwa, kikitwaliwa na shukrani : kwani kime-
 takaswa kwa neno la Muungu na kuomba.
- 6 Ukiwakumbusha ndugu haya, utakuwa mngoje
 mzuri wa Masiya Isa, mzoea maneno ya imani, na ya
 7 elimu nzuri uliyoifuata. Hadithi za kizee zisizo za dini
 8 uzikataze. Ujizoeze kwa utawa : mchezo wa mwili wafaa
 kidogo tu ; illa utawa hufaa kwa yote, ukiwa na ahadi
 ya uzima ulio sasa, nao utakaokuwa.
- 9 Amini ni neno, lastahili ukubali wote. Kwani kwa
 10

hiyo twataabika tukashutumiwa, ya kwamba twamtu-
maini Muungu aliye hayi, aliye Mwokozi wa watu wote,
kwanza wao waaminio. Agiza haya ukafundishe. 11

Mtu asitharau ujana wako; lakini uwe mfano wao 12
waaminio, katika neno, katika mwenendo, katika upe-
ndano, katika roho, katika imani, katika kuwa safi.

Hatta nikija jitie katika kusoma, kuonya, kufundi- 13
sha. Usiachilie ukarimu ulio kwako, uliopewa wewe 14
kwa unabii na kutiwa mikono ya wazee. Haya uyafikiri, 15
katika haya ukae, fayida yako ionekane na wote. Ua- 16
ngalie nafsi yako na kufundisha. Ukadumu: ukifanya
haya utajiokoa mwenyewe nao wakusikiao.

USIMKARIPIE mzee, illa mwonye kama baba; 5
walio wadogo kama ndugu: waanaake wazee kama ma- 2
ma; wadogo wao kama ndugu, katika masafi yote.

Waheshimie wajaani, walio ndio wajaani. Mjaani 3
akiwa na watoto ao wajomba, wajifunze kwanza kutenda 4
utawa kwa nyumba yao, na kuwalipia thawabu waliowa-
zaa: kwani ndilo zuri na likubalikalo mbele ya Muungu.
Aliye ndiye mjaani akaachiliwa, amemtumainia Muungu, 5
ashinda katika kuomba na sala mchana na usiku. Asi- 6
yejizua amekufa akiwa hayi. Haya uwaagize, wasilau- 7
miwe. Mtu asiyewatunza walio wake, na kwanza wa 8
nyumba yake, ameikana imani, ni mbaya kuliko kafiri.

Mjaani asiandikwe, umri wake akipunguka miaka 9
sitini, mke wa mume mmoja, aliyeshuhudiwa katika ma- 10
tendo mema; kama amelea watoto, kama amekaribisha
wageni, kama amewaosha miguu watakatifu, kama ame-
wasayidia walioteswa, kama amefuata killa tendo jema.
Wajaani wasio wa umri ule uwakatae; kwani wakine- 11
nepa juu yake Masiya, wataka kuolewa; wakiwa na hu- 12
kumu, kwamba wameiacha imani ya kwanza. Wajifa- 13
nya wavivu tena, wakizunguka nyumba kwa nyumba;
wala si wavivu tu, illa wenyi maneno mengi na wenyi
ufuthuli, wasemao yasiyowapasa.

Napenda wasio wazee waolewe, wazae watoto, watunze 14
nyumba, wasimpe mtesi nafasi ya kuaibisha: kwani 15
hatta sasa wako waliogeuka kumfuata Shetani.

Mtu mume ao mke wa imani akiwa na wajaani, awa- 16
sayidie, kanisa lisilemewe; liwasayidie walio ndio wajaani.
Wazee watawalao vema wastahilishwe heshima maru- 17
dufu, wa kwanza watendao kazi ya neno na ufundisho.

- 18 Kwani andiko lasema, Usimfunge kanwa ng'ombe afikichaye; na tena, Atendaye kazi amestahili ujira wake.
- 19 Usikubali mshtaka juu ya mzee, illa kwa mashahidi
20 wawili ao watatu. Wakosao uwakemee mbele yao wote, wapate na waliosalia kuogopa.
- 21 Nashuhudia mbele ya Muungu na Bwana Masiya Isa, na malaika wateule, ulinde haya pasipo kuchagulia, usipofanya neno kwa hawa.
- 22 Usimtie mtu mikono upesi, wala usishariki katika thambi za watu.
- 23 Ujilinde safi. Usinywe tena maji tu, illa tumia kidogo mvinyo, kwa ajili ya tumbo lako na uthaifu wako mwingi.
- 24 Kuna watu thambi zao thahiri mbele, zikitangulia
25 hukumuni; wangine zawafuata. Hivi na matendo mazuri ni thahiri mbele, nayo yasiyo hayawezi kustirika.
- 6** WALIO chini ya mafungo, watumwa, waone bwana zao wamestahili heshima yote, jina la Muungu na fundisho lisinenwe unajisi. Walio na bwana wenyi imani wasiwatharau ya kwamba wamekuwa ndugu; illa afa-thali watumikie, kwani wamekuwa wa imani na wamependwa, walio na sehemu katika kutenda vema. Haya fundisha ukaonye.
- 3 Mtu akitoa fundisho linginelo, wala haji katika maneno ya uzima, yaliyo ya Bwana wetu Isa Masiya, na
4 fundisho la utawa, amejivuna, asipofahamu neno, lakini akipuza kwa maswali na vita za maneno, katika hizi
5 zatoka hasidi, ugomvi, unajisi, kuthania mabaya, mashindano ya watu walioharibika akili, walioikosa kweli, wa-
6 kithani fayida ni utawa; katika hawa ujitenge. Uta-
7 wa na urathi ndio fayida nyingi: kwani hatukuleta kitu
8 duniani, yakini hatuwezi kuchukua kitu 'nje. Tukiwa na chakula na nguo, kwa haya tuwe rathi.
- 9 Wapendao kuwa na mali waanguka katika jaribu na kitanzi, na tamaa nyingi pasipo akili na kuthuru, ziwatosazo watu katika upotevu na uharibifu. Kwani
10 shina la mabaya yote ni kupenda fetha: wakiitamani hiyo kuna waliokosa katika imani, wakajichoma kwa huzuni nyingi.
- 11 Wewe, ee mtu wa Muungu, kimbia haya; fuata ha-
12 ki, utawa, imani, upendano, uvumilivu, upole. Pigane

pigano zuri la imani, shika uzima wa milele, ulioitiwa, ukaungama ungamo zuri mbele ya mashahidi wengi.

Nakuagiza mbele ya Muungu, avipaye vyote uzima, na 13 Masiya Isa, aliyeshuhudia kwa Pontio Pilato ungamo zuri, ulinde amri hii pasipo mawaa, pasipo laumu, hatta wonyesho 14 wa Bwana wetu Isa Masiya, atakayeonyesha wakati wake, 15 aliye mbarikiwa na Mwenyi peke yake, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa bwana, aliye peke yake hafi, akaaye 16 katika nuru isiyokaribika; mtu hakumwona wala hawenzi kumwona: aliye na heshima na uwezo milele. Amina.

Walio na mali katika dunia hii uwaagize wasijithanie 17 makuu, wala wasitumaini kwa utajiri usio yakini, illa kwa Muungu aliye hayi, atuleteaye yote kwa wingi tufurahiwe; watende vema, wawe matajiri katika matendo 18 mazuri, watawanye vema, washariki kwa moyo, wajiwekee 19 hazina, msinji mzuri kwao ujao, wapate kuushika uzima wa milele.

Ee Timoteo, ulinde amana, ukiepuka maneno matupu 20 pasipo dini, na mapigano ya elimu, kama ilivyotajwa kwa uwongo; hii wangine wakikubali wameikosa imani. 21 Neema nawe. Amina.

WARAKA WA PILI WA PAOLO MTUME

KWA

TIMOTEO.

PAOLO, mtume wa Isa Masiya, kama alivyopenda 1 Muungu, kwa ahadi ya uzima katika Masiya Isa; kwa 2 Timoteo mwanangu mpendwa: Neema, rehema, amani, ya Muungu Baba na Masiya Isa Bwana wetu.

Namshukuru Muungu, nimwabuduye tangu wazee 3 katika moyo safi, kama nakukumbuka wewe dayima katika kuomba kwangu mchana na usiku, nikitaka sana 4 kukuona, nikifahamu machozi yako, nijae furaha; nikipumbuka imani yako pasipo unafiki, iliyokaa kwanza 5 katika bibi wako Loi, na mama wako Eunike; natumaini na kwako tena.

- 6 Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uuchochee ukarimu wa Muungu ulioko kwako kwa kutiwa mikono yangu.
- 7 Kwani Muungu hakutupa roho ya hofu, illa ya nguvu na upendano, na moyo wa kiasi.
- 8 Usitahayarike na ushahidi wake Bwana wetu, wala na mimi mfungwa wake: lakini upokee mabaya pamoja
- 9 katika anjili kwa nguvu yake Muungu; aliyetuokoa, akatuita kwa wito mtakatifu, si kwa matendo yetu, illa kwa nia yake yeye na neema, tuliyopewa sisi katika
- 10 Masiya Isa mbele ya siku za milele, ikathihirishwa sasa kwa wonyesho wa Mwokozi wetu Isa Masiya, akibatilisha kufa, akiweka nuruni uzima na kutoa kufa, kwa anjili,
- 11 aliyonifanyia mhubiri, na mtume, na mwalimu wa mataifa. Kwa sababu hiyo naona mateso haya: wala sitahayariki; kwani namjua niliyemwamini, nikatumaini kama aweza kuulinda niliyomwamini hatta siku ile.
- 12 Shike utaratibu wa maneno yenyi uzima, uliyoyasikia kwangu, katika imani na upendano ulio katika Masiya
- 13 Isa. Ulilinde amana nzuri kwa Roho Mtakatifu akaaye kwetu.
- 14 Wajua hili, ya kwamba wote walio katika Asia wame-
- 15 nigeukia; wa hawa ni Figello na Hermogene. Wapewe rehema na Bwana nyumba ya Onesiforo: kwani marra nyingi aliniburudisha, wala hakutahayarika na mnyororo
- 16 wangu, lakini akiwa katika Rumi akanitafuta kwa bidii,
- 17 akaniona. Apewe na Bwana kuona rehema yake Bwana siku ile. Naye alivyoningojea katika Efeso, wajua sana.
- 2 BASSI wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema
- 2 iliyo katika Masiya Isa. Nayo uliyoyasikia kwangu kwa mashahidi wengi, haya uwatolee watu amini, watakaofaa kuwafundisha na wangineo. Uingie katika
- 3 taabu, kama asikari mzuri wake Isa Masiya. Hakuna afanyaye vita, ajitiaye katika shughuli za dunia; ampe-
- 4 ndeze ampelekaye vitani. Hatta mtu akishindana, hapewi taji asiposhindana kwa halali. Mkulima atendaye kazi ndiye iliyempasa wa kwanza kushariki katika ma-
- 5 tunda. Ufahamu nisemayo; kwani Bwana atakupa akili katika yote.
- 6 Kumbuke Isa Masiya, aliyefufuka katika wafu, wa
- 7 uzao wa Daudi, kwa anjili yangu. Katika huyu nimeseswa hatta kufungwa, kama mtenda vibaya; illakini

neni la Muungu halikufungwa. Kwa hilo nastahimili 10
yote kwa ajili yao wateule, nao wokoovu ulio katika
Masiya Isa na utukufu wa milele. Amini ni neno: 11
kwani tukifa naye, na tutaishi naye: tukistahimili, naswi 12
tutamiliki naye: tukikana, naye atatukania sisi: tusipo- 13
amini, yeye amekaa amini: kujikania mwenyewe hawezi.

Haya ukumbushe, ukishuhudu mbele ya Bwana, wasi- 14
pigane kwa maneno, pasipo kufaa, kwa upinduo wao wa-
naosikia. Ujitahidi kujionyesha mwema kwa Muungu, 15
mtenda kazi asiyetahayarika, ukilifanyia neno la kweli
njia ya kunyoka. Maneno matupu pasipo dini uyaepuke: 16
kwani yataendelea hatta kuzidi unajisi, na neno lao ka- 17
ma gangrena litakuwa likila; wa hawa ni Humenayo
na Fileto, waliokosa katika kweli, wakisema kiyama 18
kimekwisha kuwa, nao wapindua imani ya watu.

Illakini msinji wake Muungu ulio imara, umekaa, ukiti- 19
wa andiko, Amejua Bwana walio ndio wake; na, Aache
thulumu killa alinenaye jina la Masiya.

Katika nyumba kubwa havimo tu vyombo vya thaha- 20
bu na fetha, illa navyo vya mti na udongo, vingine kwa
heshima, vingine pasipo heshima. Mtu akijitakasa ka- 21
tika haya, atakuwa chombo cha heshima, kilichotakaswa,
kimfaacho bwana, kimetengenezwa kwa killa kazi iliyo
njema.

Ukimbie tamaa za ujana; fuate haki, imani, upenda- 22
no, amani, pamoja nao waliomwitia Bwana katika mi-
oyo safi. Illakini ukatae maswali ya upumbafu pasipo 23
elimu, ukijua kama yazaa magomvi: wala mtumwa wa 24
Bwana hana amri ya kupigana, illa kuwa mwanana kwa
wote, mkufunzi, mvumilivu, akifundisha kwa upole wa- 25
naoasi, hatta labuda Muungu awapekutubu na kuitambua
kweli, walevuke katika tanzi la shetani waliochukuliwa 26
naye, kama apendavyo.

JUA haya, ya kwamba siku za mwisho zitakuwa wakati **3**
wa hatari. Watu watakuwa wajipendao, wapendao fetha, **2**
wajisifuo, wenyi kiburi, wanajisi, wasiowatii wazee, wasio
na shukrani, wasio safi, wasiopendana, wavunjao maa- **3**
gano, wastakio burre, wasiojizuia, wakali, wasiopenda
mema, watoao kwa hila, waendao kassi, wajivunao, wa- **4**
pendao anasa kuliko Muungu; wakiwa na umbo la uta- **5**
wa, wakikana nguvu yake: ugeuke katika hawa. Kwa- **6**
ni wa hawa ni wale wanaojiingiza katika nyumba,

- wakiwapata waanaake wajinga wenyi mizigo ya thambi,
 7 waliochukuliwa na tamaa zile na zile, wakijifunza siku
 8 zote, wasiweze kabisa kufika kuijua kweli. Kama
 Yanne na Yambre walivyosimama juu yake Musa, hivi
 na hawa wasimama juu ya kweli; watu walioharibika
 9 akili, wasiokubalika kwa mambo ya imani. Illakini
 hawataendelea sana : kwani upumbafu wao utaonekana
 kwa wote, kama ulivyokuwa na wao.
- 10 Lakini wewe umefuatana nami katika elimu, na mwe-
 nendo, na kusudi, na imani, na upole, na upendano, na
 11 uvumilivu, na mafukuzo, na mateso ; yalionyipata katika
 Antiokia, katika Ikonio, katika Lustra ; mafukuzo gani
 niliyoyachukua : naye Bwana akaniokoa katika yote.
 12 Na wote wapendao kwenda kwa utawa katika Masiya
 13 Isa watafukuzwa. Watu wabaya na wadanganya wa-
 tazidi kwa maovu, wakikosesha na wakikoseshwa.
- 14 Wewe ukae katika yale uliyofundishwa, ukathubu-
 15 tishwa, ukimjua uliyejifunzia, na kama tangu utoto ume-
 yajua maandiko, matakatifu, yawezayo kukuhekimisha
 16 hatta kuokoka kwa imani iliyo katika Masiya Isa. Kil-
 la andiko, pumuzi ya Muungu, lafaa kwa fundisho, kwa
 kuonyesha makosa, kwa kuongoa, kwa kuelimisha iliyo
 17 haki ; mtu wa Muungu awe mkamilifu, akitengenezwa
 kwa killa tendo jema.
- 4** NAKUSHUHUDIA mbele ya Muungu na Bwana
 Isa Masiya, atakayehukumu walio hayi na walio wafu,
 2 kwa wonyesho wake, na ufalme wake, ulihubiri neno,
 ufanye bidii kwa wakati na pasipo wakati, urudi, ukemee,
 3 uonye katika upole wote na elimu. Wakati utakuwa wa-
 takapokataa elimu ya uzima, lakini kwa nia zao wenyewe
 4 watajizoelea waalimu, wakiwaka masikio ; watakapo-
 jigeuza katika kuisikia kweli, watageuka kwa hadithi.
- 5 Lakini wewe ulevuke katika yote, uchukue mabaya,
 fanye kazi ya mwanjilisti, utimize ungoje wako.
- 6 Kwani mimi sasa namwagika, na wakati wa kufu-
 7 nguliwa kwangu umekuwa karibu. Shindano jema
 8 nimelishinda, njia imetimika, imani nimeishika : baadaye
 nimewekewa taji ya haki, atakayonipa Bwana siku ile,
 mwamuzi wa haki : wala si mimi tu, illa wote waliou-
 penda wonyesho wake.
- ⁹₁₀ Ujitahidi kuja upesi kwangu : kwani Dema ameniacha,
 akipenda dunia hii, amesafiri Thessalonika ; Kreske

kwa Galatia, Tito kwa Dalmatia. Luka peke yake 11
kwangu. Umtwae Marko umletee pamoja nawe, kwa-
ni anifaa kwa ungoje. Tukiko nimempeleka Efeso. 12
Joho nililoliacha katika Troa kwa Karpo, ukija lete, 13
na vitabu, na vya kwanza vya ngozi.

Iskander mfua shaba alinitendea mabaya mengi: 14
amlipie Bwana kwa matendo yake: ukajihathari kwake; 15
kwani amejitia sana juu ya maneno yetu.

Katika jawabu langu la kwanza hakuna aliyekuwako 16
nami; wote wakaniacha: wasihesabikiwe. Bwana ame- 17
simama nami, akanitia nguvu; kwa mimi iliyohubirika
itimilike, na mataifa wote wasikie: nikaokoka katika
kanwa la simba. Naye Bwana ataokoa katika killa tendo 18
baya, atanihifathi kwa ufalme wake wa mbinguni.
Apewe utukufu milele na milele. Amina.

Salimie Priska, na Akula, na nyumba ya Onesiforo. 19
Erasto alikaa katika Korinto. Trofimo nimemwacha 20
katika Mileto mgonjwa. Jitahidi kuja mbele ya wakati 21
wa baridi.

Akusalimia Eubulo, na Pudente na Lino, na Klaudia,
ndugu wote.

Bwana Isa Masiya pamoja na roho yako. Neema 22
kwenu. Amina.

WARAKA WA PAOLO MTUME

KWA

TITO.

PAOLO, mtumwa wa Muungu, mtume wa Isa Masiya, 1
kwa imani ya wateule wake Muungu, kwa maarifa ya
kweli iliyo kwa utawa, katika tumaini la uzima wa milele, 2
aliyeuhidi Muungu, asiye na uwongo, mbele ya zamani
za milele; akalionyesha wakati wake neno lake, katika 3
habari nililoaminiwa mimi kwa amri ya Mwokozi wetu
Muungu; kwa Tito, mwanangu mimi katika imani tu- 4
liyoishariki: Neema, rehema, amani, ya Muungu Baba,
na Bwana Isa Masiya Mwokozi wetu.

Kwa hiyo nalikuacha katika Krete, uyatengeneze 5

- yaliyosalia, ukaweke mji kwa mji wazee, kama nilivyo-
 6 kuamuru, akiwa mtuhakustakiwa, mumewa mke mmoja,
 akiwa na watoto wa imani, wasio na jeuri, na wenyi
 adabu.
- 7 Kwani imempasa askafu asishtakiwe, kama wakili wa
 Muungu; si mkaidi, si mwenyi chuki, si mnywa mvinyo,
 8 si mpigaji, si mpenda fayida ya aibu; lakini mkaribishaji,
 mpenda wema, wa kiasi, wa haki, mtakatifu, ajizuiaye,
 9 ashikaye neno la imani alilofundishwa, apate kuweza
 kuonya katika elimu ya uzima, na kuwashinda wanenao
 juu yake.
- 10 Kwani wako wengi wasio na adabu, wanenao burre,
 11 wadanganyao, nao wa kwanza wa tohara; imepasa wa-
 zibwe kanwa: wanaopindua nyumba pia, wakifundisha
 isiyopasa kwa ajili ya fayida ya aibu.
- 12 Amesema mtu wao, nabii wao wenyewe, Wakrete si-
 kuzote wawongo, nyama wabaya, matumbo mazito.
 13 Ushahidi huu ni kweli. Kwa sababu hiyo uwakemee
 14 kwa ukali, wapate uzima katika imani, wasisikilize hadi-
 thi za Kiyahudi na amri za watu waliogeuka katika
 kweli.
- 15 Yote ni safi kwao walio safi; kwao walio na uchafu,
 wasio na imani, hakuna safi, illa wanao uchafu hatta
 16 moyo na thamiri. Muungu waungama wamemjua; kwa
 matendo wamkania, wakiwa wachukiza, na waasi, na kwa
 killa tendo jema wasiofaa.
- 2 ILLA wewe uyaseme yaliyoipasa elimu ya uzima:
 2 watu wazee wawe wasiolewa, wenyi taratibu, wenyi
 kiasi, wenyi uzima katika imani, katika upendano, ka-
 3 tika uvumilivu. Hivi na waanaake wazee, kwa mwene-
 ndo wenyi utakatifu, si washtakio, si watumiao mvinyo
 4 mwingi, wafundishao mema; wawatie kadiri waanaake
 vijana, kuwapenda waume wao, kuwapenda watoto wao,
 5 kuwa na kiasi, safi, wakaa nyumbani, wema, watii waume
 wao; neno la Muungu lisinenwe unajisi.
- 6 Vijana tena hivyo uwaonye kuwa na kiasi, katika
 7 yote ukijionyesha namna ya matendo mema, katika elimu
 8 yasiyoharibika, utaratibu, pasipo kuoza, neno lenyi uzima,
 lisilohukumika; yule aliye juu yako atahayarike, asiye
 na neno thaifu kwa mambo yenu.
- 9 Watumwa wawatii bwana zao, wakiwa wapendezao
 10 pote, wasiojibu, wasiokwiba, lakini wakionyesha amini

yote njema ; elimu ya mwokozi wetu Muungu waipambe katika yote.

Kwani neema ya Muungu iwaokoayo watu wote ime- 11
onekana, ikifundisha sisi tukizikataa unajisi na tamaa 12
za duniani, tuende kwa kiasi, na haki, na utawa, katika
ulimwengu wa sasa, tukilitazamia tumaini lenyi mbaraka, 13
na wonyesho wa utukufu wake Muungu mkuu na Mwokozi
wetu Isa Masiya ; aliyejitoa kwa ajili yetu, atuko- 14
mboe katika uthalimu wote, akajisafishie watu wa miliki,
wawivu kwa matendo mema.

Haya unene ukaonye, ukakemee kwa nguvu yote. 15
Mtu asikutharau.

UWAKUMBUSHE watii ukuu na uwezo, wawafuate **3**
wenyi nguvu, wawe tayari kwa killa tendo jema, wasi- 2
mnenee mtu unajisi, wawe wanana, wema, wakionyesha
upole wote kwa watu wote.

Kwani tulikuwa na sisi tusio na akili, kuasi, kukosa, 3
kutumikia tamaa na anasa nyingi, tukienda katika uovu
na hasidi, kuchukiza na kuchukiana.

Illakini wema na upenzi kwa watu wa Mwokozi wetu 4
Muungu umeonekana, si kwa matendo ya haki tuliyoya- 5
tenda sisi, illa kwa rehema yake yeye, ametuokoa, kwa
kiogeo cha kuzaliwa kwa pili, na kufanyika mpya kwa Ro-
ho Mtakatifu, aliyetumwagia kwa wingi kwa Isa Masiya 6
Mwokozi wetu ; tupate, tukifanyizwa haki katika neema 7
yake, kufanyika warithi kwa tumaini la uzima wa milele.

Neno amini, na mambo haya nataka uyanene kwa 8
nguvu, wale waliomwamini Muungu wakumbuke kue-
ndelea katika matendo mema. Haya mazuri na kwa
fayida ya watu. Maswali ya upuuzi, na vitabu vya 9
vizazi, na ugomvi, na mashindano ya sheria, uyaepuke ;
kwani hayana fayida, nayo ubatili.

Mtu mzushi, baada ya kumrudi marra moja ao mbili, 10
mkatae, ukijua kama huyu amepinduka, naye akosa, 11
akijihukumu mwenyewe.

Nitakapompeleka Artema kwako, ao Tukiko, ujita- 12
hidi kuja kwangu hatta Nikopoli : kwani huko nimeona
vema kukaa wakati wa baridi. Zena mjua sheria, na 13
Apollo, upeleke kwa bidii, kitu kisiwapungukie. Walio 14
wetu wajifunze kuendelea katika matendo mema kwa
matumio ya lazima, wasiwe hawazai. Wakusalimia 15
walio nami wote. Wasalimie watupendao katika imani.
Neema kwenu nyote. Amina.

WARAKA WA PAOLO MTUME

KWA

FILEMONI.

- 1 PAOLO, mfungwa wake Masiya Isa, na Timoteo
aliye ndugu, kwa Filemoni mpendwa na mtenda naswi,
2 na Apfia mpendwa, na Arkippo aliye asikari pamoja na-
3 swi, na kanisa lilioko nyumbani mwako: Neema kwenu
na amani ya Muungu Baba wetu na Bwana Isa Ma-
siya.
- 4 Namshukuru Muungu wangu siku zote nikipoku-
5 mbukā wewe katika kuomba kwangu, nikisikia mapenzi
na imani yako, uliyo nayo kwa Bwana Isa na kwa wa-
6 takatifu wote; hatta usharika wa imani yako uwe na
nguvu, katika kujua sana killa wema ulio kwenu, katika
7 Masiya Isa. Kwani furaha nyingi tunazo na faraja
kwa sababu ya mapenzi yako, kama mioyo yao wataka-
tifu waburudishwa na wewe, ndugu.
- 8 Kwa hiyo, nisipokuwa na hofu kabisa nikuamuru ka-
9 tika Masiya iliyopasa, afathali kwa mapenzi nasihi, ni-
kiwa kama Paolo mzee, na sasa mfungwa wake Isa Ma-
siya.
- 10 Nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu, niliyemzaa ka-
11 tika mafungo yangu, Onesimo, aliye zamani hakukufaa,
12 illa sasa atufaaye sana wewe na mimi: niliyempeleka
13 kwako, nawe umkubali, ndiye moyo wangu: niliye-
mtaka akae nami, apate kuningojea mahali pako katika
14 mafungo ya anjili: illa sikupenda kutenda neno pasipo
nia yako; wema wako usiwe kama pasipo buddi, illa
kwa moyo.
- 15 Labuda ndiyo sababu amefarakana nawe kitambo,
16 umpokee tena hatta milele; si kama mtumwa tena, illa
juu ya mtumwa, ndugu aliyependwa, kwa mimi sana,
naye kwako si zayidi, katika mwili na katika Bwana?
17 Ukiniona mimi mshariki, mkubali buyu kama mimi.
18 Kama amekuthulumu, ao amewiwa, uniandikie mimi;
19 mimi Paolo nimeandika kwa mkono wangu, nitakulipa:

nisikwambie kama nakuwia na moyo wako. Haya, 20
ndugu, nikufayidie katika Bwana : uniburudishe moyo
katika Masiya. Nikitumainia kutii kwako nimekua- 21
ndikia, nikijua kama utazidi kufanya kuliko ninenavyo.

Illakini uniweke tayari pa kukaa : nataraja kwa ku- 22
omba kwenu nitaneemeshwa kwenu.

Akusalimia Epafra, aliyefungwa pamoja nami katika 23
Masiya Isa ; Marko, Aristarko, Dema, Luka, watendao 24
nami. Neema ya Bwana wetu Isa Masiya pamoja na 25
roho yenu. Amina.

WARAKA WA PAOLO MTUME

KWA

WAEBRANIA.

KWA sehemu nyingi na kwa namna nyingi aliye- 1
sema zamani nazo baba katika manabii, Muungu, huyu 2
mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana,
aliye'mweka mrithi yote, kwaye akazifanya zamani ;
aliye akiwa mwanga wa utukufu na namna ya nafsi 3
yake, achukuaye yote kwa tamko la uwezo wake, aki-
fanya peke yake utakaso wa thambi, akaketi mkono wa
kuume wa ukuu palipo juu ; akiwa mwema kuwapita 4
malaika kwa kadiri alivyorithi jina mashuhuri kuliko
wao.

Kwani malaika yupi, aliyemwambia lini, Mwana 5
wangu ndiwe, mimi leo nimekuzaa ? na tena, Nitakuwa
kwake baba, naye kwangu mwana ? Tena akimleta 6
mzaliwa wa kwanza katika ulimwengu anena, Na ma-
laika wote wa Muungu wamwabudu.

Kwa malaika anena, Afanyaye malaika zake roho, na 7
watendao kazi yake ndimi za moto. Na kwa Mwana, 8
Kiti chako, ee Muungu, hatta zamani na milele ; fimbo
ya kunyoka fimbo ya ufalme wako. Umependa haki, 9
ukachukia maasi ; kwa hiyo Muungu, Muungu wako,
amekutia mafuta, mafuta ya kucheka kuliko wenzako.
Na, Wewe mwanzo, Bwana, umetia misinji ya inchi, na 10

11 kazi ya mikono yako ni mbingu; hizi zitaharibika;
 12 wewe ukaaye; zote kama nguo zitachakaa, na kama
 vazi utazizinga, nazo zitabadilika: illa wewe ndiwe
 uliye, wala miaka yako haitapunguka.

13 Kwa malaika yupi amenena tena, Uketi mkono wa
 kuume wangu, hatta nitakapoweka adui zako chini ya
 14 nyayo zako? Si hawa wote roho zitumikazo, waki-
 tumwa kuwangojea watakaourithi wokovu?

2 KWA hiyo imepasa kuzidi kuziangalia sisi tulizosi-
 2 kia, tusipotee. Kwani neno lililonenwa kwa malaika
 likiwa imara, na killa kosa na kuasi kumepewa kisasi
 3 cha haki; tupateje sisi kujiponya, tusipoangalia wokovu
 kama huo? uliokuwa na mwanzo ukinenwa na Bwana,
 4 ukathubutika kwetu nao waliosikia; Muungu akiongeza
 ushahidi kwa ishara, na ajabu, na nguvu ngingengine,
 na kugawanya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda.

5 Kwani hakuutia ulimwengu utakaokuwa chini ya
 6 malaika, tunaounena. Kwani mmoja ameshuhudia ma-
 hali hivi, Mwana Adamu ni nini, umkumbuke? ama
 7 mwana wa mtu, umwangelie? Umemfanya mdogo
 punde kuliko malaika, ukamtia kwa taji utukufu na
 heshima, uka'mweka juu ya kazi za mikono yako;
 8 umetia yote chini ya nyayo zake.

Katika kutiwa yote chini yake hakutoa kitu kisicho-
 tiwa. Illa sasa hatujaona yote yametiwa chini yake.

9 Naye aliyefanyika mdogo punde kuliko malaika, twa-
 mwona Isha, kwa kupatwa na kufa, ametiwa taji utukufu
 na heshima. Hatta kwa neema ya Muungu ameonja
 10 kufa kwa ajili yao wote. Kwani imempasa yule, kwaye
 yote, na kwa ajili yake yote, akileta waana wengi kwa
 utukufu, amkamilishe kiongozi cha wokovu wao kwa
 11 mateso. Kwani atakasaye nao watakasikao wote wa
 mmoja: kwa ajili hii hatahayariki kuwaita ndugu zake,
 12 akinena, Nitatoa jina lako kwa ndugu zangu; kati ya
 13 kanisa nitakwambia: na tena, Nitakuwa nimemwamini:
 na tena, Tazama mimi na watoto niliopewa na Muungu.

14 Bassi kama watoto wameshariki damu na mwili, naye
 vivyo akatwaa sehemu katika haya, illi kwa kufa amha-
 15 ribu aliye na uwezo wa kufa, ndiye shetani, akawaokoe
 wale waliokuwa kwa hofu ya kufa maisha yao yote
 wenyi utumwa.

16 Kwani yakini hakutwaa ya malaika, lakini ametwaa

ya uzao wa Ibrahimu. Hivi ikampasa kwa yote kufa- 17
 nanishwa na ndugu zake, apate kuwa mkohani mkuu
 mwenyi rehema na amini katika mambo ya Muungu,
 hatta kusuluhisha thambi za watu. Katika kuwa ame- 18
 teswa akijaribiwa, aweza kuwasayidia wanaojaribiwa.

HIVI, ndugu watakatifu, wenyi sehemu ya wito wa 3
 mbinguni, mfikirini sana Mtume na Mkohani Mkuu wa
 kuungama kwetu, Isa; aliye amini kwake aliyemfanya, 2
 kama na Musa katika nyumba yake yote. Kwani huyu 3
 amestabilishwa heshima kuliko Musa, kama alivyo na
 heshima aitengenezaye zayidi ya nyumba. Kwani killa 4
 nyumba ametengenezwa na mtu; naye aliyetengeneza
 yote ni Muungu.

Na Musa amini katika nyumba yake yote kama mtu- 5
 mishi, kwa ushahidi wao yatakayonenwa; Masiya kama 6
 mwana, juu ya nyumba yake; nyumba yake ni sisi,
 tukishika imara uthabiti na kujisifu kwa tumaini hatta
 mwisho.

Kwa hiyo, kama alivyonena Roho Mtakatifu, Leo, 7
 mkisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, 8
 kama katika kukasirisha, siku ya ujaribu katika jangwa,
 waliponijaribu baba zenu, katika kuhakiki, wakaona 9
 matendo yangu miaka arobaini. Kwa hiyo nikachukizwa 10
 na kizazi hiki, nikasema, Wanakosa sikuzote mioyoni:
 hawa hawakujua njia zangu; kama nilivyoapa katika 11
 hasira yangu, wasiingie rahani mwangu.

Angalieni, ndugu, usiwe kabisa kwenu moyo mbaya 12
 wa kutoa kuamini katika kumwacha Muungu aliye hayi.
 Lakini mwonyane siku kwa siku, hatta iitwapo leo; mtu 13
 wenu asifanyike mgumu katika udanganifu wa thambi.
 Kwani tumepewa sehemu na Masiya, tukishika imara 14
 mwanzo wa tumaini hatta mwisho: katika kunena, Leo, 15
 mkisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu,
 kama katika kukasirisha. Kwani nani waliolisikia wa- 16
 kakasirisha? sio wote waliotoka katika Misri kwa
 Musa? Na nani aliochukizwa nao miaka arobaini? sio 17
 waliokosa, mizoga yao ikaanguka katika jangwa? Nani 18
 aliowaapia wasiingie katika raha yake, illa wasioamini?

Bassi twaona kama hawakuweza kuingia kwa sababu 19
 ya kukosa imani.

TUOGOPE tena, ikisalia ahadi ya kuingia katika 4
 raha yake, mmoja wapo wenu aonekane amepunguka.

- 2 Kwani na sisi tumehubiriwa kama wale: lakini neno la kusikiwa halikuwafaa wale, lisipochanganyika na imani
- 3 kwao waliosikia. Kwani twaingia katika raha tulio na imani; kama alivyosema, Nilivyoapa katika hasira yangu, wasiingie katika raha yangu: kazi zikiwa zime-
- 4 kuwa tangu kuandikwa ulimwengu. Kwani alisema hivi pahali kwa siku ya saba, Akastarehe Muungu katika kazi zake zote siku ya saba. Na hapa tena, Wasiiingie katika raha yangu.
- 6 Bassi ikisalia watu waingie katika raha yake, nao waliohubiriwa kwanza wasipoingia kwa kukosa imani,
- 7 aandika tena siku, Leo, akinena katika Daud baada ya wakati kama ule, kama alivyotangulia kunena, Leo mkisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu.
- 8 Kwani Isa kama angaliwastarehesha, hangalisema neno tena la siku ngineyo baadaye.
- ⁹₁₀ Illa imesalia wastareheke watu wa Muungu. Kwani aingiaye katika raha yake, yule amestarehe katika
- 11 kazi zake, kama Muungu katika zake yeye. Tufanye bidii tuingie katika raha ile, asianguke mtu katika mfano ule wa kuasi.
- 12 Neno la Muungu ni hayi na tendaji, likatalo kuliko upanga mkali kuwili, liwezalo hatta kutenga maisha na roho, viungo na bongo, lihukumulo nia na fikara za moyoni. Wala hakuna kiumbe kisichoonekana mbele yake, illa yote matupu na yamefunuliwa machoni pake tumnaye.
- 14 Bassi tukiwa na Mkohani Mkuu, aliyepita mbinguni, Isa Mwana wake Muungu, tulishike tuliungamalo.
- 15 Kwani hatunaye mkohani mkuu asiyeweza kuziona thaifu zetu, lakini amejaribiwa kabisa kwa ginsi moja, 16 pasipo thambi. Bassi tuje, tusiwe na hofu, kwa kiti cha neema, tupewe rehema na tuone neema kwa msaada wakati wake.
- 5 KILLA mkohani mkuu, aliyetwaliwa katika watu, amewekwa kwa ajili ya watu mbele ya Muungu, atoe
- 2 sadaka na thabihu kwa ajili ya thambi: awaonaye kwa kadiri wajinga na wakosao, kwani na yeye yu katika
- 3 uthaifu. Kwa hiyo imempasa kama kwa ajili ya watu, hivi kwa ajili yake yeye, kutoa kwa thambi.
- 4 Wala mtu hajitwalii heshima hii, illa aliyeitwa na
- 5 Muungu, kama na Haruni. Hivi naye Masiya, haku-

jitukuza kuwa Mkohani Mkuu, illa yeye aliyemwambia,
 Mwana wangu u wewe, mimi leo nimekuzaa: kama 6
 panginepo, Wewe Mkohani milele kwa ginsi ya Melki-
 zedeki. Aliye, siku za mwili wake, ametoa kuomba na 7
 kusihi kwa yeye awezaye kumwokoia katika kufa, kwa
 kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa upole wake,
 hatta akiwa Mwana, amejifunza kutii kwa haya yaliyo- 8
 mpata; naye akikamilika amekuwa sababu ya wokovu 9
 wa milele kwao wote wanaotii; akitajwa na Muungu 10
 Mkohani Mkuu kwa ginsi ya Melkizedeki.

Kwa huyo tunayo maneno mengi tuyanene, nayo 11
 yasiyofasirika upesi, mkiwa wazito wa masikio. Kwani 12
 ikiwapasa kuwa wakufunzi kwa wakati *uliopita*, mwa-
 hitaji tena mtu awafundishe nini elimu za kwanza za
 maneno ya Muungu: mmekuwa mwataka maziwa, wala
 si lisho lenyi nguvu. Kwani killa atwaaye maziwa 13
 hajui sana neno la haki, kwani ni mtoto. Lisho lenyi 14
 nguvu ni lao waliokamilika, walio na akili zilizozoea
 kwa kutumiwa, kuyapambanua mazuri na mabaya.

KWA hiyo, tukiliacha neno la kwanza lake Masiya, 6
 tuendeleo kwa ukamilifu; tusitie tena misinji ya kutubu
 katika matendo mafu, na imani kwa Muungu, elimu ya 2
 mabatizo, na kutia mikono, na kufufuka katika wafu,
 na hukumu ya milele. Ndilo tutakalofanya, tukijaliwa 3
 na Muungu. Kwani haiyamkini waliokwisha pewa 4
 nuru, wakilionja lililotolewa katika mbinguni, wakipokea
 sehemu ya Roho Mtakatifu, walioonja neno zuri la 5
 Muungu na nguvu za ulimwengu ujao, wakaanguka, 6
 kuwafanya marra ya pili kwa toba; wakimsulibisha
 kwao Mwana wa Muungu, wakamfanya aibu la wazi.

Kwani inchi inywayo mvua ijiayo marra nyingi, iki- 7
 zaa mboga za kuwafaa wailimao, imepewa baraka na
 Muungu: ikitoa miiba na magugu yasiyofaa, ni karibu 8
 ya laana, mwisho wake ni kuteketea.

Lakini tumewathania, wapenzi, mambo mema yenyi 9
 wokovu, hatta tukisema hivi: kwani Muungu hana 10
 thulumu, ayasahau matendo yenu, na upendano, mlio-
 uonyesha kwa jina lake, mliowangojea watakatifu, na
 mngojeao. Nawatakia killa mmoja wenu aonyeshe 11
 bidii ileile kwa kujaa tumaini hatta mwisho: msiwe 12
 wavivu, illa wafuatao wale waliorithi ahadi, kwa imani
 na uvumilivu.

13 Kwani Muungu, akimwahidia Ibrahimu, asipokuwa
na neno kuu la kuapia kuliko Yeye, akaapa kwa mwe-
14 nyewe, akinena, Kubariki nitakubarikia, kuzidisha nita-
15 kuzidisha. Na hivi kwa uvumilivu akaipata ahadi.
16 Kwani watu wamwapia aliye mkuu: na kikomo cha
killa ugomvi kufanya imara ni kiapo.

17 Katika hiyo, Muungu akitaka kuzidi kuwaonyesha
wairithio ahadi ginsi yasivyobadilika mapenzi yake,
18 akajiweka kati kwa kiapo, illi kwa mambo mawili yasi-
yobadilika, Muungu asipoweza kunena uwongo, tuwe
na faraja imara, tukimbiao tulishike tumaini lilioko
19 mbele yetu; tukiwa nalo kama nanga ya roho, salama
20 na imara, iliyoingia ndani katika pasia la ndani, humo
alimoingia mtangulia kwa ajili yetu, Isa, aliye kwa
ginsi ya Melkizedeki Mkohani Mkuu hatta milele.

7 KWANI huyu Melkizedeki, mfalme wa Salemi, mko-
hani wa Muungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu
2 aliporudi katika kuwaua wafalme, akambariki, aliyega-
wanyikiwa na Ibrahimu sehemu ya kumi katika yote
(kwanza kwa tafsiri Mfalme wa haki, tena na Mfalme
3 wa Salemi, ndio Mfalme wa amani; hapana baba,
hapana mama, hapana wazee, wala mwanzo wa siku,
wala mwisho wa maisha, illa akifananishwa na Mwana
4 wa Muungu), hukaa mkohani dayima. Angalieni mtu
huyu alivyo mkuu, aliyepewa na Ibrahimu baba mkuu
sehemu ya kumi ya mateka yaliyo mema.

5 Nao waana wa Lawi waliopokea ukohani, wana amri
kwa torati wawatwalie sehemu ya kumi watu walio
ndugu zao, wakiwa wametoka katika viuno vya Ibra-
6 himu. Illa yeye asiyehesabika katika jamaa zao aka-
mtwalia ya kumi Ibrahimu, naye aliye na ahadi alibari-
7 kiwa naye. Hapana shaka kabisa mdogo hubarikiwa
8 na mkuu. Hivi watu wafao wapokea sehemu ya kumi,
9 huko aliyeshuhudiwa yu hayi. Hatta, kusema neno,
kwa Ibrahimu naye Lawi, apokeaye ya kumi, ametwa-
10 liwa ya kumi; kwani alikuwa katika viuno vya babaye,
alipokutana naye Melkizedeki.

11 Kwani ukamilifu kama ungalikuwa kwa ukohani wa
Kilawi (kwani watu chini yake walipewa torati), yata-
kaje tena mkohani mwingine aondoke wa ginsi ya Mel-
12 kizedeki, wala asiitwe kwa ginsi ya Haruni? Kwani
ukohani ukibadilika, hapana buddi na sheria ibadilike.

Kwani aliyenenewa haya ni mtu wa kabila ngineyo, 13
isiyo na mtu aliyeingojea mathbahu. Kwari thahiri 14
kama Bwana wetu ametokea katika Yuda, kabila
isiyonenwa na Musa kwa mambo ya ukohani.

Imezidi sana kuwa thahiri, kama kwa mfano wa 15
Melkizedeki mkohani mgine amesimama, asiye kwa 16
sheria ya amri ya mwilini, illa kwa nguvu za uzima
usiolegezekana: kwani ashuhudu, kwamba Wewe 17
Mkohani hatta milele kwa ginsi ya Melkizedeki.

Ondoleo la amri iliyotangulia limekuwa kwa uthaifu 18
na kutoa kufaa: kwani torati haikutimiza neno, illa 19
kuleta baadaye tumaini lililo bora, kwalo twamkaribia
Muungu.

Na kama si pasipo kiapo (kwani wale wakohani ²⁰₂₁
pasipo kiapo, huyu kwa kiapo; akamwambia, Bwana
ameapa wala hageuki, Wewe Mkohani milele kwa
ginsi ya Melkizedeki), hivi wa agano lililo bora aliye 22
mthamini ni Isa.

Nao wale walikuwa wakohani wengi, kwa sababu 23
ya kufa hawakupata kukaa; huyu, kwa kukaa yeye 24
milele, anao ukohani us'opita. Kwa hiyo aweza ku- 25
waokoa kabisa wamjiao Muungu kwa yeye, akiwa
sikuzote hayi ajitie kwa ajili yao.

Imetupasa kuwa na mkohani mkuu kama kuyu, 26
mtakatifu, asiye na uovu, safi, aliyetengwa katika
wakosaji, aliye juu kuliko mbingu: asiyelazimishwa 27
killa siku, kama wakohani wakuu wale, kwanza kutoa
thabihu kwa thambi zake yee, baadaye kwa watu:
kwani ameifanya marra moja, akijitoa mwenyewe. Kwa- 28
ni torati iliwa weka wakohani wakuu walio na uthaifu:
neni la kuapa, lililo baada ya torati, Mwana, aliyekami-
lika hatta milele.

JUMLA yao yaliyonenwa, tunaye Mkohani Mkuu, **8**
akaaye mkono wa kuume wa kiti cha Ukuu katika
mbingu, afanyaye ibada, na wa hema iliyo ya kweli, **2**
aliyeiweka Bwana, wala si mwana Adamu.

Kwani killa mkohani mkuu amewekwa atoe sadaka **3**
na thabihu: hana buddi na huyu awe na kitu akitoe.

Akiwa tena katika inchi, hangalikuwa mkohani, wa- **4**
kiwa watoao sadaka kwa torati, wutumikao kwa mfano **5**
na kivuli chao yaliyo mbinguni, kama Musa alivyoagi-
zwa akiwa katika kuitengeneza hema: kwani, Angalia,

asema, uifanye kwa namna uliyoonyeshwa katika mlima.

- 6 Sasa amepewa dini isiyo ileile, kama alivyo mleta agano lililo bora, lililowekwa juu ya ahadi zilizo bora.
- 7 Kwani la kwanza kama lingalikuwa halina upungu-
8 fu, haingalitafutikana nafasi kwa lile la pili. Kwani akionya upungufu kwao, anena, Angalia, siku zinakuja, anena Bwana, nami nitafanyiza kwa nyumba ya Israeli
9 na kwa nyumba ya Yuda agano jipya; wala si kwa agano nililowafanyia baba zao, siku nilipowatwaa mkono kuwaleta katika inchi ya Misri; kwa sababu hawa hawakukaa katika agano langu, wala mimi si-
10 kuwaangalia, anena Bwana. Hilo ndilo agano nitakalowafanyia nyumba ya Israeli baada ya siku zile, anena Bwana: Nitatia sheria zangu katika akili zao, na juu ya moyo wao nitaziandika: nami nitakuwa kwao
11 Muungu, nao kwangu watu. Wala hawatafundisha killa mtu jirani wake, na killa mtu ndugu yake, akinena, Mjue Bwana: ya kuwa wote watanijua, tangu
12 mdogo hatta mkuu wao. Kwamba nitakuwa na rehemama kwa thulumu zao, wala thambi zao wala makosa
13 yao sitayakumbuka tena. Akinena Jipya, amelifanya la kwanza kukuu. Iliyo kukuu na iliyochakaa ni karibu kutoweka.

9 NALO la kwanza likawa na hukumu za dini, napo
2 patakatifu, pa duniani. Kwani hema ya kwanza ilite-
ngenezwa, katika yake taa, na meza, na wonyesho wa
3 mikate, palipoitwa Patakatifu. Nyuma ya pasia la pili
4 hema iliyoitwa Takatifu ya matakatifu; iliyo nayo vukizo la thahabu, na sanduku ya agano, iliyofunikizwa pote na thahabu, katika yake kopo la thahabu lenyi manna, na fito ya Haruni iliyochupuka, nazo meza za
5 agano; juu yake na Makerubi ya utukufu yakitia kivuli mahali pa rehema; kwa haya hatunao sasa kunena sehemu kwa sehemu.

6 Haya yakiwa yametengenezwa, katika hema ya kwanza wakohani huingia sikuzote wakitimiza dini: katika ile ya pili marra moja kwa mwaka peke yake mkohani mkuu, wala si pasipo damu, aitoe kwa ajili ya matelezo
8 yake yeye na yao watu: hivi huonyesha Roho Mtakatifu ya kwamba njia ya matakatifu haijathihirishwa, hema
9 ya kwanza ikisimama mahali pake. Ndio mfano wa wakati uliokuwako; katika yake sadaka na thabilu

zikitolewa, zisizoweza kumtimiza moyo aabuduye, illa 10
katika vyakula na vinywa, na maosheo manginemangine,
hukumu za mwili, walizotiwa hatta wakati wa kute-
ngeneza.

Masiya akiwapo, Mkohani Mkuu wa mema yajayo, 11
kwa hema iliyo bora na kamilifu, isiyofanyika kwa mi-
kono, ndiyo isiyo ya kiumbe biki, wala kwa damu ya 12
mbuzi na ndama, illa kwa damu yake yeye, aliingia marra
moja katika patakatifu akiisha kupata ukombozi wamilele.

Kwani damu ya mbuzi na ng'ombe na majifu ya 13
mwana ng'ombe mke yaliyonyunyizwa juu yao wachafu,
kama yangalisafisha kwa kutakasa mwili, si zayidi damu 14
yake Masiya, aliyejitoa mwenyewe kwa Muungu pasipo
hatiya kwa Roho wa milele, atatutakasa moyo katika
matendo mafu kwa kumwabudu Muungu aliye hayi?

Na hivi ni mleta agano lililo jipya, hatta akiwa ame- 15
kufa kwa ukombozi wa makosa yaliyo katika agano la
kwanza, wapewe walioitwa ahadi ya urithi wa milele.

Kwani agano la urithi lilipo haina buddi kuwa kufa 16
kwake aliyeagana. Agano ni imara juu yao waliokufa; 17
wala haina nguvu kabisa aliyeagana akiwa hayi. Kwa 18
hiyo wala lile la kwanza halikuanzwa pasipo damu.

Kwani killa amri ya sheria ilipokwisha kunenwa na 19
Musa kwa watu wote, akitwaa damu ya ndama na mbuzi
pamoja na maji na sufu nyekundu na hussopo, akanyu-
nyizia na kitabu na watu wote, akinena, Ndiyo damu 20
ya agano, Muungu alilowaamria. Na hema na vyombo 21
vyote vya ibada akavinyunyizia damu vivyo. Na karibu 22
na yote hutakaswa na damu kwa torati: wala pasipo
kumwaga damu hapana ondoleo. Kwani sharti ishara 23
zao zilizo mbinguni zitakasike na haya; nayo yaliyo
mbinguni kwa thabihu njema kuliko hizi.

Kwani si katika patakatifu palipofanyika kwa mikono 24
Masiya alipoingia, ishara zao palipo pa kweli, illa katika
uwingu mwenyewe, aonekane sasa usoni pa Muungu kwa
ajili yetu; wala asijitoe marra nyingi, kama mkohani 25
mkuu aingiavyo katika patakatifu mwaka kwa mwaka,
kwa damu isiyo yake; kwani hivi ingalimpasa kuteswa 26
marra nyingi tangu kuwekwa ulimwengu: illa sasa
marra moja, zamani zikitimia, amekana kwa ondo-
leo la thambi kwa kutolewa yeye.

Na kama imewapasa watu marra moja kufa, na baadaye 27

28 hukumu ; hivi Masiya, akitolewa marra moja, aziondolee thambi za watu wengi, marra ya pili, pasipo thambi, atonekana nao wantazamiao, kwa wokovu.

10 KWANI torati ikiwa na kivuli cha mema yajayo, wala si mfano wa matendo, killa mwaka thabihu zilezile, walizozitoa dayima, haziwezi po pote kuwatimiza
2 waliokuja kwao : kama hiyo hazingalikoma kutolewa, kwa sababu waabuduo hawangalikuwa tena na moyo
3 wa thambi ? Lakini katika hizo ukumbuko wa thambi killa mwaka.

4 Kwani haiwezi damu ya ng'ombe na mbuzi kuondoa
5 thambi. Kwa hiyo akija ulimwenguni asema, Sadaka na
6 thabihu hukuzipenda ; umenifanyizia mwili. Kafara na
7 thabihu hukupendezewa nazo : ndipo niliponena, Angalia naja (katika mwanzo wa chuo nimeandikiwa), nilitende,
8 ee Muungu, ulipendalo. Akinena juu, ya kwamba, Thabihu, na sadaka, na kafara, na kwa thambi hukuzipenda, wala hukupendezewa nazo (zilizotolewa kwatorati),
9 halafu akanena, Angalia naja, nilifanye ulipendalo. Aondoa la kwanza, la pili alisimamishe. Katika hilo alipendalo tumetakasika, kwa kutolewa mwili wake Isa Masiya marra moja tu.

11 Na killa mkohani husimama siku kwa siku akifanya ibada, akitoa marra nyingi thabihu zilezile, zisizoweza
12 po pote kuondoa thambi. Huyu akiisha kutoa thabihu moja kwa thambi kwa dayima, ameketi mkono wa kume wa Muungu, akingoja baadaye hatta adui zake zitiwe
13 chini ya nyayo zake. Kwani kwa sadaka moja amewatimiza kwa dayima wanaotakasika.

15 Naye Roho Mtakatifu atushuhudia. Kwani baada
16 ya kunena, Ndilo agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana, nitatia sheria yangu moyoni
17 mwao, na juu ya akili zao nitaziandika, Wala thambi
18 zao wala makosa yao sitayakumbuka tena. Ondoleo lao lilipo, hapana tena sadaka kwa thambi.

19 Bassi tukiwa, ndugu, hatuna hofu katika kuingia
20 kwa patakatifu kwa damu ya Isa, njia aliyoituanzia
21 mpya na hayi katika pasia, ndiyo mwili wake ; tukiwa tena na Mkohani Mkuu juu ya nyumba yake Muungu ;
22 tukaribie kwa moyo wa kweli katika kujaa imani, tukinyunyizwa moyo katika ufahamu mbaya, tukaoshwa
23 mwili kwa maji safi. Tushike kuungama tumaini

pasipo kugeuka. Amini ndiye aliyeahidi. Tukafiki- 24
riane kwa bidii ya mapenzi na matendo mema; tusiache 25
kukusanyika pamoja, kama desturi ya wangineo, lakini
tukionya; na tukizidi, kama tuonavyo siku ile ina-
karibia.

Kwani wakosao kasidi baada ya kupewa kuijua 26
kweli, haikusalia kwao tena thabihu kwa thambi, illa 27
kutazamia kwa hofu hukumu, na moto wa uwivu
utakaowala waasio.

Asiyeifuata torati ya Musa, pasipo huruma, chini ya 28
mashahidi wawili ao watatu, alikufa. Wathanije zayidi 29
amestahili athabu, aliyemkanyaga chini Mwana wa
Muungu, aliyeiona si kitu damu ya agano aliyotakasiwa,
akamfanyia jeuri Roho ya neema? Kwani twamjua 30
aliyenena, Kisasi ni changu, mimi nitalipa, anena
Bwana; na tena, Bwana awahukumu watu wake. Ndilo 31
la hofu kuanguka mkononi mwake Muungu aliye hayi.

Lakini kumbukeni siku za kwanza mlipotiwa nuru, 32
mkastahimili shidda nyingi ya kuuma; ndipo, mlipota- 33
zamiwa kwa mashutumumu na mateso; na ndipo, mkisha-
rikiana nao waliotendewa haya. Kwani mmewahuru- 34
mia waliofungwa, mkavumilia kwa furaha kunyang'a-
nywa mali zenu, mkijua mnazo zilizo zenu zenyi asili
bora katika mbingu zisizokoma.

Msitupie mbali kuthubutu kwenu, kuliko thawabu 35
kuu. Mwahitaji uvumilivu, illi, mkifanya alipendalo 36
Muungu, mpate ahadi. Kwani bado kama kidogo, 37
naye ajaye atakuja, wala hatakawia. Mwenyi haki 38
ataishi kwa imani: illa atakayerudi, moyo wangu
haupendezewi naye. Sisi si wa kurudi kwa kupotea, 39
illa wa imani tupate uzima.

IMANI ndiyo tegemeo lao yaliyotumainiwa, ithubuti- 11
shayo mambo yasiyoonekana. Katika hiyo wakashu- 2
hudiwa wazee.

Kwa imani twajua kama ulimwengu ulifanyika na 3
neni la Muungu, hatta tuyaonayo hayakuwa kwa vitu
vilivyoonekana.

Kwa imani Habil alimtolea Muungu thabihu bora 4
kuliko Kain, kwa hiyo akashuhudiwa kuwa na haki,
Muungu akizishuhudia sadaka zake: kwa hiyo tena
hatta akiisha kufa hunena.

Kwa imani Enok amepewa asione kufa; wala haku- 5

- onekana, kwa sababu ametwaliwa na Muungu : kwani mbele ya kutwaliwa alishuhudiwa amempendeza Muungu. Pasipo imani haiwezekani kumpendeza : kwani sharti amjiaye Muungu aamini ya kwamba yupo, naye awapaye thawabu wamtakao.
- 7 Kwa imani Nuhu akipewa habari ya mambo yasiyonekana bado, akihatharishwa, akatengeneza safina kwa wokovu wa nyumba yake. Kwa hiyo akaiamua dunia, akapata kuirithi haki iliyo kwa imani.
- 8 Kwa imani Ibrahimu akiitwa aende mahali atakapopapata kwa urithi, akasikia, akatoka, asipojua aendako.
- 9 Kwa imani akakaa katika inchi ya ahadi kama ugenini, akikaa katika hema pamoja na Isaak na Yakob,
- 10 warithi pamoja naye ya ahadi ileile : kwani akatazamia mji mwenyi misinji, aujengaye naye auwanyaye Muungu.
- 11 Kwa imani naye Sara akapata nguvu azae mzao, akazaa wakati wa umri ulipopita, akiwa amemwona
- 12 amini aliyeahidi. Hivi katika mmoja, naye kama amekufa, wakapata kuwa kama nyota za mbinguni kwa kuwa wengi, na kama mchanga ulioko ukingoni mwa bahari usiohesabika.
- 13 Hawa wote wakafa katika imani, hawakuzipokea ahadi, lakini wakiziona mbali, wakizisadiki wakasalimia, wakaungama kama walikuwa katika inchi wageni na
- 14 wasafiri. Kwani wanenao haya waonyesha kama wata-
- 15 futa inchi yao. Na kama wangaliifikiria waliyotoka
- 16 walikuwa na nafasi ya kurudi. Sasa wataka iliyo bora, ndiyo ya mbinguni. Hivi Muungu haoni haya kuitwa Muungu wao : kwani amewatengenezea mji.
- 17 Kwa imani Ibrahimu akamtoa Isaak, alipojaribiwa :
- 18 mzao wa pekee akatolewa naye aliyezipokea ahadi ; ali-
- 19 yenenwa, Katika Isaak uzao wako utaitwa : akihesabu kama kuwafufua wafu Muungu awezaye ; kama alivyompokea kwa mfano.
- 20 Kwa imani Isaak akawabarikia Yakobo na Esau, kwa mambo yatakayokuwa.
- 21 Kwa imani Yakobo katika kufa akambariki killa mwana wa Yusuf, akaabudu juu ya ncha ya gongo lake.
- 22 Kwa imani Yusuf, akifariki, akakumbusha kutoka kwao waana wa Israeli ; akaiamria mifupa yake.
- 23 Kwa imani Musa, akizaliwa, akafichwa miezi mitatu

na wazee wake, kwa sababu wakamwona mtoto mzuri; wala hawakuiogopa amri ya mfalme. Kwa imani Musa, 24 akiwa mzima, akakataa kunenwa mwana wa binti Farao; akichagua kupatwa na mabaya pamoja na watu 25 wa Muungu kuliko kuwa na raha ipitayo ya thambi; akiona mali ya kupita hazina za Misri ndiyo shutumu 26 yake Masiya: kwani akaiangalia thawabu. Kwa imani 27 akaacha Misri, asipoogopa hasira ya mfalme: kwani kama aonaye yasiyoonekana hakugeuka. Kwa imani 28 akafanya Pasaka, na kunyunyiza damu, awauaye wazaliwa wa kwanza asiwaguse. Kwa imani wakapita 29 Bahari ya Sham kama pakavuni: Wamisri wakishika kujaribu wakatoswa.

Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipozungu- 30 kwa siku saba. Kwa imani Rahab kahaba hakupotea 31 pamoja nao wasioamini, akiwa amewakaribisha wapelelezi kwa amani.

Ninene nini tena? Wakati haungenitosha kuwaandika 32 Gideon na Barak, Samson na Yeftha, Daud na Samwil na manabii: ndio walio kwa imani wakashinda ufalme, 33 wakafanya haki, wakapata ahadi, wakaziba makanwa ya simba, wakazimia nguvu za moto, wakakimbia ukali wa 34 upanga, wakapata nguvu wakiwa thaifu, wakawa hodari katika vita, wakakimbiza majeshi ya wageni. Waa- 35 naake wakapokea wakifufuka wafu wao.

Wangine wakapigwa hatta kufa, wasipokubali uko- mbozi, wapate ufufuo ulio bora. Wangine wakajaribiwa 36 kwa thihaka na mijeledi, hatta na mafungo na kutiwa gerezani; walitupiwa mawe, walikatwa kwa mismeno, 37 walishawishwa, wakafa wakiuawa kwa upanga; walipotea wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; wakiachwa, wakiteswa, wakitendewa vibaya (dunia isio- 38 wastahili), wakizunguka katika majangwa na katika milima, na mapaango na mashimo ya inchi.

Hawa wote walioshuhudiwa kwa imani hawakuchukua 39 ahadi, Muungu akituonea sisi iliyo bora, wasipate pasipo- 40 kuwako sisi kukamilika.

BASSI tena na sisi, tukiwa tumezungukwa na wingu 12 kama hili la mashahidi, tuweke killa kizito, na thambi iliyoambatana nasi; kwa kustahimili tuende mbio shindano tulilo nalo, tukimwangukia mkuu wa imani na 2 mtimiza, Isa, aliystahimili msalaba kwa furaha iliyo

mbele yake, akiitharau aibu, akaketi mkono wa kuume
3 wa kiti cha Muungu. Mkumbukeni sana aliyestahimili
makatazo haya yao wakosao, msichoke wala msilegee
mioyoni mwenu.

4 Hamjapigana hatta damu, mkishindana na thambi:
5 nanyi mmesahau kuonya, kusema nanyi kama na waana,
Mwanangu, usitharau kurudi kwa Bwana, wala usizimie
6 ukikemewa naye; kwani Bwana ampendaye ndiye amru-
7 diye, naye ampiga killa mwana amkubaliye. Mkista-
himili kurudika, Muungu awatendea kama waana;
8 kwani mwana gani yule, baba asiyemrudi? Mkiwa pa-
sipo kurudika, walikosharikiana wote, wa haramu ninyi,
9 wala si waana. Hatta na sisi tulikuwa na baba za mwi-
lini walioturudi, tukawasikiliza: si zayidi sana tumtii
10 Baba wa roho, tukaishi? Hawa siku chache walivyopo-
penda wameturudi: huyu ilivyopasa, illi tupate haki
11 yake. Kurudika kwote wakati wake hakuonekani kuwa
na furaha, illa uzito: baadaye hutoa matunda yenyi
amani ya haki kwao waliozcezwa.

12 Kwa hiyo nyosheni mikono iliyoangika, na magote
13 yaliyolegea; mkafanye njia za kunyoka kwa miguu
yenu, ishangaayo isipotee, illa afathali ipone.

14 Fuateni amani kwa wote, na utakatifu, pasipo huo
15 hapana atakayemwona Bwana: mkiangalia mtu asipu-
nguke katika neema ya Muungu, shina la uchungu
lisichupuke kwenu liwasumbue, na kwa hilo wengi wa-
16 tiwe uchafu. Mtu asiwe mwasharati, wala mnajisi,
kama Esau, aliyebadili urithi wake kwa chakula kimoja.
17 Kwani mwajua kama baadaye alipotaka kuurithi mba-
raka akakatazwa, wala nafasi ya kutubu hakuiona, hatta
akiitafuta sana kwa machozi.

18 Kwani hamkuja kwa mlima wa kupapaswa, uwakao
19 na moto, na tháruba na giza na tufanu, na kulia paanda,
na sauti ya maneno; hatta wale walioisikia wakataka
20 neno lisiwajie tena: kwani hawakuchukuliana na agano,
Hatta nyama akiugusa mlima, atupiwe mawe hatta
21 kufa, ao achomeke na mkuke; nayo yaliyoonekana ya
kuogofya, hatta Musa akanena, Nimeshikwa na hofu na
tetemeko.

22 Lakini mmekuja kwa mlima Sayuni, na mji wa Mu-
ungu aliye hayi, Yerusalemi wa mbinguni, na malaika
23 elfu nyingi, na kusanyiko kuu na kanisa lao wazaliwa

wa kwanza, walioandikwa mbinguni, na Muungu mhukumu wote, na roho zao wenyi haki waliokamilika, na 24
mleta agano jipya, Isa, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habil.

Angalieni msikatae anenaye. Kwani hawa wasipoo- 25
koka waliomkataa aliyetoa wosia wake juu ya inchi, zayidi sana sisi tukimgeukia aliye mbinguni: sauti yake 26
ikitetemesha inchi wakati ule: sasa ameahidi, akinena, Marra moja tena tu natetemesha si inchi peke yake, illa na uwingu. Kunena marra moja tu, kuonyesha ondoleo 27
lao yatetemeshwayo, kama yaliyofanyika, yasiyotetemeshwa yaka.

Kwa hiyo, tukipokea ufalme usiotetemeshwa, tuwe na 28
neema, tumtumikie Muungu kumpendeza kwa haya na hofu. Kwani Muungu wetu moto ulao. 29

UPENDANO ukae. (2) Kukaribisha wageni msisa- 13
hau: kwani kwa hiyo wangine wasipojua wamekaribisha malaika.

'Mwakumbuke waliofungwa, kama mmefungwa pa- 3
moja nao; nao wanaothulumiwa, kama wenyewe katika mwili.

Ndoa inayo heshima kwa wote, na malalo safi: waasharati na wazini Muungu atawahukumu. 4

Pasipo kupenda fetha desturi zenu; yakiwatosha 5
mliyo nayo: kwani ndiye aliyesema, Sikomi mimi kwako, wala sitakuacha. Hatta twathubutu kusema, Muungu ndiye anisayidiaye, wala sitaogopa wanifanyieje watu. 6

'Mwakumbuke walio juu yenu, waliowaambia neno 7
la Muungu; mkiangalia mwisho wa mazumgumzo yao, ifuateni imani. Isa Masiya jana na leo mmoja, na hatta 8
milele. Msichukuliwe na elimu zisizo moja na ngeni: 9
ndilo jema moyo ukiwa imara kwa neema, wala si kwa vyakula, visivyowafaa waliokwenda navyo. Tunayo 10
mathbahu, katika hiyo hawana uwezo wa kula waabuduo katika hema. Kwani nyama, damu zao zikichukuliwa 11
kwa ajili ya thambi katika patakatifu na mkohani mkuu, miili yao huteketezwa 'nje ya kituo. Hivi na 12
Isa, awatakase watu kwa damu yake yeye, akaumwa 'nje ya mlango. Bassi, tuende 'nje kwake, 'nje ya kituo, 13
tukichukua shutumu lake: kwani hapa hatunao mji uka- 14
ao, lakini twautazamia ujao. Kwa huyo tutoe siku- 15

zote thabihu ya sifa kwa Muungu, ndiyo tunda la midomo ; tukiungama jina lake.

- 16 Kutenda vema na kushariki msisahau : kwani kwa thabihu kama hizo Muungu hupendezewa.
- 17 'Mwafuate walio juu yenu, mkatii : kwani wakesha kwa ajili ya maisha yenu kama watakaotoa hesabu ; wafanye kwa furaha, wala si wakiugua : kwani ndiyo hasara yenu.
- 18 Mtuombe sisi : kwani twaamini kama tunao moyo
19 mwema katika yote, tukitaka kuongea vema. Nazidi kuwasihi kufanya hivi, nirudishwe kwenu upesi.
- 20 Muungu wa amani, aliyeleta tena katika wafu Mchungwa wa kondoo aliye mkuu, katika damu ya agano la mi-
21 lele, Bwana wetu Isa, awafanyizie kwa killa tendo jema, mlifanye alipendalo, akitenda mwenu lipendezalo mbele yake kwa Isa Masiya : asifiwe milele na milele. Amina.
- 22 Nawasihi, ndugu, 'mvumilie neno la kuonya : kwani
23 na kwa machache nimewaandikia. Jueni kama ndugu yetu Timoteo amefunguliwa. Pamoja naye, akija upesi,
24 nitawaona. Salimieni wote walio juu yenu, nao wata-
25 katifu wote. Wawasalimia walio wa Italia. Neema kwenu nyote. Amina.

WARAKA WAKE

YAKOBO.

- 1 YAKOBO, mtumwa wa Muungu na wa Bwana Isa Masiya, kwa kabila thenashara waliotawanyika : Salaa-
2 mu. Ndugu zangu, ihesabuni pia kwa furaha mkipatwa
3 na majaribu menginemengine, mkajue kama kujaribiwa
4 imani yenu hufanya saburi. Mkaache saburi kazi yake
5 itimie, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu, msipu-
6 nguke kabisa. Mtu wenu akihitajia hekima, amtake Muungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hanenei,
7 naye atapewa. Illa atake katika imani, asibadilibadili. Kwani abadiliye amefanana na wimbi la baharini, lichu-
7 kuliwalo na upepo likatupwa. Wala mtu yule asithani

atapewa neno na Bwana. Mtu mwenyi nia mbili hute- 8
temeka katika njia zake zote.

Ndugu asiye na cheo afurahi kwani ametukuzwa, na 9
mtajiri kwani ameshushwa: kwa sababu kama ua la 10
majani atapita. Kwani jua likitoka likichomoza huka- 11
usha na majani; ua lake huanguka na uzuri wa umbo
lake umepotea: vivi mtajiri atanyauka katika njia zake.
Amebarikiwa aliyestahimili jaribu: kwani akiisha ku- 12
jaribiwa, atapewa taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia
wampendao.

Mtu asiseme akijaribiwa, Ninajaribiwa na Muungu: 13
kwani Muungu hawezi kujaribiwa na uovu, wala ha-
mjaribu mtu: lakini killa mtu hujaribiwa akivutwa 14
na tamaa yake yee, akashawishwa. Halafu tamaa, iki- 15
zaa, huzaa thambi: na thambi, ikimalizwa, huzaa kufa.

Msikose, ndugu zangu niwapendao. Killa kutoa ¹⁶/₁₇
kwema, na killa kilichotolewa kikamilifu, hutoka juu,
kinashuka katika Baba wa nuru, asiye na kubadili wala
kivuli cha kugeuka. Kwa kupenda kwake tumezaliwa 18
naye kwa neno la kweli, tuwe kama malimbuko ya
viumbe vyake. Kwa hiyo, ndugu zangu niwapendao, 19
killa mtu awe mpesi kusikia, wala si mpesi kunena, si
mpesi kuona hasira: kwani hasira ya mwana Adamu 20
haitendi haki ya Muungu. 'Mwekee mbali uchafu 21
wote wa kuzidi kusikofaa, mkapokee kwa upole neno
lililopandika, liwezalo kuwaokoa roho.

Mlitende neno, wala msisikie tu, mkijidanganya 22
mioyo. Mtu akilisikia neno wala halitendi, ndiye kama 23
mtu akijiona uso wake wa mwilini katika kioo: kwani 24
hujiona, huenda zake, husahau marra moja mtu gani
aliyekuwa. Lakini aliyetazama katika sheria kamilifu 25
ya kuwa huru, akadumu, wala si msikia msahaulifu,
lakini mtenda kazi, mtu yule atabarikiwa kazini mwake.
Mtu wa kwenu akionekana kuwa mcha Muungu, wala 26
hauzui ulimi wake, akijidanganya moyo, dini yake huyu
haifai. Dini iliyo safi wala haina taka mbele yake 27
Muungu na Baba, ndiyo kuwaangalia wasio na baba na
waliofiwa na mume katika mateso yao, na kujilinda
asiwe na mawaa katika dunia.

NDUGU zangu, msiwe na imani yake Bwana wetu 2
Isa Masiya wa utukufu kwa kuwafathilia watu. Kwani 2
akija katika sunagogi lenu mtu mwenyi pete la thahabu

- 3 na mavazi manyonge; mkamfathilia avaaeye vizuri,
 mkamwambia, Kae hapa katika mahali pema; mka-
 mwambia maskini, Simama huku, ao kae hapa miguuni
 4 pangu; hammekuwa wenyi hawa kwa ndani, na waa-
 5 muzi wa fikara zisizo njema? Sikilizeni, ndugu niwa-
 pendao. Muungu hakuwachagua maskini wa duniani
 matajiri katika imani, na warithi wa ufalme aliowaahidia
 6 wampendao? Illa ninyi mmewatharau masikini. Ma-
 tajiri hawawaonei? hawawavuti katika viti vya huku-
 7 mu? hawalineni vibaya jina lile zuri mliloitiwa? Mki-
 8 timia sheria ya kifaume, ilivyoandikwa, Umpende jirani
 9 yako kama moyo wako, mwatenda vema. Lakini mki-
 wafathilia watu, mmetenda thambi, mkathubutika na
 10 sheria kama wakosao. Atakayeshika sheria yote, aki-
 11 kosa katika moja, amekosa katika yote. Kwani aliye-
 sema, Usizini, akasema tena, Usiue. Bassi kama huku-
 zini, illa umeua, umekosa sheria.
- 12 Semeni ninyi katendeni kama watakaohukumiwa
 13 kwa sheria ya kiungwana. Kwani atapata hukumu
 pasipo rehema asiyehurumia: na rehema hufurahi juu
 14 ya hukumu. Yafaa nini, ndugu zangu, mtu akisema
 anayo imani, wala hana matendo? Imani yatosha
 15 kumwoko? Ndugu mume ao mke akiwa utupu, aki-
 16 punguka chakula cha killa siku, mmoja wenu akiwaa-
 mbia, Enendeni katika amani, mpate moto na kushiba,
 wallakini hawapi vitu mwili uvihitajivyo, yafaa nini?
 17 Hivi na imani, isipokuwa na matendo imekufa, ikiwa
 18 peke yake. Illa mtu aseme, Wewe unayo imani, nami
 ninayo matendo: nionyeshe imani yako pasipo matendo
 yako, nami nitakuonyesha imani yangu kwa matendo
 yangu.
- 19 Wasadiki ya Muungu kuwa mmoja; watenda vema:
 20 mashetani tena wasadiki, wanatetemeka. Illa wapenda
 kujua, mtu thaifu, kama imani pasipo matendo imekufa?
 21 Baba wetu Ibrahimu hakupata kuwa na haki kwa
 matendo, alipomtoa Isaak mwanawe juu ya mathbahu?
 22 Huoni ginsi ilivyotenda imani pamoja na matendo yake,
 23 na kwa matendo imani imekamilika? Maandiko yaka-
 timizwa yaliyonena, Ibrahimu akamwamini Muungu,
 akahasabikiwa kwa haki, akaitwa rafiki ya Muungu.
- 24 Mwaona mtu alivyofanyika kuwa na haki kwa matendo,
 25 wala si kwa imani tu. Naye Rahab kahaba hakufa-

nyika kuwa na haki kwa matendo, alipowakaribisha wajumbe akawapeleka njia ngine? Kwani kama mwili 26 pasipo roho umekufa, hivi na imani pasipo matendo imekufa.

MSIWE waalimu wengi, ndugu zangu, mkijua kama 3 tutapata hukumu ya kuzidi. Kwani katika mambo 2 mengi twachukiza wote. Mtu asiyekosa kwa maneno ndiye mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wote. Angalie, twawatia frasi hatamu kanwani watutii, tuki- 3 wageuza mwili wote. Angalia tena, merikebu, zilizo 4 kubwa sana, zikichukuliwa na pepo kali, hugeukageuka na msukani mdogo sana, appendako mshiki. Hivi ulimi 5 ni kiungo kidogo, hujisifu makuu.

Angalia jambo lipi kubwa moto mdogo huwasha. Na ulimi moto, ulimwengu wa uovu. Ulimi hivi 6 katika viungo vyetu, hatta kubaribu mwili wote: huwasha taratibu ya ulimwengu, hukawashwa na jehannum. Kwani killa namna ya nyama, ya ndege, ya 7 nyoka, ya vitu vya baharini, inafugika na imefugika na waana Adamu: illa ulimi hawezi mtu kuufuga, uovu 8 usio na taratibu, umejaa sumu ya kufisha. Twambarikia nao Muungu na Baba; twawalaani nao watu, waliofanyika kwa mfano wa Muungu. Katika kanwa 10 moja hutoka kubariki na kulaani. Ndugu zangu, haya hayakupasa kuwa. Chemchemi hutoa pahali pamoja 11 maji matamu na machungu? Mtini, ndugu zangu, 12 huweza kutoa mazetuni, ao mzabibu tini? Wala chemchemi haiwezi kuyatoa na maji ya chumvi nayo yaliyo matamu.

Nani aliye na akili na mwenyi maarifa kwenu? 13 Aonyeshe katika mwenendo mwema matendo yake kwa upole wa hekima. Lakini mkiwa na hasidi chungu na 14 ugomvi moyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uwongo juu ya kweli. Hekima hii siyo iliyoshuka katika juu, 15 illakini ni ya dunia, ya tamaa, ya shetani. Kwani 16 uwivu uwapo na ugomvi, huko kuchafuka na killa tendo baya. Lakini hekima ishukayo katika juu kwanza 17 safi, tena ya amani, nyanana, iliyosihwa upesi, imejaa rehemu na mazao mema, pasipo hawa, pasipo unafiki. Nalo zao la haki hupandwa katika amani nao wafanyao 18 amani.

KUTOKA wapi vita na mapigano kwenu? Si huko, 4

- katika tamaa zenu zinazopigana katika viungo vyenu?
- 2 Mwatamani, wala hamna: mwaua, mkitaka, wala hampati: mwafanya vita, mkipigana: wala hamna, kwa
- 3 sababu hamwombi: mwaomba, wala hampewi, kwa sababu mwakosa katika kuomba, mtumie kwa tamaa
- 4 zenu. Enyi wazini, hamjui kama urafiki wake dunia ni wadui wake Muungu? Killa atakaye kuwa rafiki yake
- 5 dunia ni adui yake Muungu. Mwathani kama maandiko husema burre, Roho ikaamo mwetu hutamani kwa
- 6 hasidi? Lakini huzidi kutoa neema. Kwa hiyo husema, Muungu huwazuia wenyi kiburi, huwapa neema wanenyekevu.
- 7 Mtiini Muungu. Mpigane na shetani, naye atakimbia. Mkaribuni Muungu, naye atawakaribia ninyi. Takaseni mikono, enyi wenyi thambi; safisheni mioyo,
- 9 wenyi nia mbili. Mteswe, mhuzunike, mlie, macheko yenu yageuke kuwa malio, na furaha kuwa hamu.
- ¹⁰₁₁ Mjithili machoni pake Bwana, naye atawainua. Msineaneane vibaya, ndugu. Amneneaye vibaya ndugu, amhukumuye ndugu, huinenea vibaya sheria, huihukumu sheria. Lakini ukiihukumu sheria, wewe si mtenda
- 12 sheria, illa mhukumu. Yuko mmoja atoaye sheria, awezaye kuokoa na kuharibu: nani wewe umhukumuye mgine?
- 13 Gissi gani, ninyi msemao, Leo ao kesho tutakwenda hatta mji fullani, tutakaa humo mwaka, tukinunua na
- 14 kuza, tukapate fayida: mkiwa hamjui nini kesho? Kwani nini maisha yenu? Ni umande uonekanao kita-
- 15 mbo, baadaye hutoweka. Mahali pa kusema, Bwana
- 16 akipenda, tutaishi, tutaifanya hivi ao hivi. Lakini sasa mwafurahi katika kujisifu kwenu: furaha hii yote si
- 17 njema. Kwa hiyo kwake ajuaye kutenda mema wala hatendi, kwake thambi.
- 5 GINSI gani, matajiri? Lieni, mkaomboleze, kwa
- 2 misiba itakayowapata. Mali zenu zimeharibika, na
- 3 mavazi yenu yameliwa. Thahabu yenu na fetha zimeharibika; na kutu yao itawashuhudia, itawala nyama kama ingalikuwa moto. Mmekusanya fetha chungu
- 4 chungu kwa siku za mwisho. Angalieni, ijara yao wakulima, walioyavuna mashamba yenu, msioitolea kwa hila, inalia: malio yao waliovuna yameingia masikioni
- 5 mwake Bwana wa Sabaath. Mmefanya fahari katika

dunia; hamkujizuia; mmejilisha moyo, kama siku ya kuchinja. Mmehukumia mkamua mwenyi haki; haku- 6
waasi.

Mstahimili, ndugu, hatta kuja kwake Bwana. Anga- 7
lieni, mkulima hungoja mazao ya thamani ya inchi, hustahimili sana, hatta kupokea mvua na ya kwanza na ya mwisho. Nanyi mstahimili; 'mweke imara 8
mioyo yenu: kwani kuja kwake Bwana kunakaribia.

Msikasirike ninyi kwa ninyi, ndugu, msihukumiwe: 9
angalieni, mwamuzi yupo mlangoni. Twaeni kwa 10
mfano wa kuteswa, ndugu zangu, na kustahimili, manabii walionena kwa jina la Bwana. Twawaona wa heri 11
waliiodumu. Mmesikia uvumilivu wa Ayub, mmeuona mwisho wa Bwana, kama Bwana mwenyi huruma nyingi na msikitikifu.

Illa juu yote, ndugu zangu, msiape, wala kwa mbingu, 12
wala kwa inchi, wala kwa kiapo kingine cho chote: lakini ndio yenu ndio, na sio, sio; msianguke katika kuhukumiwa.

Mtu wa kwenu ameteswa? aombe. Mtu amefura- 13
hiwa? aimbe zaburi. Mtu wa kwenu akiwa hawezi, 14
awaite wazee wa kanisa; wakamwombee, wakimtia mafuta kwa jina lake Bwana: na kuomba kwa imani 15
kutamwokoia mgonjwa, naye Bwana atamwinua; na kama ametenda thambi atasamehewa.

Ungamenimakosa ninyikwaninyi, mkaombeane, mpate 16
kupona. Kufaa sana kuomba kwake mwenyi haki kwa bidii. Eliya alikuwa mtu aliyesumbuka kama sisi; akio- 17
mba akaomba mvua isinye; wala mvua haikunya juu ya inchi muda wa miaka mitatu na miezi sita. Akaomba 18
tena, mbingu zikatoa mvua, inchi ikazaa matunda yake.

Ndugu, mmojawapo wenu akikosa katika kweli, mtu 19
akimwongoa, ajue kama amwongoaye mwenyi thambi 20
katika makosa ya njia yake, ataokoa roho katika kufa, atasetiri wingi wa thambi.

WARAKA WA KWANZA

WA

PETRO.

- 1 PETRO, mtume wa Isa Masiya, kwa wateule wa uta
 wanyiko wakao katika Ponto, Galatia, Kappadokia,
 2 Asia, na Bithunia, kwa kujua mbele Muungu Baba,
 katika utakaso wa Roho, kwa kutii na kunyunyizwa
 damu yake Isa Masiya : Neema kwenu na amani izidi.
- 3 Mbarikiwa Muungu na Baba wa Bwana wetu Isa
 Masiya, aliyetuzaa marra ya pili kwa rehemu yake nyi-
 ngi katika tumaini lenyi uzima kwa ajili ya ufufuo
 4 wake Isa Masiya katika wafu, kwa urithi usioharibika,
 usiotiwa uchafu, usiokauka, mliotunziwa ninyi mbi-
 5 nguni, mnaolindwa na nguvu za Muungu katika imani,
 kwa wokovu, ulio tayari ufunuke wakati wa mwisho :
 6 mnaofurahia, ikiwa kidogo, kama imewapasa, mmehu-
 7 zunishwa kwa majaribu manginemangine, ujaribu wa
 imani yenu, iliyo na thamani kuu kuliko thahabu ipo-
 teayo, ikiwa hujaribiwa kwa moto, uonekane kwa sifa
 na utukufu na heshima, katika kufunuka Isa Masiya :
 8 msipomwona mmpendaye ; naye hatta sasa hammwoni ;
 mkimwamini, mwafurahi kwa furaha isiyonenwa na
 9 iliyotukuzwa : mkipokea mwisho wa imani yenu, wo-
 10 kovu wa maisha. Kwa mambo ya wokovu huu waka-
 tafuta, wakapekua manabii waliotoa unabii wa neema
 11 iliyo kwenu : wakitafuta wakati upi na wakati gani
 Roho ya Masiya iliyomo mwao ionyeshao, ikishuhudia
 mbele mateso yake Masiya na baadaye utukufu wake :
 12 waliofunuliwa kama si kwao wenyewe, illa kwetu, wa-
 nangojea haya, yaliohubiriwa sasa kwenu nao waliowa-
 hubiria anjili kwa Roho Mtakatifu aliyepelekwa katika
 mbinguni ; katika haya nao malaika wataka kuchu-
 ngulia.
- 13 Kwa hiyo fungeni viuno vya akili zenu, mkiwa na
 kiasi mkatumaini hatta mwisho kwa neema mliyoletewa

kwa ufunuo wake Isa Masiya; kama watoto wasikiao, 14
msipozifuata tamaa za kwanza za ujinga wenu : lakini 15
awaitaye alivyo mtakatifu, 'mwe na ninyi watakatifu
katika mazungumzo yote : kama ilivyoandikwa, 'Mwe 16
watakatifu ; kwani mimi mtakatifu.

Nanyi mkimwitia Baba, abukumuye pasipo kua- 17
ngalia cheo, kwa kazi yake killa mtu, ongeeni katika
hofu wakati wenu wa kukaa hapa : mkijua kama si kwa 18
vitu viharibikavyo, kwa fetha ao thahabu, mmekombo-
lewa katika maongeo yasiyofaa mliyoyapokea kwa baba
zenu ; illa kwa damu ya thamani, kama ya mwana ko- 19
ndoo pasipo ila pasipo mawaa, Masiya : aliyejuliwa 20
mbele ya kuwekwa ulimwengu, akaonekana mwisho wa
zamani kwa ajili yenu, mliomwaminia Muungu kwa 21
yeye, aliyemfufua katika wafu, akampa utukufu ; hatta
imani na tumaini lenu liwe kwa Muungu.

Mkiwa mmesafisha maisha yenu kwa kuitii kweli 22
kwa Roho, kwa upendano usio na hila, kwa mioyo safi
mpendane kwa nguvu : mliozaliwa si kwa mbegu ziha- 23
ribikazo, illa isiyoharibika, kwa neno hayi la Muungu,
liishilo milele. Hivyo, Mwili wote kama majani, na 24
killa utukufu wake kama ua la majani. Majani hu-
kauka, na ua lake huanguka : Bwana anenalo laishi 25
hatta milele.

Ndilo anenalo mliohubiriwa ninyi.

BASSI mkiwekea mbali uovu wote na hila zote, na **2**
unafiki, na hasidi, na usingizio wote, kama vitoto vya **2**
leo myatamani maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, mpate
kwa haya kukua kwa wokovu ; kama mmeonja Bwana **3**
afaavyo.

Mkimjia kama jiwe lililo hayi, lisilokubalika na **4**
watu, illa alilolichagua Muungu, lenyi thamani, nanyi **5**
kama mawe yaliyo hayi, mmejengwa, nyumba ya roho,
ukohani mtakatifu, mtoao thabihu za roho, mliokubali-
wa na Muungu kwa Isa Masiya. Kwa hiyo ndivyo **6**
ilivyo katika maandiko, Angalia, naweka katika Sayuni
jiwe kuu la pembeni, teule, la thamani : naye amwami-
niye hatatahayarika. Bassi kwenu mwaminio thamani : **7**
kwa wasiotii, Jiwe wasilolikubali waliojenga, hili lime-
kuwa lililo juu pembeni, na, Jiwe la kujikwaa, na mwa- **8**
mba wa kuchukiza ; wajikwaa katika neno, wasipotii :
kwa hiyo nao wakawekwa.

9 Ninyi uzao mteule, ukohani wa kifaume, taifa taka-
tifu, watu wa milki, hatta kuhubiri nguvu zake aliye-
10 waita katika giza kwa nuru yake ya ajabu: walio kwa-
nza si taifa, sasa taifa la Muungu: wasiorehemewa, sasa
waliorehemewa.

11 Wapenzi, nawasihi kama wageni na wasafiri, mwe-
pukane na tamaa za mwili, zipiganazo na maisha;
12 mkiwa na maongeo yaliyo mazuri kwa mataifa; illi,
kama walivyowanenea kama watenda vibaya, waki-
yaona matendo yenu mema wantukuze Muungu siku
ya kuangaliwa.

13 Mjitie chini ya killa kiumbe cha watu kama kwa
14 Bwana: akiwa mfalme, kama aliye juu, wakiwa wa-
kuu, kama waliopelekwa naye kufanya haki juu yao
15 watendao vibaya, kwa sifa zao watendao vema. Kwani
ndivyo apendavyo Muungu, mtendapo mema mfumbe
16 kanwa la ujinga wa watu wasio na akili: kama huru,
wasiotumia uhuru kwa kisetiri cha ubaya, lakini kama
17 watumwa wa Muungu. 'Mwaheshimie wote. 'Mwa-
pende ndugu. 'Mmwogope Muungu. Mpeni mfalme
heshima.

18 Watumishi, 'mwatii bwana kwa hofu wote; sio walio
19 wema na wenyi upole tu, illa nao walio wakali. Kwani
ndilo neema, mtu akivumilia kwa kumkumbuka Mu-
20 ungu, akiteswa pasipo haki. Sifa gani kuvumilia mki-
kosa mkapigwa? Lakini mkitenda vema mkateswa,
mkivumilia, ndiyo neema kwa Muungu.

21 Kwani kwa hiyo mmeitwa: kwamba na Masiya ali-
vyoteswa kwa ajili yetu, akituachilia andiko, mfuata
22 nyayo zake; asiyetenda thambi, wala hila haikuone-
23 kana kanwani mwake: akishutumiwa hakushutumu te-
na; akiteswa hakuogofya; akajiwekea kwa yeye ahu-
24 kumuye kwa haki: aliyemitweka thambi zetu mwe-
nyewe katika mwili wake juu ya mti, illi sisi tukifa-
riki kwa thambi, tuwe hayi kwa haki; kwa mapigo
25 yake mmepona. Kwani mlikuwa kama kondoo walio-
potea; lakini mmemrudia Mchungu na Askafu wa
maisha yenu.

3 HIVI na wake, wakiwatii waume wao; illi wasioia-
mini neno, kwa mwenendo wa wake, pasipo neno, wa-
2 fayidiwe, wakiangalia mwenendo wenu wa hofu na safi.
3 Kupamba kwao kusiwe kwa 'nje, kusuka nyele na kuji-

tia thahabu na kuvaa mavazi; illa kwa ndani, mtu wa 4
 moyoni pasipoonekana, pasipoharibika, roho ya upole
 na tulivu, iliyo ya thamani kuu mbele ya Muungu.
 Kwani hivi na zamani, wake watakatifu waliomtu- 5
 mainia Muungu wakajipamba, wakiwatii waume wao:
 kama Sara alivyomsikiliza Ibrahimu, akimwita bwana: 6
 nanyi watoto wake, mkitenda vema, wala hamwogopi
 kwa woga wo wote. Hivi na waume, mkikaa nao kwa 7
 akili, mkiwagawanyia heshima kama chombo kike ki-
 sicho na nguvu, na kama warithio pamoja neema ya
 uzima; msizuiliwe katika kuomba kwenu.

Mwisho, wote wa nia moja, waonao mamoja, wape- 8
 ndanao, wa rehema, wanenyekevu: wasiolipia uovu kwa 9
 uovu, ao shutumu kwa shutumu; illa mbali wabarikio;
 mkijua ndilo mwitalo, mrithi mbaraka. Kwani, Ata- 10
 kaye kupenda uzima na kuona siku njema, akomeshe
 ulimi wake katika uovu, na midomo yake isinene hila.
 Mgeuke katika uovu, mkafanye mema; tafuteni amani 11
 mkaifuata. Kwamba macho yake Bwana kwao wenyi 12
 haki, na masikio yake kwa kusihi kwao: uso wake
 Bwana juu yao watendao maovu. Nani atakayewa- 13
 thuru, mkiwa na uwivu kwa mema? Lakini mkiteswa 14
 kwa haki, m heri. Msiogope woga wao, wala msita-
 abike. Mkamfanye mtakatifu Bwana Muungu mioyoni 15
 mwenu. Tayari sikuzote kutoa sababu kwa killa awa-
 ulizaye neno la tumaini liliomo mwenu, lakini kwa
 upole na hofu: mkiwa na moyo mwema; illi walivyo- 16
 wanenea kama watendao vibaya, watahayarike wastakio
 burre mwenendo wenu mwema katika Masiya.

Afathali mkitenda vema, pendo la Muungu liki- 17
 penda, kuteswa, kuliko mkitenda vibaya: ya kuwa naye 18
 Masiya akateswa marra moja kwa thambi, Mwenyi haki
 kwa ajili yao wasio na haki, atulete kwa Muungu;
 akiuawa kwa mwili, akifufuka kwa roho; kwa hiyo aki- 19
 waendea roho walio mafungoni akahubiri, wasiotii kwa- 20
 nza, ulipongoja uvumilivu wa Muungu, siku za Nuhu,
 safina ikitengenezwa, katika ile wachache, ndio watu
 wanane, wakaokoka kwa maji. Mfano wake hiyo sasa 21
 atuokoa, ndiyo ubatizo; sio kuwekea mbali uchafu wa
 mwili, illa jibu la moyo mwema kwa Muungu, kwa
 ufufuo wake Isa Masiya; aliyoko mkono wa kuume wa 22
 Muungu, akienda mbinguni; wakiwekwa chini yake
 malaika na nguvu na uwezo.

- 4 MASIYA akiteswa kwa ajili yetu kwa mwili, mjifanyie selaha kwa nia ileile; ya kuwa ateswaye katika
 2 mwili amekoma katika thambi; asiishi kwa tamaa za watu, illa apendavyo Muungu, wakati uliosalia wa katika mwili.
- 3 Wakati uliopita watutosha kutenda kwa shauri la mataifa, kuenenda katika asharati, tamaa, kunywa mvi-
 4 nyo, ulafi, ulevi, na ukafiri usio na sheria: wakiona vigeni msiende nao katika kumwaga shari, wakiwanenea
 5 vibaya: watakaotoa hesabu kwake aliye tayari kuwa-
 6 hukumu wahayi na wafu. Kwa hiyo na wafu wamehubiriwa, wahukumwiwe kwa watu katika mwili, wapate kuwa hayi kwa Muungu katika roho.
- 7 Mwisho wa yote unekaribia: 'mwe na kiasi, mkale-
 8 vuke kwa kuomba: juu yote mkiwa kwa bidii na upendano kwenu; kwani kupenda husetiri wingi wa tha-
 9 mbi: mkikaribishana pasipo kunung'unia. Killa mtu
 10 kama alivyopewa ukarimu, hivi mkiungojea ninyi kwa ninyi, kama mawakili wema wa neema zilizo nyingi za
 11 Muungu. Mtu akinena, kama wosia wa Muungu; mtu akingojea, kama kwa uwezo alioruzukiwa na Muungu: illi kwa yote Muungu atukuzwe kwa Isa Masiya, aliye nao utukufu na uwezo hatta milele na milele. Amina.
- 12 Wapenzi, msione vigeni moto wa kujaribia ulio
 13 kwenu, kama jambo geni limewapata. Lakini kama mkishariki katika kuteswa kwake Masiya, furahini, illi utukufu wake utakapofunuka, mfurahiwe tena kwa furaha kuu. Mkishutumiwa kwa neno lake Masiya, heri
 14 *ninyi*; ya kuwa Roho ya utukufu na ya Muungu unawakalia: kwa wale amenenwa unajisi, kwa ninyi ametukuzwa.
- 15 Illa mtu wenu asiteswe kama muuaji, ao mwivi, ao
 16 mtenda vibaya, ao ajitiaye juu ya mambo ya watu. Lakini akiteswa kama Mmasihiya asione haya; amtukuze
 17 Muungu kwa neno hili. Kwani ni wakati wa kwanza hukumu katika nyumba ya Muungu. Mwanzo ukiwa kwetu, mwisho gani wao wasioitii anjili ya Muungu?
 18 Mwenyi haki akiokoka kwa shidda, mnajisi na mkosaji
 19 ataonekana wapi? Hatta wateswao apendavyo Muungu wa'mwekee maisha yao kama kwa muumba amini katika kutenda vema.
- 5 NAWASIHI wazee walio kwenu mimi, niliye mzee na shahidi wa mateso yake Masiya, na mshariki utukufu

utakaokuwa umefunuka : Chungeni kundi lake Muungu, 2
 mkisimamia, pasipo kulazimishwa, illa kwa moyo ; wa-
 siotaka fayida ya aibu, illa kwa nia ; wala si kama 3
 wajifanyao bwana za urithi, illa mkiwa namna kwa
 kundi. Hatta Mchungu mkuu atakapoonekana mpewe 4
 taji la utukufu isiyokauka.

Hivi na vijana, 'mwatii wazee. Ninyi kwa ninyi 5
 mtiane wote, mkajifungie unenyekevu : akiwa Muungu
 juu yao wenyi kiburi, wanenyekevu wapewa neema naye.
 Bassi mnenyekee chini ya mkono wa uwezo wa Muungu, 6
 awainue kwa wakati ; mkimtupia taabu yenu yote, 7
 kwani yeye awatunzaye.

Mlevuke, mkeshe : kwa sababu adui wenu shetani, 8
 kama simba angurumaye, hutembea, akitafuta ataka-
 yemla : simameni juu yake, imara katika imani, mkijua 9
 kama mateso yaleyale yametimika kwa ndugu zenu wa-
 liopo ulimwenguni.

Muungu wa neema yote, aliyetuita kwa utukufu wake 10
 wa milele katika Masiya Isa, mkiisha kuteswa kidogo,
 atawatengeneza, atawategemeza, atawatia nguvu, ata-
 waweka vema. Utukufu kwake na uwezo hatta milele na 11
 milele. Amina.

Kwa Silwano, kwenu ndugu aliye amini, kama nio- 12
 navyo, kwa machache nimewaandikia, nikionya, nikishu-
 hudia ndiyo neema ya kweli ya Muungu msimamapo.

Lililo teule pamoja nanyi, katika Babeli, lawasalimia ; 13
 na Marko mwanangu. Msalimiane kwa busu la u- 14
 pendano. Amani kwenu nyote katika Masiya Isa.
 Amina.

WARAKA WA PILI

WA

PETRO.

SIMAN Petro, mtumwa na mtume wa Isa Masiya, 1
 kwao waliopata imani yenyi thamani moja na sisi,
 katika haki ya Muungu wetu na Mwokozi Isa Masiya :

- 2 Neema kwenu na amani ijae katika kumjua Muungu na Isa Bwana wetu.
- 3 Kama uwezo wake wa Muungu utupavyo yote yaliyo
4 kwa uzima na utawa, kwa kumjua aliyetuita kwa utu-
5 kufu na wema; kwa hiyo tumepewa ahadi zilizo bora na
6 za thamani; illi kwa hizo mpate kushariki sifa ya
7 Muungu, mkiokoka katika uharibifu uliopo duniani kwa
8 tamaa. Na kwa hiyohiyo mkijitia kwa bidii yote,
9 mkaongeze imani yenu kwa wema, na wema kwa maa-
10 rifa, na maarifa kwa kujizuia, na kujizuia kwa uvumi-
11 livu, na uvumilivu kwa utawa, na utawa kwa kupenda
12 ndugu, na kupenda ndugu kwa upendano. Kwani
13 mkiwa na haya mkazidi, yafanya si wavivu wala si wasio
14 na matunda kwa maarifa ya Bwana wetu Isa Masiya.
- 15 Mtu, pasipo haya, kipofu, haoni mbali, akisahau kuta-
16 kasika katika thambi zake za zamani.
- 17 Kwa hiyo, ndugu, afathali mfanye bidii kufanya imara
18 wito wenu na uteule: mkitenda haya hamtajikwaa ka-
19 bisa; kwani hivi mtaruzukiwa sana kuingia katika
20 ufalme wa milele wa Bwana wetu na Mwokozi Isa Masiya.
- 21 Kwa hiyo nitaangalia niwakumbushe sikuzote mambo
22 haya, mkiwa mmeyajua, mkawa imara katika kweli
23 iliyopo. Kwani naiona ya haki nikiwa mimi katika
24 masikani hii, kuwaamsha katika kukumbusha, nikijua
25 kama upesi nitaiuvia masikani yangu, kama Bwana wetu
26 Isa Masiya alivyonyesha. Najitahidi kufanya wakati
27 wote 'mwe ninyi baada ya kufariki kwangu na ukumbu-
28 ko uleule.
- 29 Kwani hatukufuata hadithi zilizofanyika kwa hekima,
30 tukiwajulisha ninyi nguvu na kuja kwake Bwana wetu
31 Isa Masiya, lakini tumeona kwa macho yetu ukuu wake:
32 kwani akipewa na Muungu Baba heshima na utukufu,
33 akiletewa sauti katika utukufu ulio mkuu, Huyu ndiye
34 mwanangu nimpdaye, niliyependezewa naye. Na
35 sauti hiyo sisi tukasikia imeletwa katika mbinguni, tu-
36 kiwa pamoja naye katika mlima ulio mtakatifu.
- 37 Tunalo na neno la unabii lililo imara; mwatenda
38 vema mkiliangalia, kama fanusi ikimulika mahali pa
39 uchafu, hatta mchana utakapomwangaza, na nyota ya
40 asubui itazuka mioyoni mwenu. Mkijua kwanza hiyo,
41 kama unabii wote wa andiko haupati kufasirika kwake

tu. Kwani unabii haukuletwa zamani kwa mapenzi ya 21
mtu: illa watu walio watakatifu wa Muungu wamenena
wakiehukuliwa na Roho Mtakatifu.

WAKAWA na manabii wa uwongo katika watu, 2
kama kwenu watakuwa waalimu wa uwongo, watakaoi-
ngiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkania
naye Bwana aliyewanunua, wakijiletea upotevu usioka-
wia. Na wengi watafuata jeuri zao; kwa ajili yao njia ya 2
kweli itanenwa unajisi. Na katika kutamani watajipa- 3
tia fayida kwenu kwa maneno yaliyotengenezwa: hukumu
yao tangu zamani haikawii, wala upotevu wao hausinzii.

Kwani Muungu asipowaachilia malaika waliokosa, 4
lakini mafungoni mwa giza wakitiwa shimoni akawatoa
walindwe kwa hukumu; wala ulimwengu wa kwanza 5
hakuuachilia, lakini Nuhu mhubiri haki wa nane aliye-
mhifathi, akileta gharika juu ya ulimwengu wa wanajisi;
na miji ya Sodom na Gomora akiifanya majifu akahuku- 6
mu kwa upotevu, ameiweka kwa dalili kwao watakaofa-
nya unajisi; na Lut mwenyi haki, akisumbuka na ma- 7
ngeo yao wasio na adabu katika jeuri, akamwoko-
(kwani katika kutazama na kusikia, mtu wa haki akikaa 8
kwao, siku kwa siku roho yake ya haki ikateswa na
matendo yasiyo na sheria): Bwana amejua kuwaokoa 9
watawa katika jaribu, na kuwaweka wathalimu wakia-
thibiwa kwa siku ya hukumu. Nao wa kwanza wafuatao 10
mwili katika tamaa ya ujusi, wakitharau ukuu: wasio
na hofu, wajivunao, hawatetemeki wakiyanenea unajisi
matukufu: ikiwa malaika, walio bora kwa uwezo na 11
nguvu, hawawastaki kwa unajisi mbele ya Bwana.
Hawa, kama nyama wasio na akili, walio kwa asili wa 12
kutwaliwa na kupotezwa, katika yale wasiyoyajua wa-
nena unajisi: katika upotevu wao watapotea, wakipata 13
ujira wa uthalimu: waionao anasa kujivimbisha mchana;
mawaa na aibu, wakijivimbisha katika madanganya yao,
wakifanya karamu nanyi; wakiwa na macho yajaayo 14
mazini, yasiyostarehe katika thambi; wakishawishi
watu wasio imara; wakiwa na moyo uliozoea kutamani;
waanā wa laana. Wameacha njia iliyo sawa, wakapotea, 15
wakifuata njia ya Balaam wa Bosor, aliyependa ujira wa
thulumu, akategwa katika kukosa sheria: nyama isiyo- 16
nena akisema kwa sauti ya mwana Adamu, akakataza
wazimo wa nabii.

- 17 Hawa visima pasimo maji, na mawingu yaliyofukuzwa na tufanu: wanaolindiwa weusi wa giza hatta milele.
- 18 Kwani, wakinena makuu mno ya ubatili, wawashawishi kwa tamaa za mwili, na jeuri, wale waliokimbia kabisa
- 19 katika kwao waongea katika kukosa; wakiwaahidia kuwa huru, wakiwa wenyewe watumwa wa upotevu;
- 20 kwani aliyeshindwa naye, huyu humtumikia. Kwani waliokimbia katika ujusi wa dunia kwa maarifa yake Bwana na Mwokozi Isa Masiya, wakinaswa tena wakashindwa, hawa, ya mwisho yao yamekuwa mabaya
- 21 kuliko ya kwanza. Kwani afathali hawangalijua njia ya haki, kuliko walipojua kugeuka katika amri takatifu
- 22 waliyopewa. Imewapata kwa methali ya kweli, Mbwa amerudi kwa matapiko yake, na nguruwe aliyeoshwa kwa kufingirika matopeni.
- 3** WARAKA huu wa pili, wapenzi, sasa nawaandikia; 2 katika hizi nawaamsha akili safi kwa kukumbuka, mpate kukumbuka maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu, na amri ya mitume wake Bwana na Mwokozi:
- 3 mkijua kwanza, ya kwamba siku za mwisho watakuja katika kufanya thihaka wenyi thihaka, waendao kwa
- 4 tamaa zao wenyewe, wakinena, Iko wapi ahadi ya kuja kwake? kwani, tangu walipolala babu, yote yamekaa vivyo tangu mwanzo wa kuumba.
- 5 Kwani kwa moyo hawajui kama mbingu zilikuwa za kale, na inchi katika maji kwa maji imesimama kwa neno la Muungu. Kwa hizo ulimwengu wa wakati ule, ukigharikiwa na maji, ukaharibika. Mbingu za sasa, na inchi, zimewekwa kwa neno lile, zikilindwa kwa moto, hatta siku ya hukumu na kupotezwa watu wa thulumu.
- 8 Hili moja, wapenzi, lisisahauliwe kwenu, ya kwamba siku moja kwa Bwana kama miaka elfu, na miaka elfu kama siku moja. Bwana hakawii kwa ahadi, kama wengine wahasibuvyo kukawia; illa mvumilivu kwetu, asipende watu wapotee, illa wote wafike kutubu.
- 10 Siku ya Bwana itakuja kama mwivi usiku; katika ile mbingu zitapita zikienda kassi, na vitu vitalegea vikiungua, na inchi na matendo yaliyomo yatateketea.
- 11 Bassi haya yote yakilegea, watu gani imetupasa tuwe
- 12 sisi katika maongeo matakatifu na utawa, tukitazamia tukihimia kuwako siku ya Muungu, kwa ile mbingu

zitalegea zikiwa na moto, na vitu vitayeyuka vikiungua.

Twatazamia mbingu mpya na inchi mpya, kwa ahadi 13 yake, ikaamo haki.

Kwa hiyo, wapenzi, mkiyatazamia haya, mkafanye 14 bidii mwonekane naye, pasipo mawaa wala aibu, katika amani. Nao uvumilivu wa Bwana kwenu 'muhasibu 15 kuwa wokovu; kama na ndugu yetu Paolo tumpendaye, kwa hekima aliyopewa, amewaandikia; kama na katika 16 nyaraka zote, akiyanena haya. Katika hizi mangine yasiyofahamiwa upesi; haya wasio na elimu na wasio imara huyapotoa, kama maandiko yaliyosalia, kwa upotevu wao wenyewe.

Bassi ninyi, wapenzi, mkijua mbele, mjilinde, msipate 17 kuchukuliwa na kukosa kwao wasio na sheria, msianguke katika imara yenu. Illa mkue katika neema na 18 kumjua Bwana wetu na Mwokozi Isa Masiya. Utukufu kwake na sasa na hatta siku za milele. Amina.

WARAKA WA KWANZA

WA

YOHANA.

YALIYOKUWA tangu mwanzo, tuliyoyasikia, tuli- 1
yoyaona, macho yetu tuliyoyatazama, na mikono yetu 2
tuliyoyapapasa; ya Neno la uzima (uzima ukaonekana, 3
tukaona, tukashuhudu, tukahubiri kwenu, uzima wa 4
milele ulio katika Baba, ukaonekana kwetu); tuliyo- 5
yaona tukayasikia, twahubiri kwenu, nanyi mpate ku- 6
sharikiana na sisi: na usharika wetu ni wake Baba, na 7
wake Mwanawe Isa Masiya. Nasi twawaandikia haya, 8
furaha yenu ijae.

Ndizo habari tulizosisikia kwake, tunazowatolea, kama 9
Muungu ndiye nuru, wala hapana giza kwake kabisa. 10
Tukisema twasharikiana naye, tukienda katika giza, 11
twasema uwongo, wala si kweli. Tukienda katika nuru, 12
kama yuko katika nuru, tumesharikiana sisi kwa sisi, 13

na damu yake Isa Masiya hutusafisha katika thambi
8 yote. Tukisema hatunayo thambi, tumejikosesha, wala
9 kweli haimo mwetu. Tukiziungama thambi zetu, ni
amini na mwenyi haki, atuondolee thambi, akatusafishe
10 katika yote yasiyo haki. Tukisema hatukukosa, tume-
mfanya 'mwongo, wala neno lake halimo mwetu.

2 WATOTO wangu, nawaandikia haya, msikose. Hat-
ta akiwa mtu amekosa, tunaye Mwombezi kwa Baba,
2 Isa Masiya Mwenyi haki. Ndiye sadaka kwa thambi
zetu; wala si kwazo zetu tu, illa kwazo za ulimwengu
3 wote. Hivi twajua kama tumemjua, kwa kushika amri
4 zake. Asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake,
5 ndiye 'mwongo, wala kweli haimo mwake. Alishikaye
neno lake, ndiye mapenzi ya Muungu aliyemtimilia.
6 Hivi twajua kama tumo mwake. Asemaye anakaa
mwake, imempasa, kama alivyokwenda yeye naye aende
vivyoo.

7 Wapenzi, siwaandikii amri mpya, illa amri ya zama-
ni, mliyo nayo tangu mwanzo. Amri ya zamani ndiyo
8 neno mlilosikia tangu mwanzo. Tena amri mpya na-
waandikia, iliyo kweli kwake na kwenu. Kama giza
9 linapita, na nuru ya kweli sasa imeonekana. Asemaye
yuko katika nuru, akimchukia nduguye, yuko katika
10 giza hatta sasa. Ampendaye nduguye yuko katika
11 nuru, wala cha kujikwaa hakimo mwake. Amchukiaye
ndugu yake yuko katika giza, anakwenda katika giza,
wala hajui aendako, kwani giza limempofusha macho.

12 Nawaandikia, watoto, kwani mmeondolewa thambi
13 kwa jina lake. Nawaandikia, baba, kwani mmem-
jua aliye tangu mwanzo. Nawaandikia, vijana,
kwani mmemshinda mwovu. Nimewaandikia, watoto,
14 kwani mmemjua Baba. Nimewaandikia, baba, kwani
mmemjua aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia, vija-
na, kwani hodari ninyi, nalo neno la Muungu lakaa
15 mwenu, mkamshinda mwovu. Msiipende dunia, wala
mambo yake dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda
16 Baba hakumo mwake. Kwani killa kilichomo duniani,
tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima,
17 hazinazo kwa Baba, illa kwa dunia. Dunia hupita, na
tamaa zake: afanyaye ayapendayo Muungu ndiye
akaaye milele.

18 Watoto, wakati wa mwisho. Kama mlivyosikia ka-

ma anakuja adui yake Masiya, hatta sasa adui wengi wake Masiya wako; hivi twajua kama ndio wakati wa mwisho. Walitoka kwetu, wala sio wa kwetu; kama 19 wanalikuwa wa kwetu wanalikaa naswi: lakini waonekane kama wote si wa kwetu. Illa ninyi mmetiwa 20 mafuta naye aliye Mtakatifu, mmejua yote. Sikwandika 21 kwenu kwa sababu hamkujua yaliyo kweli, lakini kwa sababu mmeyajua, na kama uwongo wo wote sio wa kweli. Nani aliye 'mwongo, illa akanaye kama Isa 22 ndiye Masiya? ndiye aliye adui yake Masiya, amkanaye Baba na Mwana. Killa amkanaye Masiya amekosa na 23 Baba: amwungamaye Mwana anaye na Baba. Nanyi, 24 yakae katika ninyi mliyoyasikia tangu mwanzo. Yakikaa katika ninyi mliyoyasikia tangu mwanzo, ninyi mtakaa katika Mwana na katika Baba. Ndiyo ahadi 25 aliyotuahidia, uzima wa milele. Haya nimewaandikia 26 wawakoseshao. Ninyi, mafuta mliyopewa naye hukaa 27 mwenu, wala hamhitaji mtu awafundishe; lakini kama mafuta huwafundisha yote, nayo kweli, wala si uwongo, na kama yalivyowafundisha, mkae mwake. Hatta sasa, 28 watoto, mkae mwake; illi atakapotokea tusiaibike naye akiwapo. Mkimjua kama ana haki, Mwajua kama killa 29 atendaye haki amezaliwa naye.

ANGALIENI upendo gani tuliopewa na Baba, tu- 3
itwe waanawe Muungu. Kwa hiyo dunia haitujui sisi, kwa sababu haikumjua yeye. Wapenzi, sasa tu watoto 2
wa Muungu, wala haijaonekana nini tutakaokuwa: twajua kama akionekana, tutakuwa kama yeye; kwani tutamwona kama ndivyo. Killa aliye nalo tumaini hili, 3
hujisafisha, kama yule ni safi. Killa atendaye thambi 4
ameasi: kwani thambi ndiyo kuasi. Mkajua kama 5
yeye ameonekana aziondoe thambi zetu; wala thambi mwake ha'mna. Killa akaaye mwake hakosi: akosaye 6
yote hakumwona, wala hakumjua. Watoto, mtu asi- 7
wadanganye: afanyaye haki ndiye wa haki, kama yeye wa haki: afanyaye thambi ni wa shetani; kwani she- 8
tani hukosa tangu mwanzo. Kwa hiyo akaonekana Mwana wa Muungu, azivunje kazi za shetani. Killa 9
aliyezaliwa na Muungu hatendi thambi, kwani uzao wake hukaa ndani yake: wala hawezi kukosa, kwani amezaliwa na Muungu. Hivi waonekana waana wa Muungu na 10
waana wa shetani: killa asiyetenda haki siye wa Muu-

11 ngu, wala asiyempenda ndugu yake. Kwani ndizo habari
 12 mlizosisikia tangu mwanzo, tupendane sisi kwa sisi: si
 kama Kain, aliye wake mwovu, akamua nduguye. Akamua
 kwa nini? kwani matendo yake maovu, nayo ya
 nduguye ya haki.

¹³₁₄ Si taajabuni, ndugu, dunia ikiwachukiza. Sisi tume-
 jua kama tumetoka katika kufa kwa uzima, kwani twa-
 15 wapenda ndugu: asiyependa hukaa katika kufa. Killa
 asiyempenda nduguye ni muuaji: mkajua kama hapana
 16 muuaji mwenyi uzima ukikaa mwake. Hivi tumejua
 kupenda, kwani huyu ametoa maisha yake kwa ajili yetu:
 imetupasa naswi tutoe maisha zetu kwa ajili yao ndugu.
 17 Aliye nazo riziki za duniani, akimwona ndugu yake
 amepunguka, akijifunga moyo kwake, gisi gani ku-
 18 mpenda Muungu kumekaa mwake? Watoto, msipende
 kwa neno, wala kwa ulimi, illa kwa tendo na kwa kweli.
 19 Hivi tutajua kama sisi wa kweli, na mbele yake mioyo
 20 yetu tutatumaini: moyo ukituhukumu, mkuu kuliko
 21 moyo wetu ni Muungu, ajuaye yote. Wapenzi, moyo
 22 usipotuhukumu, hatuna haya mbele zake Muungu; nasi
 tukitaka, tutapewa naye, kwani twazishika amri zake,
 23 tukayafanya yapendezayo mbele yake. Ndiyo amri
 yake, tuamini kwa jina la Mwanawe Isa Masiya, tuka-
 24 pendane sisi kwa sisi, kama alivyotuamuru. Azishikaye
 amri zake hukaa mwake, naye mwake. Hivi twajua
 kama twakaa mwake, kwa Roho tuliopewa naye.

4 WAPENZI, msiamini kwa roho yote, illa zizaribuni
 roho, kama zake Muungu: kwani nabii za uwongo
 2 wengi wameingia ulimwenguni. Hivi mwajua Roho
 ya Muungu: killa roho iungamaye Isa Masiya amekuja
 3 katika mwili, ndiyo ya Muungu: na killa roho isi-
 youngama kama Isa Masiya amekuja katika mwili, siyo
 wa Muungu: ndiyo adui wake Masiya, mliyemsikia
 4 anakuja; hatta sasa naye yuko ulimwenguni. Ninyi
 wa Muungu, watoto, mmewashinda: kwani aliye mwe-
 5 nu mkuu kuliko yule aliye duniani. Wale wa dunia:
 kwa hiyo wanenayo ya dunia, na dunia huwasikia.
 6 Sisi wa Muungu: amjuaye Muungu hatusikia; asiye
 wa Muungu hatusikii. Hivi twajua roho ya kweli na
 roho ya kukosa.

7 Wapenzi, tupendane sisi kwa sisi: kwani kupenda
 ni kwa Muungu; na killa apendaye amezaliwa na

Muungu, amemjua Muungu. Asiyependa hakumjua 8
 Muungu; kwani Muungu ni kupenda. Hivi imeone- 9
 kana Muungu alivyotupenda, kwani Muungu akampe-
 leka Mwanawe wa pekee katika ulimwengu, tupate
 uzima kwaye. Hivyo ndivyo kupenda: si kwamba sisi 10
 tumependa Muungu, illa kwamba yeye ametupenda
 sisi, akapeleka Mwana wake kuwa sadaka kwa thambi
 zetu. Wapenzi, Muungu akiwa ametupenda sisi hivyo, 11
 imetupasa na sisi kupendana sisi kwa sisi. Hapana 12
 mtu aliyemwona Muungu po pote: tukipendana sisi
 kwa sisi, Muungu hukaa mwetu, na mapenzi yake yame-
 timilia mwetu. Hivi twajua kama twakaa mwake naye 13
 mwetu, kwani ametupa ya Roho yake. Naswi tume- 14
 ona, tukashuhudu, kama Baba amempeleka Mwana,
 Mwokozi wa ulimwengu. Aungamaye kama Isa ni 15
 Mwana wa Muungu, Muungu hukaa ndani mwake, naye
 katika Muungu. Naswi tumejua tukasadiki ginsi alivyo- 16
 tupenda Muungu. Muungu ndiye kupenda; naye akaaye
 katika kupenda hukaa katika Muungu, na Muungu
 katika yeye. Hivi kumetimia kupenda, tusiwe na haya 17
 siku ya hukumu. Kwani yeye alivyo, naswi tupo ka-
 tika ulimwengu huu. Hapana hofu katika kupenda: 18
 lakini kupenda kukitimia kwatupa 'nje hofu, kwani
 hofu inayo mashaka; wala aliye na hofu hakutimia
 katika kupenda. Sisi twapenda kwa sababu yeye kwa- 19
 nza ametupenda sisi. Mtu akisema kama Nampenda 20
 Muungu, akimchukia ndugu yake, ni 'mwongo: asiyem-
 penda ndugu yake aliyemwona, Muungu asiyemwona
 apateje kumpenda? Naswi amri hii tumepewa naye, 11
 ampendaye Muungu ampende na ndugu yake.

KILLA aaminiye kama Isa ndiye Masiya amezaliwa **5**
 na Muungu: na killa ampendaye aliyezaa humpenda
 aliyezaliwa naye. Hivi twajua kama twawapenda wa- 2
 toto wake Muungu, tukimpenda Muungu, tukatenda
 amri zake. Ndiyo kumpenda Muungu, kuzishika amri 3
 zake: wala amri zake si nzito. Kwani killa aliyeza- 4
 liwa na Muungu huishinda dunia. Na kushinda
 kuishinda dunia ndiyo imani yetu. Nani aishindaye 5
 dunia, illa aaminiye kama Isa ni Mwana wa Muungu?
 Ndiye ajaye kwa maji na damu, Isa Masiya; si katika 6
 maji tu, illa katika maji na katika damu. Na Roho 7
 ndiyo shahidi, kwani Roho ni kweli. Kwani tatu ni

- 8 mashahidi, Roho, maji, na damu: na tatu hizi katika
 9 moja. Tukiukubali ushabidi wa watu, ushabidi wa
 Muungu ndio mkuu: kwani ndio ushabidi wa Muu-
 10 ngu, aliomshuhudia Mwana wake. Amwaminiye Mwa-
 na wa Muungu anao ushabidi ndani yake. Asiye-
 mwamini Muungu, amemfanya 'mwongo; kwani ha-
 kuuamini ushabidi aliomshuhudia Muungu Mwana
 11 wake. Ndio ushabidi, kama tumepewa na Muungu
 uzima wa milele, na uzima huu ni katika Mwana wake.
 12 Aliye naye Mwana anao uzima; asiye naye Mwana wa
 Muungu uzima hanao.
- 13 Haya nimewaandikia, mjue kana mnao uzima wa
 milele, mwaminio kwa jina la Mwana wa Muungu.
 14 Na hii sababu tusione haya mbele yake; kwani tuki-
 15 taka kwa ginsi apendavyo, atusikia; nasi tukijua kama
 atusikia tukitaka, twajua kama tunazo haja tulizozitaka
 16 kwake. Mtu akimwona nduguye akikosa kosa lisilo la
 kufa, atataka, naye atampa uzima kwao waliokosa, wala
 si kwa kufa. Kosa liko la kufa: silineni aliulizie.
 17 Killa lisilo haki ni kosa: na kosa liko lisilo la kufa.
- 18 Twajua kama aliyezaliwa na Muungu yote hakosi;
 lakini aliyezaliwa na Muungu hujitunza, wala mwovu
 19 hamshiki. Twajua kama sisi wa Muungu, na dunia
 20 yote hukaa katika uovu. Twajua kama Mwana wa
 Muungu amekuja, ametupa sisi akili tumjue aliye wa
 kweli, naswi katika yule aliye wa kweli, katika Mwana-
 we Isa Masiya. Ndiye aliye Muungu wa kweli, na
 21 Uzima wa milele. Watoto, mjilinde katika sanamu.
 Amina.

WARAKA WA PILI

WA

YOHANA.

- 1 MZEE kwa bibi mteule na waanawe, niwapendao
 katika kweli; wala si mimi tu, illa na wote waijuao kweli;
 2 kwa ajili yake kweli ikaayo mwetu, itakayokuwa kwetu

milele: Neema, rehema, na amani kwenu, katika kwa 3
Muungu Baba, na Bwana Isa Masiya Mwana wake
Baba, katika kweli na upendano.

Nalifurahiwa sana nikiona wa waana wako wakienda 4
katika kweli, kama tumepewa amri katika kwa Baba.
Na sasa nakutaka, bibi, si kama nikuandikie amri mpya, 5
illa tuliyo nayo tangu mwanzo, tupendane. Ndio upe- 6
ndano, tuende kwa amri zake. Ndiyo amri, kama
mmesikia tangu mwanzo, tuende katika hiyo. Kwamba 7
wadanganya wengi wametokea ulimwenguni, wasiou-
ngama Isa Masiya akija katika mwili. Huyu ndiye 8
mdanganya na aliye juu yake Masiya. Angalieni mambo
yasipotee tuliyoyatenda, lakini tupokee thawabu pia.
Killa atanguliaye asiyekaa katika elimu yake Masiya, 9
hana Muungu: akaaye katika elimu, huyu anao na
Baba na Mwana. Mtu akija kwenu wala haleti elimu 10
hii, msimkaribishe nyumbani, wala msimwambie heri;
amwambiaye heri ashariki matendo yake maovu. 11

Nikiwa na mambo mengi niyaandike, sipendi kwa 12
karatasi na wino: lakini nataraja kuwako kwenu na
kunena kanwa kwa kanwa, furaha yetu ipate kujaa.
Wakusalimia watoto wa ndugu yako aliye mteule. 13

WARAKA WA TATU

WA

YOHANA.

MZEE kwa Gayo mpenzi, nimpendaye katika kweli. 1
Mpenzi, nakuombea kwa yote uende vema ukaone afya, 2
kama maisha yako ilivyokwenda vema. Nalifurahiwa 3
sana, wakija ndugu wakiishuhudia kweli yako, kama
uendavyo katika kweli. Sina furaha iliyo kuu kuliko 4
kusikia waana wangu waendao katika kweli.

Mpenzi, wafanya amini uyafanyayo kwa ndugu na 5
wageni wote, waliokushuhudia upendano wako mbele 6
ya kanisa: watenda vizuri ukiwapeleka mbele kama

- 7 astahilivyo Muungu. Kwani kwa ajili ya Jina walito-
 8 ka wasitwae kitu kwa mataifa. Imetupasa kuwaka-
 ribisha kama hawa, tushariki kazi katika kweli.
- 9 Naliandika kwa kanisa: lakini Diotrefe, apendaye
 10 kuwa wa kwanza, hatukubali. Kwa hiyo nikija, nita-
 mkumbushia matendo ayatendayo, akitoa upuuzi juu
 yetu kwa maneno maovu: wala haya hayamtoshi: ha-
 wakaribishi ndugu, nao watakao awazuia, na katika
 kanisa awaondoa.
- 11 Mpenzi, usifuate ubaya, illa wema. Atendaye mema
 ndiye wa Muungu: atendaye mabaya hakumwona Muu-
 12 ngu. Demetrio ameshuhudiwa na wote, hatta na kweli
 yenyewe: na sisi twashuhudu; na ushahidi wetu umejua
 kama wa kweli.
- 13 Nalikuwa na mengi nikuandikie, illa sipendi kuku-
 14 andikia kwa wino na kalamu: nataraja kukuona upesi,
 na kanwa kwa kanwa tutanena. Amani kwako. Wa-
 kusalimia marafiki. Salimie marafiki kwa jina.

WARAKA WA YUDA.

- 1 YUDA, mtumwa wa Isa Masiya, ndugu wa Yakobo,
 kwao waliotakaswa katika Muungu Baba, wanaolindwa
 2 katika Isa Masiya, walioitwa: Rehema kwenu na amani
 na upendano uzidike.
- 3 Wapenzi, bidii yote nikifanya kuwaandikia kwa ma-
 mbo ya wokovu uliosharikiwa, sina buddi kuwaandikia
 nikiwaonya, mshindane kwa imani iliyotolewa kwa marra
 moja kwa watakatifu.
- 4 Kwani wameingia kwa siri watu, walioandikiwa za-
 mani kwa hukumu hiyo, wanajisi, wabadilio neema ya
 Muungu wetu kuwa jeuri, na wamkanao aliye Mola
 peke yake, na Bwana wetu Isa Masiya.
- 5 Nataka kuwakumbusha, waliojua kwanza yote, ya
 kwamba Bwana akiwaokoa watu katika inchi ya Misri,
 6 baadaye akawapoteza wasioamini. Malaika wasiolinda
 mwanzo wao, lakini wakiacha makao yao, amewalinda
 kwa hukumu ya siku iliyo kuu katika mafungo ya ahera

chini ya giza. Kama Sodoma na Gomorra, na miji ili- 7
yoizunguka, kwa ginsi hiyo kama hawa, wakifanya
asherati, wakifuata mwili mgeni, imewekwa kwa dalili,
ikihukumiwa moto wa milele.

Hivi na hawa waotao, wautia mwili ujusi, ukuu hawa- 8
ukubali, utukufu waunenea unajisi. Naye Mikael, ma- 9
laika mkuu, akijadiliana na shetani akafanya maneno
kwa mwili wa Musa, hakuthubutu kumstakia mshtaka
kwa unajisi, illa akasema, Bwana akukemee. Hawa, 10
wasiyoyajua wayanenea unajisi: wayafahamuyo kwa
asili, kama nyama wasio na akili, katika haya wajipoteza.

Ole wao! waendao njiani mwa Kain, kwa kosa la 11
Balaam wajimwagia kwa ujira, wamepotea katika maasi
ya Kora.

Hawa katika karamu za upendano zenu mawaa, 12
wakifanya karamu pasipo hofu, wakijilisha; mawingu
yasiyo na maji, yachukuliwayo na pepo; miti iliyopu-
kutika, isiyo na matunda, iliyokufa kuwili, iliyong'oka;
mawimbi ya bahari yenyi pofu, yakitoa aibu zao wenye- 13
we; nyota zipoteazo, zilindiwazo weusi wa giza hatta
milele.

Akatoa mbele unabii wa hawa, wa saba baada ya 14
Adamu, Enok, akinena, Angalia, Bwana amekuja na
elfu kumi za watakatifu wake, afanye hukumu juu ya 15
wote, awahukumie wote wanajisi wao kwa ajili ya mate-
ndo yote ya unajisi waliyoyatenda kwa unajisi, na kwa
ajili ya magumu yote waliyoyanena juu yake wanajisi
wenyi thambi.

Hawa ndio wanung'unika, wasioona heri, waendao 16
kwa tamaa zao, na kanwa lao lanena makuu mno, waki-
taajabika na watu wa cheo kwa ajili ya fayida.

Ninyi, wapenzi, kumbukeni maneno yaliyonenwa 17
mbele na mitume wa Bwana wetu Isa Masiya, ya kwa- 18
mba waliwaambia, ya kwamba wakati wa mwisho
watakuwa wafanyaji thihaka, wakienda kwa tamaa zao,
walio wanajisi. Ndio wajitengao, wa maisha hii, wa- 19
sio na Roho.

Ninyi, wapenzi, mkijijengea juu ya imani yenu iliyo 20
takatifu, mkiomba katika Roho Mtakatifu, mjilinde 21
katika mapenzi ya Muungu, mkitazamia rehema ya
Bwana wetu Isa Masiya kwa uzima wa milele.

Wangine mkarehemee, wakishindana; wangine 22
23

- 23 'mwaokoe katika hofu, mkiwanyakua katika moto mkichukizwa hatta na vazi lililotiwa mawaa na mwili.
- 24 Kwa yule awezaye kuwalinda msijikwae, na kusimamisha mbele ya utukufu wake pasipo aibu katika furaha, kwa Muungu aliye mmoja mwenyi hekima, Mwo-
25 kozi wetu, kwa Isa Masiya Bwana wetu, utukufu, ukuu, uwezo na nguvu, mbele ya zamani zote, na sasa na hatta milele yote. Amina.

UFUNUO WA YOHANA.

- 1 UFUNUO wa Isa Masiya, aliopewa na Muungu awaonyeshe watumwa wake yalivyopasa kuwa upesi: akathahirisha, akituma kwa malaika wake, kwa mtu-
2 mwa wake Yohana; aliyeshuhudia Neno la Muungu,
3 na ushahidi wake Isa Masiya, alivyoviona. Heri asomaye, nao wasikiao maneno ya unabii, wayalindao yaliyoandikwa katika huo: kwani wakati karibu.
- 4 YOHANA kwa makanisa saba yaliyoko katika Asia: Neema kwenu na amani, katika kwake aliye naye, na aliyekuwa, na atakayekuwa; na katika kwa maroho
5 saba, yaliyo mbele ya kiti chake; na katika kwa Isa Masiya, shahidi aliye amini, mzaliwa wa kwanza wa wafu, na wa kwanza wa wafalme wa duniani. Kwa huyo, aliyetupenda sisi, akatuosha katika thambi zetu
6 kwa damu yake yeye, akatufanya wafalme, wakohani kwa Muungu na Baba wake; kwa huyo utukufu na uwezo hatta milele na milele. Amina.
- 7 Angalia, yuaja na mawingu; na killa jicho litamwona, nao waliomchoma; na makabila yote ya inchi yatamlilia. Ndiyo. Amina.
- 8 Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema Bwana Muungu, aliye naye, aliyekuwa, na atakayekuwa, Mwenyiezi.
- 9 Mimi Yohana, ndugu yenu na asharikiye katika teso, na ufalme, na uvumilivu wa Masiya Isa, nali-kuwako katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya neno la Muungu, na kwa ajili ya ushahidi wa Isa.

Nalikuwa katika Roho siku ya Bwana; nikasikia 10
 nyuma yangu sauti kuu, kama ya paanda, ikinena, Mimi 11
 Alfa na Omega, wa kwanza na wa kwisha. Uonayo
 uyaandike katika chuo, ukapeleke kwa makanisa saba
 yaliyo katika Asia; kwa Efeso, na kwa Smurna, na
 kwa Pergamo, na kwa Thuatera, na kwa Sardi, na
 kwa Filadelfia, na kwa Laodikia. Nikageuka nione 12
 sauti iliyosema nami. Nikigeuka nikaona taa saba
 za thahabu; na kati ya taa saba kama Mwana 13
 Adamu, amevaa hatta miguuni, akifungwa kifuni
 mshipi wa thahabu. Kitwa chake na nyele zake nyeupe 14
 kama sufu nyeupe, kama thuluji; na macho yake kama
 moto uwakao; na miguu yake kama shaba ing'aayo, 15
 kama imeyeyuka katika tanuu; na sauti yake kama
 sauti ya maji mengi: akiwa katika mkono wa kuume 16
 na nyota saba: na katika kanwa lake watoka upanga
 mkali, mkali kuwili: na nathari yake kama jua liki-
 ng'aa katika nguvu yake.

Nilipomwona nikamwangukia miguuni kama nime- 17
 kufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu,
 akiniambia, Usiogope: mimi ni wa kwanza na wa 18
 mwisho, na aliye hayi, niliyekuwa nimekufa, kaangalia
 ni hayi hatta milele na milele; nami ninazo funguo za
 kufa na ahera. Bassi andika uyaonayo, nayo yaliyo, 19
 nayo yatakayokuwa baada ya haya; siri ya nyota saba, 20
 ulizoziona katika mkono wangu wa kuume, nazo taa
 saba za thahabu. Nyota saba ndizo malaika za maka-
 nisa saba; na taa saba ulizoziona ndizo makanisa saba.

KWA malaika ya kanisa lilioko katika Efeso andika, **2**
 Haya anena aziwezaye nyota saba katika mkono wake
 wa kuume, aendaye kati ya taa saba zilizo za thahabu:
 Najua matendo yako, na kazi yako, na uvumilivu wako, **2**
 na kwamba huwezi kuchukuliana na wabaya, na ume-
 wajaribu wajiitao mitume, wala sio, ukawaona wawongo;
 unao na uvumilivu, nawe umechukuliana kwa ajili ya **3**
 jina langu, umetenda kazi, wala hukuzimia. Lakini **4**
 nina juu yako, ya kwamba umeuacha upendano wako wa
 kwanza. Kumbuka ulikoanguka, ukatubu, ukatende **5**
 matendo ya kwanza. Kama sivyo, naja kwako upesi;
 nitaondoa taa yako katika mahali pake, usipotubu.
 Lakini ndiyo uliyo nayo, ya kwamba wachukia matendo **6**
 yao Wanikolaiti, niyachukiayo na mimi. Mwenyi sikio, **7**

asikie Roho awaambiayo makanisa. Ashindaye nitampa kula ya mti wa uzima, ulioko katikati peponi mwa Muungu.

- 8 Na kwa malaika wa kanisa lilioko katika Smurna andika, Haya ayanena aliye wa kwanza na wa mwisho, 9 alikuwa mfu, akafufuka: Najua matendo yako, na shidda, na umasikini (lakini mtajiri wee), na unajisi wao wajiitao Wayahudi, wala sio, illa sunagogi la Shetani. 10 Usiogope yatakayokupata: angalia, mstaki atatupa wa kwako katika gereza mjaribiwe; mtakuwa na shidda siku kumi. Uwe amini hatta kufa, nami nitakupa taji 11 ya uzima. Mwenyi sikio, asikie Roho awaambiayo makanisa. Ashindaye hathulumiwi na kufa kwa pili. 12 Na kwa malaika wa kanisa lilioko katika Pergamo andika, Haya ayanena aliye nao upanga mkali, mkali 13 kuwili: Najua ukaapo, ndipo kiti chake Shetani: nawe washika jina langu, wala hukukania imani yangu, hatta siku za Antipa shahidi wangu amini, aliyeuawa kwenu, 14 Shetani akaapo. Lakini ninayo juu yako yasiyo mengi, ya kwamba unao huko washikao elimu ya Balaam, aliyemfunza Balak atie chukizo mbele ya waana wa 15 Israeli, kula zilizotolewa kwa sanamu, na kuzini. Hivi unao na wewe waishikao elimu ya Wanikolai, ndilo 16 nilichukialo. Bassi utubu: kama sivyo, naja kwako upesi; nitawafanyia vita kwa upanga ulio wa kanwa 17 langu. Mwenyi sikio, asikie Roho awaambiayo makanisa. Ashindaye nitampa kula manna iliyostirika, nitampa na jiwe jeupe, na juu ya jiwe jina jipya limeandikwa, asilolijua mtu illa yule aliyepewa. 18 Na kwa malaika wa kanisa lilioko katika Thuatera andika, Haya ayasemayo Mwana wa Muungu, aliye na macho kama moto uwakao, na miguu yake kama shaba 19 ing'aayo: Najua matendo yako, na upendano, na ungoje, na wamini, na uvumilivu wako, na matendo yako ya 20 mwisho yamepita matendo ya kwanza. Lakini ninayo juu yako, ya kwamba wachukuliana na mke Yezebel, ajiitaye nabii, afundishaye na akoseshaye watumwa wa 21 ngu kuzini, na kula zilizotolewa kwa sanamu. Nimempa muhulla atubu katika kuzini kwake, wala hataki kutubu. Angalia, nitamlaza kitandani, nao wazinio naye katika shidda nyingi, isipokuwa watubu katika matendo 22 yao; na waanawe nitaua kwa kufa: na makanisa yote 23

watajua ya kwamba ndimi atafutaye viuno na moyo : nami
 24 nitawapa killa mtu kwa matendo yenu. Nawaambia ninyi,
 mliosalia katika Thuatera, wasio na elimu hii, wasiojua
 yaliyo chini ya Shetani, kama wanena, Sitaweka juu yenu
²⁵₂₆ uzito, illa mliyo nayo myashike hatta nitakapokuja. Naye
 ashindaye na alindaye hatta mwisho matendo yangu, nita-
 27 mpa nguvu juu ya mataifa : atawachunga kwa fimbo ya
 chuma, kama vyombo vya udongo atawaseta ; kama nami
 28 nilivyopewa na Baba wangu : nami nitampa nyota ya
 29 assubui. Mwenyi sikio, asikie Roho awaambiayo ma-
 kanisa.

3 NA kwa malaika wa kanisa lilioko katika Sardi
 andika, Haya ayanena aliye nazo roho saba za Muungu,
 na nyota saba : Najua matendo yako, ya kwamba unalo
 2 jina la kuwa hayi, lakini umekufa. Ukeshe, ufanye
 imara yaliosalia, yaliyo katika kufa : sikuyaona matendo
 3 yako yamekamilika mbele ya Muungu. Kumbuka ginsi
 ulivyopewa, na ulivyosikia, ukajilinde, ukatubu. Usipo-
 kesha nitakuja juu yako kama mwivi, usipojua saa ipi
 4 nitakapokuja juu yako. Lakini unayo majina machache
 na katika Sardi, wasiotia uchafu katika mavazi yao : nao
 watatembea kwangu katika meupe ; ya kuwa wamesta-
 5 hili. Ashindaye, huyu atavikwa kwa mavazi meupe, wala
 sitafuta jina lake katika kitabu cha uzima ; nitaungama
 jina lake mbele ya Baba wangu, na mbele ya malaika
 6 zake. Mwenyi sikio, asikie Roho awaambiayo ma-
 kanisa.

7 Na kwa malaika wa kanisa lilioko katika Filadelfia
 andika, Haya anenayo aliye mtakatifu, mwenyi kweli,
 mwenyi ufunguo wa Daud, afunguaye wala mtu hafu-
 8 ngi, afungaye wala mtu hafungui : Najua matendo yako
 (tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa,
 wala hawezi mtu kuufunga), ya kuwa unayo nguvu isi-
 yo nyingi, nawe umelinda neno langu, wala hukukania
 9 jina langu. Angalia, nawatoa walio wa sunagogi la
 shetani, wajiitao Wayahudi, wala sio, illa wawongo,
 angalia, nitawafanya waje wasujudie miguuni pako
 10 wakajue ya kwamba mimi nimekupenda. Kwamba
 umelinda neno la uvumilivu wangu, nami nitakulinda
 katika saa ya kujaribiwa, itakayokuja juu ya ulimwengu
 11 wote, kuwajaribu wakaao juu ya inchi. Naja upesi :
 12 shika uliyo nayo, mtu asitwae taji yako. Ashindaye

- nitamfanya nguzo katika hekalu la Muungu wangu, wala hatatoka tena 'nje; nitaandika juu yake jina la Muungu wangu, na jina la mji wa Muungu wangu, Yerusalemi iliyo mpya, ishukayo katika mbinguni, katika
- 13 kwa Muungu wangu, na jina langu lililo jipya. Mwenyi sikio, asikie Roho awaambiayo makanisa.
- 14 Na kwa malaika wa kanisa lilioko katika Laodikia andika, Haya ayanena aliye Amina, shahidi amini na mwenyi kweli, mwanzo wa kuumba kwa Muungu:
- 15 Najua matendo yako, ya kwamba si wa baridi wala si wa moto: afathali ungalikuwa wa baridi ao wa moto.
- 16 Hivi, ya kwamba una uvuguvugu, wala si wa moto wala
- 17 si wa baridi, nitakutapika katika kanwa langu. Kwamba wanena, Ni mtajiri na mwenyi mali, wala sihitajii kitu; wala hujui ya kwamba wewe u maskini, na ku-
- 18 hurumiwa, na fukara, na kipofu, na utupu: nakupa shauri ununue kwangu thahabu iliyojaribiwa kwa moto, mpate kuwa na mali; na mavazi meupe, mpate kuvaa, wala aibu ya utupu wako usionekane; na marhamu ya
- 19 kupakia machoni mwako, upate kuona. Mimi niwape ndao nawakemea na nawarudi. Bassi ujitie uwivu ukatubu. Angalia, nimesimama mlangoni nabisha: mtu akisikia sauti yangu, akifungua mlango, nitaingia kwake, nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.
- 21 Ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami kitini mwangu, kama nilivyoshinda mimi, nikaketi pamoja na Baba
- 22 wangu kitini mwake. Mwenyi sikio, asikie Roho awaambiayo makanisa.
- 4 BAADA ya haya naliona, mlango umefunuka mbinguni, na sauti ya kwanza niliyoisikia kama ya paanda, ikisema nami, ikinena, Panda hatta hapa, nami nitakuo-
- 2 nyesha yapaswayo kuwa baada ya haya. Marra nalikuwa katika Roho. Kiti kimewekwa mbinguni, na juu
- 3 ya kiti akaaye; naye akaaye kama machoni jiwe la yaspi na sardio: na upindi wa mvua kuzunguka kiti, kama machoni zumaridi.
- 4 Na kukizunguka kiti viti asharini na vinne: na juu ya viti wazee asharini na wanne wameketi, wakiwikwa mavazi meupe, na juu ya vitwa vyao taji za thahabu.
- 5 Na katika kiti ukatoka umeme, na sauti, na ngurumo. Na taa saba za moto zikiwaka mbele ya kiti.

ndizo Roho saba za Muungu ; na mbele ya kiti bahari 6
ya kioo, kama krustallo.

Na kati ya kiti, na pande zote za kiti, nyama wanne, 7
wamejaa macho mbele na nyuma. Na nyama wa kwa-
nza kwa mfano wa simba, na nyama wa pili kwa mfano
wa ndama, na nyama wa tatu mwenyi uso wa mtu, na
nyama wa 'nne kwa mfano wa tai arukaye. Na nyama 8
wanne killa mmoja alikuwa na mabawa sita ; pande zote
na ndani wakajaa macho : wala hawakomi mchana wala
usiku wakinena, Takatifu, Takatifu, Takatifu, Bwana
Muungu Mwenyiezi, aliyekuwa, aliye, naye atakaye-
kuwa.

Na nyama watoapo utukufu, na heshima, na kushu- 9
kuru, kwa yule akaaye juu ya kiti, aliye hayi hatta
milele na milele, waanguka wazee asharini na wanne 10
mbele yake akaaye juu ya kiti, wamsujudia aliye hayi
hatta milele na milele, nao watupa taji zao mbele ya
kiti, wakinena, Umestahili, Bwana, kupewa utukufu, na 11
heshima, na nguvu, kwani ndiwe uliyeviumba vyote,
na kwa kupenda kwako vimekuwa vikaumbwa.

NIKAONA mkononi mwa kuume mwake akaaye juu 5
ya kiti kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kikatiwa
muhuri saba.

Nikaona malaika mwenyi nguvu akihubiri kwa sauti 2
kuu, Nani astahiliye kukifungua kitabu, na kuzivunja
muhuri zake? Wala hakuna awezaye katika mbingu, 3
wala juu ya inchi, wala chini ya inchi, kukifungua ki-
tabu, wala kukitazama.

Nikalia sana, ya kwamba hakuna aliyeonekana aliye- 4
stahili kukifungua kitabu na kukisoma, wala kukitaza-
ma. Mmoja wao wazee akaniambia, Usilie : ameshinda 5
Simba aliye wa kabila ya Yuda, Shina la Daud, kuki-
fungua kitabu na kuzivunja muhuri zake saba.

Nikaona kati ya kiti na nyama wanne, na kati ya 6
wazee, Mwana kondoo amesimama kama ameuawa,
mwenyi pembe saba na macho saba, ndizo Roho saba za
Muungu, zinaotumwa kwa inchi yote. Akaja akiki- 7
twaa kitabu katika mkono wa kuume wake akaaye juu
ya kiti. Hatta alipokitwaa kitabu, nyama wanne na 8
wazee asharini na wanne wakaanguka mbele yake
Mwana kondoo, wakiwa killa mtu na kinubi, na vitupa
vya thahabu vikijaa manukato, ndivyo masala ya wata-

- 9 katifu. Wakaimba wimbo mpya, wakinena, Umestahili kukitwaa kitabu na kufungua muhuri zake, ya kwamba umeuawa, ukamnunulia Muungu kwa damu yako katika
- 10 killa kabila na ulimi, na wa watu na wa mataifa, ukawafanya kwa Muungu wetu wafalme na wakohani; nao wamiliki juu ya inchi.
- 11 Nikaona, nikasikia sauti ya malaika wengi, pande zote za kiti, na za nyama, na za wazee; na hesabu yao elfu kumi marra elfu kumi na elfu marra elfu,
- 12 wakinena kwa sauti kuu, Amestahili Mwana kondoo aliyeuawa kupewa nguvu, na mali, na hekima, na
- 13 uwezo, na heshima, na utukufu, na mbaraka. Na killa kiumbe kilicho mbinguni, na juu ya inchi, na chini ya inchi, na juu ya bahari, navyo vilivyo ndani yao, nikavisikia vyote vikinena, Kwa yeye akaaye juu ya kiti na kwa Mwana kondoo, mbaraka, na heshima, na utu-
- 14 kufu, na uwezo, hatta milele na milele. Nyama wanne wakanena, Amina. Wazee asharini na wanne wakaa-nguka wakamsujudia aliye hayi milele na milele.
- 6** NIKAONA, Mwana kondoo alipofungua moja ya muhuri, nikasikia mmoja wa nyama wanne akinena kama
- 2 sauti ya ngurumo, Njoo kaone. Nikaona, frasi mweupe, na akaaye juu yake mwenyi upindi; akapewa taji: akatoka akishinda na illi ashinde.
- 3 Hatta alipofungua muhuri ya pili nalisikia nyama wa
- 4 pili akinena, Njoo kaone. Akatoka frasi mwingine, rangi ya moto: na akaaye juu yake amepewa kutwaa amani iliyo katika inchi, wauane: akapewa upanga mkubwa.
- 5 Hatta alipofungua muhuri ya tatu, nalisikia nyama wa tatu akinena, Njoo kaone. Nikaona, frasi mweusi; na akaaye juu yake mwenyi mizani mkononi mwake.
- 6 Nikasikia sauti kati ya nyama wanne, ikinena, Pishi ya ngano kwa dinari, na pishi tatu za shayiri dinari; na mafuta na mvinyo usiuthuru.
- 7 Hatta alipofungua muhuri ya nne, nalisikia nyama
- 8 wa 'nne akinena, Njoo kaone. Nikaona, frasi rangi ya majani meupe: naye akaaye juu yake jina lake Mauti; akafuata Ahera baadaye. Wakapewa uwezo juu ya sehemu ya 'nne ya inchi, kuua kwa upanga, na kwa njaa, na kwa kufa, na kwa nyama za inchi.
- 9 Hatta alipofungua muhuri ya tanu, naliona chini ya

mathbahu roho zao waliouawa kwa ajili yake Neno la Muungu, na kwa ushabidi walio nao: wakalia kwa 10 sauti kuu, wakinena, Hatta lini, ee Mola, mtakatifu na mwenyi kweli, huhukumii wala hufanyi iliyo haki kwa damu yetu juu yao wakaa juu ya inchi? Wakapewa 11 killa mtu nguo nyeupe, wakaambiwa wastarehe wakati haba bado, hatta watakapotimia wajoli wao na ndugu zao watakaouawa kama na wale.

Nikaona alipofungua muhuri ya sita likawa tetemeko 12 kubwa; jua limekuwa jeusi kama sako ya nyele, na mwezi umekuwa kama damu; na nyota za mbingu 13 zikaanguka hatta inchi, kama mtini upukutikavyo mapooza yake ukitikisika na upepo mwingi. Uwingu 14 ukachukuliwa kama kitabu kilichozingwa; na killa mlima na kisiwa kikaondoshwa katika mahali pake. Wafalme wa inchi, na wakuu, na majemadari, na mata- 15 jiri, nao wenyi nguvu, na killa mtumwa, na killa huru, wakajificha katika mapaango na katika miamba ya milima, wakaiambia milima na miamba, Angukeni juu 16 yetu mkatusetiri katika usoni pake akaaye juu ya kiti, na katika hasira yake Mwana kondoo: kwani siku iliyo kuu 17 ya hasira yake imekuja; na nani awezayo kuistahimili.

HATTA baadaye nikaona malaika wanne wakisimama 7 juu ya pembe 'nne za inchi, wakiziweza pepo 'nne za inchi, upepo usivume juu ya inchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti.

Nikaona malaika mwingine akipanda katika macho 2 ya jua, akiwa na muhuri ya Muungu aliye hayi: akawalilia malaika wanne kwa sauti kuu, waliopewa wai-thuru inchi na bahari, akinena, Msithuru inchi, wala 3 bahari, wala miti, hatta tutakapowatia muhuri watumwa wa Muungu wetu juu ya paji la uso wao.

Nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri, mia na arobaini na 'nne elfu, waliotiwa muhuri katika killa kabila ya waana wa Israeli. Wa kabila ya Yuda thenashara elfu 5 wakatiwa muhuri. Wa kabila ya Reuben thenashara elfu. Wa kabila ya Gad thanashara elfu. Wa kabila ya 6 Asher thenashara elfu. Wa kabila ya Nafthali thenashara elfu. Wa kabila ya Manasse thenashara elfu. Wa kabila ya Simeon thenashara elfu. Wa kabila ya 7 Lawi thenashara elfu. Wa kabila ya Issakar thenashara elfu. Wa kabila ya Zabulon thenashara elfu. Wa 8

kabila ya Yusuf thenashara elfu. Wa kabila ya Benyamin thenashara elfu wakatiwa muhuri.

- 9 Baada ya haya nikaona, makutano mengi, asiyoweza mtu kuwahasibu, kwa killa taifa, na kabila, na watu, na ulimi, wamesimama mbele ya kiti, na mbele ya Mwana kondoo, wamevikwa kwa nguo nyeupe, na matawi ya
- 10 mitende mikononi mwao; wakalia kwa sauti kuu, wakinena, Wokovu kwa Muungu wetu akaaye juu ya kiti, na kwa Mwana kondoo.
- 11 Nao malaika wote wamesimama pande zote za kiti, na za wazee, na za nyama wanne; wakaanguka mbele
- 12 ya kiti usoni mwao, wakamsujudia Muungu, wakinena, Amina: Mbaraka, na utukufu, na hekima, na kushukuru, na heshima, na nguvu, na uwezo, kwa Muungu wetu hatta milele na milele. Amina.
- 13 Akajibu mmoja wa wazee akaniambia, Hawa walio-
- 14 vikwa nguo nyeupe ni nani, na walikotoka wapi? Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hawa ndio waliotoka katika shidda iliyo nyingi, wakaosha nguo zao, wakazifanya nyeupe katika damu
- 15 yake Mwana kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti chake Muungu; nao wamwabudu mchana na usiku katika hekalu lake: naye akaaye juu ya kiti atafanya
- 16 masikani yake kwao. Hawaoni tena njaa, wala hawaoni kiu, wala jua halitawapiga, wala kuungua kwote: akiwa
- 17 Mwana kondoo aliye kati ya kiti atakayewachunga, na atakayewaleta kwa chemchemi hayi za maji: na Muungu atafuta machozi yote katika macho yao.
- 8 HATTA alipofungua muhuri ya saba, kimekuwa kimya katika mbingu kama nuss ya saa.
- 2 Nikawaona malaika saba wasimamao mbele ya Muungu, wapakewa mapaanda saba.
- 3 Malaika mwingine akaja akasimama kwa mathbahu, akiwa na vukizo la thahabu. Akapewa manukato mengi, ayatoe katika masala ya watakatifu wote juu ya
- 4 mathbahu ya thahabu iliyo mbele ya kiti. Ukapanda mvuke wa masala ya watakatifu katika mkono wa
- 5 laika mbele ya Muungu. Malaika akalitwaa vukizo akalijaza na moto wa mathbahu, akalitupa katika inchi: zikawa sauti, na ngurumo, na umeme, na tetemeko.
- 6 Nao malaika saba walio nayo mapaanda saba, wakajiweka tayari wapige.

Malaika wa kwanza akapiga paanda : ikawa mvua ya 7
mawe na moto ukichanganyika na damu, ikatupwa
katika inchi : theluth ya miti ikateketea, na killa jani
bichi likateketea.

Malaika wa pili akapiga paanda, na kama mlima 8
mkubwa ukiwaka moto ukatupwa katika bahari : the-
luth ya bahari ikawa damu ; wakafa theluth ya viumbe 9
walio katika bahari walio wahayi ; na theluth ya meri-
kebu zikapotea.

Malaika wa tatu akapiga paanda : ikaanguka katika 10
mbingu nyota kubwa ikiwaka kama taa, ikaanguka juu
ya theluth ya mito, na juu ya chemchemi za maji ; na 11
jina la nyota linakwitwa Absintho : na theluth ya maji
ikawa absintho ; wengi wa watu wakafa kwa maji, ya
kuwa yametiwa uchungu.

Malaika wa 'nne akapiga paanda : ikapigwa theluth 12
ya jua, na theluth ya mwezi, na theluth ya nyota, the-
luth yao iwe giza, wala mchana usimwangaze theluth
yake, wala usiku vivyo.

Nikaona, nikasikia malaika mmoja akiruka katikati 13
ya mbinguni, akinena kwa sauti kuu, Ole ! ole ! ole
wao wakao juu ya inchi, kwa sauti zilizosalia za paanda
za malaika watatu watakaopiga.

MALAIKA wa tanu akapiga paanda : nikaona nyota 9
ya mbinguni imeanguka katika inchi : akapewa ufu-
nguo wa shimo la abuso. Akalifungua shimo la abuso ; 2
moshi ukapanda katika shimo, kama moshi wa tanu
kubwa ; jua na anga likatiwa giza kwa moshi wa
shimo.

Katika moshi wakatoka nzige juu ya inchi ; waka- 3
pewa nguvu, kama wanazo nguvu 'nge za inchi. Waka- 4
mbiwa wasithuru majani ya inchi, wala killa kibichi,
wala killa mti, illa watu tu wasio na muhuri ya Muungu
juu ya nyuso zao. Wakapewa wasiwaue, illa wawau- 5
mize miezi mitanu. Na kuumiza kwao kama kuumiza
kwa 'nge, ampigapo mtu. Siku zile watu watatafuta 6
kufa, wala hawatakuona : watatamani kufia mbali, na
kufa kutawakimbia. Na maumbo ya nzige kama frasi 7
zilizotengenezwa kwa vita ; na juu ya vitwa vyao kama
taji kama za thahabu, na nyuso zao kama nyuso za
watu. Wakawa na nyele kama nyele za waanaake ; na 8
meno yao kama ya simba. Wakawa na mabapa kifuani, 9

- kama mabapa ya chuma. Na sauti ya mabawa yao kama sauti ya magari ya frasi wengi yakienda upesi
 10 kwa vita. Wakawa na mikia kama 'nge, na nyuma katika mikia; na nguvu yao kuwathuru watu miezi
 11 mitanu. Wanao juu yao mfalme, ndiye malaika wa abuso, jina lake kwa Kiebrania Abaddon, na kwa Kiyoni
 12 nani analo jina Mharibu. Ole wa mosi umepita: zinakuja tena ole mbili baadaye.
- 13 Malaika wa sita akapiga paanda: nikasikia sauti moja katika pembe nne za mathabahu ya thahabu, ili-
 14 yoko mbele ya Muungu, ikimwambia malaika wa sita, aliye na paanda, Fungua malaika wanne waliofungwa
 15 katika mto Eufirati ulio mkubwa. Akawafungua malaika wanne waliowekwa tayari kwa saa, na siku, na
 16 mwezi, na mwaka, wawaue theluth ya watu. Na hesabu ya majeshi wapandao frasi, elfu kumi mbili marra
 17 elfu kumi: nikasikia hesabu yao. Nikawaona hivi frasi katika njozi, nao waliokaa juu yao, wakiwa na mabapa ya kifuani ya moto, na ya samawati, na ya kiberiti: na vitwa vya frasi kama vitwa vya simba; na katika makanwa yao ukatoka moto, na moshi, na kiberiti.
- 18 Kwa haya matatu theluth ya watu wakauawa, kwa moto na kwa moshi na kwa kiberiti, kilichotoka katika maka-
 19 nwa yao. Kwani nguvu yao ni katika kanwa lao, na katika mikia yao: kwani mikia yao kama ya nyoka, yenyi vitwa; na kwa hiyo wathuru.
- 20 Na watu waliosalia, wasiouawa kwa mapigo haya, hawakutubu katika matendo ya mikono yao, wasiwasu-
 judie pepo, wala sanamu za thahabu, na za fetha, na za shaba, na za mawe, na za mti; zisizoweza kutazama,
 21 wala kusikia, wala kutembea: wala hawakutubu katika mauaji yao, wala katika uchawi wao, wala katika washerati wao, wala katika kwiba kwao.
- 10 NIKAONA malaika mwingine hodari akishuka katika mbinguni, amevikwa na wingu; na upindi wa mvua juu ya kitwa chake, na uso wake kama jua, na
 2 miguu yake kama nguzo za moto; akiwa na kitabu kidogo mkononi mwake kimefunuka: akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, na wa kushoto juu ya
 3 inchi; akalia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo.
 4 Hatta alipolia, zikanena ngurumo saba sauti zao. Hatta ziliponena ngurumo saba sauti zao, nikawa katika

kuandika: nikasikia sauti ya mbinguni ikinena, Tia muhuri juu yao ziliyoyanena ngurumo saba, wala usiyaandike.

Naye malaika niliyemwona akisimama juu ya bahari 5
na juu ya inchi, akainua mkono wake kwa mbingu, 6
akaapa kwa yeye aliye hayi hatta milele na milele, 6
aliyeumba mbingu nazo zilizomo, na inchi nazo zilizomo, 7
na bahari nazo zilizomo, ya kwamba wakati hautakuwa 7
tena: illa siku za sauti yake malaika wa saba, atakapoku-
wa katika kupiga paanda, nayo siri ya Muungu itatimia, 7
kama alivyowahubiria watumwa wake manabii.

Na sauti niliyoisikia katika mbinguni, ikisema nami 8
tena, ikanena, Ondoka, twae kitabu kidogo kilichofu- 8
nguliwa katika mkono wa malaika asimamaye juu ya 9
bahari na juu ya inchi. Nikamwendea malaika, nika- 9
mwambia, Nipe kitabu kidogo. Akaniambia, Twae, 9
ukile pia; nacho kitakutia uchungu tumboni, lakini
kamwani mwako kitakuwa tamu kama asali.

Nikakitwaa kitabu kidogo katika mkono wa malaika, 10
nikakila. Kikawa kanwani mwangu kama asali kita- 10
mu: hatta nilipokila, tumbo langu likatiwa uchungu.
Akaniambia, Imekupasa kufanya unabii tena juu ya 11
watu, na mataifa, na ndimi, na wafalme wengi. 11

NIKAPEWA unyasi kama ufito, kusema, Ondoka, 11
kapima hekalu la Muungu, na mathbahu, nao wanaosu-
judia humo. Na behewa iliyo 'nje ya hekalu utupe 'nje, 2
wala usiipime; ya kwamba imetolewa kwa mataifa: na
mji mtakatifu wataukanyaga miezi arobaini na miwili.

Nami nitawapa mashahidi wangu wawili, nao wata- 3
fanya unabii siku elfu na miteen na sitini, wakivikwa 3
na sako. Hawa ndio mizetuni miwili na taa mbili zili- 4
zosimama mbele yake Muungu wa inchi. 4

Na mtu akitaka kuwathuru, moto hutoka hatika ka- 5
nwa lao, utawala maadui yao; na mtu akitaka kuwathuru, 5
hivyo imepasa auawe. Hawa wanao nguvu ya kuzi- 6
funga mbingu, mvua isinye siku zao za unabii. Nao 6
wanao nguvu juu ya maji kuyageuza kuwa damu, na
kuipiga inchi marra wazipendazo kwa mapigo yote.

Hatta watakapomaliza ushahidi wao, nyama apanda- 7
ye katika abuso atafanya vita nao; atawashinda na 7
atawaua. Na mzoga wao katika njia ya mji ule mku- 8
bwa, ulioitwa kwa roho Sodoma na Misri, na aliposuli- 8

- 9 bishwa Bwana wao. Nao watautazama mzoga wao, wa watu, na wa makabila, na wa ndimi, na wa mataifa, siku tatu na nusu, wala mizoga yao haitachukuliwa kuwekwa kaburini.
- 10 Nao wakaaao juu ya inchi watafurahiwa juu yao na watapendezewa, nao watapelekana zawadi; ya kwamba manabii wawili hawa wakawauma wakaaao juu ya inchi.
- 11 Hatta baada ya siku tatu na nusu, roho ya uzima wa Muungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; hofu kuu ikaanguka juu yao waliowaona.
- 12 Wakasikia sauti kuu katika mbinguni ikiwaambia, Pandeni hapa. Wakapanda mbinguni katika wingu;
- 13 maadui yao wakawatazama. Saa ile ikawa tetemeko kuu, na sehemu ya kumi ya mji ikaanguka; wakauawa katika tetemeko majina ya watu elfu saba. Nao walio-salia wakaingwa na hofu, wakamtukuza Muungu wa
- 14 mbingu. Ole wa pili umepita: ole wa tatu waja upesi.
- 15 Malaika wa saba akapiga paanda; pakawa sauti kuu katika mbinguni, zikina, Ufalme wa dunia umekuwa wa Bwana wetu na wa Masiya yake, naye atamiliki
- 16 hatta milele na milele. Nao wazee asharini na wanne, wakaaao mbele ya Muungu juu ya viti vyao, wakaangu-
- 17 ka usoni, wakamsujudia Muungu, wakinena, Twakushu-kuru, Bwana Muungu Mwenyiezi, uliye nawe, na uliye-kuwa, ya kwamba umetwaa nguvu zako kuu ukamiliki.
- 18 Mataifa wakaona hasira, na hasira yako imekuja, na wakati wa wafu wahukumawe, na kupewa thawabu watumwa wako, manabii na watakatifu, nao wachao jina lako, wadogo na wakuu; na kuharibika inchi.
- 19 Likafunuka hekalu la Muungu katika mbingu; lika-onekana sanduku la agano yake, katika hekalu lake; zikawa na umeme, na sauti, na ngurumo, na tetemeko, na mvua ya mawe nyingi.
- 12 ISHARA kuu ikaonekana mbinguni. Mwanamke amevikwa kwa jua, na mwezi chini ya miguu yake, na
- 2 juu ya kitwa chake taji ya nyota thenashara; naye akiwa na mimba akalia, akiwa na utungu na akiumwa katika kuzaa.
- 3 Ikaonekana ishara ngine mbinguni; joka kubwa la moto, lenyi vitwa saba na pembe kumi, na juu ya vitwa
- 4 vyake vilemba saba: na mkia wake ukakokota theluth ya nyota za mbingu, ukaziangusha katika inchi.

Joka likasimama mbele ya mwanamke aliye katika kuzaa, illi akizaa amle mtoto wake. Akazaa mwana, mume, atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Mtoto wake akachukuliwa hatta kwa Muungu na kwa kiti chake. Mwanamke akakimbia hatta nyika, alipokuwa na mahali pamewekwa tayari na Muungu, wapate huko kumlisha siku elfu na miteen na sitini.

Palikuwa na vita mbinguni: Mikael na malaika zake wakipigana na joka; joka akapigana na malaika zake; wala hawakuweza, wala uwingu haukuwaweka tena. Akatupwa joka kubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Mstaki na Shetani, akoseshaye ulimwengu wote; akatupwa juu ya inchi, na malaika zake pamoja naye wakatupwa.

Nikasikia sauti kuu katika mbingu, ikinena, Sasa imekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Muungu wetu, na uwezo wa Masiya yake: ya kwamba ametupwa aliyewastaki ndugu zetu, awastakiye mbele ya Muungu wetu, mehana na usiku. Nao wakamshinda kwa damu yake Mwana kondoo, na kwa neno la ushahidi wao; wala hawakupenda maisha yao hatta kufa. Kwa hiyo furahini, mbingu, nanyi mtuao humo. Ole wao wakao katika inchi na bahari, kwani Mstaki amewashukia akiwa na ghatuabu nyingi, akijua ya kwamba muhulla anao haba.

Hatta alipoona joka ya kwamba ametupwa juu ya inchi, akamfukuza mwanamke aliyemzaa mume. Mwanamke akapewa mabawa mawili yake tai mkubwa, apate kuruka hatta nyikani hatta mahali pake, anapolishwa wakati, na nyakati, na nusu ya wakati, katika usoni pa nyoka. Nyoka akatupa katika kanwa lake nyuma ya mwanamke, maji kama mto, amfanye achukuliwe na mto. Inchi ikamsayidia mwanamke, inchi ikafumbua kanwa lake, ikanywa mto alioutupa joka katika kanwa lake.

Joka likaghathabika na mwanamke, akaenda afanye vita na wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Muungu, nao wanao ushahidi wake Isa.

AKASIMAMA juu ya mchanga wa bahari. **13**

Nikaona katika bahari nyama ikitoka, yenyi pembe kumi na vitwa saba, na juu ya pembe vilemba kumi, na juu ya vitwa vyake majina ya unajisi.

- 2 Na nyama niliyoiona imefanana na chui, na miguu yake kama ya dubba, na kanwa lake kama kanwa la simba. Joka likampa nguvu zake, na kiti chake, na uwezo mwingi.
- 3 Nikaona kitwa kimoja chake kama kimejeruhi hatta kufa; na pigo la kufa likaponyeka.
- 4 Inchi yote ikataajabika nyuma ya nyama. Wakamsujudia joka, ya kwamba amempa nyama uwezo; wakamsujudia nyama, wakinena, Nani kama nyama? na nani awezaye kufanya vita naye?
- 5 Akapewa kanwa linenalo makuu na manajisi; akapewa uwezo wa kufanya, miezi arobaini na miwili.
- 6 Akafumbua kanwa lake kwa manajisi hatta kwa Muungu, kumnena unajisi jina lake, na masikani yake, 7 nao watuao mbinguni. Akapewa kufanya vita nao watakatifu, na kuwashinda: akapewa uwezo juu ya killa 8 kabila, na ulimi, na taifa. Wakamsujudia wote wakao katika inchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima cha Mwana kondoo, aliyeuawa tangu kuwekwa ulimwengu.
- ⁹₁₀ Mtu akiwa na sikio, asikie. Mtu akiwa kwa kufunga, aende kufungwa: mtu akiwa kwa upanga, imempasa kuuawa kwa upanga. Ndio uvumilivu na imani ya watakatifu.
- 11 Nikaona nyama mgine akipanda katika inchi. Alikuwa na pembe mbili kama mwana kondoo, akanena kama joka. Naye afanya kwa nguvu yote ya nyama wa kwanza mbele yake, na afanya inchi nao wakao humo waisujudie nyama wa kwanza, aliyeponyeka pigo la kufa lake.
- 13 Naye afanya ishara kuu, na moto upate kushuka ka-
14 tika mbinguni hatta inchi mbele ya watu; naye awakosha wakao juu ya inchi kwa ishara alizopewa kufanya mbele ya nyama; akiwaambia wakao juu ya inchi wafanye sanamu kwa nyama, aliye nalo pigo la upanga
15 akapona. Naye akapewa kutia roho katika sanamu ya nyama, na sanamu ya nyama ipate kunena, aka-
16 fanye wasioisujudia sanamu ya nyama wauawe. Naye afanya wote, wadogo na wakuu, na matajiri na masikini, na mahuru na watumwa, awatie alama katika mkono
17 wao wa kuume, ao katika paji la uso wao; wala mtu

asiweze kununua wala kuza, asipokuwa nayo alama, ao jina la nyama, ao hesabu ya jina lake.

Hiyo ndiyo hekima. Mwenyi akili ahasibu hesabu ya 18 nyama; kwani ni hesabu ya mtu: na hesabu yake sita mia na sitini na sita.

NIKAONA, Mwana kondoo amesimama juu ya mlima **14**
 Sayuni, na pamoja naye mia na arobaini na 'nne elfu wenyi jina la Baba wake limeandikwa juu ya nyuso zao. Nikasikia sauti katika mbinguni, kama sauti ya maji **2**
 mengi, na kama sauti ya ngurumo kuu: na sauti niliyoisikia kama ya wapiga kinubi wakipiga vinubi vyao: nao waimba kama uimbo mpya mbele ya kiti, na mbele **3**
 ya nyama wanne, na wazee: wala hawezi mtu kujifunza uimbo, illa mia na arobaini na 'nne elfu walionunuliwa katika inchi. Hawa ndio wasiojitia uchafu kwa **4**
 waanaake; kwani ni bikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana kondoo killa aendako. Hawa wamenunuliwa katika watu, malimbuko kwa Muungu na kwa Mwana kondoo. Wala katika kanwa lao haikuonwa hila: kwani hawana **5**
 hatiya.

Nikaona malaika mwingine akiruka kati ya mbingu, **6**
 mwenyi anjili ya milele awahubirie wakaao juu ya inchi, na killa taifa, na kabila, na ulimi, na watu, akinena kwa **7**
 sauti kuu, Mwogopeni Muungu, mkamtukuze; ya kwamba saa ya hukumu yake imekuja: mkamsujudie aliyefanya mbingu na inchi, na bahari, na chemchemi za maji.

Na malaika mwingine akamfuata, akinena, Imeanguka, **8**
 imeanguka, Babeli, mji ulio mkubwa, uliowanyweshwa mataifa yote mvinyo wa hasira ya washarati wake.

Na malaika wa tatu akawafuata, akinena kwa sauti **9**
 kuu, Mtu akisujudia nyama na sanamu yake, naye akipokea alama juu ya paji la uso wake, ao juu ya mkono wake, naye huyu atakunwa mvinyo wa hasira ya Muu- **10**
 ngu, uliomiminika pasipo maji katika kikombe cha ghathabu yake; naye ataumwa katika moto na kiberiti, mbele yao malaika watakatifu, na mbele yake Mwana kondoo. Na moshi wakuuma kwao kupandahatta milele na **11**
 milele; wala hawana kustarehe mchana wala usiku, wasujudiao nyama na sanamu yake, wala mtu akipokea alama ya jina lake. Hapa uvumilivu wa watakatifu, **12**
 wazilindao amri za Muungu, na imani yake Isa.

- 13 Nikasikia sauti katika mbinguni, ikinena, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Ndio, anena Roho, wapate kupumzika katika taabu zao; na matendo yao yafuata pamoja nao.
- 14 Nikaona, wingu jeupe; na juu ya wingu amekaa kama Mwana Adamu, akiwa, juu ya kitwa, na taji ya
- 15 thahabu, na katika mkono wake mundu mkali. Malaika mwingine akatoka katika hekalu, akimlilia kwa sauti kuu aliyekaa juu ya wingu, Tia mundu wako kavuna: ya kuwa saa ya kuvuna imekuja; ya kuwa vuno la inchi
- 16 limekomaa. Naye aliyekaa juu ya wingu akatupa mundu wake juu ya inchi; inchi ikavunwa.
- 17 Malaika mwingine akatoka katika hekalu lililo mbi-
- 18 nguni, akiwa na yeye na mundu mkali. Malaika mwingine akatoka katika mathbahu, aliye na nguvu juu ya moto; akamlilia kwa sauti kuu aliye na mundu mkali, akinena, Tia mundu wako mkali, kachuma matawi ya mzabibu wa inchi; kwani zabibu zake zimepe-
- 19 vuka. Malaika akatupa mundu wake juu ya inchi, akachuma mzabibu wa inchi, akatupa katika shinikizo
- 20 la hasira ya Muungu lilio kubwa. Shinikizo likakanyagwa 'nje ya mji; damu ikatoka katika shinikizo hatta hatamu za frasi, hatta mastadia elfu na sita mia.
- 15 NIKAONA ishara ngine katika mbingu, kuu, ajabu; malaika saba wenyi mapigo saba ya mwisho, ya kuwa
- 2 katika haya imetimia hasira ya Muungu. Nikaona kama bahari ya kioo kimechanganyika na moto, nao walioshinda katika nyama, na sanamu yake, na hesabu ya jina lake, wamesimama juu ya bahari ya kioo, wenyi
- 3 vinubi vya Muungu: wakaimba wimbo wa Musa mtumwa wa Muungu, na uimbo wake Mwana kondoo, wakinena, Makuu na ya ajabu matendo yako, Bwana Muungu Mwenyezi; za haki na za kweli njia zako, Mfalme wa
- 4 watakatifu. Nani asiyekuogopa, Bwana, asiyelitukuza jina lako? Ya kuwa uliye safi peke yako. Ya kuwa mataifa yote watakuja watasujudia mbele yako. Ya kuwa hukumu zako zimeonekana.
- 5 Baada ya haya nikaona, likafunuka hekalu la masi-
- 6 kani ya ushahidi katika mbinguni: wakatoka malaika saba, wenyi mapigo saba, katika hekalu, wamevaa nguo nyeupe ya kitani ing'aayo, wakifungwa kifuni kwa

mishipi ya thahabu. Mmoja wa nyama wanne akawapa 7
 malaika saba vitupa saba vya thahabu, vikijaa hasira 8
 yake Muungu aliye hayi hatta milele na milele. He- 8
 kalu likajaa moshi wa utukufu wa Muungu, na wa
 nguvu zake; wala mtu hakuweza kuingia katika he-
 kalu, hatta yametimika mapigo saba ya malaika saba.

NIKASIKIA sauti kuu katika hekalu, ikiwaambia 16
 malaika saba, Mwende zenu mkavimimine vitupa saba
 vya hasira ya Muungu juu ya inchi.

Akaenda wa kwanza, akamimina kitupa chake juu ya 2
 inchi: likawa jipu baya na bovu juu ya watu walio na
 alama ya nyama, nao walioisujudia sanamu yake.

Malaika wa pili akamimina kitupa chake juu ya 3
 bahari: ikawa damu kama ya mfu; na killa kilicho hayi
 kikafa, kilichomo katika bahari.

Malaika wa tatu akamimina kitupa chake juu ya 4
 mito, na juu ya chemchemi za maji: yakawa damu. Ni- 5
 kasikia malaika wa maji akinena, Unayo haki, uliye nawe,
 na uliyekuwa, uliye safi, ya kuwa umehukumu hivi: ya 6
 kuwa damu ya watakatifu na ya manabii wameimimina,
 nawe umewapa damu wainywe: wamestahili. Nikasikia 7
 mathbahu ikinena, Ndio, Bwana Muungu Mwenyiezi;
 za kweli na za haki hukumu zako.

Malaika wa 'nne akamimina kitupa chake juu ya jua: 8
 likapewa kuwaunguza watu kwa moto. Watu wakau- 9
 ngua moto mkuu. Wakalinenea unajisi jina la Muungu
 aliye na nguvu juu ya mapigo haya: wala hawakutubu
 kumpa utukufu.

Malaika wa tanu akamimina kitupa chake juu ya 10
 kiti cha nyama: ufalme wake ukatiwa giza. Waka-
 jitafuna ulimi kwa taabu, wakamnenea unajisi Muungu 11
 wa mbingu kwa taabu zao, na kwa majipu yao; wala
 hawakutubu katika matendo yao.

Malaika wa sita akamimina kitupa chake juu ya mto 12
 ulio mkuu, Eufrate: maji yake yakakauka, njia ipate
 kufanyika tayari ya wafalme walio wa katika kucha
 jua. Nikaona katika kanwa la joka, na katika kanwa 13
 la nyama, na katika kanwa lake nabii wa uwongo, ma-
 roho matatu machafu, kama vyura: kwani haya maroho 14
 ya pepo yafanyayo ishara; yatokayo juu ya wafalme wa
 inchi na ulimwengu wote, kuwakusanya kwa vita ya
 siku ile kuu ya Muungu Mwenyiezi.

- 15 Angalia, naja kama mwivi. Heri akeshayo, na ali-
ndaye mavazi yake, asiende utupu, wakaone aibu yake.
- 16 Akawakusanya kwa mahali, paitwapo kwa Kiebrania,
Armagedon.
- 17 Malaika wa saba akamimina kitupa chake katika
hewa: ikatoka sauti kuu katika hekalu la mbinguni,
18 katika kiti, ikinena, Imefanyika. Zikawa umeme, na
sauti, na ngurumo; likawa na tetemeko kuu, kama
halikuwa tangu mtu amekuwa juu ya inchi, ginsi tete-
meko lilivyo kuu.
- 19 Mji ulio mkubwa ukawa katika sehemu tatu, na miji
ya mataifa ikaanguka. Na Babeli kuu ikakumbukwa
mbele ya Muungu, kumpa kunwa mvinyo wa hasira ya
ghathabu yake.
- 20 Killa kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonwa.
- 21 Na mvua kuu ya mawe mazito, kama talanto, yakishuka
katika mbingu juu ya watu. Watu wakamnenea una-
jisi Muungu kwa pigo la mvua ya mawe: ya kuwa pigo
lake kubwa mno.
- 17** AKAJA mmoja wa malaika saba walio navyo vi-
tupa saba, akasema nami, akinena, Haya, nitakuonye-
sha hukumu yake kahaba mkuu, akaaye juu ya maji
2 mengi; wakatanya asharati naye wafalme wa inchi,
wakalewa wakaao katika inchi kwa mvinyo wa washe-
rati wake.
- 3 Akanichukua hatta jangwani katika roho: ni-
kaona mwanamke akikaa juu ya nyama nyekundu,
ijaayo majina ya unajisi, yenyi vitwa saba na pembe
kumi.
- 4 Mwanamke amevikwa ya porfuro na nyekundu, aka-
pambwa na thahabu, na vito, na lulu, mwenyi kikombe
cha thahabu katika mkono wake, kimejaa machukizo na
5 machafu ya washerati wake, na juu ya paji la uso wake
jina limeandikwa, SIRI, BABELI ILIYO KUU,
MAMA WA MAKAHABA NA WA MACHUKIZO
YA INCHI.
- 6 Nikamwona mwanamke amelewa na damu ya wataka-
tifu na damu ya mashahidi wake Isa: nikataajabu, ni-
kimwona, ajabu kuu.
- 7 Akaniambia malaika, Mbona wataajabu? Nitakwa-
mbia siri ya mwanamke, na ya nyama amchukuaye,
mwenyi vitwa saba na pembe kumi.

Nyama uliyemwona alikuwa, wala hakuna, naye ata- 8
panda katika abuso, na kwa upotevu aendako. Nao
wakaao juu ya inchi watataajabu, wasioandikwa majina
yao juu ya kitabu cha uzima tangu kuwekwa ulimwe-
ngu, wakimwona nyama ya kwamba alikuwa, wala ha-
kuna, naye yuko.

Hapa akili zilizo na hekima. Vitwa saba ni milima 9
saba, akaapo mwanamke juu yao.

Na wafalme ni saba; watanu wameanguka, mmoja 10
yuko, mgineo hajaja; hatta atakapokuja, imempasa ku-
kaa wakati si mwingi. Na nyama aliyekuwa, wala ha- 11
kuna, naye ni wa nane, naye ni wa wale saba; naye
aenda katika upotevu.

Nazo pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, nao ha- 12
wajapewa ufalme; lakini nguvu kama wafalme watapewa
saa moja pamoja na nyama. Hawa wanao shauri 13
moja, na nguvu na uwezo wao watampa nyama. Hawa 14
watafanya vita na Mwana kondoo, na Mwana kondoo
atawashinda, ya kwamba ni Bwana wa mabwana na
Mfalme wa wafalme, nao pamoja naye walioitwa, na
wateule, na amini.

Akaniambia, Maji uliyoyaona akaapo kahaba, ni watu, 15
na makutano, na mataifa, na ndimi.

Na pembe kumi ulizoziona za nyama, hawa watamchukia 16
kahaba, nao watamfanya ameachwa na utupu, na nyama
yake watamla, nao watamunguza kwa moto. Kwani 17
Muungu amewapa moyoni mwao kutenda shauri lake, nao
watafanya shauri moja, nao watampa nyama ufalme
wao, hatta yatakapotimika maneno ya Muungu.

Na mwanamke uliyemwona ni mji ulio mkubwa, 18
mwenyi ufalme juu ya wafalme wa inchi.

BAADA ya haya nikaona malaika mwingine akishuka 18
katika mbinguni, mwenyi nguvu nyingi; inchi ikaa-
ngazwa na utukufu wake. Akalia kwa sauti ya nguvu, 2
akinena, Imeanguka, imeanguka, Babeli iliyo kubwa,
imekuwa makazi ya pepo, na gereza ya killa roho
wa uchafu, na gereza ya killa ndege mchafu na mkorofi:
ya kwamba mataifa yote wamekunywa mvinyo wa hasira 3
ya washarati wake, na wafalme wa inchi wamefanya
asharati naye, na matajiri ya inchi wamepata mali kwa
kuwa na nguvu kiburi chake.

Nikasikia sauti ngine katika mbingu, ikinena, Toke- 4
ni katika kwake, enyi watu wangu, msisharikiane na
thambi zake, na mapigo yake msiyapokee: ya kwamba 5

- thambi zake zimefika hatta mbinguni, na Muungu ame-
 6 kumbuka thulumu yake. Mlipo huyu kama alivyolipa,
 ukamzidishie marra mbili kwa matendo yake: kwa
 kikombe alichokichanganya umchanganyie marra mbili.
- 7 Kama alivyojisifu, akatenda kwa moyo wake, hivyo
 mmpe kuuma na huzuni: ya kwamba moyoni mwake
 hunena, Nimekaa malkia, wala mimi si mjaani, wala
 8 sitaona huzuni. Kwa hiyo katika siku moja mapigo
 yake yamekuja, mauti, na huzuni, na njaa; na kwa
 moto ataungua kabisa: ya kwamba aliye hodari ndiye
 Bwana Muungu amhukumuye.
- 9 Nao watalia na watataabika kwa ajili yake, wafalme
 wa inchi, waliofanya asharati naye wasiojizuia, wakiona
 10 moshi wa kuungua kwake, wakiwa wamesimama mbali,
 kwa hofu ya kuuma kwake, wakinena Ole, ole, wa mji
 ulio mkubwa, Babeli, mji ulio hodari! ya kwamba saa
 moja imekuja hukumu yako.
- 11 Nao matajiri wa inchi watalia watahuzunika kwa ajili
 yake, ya kuwa shehena zao hapana mtu tena anunuaye;
 12 shehena ya thahabu, na fetha, na vito vya thamani, na
 lulu, na kitani, na porfuro, na hariri, na nyekundu; na
 killa mti wa uudi, na killa chombo cha pembe, na killa
 chombo cha mti wa thamani nyingi, na cha shaba, na
 13 cha chuma, na cha marmari; na mdalasini, na uvumbi,
 na marhamu, na buhuri, na mvinyo, na mafuta, na unga,
 na ngano, na ng'ombe, na kondoo, na frasi, na magari,
 na miili na maisha ya watu.
- 14 Na matunda yako ya kutamanika na moyo yamepotea
 katika kwako, na yote yaliyo laini na mazuri yamepotea
 katika kwako, wala hutayaona tena.
- 15 Wafanyao biashara ya haya, waliopata mali kwake,
 watasimama mbali kwa hofu ya kuuma kwake, wakilia
 16 na wakihuzunika, wakinena, Ole, ole wa mji ulio mkubwa,
 uliovikwa kwa kitani na porfuro na nyekundu, uka-
 pambwa kwa thahabu na vito vya thamani na lulu!
 17 ya kuwa katika saa moja mali kama haya yame-
 angamia. Na killa mshika sukani, na killa aendaye pa-
 hali kwa matanga, na baharia, na wote watendao kazi
 18 baharini, wakasimama mbali, wakalia wakiona moshi
 wa kuungua kwake, wakinena, Upi ulio kama mji ulio
 19 mkubwa? Wakatupa mavumbi juu ya vitwa vyao, waka-
 lia, wakitoa machozi na wakihuzunika, wakinena, Ole,
 ole, wa mji ulio mkubwa, katika yake walipata mali wote

wenyi merikebu katika bahari, kwa thamani zake nyin gi!
ya kuwa katika saa moja umeangamia.

Furahini juu yake, mbingu, na watakatifu, na mitume, 20
na manabii; ya kuwa Muungu amehukumu hukumu
yenu juu yake.

Malaika mmoja hodari akatweka jiwe, kama la kusaga 21
lililo kubwa, akatupa katika bahari, akinena, Hivi kwa
nguvu nyingi utatupwa Babeli, mji ulio mkubwa, wala
hautaonwa tena. Na sauti yao wapigao kinubi, na wa- 22
fanyao ngoma, na wapigao filimbi, na wapigao paanda,
haitasikiwa tena kwako; na killa fundi, wa kazi yo yote,
hataonwa tena kwako; na sauti ya kusaga haitasikiwa
tena kwako; na nuru ya taahaitamulika kwako; na sauti 23
ya bwana arusi na bibi arusi haitasikiwa tena kwako:
ya kuwa waliofanya biashara kwako walikuwa wakuu wa
inchi; ya kuwa katika uchawi wako wamedanganyika
mataifa yote. Na kwake damu ya manabii na wata- 24
katifu imeonekana, na yao wote walio uawa juu ya inchi.

BAADA ya haya nikasikia kama sauti ya makutano 19
mengi katika mbingu, wakinena, Alleluya: Wokovu,
na utukufu, na heshima, na nguvu, kwa Bwana Muu-
ngu wetu: kwani za kweli na za haki hukumu zake; 2
ya kuwa amemhukumu kahaba aliye mkuu, aliyeharibu
inchi katika asherati yake, naye ameihukumia damu ya
watumwa wake katika mkono wake. Marra ya pili wa- 3
kasema, Alleluya. Na moshi wake hupaa hatta milele
na milele.

Wakaanguka wazee asharini na wanne, na nyama wan- 4
ne, wakamsujudia Muungu akaaye juu ya kiti, wakinena,
Amina. Alleluya. Sauti katika kitini ikatoka, ikinena, 5
Msifuni Muungu wetu, enyi watumwa wake wote, nan-
nyi mmchao, na wadogo na wakuu.

Nikasikia kama sauti ya makutano mengi, na kama 6
sauti ya maji mengi, na kama sauti ya ngurumo za nguvu,
ikinena, Alleluya: ya kwamba amemiliki Bwana Muungu
wetu Mwenyiezi. Tufurahi, tukafurahawe, tukampe utu- 7
kufu: kwani arusi ya Mwana kondoo imekuja, na mkewe
amejifanya tayari. Akapewa avikwe kwa kitani safi na 8
nyeupe: kwani kitani hii ni mahaki ya watakatifu.

Akaniambia, Andika, Heri walioitwa kwa chakula cha 9
arusi yake Mwana kondoo. Akaniambia, Haya maneno
yaliyo ya kweli ya Muungu. Nikaanguka mbele ya mi- 10
guu yake, nikamsujudia. Akaniambia, Angalia sivyo:

mimi mjoli wako, na wa ndugu zako walio na ushahidi wa Isa. Msujudie Muungu : kwani ushahidi wa Isa ni roho ya unabii.

- 11 Nikaona mbingu zimefunuka ; na frasi nyeupe, na aliyekaa juu yake aitwa Amina na Wa kweli ; na katika
 12 haki ahukumu na kufanya vita. Na macho yake kama moto uwakao, na juu ya kitwa chake vilemba vingi ; akiwa na jina limeandikwa, asilolijua mtu illa mwenyewe.
 13 Naye amevikwa kwa vazi lililochoveka katika damu.
 14 Na jina lake likaitwa, Neno la Muungu. Na majeshi yaliyo mbinguni yakamfuata juu ya frasi nyeupe,
 15 wamevaa kitani nyeupe safi. Na katika kanwa lake watoka upanga mkali, apate kwao kuwapiga mataifa. Naye awachunga kwa fimbo ya chuma. Naye akanyaga shinikizo la mvinyo wa hasira na ghathabu ya Muungu Mwenyiezi. Na juu ya vazi na ya paja lake jina limeandikwa, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA.
 17 Nikaona malaika mmoja amesimama katika jua ; akalia kwa sauti kuu, akiwaambia ndege zote zirukazo katika anga, Haya, kusanyikeni kwa chakula cha Muungu aliye mkuu ; mpate kula nyama ya wafalme, na nyama ya majemadari, na nyama yao walio hodari, na nyama ya frasi na yao wawapandao, na nyama ya wote wangwana na watumwa, na wadogo na wakuu.
 19 Nikamwona nyama, na wafalme wa inchi, na majeshi yao, wakikusanyika wafanye vita naye akaaye juu ya frasi na majeshi yake.
 20 Akatwaliwa nyama, na nabii wa uwongo aliye pamoja naye, aliyefanya ishara mbele yake, kwa hizo akawadanganya waliopokea alama ya nyama, nao walioisujudia sanamu yake : wakatupwa hayi hawa wawili katika ziwa la moto uwakao kwa kiberiti.
 21 Nao waliosalia wakauawa kwa upanga wake akaaye juu ya frasi, utokao katika kanwa lake : na ndege zote zikashiba kwa nyama zao.
 20 NIKAONA malaika akishuka katika mbingu, mwenyi ufunguo wa abuso, na mnyororo mkuu mkononi
 2 mwake. Akamshika joka, nyoka wa zamani, aliye
 3 Mstaki na Shetani, akamfunga miaka elfu, akamtupa katika abuso, akafunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena hatta itakapotimia miaka elfu : baadaye imepasa afunguliwe wakati si mwingi.

Nikaona viti, nao waliokaa juu yao, wakapewa huku- 4
mu : na roho zao, waliokatwa kitwa kwa ajili ya usha-
hidi wake Isa, na kwa ajili ya neno lake Muungu, na
wasiomsujudia nyama, wala sanamu yake, wala hawa-
kupokea alamajuu ya pajila uso wao, walajuu ya mkono
wao ; wakawa hayi, wakamiliki pamoja naye Masiya mi-
aka elfu.

Wafu waliosalia hawakuwa hayi hatta ikitimia miaka 5
elfu.

Ndio ufufuo wa kwanza. Heri na mtakatifu aliye 6
nayo sehemu katika ufufuo wa kwanza : juu yao mauti
ya pili haina nguvu ; lakini watakuwa wakohani wa
Muungu na wa Masiya, nao watamiliki naye miaka elfu.

Hatta miaka elfu ilipotimia, Shetani atafunguliwa 7
katika lindo lake, naye atakuja kuwadanganya mataifa 8
walioko katika pembe 'nne za inchi, Gog na Magog, ku-
wakusanya kwa vita : hesabu yao kama mchanga wa
bahari.

Wakapanda juu ya upana wa inchi, wakakizunguka 9
kituo cha watakatifu, na mji uliopendwa : moto ukashu-
ka katika mbingu katika kwa Muungu, ukawala. Naye 10
Mshtaki awadanganyaye akatupwa katikaziwa la moto na
kiberiti, walipo nyama na nabii wa uwongo ; wakaumwa
mchana na usiku hatta milele na milele.

Nikaona kiti kikubwa cheupe, naye akaaye juu yake, 11
mbele ya uso wake zikakimbia inchi na mbingu ; wala
mahali pao hapakuonekana.

Nikawaona wafu, wakuu na wadogo, wakisimama 12
mbele ya kiti ; vitabu vikafunuliwa : hatta kitabu ki-
ngine kikaletwa, ndicho cha uzima : wafu wakahukumi-
wa kwayo yaliyoandikwa katika vitabu, kwa matendo
yao.

Bahari ikawatoa wafu waliomo mwake ; na Mauti na 13
Ahera wakawatoa wafu waliomo mwao : wakahukumiwa
killa mtu kwa matendo yao.

Na Mauti na Ahera wakatupwa katika ziwa la moto. 14
Ndio mauti ya pili. Naye mtu asiyeonwa ameandikwa 15
katika kitabu cha uzima, akatupwa katika ziwa la moto.

NIKAONA mbingu mpya na inchi mpya : kwani 21
mbingu za kwanza na inchi ya kwanza imekwenda zake ;
wala bahari hapana tena.

Nami Yohana nikauona mji mtakatifu, Yerusalemi 2
mpya, ukishuka katika mbinguni katika kwa Muungu,

- umetengenezwa kama arusialiyepambwa kwa mume wa-
 3 ke. Nikasikia sauti kuu katika mbinguni, ikinena, Anga-
 lia, masikani ya Muungu pamoja na watu, naye atautua
 pamoja nao, nao watakuwa watu wake, naye Muungu
 4 pamoja nao atakuwa Muungu wao: naye atafuta killa
 chozi katika machoni mwao; wala mauti haitakuwa
 tena; wala huzuni, wala kilio, wala taabu haitakuwa
 tena: ya kuwa mambo ya kwanza yamepita.
- 5 Akanena akaaye juu ya kiti, Angalia, nayafanya yote
 mapya. Naye anena, Andika: ya kwamba haya maneno
 6 amini na ya kweli. Akaniambia, Imekuwa. Mimi ni
 Alfa na Omega, mwanzo na mwisho. Mimi nitampa
 7 mwenyi kiu ya kisima cha maji ya uzima bure. Ashi-
 ndaye atayarithi haya; nitakuwa kwake Muungu, naye
 8 atakuwa kwangu mwana. Nao waoga, na wasioamini,
 na wachukizao, na wauaji, na wenyi asharati, na wacha-
 wi, na makafiri, nao wawongo wote, sehemu yao katika
 ziwa liwakalo moto na kiberiti; ndio mauti ya pili.
- 9 Akaja kwangu mmoja wa malaika saba walio navyo
 vitupa saba vya mapigo saba ya mwisho, akasema nami,
 akanena, Haya, nitakuonya bibi arusi, mkewe Mwana
 kondoo.
- 10 Akanichukua katika Roho juu ya mlima mkubwa
 na mrefu, akanionyesha mji ulio mtakatifu, Yerusalemi,
 11 ukishuka katika mbinguni katika kwa Muungu, mwenyi
 utukufu wa Muungu, ukimulika kama kito cha thamani
 12 nyingi, kama jiwe yaspi la krustallo. Ukawa na ukuta
 mkubwa na mrefu, mwenyi milango thenashara, na juu
 ya milango malaika thenashara, na majina yameandi-
 kwa, ndiyo ya makabila thenashara ya waana wa Israeli.
- 13 Kwa mashariki milango mitatu, kwa kaskazini milango
 mitatu, kwa kusini milango mitatu, kwa magarihi mila-
 14 ngo mitatu. Na ukuta wa mji ulikuwa na misinji the-
 nashara, na juu yao majina thenashara yao mitume the-
 nashara wa Mwana kondoo.
- 15 Naye asemaye nami alikuwa na unyasi wa thahabu,
 16 aupime mji, na milango yake, na ukuta wake. Na mji
 umewekwa mraba, na urefu wake sawa na upana wake:
 akaupima mji kwa unyasi, hatta mastadio thenashara
 elfu: urefu wake, na upana wake, na kwenda juu kwake,
 mamboja.
- 17 Akapima ukuta wake, mikono mia na arobaini na 'nne,
 cheo cha mtu, ndiye malaika.

Na uwashi wa ukuta wake wa yaspi : na mji thahabu 18
safi, kama kioo safi.

Na misinji ya ukuta wa mji imetengenezwa kwa killa 19
jiwe la thamani : wa kwanza, yaspi ; wa pili, sapfiro ;
wa tatu, kalkedo ; wa 'nne, smaragdo ; wa tanu, sardo- 20
nuksi ; wa sita, sardio ; wa saba, krusolitho ; wa nane,
berullo ; wa tissa, topazio ; wa kumi, krusopraso ; wa
edashara, huakintho ; wa thenashara, amethusto.

Na milango thenashara, lulu thenashara ; killa mlango 21
mmoja wa lulu moja. Na njia ya mjini thahabu safi,
kama kioo ikipenyacho nuru.

Hekalu sikuona katika yake. Kwani Bwana Muungu 22
Mwenyiezi ndiye hekalu lake, naye Mwana kondoo.
Wala mji hauhitaji jua wala mwezi uangaze kwake : 23
kwani utukufu wa Muungu huutia nuru, na taa yake *ni*
Mwana kondoo.

Nao mataifa waokokao hutembea katika nuru yake : 24
na wafalme wa inchi wauletea utukufu wao na heshima
yao. Wala milango yake haifungwi mchana : kwani 25
huko hakuna usiku. Nao wauletea utukufu na heshima 26
ya mataifa : wala hakiingii kwake kilicho kinyonge 27
chote, wala afanyaye chukizo wala uwongo : illa walio-
andikwa katika kitabu cha uzima chake Mwana kondoo.

AKANIONYESHA mto wa maji ya uzima ung'aoo **22**
kama krustallo, ukitoka katika kiti cha Muungu na
Mwana kondoo. Kati ya njia yake na ya mto, upande 2
huu na ule, mti wa uzima, uliozaa matunda thenashara,
killa mwezi ukatoa tunda lake : na majani ya mti kwa
kuwaponya mataifa.

Wala hapana tena laana. Na kiti cha Muungu na 3
cha Mwana kondoo kitakuwako ndani yake : na watumwa
wake watamwabudu ; nao watamtazama uso ; na jina 4
lake juu ya paji la uso wao. Wala hautakuwa tena usi- 5
ku ; wala hawahitaji taa wala nuru ya jua ; kwani Bwana
Muungu atiaye nuru kwao. Nao watamiliki hatta mi-
lele na milele.

Akaniambia, Haya maneno amini na ya kweli : naye 6
Bwana Muungu wa manabii watakatifu ametuma ma-
laika yake awaonyeshe watumwa wake yatakayokuwa
upesi. Kaangalia, naja upesi. Heri ayalindaye mane- 7
no ya unabii wa kitabu hiki.

Nami Yohana ndimi niyasikiaye na niyaonaye haya.

- Hatta niliposikia, nikaona, nikaanguka nisujudie mbele
 9 ya miguu yake malaika anionyeshaye haya. Akaniambia,
 Angalia sivyo: mimi mjoli wako, na wa ndugu zako
 manabii, nao wayalindao maneno ya kitabu hiki. Msuju-
 die Muungu.
- 10 Akaniambia, Usitie muhuri juu ya maneno ya unabii
 11 wa kitabu hiki; kwani wakati u karibu. Mwenyi thu-
 lumu, awe tena na thulumu, na mchafu awe tena mchafu,
 na mwenyi haki awe tena na haki, na mtakatifu awe tena
 12 mtakatifu. Angalia, naja upesi; na thawabu yangu
 pamoja nami, nimlipe killa mtu kama itakavyokuwa
 13 kazi yake. Mimi Alfa na Omega, mwanzo na mwisho,
 wa kwanza na wa kwisha.
- 14 Heri wafanyao amri zake, wapate kuuweza mti wa
 15 uzima, wakaingie milangoni mwa mji. 'Nje mbwa, na
 wachawi, na washerati, na wauaji, na makafiri, na killa
 apendaye na afanyaye uwongo.
- 16 Mimi Isa nimepeleka malaika wangu awashuhudie
 ninyi haya katika makanisa. Mimi ni Shina na Mzao wa
 17 Daudi, Nyota ing'aayo ya ussubui. Naye Roho na bibi
 arusi wasema, Njoo. Na asikiaye aseme, Njoo. Naye
 mwenyi kiu aje: apendaye atwae maji ya uzima pasipo
 thamani.
- 18 Namshuhudia killa ayasikiaye maneno ya unabii wa
 kitabu hiki, mtu akitia juu yake, Muungu atatia juu
 19 yake mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu
 akiondoa katika maneno ya kitabu cha unabii huu, Muu-
 ngu ataondoa sehemu yake katika kitabu cha uzima, na
 katika mji ulio mtakatifu, nayo yaliyoandikwa katika
 20 kitabu hiki. Anena ayashuhuduye haya, Ndiyo: naja
 upesi. Amina: njoo, Bwana Isa.
- 21 Neema yake Bwana Isa Masiya pamoja nanyi nyote.
 Amina.



10410^r

Bible
Swahili
1883

Bible. Swahili

Kitabu cha Agano Jipya. 1883.

UNIVERSITY OF TORONTO
LIBRARY

DO NOT
REMOVE
THE
CARD
FROM
THIS
POCKET



